بسم الله الرحمن الرحيم

# MDAHALO BAINA YA MWANACHUONI WA KISUNNI NA MWANACHUONI WA KISHIA (AL-MURAJA'AAT)


**Kimeandikwa na:**

Allamah Sayyid 'Abdul-Husein Sharafud-Din al-Musawi

**Kimetarjumiwa na:**

Dr. M. S. Kanju na Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimehaririwa na:**

Al-Haj Hemedi Lubumba Selemani

ترجمة

المراجعات

# أبحاث جديدة في أصول المذهب والإمامة العامة

تحقيق و تعليق
حسين الراضي

تأليف
الامام عبد الحسين شرف الدين

من اللغة الإنجليزية الى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 - 17 – 038 – 8

**Kimeandikwa na:**
Allamah Sayyid 'Abdul-Husein Sharafud-Din al-Musawi

**Kimetarjumiwa na:**
Dr. M. S. Kanju
**Barua pepe:** mokanju2000@yahoo.com
na
Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimehaririwa na:**
Al-Haj Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Januari, 2014
Nakala: 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| Dibaji | | 01 |
| Neno la Mchapishaji | | 02 |
| Barua ya 1 – Salaam kwa Mjadili na Kuomba ruhsa ya mdahalo | | 03 |
| Barua ya 2 – Salaam zajibiwa na Ruhusa ya mdahalo yatolewa | | 03 |
| Barua ya 3 | | 05 |
| i | Kwa nini Shi'a hawafuati Madhehebu ya walio wengi? | 05 |
| ii | Haja ya Umoja | 05 |
| iii | Umoja hupatikana tu kwa kufuata Madhehebu ya walio wengi | 00 |
| Barua ya 4 | | 06 |
| i | Uthibitisho wa Kisheria Unaamuru Ufuasi Kwenye Madhehebu ya Ahlul-Bayt , | 06 |
| ii | Hakuna Uthibitisho Unaoamuru Ufuasi Kwenye Madhehebu ya Wengi, | 06 |
| iii | Vizazi vya Karne Tatu za Mwanzo Kamwe Havikujua Madhehebu haya Manne [ya Sunni], | 06 |
| iv | Uwezekano wa Ijtihad, | 06 |
| v | Umoja Unaweza Kupatikana kwa Kuyaheshimu Madhehebu ya Ahlul-Bayt. | 06 |
| Barua ya 5 | | 09 |
| i | Kukubaliwa kwa Hoja, | 09 |
| ii | Kuomba Ushahidi wa Kina. | 09 |
| Barua ya 6 | | 10 |
| i | Rejea za Ushahidi Unaolazimisha Kufuata Ahalul-Bayt | 10 |
| ii | Amirul-Mu'minin (a.s.) Atoa wito wa Kufuata Madhehebu ya Ahlul-Bayt. | 10 |
| iii | Kauli Yenye Kufaa ya Imam Zaynul-Abidiin. | 10 |
| Barua ya 7 | | 13 |
| i | Maombi ya Uthibitisho Kutoka kwenye Maneno ya Allah na Mjumbe Wake, | 13 |
| ii | Hoja Kutoka kwa Ahlul-Bayt Hazikubaliki. | 13 |
| Barua ya 8 | | 14 |
| i | Kupuuza Maelezo Yetu Ya Mwanzo, | 14 |
| ii | Kosa Katika Hoja Ya Mzunguko (Ya Mantiki), | 14 |
| iii | Hadithi Ya Vizito Viwili, | 14 |
| iv | Tawatur Yake, | 14 |
| v | Wasioshikamana Na Itra Watapotea, | 14 |
| vi | Kufanana kwao na Safina ya Nuh, Lango la Wokovu,<br>Na Usalama Dhidi ya Mfarakano wa Kidini, | 14<br>14 |
| vii | Ahlul-Bayt Inamaanisha Nini Kuhusiana na Suala Hili, | 14 |
| viii | Sababu za kufanana na Safina ya Nuh na Lango la Wokovu. | 14 |
| Barua ya 9 - Maombi Ya Maandiko Zaidi Yanayohusika | | 20 |
| Barua ya 10 - Kutupia Macho Maandiko ya Kutosha | | 21 |

Barua ya 11 26

i Kuvutiwa na Maelezo Yetu ya Wazi, 26

ii Wasiwasi wa Kuafikiana nayo Pamoja na Imani za Wengi, 26

iii Maombi ya Dalili ya Wazi Kutoka Kitabu cha Allah. 26

Barua ya 12 Ushahidi wa Qur'ani Tukufu 27

Barua ya 13 36

i Uwezekano wa Kwamba Hadith hizi 36

ii Kuhusiana na Aya za Qur'ani sio Sahihi. 36

Barua ya 14 37

i Kuthibitisha Makosa Ya Hoja Ya Wakosoaji, 37

ii Wakosoaji Hawajui Maana ya neno "Shi'a". 37

Barua ya 15 39

i Mwanga wa Ukweli, 39

ii Maombi ya Maelezo juu ya Masunni Wanaotegemea Vyanzo vya Mashia. 39

Barua ya 16 40

i Vyanzo Mia moja (Pamoja na Majina yao) 40

ii Vya Mashia Wanaotegemewa na Masunni. 40

Barua ya 17 87

i Kushukuru Upole wa Mjadili, 87

ii Kukubali Ukweli kwamba Hakuna Sababu kwa nini Sunni Wasitegemee Riwaya za Wanachuo wa Kishia, 87

iii Kuamini kwake Aya Zinazowahusu Ahlul-Bayt, 87

iv Mshangao Katika Kulinganisha Kati ya Haya na Yanayoaminiwa na Waislamu. 87

Barua ya 18 89

i Shukurani kwa Maneno ya Upole, 89

ii Kosa la Kufunga Istilahi "Watu wa Qibla" kwenye Madhehebu Maalum, 89

iii Wanasiasa ndio Waliogeukia Mbali na Njia ya Ahlul-Bayt, 89

iv Maimamu wa Ahlul-Bayt kwa Hali Yoyote sio Duni kwa Maimamu Wengine, 89

v Hakuna Mtu Mwadilifu Anayeweza Kuwashutumu Wafuasi wa Ahlul-Bayt kwa Kupotoka. 91

Barua ya 19 91

i Wafuasi wa Ahlul-Bayt Hawawezi Kuhukumiwa kama Waliopotoka, 91

ii Kufuata Imani yao ni Kutekeleza Wajibu Kunakotosha, 91

iii Inaweza Kusemwa Ahlul-Bayt ndio Wanaostahiki Zaidi Kufuatwa Kuliko Wengine,

iv Kuomba Nususi Zisizo na Shaka Kuhusiana na Ukhalifa. 91

Barua ya 20 92

i Utajo Mfupi wa Nususi,

ii Nasu ya Siku ya Onyo kwa Jamaa wa Karibu, 92

iii Ahlus-Sunna Wameiandika na Kuisimulia Nasu hii. 92

Barua ya 21 - Hadithi Hiyo ina Mashaka Juu ya Ukweli Wake 94

Barua ya 22 95

i Kutoa Ushahidi wa Usahihi wa Hadithi hii, 95

ii Kwa nini wao (Bukhari na Muslim) Wamekwepa Kuiandika, 95

iii Yeyote Anayewafahamu Masheikh hawa Hataona Ajabu. 95

Barua ya 23 97

i Kukiri Usahihi wa Hadithi hii, 97

ii Hadithi Kutotumika kama Hoja ya Nguvu kwa Sababu ya Uchache wa Usimuliwaji wake, 97

iii Kwa Vyovyote Inathibitisha Urithi Maalum (wenye mipaka), sio Ukhalifa wa kila yeyote. 97

iv Hadithi Imepewa Mbadala. 97

Barua ya 24 98

i Kwa nini Tumetoa kama Hoja Hadithi Inayosemwa kwamba si Mutawatir, 98

ii Urithi Wenye Mipaka ni Kinyume na Maoni ya Pamoja ya Wanachuoni wote wa Kiislam, 98

iii Hapa Ufutwaji ni jambo Ambalo Haliwezekani. 98

Barua ya 25 99

i Imani yake Juu ya Hadith, 99

ii Kuomba Utetezi zaidi (Juu ya Uimam wa Ahlul-Bayt). 99

Barua ya 26 100

i Hadithi za Wazi Zinazoorodhesha Sifa 10 za Ali (a.s.) 100

ii Uthibitisho wa Haki ya Ali ya Urithi Unaotolewa na Hadith hizo 100

Barua ya 27 - Mashaka Kuhusu Usahihi wa Hadithi ya Manzila 103

Barua ya 28 104

i Hadithi ya Manzila ni Moja kati ya zile Hadith Ambazo Usahihi wake Umethibitishwa sana, 104

ii Hoja Kuhusu Usahihi wake, 104

iii Hadithi Imesimuliwa na Wasimuliaji wa ki-Sunni, 104

iv Kwa nini Al-Amidi Alikuwa Anashuku Usahihi wake. 104

Barua ya 29 107

i Kuamini Hoja zetu Kuhusu Usahihi wa Hadithi ya Manzila, 107

ii Kutilia Shaka Matumizi yake ya Jumla, 107

iii Shaka juu ya Hadith kuwa Uthibitisho wa Uimam wa Jumla wa Ali. 107

Barua ya 30 108

i Wenye Asili ya Lugha ya Kiarabu Wanaiona ya Jumla, ya Kutumika pote, 108

ii Uongo wa Maoni Kwamba Riwaya ilihusu Tukio Maalum, 108

iii Kupingana kwa Maoni kwamba Riwaya hiyo siyo Ushahidi wa Uandamizi wa Jumla wa Ali. 108

Barua ya 31 - Kuomba Matukio Mengine ya Hadithi hii 111

Barua ya 32 112

i Moja ya Matukio ni pale Mtume (s.a.w.w.) Alipokutana na Umm Saliim, 112

ii Suala la Binti wa Hamza, 112

iii Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Kumuegemea Ali, 112

iv Udugu wa Awali, 112

v Kufunga Milango, 112

vi Mtukufu Mtume Alitumia Kutoa Mfano wa Farqdain (Nyota mbili Angavu Karibu na Ncha ya Kaskazini ya Dunia Ambazo Wanamaji Hugundulia Mwelekeo) Kati ya Ali na Harun. 112

Barua ya 33 116

i Ni Lini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Aliwafananisha 116

ii Ali na Harun na Hizo Nyota Mbili (Farqadain)? 116

Barua ya 34 117

i Katika Siku ya Shabar, Shubayr, na Mushbir, 117

ii Siku ya Tukio la Kuunga Udugu, 117

iii Siku ya Kufunga Milango. 117

Barua ya 35 - Kuomba Uthibitisho Zaidi 122

Barua ya 36 123

i Hadith Zilizosimuliwa Kutoka kwa Ibn Abbas, Imran, Buraydah', Ali, Wahab, na Ibn Abu Aasim, 123

ii Hadithi ya Fadhila Kumi. 123

Barua ya 37 126

i "Walii" Ni Neno Lenye Maana Nyingi, 126

ii Sasa, Uko Wapi Ushahidi wa Wazi? 126

Barua ya 38 127

i Maana Halisi Ya Neno "Walii", 127

ii Vidokezo Vya Maudhui na Mpangilio wa Maneno. 127

Barua ya 39 - Kuomba Aya ya Wilayat (Ubwana au Ulezi au Mamlaka ya Juu, ya Imam Ali (a.s.) 129

Barua ya 40 130

i Aya ya Wilayat na Kushuka Kwake Kuhusu Ali, 130

ii Ushahidi Kuhusu Kushushwa Kwake, 130

iii Sababu ya Kuitumia Kama Hoja. 130

Barua ya 41 - Wale Walioamini "Waumini - yaani Waislam" ni Katika Uwingi. Inawezaje Kutumika kwa Ajili ya Mtu Mmoja? 133

Barua ya 42 134

i Waarabu Hutumia Muundo wa Uwingi Kuashiria Mtu Mmoja, 134

ii Mfano wa Kutumia Uwingi kwa Ajili ya Mtu Mmoja, 134

iii Maoni ya Imam Tabrasi, 134

iv Maelezo ya Zamakhshari, 134

v Mtazamo Wetu Sisi Wenyewe. 134

Barua ya 43 137

Mwelekeo na Muktadha wa Aya Unaashiria Neno 'Walii' au 'Mawla' lina Maana ya Msaidizi au Rafiki au Watu Kama Hao. 137

Barua ya 44 138

i Muktadha Hauthibitishi Kwamba Neno 'Walii' Katika Aya hii lina Maana ya "Msaidizi" au Mfano Wake, 138

ii Muktadha Peke yake Haubebi Uzito Dhidi ya Hoja Sahihi. 138

Barua ya 45 140

i Ni Lazima Kutafsiri Aya Kinyume chake kwa Ajili ya Kulinda Heshima na Hadhi ya Wahenga Wetu. 140

Barua ya 46 141

i Sio Lazima Kutafsiri Aya Kinyume chake kwa Ajili tu ya Kulinda Heshima na Hadhi ya Wahenga, 141

ii Tafsir ya Kinyume Haiwezekani. 141

Barua ya 47 - Kuomba Hadithi Zenye Uthibitisho 142

Barua ya 48 - Riwaya Arobaini Zinazounga Mkono Ukweli wa Wazi wa Hadithi. 143

Barua ya 49 152

i Kukiri Sifa Bora za Ali, 152

ii Sifa hizo Hazihalalishi Cheo chake cha Ukhalifa. 152

Barua ya 50 153

i. Nususi Juu ya Sifa na Ubora wake, Zimetolewa Kama Hoja 153

ii Juu ya Uimam Wake 153

Barua ya 51 - Hoja Pinzani Kwa Msingi wa Riwaya Zinazosifia Wengine 154

Barua ya 52 - Kukataa Hoja Pinzani 155

Barua ya 53 - Maombi Ya Hadithi ya Ghadir 156

Barua ya 54 - Mnyororo wa Hadith ya Ghadir Unaong'ara 157

Barua ya 55 - Kwa nini Riwaya hii Imetumika Kama Ushuhuda, Ingawa Haikusimuliwa Mfululizo (mutawatir) 161

Barua ya 56 162

i Uhalisia wa Mambo Unaifanya Hadith Ya Ghadir Kuwa Mutawatir, 162

ii Ilikuwa ni Fadhila Maalum za Mwenyezi Mungu Mtukufu, 162

iii Mtume Wa Allah (s.a.w.w.) Aliipa Umuhimu Maalum, 162

iv Amirul Muminin (a.s.) Aliipa Umuhimu Maalum, 162

v Al-Husein (a.s.) Aliipa Umuhimu Maalum, 162

vi Maimamu Miongoni mwa Ahlul-Bayt (As) Waliipa Umuhimu Maalum, 162

vii Shi'ah Waliipa Umuhimu Maalum, 162

viii Imesimuliwa Mfululizo (Mutawatir) Kwa Maoni ya Umma wa Kiislam. 162

Barua ya 57 170

i Tafsiri ya Hadith Al-Ghadir, 170

ii Uwezekano wa Ukweli wa Tafsiri hiyo. 170

Barua ya 58 171

i Hadith ya Ghadir Haikubali Tafsri Nyingine. 171

ii Uwezekano wa Tafsiri Tofauti ni Maongezi Yasiyo na Mpango Maalum na ni ya Upotoshaji kwa Hakika. 171

Barua ya 59 176

| | | |
|---|---|---|
| i | Ukweli Wadhihiri, | 176 |
| ii | Kukwepa. | 176 |
| Barua ya 60 - Kukanusha Ukwepaji na Matumizi Mabaya | | 177 |
| Barua ya 61 - Maombi ya Riwaya Zilizosimuliwa na Vyanzo vya Shi'ah | | 180 |
| Barua ya 62 - Hadithi Arobaini za Wazi Kabisa | | 181 |
| Barua ya 63 | | 188 |
| i | Riwaya zilizosimuliwa na shi'ah pekee hazikubaliwi kama hoja, | 188 |
| ii | Kwa nini wasio shi'ah hawakuzisimulia? | 188 |
| iii | Maombi ya riwaya zaidi zilizosimuliwa na kuandikwa na sunni. | 188 |
| Barua ya 64 | | 189 |
| i | Tumenukuu riwaya hizo kulingana na maombi yako, | 189 |
| ii. | Riwaya zilizonukuliwa kabla kutoka kwenye vitabu vyenu vya hadithi sahih zinatosha kuridhisha walio wengi, | 189 |
| iii | Kwa nini hawakusimulia hadithi hizi sahihi zilizo kwenye kumbukumbu zetu, | 189 |
| iv | Kutajwa kwa hadithi ya urithi. | 189 |
| Barua ya 65 - Maombi ya hadithi inayohusiana na urithi | | 192 |
| Barua ya 66 - Ali (a.s.) Ni mrithi wa mtume (s.a.w.w.) | | 193 |
| Barua ya 67 - Kuuomba wosia wa mtume | | 195 |
| Barua ya 68 - Hadithi za wazi za mtukufu mtume (s.a.w.w.) Kuhusu urithi wa ali (a.s.) | | 196 |
| Barua ya 69 - Hoja inayokataa kwamba mtukufu mtume (s.a.w.w.) Ameacha wosia | | 199 |
| Barua ya 70 | | 200 |
| i | Kufanya wosia kwa mtukufu mtume (s.a.w.w.) Hakukanushiki, | 200 |
| ii | Sababu ya kukataliwa wasia, | 200 |
| iii | Riwaya ya talha bin masrif ndani ya bukhari sio hoja dhidi yetu, | 200 |
| iv | Mantiki na kipawa cha kufikiri vinathibitisha kwamba mtukufu mtume (s.a.w.w.) Alitoa wosia. | 200 |
| Barua ya 71 - Kwanini umekataa hadithi ya ummul muuminiin, ambaye ni mke bora wa mtukufu mtume (s.a.w.w.)? | | 205 |
| Barua ya 72 | | 206 |
| i | Aisha hakuwa mke bora zaidi wa mtukufu mtume (s.a.w.w.), | 206 |
| ii | Mke bora alikuwa ni bibi khadija (s.a.), | 206 |
| iii | Maelezo mafupi juu ya sababu ya kuikataa hadithi yake. | 206 |
| Barua ya 73 - Kuomba maelezo ya kukataa kwetu hadithi za aisha | | 208 |
| Barua ya 74 | | 209 |
| i | Sababu za kuzikataa kwetu hadithi ya aisha, | 209 |
| ii | Akili inathibitisha mtume aliacha wosia kwa fadhila ya ali, | 209 |
| iii | Madai yake kwamba mtume alifariki akiwa ameegemea juu ya kifua chake sio ya kweli. | 209 |
| Barua ya 75 | | 213 |
| i | Mama wa waumini hatawaliwi na chuki au hisia katika kusimulia hadithi ya mtukufu mtume (s.a.w.w.), | 213 |
| ii | Yenye kupendeza au kuchukiza yanaamuliwa kwa sheria ya dini, | 213 |
| iii | Kuna riwaya yoyote inayopingana na madai ya mama wa waumini? | 213 |

Barua ya 76 214

i Alitawaliwa na hisia kali za moyoni, 214

ii Uthibitisho wa uzuri na ubaya kuamuliwa na akili, 214

iii Hadithi sahih zakanusha madai ya ummul-mu'minin, 214

iv Hadithi iliyosimuliwa na umm salama ni bora zaidi kuliko yake. 214

Barua ya 77 - Kuomba sababu za kupendelea hadithi za umm salamah 220

Barua ya 78 - Sababu za kupendelea hadithi ya umm salamah kwa nyongeza ya zile zilizokwisha tangulia 221

Barua ya 79 - Makubaliano ya wote pamoja (ijmai) yalithibitisha ukhalifa wa siddiq 224

Barua ya 80 - Hakuna makubaliano ya pamoja – (ijmai) 225

Barua ya 81 - Makubaliano ya Maoni ya Pamoja Yalijitokeza Yenyewe tu Wakati Upinzani Ulipokoma 228

Barua ya 82 - Hayakuwapo Makubaliano ya Maoni ya Pamoja (Ijmai), na Ugomvi na Mgawanyiko Havikwisha 229

Barua ya 83 - Utathibitishaje Kwamba Masahaba wa Mtume, kwa Kujua Hasa, Walipuuza Hadithi Zake na Bado Wakawa Hawana Hatia ya Upotofu? 233

Barua ya 84 - uainishaji wa Kauli hizi Mbili, Sababu za Imamu Kukataa Kudai Haki Yake 234

Barua ya 85 - Maombi ya Mifano ya Maeneo Ambayo Masahaba Hawakutii Amri na Hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) 238

Barua ya 86 - Msiba Mkubwa wa Alhamisi, Sababu Iliyomfanya Mtume (s.a.w.w.) Asiandike wosia 239

Barua ya 87 - Udhuru Katika Tukio la Msiba Mkubwa, Na Mjadala Muhimu juu ya Udhuru huo 244

Barua ya 88 - Visingizio na Maelezo ni Batili na Bandia 247

Barua ya 89 252

i Kukiri kwa Visingizio na Maelezo kuwa Dhaifu, 252

ii Maombi ya Kadhia nyingine za Masahaba Kukaidi Amri na Hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). 252

Barua ya 90 - Jeshi La Usamah 253

Barua ya 91 257

i Utetezi wa Masahaba Kutokwenda na Jeshi la Usamah, 257

ii Kukosekana Hadith Sahih, Mutawatir Inayowalaani wale Ambao Hawakujiunga na Jeshi hilo. 257

Barua ya 92 259

i Kisingizio kwa Niaba ya Sahaba Hakipingani na Maelezo yetu, 259

ii Hadithi ya Shahristani Imethibitishwa na Wanahadith Mashuhuri. 259

Barua ya 93 - Maombi ya Matukio Mengine ya Sahaba Kukiuka Amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) 262

Barua ya 94 - Amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ya Kumuuwa Mhaini 263

Barua ya 95 - Kisingizio cha Kutokumuuwa Mhaini 265

Barua ya 96 - Kupingwa kwa Kisingizio 266

Barua ya 97 - Maombi ya Kadhia Zote Ambamo Masahaba Walikaidi Amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) 267

Barua ya 98 268

i Dokezo Kwenye Baadhi ya Matukio Ambamo Masahaba Hawakutekeleza Amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), 268

ii Kugusia Matukio Mengine ya Masahaba Kutenda Kulingana na Maamuzi yao Binafsi Kuliko Kutii Amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). 268

Barua ya 99 270

i Katika Matukio Hayo Walipendelea Kufanya kile Kilichokuwa ni kwa Masilahi ya Umma, 270

ii Maombi ya Matukio Yaliyobaki. 270

Barua ya 100 271

i Masahaba Hata Wawe Wametenda kwa nia na Azma Njema, Hilo Liko Nje ya Mada ya Mjadala, 271

ii Kukubali Maombi. 271

Barua ya 101- Kwa nini Imamu Hakumpinga Abu Bakr na Wafuasi wake Dhidi ya Kuchaguliwa na Kula Kiapo Kwake Huko Saqifa kwa Msingi wa Hadithi Yoyote ya Wazi Inayohusu Ukhalifa na Urithi Wake? 274

Barua ya 102 275

i Sababu ya kwa nini Imamu Hakupinga Mnamo Siku ya Saqifa, 275

ii Dokezo Fupi la Upinzani wake na ule Upinzani wa Wafuasi wake na Vikwazo Katika Njia yao. 275

Barua ya 103 - Ni Lini Ali na Wafuasi wake Walifanya Malalamiko? 275

Barua ya 104 279

i Idadi Kubwa ya Matukio ya Upinzani wa Imamu na Wafuasi wake, 279

ii Malalamiko ya Zahra (as). 279

Barua ya 105 - Maombi ya Hadithi Nyingine Kutoka kwa Wengineo 284

Barua ya 106 285

i Malalamiko ya Ibn Abbas, 285

ii Malalamiko ya Hasan na Husein, 285

iii Hoja Ya Sahaba Mashuhuri Shi'ah, 285

iv Ya Shi'ah Maarufu Miongoni mwa Sahaba. 285

v Dokezo za Haki ya Urithi wa Ali (a.s.) Katika Malalamiko. 285

Barua ya 107 - Ni Wakati gani Walitaja Haki ya Uwasii wa Ali? 288

Barua ya 108 - Kuthibitisha Hoja ya Uwasii 289

Barua ya 109 297

Barua ya 110 298

i Imani ya Shi'ah ni kwa Msingi wa Mafunzo ya Maimamu wa Ahlul-Bayt, 298

ii Shi'ah Walikuwa wa Mwanzo Katika Shughuli za Uandishi na Waliandika na Kukusanya Vitabu Wakati wa Kipindi cha Masahaba, 298

iii Walikuwepo Waandishi Wasio na Idadi Wakati wa Tabi'in, na Wafuasi 298

Barua ya 111 - Kusadikisha 310

Barua ya 112 - Shukurani 311

Angalizo 311

# DIBAJI

## WASIFU MFUPI WA MWANDISHI WA KITABU HIKI SAYYID ABDULHUSAIN SHARAFUDDIN AL-MUSAWI

Sayyid Abdulhusain Sharafuddin al-Musawi alizaliwa mwaka wa 1290 Hijria huko Kadhmain (kaskazini ya Baghdad, Iraq). Baba yake alikuwa ni Yusuf bin Jawad bin Ismail. Mama yake ni Zahra bint Sayyid Hadi bin Sayyid Muhammad Ali na kuishia kwa nasaba fupi ya Sharafuddin, mmoja wa watu watukufu wa familia hii nzuri.

Amesoma katika miji ya Samarra na Najaf huko Iraq, na alikuwa ni mwanafunzi mwenye bidii sana na alifuzu vizuri masomo yake. Akiwa na umri wa miaka 32 alihamia Milla, kaskazini ya Lebanon. Akiwa huko alfundisha na kufungua shule, madrasah na hawza kadhaa ambazo zipo hadi leo.

Kutokana na uvamizi wa Wafaransa na kutaka kumuua, ilimbidi ahamie mjini Damascus kwa muda yeye na familia yake pamoja na chifu wa Milla.

Sayyid Abdulhusain Sharafuddin al-Musawi alikuwa mwanachuoni mkubwa, na katika mambo yaliyokuwa yanamsumbua ni kukosekana kwa umoja wa Waislamu, hususan Sunni na Shia wakati tofauti zao sio za kimsingi kiasi cha kutengana hivyo. Alifikiria njia ya kufanya, hatimaye, mwaka wa 1329 Hijria aliamua kusafiri kwenda Misr ili kuonana na wanazuoni wa huko na ajaribu kufanya mazungumzo nao juu ya suala hili la umoja. Lakini kabla ya kufikia lengo hili, aliona kwamba kuna haja kwanza ya kufanya mdahalo ili kujadiliana juu ya hitilafu zilizopo na kuzitolea ufafanuzi na ufumbuzi (kwani yeye aliona ni hitilafu ndogo sana na haziwezi kuzuia umoja wa Waislamu).

Kwa bahati nzuri, akiwa Misr alikutana na ulamaa kadhaa wenye busara na akajadilana nao katika mambo mengi ya dini kwa hali ya maelewano sana. Kati ya wanazuoni ambao alijadiliana nao, mmoja wao alikuwa Sheikh Salim al-Bisri al-Malik ambaye alikuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha al-Azhar. Baada ya kujadiliana kwa muda, Sheikh Salim al-Bisri aliomba aandike maswali yake kwa mtindo wa barua na yeye Sayyid Sharafuddin ajibu, na iwe wanajadiliana kwa njia hiyo. Walikubaliana na mjadala ukaanza ambao umezaa kitabu hiki ambacho unacho mikononi mwako.

Kitabu hiki ni kizuri sana kwa wale ambao wanatafuta ukweli na ambao wanautakia mema Uislamu ili hatimaye upatikane umoja wa Waislamu bila kuathiri madhehebu yoyote.

Allah Mwenye kujazi amlipe aalimu wetu huyu malipo mema kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kupigania umoja wa Waislamu na atujalie na sisi tufuate nyendo zake na hatimaye umoja huu upatikane, insha'Allah. Allah amuweka katika ujirani wa Maasumina wetu 14 na roho yake ipumzike kwa amani - insha'Allah.

**Dr. M. S. Kanju**

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichokuwa nacho mikononi mwako ni mjadala uliofanyika baina ya mwanachuo wa Kisunni (Sheikh Salim bin al-Bisri al-Malik aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar - Misr) na mwanchuo wa Kishia (Sayyid Sharafu-ddin wa Lebanon) katika miaka ya 1329 A.H. Mjadala huu ulikuwa katika muundo wa barua.

Hiki ni kitabu kikubwa cha rejea ambacho ni kuzuri sana kwa wale wanaofa nya utafiti wa kisomi.

Sisi tumekiona kitabu hiki kuwa ni chenye manufaa sana husuan wakati huu ambao kuna propanganda nyingi za ndani na nje za kuwapotasha Waislamu ili wasifikie lengo lao la umoja.

Kutokana na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Hii ni katika kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi hii ya Al-Itrah. Tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kuanzia kwa watarjuma na wengine hadi kufikia kuchapishwa kwa kitabu hiki. Allah (swt) awalipe kila la kheri hapa duniani na Akhera pia.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# BARUA YA KWANZA

**I. Salaam kwa Mjadili,**

**II. Kuomba ruhsa ya mdahalo.**

(I) Amani na rehema ya Allah na baraka Zake ziwe juu ya mwanachuoni mheshimiwa Sheikh Abdul-Hussein Sharafuddin Al-Musawi.

Bado sijawa mzoefu na dhamiri ya Shi'a wala sijaonja mwenendo wao, kwa vile sijawahi kufanya urafiki na yeyote katika wao, wala kujua desturi za wafuasi wake. Lakini siku zote nilikuwa na shauku ya kujadiliana (mdahalo) na wanachuo wao mashuhuri, hamu kubwa ya kuchanganyikana na watu wake wa kawaida ili kuchunguza misimamo yao na kujaribu kujua mielekeo yao, mpaka Allah (swt) aliponisaidia kusimama mbele ya fukwe ya bahari yako ya elimu, na ukaniruhusu kuonja kikombe chako kilichojaa tele; Allah alinisaidia kuzima kiu yangu. Naapa kwa jiji la elimu ya Allah, Mteule Babu yako, na kwa mlango wake, mhenga wako aliyeridhiwa, kwamba sijaonja kitu chenye kutosheleza mno kiu na chenye kuponyesha mno kwa wagonjwa kama mto wako uliofurika. Nimezoea kusikia kwamba ninyi wafuasi wa Shi'a mnapendelea kuwaepuka ndugu zenu Masunni, na kujitenga mbali nao, na kwamba mnajisikia raha na utulivu katika hali ya upweke na kukimbilia kujitenga na kadhalika. Lakini nimeiona nafsi yako ni yenye uchangamfu tulivu, makini katika kujadiliana, yenye adabu, imara katika hoja, mcheshi mzuri, mwaminifu katika kutetea hadhi, anayekubalika wakati wa kutoelewana, anayethaminiwa katika mashindano; kwa hiyo nimewaona Shi'a ni manukato mazuri ya kukaa nayo, na sehemu ya kutafutia kila msomi.

(II) Wakati nikuwa nimesimama kwenye ufukwe wa bahari yako iliyochafuka, naomba ruhusa yako kuogelea ndani yake na kupiga mbizi kwa ndani sana katika kutafuta vito vyake. Kama utanipa ruhusa yako, tutachimba kwa ndani kabisa ili kutafuta sababu za msingi za maelezo na utusitusi ambao kwa muda mrefu zimekuwa zikinikera; laa sivyo, yote itakuwa ni juu yako. Katika kuleta maswali yangu, sitafuti makosa au kasoro wala sipingi wala sikanushi, badala yake nina shida moja tu, kutafuta ukewli. Kama ukweli unadhihiri basi unastahiki kufuatwa kama sivyo niko kama mshairi mmoja ambaye alisema:

"Sisi katika tulichonacho, nanyi katika mnachotoa

wote tumeridhia, hata kama maoni yetu yanatofuatiana."

Kama utaniruhusu, mdahalo wangu na wewe utakomea kwenye mada mbili. Moja inashughulika na **Uimamu** wa madhehebu katika mizizi yake na matawi yake na nyingine inashughulika na Uimamu wa jumla, yaani urithi kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w). Sahihi yangu mwisho wa mijadala yangu yote itakuwa "S", na ya kwako na iwe "Sh." Kwa kutanguliza, naomba msamaha wako kwa kila kosa, na amani iwe pamoja nawe.

**Wako Mwaminifu. S.**

# BARUA YA PILI

## DHUL-QA'DAH 6, 1329 A.H.

**I. Salamu zajibiwa,**

**II. Ruhusa ya mdahalo yatolewa.**[1]

(1) Amani ya Allah iwe pamoja na Maulana Sheikhul-Islam, rehema na baraka Zake pia. Barua yako ya upole mno imenipa mimi na kunifadhilisha baraka nyingi ambazo kwamba ulimi hauwezi kukushukuru wewe kwa kutosheleza, wala hauwezi kukamilisha sehemu ya jukumu lake hata katika muda wake wote wa maisha. Umeweka matumaini yako juu yangu na kuniletea maombi yako ambapo wewe mwenyewe ni tumaini la mtu yeyote mwenye kutafuta, wewe ni kimbilio la yeyote yule anayetafuta hifadhi; mimi mwenyewe nimekuja njia yote kutoka Syria ili kuonja utamu wa ilimu yako na kutaka msaada wako, na nina hakika nitakuacha ukiwa imara katika msimamo wa matumaini mema isipokuwa Allah (swt) apende vinginevyo.

(2) Umeomba ruhusa ya kuongea. Unayo haki ya kuuliza na kuhoji. Sema chochote upendacho: Umepewa heshima hiyo; uamuzi wako ni wa mwisho na hukumu yako ni ya haki, na amani iwe pamoja nawe.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[1] Akiwa amepata ruhusa ya mdahalo alianza kueleza mambo ya masuala ya mdahalo hivyo kuonesha ustadi wake wa maadili na ubora wake kadiri ambavyo taratibu za mdahalo zinavyohusika. Utumiaji wa herefu "S" na "Sh" kwa dhahiri ni kipando kizuri kwa ajili ya kubebea mdahalo huu kwa vile "S" inaashiria jina lake "Salim" na kuwa kwake Sunni, ambapo "Sh" inaashiria jina la ukoo la mwandishi "Sharafud Din" na yeye akiwa ni Shia.

# BARUA YA TATU

## DHUL-QA'DAH 7, 1329 A.H.

**I. Kwa nini Shi'a Hawafuati Madhehebu ya Walio Wengi?**

**II. Haja ya Umoja**

**III. Umoja Hupatikana tu kwa Kufuata Madhehebu ya Walio Wengi.**

(1) Sasa nakuuliza sababu ya kwa nini ninyi Shi'a hamfuati madhehebu ya Waislamu wengi, namaanisha madhehebu ya *al-Ash'ari* katika kuamua kanuni za imani na Madhehebu manne katika matawi yake. Waislamu wamekubaliana kushikamana nayo katika kila zama na katika hali yoyote, wakikubaliana wote pamoja juu ya uadilifu wa waasisi wake na ijtihad yao, uaminifu wao, uchamungu, kuupa nyongo utajiri wa kidunia, ukweli, maadili mema na hadhi ya juu zaidi katika ilimu na matendo.

(2) Ukubwa ulioje leo wa haja yetu kwa ajili ya umoja na ulinganifu! Hili laweza kufanikiwa kwa ninyi kufuata madhehebu hizi kwa mujibu wa makubaliano ya Waislamu wote, hususani wakati huu ambapo maadui wa dini wameamua kutudhuru kwa njia zote zinazowezekana. Wameweka akili zao na mioyo yao juu ya malengo haya ambapo Waislam hawana habari, kama vile wameshikwa na usingizi mzito, wakiwasaidia maadui wao wenyewe kwa kuwaacha wazichambue safu zao wenyewe waupasue vipande vipande umoja wao kupitia ufuasi na ushabiki, ukiwaacha wametengana makundi ikiwapelekea kila mmoja kwenye upotofu, kukatiana mawasiliano wenyewe kwa wenyewe, hivyo mbwa mwitu wakatuwinda na huku mbwa wakionea uchu nyama zetu.

(3) Je, unaona vingine kuliko haya tunayoeleza hapa? Allah aongeze hatua zako kwenye kuunganisha safu zetu. Niambie kwani utasikilizwa wakati ukizungumza na kutiiwa wakati ukitoa amri, na amani iwe pamoja na wewe.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA NNE

## DHUL-QA'DAH 8, 1329 A.H.

**I. Uthibitisho wa Kisheria Unaamuru Ufuasi Kwenye Madhehebu ya Ahlul-Bayt,**

**II. Hakuna Uthibitisho Unaoamuru Ufuasi Kwenye Madhehebu ya Wengi,**

**III. Vizazi vya Karne Tatu za Mwanzo Kamwe Havikujua Madhehebu haya Manne [ya Sunni],**

**IV. Uwezekano wa Ijtihad,**

**V. Umoja Unaweza Kupatikana kwa Kuyaheshimu Madhehebu ya Ahlul-Bayt.**

(1) Kushikamana kwetu, katika kanuni za imani kwenye madhehebu nyingine mbali na ile ya *Ashaira,* na kufuata kwetu katika matawi ya Uisilamu ya madhebu nyingine mbali na hizo madhehebu nne, kamwe haijawa kwa sababu ya kuwa na ushupavu au ushabiki, wala haikuwa kwa sababu ya kuwa na mashaka na Ijtihad ya Maimamu wa madhehebu hizi, uadilifu wao, uaminifu, umoja wao, au ukubwa wao katika ilimu na matendo.

Bali uthibitisho wa kisheria, umetuamuru sisi kufuata madhehebu ya Maimamu kutoka Nyumba ya Mtume, chanzo cha Ujumbe, nyumba ambayo malaika wanatembelea mara kwa mara, makazi ya wahyi na msukumo wa kiroho. Kwahiyo, wakati wote tumerejea kwao ili kufahamu masuala yote yanayohusiana na matawi ya imani *fiqh* katika mizizi na misingi (*doctrines*), katika elimu ya maadili, mwenendo na tabia. Tumefanya yote haya kwa kuafikiana na hukumu ya ushahidi na uthibitisho, huku tukifuata Sunnah ya Bwana wa Mitume na Manabii, amani ya Allah iwe juu yake na kizazi chake chote.

Lau uthibitisho ungeturuhusu sisi kuwa tofauti na Maimamu wa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.), au lau tungelikuwa na uwezo wa kuupata ukaribu wa Allah (swt) kwa kufuata madhehebu za wengine, basi tungelifuata kwa ujumla nyayo za umma, huku tukisisitiza urafiki wa kuimarisha mfungamano wa undugu. Kinyume chake, uthibitisho bayana unasimama katikati ya njia ya muumini, ukimgeuza kutokana na kufuata mtazamo wake mwenyewe.

(2) Bado, huo wingi hauwezi kuthibitisha kwamba madhehebu yao wenyewe lazima ipendelewe juu ya hizo nyingine achilia mbali kule kuifanya kuwa ni wajibu. Tumetazama kwenye nyudhuru za Waislamu kama mtu anayechunguza kwa kina kwa macho makali, lakini hatukuona uthibitisho wa hoja yako isipokuwa kile ulichotaja cha ijtihad zao, uadilifu wao na ubora wao. Hata hivyo wewe unajua kwamba ijtihad, uaminifu, uadilifu na ubora wa hadhi siyo milki ya wao peke yao, kwa hiyo, vipi ikiwa hali ni kama hiyo, Madhehebu zao ziweze kuwa ni wajibu kwa sababu tu ya kuyaonesha kwako? Sidhani kwamba kuna yeyote ambaye anadiriki kutetea kupendelewa wao zaidi katika ilimu au matendo kuliko Maimamu wetu ambao ni kizazi - *al-Itrah*, kilichotoharishwa, safina za uokoaji za umma, Lango la wokovu, usalama dhidi ya mfarakano katika dini, bendera za mwongozo, kizazi cha Mjumbe wa Allah swt. na mabaki yake katika umma. Yeye (saww) alisema "Msiwatangulie mbele yao msije mkaangamia, wala msibakie nyuma yao msije mkaangamia. Msiwafundishe, kwani wao wana ilimu zaidi kuliko nyinyi." Lakini ni amri za siasa za zama za mwanzo wa Uislamu (ndizo zilizobadilisha mambo).

Nashangaa kuhusu madai yako kwamba vizazi vizuri vilivyopita wamefuata madhehebu hayo, na kuyaona ya haki zaidi na madhehebu bora na kwamba walikubali kushikamana nayo katika kila zama na nchi za mbali. Unasema hivyo kama vile hujui kwamba watangulizi wetu, vizazi vizuri vilivyopita, kwamba vilifuata kizazi cha Muhammad na kile ambacho haswa kiliunda nusu ya idadi ya Waislamu wote, walifuata tu imani ya Maimamu miongoni mwa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w). Hawakuona mbadala kwayo, na wamekuwa hivyo tangu wakati wa Ali na Fatima (a.s.), wakati ambapo si *al-Ash'ari* wala Imamu yeyote wa madhehebu manne, au hata baba zao aliyekuwepo hai (yaani, hawajazaliwa bado), kama ambavyo unajua vema.

(3) Vizazi vya karne tatu za kwanza, kamwe hawakufuata yoyote kati ya madhehebu hizo kabisa. Basi zilikuwa wapi madhehebu hizo wakati wa kipindi hicho cha vizazi vitatu, vizazi vilivyokuwa bora mno? Al-Ash'ari alizaliwa 270 A.H na kufa 320 A.H. Ibn Hanbal kazaliwa 164 A.H na kufa 241 A.H. Al-Shafii kazaliwa 150 A.H. na kufa 204 A.H. Malik alizaliwa 95 A.H.[2] na kufa 179 A.H. Abu Hanifah alizaliwa 80 A.H. na kufa 150 A.H. Mashia wanafuata madhehebu ya Maimamu kutoka Nyumba ya Mtume, na hakika watu wa nyumba wanajua nyumba yao ina kitu gani ndani yake. Wasiokuwa Shi'ah wanafuata madhehebu ya maswahaba wanachuoni na *tabi'ini*; sasa ni kipi kinachofanya kuwa ni "lazima" juu ya Waislamu wote, baada ya karne hizo tatu kupita, kufuata madhehebu hizo badala ya ile iliyokuwa ikufuatwa kabla yao?

Ni kitu gani kilichowafanya wageuze nadhari zao kutoka kwa wale ambao walikuwa hirimu pekee tu na Kitabu cha Allah chenyewe na wenza wake, kizazi cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na wadhamini wake, na safina ya umma ya wokovu, viongozi, walinzi, na lango la wokovu?

(4) Nini kilichosababisha mlango wa ijtihadi kufungwa mbele ya Waislamu baada ya kuwa uliwekwa wazi kabisa wakati wa karne tatu za kwanza kama si kukosa ari, kuendeleza starehe, uzembe, kukubali kunyimwa na kutosheka na ujinga? Nani atajiachia mwenyewe, kwa kujua au kwa kutokujua, kusema kwamba Allah (swt.) hakutuma mbora wa Wajumbe na Mitume akiwa na mafundisho Yake, wala hakutuma *wahyi* kwake ambao ni Kitabu bora na Sahifa bora kushinda vitabu vyote, kikiwa na hukumu na *aqida*, wala hakukamilisha dini Yake kwa ajili yake na hakukamilisha neema zake juu yake, wala hakumfundisha yeye ilimu ya mambo yaliyopita na yaliyopo, isipokuwa kwa lengo moja tu kwamba jambo lote lingeishia kwenye maimamu wa madhehebu zile ili kuyahodhi kwa ajili yao wenyewe? Kisha wangewazuia wengine kulipata kutoka vyanzo vyovyote vingine, kana kwamba imani ya Kiislamu, katika Kitabu Chake na Sunnah, dalili zote nyingine na maelezo ni mali yao wenyewe na kwamba wamezuia kuendelea nayo katika njia yeyote kinyume na maoni yao… Je, wao walikuwa warithi wa Mtume au Allah swt. alifunga kupitia kwao warithi na Maimamu au amewafundisha ilimu ya mambo yaliyopita na yajayo, na kwamba amejaalia juu yao ambacho hajajaalia juu ya yeyote miongoni mwa wanadamu?

Hapana! Walikuwa sawa tu kama watu wengine wengi, nguzo na walinzi wa ilimu, mawaziri na walinganiaji. Wale ambao hulingania kwa ajili ya ilimu wako mbali sana na ufungaji wa milango dhidi ya wengine au kuwazuia wengine wasiifikie. Wao kamwe hawazifungi akili wala kuishiliza nadhari ya umma kwao wenyewe tu, wala hawawezi kuzifunga nyoyo za watu au kuwafanya wengine kuwa mabubu, vipofu, kuwafunga pingu au minyororo. Hili kamwe haliwezi kuhusishwa nao isipokuwa kama shutuma za muongo, na maelezo yao wenyewe hushuhudia maelezo yetu.

---

[2] Katika wasifu wake wa Maliki, Ibn Khallikan anaonesha katika kitabu chake *Al-a'yan* kwamba mtu huyo alikaa kwenye tumbo la ama yake kwa takriban muda wa miaka mitatu. Kauli kama hiyo inatajwa na Ibn Qutaybah ambaye anamjumuisha Malik miongoni mwa wenye busara na hekima katika uk. 170 wa kitabu chake Al-Ma'arif, akimuelezea katika. uk 198 miongoni mwa watu ambao kwamba mimba za mama zao zilivuka kipindi cha kawaida.

(5) Ngoja sasa tutafakari juu ya suala ambalo kwalo umevuta nadhari yetu; Umoja wa Waisilamu. Ninachokiona ni kwamba suala hili halitegemei juu ya *Shi'a* kuiacha imani yao, wala *Sunni* kuacha imani yao. Kuwataka *Shi'a* kufanya hivyo bila ya kuwataka na wengine (Sunni) kufanya kama hivyo ni kustahabu bila kuenea, au hata kupendelea wasio mustahabu. Ni kumdai mtu kisicho katika uwezo wake kama inavyojulikana kutoka kwenye utangulizi wetu.

Ndio, umoja na mlingano vyaweza kupatikana kama mtaiacha huru madhehebu ya Ahlul-Bayt na kuiona kama mnavyoiona madhehebu yenu wenyewe ili kwamba Shafii, Hanafi, Maliki na Hanbali watawachukulia wafuasi wa Ahlul-Bayt kama wanavyojiona wao wenyewe. Ni hapo tu umoja wa Waisilamu waweza kupatikana, na wataunganika katika kundi moja la waumini.

Tofauti miongoni mwa madhehebu za Sunni sio kidogo kama ilivyo kati ya madhehebu za Sunni na Shi'a kama inavyo shuhudiwa na maelfu ya vitabu juu ya kanuni na matawi ya imani ya makundi yote (ya Sunni); kwa hiyo, kwanini watu mbalimbali miongoni mwenu wanawalaumu Shi'a kwa kutofautiana na Sunni? Kwanini kwa dalili hiyohiyo wasiwalaumu Sunni kwa kutofautiana na Shi'a, bali hata kwa kutofautiana wao wenyewe kwa wenyewe? Kama madhehebu zaweza kuwa nne, kwanini zisiwe tano? Vipi inakuwa sahihi kuwa na madhebu nne lakini sio tano? Vipi madhehebu nne zionekane kama zinazoweza "kuunganisha Waislamu", na wakati zikiongezeka kufikia tano umoja unavunjika na Waislamu wanagawanyika wenyewe miongoni mwao? Napenda wakati unatuita kwenye "umoja wa madhehebu" vilevile uwaite wafuasi wa madhehebu manne kwenye umoja huo huo, kufanya hivyo ni rahisi mno kwako na kwao. Lakini hata hivyo kwa nini umetulenga sisi katika mwito wako? Je, umewaona wafuasi wa Ahlul-Bayti wanavunja umoja ambapo wafuasi wa madhehebu nyingine wanaunganisha nyoyo na dhamiri ingawa madhehebu zao na akili zao ni tofauti, kuhisi kwao na mielekeo yao ni mingi? Sikufikirii wewe hilo nikijua mapenzi yako kwa ndugu zako, na amani iwe pamoja nawe.

**Wako Mwaminifu Sh.**

# BARUA YA TANO

## 9 DHUL-QA'DAH, 1329 A.H.

**1. Kukubaliwa kwa Hoja,**

**II. Kuomba Ushahidi wa Kina.**

Assalaam 'Alaykum.

Barua yako imekuwa yenye kueleweka wazi kabisa, iliyopangwa vizuri, yenye taadhima. Ni barua ambayo ina ufasaha mwingi, yenye nguvu katika dhamira. Haikuacha jaribio lolote ili kuthibitisha kwamba kufuata madhehebu ya walio wengi katika misingi na matawi sio lazima, na kutoacha juhudi zozote kuthibitisha kwamba mlango wa Ijtihadi unapaswa kuwa wazi. Barua yako kwa hiyo ina nguvu juu ya mambo yote haya, sahihi katika kuthibitisha kila mojawapo, na sisi hatukanushi utafiti wako makini kuhusiana nayo, ufafanuzi wako juu ya utusitusi wake, ingawa kwa kweli tulikuwa hatuna ufahamu nao, na maoni yetu kuhusiana nayo yanafanana na yako.

Tuliuliza juu ya sababu ya kwa nini ninyi Mashia mnakataa madhehebu yanayofuatwa na wengi, na majibu yako yalikuwa kwamba ni kwa sababu za "ushahidi wa kisheria" ambapo ulitarajiwa kuelezea hili kwa urefu. Je unaweza kukubali sasa na kuzieleza pamoja na ushahidi unaokubalika kutoka katika Qur'ani au Sunnah ambazo kama ulivyosema, hizo zinamzuia muumini wa kweli kufuata matakwa yake binafsi. Ahsante, na amani iwe juu yako.

**Wako mwaninifu, S.**

# BARUA YA SITA

## DHUL-QA'DAH 12, 1329 A.H.

**I. Rejea za Ushahidi Unaolazimisha Kufuata Ahalul-Bayt**

**II. Amirul-Mu'minin (a.s.) Atoa wito wa Kufuata Madhehebu ya Ahlul-Bayt.**

**III. Kauli Yenye Kufaa ya Imam Zaynul-Abidiin.**

Alhamdulillahi wewe ni mtu unayeweza kushawishika kwa dokezo tu, bila kuhitaji maelezo marefu, uko mbali na kutilia shaka ukweli wenyewe hasa kwamba kile kizazi kilichotakaswa, *itrah* - Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) ni wabora kuliko wengine wote. Hali yao inajulikana sana, wao wamewapita wale wote wenye sifa za juu na wamejitofautisha wenyewe kwa kutokufanana na wao. Wamebeba kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) elimu ya Mitume waliopita, na kutoka kwake wamemeng'enya na kuelewa vema sheria za kisekula na kidini.

(1) Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa hiyo aliwatangaza wao kuwa sawa tu na Qur'ani Tukufu na kuwaweka kama vigezo vya mfano wa tabia njema kwa wale waliojaaliwa kuwa na tafakari; na Safina ya salama wakati unafiki na mawimbi yake yenye ghasia utakapouzonga usalama wa umma, na kuulinda kutokana na faraka kama dhoruba za mgawanyiko zikijitokeza; na Lango la Wokovu: yeyote atakayeliingia atasamehewa; na kama kamba imara ya Mwenyezi Mungu ambayo haiwezi kukatika.

(2) Amirul Mu'minin (a.s) ananukuliwa katika khutba 86 katika *Nahjul Balaghah* akisema:

"Basi mnakwenda wapi (8:26). Mnageuzwa wapi (6:95; 10:34; 35:3; 40:62), wakati bendera zimepandishwa juu, ishara ziko wazi, na mnara wa taa umesimamishwa? Basi mnageuziwa wapi? Hapana! Mnawezaje kufumbwa macho kama vipofu ambapo Ahlul-Bayt wa Mtume wenu wapo miongoni mwenu? Wao ndio wasimamizi wa haki, Bendera za dini na ndimi za kweli. Kwa hiyo waheshimuni kama mnavyoiheshimu Qur'ani na wafuateni kwao kama ngamia wenye kiu wanavyoyafuata maji. Enyi watu; chukueni hili[3] kutoka kwa Mtume wa Mwisho (s.a.w.). 'Yeyote yule kutoka miongoni mwetu anapokufa, kwa kweli hakufa hasa, na yeyote yule kutoka miongoni mwetu akigeuka kuwa vumbi (baada ya kufa), hageuki kuwa vumbi kweli;' kwa hiyo msiseme msiyoyajua, kwani kuna ukweli mkubwa kabisa katika yale mnayokanusha. Kubali hoja ya mtu ambaye huna hoja dhidi yake, na mtu huyo ni mimi. Je, sikushughulika kwa mujibu wa kile Kizito Kikubwa Zaidi'[4] (Qur'ani)? na ninawaachia miongoni mwenu 'Kizito Kidogo' (Ahlul-Bayt), na nimesimika miongoni mwenu bendera za imani?"[5]

Yeye (a.s.) anasema katika hotuba ya 96 ndani ya *Nahjul-Balaghah*: "Waangalieni Ahlul-Bayt wa Mtume wenu (s.a.w.); waigizeni mfano wao na fuateni nyayo zao kwani wao kamwe hawatawatoeni kwenye mwongozo wala hawatawarudisheni kwenye uharibifu; simameni wanaposimama na kaeni wanapokaa. Msiwatangulie mbele yao msije mkapotea na msikawie mbali mno nyuma yao msije mkaangamia." [6]

[3] Ana maana ya kusema: "Jifunzeni hili kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu swt. amani iwe juu yake na juu ya kizazi chake: 'Wakati mtu wa Nyumba ya Mtume (s.a.w.w.) anapofariki, kwa uhalisia huwa hafi,'" yaani nafsi yake hubakia iking'ara katika ulimwengu ule wa kweli. Hili pia limeelezwa na Sheikh Muhammad Abduh na wengineo.

[4] Amirul-Mu'minin (a.s.) alishughulika kulingana na Kizito Kikubwa zaidi, yaani Qur'ani Tukufu, akaacha vile Vizito Vidogo, yaani watoto wake, nyuma yake. Inasemekana pia kwamba kizazi chake ndio vigezo vya mfano wa tabia njema kwa watu wengine, kama ilivyoelezwa na Sheikh Muhammad Abduh na wafasiri wengine wa *Nahjul-Balaghah.*

[5] Nahj al-Balagha (nakala ya Cairo) Hotuba Namba 83, pt.1 uk. 152.

[6] *Nahj al-Balaghah* (Nakala ya Cairo) *Hutuba namba* 93, pt. 1, uk. 189 tafsiri ya shamin, *Hotuba namba* 100.

Yeye (a.s.) amewataja tena kama ilivyoelezwa kwenye hotuba 237 ya *Nahjul-Balaghah,* anasema: "Wao ni uhai wa elimu na kifo cha ujinga; uvumilivu wao unakujulisheni elimu yao; muonekano wao wa nje unakujulisheni dhamira zao, na kimya chao kinaonyesha hekima ya maneno yao. Hawatofautiani na ukweli wala hawapingani wao kwa wao kuhusu ukweli. Wao ni nguzo za Uislamu na milango ya wokovu. Kupitia kwao haki ilipatikana na batili iliondolewa na ulimi wake uling'olewa. Wanaitambua dini kwa uangalifu na kujali, sio kama kusikia na kusimulia, kwani 'wasimuliaji' wa elimu ni wengi mno lakini wanaojali kuilinda ni wachache."[7] Yeye (a.s.) kama ilivyoelezwa kwenye *Nahjul-Balaghah* hotuba ya 153 amesema pia: "Kizazi (Ahlul-Bayt) chake ndio bora sana na familia yake ndio bora zaidi kuliko familia zingine, na mti wake ndio mti bora, ulipandwa mahali patakatifu (Haram), na ulikua kama mzaituni; matawi yake ni marefu na tunda lake halipatikaniki."[8]

Yeye (a.s.) ananukuliwa katika hotuba ya 153 ya *Nahjul-Balaghah* akisema tena: "Sisi ndio bendera, wenza na milango." "Nyumba hazipaswi kuingiwa isipokuwa kwa kupitia katika milango yake (Rejea Qur'ani Takatifu (2:189), yeyote anayeingia nyumba kinyume na mlangoni mwake anaitwa mwizi." akaendelea hadi akafikia kusema, wakati akielezea kizazi (*Itrah*): "Wao ni sehemu muhimu ya Qur'ani na ni hazina ya Mwingi wa Rehema. Wanapozungumza husema ukweli au wanaponyamaza hakuna anaye thubutu kuzungumza mbele yao. Kwa hiyo ngoja mhenga azungumze ukweli kwa watu wake, akiendeleza hoja yake."[9] Amesema katika hotuba 146 ya *Nahjul-Balaghah*: "Tambua kwamba huwezi kuujua mwongozo mpaka umjue ni nani anayeutelekeza, wala huwezi kufuata Kitabu (Qur'ani Tukufu) mpaka umjue anayekipinga, na kamwe hutashikamana nacho mpaka ujue nani amekiacha; kwa hiyo yatafute hayo kutoka kwa wale wanaokimiliki, kwani wao ni uhai wa elimu na kifo cha ujinga. Wao ni watu ambao hukmu zao zinakujulisha juu ya elimu yao, kimya chao kinakujulisha juu ya nguvu ya maneno yao, muonekano wao wa nje unakujulisha juu ya nafsi zao za ndani; kamwe hawaivunji dini, wala kufarakana miongoni mwao wenyewe katika hilo, ambapo kuna shahidi mkweli miongoni mwao na mzungumzaji mkimya (Qur'ani)."[10]

(1) Kuna semi nyingine nyingi mno za Amirul-Mu'minin kuhusu Ahlul-Bayt, kama hii: "Kupitia kwetu mnaongozwa katika giza, mnapanda hadi kwenye vilele vya hadhi, na kwa kupitia kwetu mmeufikia mwanga wenye kuondosha giza nene.[11] Sikio lisilomsikiliza mlinganiaji nalifanywe kiziwi."[12]

(2) Anazidi kusema: "Enyi watu! Pateni nuru yenu kutoka kwenye mwanga wa taa za mlinganiaji anayefuata yale anayolingania, na kunyweni kutoka kwenye chemchemi ambayo imesafishwa kutokana na uchafu.13

(3) Anasema tena: "Sisi ndio mti wa Utume na wapokeaji wa Ujumbe, na mahala ambapo malaika wanazuru kila mara, na sisi ni hazina ya elimu, chemchemu za hekima. Mfuasi na mpenzi wetu anayo haki ya kutumaini rehema za Allah, na yule anayetuchukia na kutufanya sisi maadui zake anasubiri ghadhabu za Mwenyezi Mungu."[14]

---

[7] *Nahj al-Balagha* (Nakala ya Cairo) Hotuba na 234, pt.1 uk. 259-Tafsiri ya Salmin Hotuba namba 240. *Nahj al-Balaghah* (Nakala ya Cairo) Hutuba namba 93, pt. 1, uk. 189 tafsiri ya Salmin, Hotuba namba 100.

[8] *Nahj al- Balaghah* (nakala ya Cairo), Hotuba Na. 190, uk.185.-Tafsiri ya Salmin Hotuba na.97.

[9] *Nahj al-Balaghah* (toleo la Cairo), Hotuba na. 150, pt.1, uk.58.-Tafsiri ya Salmin Hotuba na 155.

[10] *Nahj al-Balaghah* (nakala ya Cairo), Hotuba Na.143pt.2.uk. 73 –Tafsiri ya Salmin Hotuba Na.149.

[11] Shayky Muhammad Abduh, Mshereheshaji wa kitabu cha *Nahujul-Balaghah*, ameelezea juu maneno 'usiku wa giza' kuwa na maana ya usiku ambao mwezi unafunikwa kabisa, baada ya hapo mwezi mchanga hutokea.

[12] *Nahjul-Balaghah* (Nakala ya Cairo), Hotuba na. 3, uk. 33 Tafsiri ya Salmin Hotuba Na. 8

[13] *Nahjul-Balaghah* (nakala ya Cairo). Na. 201 pt. Tafsiri ya Salmin Hotuba na. 108.

[14] *Nahjul-Balaghah* (nakala ya Cairo), Hotuba na. 105, pt.1 uk. 214 Tafsiri ya Salmin Hotuba na.112

(4) Miongoni mwa yale ambayo amesema kuhusiana na haya ndani ya Nahjul-Balaghah ni: “Wako wapi wale wanaodai kwamba wamezama kwa kina katika elimu kuliko sisi? (angalia Qur’ani Tukufu 3:7 na 4:162). Madai yao ni ya uwongo na uovu dhidi yetu, kwani Mwenyezi Mungu ametunyanyua daraja sisi na kuwatweza wao; na ametujaalia sisi na kuwanyima wao; na ameturuhusu sisi kuingia (kwenye ngome ya elimu) na akawatoa wao nje. Kupitia kwetu mwongozo unapatikana na upofu huondoshwa. Hakika, Maimamu kutoka miongoni mwa Kureishi walipandikizwa ndani ya kizazi cha Hashim. Uimamu hauwezi kumstahiki mwingine yeyote wala serikali pia.” Kisha amesema: Lakini watu wanapendelea mapato ya haraka kuliko ya baadae; wanakiacha kisima safi na kunywa kutoka kwenye kichafu,”15 mpaka mwisho wa maelezo yake.

(5) Anazidi kusema: “…. Kwa yule miongoni mwenu anayekufa kitandani mwake, huku akijua haki za Mola wake na Mtume wake na Ahlul-Bayt, anakufa kama shahidi wa dini na malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu, na anasitahiki ujira wake kwa matendo mema aliyoyanuia kuyafanya: nia yake mwenyewe itasimama kufidia kama matumizi ya upanga wake (katika jihadi).” 16

(6) Anasema tena: “sisi ni watakatifu; kizazi chetu ni kizazi cha Mitume. Kikundi chetu ni kikundi cha Mwenyezi Mungu, na kile cha maadui wetu ni cha shetani. Yeyote anayetulinganisha sisi na maadui zetu si mwenzetu.” [17]

Na Imamu Hasan (a.s), mjukuu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), anasema “Muogopeni Mwenyezi Mungu kuhusu misimamo yenu kwetu, kwani sisi ni watawala wenu. “[18]

Imamu Zainul Abidin ‘Ali ibn al-Husein alipokuwa akikariri aya ifuatayo ya Qur’ani Tukufu: **“Enyi mlioamini. Muogopeni Mwenyezi Mungu na mshikamane na wale ambao ni wakweli.”(9: 119),** Baada ya hapo anaomba dua ndefu ambayo ilikuwa na maombi kwa ajili ya kupata daraja la juu kwa kuwa na “Wakweli.” Akieleza matatizo na uzushi wa wale ambao wamejitenga na Maimamu wa uongofu na Mti wa Utume. Aliendelea kusema kama ifuatavyo: “Wengine walikosea kutukadiria sisi, kwa visingizio vya aya za Qur’ani Tukufu zenye kufanana kwa mtazamo wao, na wakazipa tafsiri zao na kutilia shaka kuhusu riwaya zilizosimuliwa kuhusu hadhi zetu,” mpaka aliposema: “Ni kwa nani watu wa ulimwengu huu watatafuta kimbilio, kwani zile nguzo za dini zimesahauliwa na umma umegawanyika katika matapo, kila moja likikufurisha jingine, ambapo Mwenyezi Mungu anasema: **“Wala msiwe kama wale waliofarakana wakakhitilafiana baada ya kuwafikia dalili za wazi ….." (3:105).** Ni nani basi ambao wataaminiwa katika kuwasilisha hoja za ki-Mungu na kutafsiri hukmu zake mbali na wale wenza wa Qur’ani na kizazi cha Maimam wa Uongofu, na taa iliyo katikati ya giza, ambao Mwenyezi Mungu amewasimamisha kama Hoja Zake juu ya waja Wake? Yeye swt, hajawaacha waja Wake peke yao bila ya Hoja. Je, unawajua au unaweza kuwapata kwingine badala ya kutoka kwenye matawi ya Mti Uliobarikiwa, masalia ya wasomi ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea dosari zote, akawatakasa kikamilifu na kuwalinda dhidi ya madhambi na akaamuru kuwapenda wao, kama ambavyo inasemwa katika Qur’ani Tukufu.”[19]

Haya ni maneno halisi ya Imamu Zainul Abidini (a.s). Yatazame hayo na tazama nukuu yetu kutoka kwenye maneno ya Amir al-Muuminin (a.s), utaona kwamba yote yanawakilisha fikra ya madhehebu ya Shia kuhusiana na hili kwa dhahiri kabisa. Yanakubaliana kwa pamoja juu ya jambo hili, na vitabu vyetu vilivyo sahihi vyenye kuyanukuu hayo vinakubaliana katika hilo (ni *mutawatir*), na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

[15] *Nahjul-Balaghah* (nakala ya Cairo) Hotuba na. 104 pt. 2, uk. 36 Tafsiri ya Salmin Hotuba na. 146.

[16] *Nahjul-Balaghah* (nakala ya Cairo), mwisho wa Hotuba Na. 85, seh. 2, 156. Tafsiri ya salmin Hotuba na. 191.

[17] Imeripotiwa pamoja na mambo mengine, na Ibn Hajar al-Makki katika kitabu chake: *Sawa’iq Al-Mukhriqah*, uk. 142.

[18] Kitabu cha Ibn Hajar cha *Sawa’iq al-Mukhriqa* uk. 34, mwisho wa wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

[19] Angalia Tafsiri ya Aya ya Qur’ani, “**Shikamaneni wote kwa pamoja kwenye kamba ya Mwenyezi Mungu**.” Inapatikana kwenye kitabu cha Ibn Hajar cha *Sawaiq al-mukhriqah*, seh. 1 sura ya 2 uk. 90.

# BARUA YA SABA

## DHUL-QA'DAH 13, 1329 A.H.

**I. Maombi ya Uthibitisho Kutoka kwenye Maneno ya Allah na Mjumbe Wake,**

**II. Hoja Kutoka kwa Ahlul-Bayt Hazikubaliki.**

(1) Nipe uthibitisho wa kweli kutoka kauli ya Allah na Mjumbe Wake yenye ushahidi wa kuhalalisha kula kiapo cha utii kwa Maimamu miongoni mwa Ahlul-Bayt pekee. Na yaache kando maelezo ya mtu yeyote yule kuhusiana na suala hili isipokuwa ya Allah na Mjumbe Wake.

(II) Maelezo ya Maimamu wako hayawezi kutosheleza kutumika kama hoja dhidi ya wapinzani wao, na hoja kama hiyo hutengeneza mantiki ya mzunguko, kama ujuavyo, na amani iwe juu yako. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, S**.

# BARUA YA NANE

## DHUL-QA'DAH 1329 A.H.

**I. Kupuuza Maelezo Yetu Ya Mwanzo,**

**II. Kosa Katika Hoja Ya Mzunguko (Ya Mantiki),**

**III. Hadithi Ya Vizito Viwili,**

**IV. Tawatur Yake,**

**V. Wasioshikamana Na Itra Watapotea,**

**VI. Kufanana kwao na Safina ya Nuh, Lango la Wokovu, Na Usalama Dhidi ya Mfarakano wa Kidini,**

**VII. Ahlul-Bayt Inamaanisha Nini Kuhusiana na Suala Hili,**

**VIII. Sababu za kufanana na Safina ya Nuh na Lango la Wokovu.**

(1) Sikuziacha hadithi za Mtume; kwa kweli nilizitaja tangu mwanzoni kuonyesha kwamba ni lazima kuwafuata Maimamu ambao wanatokana na Ahlul-Bayt na sio wengine kwa kusema katika barua yangu kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amewaonyesha wao kuwa waunganishwa na Qur'ani kama viongozi ambao wana uwezo wa juu wa akili, kama Safina ya wokovu, kama usalama wa Waislamu na Mlango wa Toba, nilirejea hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambazo zina maneno hayo, ambayo yamo katika vitabu vingi vya hadithi. Pia niliandika kwamba, kwa rehema za Mwenyezi Mungu ungekuwa na hekima ya kutosha ya kuelewa hata marejeo mafupi tu hivyo kwamba haingekuwa muhimu kuelezea kila kipengele kwa urefu. Hivyo basi, baada ya kuonyesha kwamba ni muhimu kuwafuata na kuwatii Maimamu wetu, kinachofuata ni kwamba hadithi zao zinaweza zikanukuliwa na zikawa ushahidi kwa wapinzani wao na hivyo haiwi sawa na kuzungusha maneno. Walakini sasa nataka kuelezea kwa kirefu hadithi zile zote za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambazo niliziandika kwa ufupi. Mtukufu Mtume alisema wazi na hadharani: "Enyi watu, nawaachieni miongoni mwenu vitu viwili ambavyo kama mkivifuata, hamtapotoka kamwe baada yangu, vitu hivyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu - (Qur'ani Tukufu na Ahlul-Bayt wangu."[20] Alisema pia: "Miongoni mwenu nimewaachieni vitu fulani na mkivipenda kamwe hamtapotea. Vitu hivyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu- (Qur'ani Tukufu) ambacho kipo kama kamba ambayo inatambaa kutoka mbinguni mpaka aridhini, na kizazi changu. Ambao ni Ahlul-Bayt. Vitu hivi viwili havitaachana kamwe mpaka vitakapokuja kwangu katika chemchemu ya Kawthar (huko peponi) hivyo, muwe waangalifu katika kuwa navyo."[21]

Alisema pia: "Nawaachieni miongoni mwenu vitu viwili vizito, Kitabu cha Mwenyezi Mungu – (Qur'ani Tukufu) na Ahlul-Bayt wangu; na vitu hivi viwili havitaachana mpaka vitakapokuja kwangu Siku hiyo ya Hesabu. "[22]

---

[20] Imesimuliwa na Tarmidhi na Nasa'i kutoka kwa Jabir na kunukuliwa na Al-Muttaqi wa India mwanzoni mwa sura ya "Mshikamaano" kwenye kitabu chake *Kanz al-Ummal* pt. uk.44.

[21] Hadithi Na 874 katika *Sahih al-Tirmidhi*, kama ilivyosimuliwa na Zayd ibn Al-Arqam miongoni mwa hadithi zilizochukuliwa kutoka *Kanz al-ummal*, pt. 1 uk.44.

[22] Kama ilivyosimuliwa na Imam Ahmad (ibn al-Hambal) kutoka vyanzo viwili vya uhakika – katika *Musnad* yake kitabu cha 5 uk. 182 na kitabu cha 5 uk. 189 mwishoni. Pia kama ilivyosimuliwa na Tabraniy kwenye *Mu'jam al-Kabir* yake kutoka kwa Zayd ibn Thabit na kwenye *Kanz al-Ummal*, Juz. ya 1, uk. 44 pia kama ilivyosimuliwa na Al-Hakim kwenye *Mustadrak* yake sehemu ya 3, uk. 148

Alisema pia: “Baada ya muda sio mrefu mimi nitaitwa hivyo itabidi niondoke kutoka miongoni mwenu, lakini nawaachieni miongoni mwenu Vitu Viwili Vizito, Kitabu cha Aliye juu na Mwenye nguvu zote na kizazi changu. Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur’ani Tukufu) - ni kama kamba ambayo inatambaa kutoka mbinguni mpaka ardhini na kizazi changu ni (Ahlul-Bayt) watu wa nyumba yangu. Mwenyezi Mungu ambaye ni Mjuzi na Mtambuzi wa yote ameniambia kwamba viwili hivi havitaachana kamwe mpaka vitakapokuja kwangu Siku hiyo ya Hesabu. Kwa hiyo muwe waangalifu katika kuwa navyo.”[23]

Wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa anarudi kutoka kwenye Hija ya mwisho kwenda Madina, alipofika Ghadir-Khum alisimamisha msafara na akasema: “Inaonyesha kana kwamba mimi nimeitwa na ninakwenda zangu. Hata hivyo, ninawaachieni miongoni mwenu Vitu Viwili Vizito ambapo kimojawapo ni kikubwa kuliko kingine. Vitu hivyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu zote (Qur;an Tukufu) na kizazi changu. Kwa hiyo, muwe waangalifu katika kuwa navyo baada yangu. Vitu hivi viwili havitaachana mpaka vitakapokuja kwangu Siku ya Hesabu.”

Aliendelea kusema: “Mola, Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu zote ni Maula wangu na mimi ni Maula wa kila muumini wa kweli.” Halafu akaushika mkono wa Ali (a.s.) kwa mkono wake na akasema yeye (Ali) ni maula wa hao wote ambao mimi ni maula wao. Ee Mwenyezi Mungu wapende wale wampendao Ali na wachukie wale wanaomchukia…”[24]

Abdullah ibn Hantab alisema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu swt. alituhutubia pale Juhfah akasema: “Je, mimi si mwenye madaraka juu yenu kuliko mliyo nayo juu yenu wenyewe?” wote walisema; “Ndivyo unayo.” Halafu akasema: “Mtawajibika juu ya vitu viwili kwangu, navyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur’ani Tukufu) na kizazi changu.”[25]

Hadithi zote hizi za uhakika, ambazo zathibitisha moja kwa moja kwamba ni lazima kufuata Qur’ani Tukufu na Ahlul-Bayt sio hadithi za hivi hivi, zimerudiwa mara nyingi na zinasimuliwa kutoka kwa masahaba wa Mtume wasiopugua ishirini kwa kupitia vyanzo mbalimbali. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyarudia maneno haya tena na tena sio mahali pamoja tu bali ni kwenye sehemu nyingi na mara nyingi katika hadhara ili kuonyesha kwamba ni wajibu kuwafuata na kuwatii Ahlul-Bayt. Alitangaza habari hii wakati wa Hijja ya Mwisho, siku ya ‘Arafat na kule Ghadir-Khum, wakati wanarudi kutoka Ta’if, na Madina kwenye mimbari ya Msikiti. Mwisho kabisa, wakati akiwa kwenye kitanda yalipomkuta mauti na chumba chake kilijaa Masahaba wake, alisema: “Enyi watu! Baada ya muda sio mrefu nitatoweka na ingawaje nimekwishawaambia, ninarudia kwa mara nyingine tena kwamba nawaachieni miongoni mwenu vizito viwili, navyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Qur’ani Tukufu na kizazi changu – yaani, Ahlul-Bayt.” Halafu akamnyanyua Ali kwa mkono wake na akasema:

---

pamoja na ufafanuzi kwamba Hadithi hii ni ya uhakika kufuatia vipimo vilivyofungwa na Masheikh wawili Muslimu na Bukhari ingawaje hawakuingiza katika vitabu vyao. Dhahabi ameingiza katika vitabu vyake kutoka *Mustadrak* kwa sababu ya usahihi kwa mujibu wa vipimo vilivyofuatwa na Maheikkh wawili.

[23] Imeandikwa na Imam Ahmad (ibn Hambal) kutoka kwenye hadithi iliyosimuliwa na Abu Sa’id al-Khudri kwa njia mbili kwenye *Musnad* yake 3.3, kwanza mwishoni mwa ukurasa wa 17 na pili, mwishoni mwa ukurasa wa 26. pia imesimuliwa na Ibn Abi Shaybah, Abu Ya’li na Ibn al-Sa’id kutoka kwa Abu Sa’id, ikiwa ni hadithi na 945 kwenye *Kanz al-Ummal*, Jz.1, uk. 47.

[24] Imesimuliwa na al-Hakim kutoka kwa Zayd ibn Arqam katika Jz.3, uk. 109 kwenye *Mustadrak* yake, pamoja na ufafanuzi kwamba hadithi hii ni ya kweli kufuatia vipimo vilivyofanywa na kuhakikishwa na Masheikh wawili, ingawaje hawakuliingiza katika vitabu vyao kikamilifu. Pia imesimuluwa kupitia chanzo kingine kutoka kwa Zayd ibn al-Arqam na kusimuliwa kwenye *Mustadrak* Jz. 3, uk 533 pamoja na ufafanuzi kwamba ni sahihi, ingawaje masheikh wawili hawakuingiza kwenye vitabu vyao. Dhahabi pia ameiandika kwenye *Talkhis* yake kama hadithi sahihi.

[25] Tabraniy ameandika hadithi hii kama ilivyotajwa na ‘Allamah al-Mayyit. Pengine hamna ya ukweli kwamba khutuba iliyotolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) juu ya jambo hili haikuishia hapa kwa sababu khotuba ni maneno mengi, lakini sababu za kisiasa ziliwazuia waandishi wengi wa hadithi kutoa maelezo kamili ya khotuba hii. Hata hivyo, taarifa hii fupi kutoka katika khotuba hiyo inatosha kwa madhumini yetu.

"Angalieni huyu ni Ali: Yeye yuko na Qur'ani nayo Qur'ani ipo pamoja naye. Kamwe hawataachana mpaka watakapokuja kwangu kwenye hodhi ya Kawthar – Siku ya Hesabu" [26]

Kundi kubwa la watu mashuhuri ambao ni katika sehemu kubwa ya Waislam wamekiri kwamba huo ulikuwa wosia wa mwisho wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hata Ibn Hajar baada ya kuiandika *Hadith al-Thaqalaini* (Hadithi ya Vizito viwili), anatoa dondoo kwa kusema: "Hadithi ya 'Kushikamana' imetufikia kupitia kwenye vyanzo vingi na zaidi ya Masahaba ishirini wamesimulia." Kisha kitambo kidogo, akaendelea kusema: "Hapa shaka hujitokeza, na ni kwamba wakati ambapo hadithi hii imetujia kutoka vyanzo mbalimbali, bado vingine vinasema kwamba maneno haya aliyasema wakati wa Hijja yake ya mwisho, wengine wanasema ameyasema maneno haya akiwa Madina akiwa yu mgonjwa amelala kwenye kitanda chake alichofia na chumba kikiwa kimejaa masahaba wake, bado wengine wanasema ameyasema maneno haya akiwa Ghadir Khum au wakati wa kurudi kutoka Ta'if. Lakini hakuna ukinzani kwani inawezekana kwamba, kwa kuchukulia umuhimu na ukubwa wa Qur'ani na Ahlul-Bayt, na mtazamo wa kusisitizia jambo hili kwa watu, huenda Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameyarudia maneno haya kwenye nyakati na sehemu zote hizi ili kwamba mtu yeyote ambaye hakuyasikia maneno haya kabla aweze kuyasikia sasa.[27]

Aidha, kwa vile Ahlul-Bayt wanabeba uzito mkubwa mbele ya Allah kama Qur'ani Tukufu, Ahlul-Bayt wana sifa sawa na Qur'ani. Kama ambavyo Qur'ani ni haki kuanzia mwanzo mpaka mwisho bila kivuli chochote cha uwongo ndani yake, na kama ambavyo ni wajibu kwa kila Mwislamu kutii amri zake (Qur'ani), hivyo lazima Ahlul-Bayt wawe walinzi wa kweli kwa ukamilifu na uaminifu ambao amri zao lazima zifuatwe na wote. Kwa hiyo, hakuwezi kuwa na ukwepaji wa kuukubali uongozi wao na kufuata itikadi yao na imani yao. Waislamu wanafungwa na semi hizi za Mtume (s.a.w.w.) kuwafuata wao na sio mwingine yeyote. Kama ambavyo haiwezekani kwa Mwislamu yeyote kuipa mgongo Qur'ani au kufuata mfumo wowote wa sheria ambazo ni tofauti nayo, hivyo, wakati Ahlul-Bayt wameelezewa bila ubishi kama walio sawa katika uzito na umuhimu kama Qur'ani, mwelekeo huohuo lazima ufuatwe kufuatana na utukufu wao, na haiwezi kuruhusiwa kuwapa mgongo ili kuwafuata watu wengine wowote.

Katika usemi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w): "Ninakuachieni miongoni mwenu vizito viwili; kama mtashikamana navyo vyote kamwe hamtapotea; navyo ni Kitabu cha Allah na kizazi changu," haja ya kushikamana navyo vyote lazima ichungwe kwa umahususi. Kwa uwazi huonesha kwamba yeyote yule anayeshikamana navyo au kuvifuata vyote kama walinzi wake, ataokolewa kutokana na kupotea. Kwa hiyo, kama mtu atachukua kimojawapo bila ya kuchukua kingine kama mlinzi atapotea. Nukta hii bado ni wazi yatiwa nguvu na kauli ya Mtume ya hadithi ya vizito viwili iliyopo kwa Tabrani: "Chunga! Na wala usiende mbele yao wala nyuma yao, kwani kwa kila hali utaangamizwa; na usijaribu kuwafundisha kwani wanajua zaidi kuliko wewe."

Ibn Hajar anayachukulia maneno haya kwamba mwenye kupata sifa za juu miongoni mwao na wajibu za kidini, ndiye mwenye kutangulizwa kabla ya mwingine.[28]

---

[26] *Sawa'iq al-Muhriqah* ya Allah Ibn Hajar, mistari michache ya mwisho ya sura 9 kichwa cha habari kidogo Na. 2.

[27] *Sawa 'iq al-Muhriqah* ya Allah Ibn Hajar, sura ya 11 kichwa cha habari kidogo Na. 1 uk. 89.

[28] *Sawa'iq al-Muhriqah*, sura juu wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ukurasa wa 136. kwa sababu ya kukiri haki Ibn Hajar anapaswa kujibu angalau maswali yafuatayo: "kwanini imani ya Ashari imependelewa zaidi ya ile ya Ahlul-Bayt? Kwa nini waliotangulia (Ahlul-Bayt) wameachwa na waliofuata wamekubaliwa kama chimbuko la imani katika mambo ya sheria na ibada? Kwa nini Abu Hanifah, Al-Malik, Al-Shafi'i na al-Hambal wanaonekana bora zaidi ya Ahlul-Bayt? Kuhusu swala la hadithi kwanini khariji kama Imran ibn Hattan amependelewa zaidi? Kwa nini katika swala la kutafisiri Qur'ani Tukufu. Tafisiri ya Al-Muqatil ibn Sulayman (ambaye alikuwa wa madhehebu ya murji'i ambao wanaamini kwamba Mwenyezi Mungu ana mwili) inapewa uzito zaidi kuliko tafsiri ya Ahlul-Bayt. Halikadhalika, katika matawi mengine ya elimu, kwa nini watu wengine wanapendelewa zaidi kuliko Ahlul-Bayt? Na kwa nini katika jambo la ukhalifa yaani urithi kwa Mtukufu Mtume, binamu yake na mfuasi wake muaminifu ambaye kuhusu yeye Mtukufu Mtume alisema: "Ni Ali tu ndiye anayeweza kutimiza ahadi zangu," aliwekwa kando na uzawa wa Al-Marwan wanakubaliwa kuwa Makhalifa badala ya kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.); na anaendelea zaidi, anasema, "Hapa kuna shaka inajitokeza, kwamba wakati hadithi imekuja kupitia vyanzo kadha wa kadha, wengine wanasema kwamba maneno haya yalisemwa kule Madina alipokuwa kwenye kitanda chake alichofia na chumba kilikuwa kimejaa masahaba wake, ambapo wengine wanasema kwamba alisema maneno haya kule Ghadir Khum au wakati wa kurudi kutoka Ta'if. Lakini hakuna kutokupatana kwa sababu inawezekana kwamba, kwa kutilia maanani umuhimu na ukubwa wa Qur'ani na Ahlul-Bayt na fikira ya kusisitiza jambo hili kwa watu, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alirudia maneno haya katika nyakati zote hizo kwa sababu kama kuna yeyote ambaye alikuwa hajasikia basi ayasikie sasa." Aidha, kwa kuwa uzito wa Ahlul-Bayt

Hadithi nyingine ambayo inamlazimisha kila Mwislamu kuwafuata Ahlul-Bayt (a.s.) na kutomkubali yeyote yule kama mlinzi katika masuala ya dini, ni ile ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Chungeni! Ahlul-Bayt wangu ni kama Safina ya Nuh; yeyote yule aliyeipanda aliokolewa, na yeyote aliyeipa mgongo aliangamizwa."[29] Bado hadithi nyingine inatuambia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Ahlul-Bayt wangu ni kama Lango la Toba[30] la Wana wa Israil; yeyote ambaye aliingia humo aliokolewa."[31]

kwenye macho ya Mwenyezi Mungu ni sawa na uzito wa Qur'ani cha kwanza kina sifa sawa kama kile cha pili kama vile ambavyo Qur'ani Tukufu ni kweli tupu toka mwanzo mpaka mwisho bila ya hata doa la uongo ndani yake, na kama ilivyo wajibu kwa kila Mwislamu kutii amri zake, hivyo vile vile lazima Ahlul-Bayt wawe wakweli kikamilifu, na viongozi waaminifu amri zao lazima zifuatwe na wote. Kwa hiyo, hakuna namna ya kukwepa uongozi wao bali kufuata kanuni na imani yao tu. Waislamu wanashurutishwa na hadithi hizi za Mtume kuwafuata wao tu na sio mwingine yeyote. Kama ambavyo haiwezekani kwa Mwislamu kuipa kisogo Qur'ani Tukufu au kufuata mfano wowote wa kanuni ambazo hazipatani nayo, hivyo wakati ambapo Ahlul-Bayt wameelezewa kwa wazi mno kwamba ni sawa katika uzito na muhimu kama ilivyo Qur'ani, hivyo hali hiyo hiyo yapaswa msimamo huo huo kufuatwa kuhusiana na mafundisho yao, na haitaruhusiwa kuwakataa wao na kuwafuata wengineo.Kwenye hadithi ya Mtume isemayo: "Miongoni mwenu nawaachieni vizoto viwili kama, kama mkishikamana na vyote hivyo, hamtapotea, na vitu hivi ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur'ani Tukufu) na kizazi changu (Ahlul-Bayt), hususan mambo ya kushikamana na vyote viwili yapaswa kuangaliwa, inaonyesha wazi kwamba yeyote atakayeacha kushikamana au kufuata vyote viwili kama viongozi wake, anaweza akapotea. Nukta hii bano linakuwa wazi zaidi kwa kuweka maanani simulizi ya Tabrani ambayo ina nguvu zaidi: "Angalieni: Na msije mkaenda mbele yao au mkabaki nyuma yao kwani katika hali zote (mkiwa mbele au nyuma) mtateketea; na msijaribu kuwafundisha kwani wao wanajua zaidi yenu" Ibn Hajaar anashikilia kwamba maneno haya yanaonyesha kwamba wale Ahlul-Bayt ambao walikuwa na sifa hizi walikuwa bora zaidi ya watu wote. Hadithi nyingine ambayo inalazimisha kila Mwislam kuwafuata Ahlul-Bayt na kutomkubali yeyote kama kiongozi katika mambo ya dini ni kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Agalieni Ahalul-Bayt wangu wapo kama Safina ya Nuhu, yeyote aliyeingia humo aliokoka na yeyote aliyekataa kuingia humo aliangamia." Pia haadithi nyingine inatuambia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema "Ahlul-Bayt wangu ni kama Lango la toba, la wana wa Israeli; yeyote aliyeingia humo alisamehewa." Hadithi nyingine tena inasema: "Nyota huwalinda waishio juu ya ardhi wasife maji, na Ahlul-Bayt wangu ni walinzi wa wafuasi wangu dhidi ya mifarakano ya mambo ya kidini. Hivyo basi, kundi lolote miongoni mwa waarabu ambalo litawapinga Ahlul-Bayt wangu katika maswala yahusuyo sheria za Mwenyezi Mungu litagawanywa na fitina na kuwa kundi la shetani." Kwa hiyo hadithi hizi hazikuacha nafasi ya shaka yoyote. Hapawezi kuwepo na namna nyingine isipokuwa kuwafuata Ahlul-Bayt (a.s.) na kuacha upinzani dhidi yao. Upatanisho wa wazi kabisa ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ametuelekeza kuhusu mambo haya katika hadithi zilizotajwa hapo juu hauwezi kuzidiwa au kulinganishwa na mwingine katika lugha nyingine yeyote. Hapa Ahlul-Bayt (a.s.) wamefanyiwa rejea wote kwa ujumla. Tamko linawahusu Ahlul-Bayt wote. Aidha hii inawahusu wale tu ambao ni Mitume wa Mwenyezi Mungu na wanao wadhifa wa Imamu kwa Amri ya Mwenyezi Mungu kama ilivyothibitishwa na hoja na kushikiliwa na hadithi. Wanachuoni kutoka katika madhehebu makubwa ya Waislamu wamekiri hivyo pia. Kwa mfano: Ibn Hajar ameandika katika *Sawa'iq Muhriqah* yake; "Watu wengine wanafikiri kwamba labda 'Ahlul-Bayt ambao Mtukufu Mtume amewataja kama walinzi ni hao wanachuo wasomi miongoni mwa Ahalul-Bayt, kwani mwongozo unapatikana kupitia kwao tu. Wao ni kama nyota ambao kupitia kwao tunaongozwa kuelekea kwenye haki, na kama nyota zinaondolewa au zikifichwa tungekutana uso kwa uso na alama za Mwenye Nguvu zote kama ilivyoahidiwa - yaani Siku ya Ufufuo. Haya yatatokea wakati ambapo Mahd atakuja, kama ilivyoelezwa kwenye hadithi, na Mtume Isa ataswali swala zake nyuma yake, Dajjal atauawa na halafu alama za Mwenye Nguvu zote zitaonekana moja baada ya nyingine" Mahali pengine Ibn Hajar ameandika: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa kwamba hali ya watu itakuwaje baada ya Ahlul-Bayt na alijibu: Hali yao itakuwa kama punda ambaye uti wa mgogo wake umevunjika." Unaelewa vema kwamba hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambayo inasema kwamba Ahlul-Bayt ni kama mfano wa safina ya Nuhu inaelekeza kwenye kutanabahi kwamba wale wanaokubali imani yao na kuwafuata wao, wataokolewa kutoka kwenye adhabu ya jahannamu, ambapo wale ambao watawakimbia watakutana na hatima ya mmoja wa aliyejaribu kuokoa maisha yake kwa kupanda mlima, pakiwepo na tofauti moja tu kwamba wakati ambapo mwanae Nuhu aliyepotoka alifariki maji, watu hawa watazama na kuteketea kwenye moto wa jahannam. Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipotumia mfano wa Lango la Toba humanisha kwamba kama vile lile Lango lilivyo, Ahlul-Bayt ni udhihirisho wa Utukufu na mamlaka ya Mola Aliye juu zaidi ambaye tujisalimishe kwake na kumpa utii wa kiwango cha juu, Ibn Hajar anayashugulikia masuala haya pia. Baada ya kutaja hadithi hizi, ameongezea kwa njia ya ufafanuzi kwamba ule mfano wa Safina ya Nuh (a.s.) unamanisha kwamba wale ambao watawapenda na kuwaheshimu Ahlul-Bayt (a.s.) na kupata faida ya mwongozo wao wataokolewa kutoka kwenye giza la upinzani, na wale ambao watawakataa watazama kwenye bahari ya utovu wa shukrani na watateketea kwenye jangwa la maasi na uhalifu. Na kuhusu hadithi ya Lango la Toba, ameandika kwamba Mwenyezi Mungu swt. ameamuru kwamba kwa kuingia Lango la Toba katika hali ya unyonge, unyenyekevu na toba, Wana wa Israel wangepata msamaha. Kwa njia ileile ameelezea upendo na huba kwa Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa Waislamu kupata msamaha wa dhambi zao.Kwa hiyo ni wazi kwamba kuna hadithi nyingi za uhakika (hata miongoni mwa madhehebu makubwa ya Waislamu) zinazoonyesha kwamba ni lazima kuwatii na kuwafuata Watukufu Ahlul-Bayt (a.s.). Walikuwa na sifa ambazo ziliweza kuthibitisha upendeleo huo. Kwa sababu hiyo, wanaowafuata maadui na wapinzani wa Ahlul-Bayt wanaweza kuulizwa jinsi gani wamefanya kuhusu hadithi ya al-Thaqalayn na hadithi nyingine nyingi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambamo humo wamepewa amri ya kuwatii Ahlul-Bayt (a.s.) na wanawezaje kudai kwamba wao wameshikamana na Ahlul-Bayt au kuchukua hadithi ndani ya safina ya wakovu au kuingia kwanye lango la Toba?"

[29] *Mustadrak* (kitabu) cha Imamu Hakimu Jz. 3, uk.151 hadith iliyowasilishwa kupitia vyanzo sahihi kutoka kwa Abu Dharr (R.A.).

[30] Kisa cha "Lango la Toba" kimeandikwa kwenye Qur'ani Tukufu 2:57-58

[31] Hadithi hii imeandikwa na Al-Tabarani kwenye *Awsat* yake (hadithi Na. 18) kama ilivyosimuliwa na Abu Sa'id na pia imeandikwa na Al-Nabahani kwenye *Arba'in* yake uk. 216.

**Hadithi nyingine ni hii ifuatayo:**

"Nyota huwalinda wakazi wa duniani kutokana na kuangamia, na Ahlul-Bayt wangu ni walinzi wa wafuasi wangu dhidi ya faraka (katika masuala ya dini). Kwa hiyo, kundi lolote miongoni mwa Waarabu litakalowapinga Ahlul-Bayt wangu (kuhusiana na masuala ya Amri ya Mungu) watagawanyika katika faraka na kuwa makundi ya shetani." [32] Kwa hiyo, hadithi hizi haziachi mwanya wa shaka. Hakuwezi kuwepo na njia nyingine isipokuwa kuwafuata Ahlul-Bayt na kuachana na upinzani wote kwao. Maneno ya wazi na yasiyopingika ambayo kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ametuelekeza kuhusu masuala haya katika hadithi zilizotajwa hapo juu hayawezi kupitwa au kulinganishwa na lugha yoyote nyingine.

Hapa Ahlul-Bayt (a.s.) wametajwa kwa ujumla. Maelezo hujumuisha Ahlul-Bayt wote. Sifa hii hutumika tu kwa wale ambao ni Hoja wa Allah na wenye kushika nafasi makhususi kwa Amri ya Mungu, kama ilivyothibitishwa na akili na kuelezewa na hadithi. Wanachuoni mahiri kutoka sehemu kubwa ya Waislamu vilevile wanalikubali hili. kwa mfano, Ibn Hajar anaandika katika kitabu chake *Sawa'iq al-Muhriqah*: "Baadhi ya watu wanafikiri kwamba pengine Ahlul-Bayt ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amewateuwa kama walinzi ni wale watu wenye ilimu miongoni mwa Ahlul-Bayt, kwa vile mwongozo waweza tu kupatikana kupitia kwao. Wao ni kama nyota ambao kupitia kwao tunaongozwa kwenye upande ulio sawa, Na kama nyota zinaondolewa (au zinafichwa) tungekuja uso kwa uso na dalili za Allah Aza wa Jallah kama ilivyoahidiwa (yaani, Siku ya Ufufuo). Hii itatokea wakati Mahdi atakapokuja, kama ilivyotajwa katika hadithi, na Nabii Isa (a.s.) ataswali nyuma yake, Dajjal atauawa, na kisha dalili za Allah zitatokea moja baada ya nyingine." [33]

Katika sehemu nyingine Ibn Hajar anaandika: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliulizwa watu watakuwa na hali gani baada ya Ahlul-Bayt, na alijibu: 'Hali yao itakuwa kama ile ya farasi ambaye uti wake wa mgongo umevunjika.'" [34]

Unafahamu vizuri sana kwamba hadithi ya Mtume ambayo inasema kwamba Ahlul-Bayt wangu ni kama Safina ya Nuh huelekeza kwenye hitimisho kwamba wale ambao wamefuata itikadi yao na wakawafuata wataokolewa kutokana na adhabu ya Jahannam, ambapo wale ambao wamewapa mgongo na kuwakimbia watakutana na mateso ya yule ambaye alijaribu kuokoa maisha yake kwa kupanda juu ya mlima, pamoja na tofauti moja tu kwamba wakati ambapo yeye (mtoto asi wa Nuh) alifariki maji, watu hawa watatumbukizwa kwenye moto wa Jahannam. Na Mtume kutumia kwake mfano wa Lango la Toba kwamba kama ilivyo Lango hilo, Ahlul-Bayt ni vidhihirisho vya Mwenye nguvu na Utawala wa Mola Aliye Juu ambaye kwamba Kwake lazima tujisalimishe na kutoa unyenyekevu wetu na utii. Ibn Hajar ameshughulika na masuala haya pia. Baada ya kutaja hadithi hizi anaongeza kwa njia ya ufafanuzi kwamba mfano wa Safina wa Nuh humaanisha kwamba wale ambao watawapenda na kuwaheshimu Ahlul-Bayt na kupata faida kutokana na mwongozo wao wataokolewa kutoka kwenye giza la upinzani, na wale ambao watageuka dhidi yao watazamishwa kwenye bahari ya utovu wa shukurani na watapotea katika jangwa la ukaidi na uasi. [35]

Na amma kuhusu hadithi ya Lango la Toba, anaandika kwamba Allah swt. ameamrisha kwamba kwa kuingia kwenye Lango la Toba katika unyenyekevu, udhalili na kujuta, Wana wa Israil watapata msamaha. Kwa njia hiyohiyo Allah swt. ameelezea upendo na mapenzi kwa Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa Waislamu kwa ajili ya kufuta dhambi zao. [36]

---

[32] Mustadrak kitabu cha Imamu Hakim Juzuu ya 3 uk. 149, kama ilivyosimuliwa na Ibn Abbas, pamoja na maneno kwamba hii ni hadithi sahihi, lakini haikuandlikwa na masheikh wawili (yaani, Bukhari na Muslim).

[33] Kama ilivyosimuliwa na Ibn Abbas, na taarifa ya maandishi kwamba hii ni Hadithi sahihi lakini haikuandikwa na masheikh wawili, Muslim na Bukhari.

[34] *Sawa'iq al-Muhriqah* uk. 143. Sasa, tunamuuliza Allamah Ibn Hajar kwamba wakati ambapo Ahlul-Bayt (a.s.) wanashika nafasi ya juu kiasi hicho hali itakuwaje kwa wale ambao wanawadharau?

[35] *Sawa'iq al-Muhriqah* sura ya 11 uk 91 inayoshugulika na tafsir ya aya ya saba ambayo rejea yake imetajwa humo.

[36] Baada ya kuona rai hii ya Ibn Hajar, ni juu yako kuamua kwamba ni kwa kiwango gani anaweza kuthibtisha katika kukataa uongozi wa

Kwa hiyo, ni wazi kwamba kuna kundi la hadithi sahihi (hata miongoni mwa kundi kubwa la Waislamu) zinazoonesha kwamba ni lazima kuwaheshimu na kuwafuata Ahlul-Bayt (a.s.). Hadithi ambazo zimekuja kwetu kutoka midomoni mwa Ahlul-Bayt ni nyingi sana lakini kwa sababu sipendi kuwasumbua, sikuziweka hapa hadithi hizo. Hadithi chache ambazo nimezisimulia zinatosha.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

Maimamu katika mambo ya msingi ya masharti ya imani, ibada, desturi na sheria na kwa nini hapati faida kutoka kwenye mafundisho ya Ahlul-Bayt (yaani Maimamu) kuhusiana na tafsir ya Qur'ani, Sunnah, unyofu na sosholojia. Kwa hiyo, basi aliwakataa na akajizamisha katika bahari ya maasi na utovu wa adabu, na kwanini amechagua kuteketea kwenye jangwa la wasioshukuru? Hata hivyo, Allah swt. amsamehe kwa shutuma za uongo ambazo amezifanya dhidi yetu sisi Mashia, na matusi ambayo ametulundikia kweye kitabu chake.

# BARUA YA TISA

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**Maombi Ya Maandiko Zaidi Yanayohusika.**

Usiizuie kalamu yako, na huna haja ya kuogopa kunisumbua. Ninakusikiliza kwa masikio yote; kifua changu ni kipana, na kujifunza kutoka kwako, moyo wangu umetulia, na nafsi katika amani na utulivu. Uthibitisho wote na hoja ambazo umezielezea zimenifanya kuwa na shauku zaidi, na hivyo kuondoa vikwazo vya uchovu. Kwa hiyo nitumie zaidi khutba zako zenye kuvutia na vidhihirisho vya vipawa vya busara. Nimeona katika khutba zako uchunguzi wa mwenye busara, na hivyo hulowesha zaidi moyo wangu kuliko maji safi na ya baridi; hivyo naomba zaidi, Allah ambariki baba yako, na amani iwe juu yako. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA KUMI

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**Kutupia Macho Maandiko ya Kutosha.**

Kama umependezewa na kupokea barua yangu, na kama umepitia kwa kujitosheleza, basi wakati wote nimeweka matumaini yangu juu yako kwa ajili ya kuhitimisha juhudi yangu kwa mafanikio. Yeyote yule akusudiaye vizuri, afuataye mwendo mzuri wakati akiwa mnyenyekevu, mpole, mwenye heshima, aliyejazwa ilimu, mwenye tabia nzuri na subira, huyo hakika anafaa kuwa mwaminifu katika kile anachosema na kuandika, ambapo uadilifu na uaminifu viko katika mkono wake na kwenye ulimi wake.

Ni wewe ambaye kwako nawiwa shukurani zangu wakati uliponiomba zaidi na zaidi, kwani ni nani mwingine awezaye kuwa na uzuri zaidi, mpole na mnyenyekevu? Ili nikupatie maombi yako na kupoza macho yako, ningependa kueleza yafuatayo:

Tabarani katika *Mu'jam al-Kabir* yake na Rafai katika *Musnad* yake wametoa na kuishajiisha hadithi kutoka kwa Ibn Abbas ambaye anasema: Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Yeyote yule anayetaka kuishi na kufa kama mimi, na kukaa katika Bustani ya Eden aliyoiandaa Mola Wangu, naamkubali Ali kama bwana wake baada yangu mimi, na amtii yeyote atakayemuweka juu yake, awafuate Ahlul-Bayt baada yangu, kwani wao ni kizazi changu na wameumbwa kutokana na dongo nililoumbiwa mimi na kujaliwa maarifa na utambuzi wangu mimi mwenyewe. Ole wao wale wafuasi wangu watakaowakana Ahlul-Bayt na wakautenga uhusiano na undugu wao na mimi. Kamwe Mwenyezi Mungu asiwajaalie kufaidika na maombezi yangu."[37]

Mutir, Al-Burudi, Ibn Jarir, Ibn Shahin na Ibn Mundah wameiandika hadithi ambayo ilipatikana kutoka kwa Ziyad ibn Matraf kupitia kwa Ishaq isemayo: "Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema: 'Yeyote yule anayetaka kuishi na kufa kama mimi na kuingia pepo ya milele, basi amkubali Ali na watoto wake baada yake kama mabwana zake, kwa sababu ni watu ambao hawatawatoa kwenye uongofo na wala hawatawaacheni kuingia kwenye upotofu.'" [38]

Halikadhalika imesimuliwa na Zayd Ibn al-Arqam kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Yeyote yule anayetaka kuishi kama nilivyoishi mimi na kufa kifo kama changu na kuingia kwenye Bustani yenye kipeo cha furaha ya milele ambayo Mwenyezi Mungu ameniahidi, na amfanye Ali kuwa kiongozi wake kwa sababu kamwe hatakuongozeni nje ya njia ya muongozo wa kweli wala hatawapelekeni kwenye makosa " [39]

[37] Hadith hii inaonekana kwa maneno yale yale katika *Kanz Al-Ummal*, Jz. 6 uk. 217 Hadithi Na. 3819 na pia imeandikwa katika toleo la mukhtasari wa *Kanz al-Ummal*, angalia kwenye pambizo la *Musnad Ahmad Ibn Hanbal*, Jz. 5 uk. 94. Tofauti moja tu iliypo ni kwamba katika toleo la mukhtasari neno "elimu" limeachwa, lakini inawezekana hili ni kosa la mchapishaji. Hafiz Abu Nu'aim ameandika Hadithi hii katika *Hiliyah* yake na Ibn Abi'l-Hadid Mutazilah amechukua kutoka kwake na kuiweka katika sharhe yake ya *Nahj al-Balagha* (angalia toleo la Cairo, Jz. 2, uk. 450). Ahmad Ibn Hanbal pia ameandika Hadithi kama hiyo katika *Musnad* yake na katika kitabu chake *Manaqib Ali ibn Abi Talib*.

[38] *Kanz al-Ummal*, Jz. 6, uk. 155 Hadithi Na. 2578; vile vile muhutasari wa *Kanz al-Ummal* kwenye pambizo la *Musnad* ya Ahmad ibn Hanbal Jz. 5, uk 32. Allamah Ibn Hajar al-Asqalani ameandika hadithi hii kwa kifupi kwenye kitabu chake *Isabah* kuhusiana na maisha ya Ziyad ibn Matraf, pamoja na maelezo kwamba "Hadithi hii imepatikana kutoka kwa Yahya ibn Yali al-Muharibi na kwa hiyo ni hadithi dhaifu." Lakini kwa maoni yangu, maelezo ya Ibn Hajar ni ya kushangaza sana kwa sababu Yahya ibn Yali amekubalika na wote kwamba yeye ni msimulizi wa kuaminika wa hadithi. Imam Muslim amechukua hadithi kutoka kwake (Yahya ibn Yali al-Muharibi) kwenye sura inayozungumzia "Adhabu" katika *Sahih* yake. Allamah Dhahabi amesema katika *Al-Mizan* yake kwamba kuaminika kwake ni kama ilivyothibitishwa na Allamah Qaysarani na wengineo wanamuona yeye (Yahya ibn Yali al-Muharibi) kuwa ni miongoni mwa wasimulizi ambao Muslim na Bukhari wanawaona kama wakweli na thabiti.

[39] *Mustadrak* kitabu cha Imam Hakim, Jz. 3, uk. 128 mnayo hadithi hii pamoja na maelezo kwamba ni hadithi sahihi lakini masheikh wawili

Ammar Ibn Yasir (R.A.) alisimulia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Ninamuonya kila aliyeniamini mimi na ambaye ameyakinisha kuwa mimi ni mkweli aikubali serikali ya Ali ibn Abi Talib, kwani yeyote amkubaliaye Ali kama mtawala wake amenikubali mimi hivyo, na yeyote ampendaye Ali amenipenda mimi na anayenipenda mimi amempenda Allah. Yeyote anayemchukia ananichukia mimi na mwenye kunichukia anamchukia Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu zote." [40] Ammar anasimulia tena kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Ewe Mola Wangu! Yeyote yule anayeniamini mimi na ameyakinisha ukweli wangu naamchukulie Ali kama bwana wake, kwani serikali yake ndio yangu mimi, na serikali yangu mimi ni ile ya Mwenyezi Mungu, Aliye juu zaidi."[41]

Katika hadithi nyingine Ammar anasimulia kuwa: Wakati mmoja Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliwahutubia watu akasema: "Enyi watu! Kwa kweli fadhila, heshima na hadhi ni kwa ajili ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kizazi chake; hivyo, msiache udanganyifu wowote uwapotoshe."[42] Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Katika kila kizazi cha umma wangu watakuwepo watu wenye haki na uadilifu katika Ahlul-Bayt wangu ambao ni sawa na mimi tu na watakaozuia upotofu wa wahalifu katika dini yangu, na tafsiri za wajinga. Tambueni kwamba Maimamu wenu watakuwa wawakilishi wenu mbele ya Mwenyezi Mungu. Hivyo muwe waangalifu ni kina nani mnawafanya kuwa wawakilishi wenu Kwake."[43] Mtukufu Mtume pia alisema: "Msitangulie mbele yao mkaja mkaangamia, wala msiwe mbali nyuma yao msije pia mkaangamia na msiwafundishe kwani wao wanajua zaidi yenu"[44] Pia alisema (s.a.w.w): "Wachukulieni Ahlul-Bayt wangu miongoni mwenu kama vile mnavyokichukulia kichwa cha mwili, na macho yaliyo katika kichwa, kwani kichwa kinaongozwa na macho."[45]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) pia alisema: "Shikeni mapenzi ya Ahlul-Bayt kwa umuhimu kabisa, kwani yeyote anayekutana na Muumba wake akiwa anatupenda sisi ataingia peponi kwa uombezi wetu. Naapa kwa Yule ambaye uhai wangu uko mikononi Mwake, hakuna matendo mema ya mtu yatakayofanya anufaike mpaka azitambue haki zetu."[46]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliendelea kusema zaidi: "Elimu ya Aali Muhammad (kizazi cha Muhammad) inaleta wokovu kutokana na Moto wa Jahannam na kuwapenda wao ni kibali cha kutembea kwenye

(Muslim Bukhari) hawakuiandika. Pia iliandikwa katika kitabu cha Tabarani, Abu Na'im katika *Fadha'il al-Sahabah* cha Tabarani, Abu Nu'aim katika Faza'il al-Sahabah na katika *Kanz al-Ummal* kwenye pambizo ya *Musnad* Jz. 5, uk. 32.

[40] Imeandikwa na Tabarani katika kitabu cha *Al-Kabir,* na Ibn Asakir kwenye kitabu chake cha historia, na pia inaonekana kwenye *Kanz al-Ummal,* Jz. 6, kama hadithi Na. 2571 mwishoni mwa uk. wa 154.

[41] Al-Tabarani, kwenye kitabu *Al-Kabir* amesimulia hadithi hii kutoka kwa Muhammad, mtoto wa Abu Ubaydah, mtoto wa Muhammad, mtoto wa Ammar ibn Yasir kwamba ilikuwa inasimuliwa kutoka baba kwenda kwa mjukuu kwenda kwa kilembwe na ni Hadithi Na.2576 katika Jz. 6, uk. 155 wa *Kanz al-Ummal* na pia imewekwa kwenye toleo la mukhutasari wa kitabu hicho.

[42] Abu al-Shaykh ameiweka (hadithi hii) katika hadithi ndefu na Ibn Hajar amechukua kutoka kwake na kuiandika kwenye *Sawiq al-Muhriqah*, uk. 105 kichwa cha habari Na. 4 kwenye mazungumzo yake ya Aya ya 23 sura ya 42 ya Qur'ani Tukufu.

[43] Imeandikwa na Al-Mulla, kwenye kitabu chake *Sirat* na pia Ibn Hajr katika *Sawaiq al-Muhriqah* uk. 90, kuhusiana na tafsiri ya aya, "Na wasimamisheni. **Hakika hao wataulizwa** (Qur'ani Tukufu 37:24).

[44] Imeandikwa na al-Tabarani kama sehemu ya hadithi ya Thaqalayn (vizito viwili) na imetajwa na Ibn Hajar katika kitabu chake kuhusiana na tafsiri ya aya ya 24, sura ya 37, kwenye *Sawaiq al-Muhriqah*, sura 11, uk. 89.

[45] Hadithi imetujia kutoka kwa masahaba kadhaa ambao wamesimulia sunnah, kuna iliyopokelewa kutoka kwa Abu Dharr na imeandikwa na Imam al-Saban katika kitabu chake cha *Is'af al-Raghibn* na Shaykh Yusuf al-Nabahani kwenye uk. 31 wa *Al-Sharaf al-Muabbad* kutoka kwa zaidi ya mtu mmoja. Ni uthibitisho wa ukuu wa Ahlul-Bayt (a.s.) na wa imani kwamba mwongozo wa kweli unapatikana kutoka kwao tu.

[46] Imeandikwa na Al-Tabarani kwenye kitabu chake *Awsat*, imeandikwa na Allamah Suyuti kwenye kitabu chake Ihya al- Mayyit, imeandikwa na Allamah al-Nabahani kwenye Arbain al-Arbain, na Allamah Ibn Hajar kwenye *Sawaiq al-Muhriqah*. Hebu tafakari usemi huu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa makini kwamba hakuna matendo mema ya mtu yatakayomnufaisha yeye mpaka akubali haki zetu. Na niambie ni haki zipi ambazo zimefanywa kuwa ni sharti la mbele kwa ajili ya kukubaliwa kwa matendo yetu mema. Je, haina maana kwamba yatupasa kuwatii na kuwafuata Ahlul-Bayt (a.s.) kutekeleza maelekezo yao na kuomba mkuruba kwa Allah kwa mwongozo wao? Ni maana gani nyingine yaweza kuwa kwa neno 'haki' isipokuwa *Nubuwwah* (utume) na ukhalifa (ukaimu) wakati ambapo kuwakubali wao yote haya ni muhimu mno na kuyashika yote? Lakini ole wetu, lazima tushughulike na watu ambao hawafikirii na kuagalia mambo haya. **Hakika kabisa tumetoka kwa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.**

njia iliyonyooka na kuwatii kwao ni kinga kutokana na Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu."[47] Na Mtume Mtukufu (s.a.w.w) anasema: "Siku ya Hukumu hakuna hata mmoja ambaye ataweza kuondoka mahali pa hesabu ya matendo yake mpaka awe ameulizwa juu ya mambo manne: jinsi alivyoyatumia maisha yake na mali yake na wapi amepata mali yake hiyo na pia ataulizwa kuhusu kutupenda sisi Ahlul-Bayt."[48]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w) anazidi kusema: "Kama yeyote atasimama na kuswali katikati ya Rukn na Maqaam lakini akawa anakichukia kizazi cha Muhammad (amani na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote) bado atakwenda Jahanamm tu."[49] Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) anasema: "Yeyote atakayekufa kwa ajili ya mapenzi yake kwa Aali Muhammad atakuwa shahidi. Yeyote atakayekufa kwa ajili ya kuwapenda Aali Muhammad atakufa kama muumini mwenye imani kamili. Na yeyote atakayekufa kwa ajili ya kuwapenda Aali Muhammad atabashiriwa na malaika wa mauti kisha na Mankir na Nakiir juu ya habari njema za kuingia Peponi. Na yeyote atakayekufa kwa ajili ya kuwapenda Aali Muhammad atapelekwa Peponi kwa fahari kubwa ambayo kwamba bibi harusi hupelekwa nyumbani kwa mumewe. Yeyote atakayekufa kwa ajili ya kuwapenda Aali Muhammad, milango miwili inayoelekea Peponi itafunguliwa kwa ajili yake humo kaburini mwake. Mwenyezi Mungu atalifanya kaburi lake kuwa mahali pa kuzuru malaika wa Rehema. Na yeyote atakayekufa kwa ajili ya kuwapenda Aali Muhammad atakufa katika sunna (ya Mtume) na makubaliano (*'Ijma'ah*) na angalieni, yeyote atakayekufa akiwa adui wa Aali Muhammad, itaandikwa katikati ya macho yake katika Siku ya Hukumu, kwamba 'Anapaswa kukata tamaa juu ya rehma za Mwenyezi Mungu…," mpaka mwisho wa hotuba yake isiyo na kifani ambayo kwayo alitaka kugeuza mielekeo na misukumo ya matakwa.

Hii imenukuliwa kutoka kwenye khutuba 'Asma' ambayo imesimuliwa na wanachuoni wote wa Ki-Sunni wenye kuaminika.[50]

Mada zote zilizoshugulikiwa katika hadithi hizi zinakubalika kwa wote, hususan kwa wanachuoni wa kuaminika wa Ahlul-Bayt.

---

[47] Kitabu *Al-Shafa* kilichoandikwa na Qadhi Ayadh, Jz. 2, uk. 40 kilichochapishwa Astanbul mwaka wa 1328 Hijiria. Unaweza ukaona vizuri sana kwamba "kukubali" katika fuo hili hakumaanishi kujua majina yao tu au kufahamu uhusiano wao wa kidugu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwa sababu hata Abu Lahab na Abu Jahli walijua na kuelewa mambo haya. "Kukubali" maana yake ni kwamba inapasa wakubaliwe kama wapenzi wa Mungu. Kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alivyosema: "Yeyote anayekufa bila kumkubali Imamu wa zama zake anakufa kifo cha kijahilia." Mapenzi kwa Mwenyezi Mungu maana yake kiwango cha mapenzi ambacho ni Mitume na Maimamu tu wanaoweza kupata na ni muhimu kwamba kila atafutaye kweli yampasa awapende, awaheshimu na kuwatii wao katika nguvu zote kwenye nafsi kwa kiwango kile kile na hii inalifanya jambo hili kuwa wazi kama mwanga wa mchana.

[48] Lau kama ingekuwa Ahlul-Bayt (a.s.) hawakuteuliwa na Muweza Mwenye nguvu kwenye cheo hiki cha juu mno ambacho huhitaji maigizo ya mfano wao na utii wa amri zao, jukumu la kuwapenda wao halingekuwa sharti na lazima kiasi hicho. Hadithi hii imeandikwa na Al-Tabarani kutoka kwa Ibn Abbas na kutoka kwake Allamah Suyuti na Al-Nabahani kwenye vitabu vyao *Ihya al-Mayyit* na *Arbain* (kila mmoja chake kwa mfuatano huo) Maulamaa wengi wengine pia wameiandika hadithi hii.

[49] Imeandikwa na Al-Tabarani, Al-Hakim, Al-Nabahani (kwenye kitabu chake *Arbain*) Suyuti (kwenye kitabu chake *Ihya al-Mayyit*) na wengineo. Hadithi hii inafanana na hadithi zingine ambazo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema kuwa "Yeye ambaye anauwezo juu ya uhai wangu na kifo changu, hakuna matendo mema ya mtu yeyote ambayo yatamnufaisha mpaka awe amekubali haki zetu, lakini kwa ajili ya kweli kwamba uadui au uovu kwa dhuria wa Muhammad (s.a.w.w.) ni sawa na kufanya uadui na Mwenyezi Mungu, na matendo mema ya mtu kamwe hayangekanushwa kwa sababu hizi na lau kama ingekuwa AaIi Muhammad sio warithi wawakilishi wa kweli wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ingewezekanaje haki zao kupewa umuhimu wa kiasi hicho? Allamah al-Nabahani kwenye kitabu chake *Arbain* na Suyuti kwenye kitabu chake *Ihya al-Mayyit* wote wameandika kwamba Imam Hakim na Ibn Hayyan wameandika katika vitabu vyao vya hadithi kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Kwa Yeye ambaye anashirikilia uwezo wa uhai na kifo juu yangu yeyote anayetuonea kijicho sisi Ahlul-Bayt, ataadhibiwa kwa moto wa Jahannam." Halikadhalika, al-Nabahani kwenye kitabu chake na Suyuti kwenye kitabu chake *Ihya al-Mayyit* wote wanasema kwamba Imam Hassan alimwambia Muawiyah ibn Khadij: "kuweni waangalifu na kamwe msije mkatuonea kijicho kwani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Yeyote yule ambaye kwa namna moja au nyingine anatufanya sisi maadui zake au anatuonea kijicho sisi, atapigwa akiwa mbali na Chemchem ya Kawthar kwa mijeledi ya moto katika Siku hiyo ya Hukumu. "Na siku moja Mtukufu Mtume alisema kwenye khotuba yake: "Enyi watu yeyote mwenye uadui kwetu sisi Ahlul-Bayt, atatendewa kama Myahudi katika Siku Hukumu." kama ilivyoandikwa na Al-Tabarani katika kitabu chake *Awsat*. Tafadhali angalia pia *Ihya al Mayyit* na *Arbain.*

[50] Imeandikwa na Imam Thalabi kuhusiana na maelezo ya aya ya 23 ya sura ya 42 ya Qur'ani tukufu katika *Tafsir al-Kabir* yake kutoka kwa Jarir ibn Abdullah al-Bajali ambaye alisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume mwenyewe. Pia imesimuliwa na al-Zamakshari katika *Tafsir* yake kuwa imethibitishwa bila kupingwa.

Sasa basi, suala ni kwamba ama Mtukufu Mtume (s.w.w.w) alisema kwa kurudia rudia mambo haya kuhusu Ahlul-Bayt kila wakati sio kwa sababu tu walikuwa na uhusiano naye wa udugu wa damu. Kama ingelikuwa hivyo, Mtukufu Mtume asingekuwa na ubora wowote ule kuzidi ule wa mtu wa kawaida ambaye aliwapendelea ndugu zake kwa sababu ya uhusiano wa udugu wa damu. Kinyume chake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alitangaza kwa kusisitiza umuhimu wa Ahlul-Bayt kwa sababu ya ukweli kwamba wao ni Hoja za dhahiri za Mwenyezi Mungu, Chemchemu za falsafa ya sheria Zake, wawakilishi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) katika kazi yake ya kuamrisha mema na kukataza mabaya, manaibu wake mwenyewe kwa maneno ya wazi zaidi. Kwa hiyo, yeyote anayewapenda wao anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na yeyote atakayewachukia ni adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w). Yeye Mtukufu Mtume amesema: "Yeyote anayetupenda ni muumini na mchamungu wa kweli na yeyote anayetuchukia huyo ni mnafiki mdhalilifu"[51] Na kwa ajili hiyo, Farazadaq, mtunzi wa mashairi alisema katika kuwasifu:

"Ninyi ni wale ambao mapenzi kwangu ni imani,

na kinyongo kwangu ni uchukivu;

ukaribu kwenu hakika ni usalimishaji na wokovu.

"Tukiwahesabu wachamungu, ninyi mtakuwa viongozi wao; hilo ni kweli.

Kama mtu atauliza: 'Ni nani wabora wa watu?' majibu yatakuwa ni ninyi"

**Amir al-Muminin (a.s) anasema:**

"Mimi na wale watakatifu miongoni mwa kizazi changu ndio wabora mno wa tabia katika utoto na wenye elimu zaidi tunapo kuwa watu wazima. Kupitia kwetu sisi Mwenyezi Mungu huufuta uongo, na kupitia kwetu sisi huvunja uwezo wa meno ya mbwa mwitu. Kupitia sisi huzitibia huzuni zenu, na kupitia kwetu Yeye huwakomboeni ninyi. Kupitia kwetu Mwenyezi Mungu huanza (mambo yote) na kumaliza (mambo yote)."[52]

Kwahiyo, sababu ambayo inatutosha sisi tuwafadhilishe juu ya wengine wote ni kwamba Mwenyezi Mungu Mwenyewe ametoa fadhila kwao juu ya wote, na jambo la kuwaswalia wao kuwa sehemu ya wajibu katika sala zetu ijapokuwa anayeswali awe ni Sidiq, Faruuq au mwenye nuru moja, mbili ama nuru nyingi. Hakika! Kila anayemuabudu Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza wajibat Zake swt., kadhalika anamuabudu huku akiwatakia rehema na amani juu ya Muhammad na kizazi chake, kama vile tu anavyomuabudu Yeye wakati anapotamka *Kalimah at-Tashshahuud (La ilaha illa Allah Muhammad Rasul Allah)*. Huu ni hadhi ambayo mbele yake umma wote umeinamisha vichwa vyao, na ambao mbele yake yoyote utakayemtaja kati ya Maimam wamejisalimisha kwa unyenyekevu. Imam shafi'i (R.A.) amesema:

"Enyi Ahlul-Bayt wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!
Kuwapendeni ninyi ni wajibu,

ambao Allah ameulazimisha katika Qur'ani Tukufu.

Inakutosheni heshima kubwa kwamba,

yeyote anayeswali bila kuwaswalieni swala yake ni batili,

Ni kana kwamba yeye hakuswali kabisa."

[51] Angalia *Sawaiq al-Muhrigah*, sura ya 11
[52] *Aydah al-Ishkal* na *Abd al-Ghani* na *Kanz al-Ummal* Jz.6, ukurasa 396.

Hii mistari ya shairi inajulikana sana miongoni mwa watu wa zungumzao Kiarabu kiasi cha kutohitaji rejea yeyote. Lakini kwa faida ya wale ambao watasisitiza juu ya rejea angalia *Sawaiq al-Muhriqah* ukurasa 88 ya Ibn Hajar kuhusu tafsiri yake ya Aya ya 33 Sura ya 33 ya Qur'ani Tukufu, *Sharaf al-Muabbad* ya Al-Nabhani, *Rishfat al-sadi* ya Imam Abu Bakr *Shabab al-Din* na wegineo.

Hivyo ninamaliza kwa sasa kwa kuweka mbele yako hadithi za Mtukufu Mtume ambazo nimezitaja katika barua hii katika uthibitisho wa imani kwamba ni lazima kufuata nyayo za Ahlul-Bayt na kufuata mfano wao. Qur'ani Tukufu yenyewe inazo aya nyingi ambazo zinaeleweka bila utatanishi na zinathibitisha mambo haya haya kwa jinsi ilivyo, kwa rehema za Mwenyezi Mungu, umejaliwa uwezo mkubwa, akili na uoni wa kina, ninahitaji tu kufahamisha ukweli huu kwako na wewe mwenyewe utaziona aya hizi wakati utakaposoma Qur'ani Tukufu. Shukurani zote zinamsitahiki Allah Mola wa walimwengu wote.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA KUMI NA MOJA

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**I. Kuvutiwa na Maelezo Yetu ya Wazi,**

**II. Wasiwasi wa Kuafikiana nayo Pamoja na Imani za Wengi,**

**III. Maombi ya Dalili ya Wazi Kutoka Kitabu cha Allah.**

(1) Ni heshima kubwa niliyopata kwa kupokea barua yako adhimu, ambayo nimeiona kuwa sahihi katika mkondo wake mkuu wenye kueleweka. Wingi wa ufasaha wako mkubwa wa kujieleza umepita vilele vya milima; nimechunguza barua yako kwa makini sana, na nimekuona wewe kuwa uko mbali katika visheni, imara, nguvu katika hoja na msema kweli.

(2) Nimetafakari juu ya hoja zako nzuri na nikazama kwenye ushahidi wako, najikuta nipo katika hali ya hatari, ya mtanziko. Ninapouangalia ushahidi wako ninaukuta ni wenye kuvutia. Ninapoyafikiria maelezo yake nayaona yenye kuarifu. Ninapowatazama Maimamu watokanao na familia nyoofu na takatifu ya Mtume nakuta kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wamewatukuza nafasi yaona kusisitiza juu ya ukuu wa heshima na hadhi yao. Kwa upande mwingine, ninapowaangalia wengi wa Waislamu, ambao wanawakilisha takriban sehemu kubwa ya umma naona wanatofautiana na Ahlul-Bayt kinyume na wajibu wa uthubutu huo. Hivyo, najikuta nimegawanywa katika sehemu mbili; sehemu moja ikikubaliana na ushahidi huo, ambapo nyingine huniburuza na kunielekeza kwenye kundi la Waislam walio wengi. Nimeisalimisha kwako ile sehemu ya kwanza ili uiongoze, ni tiifu mikononi mwako ambapo sehemu ya pili imekukataa kwa ubishi kabisa.

(3) Kwa hiyo, je, tafadhali waweza kutoa hoja za kuthibitisha zenye nguvu kwenye Qur'ani Tukufu ili kuushinda ubishi wa hii sehemu ya pili na kuweza kuidhibiti na kuigeuza kutokana na kukubaliana na imani za kawaida? Wassalam.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA KUMI NA MBILI

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**Ushahidi wa Qur'ani Tukufu.**

Wewe, shukurani zimuendee Allah, kwa rehema za Mwenyezi Mungu, umeisoma Qur'am Tukufu kwa ukamilifu, tafsiri zake na ukazifahamu maana zake zote za dhahiri na zilizofichika. Kwa hiyo, kuna mtu yoyote aliyetukuzwa humo kama Ahlul-Bayt? Je, Qur'ani Tukufu ina tamko la wazi juu ya kuondoa uchafu kutoka kwa yeyote isipokuwa Ahlul-Bayt? Je, 'Aya ya utakaso' iliteremshwa kwa heshima ya mtu mwingine? Je, wahyi Mtukufu umeamuru mapenzi kwa wengineo wowote? **"Sema siombi ujira kutoka kwenu kwa sababu ya hicho isipokuwa muwapende watu wa nyumba yangu. Na yeyote yule afanyae tendo jema tunaongezea juu yake wema mkubwa zaidi kwake. Elewa Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Msikivu." (42:23).** Jibril alileta aya ya Mubahila kwa utukufu wa mtu mwingine yeyote yule? **"Na yeyote yule atakaye hojiana nawe kuhusu yeye baada ya habari ya ufunuo ambao umepewa, muambie, 'Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, wanawake zetu na wanawake zenu; na sisi na ninyi; halafu tuombe kwa unyeyekevu laana ya Allah iwashukie wale ambao ni waongo." (3:6(1)**

Je, **"Hal Ata"**[53] imeteremshwa kwa kuwasifia wengine? Hapana! Naapa kwa Jina la Mola Ambaye kwa haki kabisa aliitumia kwa ajili yao, Ambaye Yu sahihi na Mwenye haki.

Je! Ahlul-Bayt sio 'kamba ya Mwenyezi Mungu' ambao kuhusu wao amesema: [54] **"Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu wote kwa pamoja na msiachane…" (3:103).** Na "Wakweli" ambao kuhusu wao Yeye swt. amesema: **"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli." (9:119).**[55] Je! Ahlul-Bayt sio 'njia ya Allah' ambayo Mwenyezi Mungu anasema: **"Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu iliyonyooka,[56] basi ifuateni wala msifuate njia nyingine zikawatenga mbali na njia Yake. Hayo amewausia ili muwe na takua. " (6:153).** Ni Ahlul-Bayt tu ndio "wenye mamlaka miongoni mwenu" kama ilivyoandikwa kwenye aya hii: [57] **"Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka miongoni mwenu…"(4:59)**. Ndio "wenye ujuzi wa wahyi" ambao Mwenyezi

---

[53] Maudhui ya Sura ya Al-Dahr (76) katika Q'ur'ani Tukufu.

[54] Imam Thalabi ameandika katika tafsir yake iitwayo *Tafsir Al-Kabir* kutoka kwa Aban ibn Taqlib kwamba alisikia kutoka kwa Imam Jafr al-Sadiq (a.s.) akisema: "Sisi ni 'kamba ya Mwenyezi Mungu' ambayo kwayo Mwenyezi Mungu amesema: "**Shikeni sana kwenye kamba ya Mwenyezi Mungu …."** Ibn Hajr pia ameiweka hii miongoni mwa aya zingine zilizoteremshwa kuhusu sifa za Ahlul-Bayt; angalia *Swaiq al-Muhriqah*, sehemu ya kwanza sura ya 11. Imam Shafi'i ameripotiwa na Imam Abu Bakr ibn Shahab Al- Din kwenye *Rishafaht Al-Sadi* kwamba alisema: "Nilipowaona watu madhehebu yao yamewapeleka kwenye habari ya upotovu na ujinga kwa jina la Mwenyezi Mungu nilipanda meli ya wokovu, yaani Ahlul-Bayt wa Mustafa, Mtume wa mwisho. Na nilishikilia kamba ya Mwenyezi Mungu yaani mapenzi kwao kama alivyotuamrisha sisi tushike sana kamba."

[55] Kwa kusema "**wakweli**" maana yake ni Mtume na kizazi chake. Vitabu sahihi vinakubaliana katika kuelezea kwamba aya hii inawahusu Ahlul-Bayt. Angalia Hafiz Abu Nu'aim; Muwaffaq ibn Ahmad; na Ibn Hajar kwenye *Sawaiq Al-Muhrigah* yake, sura ya 11 ukurasa wa 90, kutoka kwa Imam Zainul-Abidin (a.s) kama nilivyotaja mwishoni mwa barua yangu ya sita (6).

[56] Imam Muhammad Baqir (a.s.) na Imam Ja'far Al-Sadiq (a.s.) wanasema: "**njia iliyonyooka**" inamaanisha 'Imam' na '**na msifuate njia zingine'** inamaanisha 'njia za maimam wengine ambao wanawapotosha ninyi!' Kwa hiyo, msiondoke na kutuacha sisi."

[57] Sheikh Muhammad ibn Yaqub Lulayni (R.A) ameandika katika kitabu sahihi cha *Buraydah Al-Ajali* ambaye anasema "Nilimuuliza Imam Muhammad Al-Baqir (a.s.) kuhusu aya hii na alisoma aya nyingine ambayo ni: 'Hamjawaoana wale ambao wamepewa sehemu ya kitabu, jinsi wanavyoamini masanamu na miungu ya uongo na jinsi wanavyosema kuhusiana na wale wasioamini, 'Hao ndio walioongozwa vizuri ambao Mwenyezi Mungu amewanyima rehema zake, na yeyote ambaye Mwenyezi Mungu amemnyima rehema zake hawezi kumpa msaidizi mwingine yeyote. (Qur'ani, 4:51:52) Wanasema kuhusu 'Maimam' wa upotovu na ambao hawaamini kwamba wao ni viongozi wazuri zaidi kuliko Aali Muhammad: kwa hiyo, Mwenyezi Mungu amewalaani kwenye Kitabu Chake Kitakatifu.

Mungu anasema: **"Waulizeni wale wenye ujuzi kama hamjui." (21:7)** [58] Wao ndio 'waumini wa kweli' ambao Mwenyezi Mungu asema juu yao: **"Na mwenye kumpinga Mtume baada ya kumdhihirikia yeye**[59] **uongofu, na akafuata njia isiyokuwa ya wenye kuamini, tutamwelekeza alikoelekea na tumtie katika Jahannam, na ndio marejeo maovu. " (4:115).** Na wao ndio '**viongozi**' na Mwenyezi Mungu anasema juu yao: **"…Hakika wewe (Mtume) ni mwonyaji tu. Na kila kaumu ina wa kuwaongoza." (13:7).**[60]

Na je sio hao Ahlul-Bayt ambao "Mwenyezi Mungu amewaneemesha" na akawarejea katika Qur'ani Tukufu akisema juu yao: **"Tuongeze kwenye njia iliyonyooka: njia ya wale ambao umewaneemesha …." (1:6-7).** [61] Na katika aya nyingine Anasema: **"….. hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa manabii, na mashahidi, na masiddiki, na watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!"**[62] **(4:69).**

Je! Sio kweli kwamba Mwenyezi Mungu amewapa Ahlul-Bayt uongozi wa watu kwa jumla na baada ya Mtukufu Mtume Amewapa uongozi wao tu miongoni mwa watu? Soma aya ifuatayo: **"Hakika kabisa kiongozi wenu ni Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na wale waaminio: wale wanaosimamisha swala na kutoa zaka huku wakiwa kwenye rukuu."** [63]**(5:55).** Je! Mwenyezi Mungu hakufanya wokovu kwa wale wanaotubia na kufanya matendo mema kutegemea mamlaka yao yaliyoongozwa akisema: **"Hakika mimi ni mwingi wa maghufira kwa anayetubia na akaamini na akatenda mema tena akaongoka." (20:82)?** [64] Je!

[58] Imam Thalabi ameripoti kutoka kwa Jabir ibn Abdullah Ansari (R.A.) kwenye *Tafsir* yake kwamba aya hiyo ilipoteremshwa Amir Al-Muuminn (a.s) alisema: "Sisi ni hao wakumbukao," na hii imerudiwa na Maimamu wote wa Ahlul-Bayt. Allamah Bahrayni ameandika zaidi ya hadithi ishirini kwenye sura ya 35 aya kitabu chake, zinazothibitisha hayohayo.

[59] Ibn Marduwayh ameandika kwenye *Tafsir* yake kuhusu aya hii kwamba 'upinzani kwa Mtume' ina maanisha upinzani kuhusiana na yale ambayo Mtume aliamuru kuhusiana na 'Ali, na usemi huu, '**baada ya muongozo kudhihirishwa kwake**' humaanisha mwongozo kuhusu umakamu wa Ali. 'Ayyashi pia anaelezea hadithi moja katika Tafsir yake kuhusu jambo hilo na kuwa hadithi nyingi sana ambazo zimetufikia sisi kupitia kwa Maimam wa Ahlul-Bayt ambazo zinaonyesha kwamba '**njia ya waumini wa kweli'** inamaanisha njia ya Maimam hao.

[60] Tha'labi katika *Tafsiir* yake ameelezea kutoka hadithi iliyopokelewa na IbnAbbas kwamba wakati aya hii ilipoteremshwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Mimi ni mwonyaji na Ali ni kiongozi. Ewe Ali kupitia kwako wale wanaoogozwa watapata uongozi wa kweli." Hadithi kadhaa zimesimuliwa na wafasiri na wakusanyaji wa hadithi. Imesimuliwa na Muhammad ibn Muslim kwamba alipomuuliza Imam Ja'far al-Sadiq (a.s.) alisema kwamba kila Imam alikuwa kiongozi wa wakati wake. Imam Muhammad Baqir (a.s.) alisema kwamba "**Mwonyaji**' maana yake ni Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na '**kiongozi**' maana yake ni 'Ali (a.s) na kuongezea kitu hiki (yaani, mamlaka ya kuongoza) bado yanaendelea miongoni mwetu"

[61] Imeandikwa kwenye Tafsiri ya Thalabi hadithi kutoka kwa Abu Buraydah kwamba '**njia iliyonyooka**, maana yake ni njia ya Muhammad (s.a.w.w.) na watoto wa Muhammad na tafsir ya Ibn al-Jarrah juu ya aya hii ni kwamba alisikia kutoka kwa Sufyan Al-Thawri, ambaye alisikia kutoka kwa Al-Sadi, ambaye alisikia kutoka Asbat na Mujahid, ambao walisikia kutoka kwa Ibn Abbas ambaye alisema: "Tuongoze kwenye mapenzi ya Muhammad na watoto wake."

[62] Hapana shaka kwamba Maimam ni viongozi wa watu wote wasadikishao mashahidi na waadilifu. Kwa mujibu wa hadithi moja waliobarikiwa miongoni mwa mitume' ni Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w) na miongoni mwa wasadikishao ni Ali (a.s) na miongoni mwa mashahidi ni Imam Hasan na Imam Husein (a.s) na miongini mwa waadilifu ni Maimamu wegineo kwa sababu Ali alikuwa mwanaume wa kwanza kusilimu na kuwa Mwislamu na kusadikisha ujumbe wa Mtume: na hakuna yeyote anayeweza kuitwa Saddiq kwa sababu wengine walikuwa waabudu masanamu mpaka kwenye umri wa miaka thelathini au arobaini ambapo Ali kamwe hakuabudia sanamu lolote. Hivyo pia Imam Hasan na imam Husein ni mashahidi wakubwa kabisa katika historia ya binadamu, na uadilifu wa Maimam waliobaki hauna shaka lolote.

[63] Wafasiri wote kwa pamoja wanakubaliana kama Imam wa ki-Ashari Quushaji anavyokiri kwenye *Sharh Al-Tajrid* kuhusu suala la Uimam, kwamba aya hii inalenga kwa Amir Al-Muuminin Ali (a.s.) wakati alipompa masikini pete yake wakati alipokuwa kwenye rukuu akiswali. Imam Nasa'i pia ameandika hadithi hii katika *Sahihah al-Nasa'i* yake kutoka kwa Abdullah ibn Salam na hivyo hivyo alifanya mwandishi wa *Al-jama Bayn al-Sihah al-sitta* (mkusanyiko wa vitabu sita vilivyo sahihi) katika mjadala wa tafsir kuhusu Sura ya Maidah na ndivyo hivyo Thalabi amefanya.

[64] Ibn Hajar ametafisiri aya hii katika *Sawiq Al-Muhriqah* sura ya 11 sehemu ya 1 kama ifuatavyo: "Katika kila tukio ni msamehevu kwa yule atubiaye, aaminiye na anayefanya mema na wakati uleule anakubali mwongozo pia.' Thabit al-Banni anasema kwamba 'anayekubali mwongozo' maana yake ni kuongozwa kwa Ahlul-Bayt, na kuendelea kusema kuwa imesimuliwa na Imam Muhammad ibn Baqir (a.s.) na Imam Ja'far al-Sadiq (a.s.) kwamba hii ndio maana yake. Ibn Hajar ameandika hadithi ambazo zinaonyesha kwamba 'mwongozo' maana yake ni uongozi wa Ahlul-Bayt anaeleza kile Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) alichosema kwa Harith ibn Yahaya, "Ee Harith, huoni jinsi Mwenyezi Mungu ambavyo ameweka sharti kwamba ameamuru hali ya toba, imani na matendo mema hayawezi kumnufaisha yeyote mpaka aongozwe kwenye kukubali kwama sisi ni viongozi wake?" Halafu akasimulia kwamba Amir al-mumin (a.s) alisema: kama yeyote anatubu na kushika imani na kutenda mema lakini hafuati uongozi wetu na hatambui nafasi yetu haitamfaa chochote." Abu Nu'aim al-Hafiz pia anaelezea hadithi ya Amir al-Muumin kupitia kwa Aun ibn Abu Jahifah, na ndivyo walivyosema Imam Hakim, Thabit al-Ibnani na Anas Ibn Malik.

Sio kwamba uongozi wao ni sehemu ya '**amana**' ambayo Qur'ani inazungumzia juu yake: **"Kwa hakika tulizitolea amana mbingu na ardhi na milima na zikakataa kuichukua na zikaiogopa, lakini mwanadamu akaichukua. Hakika yeye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana," (33:72).** [65]

Je! wao Ahlul-Bayt hawakuwa ndio "amani" ambamo Allah ameamuru kila mtu kuiingia akisema: **"Enyi mlioamini ingieni katika amani wote na msifuate nyayo za shetani. "(2:208).** [66] Je! Ahlul-Bayt sio '**neema**' ambayo juu yake Qur'an inasema: **"Halafu, katika Siku hiyo, mtaulizwa kuhusu hiyo neema." (102:8).** [67] Je! Haikuwa kuhusu neema ambayo Mtukufu Mtume aliamuriwa kuufikisha yote haya? Je Mwenyezi Mungu hakusisitiza kuufikisha kwa lugha ambayo ilivuma kama ya kutisha ikisema ifuatavyo: **"Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri." (5:67).**[68] Hivi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuufikisha ujumbe huu pale Ghadir Khum, baada ya kufika kwenye mawanda hayo ambapo baada ya hilo Allah akashusha aya hii ya pongezi: **"…Leo nimewakamilishia dini yenu na kuwatimizia neema yangu na nimewapendelea Uislamu kuwa dini…" (5:3).** [69]

Umeona Mola Wako alivyomfanya yule mtu aliyekataa waziwazi uongozi wao akisema: "Ee Mwenyezi Mungu! Kama hili ni kweli linatoka Kwako basi mvua ya mawe itunyeshee kama mvua kutoka mbinguni na kufanya adhabu kubwa juu yetu sisi.?" Allah akamuangushia Jiwe la Sijjil kama vile alivyofanya kwa jeshi la tembo. Aya zifuatazo ziliteremshwa kufuatana na tukio hilo. [70] **"Muulizaji aliomba juu ya adhabu itakayotokea, na kwa makafiri hakuna wa kuizuia." (70:1-2).**

Kwa hakika watu wataulizwa kuhusu mamlaka kama hayo watakapofufuliwa, kama ilivyoashiriwa katika maelezo ya aya hii: **"Wasimamisheni, kwani ni lazima waulizwe." (37:24).** [71] "Fuateni nyayo zao kwani wao wana mamlaka." Hakuna nafasi ya kushangaa zaidi ya hapo hususan pale tunapotambua ukweli kwamba mamlaka yao yameamriwa na Allah swt. juu ya watu kwa kupitia kwa Manabii Wake, wakitoa ushahidi na hoja juu ya hilo, kama ilivyoashiriwa na maelezo ya maneno Yake: **"Waulize mitume wetu tuliowapeleka kabla yako. (43:45).**[72]

---

[65] Tazama *Tafsir al-safi* na Tafsir Ali ibn Ibrahim Al-Qummi; pia hadithi zilizosimuliwa na Ibn Babawayh kutoka kwa Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) na Imam Ja'far al-Sadiq (a.s.) na hadithi za Sunni zilizoandikwa na Allamah Bahrayni kwenye kitabu chake *Ghayanal-Maria,* sura ya 115.

[66] Katika Sura ya 224 ya *Ghayat al-Maraam*, mwanachuoni wa Bahrain ananukuu riwaya kumi na mbili kutoka kwenye Sahih zetu zinazothibitisha kwamba aya hii ilishuka kuhusu wilayat ya Ali na ile ya Maimam (a.s.) kutokana na kizazi chake na kuzuia uongozi kushikwa na wengineo. Katika sura ya 223 anaeleza kwamba al-Asfahani al-Amawii anasimulia vivyo hivyo kuhusu Ali (a.s.) akinukuu vyanzo kadhaa.

[67] *Ghayah al-Maram* cha Allamah Bahrayni sura ya 48, ambacho kina hadithi tatu ambazo zimesimuliwa kutoka kwa wasimulizi wa Sunni, ikionyesha kwamba katika aya hii neno '**neema**' maana yake ni kuneemeshwa kwa uongozi kupitia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na Maimam (a.s). Sura 49 ya kitabu hicho hicho inazo hadithi sahihi 12 za Shia ambazo zinazungumzia suala hilo hilo.

[68] Idadi kubwa ya wasimuliaji wa hadithi pamoja na Imam Wahidi (kwenye *Asbab al-Nuzul*) wamesimulia kutoka kwa Hadhrat Abu said al-Khudri na wengineo kwamba aya hii, ilteremshwa kule Ghadir Khum kuhusu Hadhrat Ali (a.s.). Thalabi kwenye *Tafsir* yake amesimulia kupitia vyanzo viwili kutoka kwa Allamah Hamuyani Shafii amesimulia kwenye kitabu chake *Al-Faraidah* kupitia kwa wasimulizi wengi kutoka kwa Abu Hurayrah, Abu Nu'aim kwenye kitabu chake *Nuzul Al-Qur'ani* amesimulia kupitia kwa wasimuliaji wawili kutoka kwa Abu Rafi na Al-A'mash na wao kutoka kwa Atiyah, *Ghayah al-Maram* inayo Hadithi tisa kutoka wasimulizi wa Sunni na hadithi nane kutoka kwa wasimulizi wa Shia zote zinazungumzia suala moja (Sura 37 na 38).

[69] Ni muhimu kwamba neno hilo hilo '**neema**' limerudiwa hapa, Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) na Imam Ja'far al- Sadiq (a.s.) wametuambia wazi wazi kuhusu hali ambayo ilikuwepo wakati aya hii inateremshwa na vitabu vya Sunni vimeandika hadithi sita kutoka kwa Mtukufu Mtume mwenyewe kuhusu ukweli huo huo (*Ghayah al-Maram* sura ya 39 na 40).

[70] *Tafsir Tha'labi; Nur al-Absar* cha Allamah Shablanji, uk. 71; *Sirah al-Halabiyah*, Jz. 3; na *Mustadrak*, Jz. 2, 502.

[71] Ibn Hajar katika kitabu chake: *Saw'iq al-Muhriqah*, ametaja aya hii miongoni mwa aya ambazo hufanya rejea kwa Ahlul Bayt na amefafanua juu yake kwa urefu na akaandika hadithi mbalimbali kuunga mkono ufafanuzi wake. Mbali na hilo, Al-Daylami anasimulia kutoka kwa Abu Sa'id al-Khudri kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba katika aya hii maneno '**ni lazima waulizwe'** yana maana kwamba lazima waulizwe kuhusiana na wilayat ya Ali na Ahlul Bayt (a.s), kwa vile Allah alimuamrisha Mjumbe Wake kutangaza kwa watu kwamba haombi malipo yoyote kwa kazi yake ya kuhubiri isipokuwa mapenzi kwa ndugu wake wa karibu. Hii ndio sababu ya kwanini wataulizwa iwapo waliitii wilayat ya Ahlu Bayt kwa ukamilifu au la. (tazama *Saw'iq al-Muhiriqah*, sura, 1(1)

[72] Itoshe tu kwako kile ambacho Abu Na'im al-Hafidh alichoandika katika kitabu chake *Hilyat al-Awliyaa* halikadhalika kama ilivyosimuliwa

Uongozi wa Ahlul-Bayt ni wa umuhimu mkubwa hivyo kwamba Mwenye Enzi alifanya mapatano kuhusu jambo hilo na roho zote za viumbe Wake kabla ya uumbaji wa maumbo ya miili yao katika siku ya *'Alastu'* kama ilivyo tajwa kwenye aya ifuatayo: **"Na Mola Wako alipowaleta katika wanadamu kutoka miongoni mwa kizazi chao, na akawashuhudilisha juu ya nafsi zao. Je, Mimi siye Mola Wenu? Wakasema: Kwa nini! Tumeshuhudia (kuwa Wewe ndiye Mola wetu)…" (7:172).**[73] Ilikuwa kupitia kwa uombezi wa Ahlul-Bayt kwamba Adam (a.s.) alijifunza maneno ya toba yaliyotajwa katika sura ya pili (2:37) kwenye Our'ani Tukufu.[74]

Mwenyezi Mungu hawaweki kwenye mateso.[75] Kwani wao ni kimbilio la wale wote waishio duniani na ni njia ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu. Wao ni wale ambao kwamba watu wanawaonea wivu kama Qur'ani 'Tukufu isemavyo:[76] **"Au wanawahusudu watu kwa yale Mwenyezi Mungu aliyowapa katika fadhila Zake? (4: 54).**[77]

Wao ni wale waliobobea kimadhubuti kwenye elimu ambao kuhusu wao Qur'ani Tukufu inasema: **"… Hakuna ajuaye taawili yake isipokuwa Mwenyezi Mungu na wale waliozama kwenye elimu, ambao husema: Tunaamini yote imetoka kwa Mola (3:7).**[78] Ni wale watu ambao wataonekana juu "**Miinuko**," na kuhusu wao Qur'ani Tukufu inasema: **"Na watu wa mahali palipoinuka wanawaita watu ambao wanawajua kwa alama zao …" (7:48).**[79] Ni watu wa kweli ambao kuhusu wao Qur'ani Tukufu inasema:

na Thaalabi, Al-Naysaburi na Al-Barqi kuhusu maana yake katika *Tafsiir* zao, halikadhalika na wenginewo miongoni mwa *Ahlu Sunnah* kama vile Ibrahim ibn Muhammad al-Hamawayni. Vilevile, Abu Ali al-Tabrasi aliielezea katika *Majm'a al-Bayan* kwa mujibu wa Amirul-Muminin (a.s) alivyosema. Na katika *Ghayat al-Maram* sura ya 44 & 45, kilichoandikwa katika maana hii ni kitu kinachoondoa shaka yoyote ile.

73 Wakati Allah (s) alipoamua kuumba ulimwengu, Alikusanya viumbe Wake wote pamoja mbele Yake Mwenyewe na akawauliza: "Ni nani Mola Wenu?" Hapo hapo wa kwanza kujibu alikuwa ni Mtukufu Mtume (s.a.w.w), na wa pili alikuwa ni Amirul Muminin (a.s) na kisha Maimamu wote ambao watakuwa kizazi chake. Wote walisema: "Wewe ni Mola wetu." Kisha Allah (s) akawafanya hazina ya Ilmu ya Mungu na akawaambia Malaika: "Tazama, hawa ni hazina ya Ilmu Yangu na hawa ndio walioaminiwa miongoni mwa viumbe Wangu wote na watakuwa walinzi wenu katika kila kitu." Kisha Allah (s) akaamuru watoto wote wa Adam wakiri kwamba Yeye ni Mola Wao na kuahidi utii Kwake na wakasema: "Tunaahidi." Hapo hapo Allah (s) aliwafanya Malaika washuhudie ahadi hii na Malaika wakasema: "Tunashuhudia." Kisha Akasema: "Wasije wakasema katika Siku ya Hukumu kwamba: 'Tulikuwa hatulijui hili,' au wakasema: 'Ilikuwa ni wahenga wetu ndio ambao hawakuamini na sisi tumekuja tu baada yao, basi Wewe utatuangamiza kwa kile ambacho waovu walikuwa wakikifanya?" (tazama *Tafsir al-Ayyashi*, hadith iliyosimuliwa kutoka kwa Imamu Ja'far al-Sadiq (a.s); vilevile tazama *Firdaus al-Akhyar* cha Allamah Daylami sura ya 14, uk. 274)

74 *Tafsiir Durr al-Mansur*, kitabu cha 1, ukurasa wa 61: *Kanz-al-Ummal*, kitabu cha 1, ukurasa wa 234: *Yanabi al-mawaddat* ukurasa wa 79. *Sawaiq al-Muhriqah,* sura ya 11 katika sherhe ya aya ya Qur'ani: "Lakini Mwenyezi Mungu hatawadhibu wakati wewe (Ee Muhammad) uko nao, wala hatawaadhibu wakitubu …." (Qur'ani, 8:33)

75 *Sawaiq al-Muhriqah*, sura ya 11 sharhe ya aya ya sita ambayo inawasifu Ahlul-Bayt.

76 Allamah Kulayni mwanachuo mkubwa wa Kiislam, amesimulia kutoka kwa Imam Ja'far al-Sadiq (a.s.) alisema kwamba; "Sisi ni watu ambao utiifu wetu umeunganishwa kama wajibu na Mwenyezi mungu, ni wale ambao tumejichimbia kikamilifu kwenye elimu ya mungu na ni wale ambao tulionewa wivu kwa ajili ya neema ambazo mwenyezi mungu alitujalia." Shaykh al-Sadduq pia ameelezea hadithi hiyo hiyo ya kutoka kwa Imam Ja'far Al-Sadiq katika *Tahdhib* yake.

77 Hii imekubaliwa na ibn Hajar ambaye anaihesabu aya hii miongoni mwa zile zilizoshuka kwa heshima yao, akiiweka ya 6 katika sura ya 11 ya *Sawa'iq al-Muhriqah*. Ibn al-Maghazili Shafi'i kama ilivyoashiriwa katika maelezo ya aya hii ndani ya *Sawa'iq al-Muhriqah*, anamnukuu Imam al-Baqir (A.s.) akisema: "Wallahi sisi ndio tunaoonewa wivu." Katika sura ya 60 na 61 ya *Ghayata al-Mahraam* riwaya sahihi kama thelathini hivi zimeandikwa zikiwa na maana hii.

78 Allamah Kulayni mwanachuo mkubwa wa Kiislam, amesimulia kutoka kwa Imam Ja'far al-Sadiq (a.s.) alisema kwamba; "sisi ni watu ambao utiifu kwetu umeunganishwa kama wajibu na Mwenyezi Mungu, ni wale ambao tumejichimbia kikamilifu kwenye elimu ya Mungu na ni wale ambao tulionewa wivu kwa ajili ya neema ambazo Mwenyezi Mungu alitujalia." Shaykh al-Sadduq pia ameelezea hadithi hiyo hiyo ya kutoka kwa Imam Ja'far Al-Sadiq (a.s.) katika *Tahdhib* yake.

79 *Yanabi al-Mawaddat*, uk. 83; *Ruuh al-Bayan*, kitabu cha 1, uk. 723, Ibn Abbas amesimulia kwamba Araf ni sehemu ambayo iko juu zaidi kuliko sirat ambapo Abbas, Hamzah Ali na Ja'far mwenye mbawa mbili watakuwa wanasimama. Watawatambua rafiki zao kwa nyuso zao za kung'aa na maadui zao kwa nyuso zao nyeusi. Imam Hakim alisimulia kupitia vyanzo sahihi kutoka kwa Hadhrat Ali (a.s.) kwamba alisema: "Tutasimama katika sehemu iliyopo katikati ya pepo na Jahannam Siku hiyo ya Hukumu, na tutawatambua wale waliotusaidia na tutawaelekeza kwenda Peponi, na tutawaelekeza wale waliokuwa maadui zetu Jahanamu." Darqutni pia amesimulia Hadithi hiyo hiyo (angalia *Sawaiq al-Muhriqah*, sura ya 9). Hadhrat Ali (a.s.) alisema kuiambia kamati ya watu sita ambao Umar aliwateua ili wamchague mrithi wake, wakati alipokuwa anatoa hotuba yake ndefu: "Nawaulizeni kwa kiapo ikiwa yupo yeyote miongoni mwenu isipokuwa mimi ambaye Mtukufu Mtume alisema: 'Ee Ali, utakuwa mgawaji wa Pepo na Jahannam Siku ya Hukumu." Na walisema "Hapana, hakuna yeyote isipokuwa wewe tu ambaye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kuhusu hilo. " Allamah Ibn Hajar, akizungumza kuhusu hadithi hii ameandika kwamba inathibitisha kile ambacho Antarah alichosimulia kutoka kwa Imam al-Ridha (a.s.) kwamba Mtukufu Mtume alisema:

**“Wapo watu miongoni mwa waumini waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwishamaliza nadhiri zao, na baadhi wanangojea; wala hawakubadilisha ahadi yao hata kidogo. (33:23).**[80] Ni watu ambao wakati wote humtukuza (*dhikir*) Allah kwa mfululizo, kuhusu wao Qur’ani Tukufu inasema: **“Katika nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameruhusu ziinuliwe na kutajwa humo jina lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni. Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kuisimamisha Swala na kutoa Zaka. Wanaihofu siku ambayo nyoyo na macho yatageuka.” (24:36-37)**[81]

Nyumba zao ni zile zilizotajwa na Allah Aza wa Jallah katika Qur’ani Tukufu katika maneno yenye kumetameta: “**Katika nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameamrisha atukuzwe na humo litajwe Jina Lake…” (24:35)**[82] Mwenyezi Mungu amefanya ‘kishubaki chao’ katika maneno ambayo Mwenyezi Mungu ameielezea Nuru Yake katika Sura An-Nur (24: 35), amesema: **“...Naye ndiye Mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye uwezo, Mwenye hekima.” (30:27)**

**“Mwenyezi Mungu ni nuru ya mbingu na ardhi.**

**Mfano wa nuru yake ni kama shubaka ndani yake mna taa.**

**Taa hiyo imo katika glasi; na glasi hiyo inameremeta kama nyota,**

**iliyowashwa kwa mafuta yanayotokana na mti uliobarikiwa, mzaituni.**

**Sio wa mashariki wala wa magharibi.**

**Yanakurubia mafuta yake kung’aa ingawa hayajaguswa na moto –**

**Nuru juu ya nuru. Mwenyezi Mungu humuongoza kwenye nuru Yake amtakaye.**

**Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano;**

**na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu.”**[83]

---

‘Ee Ali, wewe ni mgawaji wa Pepo na Jahannamu, utaiambia Jahanamu: ‘Huyu ni wa kwako na yule wa kwangu.’” Pia ameandika kwamba Samak amesimulia kwamba Abu Bakr alisema: “Nimesikia Mtukufu Mtume akisema kwamba atavuka Daraja yule tu ambaye Ali atakuwa amempa ruhusa.

[80] Allamah ibn Hajar ameandika kwenye *Sawa’iq al-Muhriqah* yake sehemu ya 5 sura ya 9 kwamba wakati Hadhrat Ali Amir al-Muminiin alipokuwa ameketi kwenye mimbari ya msikiti wa Kufah, mtu mmoja alimuuliza kuhusu aya hii na alijibu: ‘Aya hii iliteremshwa kuhusu mimi, ammi yangu Hamzah na binamu yangu Ubaydat ibn Harith. Ubaydat aliuawa katika vita ya Badr; ammi yangu Hamza aliyatoa maisha yake kwa ajili ya Uislamu katika vita vya Uhud, na kuhusu mimi, namgojea huyo mtu mwovu kupita wote ambaye hatimaye atapaka nywele zangu za kichwa kwa damu yangu. Bwana wangu mpendwa, Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ameniambia hivyo.” Hakim pia amesimulia hadithi hiyohiyo kutoka kwa Hadhrat Ali (a.s.).

[81] Mujahid na Ya’qub ibn Sufyan wanasimulia kutoka kwa Ibn Abbas katika ufafanuzi wa aya ya kumi na moja ya surah Jum’ah kwamba Dahyah al-Kalbi alirudi pamoja na bidhaa kutoka Syria siku ya Ijumaa moja na akasimama nje ya mji wa Madina na akatangaza kurudi kwake kwa kupiga ngoma. Watu waliposikia ngoma hizo walikimbia kuelekea huko kwenye msafara huo na wakamuacha Mtukufu Mtume (s.a.w.w) takriban peke yake juu ya mimbari ambapo alikuwa akihutubia katikia swala ya Ijumaa. Alibakia tu Imamu Hasan, Imamu Husein, Hadharat Ali, Abu Dharr na Miqdadi. Katika tukio hili Mtukufu Mtume alisema: “Tazama! Allah (s) ameweka Rehema Zake juu ya msikiti huu leo. Lau zisingekuwa hizi nafsi chache kubakia ndani yake Madina yote ingeteketezwa kwa moto, na mawe yangenyesha (kama mvua) kutoka mbinguni juu ya wakazi wake kama watu Lut.” Wakati huo aya iliyonukuliwa hapo juu (24:36-37) iliteremshwa kwa kuwatukuza wale waliobakia mle msikitini.

[82] Tha’labi, katika ufafanuzi wa aya hii anasimulia kutoka kwa Anas ibn Malik na Buraydah kwamba wakati Mtukufu Mtume aliposoma aya hii, Abu Bakr alisimama na akauliza, akielekeza kidole kwenye nyumba ya Ali na Fatma (a.s), iwapo nyumba ile ilikuwa imejumuishwa katika nyumba zilizotajwa, na Mtukufu Mtume akajibu: “Ndio, na ni bora kuliko nyumba nyingine zilizotajwa katika aya hii.”

[83] Rejea kwenye maelezo: **Mfano wa nuru yake ni kama shubaka ndani yake mna taa…(24:35)** Ibn Maghazil al-Shafi’i amesimulia kwamba ‘**Shubaka**’ maana yake Hadharat Fatmah, ‘**taa**’ maana yake Hasan na Husein, ‘**Si wa mashariki wala magharibi’** maana yake ni kwamba si Wayahudi wala Wakiristo, ‘**mti uliobarikiwa**’ maana yake Nabii Ibrahim ambaye kwaye walishuka, ‘**Yanakurubia mafuta yake kung’aa**’ humaanisha ukubwa wa ilmu yao, ‘**Nuru juu ya nuru**’ humaanisha Imamu mmoja kumrithi mwingine na ‘**Mwenyezi Mungu humuongoza kwenye nuru yake**’ yaani mapenzi kwa watoto wa Ali na Fatmah (a.s)

Nao ni wa mbele katika kuikubali dini na kuitekeleza, ni wale ambao wako karibu kabisa na Mwenyezi Mungu, kama ilivyotajwa katika Qur'ani Tukufu 56:10-11. [84] Na ni wenye kusadikisha (4:69). [85] Wao ni Mashahidi na wachamungu bora. Na kuhusu wao na wafuasi wao Qur'ani Tukufu inasema: **"Na katika wale tuliowaumba kuna taifa ambalo huwaongoza wenziwao kwa uadilifu na wanafanya haki humo." (7:18(1).** . [86] Qur'ani Tukufu inasema juu ya Ahalul-Bayt na wafuasi wake kwa upande mmoja na maadui zao kwa upande mwingine: **"Hawawi sawa watu wa motoni na watu wa peponi; watu wa peponi ndio wenye kufuzu. (59:20).** [87]

Aidha, imeonyeshwa katika Qur'ani Tukufu juu ya marafiki zao na maadui zao:

**"Je, tuwajaalie wale walioamini na kutenda mema kuwa sawa na wafanyao ubadhilifu katika ardhi? Au tuwajalie wachamungu kuwa sawa na waovu? (Qur'ani, 38:28).** [88]

**Vilevile katika aya zifuatazo kuhusu makundi yote:**

"Je! Wanafikiri wale waliofanya maovu kuwa tutawafanya kama wale walioamini na kutenda mema wakati wa uhai wao na baada ya kufa kwao? Hukumu yao ni mbaya (Qur'ani, 45:2(1). [89]

Kuhusu wao na wafuasi wao Qur'ani inasema: **"Hakika, hao waliotenda wema na walioamini, basi hao ndio wema wa viumbe. (Qur'ani, 98:7).** [90]

Kuhusu wao na maadui zao Mwenyezi Mungu anasema: **"Hawa mahasimu wawili ambao wanahasimiana kwa ajili ya Mola wao. Hivyo basi, kwa wale waliokufuru watakatiwa nguo za moto na yatamiminiwa juu ya vichwa vyao maji yachemkayo. 22:19.** [91]

**Kuhusu wao na maadui zao aya zifuatazo ziliteremshwa:**

"Je! Yule aliye muumini yupo sawa na yule aliye fasiki? Hawawi sawa. Kwa wale walioamini na wanafanya vitendo vizuri watakuwa na mabustani ya makazi mazuri. Malipo kwa yale waliyokuwa wakiyatenda. "Na wale ambao hufanya uovu, makazi yao ni motoni, watakapojaribu kutokaa humo

---

[84] Dayami anasimulia kutoka kwa Hadharat Aisha, na Tabrani na Ibn Marduwayh anasimulia kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Miongoni mwa wale walioko mbele kabisa katika mbio kuelekea kwa Allah walikuwa watu watatu : Joshua, mwana wa Nun, akielekea kwa Musa, Yasin, kuelekea kwa Yesu na Ali Ibn Abi Talib kuelekea kwangu." (*Sawa'iq al-Muhriqah* seh. 2, sura 9)

[85] Ibn Al-Najjar anasimulia kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Wamekuwepo masidiiq watatu nao ni Habib, fundi seremala, mumini wa Ali Yasin; Hizqil mumini kutoka kwa Aali Firawn na Ali ibn Abi Talib, na yeye ndiye bora kuliko wote."

[86] Mawaffaq ibn Ahmad amesimulia kutoka kwa Abu Bakr ibn Marduwayh uk. 276, kwa nyororo ya wasimulizi kutoka kwa Hadrat Ali kwamba karibu sana Waislamu watagawayika makundi 73 kati ya makundi 72 yatatupwa Jahanam na moja tu litafika Peponi. Hawa ni watu ambao kuhusu wao Mwenyezi Mungu ameteremsha aya hii na ni hao Mashia wangu.

[87] Sheikh al-Tusi anasimulia katika kitabu chake *Amali* kupitia vyanzo sahihi kutoka kwa Amirul Muminin (a.s) kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema baada ya kusoma aya hii: "Watu wa Peponi ni wale ambao watanitii mimi na kukubali Ali kama kiongozi baada yangu, na watu wa motoni ni wale ambao watakataa uongozi wa Ali na kuvunja kiapo chao na kupigana dhidi yake baada yangu." Sheikh al-Sadduq naye vilevile alisimulia hadithi kama hiyohiyo kutoka kwa Hadharat Ali, na mwanachuoni wa Sunni Muwaffaq ibn Ahmad, amesimulia kutoka kwa Jabir ibn Abdullah Ansari kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Wallahi Ali na Shia wake watafudhu Siku ya Hukumu."

[88] *Tafsir Durr al-Manthur*; *Ghayat al-Maram*, syra ya 81 &82

[89] Ibn Abbas anasimulia kwamba aya hii inamhusu Ali Ibn Abi Talib (a.s), Hamza ibn Abd al-Muttalib na Ubaydat ibn Harith; maneno 'wale wafanyao matendo maovu' yanawahusu Utbah, Shaybah na al-Walid, na maneno 'wale walioamini na kutenda mema' yanawahusu Ali, Hamza na Ubaydah.

[90] Kwa ufafanuzi zaidi tazama Saw'iq al-Muhriqa, seh. 1, sura 11.

[91] Imamu Bukhari ameandika hadithi kutoka kwa Hadharat Ali (a.s) katika Sahih *al-Bukhari* seh. 5, uk. 107, kuhusiana na tafsiri ya Surah al-Hajj kwamba Hadharat Ali (a.s) alisema: "Siku ya Hukumu nitakuwa wa kwanza kuwasilisha mgogoro wangu (mbela za Allah) kwa ajili ya uamuzi Wake." Imamu Bukhari anaendelea kusimulia kutoka kwa Qays kwamba aya hii inawazungumzia wale ambao walipigana vita vya Badr, na walikuwa Ali, Hamza na Ubaydah upande mmoja na Utbah, Shaybah na Al-Walid upande mwingine. Katika ukurasa huo huo, Bukhari anaeleza kwamba Abu Dharr alisema kwa kiapo kwamba aya hii iliteremshwa kwa ajili ya Hamza, Ali na Ubaydah kwa upande mmoja, na Utbah, Shaybah na Al-Walid upande mwingine.

watarudishwa mumo humo na wataambiwa: Onjeni tu adhabu ya moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha (Qur'ani 32:18-20).[92]

Ni kwa habari ya ubora wa Ahlul-Bayt kulinganisha na wale waliokuwa wanajivunia heshima yao ya desturi ya kuwapa maji mahujaji na usimamizi wa Ka'abah Takatifu ambapo aya ifuatayo iliteremshwa: **"Je, mnafanya kuwanywesha mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtukufu ni sawa na yule aliyemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na akapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu." (Qur'ani 9:19).** [93]

Ni katika kuwasifia Ahlul-Bayt kwa kufaulu kwao katika majaribu na mabadiliko ya maisha na kwa uvumilivu na uchangamfu wao katika matatizo mengi kwamba Qur'ani Tukufu inasema: **"Na miongoni mwa binadamu yupo anayeuza nafsi yake kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu: Na Mwenyezi Mungu ni mpole kwa waja wake. (Quran. 2:207).**[94] Na hii pia inasema: **"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa waumini nafsi zao na mali zao kwamba wao wapate Pepo, wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo wanaua na kuuawa. Ni ahadi aliyojilazimisha kwa haki katika Tawrat na Injil na Qur'ani. Na ni nani atekelezaye zaidi ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliofanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa. Wanaotubia, wanaoabudu wanaohangaika, wanaorukuu, wanaosujudu, wanaoamrisha mema na wanaokataza maovu na wanaohifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na wape bishara Waumini." (9:111-112).** Qur'ani Tukufu inasema zaidi ya hayo: **"Wale watoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola Wao; wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika (Qur'ani 2:274).**[95]

Ahlul-Bayt kwa ukweli na uaminifu walisadikisha ukweli wa ujumbe wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), kwa hiyo Mwenyezi Mungu anatamka hii sifa yao katika aya ifuatayo: **"Na aliyeleta ukweli na aliyeu-**

---

[92] Wafasiri na wakusanyaji wote wa hadithi wanakubaliana kwa pamoja kwamba aya hiyo hapo juu inawahusu Ali Ibn Abi Talib (a.s.) kwa upande mmoja na Al-Walid ibn Aqbah ibn Abi Mu'iit kwa upande mwingine. Imam Wahidi anasema katika kitabu chake *Asbab al-Nuzul* (Mazingira ya kuteremshwa kwa aya) kutoka kwa Sa'id ibn Jubayr ambaye anasimulia kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Al-Walid ibn Aqbah ibn Abi Mu'iit alisema kumwambia Amir al-Muminin: "Mkuki wangu una makali zaidi kuliko wako, hotuba yangu ni fasaha zaidi kuliko yako na jeshi langu ni kubwa zaidi kuliko la kwako." Amir al-Muminin alijibu: "Nyamaza! Kwani wewe unaishi maisha maovu tu," ndipo hapo maneno hayo hapo juu yaliteremshwa. 'Muumin' maana yake ni Ali na yule aishiye maisha maovu, maana yake ni Al-Walid ibn Aqbah.

[93] Aya hii inamhusu Abbas ibn al-Muttalib, Talhah ibn Shayba na Amir al-Muminin Ali ibn Abi Talib (a.s.). Siku moja hao wawili wa kwanza hapo juu walitambiana kwa sababu ya kule kupendelewa na kuheshimiwa kwao. Talhah alisema: "Mimi ni mwangalizi wa Kaaba Takatifu na ufunguo wake uko kwenye mamlaka yangu. Abass alisema: "Mimi ni mdhamini wa kisima kitakatifu cha Zam zam na heshima ya kuwapa maji mahujji ni yangu." Hadrat Ali alisema: "Nashangaa kwa nini mnajivunia mambo hayo. Mimi nilianza kuswali miezi 6 kabla yenu na mimi ni mwanajeshi apiganiaye katika njia ya Mwenyezi Mungu." Aya hiyo hapo juu iliteremshwa wakati huo. Allamah Wahidi anasimulia kutoka kwa Hasan Al-Basri al-Sha'bi na wengineo kwenye kitabu chake *Asbab al Nuzul*, na pia imesimuliwa kutoka kwa Ibn Sirin na Murrah Al-Hamdani kwamba Hadhrat Ali alimwambia ami yake Abbas: "Kwa nini huhami Makka? Hutaki kwenda kwa Mtukufu Mtume." Abbas alijibu: "Ninafurahia heshima ya kugawa maji kwa mahujaji kwani hiyo sio heshima kubwa zaidi kuliko kuwa Muhajirina?" Hapo Hapo aya hiyo hapo juu ndipo iliteremshwa.

[94] Kwenye *Mustadrak* ya Imam al-Hakim, Jz. 3, ukurasa wa 4 imesimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas: "Angalia! Ali alikuwa mtu aliyejiuza: lile tukio la kujifunika kwake Shuka la Mtukufu Mtume usiku wa kutisha wa kuhama kwenda Madina sio kwamba halijulikiani." Imam al-Hakim anaonyesha kwamba hadithi hii ni sahihi kabisa kwa mijibu wa viwango vilivyokubaliwa na Bukhari na Muslim ingawa wao hawakuisimulia. Hati mpinzani mkubwa kama Dhabahi anakubali usahihi wa hadithi hii kwenye Mukhutasari wa toleo lake la *Mustdrak*. Katika ukurasa huo huo wa kitabu hicho, Imam al-Hakim anasimulia kutoka kwa Imam Zain al-Abidin (a.s.): "Mtu wa kwanza katika Uislamu aliyejiuza nafsi yake ili apate radhi ya Mwenyezi Mungu alikuwa Ali alipolala kwenye kitanda cha Mtukufu Mtume katika usiku wa kugura kwake kutoka Makka." Imam al-Hakim hapo anaendelea kuandika mistari ya shairi ambalo Hadhrat Ali alitunga kuhusiana na tukio hili: 'Nilitoa mhanga maisha yangu kwa ajili ya mtu aliyekuwa mbora wa wote ambao walitufu Nyumba ya kale na jiwe Takatifu.'

[95] Waandishi wote wa Hadithi na wafasiri wote wanasimulia kutoka kwa Ibn Abbas, kupitia nyororo ya wasimuiaji wa kuaminika kwamba aya hii iliteremshwa kwa ajili ya kumsifu Hadhrat Ali (a.s.) kwani alikuwa na dirham nne, aliitoa dirham moja usiku na dirham moja mchana, moja alitoa kwa siri na nyingine kwa wazi hivyo aya hiyo ikateremshwa. Imam Wahidi ameonyesha katika *Asbab al-Nuzul* ikiwa na nyororo iliyo katizwa katizwa ya wasimuliaji mpaka kufika kwa Ibn Abbas. Mujahidi pia alionyesha hadithi hii halafu tena Kalbi alisimulia katika muundo uliogezeka. Pia tazama *Tafsiir Wahidi*, uk. 16; *Ma'alim Tanziil*, uk. 135; *Tafsiir Baidhwawi*, Jz. 1, uk. 125; *Tafsiir Naishapuur*, uk. 278, *Tafsiir al-Kabiir ar-Razi*, Jz. 2, uk. 528; *Tafsiir Ruuh al-Ma'ani*, Jz. 1, uk. 495 na wengineo.

**sadikisha hao ndio wamchao Mwenyezi Mungu. (Qur'ani, 39:33).**[96] Kwa hiyo, imethibitishwa kwamba Ahlul-Bayt ni wafuasi waaminifu na ndugu wa karibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ambao Mwenye Enzi amewateua kwa ajili ya fadhila Zake na heshima kubwa na akamwambia Mtukufu Mtume: **"Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe. (Qur'ani, 26:214).** Hawa ni ndugu zake Mtume. **"…..Na ndugu wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe, katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu. (Qur'ani 8:75 na Sura 33:6).**

Wao ndio ndugu wa karibu sana wa Mtume, na ndugu waliokaribu wanastahiki fadhila. Watakuwa naye kwenye Bustani za furaha ya milele kama inayothibitishwa na aya ifuatayo: **"Na walioamini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao, na wala hatutawapunja kitu katika vitendo vyao kila mtu ni rehani wa alichokichuma. (Qur'ani 52:2(1).**[97]

Hawa ndio wenye haki ya kupokea ambao Qur'ani inasema: **"Na umpe jamaa yako wa karibu haki yake (Qur'ani, 17:26) .** [98]

Ni watu ambao khums ni (sehemu moja ya tano) ni haki yao. Isipokuwa hapo mtu atakapoweka fungu la khums pembeni hawezi kuchukuliwa kuwa amelipa kile anachostahili. Kwa ajili hiyo, Qur'ani inasema: **"Na jueni kwamba chochote mlichopata ghanima (faida), basi khumsi yake ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume na jamaa zake…"(Qur'ani, 8:4(1)**[99] Ni watu ambao mali iliyotelekezwa ni yao, kuhusu hilo Mwenyezi Mungu ametamka katika Qur'ani Tukufu. **"Na chochote ambacho Allah ametoa kama mali (iliyoachwa bila kupigana) kwa Mtume Wake kutoka kwa watu wa vijiji, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya Mtume na jamaa zake …(Qur'ani, 59:7).**

Ni watu wa Nyumba ya Mtume ambao kuhusu wao "Aya ya utakaso" iliteremshwa: **"Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumba ya Mtume, na anataka kukutakaseni kabisa kabisa. (Qur'ani, 33:33).**

Na ni kizazi cha "Yasin" ambao Mwenyezi Mungu amewatakia salaam na amani Yake kama ifuatavyo: **"Amani kwa Aali Yasin (Qur'ani, 37:130).** [100] Ni kwa ajili ya familia ya Muhammad (s.a.w.w.) ambayo kwayo Mwenyezi Mungu ametuamrisha kuitakia rehema, akisema: **"Hakika Mwenyezi Mungu na malaika wake wanamswalia Nabii. Enyi ambao mmeamini! Mswalieni na mumsalimu kwa sal-**

---

96 '**Na aliyeleta Ukweli**' maana yake Mtume '**na aliyeusadikisha**' maana yake Ali kwa mujibu wa tafsiri ya Imamu Muhammad al-Baqir (a.s), Imamu Ja'far al-Sadiq (a.s), Imamu Musa al-Kadhim (a.s), Imamu al-Ridha (a.s), Abdullah ibn Abbas, Muhammad Hanafiyah, Abdullah ibn Hasan, Zayd al-Shahiid na Ali ibn Ja'far al-Sadiq. Amirul Muminin (a.s) mwenyewe alikuwa akisoma aya hii katika kutetea madai yake, na Ibn al-Maghazil anaandika katika *Manaqib* yake kutoka kwa Mujahid kwamba '**Na aliyeleta Ukweli**' maana yake Mtukufu Mtume na '**na aliyeusadikisha**' maana yake Ali. Hafidhan ibn Mardawayh na Hafidh Abu Na'im wao pia wameiandika hadith hii.

97 Imamu Hakim katika kitabu chake *Mustadrak*, seh. 2, uk. 468, anasimulia kutoka kwa Ibn Abbas kuhusiana na tafsiri ya Surah al-Tur kwamba: "Allah (s) atawaweka watoto wa waumini katika daraja moja la Peponi kama waumini hata kama watoto wao wangestahiki malipo kidogo kwa matendo yao."

98 Wafasir wameandika kwamba wakati aya hii ilipoteremshwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimuuliza Malaika Jibrail: "Ni nani jamaa na ni ipi haki yao?" Malaika Jibrail akajibu: "Mpe Fatimah Fadak kwa vile ni haki yake, na chochote ambacho ni haki ya Allah na Mtume kutoka ndani ya Fadak, hicho pia ni haki yake, basi kidhamini pia kwake." Wakati uleule Mtukufu Mtume alimuita Fatimah (a.s) na akaandika hati ya zawadi, akimkabidhi Fadak. (*Tafsir Durr al-Manthur*, Jz. 4, uk. 177 na wafasir wengine).

99 Tazama *Tafsiir Ruuh al-Ma'ani*, Jz. 3, uk. 637; *Tafsiir Naisapuuri*, Jz. 3, uk. 215.

100 Kuhusiana na aya zinazowatukuza Ahlul Bayt, Allamah ibn Hajar ameiandika hii kama aya ya tatu katika sura ya kumi na moja ya kitabu chake *Sawa'iq al-Muhriqah* na amezungumzia humo kutoka kwa Ibn Abbas kwamba "Aali Yasiin maana yake "Aali Muhammad." Anaandika kwamba Kalbi yeye pia ana mtazamo kama huohuo. Fakhr al-Din al-Razi anaandika kwamba Ahlul Bayt wako sawa pamoja pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika vitu vitano: Kwanza katika salaam, kwani Allah amesema: "Amani iwe juu yako Ewe Mtume," na pia alisema: "Amani iwe juu ya Aali Yasin;" pili kuomba baraka na neema za Allah wakati wa swala, baada ya kila *tashahhud*; tatu katika utakaso wao, kwani Allah (s) alimwambia Mtukufu Mtume "Ta Ha" (sura ya 20) na aliteremsha 'Aya ya Utakaso' kwa ajili ya Ahlul Bayt; nne katika sadaqah kuharamishwa kwao na tano mapenzi kwao, kwani Allah alisema kwamba tunapaswa tumfuate Mtume naye atamfanya Allah atupende. Vilevile alisema: "Sema, siwaombi malipo kwa hili bali mapenzi kwa jamaa zangu."

**amu." (Qur'ani, 33:56)**. Waislamu walimuuliza Mtukufu Mtume: "Tukuswalie vipi? Alijibu, "Semeni, "Ee Mwenyezi Mungu mbariki Muhammad na familia ya Muhammad"[101]

Kwa hiyo, inathibitishwa kwa hadithi hii kwamba salaam haikamiliki mpaka hapo familia ya Muhammad wanasalimiwa pia pamoja na Mtume. Hii ndio sababu ambayo imewafanya watu wasomi na wanachuoni wachunguzi wakaiweka aya hiyo hapo juu miongoni mwa zile aya za Qura'ni Tukufu ambazo zinawasifu Ahlul-Bayt (a.s.), na ni kwa sababu hii kwamba Allamah Ibn Hajar ameorodhesha aya hii miongoni mwa aya ambazo zinawasifu Ahlul-Bayt katika sura ya 11 ya kitabu chake. Hivyo wao ni watumishi wateule wa Mwenyezi Mungu na wao ni watangulizi ambao walifanya haraka kuelekea kwenye haki kwa amri ya Mwenyezi Mungu na kuhusu wao Mwenye Enzi anasema: **"Kisha tumewarithisha Kitabu wale ambao tumewachagua katika waja wetu. Kati yao yupo aliyejidhulumu nafsi yake, na yupo wa katikati, na yupo aliyetangulia katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo fadhila kuu. (Qur'ani, 35:32).** [102]

Tunaona hata hizi aya chache zinazowasifu Ahlul-Bayt kuwa zinatosha kwa madhumuni yetu, ingawaje Ibn Abbas alikuwa akisema kuwa katika kumsifu Ali (a.s.) peke yake kuna aya mia tatu katika Qur'ani Tukufu.[103] Tafadhali tafakari kwa makini kuhusu aya hizi na ninatumaini utaona kweli yenyewe kutokana nazo.

Wassalaam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[101] Bukhari ameisumulia katika *Sahih* yake katika sura ya "Kitabu cha Tafsiri ya Qur'ani" sehemu ya 3. Akifafanua aya hii (33:56), Muslim vilevile ameisimulia katika *Sahih* yake sehemu ya 1 ya "Kitabu cha Swala." Wafasiri wote wamefasiri kutoka kwa Ka'b ibn Ujrah.

[102] Sheikh al-Kulayni (ra) anasimulia kutoka kwa Salim kwamba alisema: "Nilimuuliza Imamu Muhammad al-Baqir (as) kuhusu aya hii na alisema kwamba: 'Wale ambao huwapita wengine katika matendo mema' maana yake Maimamu na 'wale ambao wanatembea katikati ya njia' maana yake watu ambao hawawaelewi Maimamu au wale ambao wanawakataa." Hafidh ibn Marduwayh amesimulia hadithi hii kutoka kwa Ali (as).

[103] Kama ilivyosimuliwa na Ibn Asakir kutoka kwa Ibn Abbas; tazama *Sawa'iq al-Muhriqa*, sura ya 9, sehemu ya 3, uk. 76

# BARUA YA KUMI NA TATU

## DHUL QA'DAH, 1329 A.H.

**I. Uwezekano wa Kwamba Hadith hizi**

**II. Kuhusiana na Aya za Qur'ani sio Sahihi.**

Allah atukuzwe! Mtiririko wa kalamu yako na yanayotoka kwenye akili yako ya hali ya juu haviwezi kushindana na anayekupa changamoto ama mshindani! Mazungumzo yako hayawezi kuzuiwa katika kumshawishi mwenye akili ya udadisi na uelewa! Mchango wako uliotoa kwenye suala hili ujaaliwe kuendelea na maandishi yako yarudiwe kwa faida ya wenye hekima. Mambo yote haya hayawezi kuangaliwa ila kwa mvuto wake.

Kuhusu barua yako ya nyuma inabubujika na elimu nyingi na nzuri, na ni kama bahari inayotupa mawimbi. Umeonesha aya ambazo ni za wazi na zenye nguvu kutoka kwenye Qur'ani na umetoa uthibitisho wa kudumu milele. Kwa hiyo umekamilisha kazi ambayo uliahidi kuifanya. Itakuwa ni ujinga kukupinga kwa sababu umefichua hoja za uongo za wajinga.

Hata hivyo wapinzani wako wanaweza kuhoji kwamba wale ambao wamesimulia aya hizi zinazounga mkono hoja yako ni Mashia, na hawa hawawezi kutegemewa na Masunni. Jibu lako litakuwa nini? Kwa hiyo, tafadhali nifanyie ihsani kwa kunipa jibu lako, nami nitashukuru. Amani iwe juu yako. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA KUMI NA NNE

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**I. Kuthibitisha Makosa Ya Hoja Ya Wakosoaji,**

**II. Wakosoaji Hawajui Maana ya neno "Shi'a".**

Shutuma hizi si sahihi kwani zimeegemea juu ya hoja potovu. Kuhusiana na hoja yako "kwamba waandishi wanaoelezea mazingira ambamo aya hizo ziliteremshwa walikuwa Mashia" si kweli, kwa sababu wanachuo wa kuaminika kabisa wa Ahlu Sunnah wameandika hadithi hizo kupitia kwa waandishi wao ambao ni wengi zaidi kuliko wanachuo wa Kishia. Nimeshughulika na nukta hii kwa kina zaidi katika kitabu changu *Al-Ayat al-Bahirah* (Aya zilizo wazi) na nukta hii hii vile vile imeshughulikiwa kwa kina zaidi katika kitabu *Ghayat al-Maram*, ambacho kimesambazwa sana katika ulimwengu wa Uislamu.

Kuhusu hoja yako kubwa, "kwamba Sunni hawawezi kushawishika kukubali juu ya misingi ambayo Shia wameelezea," vitabu sita vya kuaminika zaidi vya hadithi za Sunni vinathibitisha kwamba haya pia ni maelezo potofu, kwani hadithi ambazo wamechukua kutoka kwa waandishi wa ki-Shia ni nyingi sana, na waandishi hawa si watu wasiojulikana kwani ni watu mashuhuri ambao ufuasi wao madhubuti kwa Ali (a.s.) unajulikana wazi na ambao mara nyingi wameelezwa kama ni 'marafidha', 'waliopotoka' na 'mashabiki,' lakini pamoja na hayo, wakusanyaji wa vitabu sahihi vya Hadithi kama vile Bukhari na wengineo wamewahesabu (waandishi) kama waaminifu sana hivyo kwamba wamezijumuisha hadithi zao katika chaguzi ndani ya vitabu vyao. Hata baadhi ya walimu wa Bukhari walikuwa Shia. Hivyo inawezekanaje kusemwa kwamba Sunni hawatakubali hadithi zilizopatikana kutoka kwa wasimuliaji wa Kishia?

Lakini inawezekana labda wakosoaji hawa hawaujui ukweli. Hawatambui kwamba miongoni mwa Shia wamekuwepo watu ambao wamefuata nyayo za kizazi kitakatifu kistahiki ambacho wao hauwezi kuwalinganisha na wengine katika ukweli na uaminifi, uchamungu, uangalifu, utii na unyofu, nidhamu na jitihada ya kujisafisha, na ambao wamejitoa kwa juhudi kubwa mchana na usiku katika kujidhibiti, na hekima ya wazi, wastani na ya tahadhari. Wale wakosoaji kamwe hawajachukua taabu yeyote ya kujua maisha ya watu hawa lakini kwa upofu wameelekeza udaku wao dhidi ya watu kama *Thiqat al-Islam* (mwanachuo mwaminifu wa Uislamu) Muhammad ibn Yaqub al-Kulayni, Saduq al-Muslimin Muhammad ibn Ali ibn Babawayh al-Qumni na Shaykh al-Umma Muhammad ibn al-Hasan Ali al-Tusi, na wanajaribu kukataza maandishi yao matakatifu ingawaje hawa ni waangalizi wa hekima ya Aali Muhammad (a.s.) na ni wahifadhi wa ujuzi na 'Abdaal'[104] ambao walitumia maisha yao kutangaza mafundisho ya Mwenyezi Mungu, Qur'ani Tukufu, Mtukufu Mtume na Maimamu kwa faida ya Waislamu wote.

Hata mtu wa kawaida mtaani anajua kwamba hawa watu wachamungu waliona uongo kama ni dhambi mbaya sana. Kwenye maelfu ya vitabu ambavyo wameandika wameombea laana ya Mwenyezi Mungu kwa waongo na wamesema hapo hapo kwamba ni kwa mujibu wa hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w), adhabu ya uongo ni mateso ya milele na waongo watateketea, na kutamka hadithi za uongo inaonekana kwao kama ni dhambi mbaya ya kuogopesha ambayo huharibu saumu na kuifanya kuwa batili. Ni *fatwa* (uamuzi wa kisheria) yao ya pamoja kwamba kama mtu yeyote kwa kukusudia anarudia kusimulia hadithi ya uongo wakati wa mwezi wa Ramadhani, saumu yake inabatilishwa pale pale na sio afunge upya bali

[104] *Abdal'*: Maana hasa ni wingi wa *badal* (yaani mbadala) Masufi wanaamini kwamba kuna watu waadilifu na watakatifu ambao wanaishi duniani hivyo kwamba kwa sababu yao dunia inaokolewa isiharibiwe na kwamba inapotokea mmoja wao anakufa, mtu mwingine mtakatifu hushika nafasi badala yake. Watu hawa wanaitwa *'Abdal'* na Mashia wengi mashuhuri wanachukuliwa kuwa miongoni mwa *Abdal* kwa mujibu wa imani hii ya Sufi.

lazima pia alipe fidia (*kaffarah*) kama vile amevunja saumu yake kwa kukusudia (kwa mfano kunywa au kula). Wakati wanauona uongo kwa chukizo kubwa kiasi hicho uwe mkweli na uniambie itakuwaje hata kufikiria kwamba hawa watu wanyoofu, watakatifu na waliojiweka *wakf* kwa utumishi wa Mungu, ambao walikuwa wakiswali usiku kucha na kufunga mchana wangewezaje kusema uongo. Ni kweli kwamba tumefikia kwenye mpito wa majuto ikiwa hivi, hadithi zilizosimuliwa na wao zinatiliwa wasiwasi kwamba ni za uongo; maneno yao yanadharauriwa, wakati hadithi za Khawarij, Nasibi na wale walioamini Mungu kuwa ana mshirika wanaheshimiwa na wanakubaliwa kiupofu bila kivuli chochote cha shaka. Hii ni dhuluma kubwa na upendeleo wa aibu. Mwenyezi Mungu naatuepushe na hali kama hii. Wassalaam,

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA KUMI NA TANO

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**I. Mwanga wa Ukweli,**

**II. Maombi ya Maelezo juu ya Masunni Wanaotegemea Vyanzo vya Mashia.**

(1) Barua yako ya hivi karibuni ilikuwa kamili na katika mpangilio mzuri, wazi katika maneno, tamu, yenye faida kubwa, rahisi kueleweka, kubwa katika fani, yenye kuelimisha, iliyotegemezwa vizuri. Nimeiangalia kwa makini sana, mafaniko yako yameng'ara kutoka kwenye madhumuni yake, na dalili za ushindi wako zimeng'ara.

(2) Lakini maelezo yako kwamba Ahlu Sunnah kila mara wamechukua hadithi zao kutoka kwa waandishi wa Shia ni ya jumla mno na ya muhtasari. Unapaswa kufafanua zaidi juu ya hilo. Ingelikuwa vizuri zaidi kama ungetaja majina ya hao waandishi wa hadithi wa Shia na kunukuu maandiko ya Sunni yanayonesha kwamba watu hao walikuwa Mashia na kwamba hata hivyo wao wenyewe waliwategemea. Je unaweza kutupatia taarifa hizo? Tafadhali fanya hivyo ili bendera za ukweli ziweze kuonekena na mwanga wa uhakika uweze kung'ara. Amani iwe juu yako. Wasalaam

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA KUMI NA SITA

## DHUL QA'DAH 1329 A.H.

**I. Vyanzo Mia moja (Pamoja na Majina yao)**
**II. vya Mashia Wanaotegemewa na Masunni.**

Ndio. Nitakupatia kwa haraka kile ulichokiomba, nitawataja tu baadhi ya watu wale mashuhuri ambao walitembelewa na watu kutoka sehemu mbalimbali, kwa masharti kwamba sitaombwa tena kufafanua juu yao, kwa vile hakuna nafasi ya hilo katika ufafanuzi huu mfupi. Hawa ni waandishi wa Shia ambao hadithi zao zimejumuishwa katika vitabu vyenu vya *Sahih* na *Musnad*. Haya hapa majina yao na majina ya baba zao yaliyopangwa kwa alfabeti: [105]

**1. Aban ibn Taghlib ibn Riyah:**

Msomaji wa Qur'ani wa Kufah (alikuwa mwanafunzi wa Imam Zayn al-Abidin na Imam Muhammad al-Baqir (a.s.).

Nukuu ifuatayo inatoka kwenye kitabu al-Mizani cha Dhahabi.

"Aban ibn Taghlib wa Kufah; Shia mkakamavu sana lakini pia mkweli na tunahusika na ukweli wake tu ambapo kule kupotoka kwake kiimani ni tatizo lake la binafsi." Dhahabi anaendelea: "Ahmad ibn Hambal, ibn Mu'in na Abu Haatim wanamuona yeye kama ni wa kuaminika na ibn Adi anafafanua kwamba alikuwa Shia mwenye ghera sana; na Sa'idi ameandika kwamba alikuwa mfarakishaji wa wazi………"

Miongoni mwa wale ambao walimtegemea ni Muslim na waandishi wa *Sunan* nne kwa majina yafuatayo, Abu Dawuud, Tirmidhi, Nasa'i na Ibn Majah, kwa ushahidi wa utumiaji wao wa jina lake kwa kufupishwa. Aidha mnazo hadithi zake kwenye Sahih Muslim na vitabu vine vya Sunan kutoka kwa al-Hakim, al-A'mash na Fudhayl ibn Amr kama zilivyoandikwa na Muslim, Sufyan ibn Uyaynah, Shabah na Idris al-Awdi. Alifariki mwaka wa 141 A.H. Mungu amrehemu.

**2. Ibrahimu ibn Yazid ibn Amr ibn al-Aswad ibn Amr al-Nukhai:**

Mwanasheria wa Kufa. Mama yake alikuwa Malikah bint Yazid ibn Qays, pia kutoka Nakh'ah, kaka zake Al-Aswad, Ibrahim na Abd al-Rahman, watoto wa kiume wa Yazid ibn Qays walikuwa kama ami zao Alqamah ibn Qays na Ubaiy ibn Qays, Waislamu wakakamavu na ushahidi wao unachukuliwa kuwa sahihi. Waandishi wa vitabu vya *Sahih Sita* na wengineo wamechukua hadithi kutoka kwao huku wakijua fika kwamba walikuwa Mashia.

Kuhusu Ibrahimu ibn Yazid mwenyewe, Ibn Qutaybah kwenye *Ma'arif* yake amemuorodhesha yeye miongoni mwa Mashia mwenye imani isiyo na shaka. Aidha, hadithi zake zinapatikana katika vitabu vyote vya *Sahih* yaani; Bukhari na Muslim. Amezisimulia hadithi hizo ama kutoka kwa ami ya mama

[105] Barua hii imekuwa ndefu kwa sababu mada hii inahitajia kuwa hivyo. Wanachuoni hawachoshwi na urefu wake kwa sababu ya mambo yake yaliyomo humo ambayo hujumuisha faida zenye thamani zinazotafutwa na kila mtafiti na wahakiki. Wengine wasio kuwa hawa, yeyote yule ambaye amechoshwa asome sehemu yake, na ahukumu sehemu iliyobakia kwa kadiri ilivyo, na kisha aende moja kwa moja kwenye Barua ya 17 na ile iliyoitangulia. Kwa kuogopa kukuchosha kwa Barua ndefu kama hii, tumejizuia kujumuisha kwayo orodha ya vitabu vyenye thamani na taarifa za kuvutia.

yake Alqamah ibn Qays ambaye naye alizisimulia kutoka kwa Himam ibn al-Harith na Abu Ubayadah ibn Abdullah ibn Masud au kutoka kwa Ubaydah au ami yake Al-Aswad ibn Yazid. Hadithi zake zingine zilizopo kwenye *Sahih Muslim* ni zile ambazo amezichukua kutoka kwa ami yake mwingine aitwaye Abd al-Rahman ibn Yazid na pia kutoka kwa Sahm ibn Munjaab, Abu Mu'amar na Ubayday ibn Nazlah na Aabis. Hadithi zake nyingine zimesimuliwa kwenye zile sahih mbili kupitia kwa Mansuur, Al-A'mash, Zubayd, Hakam na ibn Aun; na kwenye Sahih Muslim kupitia kwa Fudhayl ibn Amr. Mughayrah, Ziyad, Ibn Kulayb, Waasil, Hasan ibn Ubaydullah, Hamad ibn Abu Sulayman na Simaak. Ibrahim ibn Yazid alizaliwa mwaka wa 50 Hijiria na alifariki mwaka wa 95 au 96 Hijria, miezi minne baada ya kifo cha Hajjaj ibn Yusuf.

**3. Ahmad ibn Mufadhal ibn al-Kuufi:**

Abu Zar'ah na Abu Haatim wamechukua hadithi kutoka kwake na wakajenga hoja zao kutokana na hadithi hizo huku wakijua na kukubali kwamba alikuwa Shia. Hivyo basi, Abu Haatim hasa anaeleza kwenye Mizan yake:

"…Ahmad ibn Mufadhal alikuwa katika tabaka la juu kabisa la Shia na alikuwa mtu mkweli..."

Dhahabi naye amemtaja katika Mizani yake na ametumia ufupisho kuonyesha jina lake. Abu Dawuud na Nasa'i pia wamechukua hadithi kutoka kwake na kuziweka kwenye Sahih zao kupitia kwa At-Thawri na amesimulia hadithi hizo kutoka kwa Asbaat ibn Nasr na Israiil.

**4. Isma'il ibn Abaan al-Azdi al-Warraaq:**

Alikuwa mmoja wa masheikh (yaani walimu na washauri) wa Bukhari. Allamah Dhahabi ameandika kwamba wote Bukhari na Tirmidhi wamejenga mawazo yao kutokana na hadithi zake na pia anasema kwamba Yahya na Ahmad wamechukua hadithi kutoka kwake. Bukhari anasema kwamba alikuwa mtu mkweli. Waandishi wegine wanasema kwamba alikuwa mfuasi wa imani ya Shia na kwamba alifariki mwaka wa 286 Hijiria. Al-Qaisaraani, hata hivyo ameweka tarehe ya kufa mtu huyo mnamo mwaka wa 216 baada ya Hijiria na pia amesema kwa uthabiti kwamba Bukhari amechukua hadithi moja kwa moja kutoka kwake kwenye vitabu vyake mbali na kitabu cha Sahih.

**5. Isma'il ibn Khaliifa**, **al-Malai al-Kuufi:**

Jina lake la ubaba (*kun'ya*) ni Abu Israiil na hili ndio jina ambalo anajulikana sana kwalo kwa kawaida. Allamah al-Dahahabi ameandika katika *Mizan al-l'tidal* yake kwamba alikuwa "Shia wa imani thabiti na alimuona Uthuman kuwa si muumini" na amejumlisha maelezo mengine kuhusu yeye. Licha ya yote hayo Tirmidhi na waandishi wengine wa Sunan wamechukua hadithi kutoka kwake, na Abu Haatim ameziainisha hadithi hizi kama "nzuri;" Abu Zar'ah anamchukulia yeye kama "msimulizi wa kweli, ingawaje mawazo yake yalikuwa yamezidi kiwango cha juhudi za kawaida"; "Imam Ahmad ibn Hanbal ameziona hadithi zake "zinastahiki kuandikwa", Ibn Mu'in anamuona yeye kuwa "mkweli;" Fallas anatoa maelezo: "Sio miongoni mwa wale wanaosema uongo, na hadithi zake zinapatikana kwenye *Sahih al-Trmidhi*;" na Ibn Qutaybah kwenye *al-Ma'arif* yake amemuorodhesha miongoni mwa Shia mashuhuri.

**6. Isma'il ibn Zakariya Khalqaani al-Kufi:**

Dhahabi anasema katika *Mizan al-Itidal* yake kwamba ni mtu 'mkweli' na ni Shia na ni mmoja wa wale ambao hadithi zao zimeingizwa katika vile vitabu sita viitwavyo *sahih*." Hadith zake zinaonekana kwenye *Sahih Bukhari* na *Sahihi Muslim.* Alifia Baghdad mnamo mwaka wa 104 baada ya Hijiriyah.

**7. Isma'il ibn Abbad Ibn Abbas al-Talaqaani**:

Maarufu kwa jina la Sahib Ibn Abbad. Abu Dawuud na Tirmidhi wamechukua hadithi kutoka kwake kama zilivyotajwa na Imam al-Dhahabi kwenye kitabu chake *al-Mizani* pamoja na maelezo kwamba

alikuwa "msomi bora sana na mwandishi na alikuwa Shia."[106] Hapana shaka kwamba yeye alikuwa Shia kwani kwa sababu ya imani yake ndio akawa Waziri Mkuu kwenye ufalme wa Buwaihiyyah. Alikuwa mtu wa kwanza kupewa cheo cha 'Sahib', kwa sababu alikuwa mwenzi wa Mu'ayid al-Dawlah wakati wa ujana wake kwa hiyo alipewa cheo hicho na al-Dawlah, kwa hiyo akajulikana kwa jina la 'Sahib' na baada ya yeye ikawa desturi kumwita Waziri Mkuu kwa kutanguliza 'Sahib.' Kwanza alikuwa waziri wa Mu'ayid al-Dawlah ambaye baada ya kufa, kaka yake Fakhr al-Dawlah, aliendelea naye katika wadhifa wake ule, alipokufa mnamo mwaka wa 24 Safar, 385 baada ya Hijiriyah akiwa na umri wa miaka 59 raia wote wa Ray (sasa Tehran) walifunga milango ya nyumba zao na walikwenda nyumbani kwa Waziri Mkuu kuhudhuria maziko yake na mfalme akisindikizwa na wafuasi wake walishiriki kwenye maziko yake. Alikuwa mwanachuo mkubwa na mwandishi wa vitabu kadhaa vya thamani na majarida (vijitabu vidogo vidogo).

**8. Isma'il ibn Abd al-Rahman ibn Abi Kariimah, (Mfasiri mashuhuri ajulikanaye kama Al-Suddi)**

Alamah al-Dhahabi ameandika katika maelezo yake kuhusu Al-Suddi kwamba "Alidaiwa kuwa ni Shia" na Husayn ibn Waaqid al-Muruuzi amesimulia kwamba alimsikia akiwashutumu sana Abu Bakr na Umar lakini pamoja na mambo haya, al-Thawri, Abu Bakr ibn Ayesha na wengine wamechukua hadithi kutoka kwake na Imam Muslim, Tirmidhi, Abu Dawuud, Ibn Majah na Nasa'i wameingiza hadithi zake kwenye Sahih zao katika hali ya kuunga mkono maoni yao. Imam Ahmad (Ibn Hanbal) amemuona yeye kama 'mwaminifu' na Ibn Adi alimwona yeye kama wa kuaminika, ambapo Yahya ibn Sa'id anasema: "Niliona kila mtu anampa sifa nzuri al-Suddi na wote wamechukua hadithi kutoka kwake." Alifariki mwaka wa 127 baada ya Hijiriyah.

**9. Isma'il Ibn Musa al-Fazaari al-Kufi:**

Allamah al-Dhahabi ameandika kuhusu yeye kwenye *Mizan al-Itidal* kwamba Ibn Adi alikuwa akisema mara nyingi kwamba "alilaumiwa kwa sababu ya kuwa Shia mkereketwa sana lakini hakuchukiwa na watu." Abdan anasimulia kwamba Hammad na Ibn Abi Shayban hakupenda sisi kwenda kwake na mara nyingi alisema kwamba tusiende kwa huyo muovu ambaye alikuwa akiwashutumu sana watu wenye kuheshimiwa. Lakini pamoja na haya ibn Khuzaymah, Abu Aruubah na wengi wengineo walijifunza hadithi kutoka kwake na alikuwa na ubora ule ule wa uwalimu kama Abu Dawuud, Tirmidhi na wengineo. Wote wamechukua hadithi kutoka kwake na kuziandika hadithi hizo katika vitabu vyao vya '*Sahih*'. Nasa'i amesema kwamba hakuna madhara kuchukua hadithi kutoka kwake. Alifariki mwaka wa 245 A.H. Waandishi wengine wameonyesha kwamba alikuwa mjukuu wa al-Suddi upande wa kikeni.

**10. Taliid ibn Sulayman al-Kufi**:

Ibn Mu'in ameandika kwamba alikuwa mkosoaji mkubwa wa Uthuman. Hivyo, wafuasi wa Uthuman waliposikia hayo walimtupia mshale na kuvunja mguu wake. Abu Dawuud amesema kuhusu yeye kwamba alikuwa rafidhi (jina la kuwakejeli Mashia) na alikuwa mpinzani mkubwa wa Abu Bakr na Umar. Lakini pamoja na yote haya, Ahmad (Ibn Hanbal) na Ibn Namiir walijifunza hadithi kutoka kwake na Imam Ahmad alisema: "Ingawaje Taliid ni Shia, hakuna madhara kupokea hadithi zake." Sahih al-Tirmithi ina hadithi kadhaa kutoka kwake.

**11. Thaabit ibn Diinar:**

(Kwa kawaida anajulikana kama Abu Hamzah Al-Thumaali). Hakuna shaka kwamba yeye alikuwa Shia. Tirmidhi ameandika hadithi kadhaa kutoka kwake.

[106] Wakati anamtaja Isma'il Ibn Abbad, al-Dhahbi anauwacha mwelekeo wake wa kawaida katika Miizan yake, anamuorodhesha kabla ya Isma'il ibn Aban al-Ghanawi, na Isma'il ibn Aban al-Azdi. Kwa hakika amejidhulumu mwenyewe huku akiitupa misingi yote ya haki.

**12. Thuwair ibn Abi Faakhtah:**

Alikuwa mtumwa aliyeachiliwa huru na Umm Haani, binti ya Abu Talib (dada wa Amirul-Muminin Ali). Dhahabi alimuelezea kwa maneno wazi kumuonyesha yeye kama rafidhi, alikuwa mmoja wa wafuasi waliojitolea wa Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) na hadithi zilizosimuliwa na yeye zipo kwenye kitabu cha *Sahih Tirmidhiy*.

**13. Jabir Ibn Yaziid Ibn Harith al-Jufi al-Kufi:**

Dhahabi ameandika kuhusu yeye kwenye *al-Mizani* yake kwamba: "alikuwa mmoja wa wasomi wajuzi wa Shia", na ameandika kwamba Sufyan alisema kwamba aliwahi kumsikia Jabir akisema kwamba Ilmu ya Mungu ilipitia kwa Mtume (s.a.w.w.) kwenda kwa Ali na kutoka kwa Ali kwenda kwa Hasan na kuendelea hivyo hivyo, kutoka kwa Imam mmoja kwenda kwa mwingine mpaka ikafika kwa Imam Ja'far al-Sadiq, Jabir aliishi wakati wa Imam Ja'far as-Sadiq na alijifunza hadithi nyingi kutoka kwake. Muslim amesema mwanzoni mwa Sahih yake kutoka kwa Jarrah kwamba Jabir alisema: 'Nina jumla ya hadithi elfu sabini ambazo zimenifikia mimi kupitia kwa Abu Ja'far (Yaani Imam Muhammad al-Baqir) kutoka kwa Mtukufu Mtume." Mwandishi huyu huyu amesimulia kutoka kwa Zuhayr kwamba Jabir alisema: "Ninazo hadithi elfu hamsini ambazo mimi sijasimulia chochote." Na kwamba alisimulia hadithi na kusema; "Hii ni moja katika zile hadithi elfu hamsini." Dhahabi alisema zaidi kwenye *al-Mizani* yake kwamba ilipotokea Jabir kusimulia hadithi yoyote kutoka kwa Imam Muhammad al-Baqir (a.s.), aliitambulisha kwa kusema: "Hivyo, mrithi wa warithi aliniambia." Mwandishi huyu huyu ameandika kwamba walio wengi walimkemea kwa sababu aliamini juu ya *rajat* (*Murdjiah* au *Morgiak* madhehebu ya zamani ya Kiislam, wafuasi wa itikadi ya heshima au matumaini. – Rejea *Encyclopaedia* ya Kiislam Jz. 3, uk. 734.) Halafu tena Dhahabi anasema kutoka kwa Zaa'idat kwamba Jabir alikuwa rafidhi na kila mara alikuwa akiwashutumu wapinzani wa Ali. Lakini pamoja na hayo, Nasa'i na Abu Dawuud wamechukua hadithi kutoka kwake pamoja na hizo ni hadithi inayohusu *sajda al-sahwi* kwa masahihisho ya kusahau wakati wa swala. Abu Dawuud na Tirmidhi wamemhesabu kama msimuliaji wao wa kuaminika. Shabah na Abu Awaanah na baadhi ya wenzao wa wakati huo, pia wamechukua hadithi na amesema: "kamwe sikumuona yeyote mwagalifu kuliko yeye," na Shabah amesema: "Jabir ni msimulizi wa kweli." Na pia anasema: "wakati wowote Jabir aliposimulia hadithi nilimuona kuwa ni mtu mkweli kuliko wote." Wakii anasema: 'kuna kitu kimoja ambacho sina shaka yeyote nacho, ni kwamba Jabir al-Jufi ni (Mwaminifu) wa kutegemewa." Ibn Abd al-Hakam alimsikia al-Shafii akimuambia Sufyan al- Thawri: "kama ningemtilia shaka Jabir al-Jufi nisingelitilia shaka hayo unayosema kuhusu yeye." Jabir alifariki ama mwaka wa 127 au 128 baada ya A.H. (Rehema zake Allah ziwe juu yake).

**14. Jabir ibn al-Hamiid, al-Dhabbi al-Kufi:**

Ibn Qutaybah amemuorodhesha yeye miongoni mwa Shia wajulikanao sana kwenye kitabu chake kiitwacho *Al-Ma'arif*, na Dhahabi amemwandika jina lake kwa kifupi kwa kumbukumbu kwenye kitabu chake *al-Miizan*, ambalo linathibitisha jinsi huyu mtu alivyokuwa wa kutegemewa katika fikra za waandishi wa vitabu vya *Sahih*. Aidha, Dhahabi anasema katika kumsifu: "Mwanachuo wa Ray, mkweli anayeonekana mtu muhimu sana kwa waandishi wa vitabu," na ameelezea kufanana kwa fikra juu ya uaminifu wake. Juu ya hayo, kuna hadithi kutoka kwake kwenye *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslim* ambazo amesimulia kutoka kwa al-A'mash, Mughayrah Mansuur, Isma'il ibn Abu Khalid na Abu Ishaq al-Shaybani na ambazo zinasimuliwa kutoka kwake na Qutaybah ibn Sa'id, Yahya ibn Yahya na Uthuman ibn Shaybah. Alifia Ray mnamo mwaka wa 187 A.H. akiwa na miaka 77 (Rehema zake Allah ziwe juu yake).

**15. Ja'far ibn Zayid, al-Ahmar al-Kufi:**

Abu Dawuud amemtaja yeye kwa maneno haya: "Ni mkweli na Shia." Al-Jawzjani alimweleza yeye kama "mtu anayepotoka kutoka kwenye njia," maana yake ni kwamba alipotoka kwenye njia ya al-Jawzjani na kwenda kwenye njia ya Ahlul-Bayt. Ibn Adi anasema kwamba alikuwa mtu mwadilifu na Shia." Mjukuu wake mwenyewe, Husayn ibn Ali ibn Ja'far ibn Ziyad anasema: "Babu yangu Ja'far, alikuwa miongoni mwa Shia walioheshimika huko Khurasan." Abu Ja'far al-Dawaniqi anamueleza kwamba yeye na Shia wenzake walifungwa mikanda ya mbwa iliyozunguka shingo zao na wakapelekwa kufungwa jela. Abu Uyaynah, Wakii, Abu Ghassan al-Mahdi, Yahaya ibn Bushr al-Hariri na ibn Mahdi wamesimulia hadithi ambazo walijifunza kutoka kwake, kwani alikuwa ni mwalimu na mshauri wao na ibn Mu'in na wengine wanakubali ukweli wake ambapo Ahmad ibn Hanbali anasema haya juu yake: "msimuliaji mzuri wa hadithi." Dhahab amemtaja yeye katika *Miizan* yake na alisema mambo kama hayo hapo juu kuhusu mtu huyu, na Tirmidhi na Nasa'i wameweka kifupisho cha jina lake kinachoashiria jinsi walivyomtumia kama hoja mara kwa mara. Aidha, zipo hadithi kwenye vitabu vyao viitwavyo *Sahih* kutoka kwa Bayaan ibn Bushir, Ata Ibn Saa'ib na wengine. Alifariki mwaka wa 167 A.H. (rehema za Allah juu yake).

**16. Ja'far ibn Sulaymani, al-Dha'bii al-Basri:**

Ibn Qutaybah amemuorodhesha miongoni mwa Shia maarufu sana kwenye kitabu chake *Ma'arif'* ukurasa wa 206. Ibn Sa'd (mwandishi wa *Tabaqaat*) amethibitisha kuwa kwake Shia na halikadhalika uaminifu wake. Ahmad Ibn Miqdaam amemueleza yeye kuwa ni raafidhi na Ibn Adi anasema: "Mtu huyu ni Shia; natumaini hakuna madhara kupokea kutoka kwake kwani usahihi wa hadithi zake haupingiki na kwa mawazo yangu hadithi ambazo zimesimuliwa naye zinapaswa kukubaliwa." Abu Talib anasimulia kwamba Ahmad ibn Hanbal alisema: "Hakuna ubaya kuchukua hadithi kutoka kwa Ja'far ibn Sulayman al-Dhab'ii," na hapo akaambiwa, "lakini Sulayman ibn Harb anatukataza sisi kuandika hadithi zake" yeye alijibu: "haiwezekani kuzuia hadithi zake, ingawaje Ja'far ibn Sulayman alikuwa Shia na alikuwa akisimulia hadithi kuhusu Ali (a.s.) …" Ibn Mu'in anasema: "Nilisikia kutoka kwa Abd al-Razzaq (mwanachuo mwigine mashuhuri wa hadithi) usemi ambao unahakikisha kile watu wanachosema kuhusu imani yake ya kidini (kwamba alikuwa Shia), na nilimwambia kwamba walimu wake wote walikuwa Sunni na kwamba Muammar, Ibn Jariij, al-Awza'i, Malik, Sufyan na Nu'man walitwaa madhehebu hiyo hiyo ambapo alisema hivi kuhusu hilo: 'Ja'far ibn Sulayman alikuja kwangu na nilimjua yeye kuwa ni mtu mwenye uwezo na mkarimu na nilikubali imani ya Shia kutoka kwake.' Lakini nikasema; "Muhammad ibn Abu Bakr al-Maqdami alikuwa na mawazo tofauti." Na kisha akasimulia kwa kirefu jinsi Ja'far ibn Sulayman alivyokubali imani za rafidhi kutoka kwa Abd al-Razzaq, kwa hiyo alimwita (majina) fulani wa fulani na akasema: "Nimempoteza Abd Razzaq, je, nimpoteze Ja'far pia kwa sababu ya Ushia wake?'"

Aqiili anaeleza kutoka kwa Ibn Khaduuthah kwamba huyu wa mwisho alimuambia Ja'far ibn Sulayman: "Nina taarifa kwamba unawatukana Abu Bakr na Umar." Alijibu: "Ama kwa kuwatukana, wala sifanyi hivyo, lakini hata hivyo ninawachukia, kwa vyovyote utakavyosema." Ibn Haban anasimulia kutoka kwa Jariiri ibn Yazid ibn Harun: "Nilitumwa kwa Ja'far al-Dhab'ii na nilimwambia hivi: 'Nimeambiwa kwamba unamsema Abu Bakr na Umar vibaya na alijibu: "Kuhusu kuwasema vibaya sifanyi hivyo lakini kuhusu kuwachukia, fanya utakalo;" kwa hivyo, alikuwa rafidhi na kadhalika …..."

Dhahabi amesimulia kuhusu Ja'far kwenye *Miizan* yake kama ambavyo imetamkwa awali na mwisho anahitimisha kwa kusema kwamba alikuwa miongoni mwa wasomi wakubwa na mchamungu pamoja na kwamba yeye ni Shia. Muslim amechukua kutoka kwake kwenye Sahih yake, akiwa wa kipekee katika hili, na mbali ya hizi zipo hadithi kutoka kwake kwenye kitabu cha *Sahih* ambazo zimesimuliwa na Thabit al-Binaani, Ja'd ibn Uthman, Abu Umran Al-Jawni, Yazid ibn ar-Rashk na Sa'id al-Jariiri. Aidha,

waandishi kama Qutan Ibn Nasiir, Yahya Ibn Yahya, Qutayba, Muhammad Ibn Ubayd ibn Hisab, Ibn al-Mahdi na Musadad wamesimulia kutoka kwake.

Ni yeye ambaye anasimulia kutoka kwa Yazidi al-Raskh, ambaye anasimulia kutoka kwa Matraf ambaye anasimulia kutoka kwa Imran Ibn Hasiin kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w). alipeleka jeshi chini ya ukamanda wa Ali (a.s.) na akasema: "Mnataka nini kutoka kwa Ali? Ali anatokana na mimi na mimi ninatokana naye na ni *mawla* (mtawala) wa kila muumini wa kweli baada yangu." Nasa'i ameandika hadithi hii kwenye Sahih yake na Ibn Adi ameandika kutoka kwenye kitabu hicho. Dhahabi pia ametaja hilo katika maelezo yake juu ya Ja'far kwenye *al-Mizani* yake. Ja'far ibn Sulayman alifariki mnamo mwezi wa Rajabu mwaka wa 178 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**17. Jami'i ibn Umayrah ibn Tha'labah al-Kufi al-Taymi, "Taymullah."**

Abu Haatim (Dhahabi) ameandika katika wasifu wake kuelekea mwishoni mwa kitabu cha *al-Mizan al-Itidal*: "Alikuwa msimuliaji wa hadithi mkweli na alikuwa miongoni mwa Shia walioheshimiwa" na mahali pengine kwenye kitabu hicho hicho ameelezewa kama 'rafidhi. Ala ibn Saalih, Sadaqah ibn al-Muthanna na Hakim ibn Jubayr wamesimulia hadithi kutoka kwake na alikuwa Sheikh (mwalimu) wao. Hadithi tatu zimesimuliwa kwenye vitabu vya Sunan kutoka kwake na Tirmidhi huzungumzia kwa kumthibitisha, na Dhahabi ameandika hadithi hii katika *Miizan* yake. Alikuwa mmoja wa *Tabiin* (Yaani katika kizazi kilichofuata baada ya masahaba) na alisikia hadithi kutoka kwa Ibn Umar na Aishah, na miongoni mwa hadithi ambazo anasimulia kutoka kwa Ibn Umar ni kwamba Mtukufu Mtume alimuambia Ali: "Wewe ni ndugu yangu hapa duniani na akhera."[107]

**18. Haarith ibn Hasiirah, Abu Nu'man al-Azdi al-Kufi**:

Abu Haatim al-Razi anasema kuhusu mtu huyu: "Alikuwa Shia muungwana aliyeheshimiwa." Abu Ahmad al-Zubayri anasema: "Aliamini katika *raj'ah* (marejeo)." Ibn Adi anasema: Huandikwa hadithi yake licha ya udhaifu niliouona, kwani alikuwa mmojawapo wa wale waliochomwa moto wakiwa hai huko Kufah kwa sababu ya kuwa waumini wa Shia." Dhunayji anasema; "Nilimuuliza Jariir kama aliwahi kumuona Harith ibn Hasiirah, na alijibu: 'Ndio nilimuona akiwa mzee, alikuwa ni mtu wa kukaa kimya kwa vipindi virefu na alikuwa ni mtu aliyependa kusisitiza juu ya jambo la muhimu sana…" Yahya ibn Mu'in anasema: 'Alikuwa mtu wa kuaminiwa na mwenye msimamo." Hali kadhalika, Nasa'i naye amemuona yeye kuwa ni mtu wa kuaminika na Al-Thawri, Malik ibn Mughuul, Abdullah ibn Namiir na wengine kadhaa kutoka kwenye kizazi hicho hicho wamechukua hadithi kutoka kwake, kwani alikuwa Shaykh wao na chanzo cha hadithi za kuaminika. Hadithi zake zimeandikwa kwenye *Sunnan* kutoka kwa Zayd ibn Wahab na Akramah na wasimulizi wengine wa kizazi hichohicho.

Nasa'i anasimulia kupitia kwa Ubbad ibn Ya'qub al-Rawaajini kutoka kwa Abdullah ibn Abd al-Malik al-Mas'udi kutoka kwa Harith ibn Hasiirah kutoka kwa Zayd ibn Wahab ambaye amesimulia kwamba alimsikia Ali (a.s.) akisema:

"Mimi ni mtumishi wa Mwenyezi Mungu na ni ndugu wa Mtukufu Mtume. Hakuna mwingine anayeweza kudai heshima hii isipokuwa muongo."

Harith ibn Hasirah pia amesimulia kutoka kwa Abu Dawuud al-Sabii, kutoka kwa Imran ibn Hasiin ambaye anasema: "Nilikuwa nimekaa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ali (a.s.) alikuwa ameketi karibu naye wakati ambapo Mtukufu Mtume alikariri aya ifuatayo:

[107] Maneno haya kwa ujumla yanahusishwa na Mtukufu Mtume kwamba aliyasema baada ya *Hijrah,* alitangaza 'Mkataba wa Kindugu' akimfanya kila *Muhajir* kuwa ndugu wa mmoja wa Ansar. Mwisho alipomaliza Ali alimuambia Mtukufu Mtume (saww): "Mimi hukunifanya ndugu wa yeyote." Mtume akamjibu: "Wewe ni ndugu yangu hapa duniani na Akhera."

**“Au ni nani yule anayemjibu aliyedhikika pale anapomwomba na akaiondoa dhiki? Na akawafanya ni warithi wa ardhi? Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayoyazingatia.” (27:62).**

Halafu Mtukufu Mtume alimpigapiga polepole Ali mgongoni na akasema:

“Yeyote akupendae wewe ni muumini wa kweli na yeyote akuchukiaye wewe ni mnafiki na hili litakuwa hivyo mpaka Siku ya Hukumu.”

Wasimulizi wa hadithi kadhaa akiwemo Muhammad ibn Kathiir na wengineo wameipata hadithi hii kupitia kwa Harith ibn Hasiirah na Dhahabi ametoa vyanzo katika maelezo yake ya Nafii’ ibn al-Harith na kumtaja Harith ibn Hasiirah kama “Mkweli lakini rafidh.”

**19. Harith ibn Abdullah, al-Hamadani:**

Mu’mini na mfuasi maalum wa Amirul-Mu’minin (a.s.), mwenye kutambulika na kuheshimiwa miongoni mwa Tabiin.

Imani yake kwenye Ushia haina shaka. Jina lake ni la kwanza miongoni mwa majina ya Shia yaliyotolewa na ibn Qutaybah (al-Daynuri) kwenye kitabu chake, *‘Ma’arif’* na Dhahabi kwenye kitabu chake *Miizan,* baada ya kukubali kwamba alikuwa mmoja wa Ulamaa wakubwa miongoni mwa Tabiin, ananukuu kutoka kwa ibn Haban kwamba alikuwa Shia mkereketwa kabisa, na anaendelea kusimulia mambo mengi ambayo yanakubaliwa na watu wa kawaida katika kuthibitisha juu ya jambo hili, na wakati huo huo anaonyesha kwamba alikuwa anaeleweka kama mwanasheria (faqih) aliyebobea sana na anaheshimiwa sana kwa ujuzi wake wa wajibat za kidini na kwamba hadithi zake zinaonekana katika vitabu vyote vinne vya *Sunan.*

Pia ameeleza kwamba Nasa’i ametegemea juu ya hadithi za Harith na kukubali riwaya zake na kwamba walio wengi pamoja na shutuma zao juu ya imani yake, walichukua hadithi kadhaa kutoka kwake kwenye sura kadhaa za vitabu vyao.

Kuhusu Al-Sha’bi baada ya kusema kwamba hakusema ukweli, bado pamoja na hayo alichukua hadithi kadhaa kutoka kwake, ni wazi kabisa kutoka kwenye kitabu cha *Miizan* kwamba Al-Sha’bi hakuamini maelezo fulani yahusuyo mambo mengine lakini amekubali hadithi zake za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwa ni za kweli. Anasema kwenye kitabu *Miizan* kwamba Harithi alikuwa miongoni mwa wasimulizi wajuzi wakweli; na anaendelea kusema, kutoka kwa ibn Sirin kwamba walikuwepo wanafunzi watano wa ibn Masud ambao walijifunza hadithi kutoka kwake. Ibn Sirin alisema: “Niliwaona wanne lakini sikumwona Harith kwa sababu alifariki kabla yangu, lakini alikuwa mbora mwenye uwezo kuzidi wenzake.” Anaendelea kusema: “Kuna tofauti ya mawazo kuhusu nani mweye uwezo zaidi miongoni mwa watatu, Alqamah, Masruq na Ubaydah…”

Lakini Al-Sha’bi ambaye anamuona Harith kama muongo, kwa bahati amewekewa upinzani na ibn Abd al-Birra kwenye kitabu chake “*Jami Bayan al-IIm*” na Ibrahim al-Nukhai amenukuu sehemu inayopinga mawazo ya Al-Sha’bi.

Kwenye toleo fupi la *Jami Bayan al-IIm wa Fadhilihi* kilichoandikwa na mwandishi wa zama hizi, Allamah Ahmad ibn Umar al-Mahamasani wa Beirut katika ukurasa wa 196 anamnukuu ibn Abd al-Birr kwamba Al-Nukhai alisema: “Nadhani al-Sha’bi atawajibika kwa kauli yake: ‘Riwaya hii imesimuliwa kwetu na Harith al-Hamadani ambaye ni muongo.’”[108] Halafu ibn Abd al-Birr alisema:

[108] Tazama ukurasa wa 196 tafsiri iliyofupishwa ya *al-Jami’ Baynal ‘Ilmi wa Fadh’ilih* cha Sheikh Ahmad ibn Umar al-Muhammasani al-Beiruti.

"Harith hajasema uwongo kamwe lakini Al-Sha'bi alikuwa na chuki naye kwa sababu ya Harithi kuonyesha mapenzi makubwa zaidi kupita kiasi kwa Ali, na kuhusu Ali kuwa ni mbora kuliko wengine." Anasema zaidi: "Sababu ambayo inamfanya al-Sha'bi amwuite yeye mwongo ni kwamba al-Sha'bi aliamini Abu Bakr ni mbora na kuwa alikuwa wa kwanza kuukubali Uislamu na pia aliamini Umar kuwa ni mbora..."

Ibn Sa'd katika sehemu ya 6 ya kitabu chake *Tabaqaat*, pia anamuona Harith kuwa sio mtu wa kuaminika, lakini hii ni kwa sababu ya tabia yake ya kuwavunja nguvu Shia na kutokuwafanyia haki hata katika mambo ya kisomi. Fikira hii ya ibn Sa'd imejengeka kwa Al Sha'bi katika macho ya wote ambao kwamba uongo wake ni kwa sababu tu yeye kuwa mfuasi wa Aali Muhammad na kutambua kwake nafasi yao kubwa. Kwamba waandishi wote hawa wanachuki, hilo linashuhudiwa wazi na ibn Abd al-Birr ambaye nimekwisha mnukuu. Harithi alifariki mwaka wa 65 A.H., rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

**20. Habib ibn Abu Thaabit al-Asadi al-Kaahili al-Kufi:**

Yeye ni wa kizazi cha pili cha Waislamu. Ameorodheshwa miongoni mwa Shia na waandishi wote, kwa uthibitisho wa kitabu cha *Ma'arif* cha ibn Qutaybah, *Al-Milal wa al-Nihal* cha Shahristan na *Miizan* cha Dhahabi. Kitabu cha mwisho katika kutajwa kina ufupisho wa jina lake kwani linaonekana mara nyingi kwenye vitabu viitwavyo *Sahih sita*, na anasema kwamba waandishi wote wa vitabu vya *Sahih* wameandika hadithi zake bila kusita. Anaendelea kusema: "Anashuhudiliwa na Yahya ibn Mu'in na wengine.

Al-Dawlaabi naye amemshughulikia na amemuainisha kuwa miongoni mwa wasimulizi dhaifu kwa sababu ya yeye kuwa Shia. Ibn Awn anafikira za kutisha, kwa sababu ya kushindwa kuonyesha kosa lolote kutoka kwa Habib kwa chuki amemuita 'mwenye jicho moja' ingawaje kuwa mwenye 'jicho moja' sio dosari ya uadilifu ambapo maneno ya kashfa na uovu ni dosari ya uadilifu. Lakini pamoja na haya, hadithi za Habib zimepata nafasi katika *Sahih Muslim* na *Sahih al-Bukhari.*

Kwenye *Sahih Muslim*, hadithi zake zinatoka kwa Muhammad ibn Ali ibn Abdullah ibn Abbas, Tawus, al-Dhahhak al-Mashriqi, Abu Abbas ibn al-Sha'ir, Abuu Minhaal Abd al-Rahman, 'Ata' ibn Yasaar Ibrahim ibn Sa'd ibn Abu Waqqas na Mujahid. Hadithi kutoka kwake zimesimuliwa kwenye vitabu viwili vya *Sahih* na Mus'ir, al-Thawri na Sha'bah. Kwenye *Sahih Muslim*, hadithi kutoka kwake zimesimuliwa na Sulayman al-A'mash, Hasiin Abd al-Aziz ibn Syah na Abu Ishaaq al-Shaybaani. Alifariki mwaka wa 119 A.H. rehema za Mwenyezi Mungu zimfikie.

**21. Al-Hasan ibn Hayy:**

Jina halisi la Hayy lilikuwa Saalih ibn Saalih al-Hamadani na alikuwa kaka yake Ali ibn Saalih. Wote ndugu hawa wawili walikuwa wajuzi sana wa ushawishi wa Shia. Walikuwa ni mapacha na Ali alikuwa mkubwa kwa saa moja: kwa hiyo hakuna hata mtu mmoja aliyemsikia al-Hasan akimuita kwa jina lake (kwa sababu ya kumheshimu) lakini alimwita yeye kwa jina la ubaba tu, Abu Muhammad. Hili limeandikwa na Ibn Sa'd katika maelezo yake kuhusu Ali ibn Sahil kwenye sehemu ya 6 ya kitabu cha *Tabaqaat*.

Dhahabi pia amewataja kwenye kitabu chake *Mizani*. Anasema katika maelezo yake kuhusu al-Hasan: "Alikuwa mmoja wa watu wasomi sana na alifuata uzushi wa Ushia na hakuswali swala ya Ijumaa na aliona maasi dhidi ya '*Mawalii*' kama ni jinai nzito na hakuonyesha kamwe huruma yeyote kwa Uthman."

Ibn Sa'd kwenye sehemu ya 6 ya *Tabaqaat* yake anasema: "Alikuwa msimulizi sahihi na wa kutegemewa wa hadithi nyingi, na alikuwa Shia…" na kwenye vitabu vyote ambamo ametajwa anahesabika miongoni mwa wasimulizi wa kuaminiwa na kutegemewa na miongoni mwa wanafunzi wa Maimam wa Kishia

(a.s.). Alisikia hadithi sabini kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.), lakini amesimulia ishirini tu kati ya hizo. Ameacha vitabu kadhaa ambavyo vimetufikia kupitia kwa Ulamaa wetu.

Ibn Qutaybah amemtaja yeye kama mmoja wa wasimulizi wa hadithi kwenye *Al-Ma'arif* yake, hasa akionyesha suala la kuwa yeye ni Shia na katika orodha ya Shia ambayo ipo mwishoni mwa kitabu cha *Al-Maarif* anamtaja Al-Hasan tena miongoni mwao.

Muslim na waandishi wa *Sunan* wamemtegemea yeye. *Sahih Muslim* ina hadithi kutoka kwake kama zinavyosimuliwa kutoka kwa Simak ibn Harb, Isma'il al-Sadi, Asim al-Ahwal na Haarun ibn Sa'd. Hadithi zimechukuliwa kutoka kwake na Ubaydullah ibn Musa al-Abasi, Yahya ibn Adam, Hamid ibn Abd al-Rahman al- Rawaasi, Ali ibn Jud, Ahmad ibn Yunus na wenye elimu wote na hadhi wa kizazi hicho.

Dhahabi anasema katika *Miizan* yake kwamba ibn Mu'in na wengineo wanamuona yeye kama mkweli, na Abdullah ibn Ahmad anasimulia kutoka kwa baba yake kwamba Al-Hasan ibn Hayy ni wa kutegemewa zaidi kuliko Shurayk. Dhahabi anasema zaidi ya hapo kwamba Abu Haatim alisema kwamba Ali-Hasan alikuwa mtu mkweli na alijua Qur'ani kwa moyo na alikuwa madhubuti (kwenye dini) na kwamba Abu Zar'ah alisema: "Alikusanya tabia zote za uimara, uwezo wa kisheria, ustahimilivu katika swala na uchamungu, na kwamba Nasa'i alikuwa anamwamini." Abu Nai'im anasema: "Ingawa nimeandika hadithi kutoka kwa wasimulizi mia nane (800) sijaona mtu yeyote mbora kuliko Al-Hasan, mwadilifu." Ubaydah ibn Sulayman anasema: "Naweza kuona kwamba Mungu Mwenye Enzi hatapenda kumuadhibu Hasan ibn Saalih." Na Yahya ibn Bukayr alimtaka Hasan ibn Saalih kumsimulia juu ya taratibu za kumuosha maiti, Hasan alilia sana kiasi kwamba alishindwa kuzisimulia kanuni hizo. Na Ubaydullah ibn Musa anasema: "Nilikuwa ninasoma Qur'ani Takatifu mbele ya Ali ibn Saalih na nilipofika sura ya 19 Aya ya 83, kaka yake Hasan aliguswa sana hivyo kwamba alianguka chini na kuanza kukoroma kama dume la ng'ombe lililokasirika ambapo Ali alimnyanyua na kumpangusa uso wake kwa maji na kumrashia maji mwili wote na alimsaidia ili aweze kusimama wima."

Na Waki'i anasema: "Hasan na Ali watoto wa Saalih na mama yao kila mara walikuwa na tabia ya kukesha wakati wa usiku kwa kuugawa usiku kati yao katika sehemu tatu: mama yao alipokufa, ndugu hao wawili waliugawa usiku sehemu mbili; na Ali alipokufa Hasan alikuwa na tabia ya kukesha usiku kucha kwa kuswali na kutaamuli (kutafakari kwa kina)." Abu Sulayman al-Darani anasema: "Sijawahi kuona hofu juu ya Mungu ikijionesha kwa wazi kwenye mabadiliko ya hali ya uso wa mtu yeyote kama kwenye uso wa Hasan ibn Saalih. Siku moja usiku aliposimama kusoma (Sura ya 78 ya Qur'ani Takatifu) alizama katika kuifuatilia na akaendelea kusoma bila ya kusita mpaka alfajiri yake. "Alizaliwa mwaka wa 100 A.H. na akafariki mwaka wa 169 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**22. Hakam ibn Utaybah, al-Kufi:**

Ibn Qutaybah anamuona yeye kuwa Shia na anamhesabu miongoni mwa Mashia kwenye *al-Ma'arif* yake. Bukhar na Muslim wamemtegemea yeye, na hadithi zake zinaonekana kwenye Sahih zao kutoka kwa Abu Juhayfa, Ibrahim al-Nukhai, Mujahidi na Sa'idi ibn Jubayr. Licha ya hayo kwenye *Sahih Muslim* hadithi zake zimesimuliwa kupitia kwa Abd al-Rahman ibn Abu Layla, Qasim ibn Mukhaymara, Abu Saalih Dhar ibn Abdullah, Sa'iid Abdul-Rahman ibn Abzi, Yahya ibn al-Jazzar, Nafi'i mtumwa wa Ibn Umar, 'Ata' ibn Abi Ribbah, Ammaarah ibn Umayr; Araak ibn Maalik, al-Sha'bi, Maymun ibn Mihraan, Hasan al-Arni, Mus'ab ibn Sa'd na Ali ibn al-Husayn. Na kwenye zile sahih mbili hadithi zake zimesimuliwa na Mansuur, Mus'ir na Sha'bah. Kwenye kitabu cha *Sahih al-Bukhari,* hasa zaidi hadithi

zake zimesimuliwa na Abd al-Maalik ibn Abi Ghuniyah na kwenye *Sahih Muslim* zimesimuliwa na Al-A'mash, Amr ibn Qays, Zayd ibn Abu Aniisah, Maalik ibn Mughuul, Ibaan ibn Taghlab, Hamzah al-Zayyaat, Muhammad ibn Juhaada, Matraf, na Abu Awaanah. Alifariki akiwa na umri wa miaka 65 mnamo mwaka wa 115 H.A. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**23. Hammad ibn Isa, al-Juhani: (Alikufa-maji kule Al-Juhfah.)**

Abu Ali anamtaja yeye kwenye kitabu *Muntaha al-Maqal* na kadhalika anafanya hivyo Hasan ibn Ali ibn Dawud katika wasifu fupi za maisha ya watu. Jina lake linaonekana kwenye kamusi kadhaa za wasifu na orodha za wasimulizi miongoni mwa watu wenye elimu wa Shia.

Kuna wakati alikwenda kwa Imam Abu al-Hasan Musa al-Kadhim (a.s.) na alimuomba yeye amuombee kwa Mwenyezi Mungu aweze kumpa nyumba, mke mtoto na mtumishi wa nyumbani na kwamba aweze kwenda kuhiji kila mwaka. Imam alimuombea kwa Mwenyezi Mungu amkubalie yeye mambo hayo yote na kwamba aweze kuhiji mara hamsini. Hammad alisema: "Aliponiombea niweze kuhiji mara hamsini, nikawa na uhakika kwamba nisingeweza kuishi zaidi ya hapo. Sasa, Mungu ameniwezesha kuishi muda mrefu wa kutosha kuhiji mara arobaini na nane na angalia hii ni nyumba yangu ambayo Mungu amenijaalia na nina mke nyuma ya pazia anasikiliza mazungumzo yangu, na huyu ni mwanangu na huyu ni mtumishi wangu; vyote hivi nimebarikiwa na Mwenyezi Mungu."

Miaka miwili baadae Hammad aliondoka tena kwenda kuhiji akifuatana na Abu al-Abbas al-Nawfali al-Qasir kwa hija yake ya hamsini na moja. Alipofika pale ambapo nguo ya ihram huvaliwa, alikwenda kuoga kwenye mto Juhfa na maji yalimbeba na kufa maji kabla ya kuhiji hija ya hamsini na moja. Haya yalitokea mwaka wa 209 A.H. Mwenyezi Mungu airehemu roho yake. Alizaliwa mahali paitwapo Kufah, aliishi Basrah, na aliishi zaidi ya miaka sabini. Nimefanya utafiti makini kuhusu maisha yake kwenye kitabu changu *Mukhtasar al-Kalaam fii Mu'allif al-Shi'a min Sadr al-Islam* – (Brief Discourse of Shia Authors from the Advent of Islam 119).

Dhahabi amemtaja yeye na kuanzisha kifupi cha Ta Qaf kwa jina lake, hivyo kuonyesha kuwa waandishi wa Sunan wamechukua hadithi kutoka kwake. Dhahabi anaongezea kusema kuwa alifariki maji mwaka wa 208 A.H. na kwamba anasimulia hadithi kutoka kwa Imamu Ja'far as-Sadiq na anamlaumu yeye kwa kumsingizia yeye shutuma za uwongo, kama alivyowalaumu wengine kwakuwa wao tu ni Mashia. Tabia ya Darqutni inashangaza; anamuona yeye (yaani Hammad) kuwa ni dhaifu na bado anategemeza hoja zake juu ya hadithi za Hammad katika *Sunan* yake.

**24. Himran ibn A'yun: (Kaka yake Zurarah)**

Wote wawili walikuwa Shia madhubuti, wahifadhi wa Shari'ah na bahari za ujuzi kuhusiana na mafunzo ya watu wa Nyumba ya Muhammad (a.s.). Walikuwa ni taa gizani na vigezo vya uongozi na hadithi zao zinatoka kwa Maimamu wawili wakubwa, Hadhrat Muhammad al-Baqir na Hadhrat Ja'far as-Sadiq (a.s). Wanachukua nafasi ya heshima miongoni mwa wanafunzi wa Maimamu ambao wameshuka kutoka nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

Kuhusu Himran, Dhahabi amemtaja katika *Miizan* yake na ameanzisha ufupisho wa "Qaf" kwa jina lake, na kuonyesha kwamba waandishi wa vitabu vya "*Sunan"* wamechukua hadithi kutoka kwake, na Dhahabi anasema: "Anasimulia kutoka kwa Abu Al-Fadhl na wengineo; na Hamza alikuwa akimsomea hadithi hizo; na alikuwa na ujuzi mkubwa katika elimu za Qur'ani." Lakini Ibn Mu'in anamuona yeye ni mtu wa kupuuzwa tu ambapo Abu Haatim anamweka kwenye daraja la Shaykh na Abu Dawuud anasema: "Alikuwa rafidhi, na kadhalika ….."

**25. Khalid ibn Mukhtad al-Qutwaani, (Abu'l Haytham al-Kufi)**

Ni Shaykh mshauri wa Bukhari kwenye *Sahih* yake. Ibn Sa'd amemtaja yeye kwenye sehemu ya 6 ya *Tabaqaat* yake, ukurasa wa 238 kama ifuatavyo: "Alikuwa Shia na alifariki akiwa Kufah katikati ya mwezi wa Muharram, mwaka wa 213 A.H. wakati wa utawala wa Khalifa Ma'mun. Alikuwa na ghera kupita kiasi katika ufuasi wake wa Ushia na anarejelewa kwa kifupi cha "Alif He" Abu Dawuud anasema: "Alikuwa msimulizi mkweli lakini alikuwa Shia."

Al-Jawzajaan anasema: "Alikuwa mkosoaji mkali ambaye alitangaza imani yake potovu wazi wazi."

Dhahabi pia anamtaja yeye akinukuu kutoka kwa Abu Dawuud na Al-Jawzajaan kwa fikira hizo hizo zilizotajwa hapo juu.

Bukhari na Muslim wamechukua hadith kutoka kwake ambazo zinaonekana mara kadhaa kwenye *Sahih* zao. *Sahih al-Bukhari* kina hadithi zake zilizochukuliwa kutoka kwa al-Mughira ibn Abdul-Rahman na katika Sahih Muslilm kutoka kwa Muhammad ibn Ja'far ibn Abul Kathiir, Malik bin Anas na Muhammad ibn Musa. Kuhusu hadithi zake zilizochukuliwa kutoka kwa Sulayman ibn Bilal na Ali ibn Mushir, hizi zinaonekana kwenye vitabu vyote vya *Sahih* (mfano cha Muslim na Bukhari) na Bukhari amechukua hadithi moja kwa moja kutoka kwake kwenye Sahihi yake, pia amechukua hadithi mbili kutoka kwake kupitia kwa Muhammad ibn Uthman ibn Karaamat. Muslim amechukua hadithi kutoka kwake kupitia kwa Abu Kurayb, Ahmad ibn Uthuman al-Awadi, Qasim ibn Zakariya, Abd ibn Hamid, Ibn Abu Shaybah na Muhammad ibn Abdullah ibn Namiir. Waandishi wote wa Sunan wametegemea hadithi zake wakati wanajua kwamba yeye alikuwa Shia.

**26. Dawud ibn Abu Awf, Abu Hijaab:**

Ibn Adi amemtaja ifuatavyo: "Sio mmojawapo wa wasimulizi ambao nimezitegemea hadithi zao; yeye ni Shia na hadithi zake nyingi zinazungumzia zaidi somo la ubora wa Ahlul-Bayt." Maneno yake haya ni ya kushangaza sana. Kauli hizi potofu za Nasibi (kama Ibn Adi) haziwezi kumdhuru Dawud; ambapo ma-Sufyaani wawili, Ali ibn Aabis na watu wengine wenye elimu wa kizazi hicho wamechukua hadithi kutoka kwake. Abu Dawuud na Nasa'i wametegemea hadithi zake na Ahmad ibn Hanbal na Yahya wamekubali kuaminika kwake. Nasa'i anasema: "Hakuna uovu kwake", na Abu Haatim anasema: "Hadithi zake ni nzuri." Dhahabi ametaja yeye kwenye *Miizan* yake na akasimulia mawazo yao ambayo tumekwishayaeleza. Zaidi ya hayo, kuna hadithi zake kwenye *Sunan* cha Abu Dawuud na Nasa'i kutoka kwa Abu Nazim al-Ashja'i, Akaramah na wengineo.

**27. Zubayd ibn al-Harith, ibn Abd al-Karim al-Yami al-Kufi:**

Dhahabi anamtaja kama "mmoja wa Tabiin wa kuaminika na Shia." Halafu anasimulia riwaya kwamba al-Qattan amemthibitisha mtu huyu kuwa msimulizi wa kweli na pia anasimulia riwaya zingine ambazo zinaonyesha kutegemewa kwake katika macho ya viongozi wa utafiti na mijadala ya kitheolojia.

Abu Is'haq al-Juziani, kwa tabia ya imani kali ya Nasibii anaandika fikira zake kama ifuatavyo:

"Miongoni mwa watu wa Kufah palikuwepo na kundi la watu ambao mtazamo wao wa kidini kwa ujumla haufikiriwi na watu kama wenye kufaa sifa yoyote. Walikuwa viongozi wa simulizi wa Kufah kama vile Abu Is'haq, Mansur, Zubayd al-Yaami, al-Amash na wengineo wa madhehebu hayo. Lakini wanaaminiwa kwa kuwa wakweli katika kusimulia hadithi na riwaya zao zimethibitisha ukweli wa mmoja baada ya mwingine………" Hivyo, pia anaukubali ukweli, kwani ukweli hutokea midomoni mwa waadilfu na hata waovu pia.

Na haileti madhara yoyote kwa hawa watu wenye elimu ambao wote ni wasimulizi mashuhuri wanaotambulika wa hadithi za Kiislamu kwamba Wanasibii hawafikirii mawazo yao ya kidini kuwa na hadhi ya kusifiwa eti tu kwa sababu wanafuata njia ya watu wa Nyumba ya Mtume, Lango la toba, walinzi wa ulimwengu baada ya kuondoka Mtukufu Mtume (s.a.w.w. ), Safina ya waokovu kwa taifa lake. Kwa hiyo, haileti tofauti yoyote kwenye umashuhuri wao ile hali ya kwamba Wanasibii hawaelekei kufikiria ubora wao; na hii tabia ya hawa wenye imani kali haitetereshi chochote kutoka kwenye sifa zao nzuri.

"Wakati roho bora za ukoo wangu zinafurahikiwa na mimi, waache kaumu ya waovu wasumbuke na hasira. Madhara yake nini?" Fikira hii ya al-Jawzajaan haikubeba uzito wowote wakati waandishi wa vitabu sita vya *Sahih* na wakusanyaji wa wasifu wa Mtukufu Mtume wametumia hadithi za watu hawa kwenye vitabu vyao. Hadithi za Zubayd zimewekwa kwenye *Sahih al-Bukhar* na kwenye Sahih *Muslim* kupitia kwa Abu Waa'il, al-Sha'bi, Ibrahim al-Nukha'i na Sa'd ibn Ubaydah; na hadidhi zake zilizosimuliwa kupitia kwa Mujaahid, zipo kwenye *Sahihi Bukhari.* Zile ambazo zimesimuliwa kupitia kwa Murrah al-Hamdani, Muharib ibn Dithaar, Ammaarah ibn Umayr na Ibrahim al-Taymi zipo kwenye *Sahih al-Muslim*. Sha'bah, Al-Thawri na Muhammad ibn Talha wamesimulia kutoka kwake kwenye *Sahih* za Bukhari na Muslim ambapo kwenye *Sahihi Muslim*, Zubayr ibn Muawiyah, Fudayl ibn Ghazwaan na Husayn al-Nukha'i wamesimulia kutoka kwake. Alifariki mwaka wa 124 baada ya Hijiria; rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

**28. Zayd Habaab, (Abu al-Hasan al-Kufi al-Tamimi):**

Ibn Qutaybah anamhesabu mtu huyu miongoni mwa wasimulizi wa Shia kwenye *Al-Ma'arif* yake na hata Dhahabi amefanya hivyo kwenye *Miizan* yake akimuelezea yeye wakati huo huo kama "imara katika swala, thabiti na mkweli." Pia amenukuu fikira za ibn Mu'in, Ibn al-Madini, Abu Haatim na Ahmad ambao wote wanakubali juu ya kutumainiwa na ukweli wake. Dhahabi ameendelea zaidi kunukuu kutoka kwa Ibn Adi akisema: "Alikuwa mmoja wapo wa nguzo za wasimuliaji wa hadithi wa Kufah na hakuna shaka juu ya ukweli wake."

Muslim amezikubali hadidithi zake ambazo zimeingia kwenye Sahihi Muslimu kupitia kwa Muawiyah ibn Saalih, Dahhak ibn Uthmani Qurrah ibn Khalid, Ibrahim ibn Naafi', Yahya ibn Ayyub, Sayf ibn Sulayman, Hasan ibn Waaqid, Akramah ibn Ammaar, Abd al-Aziz ibn Abu Salmah na Aflah ibn Sa'id. Ibn Abi Shaybah, Muhammad ibn Hatam, Hasan al-Halwaani, Ahmad ibn Mundhir, Ibn Namiir, Ibn Kariib, Muhammad ibn Rafi, Zubayr ibn Harb na Muhammad ibn Faraj wote wamesimulia hadithi kutoka kwake.

**29. Salim ibn Abu Ja'd, al-Ashja'i al-Kufi:**

Alikuwa kaka wa Ubayd, Ziyad, Imraan na Muslim, watoto wa Abu Ja'd ambao wote wametajwa na ibn Sa'd kwenye sehemu ya sita ya *Tabaqaat* yake. Ibn Sa'd alimuambia Muslim juu yao kama ifuatavyo: "Abu Ja'd alikuwa na watoto wa kiume sita, wawili miongoni mwao, Salim na Ubayd walikuwa Shia, wawili wengine walikuwa Murji'i,[109] na wawili walifuata fikira za Khawariji, hivyo kwamba baba yao alikuwa akisema: 'Mmefanya nini kiasi kwamba Mungu ameumba faraka kati yenu.'"

[109] Moja ya madhehebu za mwanzoni za Uislamu, ambao wanatofautiana sana na Khawarji, msingi wa imani yao uko katika aya 107, sura ya 9 ya Qur'ani Tukufu, isemayo kwamba Mwislamu hapotezi imani yake kwa kutenda dhambi. Khawarji wanashikilia kwamba mtu anakuwa kafiri kama akitenda dhambi kubwa, lakini Murji'i ambao jina lao hasa linamaanisha 'wale ambao wanangojea', wanashikilia kwamba dhambi zote, isipokuwa dhambi ya kuuacha Uislamu (*murtadi*), zitasamehewa, na kwa matokeo hayo wanafuata sera ya ukimya katika matendo yao ya kisiasa na wanaamini katika "kungojea hukumu ya Mungu" Tazama makala juu ya *al-Murdjiah, Encyclopedia of Islam*, 1932, J. 3, uk. 734-735.

Idadi ya wenye elimu wengine kadhaa wamethibitisha kwamba Salim alikuwa Shia na hata Shahristani naye amesema hivyo hivyo katika kitabu chake *Milal wa al-Nihal* sehemu ya 2 Ukurasa wa 27, sehemu ya maelezo juu ya Ibn Hazm.

Kwenye Miizan yake, Dhahabi amemuorodhesha miongoni mwa Tabiin walioaminiwa sana na amesema kwamba hadithi zake kutoka kwa Nu'man ibn Bashir na Jabir zinaonekana kwenye vile vitabu viwili vya *Sahih*.

Hadithi zake kutoka kwa Anas ibn Malik na Kurayb vilevile zinapatikana katika *Sahih* mbili hizo, ama kwa wale wote wanaofuatilia uchambuzi huu wanajua habari hii vizuri sana na kwa ukamilifu.

Dhahabi anaendelea kusema kwamba hadithi zake kutoka kwa Abdullah ibn Amr na kutoka kwa ibn Umar zinapatikana kwenye *Sahihi al-Bukhari*. Na hadithi zake kutoka kwa Umm al-Darda pia inapatikana kwenye *Sahih al-Bukhari*. Na kwenye *Sahih Muslim* zipo hadithi zake ambazo zimesimuliwa kutoka kwa Ma'daam ibn Abu Talhah na baba yake.

Hadithi zake zimeandikwa kwenye zile *Sahih* mbili maarufu kupitia kwa A'mash, Qitadah, Amr ibn Murrah, Mansur, na Hasim ibn abd al-Rahman. Pia amesimulia hadithi kutoka kwa Hadrat Ali (a.s.) ambazo Nasa'i na Abu Dawuud wameziandika kwenye *Sunan* zao. Alifariki mwaka wa 97 A.H. wakati wa utawala wa Sulayman ibn Abd al-Malik lakini wengine wanasema alifariki mwaka wa 100 au 101 baada ya Hijiria wakati wa utawala wa Umar ibn Abd al-Aziz.

**30. Salim ibn Abu Hafsah, al-Ajali al-Kufi:**

Shahristani, kwenye *Milal wa al-Nihal* yake amemuorodhesha miongoni mwa Shia; al-Fallaas anasema: "Ni msimulizi dhaifu, mwenye msimamo mkali kwenye Ushia wake;" Ibn Adi anasema: "Kosa lake ni kwamba ana ghera iliyopita kiasi mno, lakini naona hana dosari katika usimulizi wa hadithi." Muhammad ibn Bashiir al-Abdi anasema: "Nilimuona Salim ibn Abd Hafsah. Alikuwa mpumbavu na alikuwa na ndevu ndefu; loo, mfano gani wa ndevu ndefu alizokuwa nazo alikuwa akisema: "Natamani ningekuwa na Hadhrat Ali (a.s.) na nikashirikiana naye katika yote yaliyompitia." Husayn ibn Ali al-Jufi alisema: "Nilimuona Salim ibn Abu Hafsah. Alikuwa na ndevu ndefu na alikuwa mpumbavu. Alikuwa akisema: "Mimi hapa, ewe muuaji wa Nathal (msemo uliokuwa ukitumika kumwelezea Khalifa wa tatu, Uthman) nipo hapa, ewe mwangamizaji wa Bani Umayyah, nipo hapa!!" Na Umar ibn Dharra alimuambia: Ni wewe uliyemuua Uthman? Alisema: "Ndio, umefurahishwa na kuuawa kwake!" Ali ibn al-Madaini anasema: "Nilimsikia Jariir akisema kwamba alifarakana na Salim kwa sababu alikuwa adui ambaye alikuwa akipigana pamoja na Shia dhidi ya maadui wao."

Dhahabi pia ameandika juu yake yeye hayo mambo yote yaliyotajwa hapo juu, Ibn Sa'd pia ameandika juu yake kwenye ukurasa wa 234 sehemu ya sita kwenye *Tabaqaat* yake, akiongezea kwamba alikuwa na msimamo mkali wa kuzidi kiasi kuhusu imani yake ya Ushia; alikwenda Makka wakati wa utawala wa Bani Abbas na alisema: "Mimi hapa ninakuja, mimi hapa ninakuja, Oh muuaji wa Bani Umayyah." Kwa kuwa alikuwa na sauti kali, Daudi ibn Ali alimsikia na kumuuliza: "Nani huyu?" wakasema ni Salim ibn Abu Hafsah, na wakamuambia yeye juu mambo mengine kuhusu mtu huyo na fikira zake. Dhahabi anasema kwenye *Miizan* yake kwamba Salim alikuwa ni kiongozi wa kundi ambalo walimdhihaki Abu Bakr na Umar. Pamoja na yote haya, hawa wote Sufyani na Muhammad ibn Fadhil wamechukua hadithi kutoka kwake na Tirmidhi naye ameziandika hadithi zake katika *Sahih* yake na Ibn Mu'in amekubali uaminifu wake. Alifariki mwaka wa 137 A.H.

**31. Sa'd ibn Furayf, al- Iskaaf al-Hanzali al- Kufi:**

Dhahabi amemtaja mtu huyu na ametumia herufi *Tau Qaf* kama alama za ufupisho wa jina lake, na hapo kuonyesha ukweli kwamba waandishi wa Sunan wamechukua hadithi kutoka kwake. Pia amenukuu kutoka kwa Al-Fallaas kwamba, "Alikuwa dhaifu na alikuwa Shia mwenye ghera kupita kiasi." Lakini ukereketwa wake mkali wa Ushia haukumzuia Tirmidhi na wengineo kuchukua hadithi kutoka kwake. Zaidi ya hayo, hadithi zake zinapatikana kwenye *Sahih Tirmidhiy* kama ilivyosimuliwa kutoka kwa Akramah na Abu Waa'il na amepokea hadithi kutoka kwa Asbagh ibn Nabatah, Imran ibn Talhah na Umayr ibn Ma'mum ambapo Isra'il, Hiban na Abu Muawiyah wamesimulia kutoka kwake.

**32. Sa'id ibn Ashwa:**

Dhahabi amemtaja mtu huyu kwenye *Miizan* yake kama ifuatavyo: "Sa'id ibn Ashwa, *Sad, Kha, Mim*; Qadhi wa Kufah mashuhuri kwa ukweli wake."

Nasa'i anasema: "Hakuna dosari kwake na yeye ni Sa'id ibn Amr ibn Ashwa, rafiki yake Al-Sha'bi." Jawzajaan anasema: "Alikuwa mtu mwenye ghera kupita kiasi kuhusu imani yake kwa Ushia."

Lakini licha ya haya yote, Bukhari na Muslim wametegemeza hadithi zao juu yake, na hadithi zake kutoka kwa Al-Sha'bi zimethibitishwa kuwa ni sahihi kwenye zile Sahih mbili (*Sahihain*). Zakariya ibn Zaaidah na Khalid al-Hadhaa wamesimulia hadithi kutoka kwake kwenye Bukhari na Muslim. Alifariki wakati wa utawala wa Khalid ibn Abdullah (mnamo mwaka wa 89 au 96 A.H. takriban.).

**33. Sa'id ibn Khaytham, al–Hilali:**

Ibrahim ibn Abdullah ibn al-Junayd anasema: «Mtu mmoja alimuuliza Yahya ibn Mu'in, ‹kwa vile Sa'id ibn Khaytham alikuwa Shia mawazo yako ni nini kuhusu yeye?' Na akamjibu: 'Anaweza kuwa ni Shia lakini anaaminika.'"

Dhahabi anamtaja mtu huyu kwenye *Miizan* yake na amenukuu usemi ule ule wa ibn Mu'in wa hapo juu. Nasa'i na Tirmidhi wamebuni vifupisho vya jina lake, ikionyesha kwamba wamechukua hadithi kadhaa kutoka kwake na zinaonekana kwenye Sahih zao. Alisimulia hadithi kutoka kwa Yazid ibn Abi Ziyad na Muslim al-Malai na mtoto wa kaka yake Ahmad ibn Rashid amesimulia kutoka kwake.

**34. Salmah ibn al-Fadhal al-Abrash, Kadhi wa Ray (Tehrani ya sasa):**

Huyu ni msimulizi wa hadithi kutoka kwa ibn Ishaq, hadithi zinazohusu vita, ajulikanaye kwa jina la Abu Abdullah.

Ibn Mu'in anasema (kama ilivyoandikwa kwenye *al-Mizan* kuhusu Salmah): Salmah al-Abrash Raazi alikuwa Shia kama ambavyo imekwishaandikwa na hakuna dosari kwake." Abu Zar'ah anasema (kama ilivyoandikwa kwenye kitabu hicho hicho): "Watu wa Ray hawakumpenda yeye kwa sababu ya imani zake zisizofaa." Kauli hii peke yake inaonyesha jinsi watu wa Ray walivyowachukia Shia au wafuasi wa Ahlul-Bayt.

Dhahabi amemtaja kwenye *Miizan* yake na Abu Dawuud na Tirmidhi wamebuni vifupisho vya jina lake, hii inaonyesha kwamba walimwamini na kuhakikisha ukweli kwamba wamechukua hadithi kutoka kwake. Dhahabi anasema: "Alisimamisha swala na aliyejaa unyenyekevu katika imani zake; alifariki mwaka wa 191A.H. Halafu ananukuu kutoka kwa Ibn Mu'in: "Tumeandika hadihi zake na hakuna kitabu kilichokamilika zaidi kuhusu vile vita kuliko cha Salmah, na Zaniih anasema kwamba Salmah al-Abrash alimsikia ibn Is'haq akisimulia maelezo ya vita hivyo mara mbili na yeye (Salmah) aliandika hadith kuhusu vita hivyo.

**35. Salmah ibn Kahiil, ibn Hasiin ibn Kaadih ibn Asad al-Hadhrami:**

Jina lake la ukoo akiitwa Abu Yahya. Kikundi cha watu wenye elimu kutoka kwenye madhehebu ya Sunni kama vile Ibn Qutaybah kwenye kitabu chake *al-Ma'arif* (ukurasa wa 206 katika maelezo yake juu ya madhehebu) na Shahristan kwenye kitabu chake *Milal wa al-Nihal* (sehemu ya 11 ukurasa wa 27) wamemuhesabu mtu huyu miongoni mwa wasimulizi wa Kishia.

Wakusanyaji wa vitabu sita vya *Sahih* na wengine wamemtegemea. Kwenye *Bukhari*, Abu Juhayfah, Suwayd ibn Ghafla, Sha'bi, Ata ibn Abu Ribah na Jandab ibn Abdullah, na kwenye *Muslim*, Kurayb, Dharr ibn Abdullah, Bukayr ibn al-Ashaj, Zayd ibn Ka'b, Sa'idi ibn Jubayr, Mujaahid, Abd al- Rahman ibn Yazid, Abu Salmah ibn Abd al-Rahman, Muawiyah ibn Suwayd, Habib ibn Abdullah na Muslim al-Batiin. Al-Thawri na Sha'bah wamesimulia kutoka kwake kwenye vitabu hivi viwili ambapo kwenye *Bukhari*, Isma'il ibn Abu Khalid amesimulia kutoka kwake na kwenye *Muslim*, Sa'id ibn Masruq, Aqil ibn Khalid, Abd al-Malik ibn Abu Sulayman, Ali ibn Saalih, Zayd ibn Abu Aniisah, Hammad ibn Salmah na Waliid ibn Harb ni wale ambao wamesimulia kutoka kwake,. Alifariki tarehe 10 ya mwezi wa Muharram, mwaka wa 121 A.H.

**36. Sulayman ibn Surd, al-Khuzai al-Kufi:**

Mmojawapo wa Shia wakubwa kutola Iraq katika wakati wake na alikuwa kiongozi na mshauri wa Mashia. Walikuwa wakikusanyika nyumbani kwake walipokuwa wanaandika barua kwa Imam Husayn (a.s). alikuwa kiongozi wa Wenye kutubia' wale walioasi dhidi ya udhalimu wa Bani Umayya wakitaka kulipa kisasi cha damu ya Imam Husayn (a.s). Alikusanya jeshi la watu elfu nne kule Nukhayla mnamo wiki ya kwanza ya mwezi wa Rabi al-Thani, mwaka wa 65 A.H. na kusonga mbele dhidi ya Ubaydullah ibn Ziyad. Majeshi haya mawili yalikutana kwenye jangwa la Arabuni na mapigano makali yalianza hivyo kwamba wanajeshi wengi waliuawa kutoka pande zote. Sulayman alifariki kama shahidi wa dini siku hiyo mahali pajulikanapo kwa jina la Ayn al-Wardah. Yazid ibn Hasiin bi Namiir alimpiga kwa mshale ambao ulimuua na alikuwa na miaka 93 ya umri wake. Kwa hiyo kichwa cha Sulayman kilichukulia pamoja na kichwa cha Musayyab ibn Najbah mpaka kwa Khalifa Marwan ibn al-Hakam.

Ibn Sad amemtaja mtu huyu katika sehemu ya 6 ya *Tabaqaat* yake, Ibn Hajar ameandika kuhusu yeye kwenye sehemu ya kwanza ya kitabu chake cha *Isabah* na ibn Abd al-Birr ametoa maelezo yake kwenye *Istiabah* yake. Waandishi wote ambao wameandika kuhusu kipindi cha awali wamemtaja yeye na kumsifu kwa uaminifu na utii wake wa kiwango cha juu kwa Mwenyezi Mungu. Aliishi mpaka umri mkubwa na alikuwa na ushawishi na hadhi kubwa miongoni mwa watu wake. Alimuua Hawshab adui mbaya wa Amrul-Muuminin kwenye vita vya Sufin. Alikuwa anaamini kwa dhati kabisa kwamba maadui wa Ahlal-Bayt walikuwa moja kwa moja ni waasi. Wakusanyaji wengi wa hadithi wakimwamini. Amesimulia hadithi zingine moja moja kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) na hadithi zingine kupitia kwa Jubayr ibn Mut'am ambazo zote zinapatikana kwenye *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim*. Katika vitabu hivi viwili hadihti zake zimetoka kwa Abu Is'haq al-Sabi'i na Adi ibn Thabit ambapo kwenye vitabu vingine zimepatikana kupitia kwa Yahya bin Ya'mur, Abdullah ibn Yasaar na wengine.

**37. Sulayman ibn Tarkhaan, al-Taymi al-Basri:**

Alikuwa mtumwa wa Qays (aliyekuwa Imamu) mmoja wa wasimuliaji wakweli.

Ibn Qutaybah kwenye *Ma'arif* yake amemuorodhesha huyu miongoni mwa Shia. Waandishi wenye elimu wa vitabu sita vya *Sahihi* na wengineo wamemwamini. Hadithi zake zilizopo kwenye *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim* zimesimuliwa kutoka kwa Anas ibn Malik, Abu Majaaz, Bakr ibn Abdullah, Qitaadah na Abu Uthman al-Nahdi, na kutoka kwa wengine kadhaa pia kwenye *Sahih Muslim.* Kwenye

zile *Sahihain* hadithi zake zimesimuliwa na mwanae Mu'tamar na Sha'bah na al- Thawri. Kwenye *Sahih Muslim* wengineo pia wamesimulia kutoka kwake. Alifariki mwaka wa 143 A.H.

**38. Sulayman ibn Qarm ibn Ma'adh al-Dubbi al-Kufi (Abu Dawuud):**

Ametajwa na Ibn Haban kama inavyoonekana kutoka kwenye maelezo ya Sulayman katika kitabu cha *Mizan*, kama "Rafidh wa kuzidi kiwango." Lakini pamoja na hayo, Ahmad ibn Hanbal amehakikisha ukweli wake na ibn Adi amesema, kama ilivyoelezwa mwishoni mwa maandishi yake kwenye *Miizani:* "Hadithi zilizosimuliwa na Sulayman ibn Qarm ni nzuri, na yeye ni bora zaidi kuliko Sulayman ibn Irqam."

Hadithi zake zimeandikwa na Muslim, Nasa'i, Tirmidhi na Abu Dawuud kwenye vitabu vyao vya "*Sahih*". Dhahabi, akiandika kuhusu yeye katika kitabu cha "*Miizan*," anarejelea ufupisho wa jina lake uliobuniwa na waandishi wa "*Sahihi*"

*Sahihi Muslim* kina hadith iliyosmuliwa na Sulayman ibn Qarm ambaye alisikia kutoka kwa Al-A'mash ambaye alimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Mtu yupo pamoja na wale awapendao." Hadithi nyingine ipo kwenye *Sunan* kama ilivyosimuliwa na yeye kama alivyoisikia kutoka kwa Thabit ambaye alisikia kutoka kwa Anas ambaye alimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Kutafuta elimu ni wajibu wa kila Mwislamu." Na hadithi nyingine aliyoisikia kutoka kwa A'mash ambaye alisikia kutoka kwa Amri ibn Murrah ambaye alisikia kutoka kwa Abdullah ibn Harithi ambaye alisikia kutoka kwa Zuhayr ibn Aqmar ambaye alisikia kutoka kwa Abdullah ibn Amr kwamba Hakam ibn Abu al-Aas alikuwa amekaa karibu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambapo alikuwa anasimulia hadith kwa Maqurayshi ambapo Mtukufu Mtume alimlaani yeye na kizazi chake chote hadi Siku ya Hukumu."

**39. Sulayman ibn Mihran, al-Kaahili al-Kufi al-A'mash:**

Alikuwa mmoja wa viongozi wa Shia na bingwa miongoni mwa wasimulizi wa hadithi. Idadi fulani ya Sunni wenye mamlaka ya daraja la kwanza kama vile ibn Qutaybah (kwenye *Ma'arif* yake) na Shahristani (kwenye *Milal wa al- Nahil*) na wengineo wamekiri kwamba alikuwa Shia.

Hata hivyo, Jawzajaani anasema, kama ilivyoandikwa na Dhahabi kwenye *Miizan* yake katika maelezo yake juu ya Zubayd: "Kuna kundi la watu miongoni mwa wenyeji wa Kufah ambao mawazo yao ya kidini hayapendwi na watu; wao ni viongozi wa wasimulizi wa hadithi wa watu wa Kufah kama vile Abu Ishaq, Mansur, Zubayd al- Yami, A'mash na wengineo kama wao. Hata hivyo, watu wanategemea juu ya ukweli wa hadith zilizosimuliwa nao…" Nukuu hii yenyewe inatoa ushahidi kwamba mwandishi ana upungufu wa akili. Hakuna madhara kama manasibi (wale ambao wanaomkubali Muawiya kuwa alikuwa Khalifa wa haki wakati wa uhai wa Hadhrat Ali kama matokeo ya uhaini na uongo wa Amr ibn Aas wakati wa kile kilichoitwa 'upatanishi' baada ya vita vya Sufin) hawapendi mawazo ya kidini ya watu hawa ambao waliwapenda Ahl al-Bayt na waliofuata ushauri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kuzingatia **'Vitu viwili Vizito sana'** ambavyo aliviacha nyuma kwa ajili ya mwongozo wa Waislamu wote. Kwa hakika Nasibi hawawategemei Mashia hawa kwa sababu ya ukweli wa riwaya zao, lakini kwa sababu wasimulizi hawa ni muhimu sana kwao, kwani kama wangekataa hadithi zao wangepoteza karibu hadithi zote za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kama ambavyo Dhahabi amekiri kwenye kitabu chake cha *'al-Mizan*' katika maelezo ya Abban ibn Taghlib.

Inaelekea kwamba usemi wa Mughirah; "Wewe Abu Ashaq na A'mash ndio watu mliowaharibu watu wa Kufah (yaani, mmewapotosha kwenye njia ya maangamizi ya kiroho)", ni kwa sababu tu ya ukweli kwamba hawa wawili walikuwa Shia, kwa sababu katika mambo mengine wao walikuwa wabora zaidi kuliko watu wengine wa wakati wao huo katika hekima zao na kuhifadhi kwao hadithi na *Sunnah* za Mtukufu Mtume. (s.a.w.w).

Maisha ya A'mash yana visa vya ajabu ambavyo vinatoa mwanga kuhusu tabia yake nzuri sana ya kuvutia. Ibn Khalikan (mwana historia) anasimulia kwenye kitabu chake *Wafayaat al-A'ayaan* kwamba: "Khalifa Hisham ibn Abd al-Malik alimtuma mjumbe kwake akimwomba aandike baadhi ya sifa za Uthman na jambo la kumshushia hadhi Ali (a.s.). Hapo hapo A'mash aliweka barua ya Khalifa mdomoni mwa mbuzi ambaye aliitafuna na alisema huku akimgeukia mjumbe aliyetumwa: 'Mwambie kwamba hili ndio jibu langu.' Lakini mjumbe alisema: 'Ameaapa kwamba atanichinja kwa upanga kama sikumpelekea jibu', na aliwasihi marafiki na ndugu wa A'mash wasisitizie kwa A'mash mpaka atoe jibu. Kwa hivyo walipoweza kumsihi aliandika; "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mpaji kwa wingi, Mwenye Huruma. Kama wema wa wanadamu wote ungeonekana kwa Uthman na uovu wa wanadamu wote kwa Ali, hilo lisingekunufaisha hata kidogo. Bali ni juu yako wewe mwenyewe kuitathmini tabia yako. Ni hilo tu.'"

Ibn Abd al-Birr ameandika kwenye sura ya 'Kile baadhi ya wanachuoni wanachowaambia wanachuoni wengine' katika kitabu chake, *Jami Bayan al- Ilm wa Fadhlih* (angalia ukurasa wa 199 wa maandishi yaliyofupishwa na kuhaririwa na Allamah Shaykh Ahmad ibn Umar al-Mahmasaani al-Bayruti) kwamba imesimuliwa na Ali ibn Khashram kwamba alimsikia Fadhl ibn Musa akisema: "Nilikwenda na Abu Hanifah kumuona A'mash wakati alipougua na Abu Hanifah akamwambia: 'Ningekutembelea mara nyingi zaidi bali ni kwa sababu kwamba hilo linakukosesha raha.' A'mash alijibu: 'Kweli kabisa, kuwepo kwako ndani ya nyumba yako mwenyewe inatosha kunikosesha mimi furaha, hivyo unaweza kufikiria ninakosa raha kiasi gani wewe unapokuja kuniona nyumbani kwangu.' Aliporudi kutoka nyumbani kwa A'mash Abu Hanifah alisema: 'A'mash hafungi kabisa mwezi wa Ramadhani.' Aliposikia hivi ibn Khashram alimuuliza Fadhl: 'Ni kitu gani kimempotosha Abu Hanifah mpaka kusema kitu kama hicho.' Fadhl alimjibu: 'A'mash alikuwa akifunga saumu kufuatana na hadithi zilizofundishwa na Hudhayfah al-Yamani.'"

Hudhayfah na A'mash wote walifuata aya ya Qur'ani ifuatayo kwa maandishi na vitendo: **"Hivyo kuleni na kunyweni mpaka ule mkondo mweupe wa alfajiri unatoweka kutoka kwenye mkono mweusi, halafu fungeni saumu mpaka mwanzo wa usiku." (2:187)**

Wafuasi wa Hanafi huanza kufunga saumu kama dakika 16 au 20 hivi baadae kuliko Shia na pia wanafungua saumu kama dakika 15 au mapema zaidi kuliko Shia. Kwa hiyo, kwa Abu Hanifah kusema kwamba A'mash kamwe hakufunga saumu kwa sababu tu alianza kufunga saumu mapema na kuchelewa kufungua saumu inaonyesha jinsi akili yake ilivyo finyu na kutokumvumilia yeyote ambaye hakufuata fatwa yake.

Mwandishi wa (kitabu) *Al-Wajizah* na *Al-Bihar* anaandika kama ilivyosimuliwa na Hasan ibn Sa'id al-Nukhai ambaye alisikia kutoka kwa Shariik ibn Abdullah aliyekuwa Kadhi: "Nilienda kumuona A'mash wakati alipokuwa anaugua ugonjwa ambao ndio uliomuua na nilipokuwa naye alikuja ibn Shabramah, ibn Abu Layl na Abu Hanifa, na waliuliza kuhusu hali yake na aliwajibu akisema kwamba alikuwa anajisikia dhaifu sana na halafu akakumbuka dhambi zake ambazo kwazo alikuwa anamuogopa Mwenyezi Mungu na akaanza kulia. Hapo, Abu Hanifah alimsogelea na akasema: 'Muogope Mwenyezi Mungu, ewe Abu Muhammad na ujali roho yako kwani umesimulia hadithi fulani kuhusu Ali ambazo kama ungezikumbuka ingekuwa ni bora kwako.' Lakini A'mash alijibu: 'Unasema hayo kwa mtu kama mimi? Na akageukia upande mwingine na akasema mabaya dhidi ya Abu Hanifah kwa maneno ambayo hakuna haja ya kurudia hapa."

Mwenyezi Mungu Amrehemu, alikuwa, kama Dhahabi anavyomuelezea kwenye kitabu cha *Mizan*: "Ni mmojawapo wa Maimamu (katika muktadha huu Imamu maana yake ni kiongozi, kama vile Ibn Khalikan anavyoweza kuitwa Imam wa historia au Bukhari Imam wa hadithi au Razi Imam wa falsafa na kadhalika) wenye ukweli uliothibitishwa" na kama vile Ibn Khalilikan anavyoelezea katika kumuelezea A'mash kwenye kitabu cha *Wafayaat*: "Alikuwa mtu mwenye ukweli uliothibitishwa, msomi na maarufu.

Ukweli wake, uadilifu na uchamungu wake; vimekubalika kwa wote." Waandishi wa *Sahih* sita na mabingwa wengine wameamini taarifa zake katika maamuzi yao. Hadithi zake zimeandikwa kwenye *Sahih al- Bukhari* na *Sahih Muslim* kama zilivyosimuliwa na Zayd ibn Wahb, Sa'id ibn Jubayr Muslim ibn Batiin, Al-Sha'bi, Mujahid, Abu Waail, Ibrahim al-Nakhai na Abu Salh Dhakwaan. Kwa mujibu wa *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim*, hadithi zilisikiwa na kusimuliwa kutoka kwake na Sha'bah, Al-Thawri, Ibn Uyaynah, Abu Muawiyah Muhammad, Abu Awaanah, Jariir na Hafs ibn Ghiyaath. A'mash alizaliwa mwaka wa 61 A.H. na kufa mwaka wa 148 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**40. Shariik ibn Abdullah, Ibn Sinan Ibn Anas al-Nakhai al-Kufi al-Qadhi:**

Imam ibn Qutaybah amemhesabu huyu miongoni mwa Shia maarufu. Katika kitabu chake cha *Ma'arif*; Abdullah ibn Idris ameapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba Shariik alikuwa Shia (kama ilivyotajwa mwishoni mwa maelezo juu ya Shariik katika kitabu cha *Mizan*); na Abu Dawuud al-Rahawi (angalia *Mizan*) anataarifu kwamba alimsikia Shariik akisema: "Ali alikuwa mtu bora sana kuliko watu wengine, na yeyote anayekataa usemi huu ni kafiri."[110]

Sharik kwa kweli alimaanisha kusema kwamba Ali ni mtu bora sana kuliko watu wengine baada ya Mtukufu Mtume (rehema na amani juu yake na juu ya kizazi chake) kufuatana na imani ya Shia. Juwzjaan ametoa tamko (kama ilivyotamkwa kwenye *Mizan*) kwamba "alipotoka na kutoka kwenye njia" ni kweli kwamba alipotoka kutoka kwenye njia ya Jawzjaan na kuelekea kwenye njia ya Ahlul-Bayt. Shariik ni mmoja wa wasimulizi ambao kupitia kwake tumepokea hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambazo kwa uwazi kabisa zinamteua Ali kama mrithi wake, kama ilivyotamkwa kwenye *Mizan*, kwamba yeye anasimulia kutoka kwa Abu Rabi'ah al-Ayaadhi ambaye anasimulia kutoka kwa Ibn Buraydah, ambaye anasimulia kutoka kwa baba yake kwamba Mtukufu Mtume alisema: "Kwa kila Mtume pamekuwepo na mrithi na makamu; na Ali ni mrithi na makamu wangu."

Sharik alihamishwa na kwenda kuishi ugenini kwa sababu ya kueneza sifa za Ali bila kuwajali Bani Umayyah. Al-Hariir anasimulia kwenye *Durat al-Ghawas* yake, kama ilivyotamkwa kwenye maelezo ya Shariik kwenye *Wafayaat* ya Ibn Khalikana, kwamba mtu mmoja wa ukoo wa Bani Umayyah alikuwa na tabia ya kukaa na Shariik. Siku moja Shariik alisimulia sifa za Ali ibn Abu Talib (a.s) na mtu yule alisema kwa mshangao "Ni uzuri ulioje aliokuwa nao Ali." Shariik alikasirika na kusema: "Ni hayo tu unayoweza kusema juu ya Ali basi, kwamba alikuwa mtu mzuri tu?"[111]

Ibn Abu Shaybah ameangazia kwenye tukio ambalo amelisimulia mwishoni mwa maelezo yake kuhusu Shariik kwenye kitabu cha *Mizan*. Anasimulia kutoka kwa Ali ibn Hakiim kupitia kwa Ali ibn Qaadhim ambaye anasema: "Itaab na mtu mwingine walikwenda kwa Shariik na kusema, 'Watu wanasema kwamba wewe ni mtu mwenye kusitasita', ambapo alijibu, 'Wewe mjinga! Ninawezaje kusitasita? Lo, natamani tu lau ningeishi wakati wa uhai wa Ali, hivyo kwamba ningeweza kupaka mikono yangu kwa damu yao."

Yeyote ambaye anachunguza maisha ya Shariik atakubali kwamba alikuwa mpenzi wa Ahlul-Bayt na kwamba amesimulia hadithi nyingi sana, zenye elimu nyingi kutoka kwa wafuasi wa Ahlul-Bayt. Mtoto

[110] Anasema Ibn Adi: "Ilisimuliwa kwetu na Husein ibn Ali al-Sukuuni al-Kufi, ambaye alisikia kutoka kwa Muhammad ibn Hasan al-Sukuuni, ambaye alisikia kutoka kwa Saalih ibn Aswad, ambaye alisikia kutoka kwa A'mash, ambaye alisikia kutoka kwa Ubayh kwamba alimuuliza Jabir: 'Ni kwa kiasi gani unamtukuza Ali?' Na Jabir alijibu: 'Alikuwa mbora wa watu.'" Taarifa hiyo hapo juu pamoja na majina ya wasimuliaji inaelezewa na Muhammad ibn Ahmad al-Dhahabi katika maelezo ya Saalih ibn Abd al-Aswad katika *Mizan*, na licha ya mitazamo mikali ya ki-Naasibi, Dhahabi hakufanya tofauti yoyote katika msemo huu.

[111] Kumuelezea Ali tu kwamba alikuwa mtu mzuri, katika muktadha wa mjadala ambao ulikuwa unaendelea wakati huo ilikuwa kamwe sio utukuzaji. Wamekuwepo mamilioni ya watu ambao wanaweza kuelezewa kama watu "wazuri." Jambo la kuwa sifa hii ilitamkwa na adui haileti tofauti yoyote katika mtazamo wa mambo kwamba habari ambayo Shariik alikuwa anaisimulia ilistahiki kitu cha juu zaidi na cha heshima, kama vile Qur'ani inavyokumbusha wema wa Suleiman, haikusimama katika kusema tu: "Ni uzuri ulioje aliokuwa nao mtumishi huyu." Bali iliongeza: "Hakika, alikuwa mchamungu mno mwenye kufanya tawba." Haya ni maelezo ya tabia ya Shariik, ingawa hayakutolewa katika kitabu: *Wafayaat al-A'yan* cha Ibn Khallikan.

wake Abd al-Rahman anasema kama ilivyoandikwa kwenye *Miizani*; "Baba yangu anajua hadithi elfu kumi kutoka kwa Jabir al-Jufi – hadithi elfu kumi zilizo nadra," Hivyo hivyo, Abdullah ibn Mubarak anasema, kama ilivyoandikwa kwenye *Miizan*: "Miongoni mwa watu wa Kufah, Shariik alijua hadithi nyingi zaidi kuliko Sufyan. Alikuwa adui wa maadui wa Ali na aliwasema vibaya." Abd al-Salaam ibn Harb ilitokea akamuuliza yeye: "Je una ndugu ambaye huwa unamtembelea wakati anaugua?"

"Unamaanisha nani?" Shariik aliuza.

"Namaanisha 'Malik ibn Mughuul" alisema Abd al-Saalam.

Na Sharik akasema: "Si ndugu yangu kwa vile mimi ni mfuasi wa Ali na Ammar ibn Yasir." (Kama ilivyoandikwa kwenye *Miizan*).

Wakati ambapo mtu mmoja alisifu utulivu wa Muawiyah mbele yake, yeye alijibu: Mtu ambaye alipuuza haki na kupigana dhidi ya Ali hawezi kuitwa mtulivu."

Alikuwa ni Shariik ambaye alisimulia hadithi kupitia kwa Asim na Dharr kutoka kwa Abdullah ibn Mas'ud kwamba Mtukufu Mtume alisema: "Mtakapomuona Muawiyah amekaa kwenye mimbari yangu, muuweni."

Mazungumzo yalifanyika kati ya Shariik na Mus'ab ibn Abdullah al-Zubayri mbele ya Khalifa Mahd al-Abbasi (kama ilivyoandikwa kwenye kitabu: *wafayaat* cha ibn Khallikan) ambamo Mus'ab alisema: "Mnasema mambo ya kuwashushia hadhi Abu Bakr na Umar…?"

Lakini pamoja na mambo haya, Dhahabi anamuelezea kama Hafidh wa Qur'ani Takatifu, mtu mkweli na mmoja wa 'Maimam' na pia ananukuu fikira za ibn Mu'in kwamba "alikuwa mkweli na wa kuaminiwa." Dhahabi anaendelea kusema kwamba alikuwa mmoja wa wenye hifadhi kubwa ya elimu nyingi na Is'haq al-Azraq amechukua hadithi elfu tisa kutoka kwake na Dhahabi anamalizia maelezo yake kwa kusimulia kwamba Abu Tawbah al-Halabi[112] na wengineo wengi walikuwa kule Ramlah watu walipoanza kuuliza: Ni yupi mtu mashuhuri zaidi kuliko wengine katika Waislamu, na mtu mmoja akasema: "Ibn Lahiah" na wengine wakasema: "Maliki." Wengine walirejesha swali hilo kwa Isa ibn Yuunus, ambaye alitangaza: "Mtu mashuhuri kuliko wengine ni Shariik na bado angali anaishi."

Muslim na waandishi wengine wa vitabu vine vya *Sunnan* wamemtegemea Shariik. Zaidi ya hayo, hadithi zake kutoka kwa Ziyad ibn Ulaqah, Ammar al-Dhahabi, Hisham ibn Urwah, Ya'li ibn Ata, Abd al-Malik ibn Umayr, Ammarah ibn Qa'qa' na Abdullah ibn Shabramah zote zimeingizwa kwenye vitabu hivyo. Na miongoni mwa wale ambao wamesimulia kutoka kwake kwenye vitabu hivyo hapo juu ni Ibn Abu Shaybah, Ali ibn Hakiim, Yunus ibn Muhammad, Fadhl ibn Musa, Muhammad ibn Sabaah na Ali ibn Hajar. Alizaliwa kule Khurasan au Bukhara mwaka wa 95 A.H. na alifia huko Kufah mnamo Jumamosi ya kwanza ya Dhil-Qadah mwaka wa 177 au 178 A.H.

**41. Sha'bah ibn al- Hujjaaj al-Waasiti:**

Aliishi huko Basrah; jina lake la ubaba lilikuwa Abu Bastam. Alikuwa mtu wa kwanza miongoni mwa watu wa Iraq kuulizia juu ya habari za wasimulizi wa hadithi na kuacha hadithi dhaifu na zisizoaminika. Baadhi ya wasomi mashuhuri sana wa Sunni wamemhesabu yeye miongoni mwa Shia; mfano, ibn Qutaybah kwenye *Ma'arif* yake na Shahristan kwenye kitabu chake *Milal wa al-Nihal.*

Waandishi wa *Sahih Sita* miongoni mwa Sunni na waandishi wengine wamemtegemea yeye. Hadithi ambazo zimesimuliwa naye kutoka kwa Abu Is'haq al-Saabi'i, Isma'il ibn Abu Khalid, Mansur, A'mash na wengineo zimekubaliwa na Bukhari na Muslim na kama ilivyotamkwa na hawa

[112] Halabi ni jina la Aleppo, mji uliopo kasikazini ya Syria.

waandishi wawili, hadithi zake zimesimuliwa na Muhammad ibn Jaffar, Yahya ibn Sa'id al-Qattan, Uthman ibn Jabalah na wengineo. Alizaliwa mwaka wa 83A.H. na alifariki mwaka wa 160A.H. (Mwenyezi Mungu amrehemu).

**42. Sa'sa'ah ibn Sawhan, ibn Hajar ibn Haarith al-Abdi:**

Ibn Qutaybah amemhesabu yeye kwenye ukurasa wa 206 katika kitabu chake cha *Ma'arifa* miongoni Shia mashuhuri na ibn Sa'd ameandika katika *Tabaqaat* yake sehemu ya sita ukurasa wa 154 kwamba Sasa'ah "alikuwa mmoja wa watawala wa majimbo ya Kufah na alikuwa mfuasi wa Hadhrat Ali (a.s) na alipigana upande wa Ali kwenye vita vya Jamal pamoja na ndugu zake, Zayd na Sayhan, watoto wa Sawhan. Sayhan alikuwa khatwibu na pia alikuwa mbebaji bendera wa majeshi ya Hadhrat Ali kwenye vita ya Jamal,[113] na alipouawa, ndugu yake Zayd aliibeba bendera, na Zayd alipouawa Sa'sa'ah alibeba bendera." Ibn Sa'd anaendelea: "Sa'sa'ah amesimulia hadithi kutoka kwa Hadhrat Ali (a.s) na pia kutoka kwa Abdullah ibn Abbas na alikuwa ni bingwa ingawa alisimulia hadithi chache tu.

Ibn Abd al-Birr anasema katika *Isti'aab* yake: "Alisilimu wakati wa Uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) lakini kamwe hakupata wasaa wa kukutana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) kwa sababu alikuwa bado mdogo sana wakati huo. Alikuwa mmoja wa watemi wa ukoo wake ( ukoo wa Abd al-Quyas).

Msemaji fasaha, mwenye hekima, alikuwa na mtiririko mzuri wa hotuba, mwaminifu, mwenye elimu nyingi, mwenye kuheshimiwa na maneno yake yalijaa uthabiti. Baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alikuwa mmoja wa masahaba wa Ali (a.s)."

Ibn Abd al-Birr ananukuu kutoka kwa Yahya ibn Mu'in: "Sa'sa'ah, Zayd na Sayhaan watoto wa Sawhan, walikuwa mahatwibu. Zayd na Sayhan waliuawa kwenye vita vya Jamal." Halafu mwandishi huyo huyo anasimulia kwamba wakati wa utawala wa Khalifa wa pili, tatizo gumu lilijitokeza na Khalifa aliwaomba watu wamshauri, ndipo hapo Sa'sa'ah, ambaye alikuwa kwenye kilele cha ujana wake, alisimama na kutoa hotuba ambayo iligusa mambo yote na kuonyesha jawabu la sawa hivyo kwamba wote waliokuwepo walikubaliana naye na wakafuata ushauri wake. Si kutia chumvi kusema kwamba watoto wa Sawhan ambao walikuwa na vipaji na wabora, walikuwa ni fahari ya Arabuni.

Ibn Qutaybah anaandika kuhusu Banu Sawhaan katika *Ma'arif* yake kwenye sura yake juu ya watukufu na wanasiasa weledi wakutajika (angalia ukurasa wa 138): "Banu Sawhan, yaani kuwasema Zayd, Sa'sa'ah na Sayhan watoto wa Sawhan wa ukoo wa Abd al-Qays. Zayd alikuwa mtu mwema kama ambavyo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe amesema: 'Zayd ni mwema na Jandab, mtu mzuri aliyoje.' Masahaba wakasema: 'Kwa nini umewachagua hawa watu wawili tu?' Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alijibu: 'Wa mwanzo atapoteza mkono wake wakati anapigania Uislamu miaka thelathii kabla yeye mwenyewe hajaenda peponi na wa pili atapigania njia ya kupambanua kati ya wema na ubaya.'" Ibn Qutaybah anaendelea kusema: "Na kwa hiyo, Zayd alikuwepo siku ya Jalula na mkono wake ulikatwa na adui, na miaka thelathini baadaye wakati anapigana upande wa Ali (a.s.) kwenye vita vya Jamal alisema: 'Ewe Amirul Muminin, imehukumiwa kwamba nitauawa.' Amirul Muminin akauliza: 'Nani aliyekueleza hilo, Ee Abu Salman?' Zayd alijibu: 'Niliota kwamba mkono wangu (ambao niliupoteza katika vita) uliteremka kutoka mbinguni na kwa upole kabisa ukanibeba mimi.'" Kwa hiyo ikatokea kwamba aliuawa na Amr ibn Yathribi, ambaye pia alimuua kaka yake Sayhan siku hiyo ya vita vya Jamal.[114]

Ifahamike kwamba utabiri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) wenye maana kwamba mkono wa Zayd ungeutangulia mwili wote kwa kipindi cha miaka thelathini kwenda Peponi umetajwa na wanachuo wa Kiislamu wa madhehebu zote kama ni moja ya ushahidi wa madai ya Muhammad ya kumiliki

[113] Kama ilivyoelezwa na Ibn Hajar katika kitabu chake *Isabah*, alikuwa mmoja wa makamanda katika vita dhidi vya waasi na alibeba bendera ya Uislamu.

[114] Hii inaonekana kuwa ni makosa ya uchapaji. Vita vya Jamal vilitokea miaka ishirini baada ya vita vya Jalula.

mwongozo wa kiungu. Ni mojawapo ya ushahidi wa Uislamu na hoja ya kuthibitisha ukweli wake, hivyo basi kila mwandishi ambaye ameandika juu ya Zayd ameandika hadithi hii. Kwa mfano marejeo yanaweza kufanywa kwenye *Al-Isabah* mlango *fi tamiiz al-sahabah* na *Al-Isti'aab*. Wakusanyaji wa hadithi wamefuatilia usemi huu kupitia mikondo mbali mbali ambayo mmoja unauthibitisha mwingine.[115]

Hivyo basi kweli inajitokeza kwamba Zayd, pamoja na kwamba alikuwa Shia, alipewa bishara njema za Peponi na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe – sifa zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

Kuhusu Sa'sa'ah ibn Sawhan, ametajwa na Asqalani kwenye sehemu ya tatu ya kitabu chake cha *Isabah*, ambamo pameandikwa kwamba: "Alisimulia hadithi kutoka kwa Uthman na Ali; alikuwepo kwenye vita vya Sufin na Ali, alikuwa mzungumzaji fasaha, na mara kwa mara alifanya mazungumzo na Muawiyah. Sha'bi anasema kwamba alijifunza hotuba kutoka kwa Sa'sa'ah."

Is'haq al-Sabi'i pia alijifunza hadith kutoka kwake, na pia alifanya hivyo Minhaal ibn Amr, Abdullah ibn Buraydah na wengineo."[116]

Asqalani anaendelea kusema: "Al-Ula'i anasema kwenye maelezo yake kuhusu Ziyad kwamba Mughayrah alimhamishia mbali Sa'sa'ah kwa amri ya Muawiya, kwenda kwenye kisiwa au huko Bahrain au kama wasemavyo wengine, kwenye kisiwa cha Ibn Kafan na alifia huko (Mwenyezi Mungu amrehemu) kama vile sahaba mkubwa wa Mtukufu Mtume, Abu Dharr alifariki kabla yake akiwa uhamishoni huko Rabdhah" Dhahabi kwenye maelezo yake juu ya Sa'sa'ah amemuelezea yeye kuwa ni "chanzo mashuhuri" na anaendelea kuandika maoni ya ibn Sa'd na Nasa'i kuhusu kuaminika kwake. Pia ametumia kifupi cha jina la Sa'sa'ah kwa sababu ya uaminifu wake uliowekwa juu yake na Nasa'i; kwani yeyote akataaye kumwamini yeye angekataa kwa hasara yake mwenyewe na kwa hiyo hangeweza kufanya madhara yoyote kwa Sa'sa'ah; kama Qur'ani isemevyo "**Lakini wanajiumiza wenyewe."**

### 43. Tawus ibn Kiisan, al-Khawlaani al-Hamdaani:

Jina lake la ubaba ni Abu Abd al-Rahman. Mama yake alikuwa Muirani na baba yake Qaasit, ambaye alikuwa mtumwa wa Bujayr ibn Riisaan, alitokea Namriin. Waandishi wa Sunni wameamini ukweli kwamba Ushia wa wahenga wake umethibitishwa bila ya shaka yoyote. Kwa mfano, Shahristani kwenye kitabu chake cha *Milal wa al-Nahal* na Ibn Qutaybah kwenye *Ma'arif* yake wamemjumuisha yeye miongoni mwa Shia na pamoja na haya, waandishi wa *Sahih Sita* na wengineo, wamemtegemea yeye. Hadithi zilizosimuliwa na yeye kutoka kwa Ibn Abbas, Ibn Umar na Abu Hurayrah zimejumuishwa kwenye vitabu vya *Sahih*. *Sahih Muslim* inazo hadithi zilizosimuliwa na yeye kutoka kwa Aisha, Zayd ibn Thabit na Abdullah Amri. Kufuatana na Bukhari, Mujahid, Amr ibn Diinar na mtoto wake Abdullah wamesimulia hadithi alizozifundisha yeye. Bukhari ameandika hadithi zile tu ambazo zimesimuliwa kutoka kwake na Al-Zuhri, lakini Muslim anazitoa hadithi zake kutoka kwa wasomi kadhaa.

Alifariki wakati wa kuhiji kwake Makka, siku moja kabla ya Siku ya *Tarwyah* (yaani, tarehe 7 Dhil-Hijja) mnamo mwaka wa 104 au 106 H.A. Kifo chake kilikuwa tukio la huzuni kubwa; Abdullah mtoto wa Imam Hasan, alibeba maiti yake juu ya mabega yake na akawaita watu kufanya hivyo, hivyo

[115] Tazama Historia ya Ahmadi.

[116] Mtu mmoja alimuuliza Sha'bi (kama ilivyoelezwa katika *Mizan* na Dhahabi katika maelezo ya Rashid al-Hijri): "Vipi unawataja vibaya masahaba wa Ali ingawa ulikuwa mwanafunzi wao?" "Unamaanisha nani?" Sha'bi aliuliza. "Nina maana ya Harith na Sa'sa'ah" alisema. Na Sha'bi alikiri hilo, akisema: "Ama kwa Sa'sa'ah, alikuwa khatwibu, hivyo nilijifunza kuzungumza mbele ya hadhara kutoka kwake. Ama kuhusu Harith, alikuwa mwana hisabati, hivyo nilijifunza hisabati kutoka kwake."

kwamba kundi kubwa la watu walikusanyika na jeneza likaanguka kutoka mabegani mwake na joho lake likachanika.[117]

**44. Zaalim ibn Amr, ibn Sufyan Abu al- Aswad al-Du'wali:**

Ukweli wa kuwa yeye ni Shia unajulikana sana wala hapana haja ya maelezo mengi. Maelezo yafuatayo kuhusu yeye yamechukuliwa kutoka kwenye kitabu changu "*Mukhtasar al-Kalam*" ambacho kinashughulika na habari za maisha ya waandishi wa Kishia tangu wakati wa mwanzo wa Uislamu.[118]

Hakuna mtu mwenye shaka kwamba Zaalim alikuwa Shia na pamoja na haya, waandishi wa vitabu sita vya *Sahih* wamemwamini yeye. Hadithi zilizosimuliwa na yeye kutoka kwa Khalifa Umar ibn al-Khattab zipo katika *Sahih al-Bukhari* na kutoka kwa Abu Musa na Imran ibn Hasin kwenye *Sahih Muslim*. Hadithi zimesimuliwa kutoka kwake na Yahya ibn Yamur kwenye vitabu vyote viwili, kwenye Bukhari peke yake zimesimuliwa na Abdullah ibn Buraydah na kwenye *Sahih Muslim* peke yake zimesimuliwa na Abu Harb. Alifia Basrah mwaka wa 99 A.H. wakati wa ugonjwa wa tauni akiwa na umri wa miaka 85 (Mwenyezi Mungu amrehemu). Ndiye mtu ambaye alitengeneza mfumo wa nahau ya Kiarabu kwa kufuata kanuni alizojifunza kutoka kwa Amirul-Muminin Ali (a.s) kama ilivyoelezewa kwa kirefu kwenye marejeo ya kitabu changu kilichotajwa hapo juu.

**45. Aamir ibn Waailah, ibn Abdullah ibn Amr al-Laythi al-Makki: (Aliyejulikana kama Abu Tufayl).**

Alizaliwa mnamo mwaka wa vita vya Uhud (3 A.H.) na aliishi miaka minane wakati ule ule wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w). Ibn Qutaybah, kwenye *Ma'arif* yake amemjumuisha yeye miongoni mwa wenye raghba na rafidhi wa mwanzo kabisa na anasema kwamba alikuwa mbebaji bendera wa Mukhtar ibn Abu Ubaydah al-Thaqafi na alikuwa Sahaba wa mwisho kuondoka hapa duniani.

Ibn Abd al-Bir pia amemtaja kwenye kitabu chake kiitwacho *Isabah* mlango wa "*Kunniyat*" kwamba alifika Kufa na alidumu kuwa na Hadhrat Ali (a.s.) kwenye mikutano yote ya hadhara, na Hadhrat Ali alipouawa alirudi Makka. Mwandishi huyo huyo anaendelea: "Na alikuwa na uwezo na hekima na alikuwa bora katika kutoa majibu ya akili, mwenye ufasaha wa maneno na alikuwa Shia wa Ali (a.s)." Anasema zaidi: "Siku moja Abu Tufayl alikwenda kwa Muawiya ambaye alimuuliza, "Una mawazo gani kuhusu rafiki yako Abu al-Hasan (yaani; Hadharat Ali)? Alijibu: "Sawa sawa na hisia za mama yake Musa kuhusu mwanawe Musa na hata hivyo, lazima nilalamike kwa Mwenyezi Mungu kuhusu mapungufu yangu." Halafu Muawiyah alimuuliza. "Wewe ulikuwa mmoja wa wale ambao walizingira maskani ya Uthman?" "Hapana," yeye alijibu. "Nilikuwa mmoja wao wa wale waliokuwepo pamoja naye." 'Kitu gani basi kilikuzuia usimsaidie?' Aamir akamjibu kwa ukali: 'Nini kilichokuzuia wewe usimsaidie na nini kilikufanya wewe uwe na mashaka kuhusu yeye ingawa watu wa Syria wote walikuwa chini ya uongozi wako?' Muawiyah akasema: 'Huoni kwamba sasa ninatafuta kulipa kisasi kwa sababu ya kuuawa kwake na kuwa upande wake?' Na Aamir akasema: 'Unakuwa kama mtu yule ambaye kuhusu yeye kaka yake Juf aliimba:

'Ni huruma iliyoje kwamba baada ya kifo changu ananililia mimi,

ambaye wakati wa uhai wangu hakunipa chochote!'"

Zuhri, Abu Zubayr, Jariiri, Ibn Abu Hasiin, Abd al-Malik ibn Abjar, Qitaadah, Ma'ruuf, Wahiid ibn Jami'i, Mansur ibn Hayyaan, Qaasim ibn Abu Bardah, Amir ibn Diinar, Akramah ibn Khalid, Kulthuum

117 Kama ilivyoripotiwa na Ibn Khallikan katika maelezo ya Tawus katika kitabu chake *Wafayaat al-A'yan*.

118 Rejea za kuunga mkono maelezo hayo zinaweza kupatikana kwenye maelezo ya Ibn Hajar kuhusu yeye katika *Isabah*, sehemu ya 3, Jz. 1, uk. 241.

ibn Habib, Furaat al-Qazzaaz na Abd al-Aziz ibn Rafi'I, wote wamesimulia hadithi kutoka kwake. Hadithi zake zilizosimuliwa na watu hawa wote zinapatikana kwenye *Sahih Muslim*. Abu Tufayl (Aamir) amesimulia hadithi kwenye *Sahih Muslim* kuhusu Hijja na mwenendo wa Mtukufu Mtume na pia kuhusu swala na ushahidi wa Utume wa Muhammad (s.a.w.w) kutoka kwa Ma'adh ibn Jabal, na hadithi kuhusu uwepo wa Mungu kutoka kwa Abdullah ibn Mas'ud. Kwa mujibu wa vyanzo vyote hivyo alijifunza na kusimulia hadithi kutoka kwa Ali, Hudhayfah ibn Usayd, Hudhayfah ibn Yaman. Abdullah ibn Abbas na Umar ibn al-Khattab kama ilivyotamkwa na Muslim na wafasiri kuhusu wasimulizi wa hadithi zilizopo kwenye Sahih yake. Abu Tufayl alifia Makka mwaka wa 100 A.H., Mwenyezi Mungu amrehemu. Kuna taarifa tofauti kuhusu tarehe ya kufa kwake, ambapo inasemekana kifo chake kilitokea mwaka wa 102 A.H. 107 A.H. au 110 A.H., na kufuatana na taarifa ya ibn Qaysarani, ni mwishoni mwa mwaka wa 120 A.H.

**46. Ubbad ibn Yaq'uub, al-Asadi al-Rawaajani al-Kufi:**

Darqutni ameandika kuhusu yeye: "Ubbad ibn Yaq'uub alikuwa Shia na mtu mkweli." Na Ibn Haban ameandika: "Ubbad ibn Yaq'uub alikuwa na tabia ya kuwalingania watu kufuata imani ya rafidhi." Ibn Khuzaymah anasema: "Imeripotiwa kwa chanzo kihusikacho na mtu ambaye analaumiwa kwa sababu ya Imani yake ya kidini, yaani Ubbad ibn Yaq'uub (kama ilivyosimuliwa na Fadhal ibn Qaasim, kutoka kwa Sufyani al-Thawri, kutoka kwa Zubayd, kutoka kwa Murrah, kutoka kwa ibn Mas'ud) kwamba alikuwa na tabia ya kusoma Aya ya 25 ya Sura ya 33 ya Qur'ani ifuatavyo: **Mwenyezi Mungu anatosha kwa waaminio wanapokuwa vitani (kwa kumsaidia Ali.)**" "Ubbad amesimulia kutoka kwa Shariik, kutoka kwa Asim, kutoka kwa Dhar, kutoka kwa Abdullah kwamba Mtukufu Mtume alisema: "Ukimuona Muawiyah kwenye mimbari yangu, muuweni." Hadithi hii imesimuliwa na mwanahistoria Tabari na wengineo pia.

Ubbad alikuwa na tabia ya kusema: "Yeyote yule anayeshindwa kujitenga na maadui wa Aali Muhammad katika swala zake za kila siku atakuwa na maadui Siku ya Ufufuo," na kwamba, "Uadilifu wa Mwenyezi Mungu hauwezi kuwaruhusu Talhah na Zubayr kuingia Peponi, kwa kuwa walipigana na Ali baada ya kula kiapo cha kumtii yeye."

Saalih Jazrah anasema kwamba: "Ubbad ibn Yaq'uub alikuwa na tabia ya kumshutumu Uthman, na Ibadaan al-Ahwaazi anasema kwa uhakika kwamba Ubbad ibn Yaq'uub alikuwa na tabia ya kuwashutumu watu fulani kutoka miongoni mwa watu waliotangulia."

Bado, licha ya ukweli wote huu, wa mbele kabisa katika vyanzo vya Sunni kama Bukhari, Tirmidhi, Ibn Majah, Ibn Khuzayman na Ibn Abu Dawuud, wamekubali hadithi zake na wanamkubali kama Sheikh (mwalimu) wao na mhakiki wa hadithi zao. Abu Haatim, licha ya upinzani wake, anakubali kwamba alikuwa chanzo cha kuaminika. Dhahabi anatoa maoni kwenye *Miizan* yake juu ya Ubbad kwamba" "Alikuwa mmoja wa Mashia wenye ghera na kiongozi wa wazushi, lakini alikuwa mkweli katika kusimulia hadithi," halafu anaendelea kuandika mambo ambayo yamekwishatajwa hapo juu. Bukhari ameandika kwenye Sahih yake hadithi zihusuzo Umoja wa Mungu moja kwa moja kutoka kwake. Alifariki mwezi wa Shawwal mwaka wa 250 A.H. (Mwenyezi Mungu amrehemu). Maelezo ya Qaasim ibn Zakariya al-Mutarriz juu ya Ubbad kuchimba bahari na maji kutiririka kutoka humo ni mambo ya kutunga. Mwenyezi Mungu atulinde kutokana na upotovu wa wabunifu wa uwongo.

**47. Abdullah ibn Dawuud, (Anayejulikana kama Abu Abd al-Rahman al-Hamdani al-Kufi).**

Aliishi Harbiyah mjini Basrah. Ibn Qutaybah amemjumlisha kwenye *Ma'arif* yake miongoni mwa Mashia na Bukhari amemtegemea katika *Sahihi* yake, hadithi zake kutoka kwa A'mash, Hisham

ibn Urwah, na ibn Jariih pia zinapatikana katika *Sahih*. Na Musaddad, Amri ibn Ali na Nasr ibn Ali wamesimulia hadithi kutoka kwake ambazo zimeandikwa sehemu mbali mbali kwenye *Sahih al-Bukhar*i. Alifariki mwaka wa 212 A.H.

**48. Abdullah ibn Shaddaad ibn al-Haad:**

Aliitwa jina la Usamah ibn Amr ibn Abdullah ibn Jabir ibn Bishr ibn Atwaarah ibn Amr ibn Maalik ibn Layth; - al-Laythi, al-Kufi Abu al-Waliid na alikuwa sahaba wa Amir al-Muminin Ali (a.s).

Mama yake alikuwa Salma binti Umays al-Khath'amiyah, dada wa Asma ibn Umays. Kwa hiyo alikuwa binamu ya Abdullah ibn Ja'far na Muhammad ibn Abu Bakr na kaka wa Ammarah, binti wa Hadhrat Hamzah ibn Abdul-Muttalib kutoka upande wa mama.

Ibn Sa'd amemtaja yeye kuwa miongoni mwa mafaqih na wanachuoni wa kizazi cha pili kutoka kwa Masahaba waliokwenda Kufah, na anaeleza mwishoni mwa maelezo yake katika *Tabaqaat* yake, sehemu ya 6 ukurasa wa 86: "Aliungana na waasi pamoja na wasomaji wenzake wengine wa Qur'ani dhidi ya Hajjaj wakati wa Abd al-Rahman ibn Muhammad ibn Ash'ath na aliuawa katika vita vya Dujayl." Kwenye maelezo hayo hayo imeelezewa: "Alikuwa chanzo, mwanasheria, msimuliaji mwenye msukumo wa hadithi na alikuwa na mwelekeo wa Ushia. Vita vya Dujayl vilitokea mwaka wa 81 A.H. Waandishi wote wa vitabu vya *Sahih* na wanasheria wote mashuhuri wa Sunni walitegemea juu ya Abdullah ibn Shaddaad. Abu Ishaq al-Shaybani, Ma'bad ibn Khalid na Sa'd ibn Ibrahim wamesimulia hadihi kutoka kwa Abdullah ibn Shaddaad kama zilivyoandikwa kwenye vitabu vya *Sahih al-Bukhari, Sahih Muslim* na vitabu vingine vyenye marejeo, na kwa mujibu wa Bukhari na Muslim huyu alijifunza hadithi kutoka kwa Ali (a.s.), Maymunah na Aisha.

**49. Abdullah ibn Umar ibn Muhammad ibn Ibaan ibn Saalih ibn Umayr al-Qarashi al-Kufi. (Vilevile alijulikana kama Mishkadaanah)**

Alikuwa mwalimu wa Muslim, Abu Dawuud na al-Baghawi na waandishi wengine wengi wa kizazi chao walipata elimu yao ya hadithi kutoka kwake. Abu Haatim anamuelezea kwamba "alikuwa mkweli." Na imeandikwa kutokana na maelezo yake mwenyewe kwamba alikuwa Shia. Saalih ibn Muhammad ibn Jazrah ameandika kwamba; "alikuwa Shia ngangari," na pamoja na hayo, Abdullah ibn Ahmad anashikilia kwenye msingi wa maelezo ya baba yake kwamba Mishkdaanah alikuwa "chanzo cha kuaminika," Dhahabi anasema kwenye *Miizan* yake kwamba alikuwa "mkweli na msimuliaji wa hadithi." Alijifunza kutoka kwa ibn Mubaraka, Daraawardi na wengine., na akamfundisha Muslim, Abu Dawuud na al-Baghawi. Muslim na Abu Dawuud wamebuni ufupisho wa jina lake kwa sababu ya utumiaji wao wa mara kwa mara wa marejeo ya hadithi zake, na Muslim pia ameandika mawazo ya wasomi kuhusiana na yeye, na kusema kwamba alifariki mwaka wa 239 A.H. Mbali na haya, hadithi ambazo amezisimulia yeye kutoka kwa Abdah ibn Sulayman, Abdullah ibn Mubarak, Abd al-Rahman ibn Sulayman, Ali ibn Hashim, Abu al-Ahwas, Husayn ibn Ali al-Jufi na Muhamamd ibn Fudhayl zinapatikana kwenye *Sahih Muslim* ambamo hadithi zake zimesimuliwa moja kwa moja. Abu al-Abbas al-Siraaj anasema kwamba Mishkdanah alifariki mwaka wa 237 au 238 A.H.

**50. Abdullah ibn Lahii'ah ibn Aqbah al-Hadhrami:** (Alikuwa Kadhi na mwanachuoni wa Misri)

Ibn Qutaybah amemuorodhesha kwenye kitabu cha Ma'arif kama miongoni mwa Shia wafaao, na ibn Adi anasema kwenye kitabu *Miizan* kwamba "alikuwa Shia mwenye ghera sana." Abu Ya'li anasimulia kutoka kwa Kamil ibn Talhat ambaye anasimulia kutoka kwa ibn Lahii'ah ambaye anasimulia kutoka kwa Hayy ibn Abdullah ibn al-Maghaafiri ambaye anasimulia kutoka kwa Abu Abdur-Rahman al-Habli ambaye anasimulia kutoka kwa Abdullah ibn Amru kwamba Mtume (s.a.w.w) alisema wakati wa maradhi yake ya mwisho: "Mwambieni ndugu yangu aje kwangu," na masahaba walimuita Abu Bakr lakini Mtukufu

Mtume aligeuzia uso wake upande mwingine, halafu wakamwita Uthman na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) tena alifanya hivyo hivyo na kurudia tena kusema, "Muiteni ndugu yangu aje kwangu." Halafu walimuita Ali, ambapo Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimwambia akae karibu naye na kumfunika kwa blanketi yake na kuinamia upande wake kwa muda. Baadaye Ali alipotoka ndani ya blanketi lile masahaba walimuuliza kile ambacho Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema na Ali alijibu: "Amenifundisha milango elfu moja na kwa kila mmoja wa mlango huo ulifunua milango mingine elfu moja."

Dhahabi pia amemtaja Abu Lahii'ah kwenye *Miizan* yake na ameanzisha ufupisho wa "Dal Ta Qaf" kwa jina lake, kuonyesha waandishi wa *Sunan* ambao wamechukua hadithi kutoka kwake. Hadithi zake zinapatikana kwenye *Tirmidhi* na *Abu Dawuud* na *Musnad* zote za Sunnah. Ibn Khallikan pia amemtaja kwenye kitabu chake, *Wafayaat* na amempa hadhi ya ufasaha katika kumsifia kwake.

Kwenye *Sahih Muslim* hadithi zake zimechukuliwa kupitia kwa Ibn Wahb na pia kuna hadithi yake kuhusu Swala kwenye kitabu hicho hicho kupitia kwa Yazid ibn Habib. Ibn al-Qaysarani anamtaja yeye kwenye kitabu chake kiitwacho "Uthibitisho wa Vitabu na Abu Nasr al-Kalabadhi na Abu Bakr al-Isbahaani" kama msimulizi mmojawapo wa Bukhari pia Muslim. Ibn Lahii'ah alifariki siku ya Jumapili katikati ya mwezi wa Rabi al-Akhir, mwaka wa 174 A.H.

**51. Abdullah ibn Maymuun, al-Qaddah al-Makki:**

Alikuwa sahaba wa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s). Tirmidhi ametegemea juu yake na Dhahabi amemtaja na kubuni ufupisho wa jina lake ikionyesha kwamba amechukua hadithi kutoka kwa Abdullah ibn Maymuun. Dhahabi pia anasema kwamba alisimulia hadithi zilizopokelewa kutoka kwa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s) na Talhah ibn Amir.

**52. Abd al-Rahman ibn Saalih al-Azdi:** (Akijulikana pia kama Abu Muhammad al-Kufi.)

Sahaba na mwanafunzi wake, Abbas al-Dawri ameandika kuhusu yeye kwamba "alikuwa Shia". Ibn Adi anasema: "Alikuwa na ghera kubwa juu ya Ushia." Saalih Jazrah anasema: "Alikuwa akimlaumu Uthman;" na Abu Dawuud anasema kwamba "aliandika kitabu kuhusu kasoro za Masahaba na alikuwa mtu mwovu." Lakini pamoja na haya, Abbas al-Dawri na Imam al-Baghawi wamesimulia hadithi kutoka kwake na Nasa'i pia amechukua hadithi kutoka kwake. Dhahabi amemtaja yeye kwenye *Miizan* yake na Nasa'i amebuni ufupisho wa jina lake kuthibitisha kuaminika kwake na amenukuu baadhi ya mambo yaliyotajwa hapo juu kutoka kwa Maimamu wa Sunni kuhusu yeye na pia amesema kwamba ibn Mu'in amethibitisha kuhusu ukweli wake na kwamba alifariki mwaka wa 235 AH. Hadithi zake kama zilizopokelewa kutoka kwa Shariik na wenzake wengine wa rika lake zinapatikana kwenye vitabu vya *Sunan*.

**53. Abd al-Razzaq ibn Hamam, ibn Naafi al-Hamiiri al-Sana'ani:**

Alikuwamo kwenye kundi miongoni mwa wasomi wa Kishia na alikuwa mmojawapo wa watu waadilifu wa vizazi vya siku za nyuma. Ibn Qutaybah kwenye *Ma'arif* yake amemhesabu yeye miongoni mwa Shia na Ibn Athir kwenye kitabu chake cha *Tarikh al-Kamil* (sehemu ya 6 ukurasa wa 137) ameandika kifo chake miongoni mwa matukio yaliyotokea mwishoni mwa mwaka wa 211 A.H. akisema: "Mwaka huo Abd al-Razzaq ibn Hamam al-Sana'ani alifariki. Alikuwa *muhaddith* na mwalimu wa Ahmad ibn Hanbal na alikuwa Shia. Al-Muttaqi wa India pia amemtaja katika mazungumzo yake ya hadithi Namba 5994 kwenye kitabu chake cha '*Kanz'* yake na amehakikisha ukweli kwamba alikuwa Shia.[119]

Dhahabi anasema kwenye *Miizan* yake kwamba alikuwa "mmoja wa vyanzo na mtu mwenye elimu kubwa. Aliandika vitabu vingi, na alikuwa mwandishi wa kitabu cha *Jami al-Kabir*, ambacho ni nyumba

[119] Tazama *Kanz*, sehemu ya 6, uk.391.

ya hazina ya elimu, na watu walikuwa wakija kutoka mbali na karibu ili kujifunza kwake; kwa mfano, Ahmad, Is'haq, Yahya, Al-Dhahali, Al-Ramaadi na Abd wote walikwenda kwake." Baada ya kushughulika na (wasifu) maisha yake, Dhahabi anataja maoni ya Abbas ibn Abd al-Athim akikana usahihi wake na kumpinga kwake akisema: "Haya ni maoni ya Abbas lakini ukweli ni kwamba *hufadh* wote (wale ambao wamehifadhi Hadithi) na viongozi wa *Ulama* (wanachuoni) kwa pamoja wanakubaliana juu ya ukweli wake." Dhahabi anaendelea kueleza kutoka kwa Tayaalisi, ambaye anasema: "Nimesikia kutoka kwa ibn Mu'in, ambaye alimsikia Abd al-Razzaq akisema mambo fulani ambayo yanathibitisha ukweli kwamba yeye alikuwa Shia. Hivyo nilimuuliza kwamba ikiwa walimu wake wote walikuwa Sunni kama vile Mu'ammar, Malik, Ibn Jurayh, Sufyan na al-Awza'ai, vipi yeye alipata kuingia kwenye Ushia?" Alijibu: 'Ja'far ibn Sulayman al-Dhahba'i alikuja kwangu na nilimuona ni mtu aliyefuzu kwa mwongozo mzuri na mwenye kuridhisha, hivyo nilikubali imani hii kwa ushawishi wake." Kama hii ni kweli, ni kukubali kwa upande wa Abd al-Razzaq kwamba alikuwa Shia, na anazidi kuonyesha kwamba aliingizwa kwenye Ushia na Ja'far al-Dhahba'i, lakini Muhammad ibn Abu Bakr al-Maqdami anasema kwamba alikuwa ni Abd al-Razzaq ambaye alimwingiza Ja'far al-Dhahba'i kwenye Ushia na anamlaani Abd al-Razzaq kwa hilo, akisema kwenye *Miizan* yake: "Abd al-Razzaq na aangamie kwa sababu alimpotosha Ja'far (yaani alimwingiza kwenye Ushia)…….." Ibn Mu'in hata hivyo mara kwa mara ametegemea juu ya hadithi zilizosimuliwa na Abd al-Razzaq ambapo wakati huo huo anakubali kwamba alikuwa Shia kama ilivyoelezewa hapo juu.

Ahmad ibn Abu Khaythamah anasema:[120] "Mtu mmoja alimwambia ibn Mu'in kwamba Ahmad ana mawazo kwamba Ubaydullah ibn Musa aliziacha hadithi za Abd al-Razzaq kwa maelezo kwamba yeye alikuwa ni Shia na ibn Mu'in alijibu: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu Mmoja wa kweli kwamba Abd al-Razzaq ni mzuri mara mia moja kuliko Ubaydullah na nimesikia mara nyingi hadithi nyingi zaidi kutoka kwa Abd al-Razzaq kuliko kutoka kwa Ubaydullah."

Abi Saalih Muhammad ibn Isma'il al-Dharaari anasema: [121] "Tulipokuwa San'a (Yemen), tulikuja kufahamu kwamba Ahmad na ibn Mu'in na wengine wanazikataa au hawaziamini hadithi zilizosimuliwa na Abd al-Razzaq kwa sababu yeye ni Shia, na tulisikitika sana kusikia hilo. Hivyo tulijitayarisha kwa safari ya kwenda Makka na msafara wa mahujaji na huko tulikwenda kukutana na Yahya na nilimuuliza naye alijibu: "Ee Abu Saalih, hata kama Abd al-Razzaq angekuwa ameritadi kutoka kwenye Uislamu sitazikataa hadithi zake."[122]

Hii inaonyesha msimamo wa ustahimilivu wa waandishi wa zamani wa Kiislamu juu ya wengine, katika habari za kihistoria zinavyoweza kukubaliwa au kukataliwa bila kujali imani ya kidini ya msimuliaji. Msimuliaji hawi mwongo kwa sababu ya kufuata tapo tofauti la kanuni za kidini. Ibn Adi anasema: "Abd al-

[120] Tazama maelezo ya Abd al-Razzaq katika *Mizan*.

[121] Ibid

[122] Kinyume chake, wale ambao ni waadilifu na wasio na upendeleo wanakubali hadithi zake hizi, na zimejumuishwa katika vitabu vya Sahih kwa ukamilifu wa kuridhisha. Ni Ma-Nasibi na Ma-Khawariji tu ambao wanazichukia hadithi hizi. Miongoni mwa hadithi ni ile iliyosimuliwa na kutoka kwa Ahmad ibn Azhar na kwa kauli moja inakubaliwa: "Abd al-Razzaq alinisimulia faraghani mbali na walinzi kwamba Mu'ammar alimuambia kwamba alisikia kutoka kwa Zahri kwamba alisikia kutoka kwa Ubaydullah kwamba alisikia kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtume Muhammad (s.a.w.w) alimuangalia Ali (a.s) na akasema: 'Wewe ni kiongozi katika ulimwengu huu na kesho Akhera; yeyote anayekupenda wewe ananipenda mimi, na yeyote anayekuchukia wewe ananichukia mimi; rafiki yako ni rafiki wa Allah na adui yako ni adui wa Allah; na ole juu ya yule anayekuchukia.'" Hakim ameiandika hadithi hii katika kitabu chake, *Mustadrak*, sehemu. 3, uk. 128, pamoja na ufafanuzi: "Ni hadithi sahihi kwa mujibu wa masharti ya masheikh wawili (Bukharin a Muslim)." Hadithi nyingine kama ilivyosimuliwa na Abd al-Razzaq, ambaye alisikia kutoka kwa Mu'ammar, ambaye alisikia kutoka kwa Ibn Najiih, ambaye aliisikia kutoka kwa Mujahid, ambaye aliisikia lutoka kwa Ibn Abbas kwamba Hadharat Fatimah (a.s) alisema: "Ewe Mjumbe wa Allah umeniozesha kwa mtu ambaye hana mali", Mtume alijibu: "Je, huridhiki na ukweli kwamba Allah ameangalia watu wote katika ardhi na akachagua wawili kati yao – mmoja kuwa baba yako na mwingine kuwa mume wako?" Hadithi hii imeandikwa na Haakim katika kitabu *Mustadrak*, sehemu. 3, uk. 129, kwa chanzo cha Sarih ibn Yunus, kutoka kwa Abu Hafs, kutoka kwa A'mash, kutoka kwa Abu Saalih, kutoka kwa Abu Hurayrah kama msimuliaji wa juu zaidi.

Razzaq amesimulia hadithi fulani zinazohusu ubora wa Ali (a.s) ambazo hazikubaliwi na yeyote, na baadhi ya hadithi zingine zimetupwa kwa kisingizio kwamba zinaleta chuki,[123] na wamemlaumu yeye kwa fedheha ya kuwa Shia." Lakini pamoja na haya, wakati Ahmad ibn Hanbal alipoulizwa kama alikuwa anamjua msimuliaji wa hadithi mzuri kuliko Abd al-Raqqaz, alisema "Hapana." Ibn al-Qaysarani anasema mwishoni mwa maelezo yake kuhusu Abd al-Razzaq, kwenye kitabu chake cha *Al-Jam Baina al-Rijjaal al-Sahihayn,* kwa *sanad* (nyororo) ambayo inakwenda mpaka kwa Imam Ahmad ibn Hanbal, "inapotokea kwamba kuna tofauti ya mawazo kuhusu hadithi kutoka kwa Muammar" ambayo msimuliaji ni Abd al-Razzaq …...

Mukhallad al-Sha'iri anasema: "Nilikuwa na Abd al-Razzaq siku moja ambapo mtu mmoja alimtaja Muawiyah, na Abd al-Razzaq akasema: Usituchafulie baraza letu kwa kumtaja mtoto wa Abu Sufyan." Zayd ibn Mubarak anasema: "Tulikuwa tumekaa na Abd al-Razzaq na alikuwa anasimulia hadithi kutoka kwa ibn al-Hadthaan. Wakati Aliposoma kwamba Umar alimuambia Ali (a.s) na Abbas, 'Umekuja kudai urithi wa mpwa wako, na umekuja kudai urithi wa mke wako kutoka kwa baba mkwe wako', Abd al-Razzaq akasema: 'mwangalie mtu huyu fidhuli na mchokozi; hasemi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), lakini anamtaja kama mpwa wako na baba mkwe wako.'" Lakini pamoja na haya, wakusanyaji wa hadithi wamesimulia kutokea kwake na wamethibitisha maelezo yao kwa chanzo chake, kama ilivyoelezwa katika wasifu wa Abd al-Razzaq kwenye kitabu *Wafayaat* cha ibn Khallikan: "Kamwe watu hawakukusanyika kwa yeyote baada ya Mtukufu Mtume kama walivyokusanyika kwake." Mwandishi huyo huyo anaendelea kusema: "Viongozi wa Uislamu wakati wa uhai wake, walichukua hadithi zao kutoka kwake, na miongoni mwao walikuwa Sufyan Ibn Uyaynah, Abd al-Razzaq akiwa mmoja wa walimu wake, Ahmad ibn Hanbal, Yahya ibn Mu'in na wengineo."

Alizaliwa mwaka wa 126 A.H. alisoma mpaka alipofika umri wa miaka 20 na alifariki mwezi wa Shawwal mwaka wa 211 A.H. (Mwenyezi Mungu amrehemu) Aliishi wakati ule ule na Imam Ja'far as-Sadiq (a.s.) kwa muda wa miaka 22 na alifariki wakati wa uhai wa Imam wa tisa, Muhammad ibn Ali al-Jawad (a.s.) katika umri wa miaka 90. Mwenyezi Mungu amjalie aungane nao siku ya ufufuo kwani alikuwa na mapenzi nao ya kweli. Aidha, hadithi zake zinapatikana kwenye vitabu vyote vya *Sahih* pia kwenye *Musnad*. Vitabu hivi vimejaa masimulizi yake.

**54. Abd al-Malik ibn Ayun:**

Alikuwa ndugu wa Zurarah, Himran, Bukayr, Abd al-Rahman, Malik, Musa na Dharis ambaye pia alikuwa na dada jina lake akiitwa Umm al-Aswad. Wote hawa walikuwa miongoni mwa Shia wa kwanza walijulikana kwa kazi zao kwa ajili ya dini; watoto wao pia walineemeka kwa uongozi sahihi na walifuata itikadi hiyo hiyo. Kuhusu Abd al-Malik, Dhahabi ameandika kwenye kitabu cha *Mizani*: Imeandikwa na Abu Wa'il na wengineo kwamba Abu Haatim alisema: Alikuwa msimulizi mzuri." Ibn Mu'in alisema: "Hana umuhimu" lakini anaendelea kusema: Alikuwa mkweli na alikuwa rafidhi." Ibn Uyaynah anasema: "Nilisikia riwaya kutoka kwa Abd al-Malik, na alikuwa rafidhi." Abu Haatim anasema: "Alikuwa miongoni mwa Shia wa mwanzo na msimulizi mzuri." Hawa Sufyan wawili wamesimulia hadithi kutoka kwake. Ibn al-Qaysarani anasema kuhusu yeye kwenye kitabu chake kiitwacho *Al-Jama Baina al-Rijal al-Sahikayn* (Mkusanyiko wa habari – wasifu – za wasimulizi wa vitabu viwili vya *Sahih* ) anasema: Abd al-Malik ibn Ayun alikuwa ndugu wa Himraan al-Kufi na alikuwa Shia. Alisikia kutoka kwa Abu Wa'il Hadithi inayozungumzia kuhusu Umoja wa Mungu kwenye *Bukhari* na zile zinazozungumzia Imani katika Uislamu, na Sufyan ibn Uyaynah alisimulia kutokea kwake kama walivyokubali hawa waandishi wawili (na hao ni Bukhari na Muslim)." Alifariki

[123] Kwa hakika hazina chuki katika macho ya mtu yeyote isipokuwa kwa Mu'awiyah na waasi wengine na wahaini. Miongoni mwa hadithi hizo ni ile iliyosimuliwa na Abd al-Razzaq kutoka kwa Ibn Uyaynah, ambaye alisikia kutoka kwa Ali ibn Zayd ibn Jadh'an, ambaye aliisikia kutoka kwa Abu Nadhrah, ambaye aliisikia kutoka kwa Abu Sa'id kama msimuliaji wa juu zaidi, kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema: "Wakati mkimuona Mu'awiyah juu ya mimbari yangu, muuweni."

wakati wa uhai wa Imam Ja'far as-Sadiq (a.s) ambaye alimuombea kwa bidii sana na alikuwa mpole kwake. Abu Ja'far, ibn Babwayh anasema kwamba Imam Ja'far as-Sadiq (a.s) pamoja na wanafunzi wake, walikwenda kuzuru kaburi lake kule Madina. Hivyo, ajisikie furaha kwenye bahati yake njema hiyo.

**55. Ubaydullah ibn Musa, al-Abbasi al-Kufi:**

Mwalimu wa Bukhari, kama alivyokiri katika Sahih yake. Ibn Qutaybah amemtaja miongoni mwa wapokezi wa hadith kwenye kitabu chake, *Ma'arif* (kurasa wa 177) na kwa uwazi kabisa amemtaja kuwa alikuwa Shia kama ilivyoandikwa kwenye Sura ya 'Madhehebu' ukurasa wa 206, kadhalika ameandika hivyo ibn Sa'd kwenye kitabu chake *Tabaqat,* na anathibitisha kwamba alikuwa Shia (sehemu ya 6 ukurasa wa 279). Alikuwa na tabia ya kusimulia hadithi zenye kutetea imani ya Shia na kwa hiyo ameonekana kwa watu wengi kwamba yeye ni 'msimulizi dhaifu.' Ibn Sa'd anasema: "Alikuwa ni bingwa katika Qur'ani." Ibn Athiir ametaja kifo chake miongoni mwa matukio yaliyotokea mwishoni mwa mwaka wa 213 A.H. kwenye kitabu chake cha historia kiitwacho *Kamil*, na anasema: "Ubaydullah ibn Musa, al-Abbasi alikuwa mwanasheria na Shia na alikuwa mmojawapo wa walimu wa Bukhari kama ilivyoandikwa kwenye *Sahih* yake."

Dhahabi anazungumza kuhusu yeye kwenye *Miizan* yake: "Ubayadullah ibn Musa al-Abbasi al-Kufi mwanasheria mwenye elimu kubwa alikuwa mwalimu wa Bukhari. Yeye binafsi alikuwa mtu mwaminifu lakini alikuwa Shia, aliyepotoka." Abu Haatim na ibn Mu'in pia wamekubali ukweli wake na uaminifu wake. Ibn Mu'in anasema: "Na Abu Haatim anasema kwamba Abu Na'im alikuwa mbora zaidi' lakini Ubaydullah alikuwa amethibitishwa zaidi katika simulizi zake kupitia kwa Israil." Ahmad ibn Abdullah al-Ajali anasema kuhusu Ubaydullah ibn Musa: "Alikuwa ni chanzo mashuhuri cha Qur'ani. Kamwe sikumuona ananyanyua kichwa chake kwa maringo wala sikuwahi kumuona yeye akicheka." Abu Dawuud anasema: "Ubayadullah ibn Musa alikuwa Shia, aliyepotoka." Dhahabi anasema kwenye *Miizan* yake mwishoni mwa maelezo yake kuhusu habari za Matar ibn Maymun kwamba: "Ubaydullah alikuwa mtu mwaminifu na Shia." Ibn Mu'in amechukua hadithi kupitia kwa Ubaydullah ibn Musa na Abd al-Razzaq akijua wazi kwamba walikuwa Mashia. Imesemwa katika maelezo ya habari za Abd al-Razzaq kwenye kitabu cha *Mizan* kilichoandikwa na Dhahabi kwamba Ahmad ibn Abu Khaythamah alisema: "Nilimuuliza ibn Mu'in kwa mtazamo wa ukweli kwamba niliwahi kusema kwamba Ubaydullah ibn Musa alisimulia hadithi za kutetea imani ya Ushia na ibn Mu'in alijibu: "Naapa kwa jina la Mungu Mmoja kwamba Ad al-Razzaq alikuwa mara mia zaidi kuliko yeye na nimechukua hadithi nyingi zaidi kutoka kwa Abd al-Razzaq kuliko kutoka kwa Ubaydullah."

Wapokezi sita na wengineo wote wametegemezea hoja zao juu ya hadithi zilizosimuliwa na Ubaydullah kwenye vitabu vyao viitwavyo *Sahih*. Hadithi zake zimesimuliwa kwenye vitabu vyote vya *Sahihi* kupitia kwa Shayban ibn Abd al-Rahman. *Sahih al-Bukhari* ina hadithi zake kutoka kwa Al-Rahman. *Sahih Bukhari* kinazo hadithi zake kutoka kwa al-A'mash, Hisham ibn Urwah na Isma'il ibn Abu Khalid, na *Sahih Muslim* ina hadithi kutoka kwa Israil, Hasan Saalih na Usamah ibn Zayd. Bukhari amechukua hadithi moja kwa moja kutoka kwake na pia kupitia kwa Is'haq ibn Ibrahim, Abu Bakr ibn Abu Shaybah, Ahmad bin Is'haq al-Bukhari, Mahmud ibn Ghilan, Ahmad ibn Abu Sariij, Muhammad ibn al-Hasan ibn Ishkaab, Muhammad ibn Khalid al-Dhahali na Yusuf ibn Musa al-Qattan, na Muslim amechukuwa hadithi kupitia kwa Hajjaaj ibn al-Shaair, Qasim ibn Zakariya, Abdullah al-Dharimi, Ishaq, ibn Mansur, ibn Abu Shaybah, Abd ibn Hamiid, Ibrahim ibn Diinaar na ibn Namiir.

Dhahabi anasema kwenye *Miizan* yake kwamba Ubaydullah alifariki mwaka wa 213 A.H. na anaongeza kwamba alikuwa mchamungu na mtiifu kwa Mwenyezi Mungu kwa nguvu ya tabia. Alifariki mwanzoni mwa mwezi wa Dhil-Qadah. Mwenyezi Mungu amrehemu na amuweke mahali pema.

**56. Uthman ibn Umayr, Abu al-Yatan al-Thaqfi al-Kufi al-Bakhli, (Pia anajulikana kama: Uthman bin Abu Dhar'a, Uthman bin Qais, Uthman bin Abu Hamiid)**

Abu Ahmad al-Zubayr anasema: "Aliamini kuhusu 'Marejeo' (*rajah*)." Ahmad ibn Hanbal anasema: "Abu al-Yaqzaan alijiunga na maasi ya Ibrahim ibn Abdullah ibn Hasan," na ibn Adi anasema: "Alikuwa mzushi na aliamini kuhusu 'Ufufuo,' lakini hata hivyo, mabingwa wa kuaminika wamechukuwa hadithi kutoka kwake licha ya udhaifu wake." Kwa maoni yangu, ilikuwa kawaida kwa waandishi kutoa shutuma kuhusu 'Marejeo' kwa msimulizi yeyote wa hadithi ambaye ni Shia waliyependa kumpaka matope na kumdogesha. Kwa hiyo, wamemuweka Uthman ibn Umayr katika daraja la msimuliaji dhaifu, na matokeo yake ni kwamba ibn Mu'in anasema: "Hana umuhimu." Lakini kiasi chochote cha shutuma zao dhidi yake, watu kama Al-A'mash, Sufyan, Sharik na wengineo wa rika lao hawakuzuiwa na chochote kuchukua hadithi kutoka kwake. Hata hivyo, Abu Dawuud, Tirmidhi na wengineo wamejenga mawazo yao kwenye hadithi zake zilizopo kwenye vitabu vya *Sunan* na wote kwa pamoja wamemkubali. Aidha, hadithi zake za kutoka kwa Anas na wengineo pia zimeandikwa na wao. Dhahabi amemtaja kwenye *Miizan* yake na kutaja mambo fulani ya wasifu wake halikadhalika na maoni ya wasomi wengine kuhusu yeye ambayo yametajwa hapo juu. Dhahabi amebuni ufupisho wa jina lake; *Dal, Ta, Qaf* kama rejea ya hadithi zilizochukuliwa kutoka kwake na waandishi wa *Sunan*.

**57. Adii ibn Thabit, al-Kufi:**

Ibn Mu'in anamtaja yeye, akimwelezea yeye kama Shia mkali; Darqutni anamrejea yeye kama "rafidhi mwenye ghera, lakini anaaminika;" Jawzajaan anasema kwamba 'alikuwa mpotovu,' na Masudi anasema: "Sijapata kukutana na mtu msemaji zaidi kuhusu imani yake ya Shia kama Adi ibn Thabit." Dhahabi amemtaja yeye kwenye kitabu chake, *al-Miizan*, amesema: "Alikuwa Shia mwenye elimu nyingi na mtu mkweli miongoni mwao; alikuwa pia ni Kadhi na Imam wa msikiti wa Shia, na kama Shia wote wangekuwa kama yeye, matatizo yao yangepungua." Halafu Dhahabi anaendela kunukuu maoni ya wasomi wengine kuhusu Adi ibn Thabit, ambayo tumekwisha kuyataja hapo juu, akinukuu yale yaliyoandikwa na Darqutni, Ahmad ibn Hanbal, Ahmad al-Ajali na Ahmad al-Nasai katika kuunga mkono uaminifu wake. Dhahabi pia amebuni ufupisho wa jina lake kwa vile vitabu vya *Sahih* vya Sunni vimekubali kwa pamoja usahihi wa hadithi zake. Hadithi zake zinapatikana kwenye vitabu vya *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim* kama zilivyopokelewa naye katika mafunzo yake kutoka kwa Bara'a ibn Azib na Abdullah ibn Yaziid ambaye alikuwa babu yake kwa upande wa mama yake na pia kutoka kwa Abdullah ibn Abu Awfa, Sulayman ibn Abu Sard na Sa'id ibn Jubayr. Aidha, hadithi ambazo zilipitia kwake kutoka kwa Zar ibn Habish na Abu Hazim al-Ashja'i zimeandikwa kwenye *Sahih Muslim*, Al-A'mash, Mus'ir, Sa'id, Yahya ibn Sa'id al-Ansari, Zayd ibn Abu Unaysah na Fudhayl ibn Ghazwaan wamejifunza hadithi kutoka kwake.

**58. Atiyah ibn Sa'd, ibn Junadah al-Awfi, (Abu al-Hasan al-Kufi):**

Alikuwa *Tabi'in* (mfuasi wa masahaba) mashuhuri. Dhahabi amemtaja yeye katika *Miizan* yake, akielezea kutoka kwa Salim al-Muradi kwamba "Atiyah alikuwa Shia." Imam Ibn Qutaybah amemtaja miongoni mwa wasimulizi wa hadithi na mwanachuo. Ibn Qutaybah mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa mjukuu wa Atiyah, Husayn ibn Hasan ibn Atiyah al-Awfi al-Qadhi anasema: "Atiyah ibn Sa'd alikuwa mwanasheria na faqihi wa wakati wa Hajjaj na alikuwa Shia." Ibn Qutaybah pia amemtaja Atiyah kwenye sura ambayo inashughulika na madhehebu mbali mbali. Ibn Sa'd pia amemtaja kwenye kitabu chake *Tabaqat* sehemu ya 6 ukurasa 212 katika namna ambayo inathibitisha uimara wa msingi na ufuasi wake mkali wa mafundisho ya Ushia. Baba yake Atiyah, Sa'd ibn Junadah, alikuwa sahaba wa Hadharat Ali (a.s.). Siku moja alikwenda kwa Ali (a.s) huko Kufah na akasema. Ewe Amiri wa waumini, amezaliwa mtoto wa kiume kwangu kwa hiyo tafadhali pendekeza jina kwa ajili yake." Ali

(a.s) alijibu: “Huyo ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo mpe jina la Atiyah (ambalo maana yake ni zawadi).”

Ibn Sa’d anasimulia: “Atiyah alijiunga na maasi ya ibn al-Ashath dhidi ya yule dhalimu Hajjaj. Na wakati majeshi ya ibn al-Ashath yaliposhindwa, Atiyah alikimbilia Fars (Persia). Halafu Hajjaj alimwandikia Muhammad Ibn al-Qassim amuite Atiyah na amutake kumlaani Ali ibn Abu Talib; kama akikataa kufanya hivyo, basi atandikwe viboko mia nne na kunyolewa kichwa na ndevu zake. Hivyo, Muhammad ibn al-Qasim alimwita Atiyah na alipokataa kufanya hivyo alivyoambiwa aliadhibiwa kama Hajjaj alivyoelekeza. Baada ya muda kidogo, wakati Qutaybah alipoteuliwa kuwa Gavana wa Khurasan, Atiyah aliasi dhidi yake na hakuondoka Khurasan mpaka Umar ibn Hubayrah alipopata ugavana wa Iraq, ndipo hapo Atiyah akamuandikia barua kuomba ruhusa aende kwake. Alipopata ruhusa ya Gavana, Atiyah alikwenda Kufah ampapo aliendelea kuishi mpaka alipofariki mwaka wa 111 A.H. Atiyah alikuwa chanzo cha kuaminika na hadithi nyingi nzuri zimesimuliwa na yeye.

Kizazi cha Atiyah wote walikuwa Mashia wa Mtume na kizazi chake kitakatifu na wapo miongoni mwao wanachuo mashuhuri wakuheshimika kama vile Husayn ibn al-Hasan ibn Atiyah ambaye alimrithi Hafs ibn Ghayath kama Kadhi mkuu wa Mamlaka ya Mashariki (angalia kitabu cha *Ma’arifa* kilichoandikwa na Ibn Qutaybah uk. 186) Baadaye alihamishiwia Askar al Mahdi na alifariki mwaka wa 201 A.H. Alikuwepo pia Muhammad ibn Sad ibn Muhammad ibn al-Hasan ibn Atiyah Kadhi wa Baghdad (angalia Jz. 1 ya *Isabah* ambamo ametajwa katika maelezo ya mhenga wake Sa’d ibn Janadah). Ambaye ni mmoja wa waandishi wa hadithi, alizipata hadithi zake kupitia kwa baba yake Sa’d, ambaye alijifunza kutoka kwa ami yake Husayn ibn Hasan ibn Atiyah.

Lakini kurudia habari za Atiyah mwenyewe, inajulikana wazi kwamba Abu Dawuud na Tirmidhi wamemwamini na hadithi zake zimepatikana kutoka kwa Ibn Abbas, Abu Sa’id, Ibn Umar na Abdullah ibn Al-Hasan ambaye anasimulia kutoka kwa baba yake, Imam Hasan (a.s.) ambaye anasimulia kutoka kwa mama yake, Hadhrat Fatmah (a.s) bint wa Mtume, Bibi wa wanawake wa peponi, wamewekwa kwenye kitabu cha *Sunan* cha Abu Dawuud na *Sahih* ya Tirmidhi. Miongoni mwa wale waliojifunza hadithi kutoka kwake na kusimulia kutoka kwake ni watoto wake wa kiume Hasan ibn Atiyah, Hajjaj ibn Artaat, Mus’ir na Hasan ibn Udwaan.

**59. Al-Ala ibn Saalih, al-Taymi al-Kufi:**

Abu Haatim anamtaja yeye kama ilivyosemwa kwenye maelezo yake kwenye *Miizan*, kwamba “Yeye alikuwa mmojawapo wa wazee wa Kishia.” Lakini pamoja na haya, Abu Dawuud na Tirmidhi wamemwamini na ibn Mu’in amemthibitisha yeye. Abu Haatim na Abu Zar’ah wanasema kwamba: “Hakuna kasoro kwake.” Mbali na hadithi zilizosimuliwa naye kupitia kwa Yaziid ibn Abu Maryam na Hakam ibn Utaybah zimeandikwa kwenye vitabu viwili vya *Sahihi* ya Tirmidhi na Abu Dawuud na vitabu vingine sahihi vya *Sunnah*. Abu Na’im na Yahya ibn Bukayr na wasimulizi wa hadithi wengine kadhaa wa kizazi hicho wamejifunza hadithi kutoka kwake. Al-Ala ibn Saalih asichanganywe na Al-Ala ibn Abbas ambaye alikuwa mshairi kutoka Makka. Huyu Al-Ala mshairi alikuwa mmoja wa Masheikh wa akina Sufyan wawili na amesimulia hadithi kutoka kwa Abu Tufayl, ambaye aliishi kabla ya Al-Ala ibn Saalih na, aidha, Al-Ala ibn Saalih alitokea Kufah, ambapo Al-Ala mshairi alitokea Makka. Dhahabi amewataja wote wawili kwenye *Miizan* yake, na kunukuu humo kwamba wote walikuwa Shia tangu siku za nyuma na kwamba Al-Ala mshairi kwenye baadhi ya sifa zake ana baadhi ya mashairi ya kumsifia Amirul-Muumin Ali (a.s) yaliyojengewa hoja zenye ushahidi usiopingika. Pia ameandika mashairi ya maombolezo ya Mkuu wa Mashahidi. Mwenyezi Mungu amjaalie kupokea thawabu kutoka Kwake na kwa Mtume Wake na waumini wa kweli.

**60. Alqamah ibn Qays ibn Abdullah (Abu Shibli):**

Alikuwa ni ami yake As'wad na Ibrahim, watoto wa Yazid, na wapenzi wa Aali Muhammad (s.a.w.w). Shahristani kwenye kitabu chake cha *Milal wa al-Nahal* anamhesabu yeye kuwa miongoni mwa Shia. Na yupo miongoni mwa viongozi wa wasimulizi wa hadithi kama ilivyosemwa na Abu Is'haq al-Jawzajaan, ambaye anasema: "Walikuwapo watu huko Kufah ambao imani zao za kidini zilikuwa hazikubaliwi kwa sababu ya wao kuwa Mashia, (lakini) walikuwa viongozi wa wasimulizi wa hadithi hapo Kufah….. na Alqamah na ndugu yake Ubayy walikuwa masahaba wa Ali (a.s.); walikuwa katika jeshi lake wakati wa vita vya Sufin ambapo Ubayy aliuawa shahidi." Ubayya alikuwa anajulikana kama 'Ubayy mfanya ibada' kwa sababu alikuwa anashughulika kupita kiasi kuhusu Swala. Na kuhusu Alqamah, aliupaka upanga wake kwa damu ya waasi wengi na yeye alijeruhiwa kwenye mguu na kwa hali hiyo amekuwa akihesabiwa miongoni mwa wapiganaji mashujaa wa Uislamu. Kamwe hakuacha kuwa adui wa Muawiyah katika uhai wake wote. Ilitokea wakati mmoja Abu Bardah aliandika jina lake kwenye ujumbe uliokuwa unakwenda kuonana na Muawiyah wakati alipokuwa Khalifa. Lakini Alqamah alimuandikia Abu Bardah kufuta jina lake na hakupumzika mpaka hapo jina lake lilipoondolewa kwenye orodha. Mambo hayo hapo juu yameandikwa na ibn Sa'd (Mwandishi wa *Tabaqat*) kwenye maelezo yake kuhusu Alqamah (sehemu ya 6 ukurasa wa 52). Uadilifu wake na uaminifu, heshima na utukufu machoni mwa waandishi wa Sunni, pamoja na kwamba alikuwa Shia, ni ukweli uliothibiti. Waandishi wa *Sahih Sita* na wengineo pia wametegemea juu yake. Hadithi zilizosimuliwa naye kutoka kwa Ibn Mas'ud, Abu Darda na Aisha zimeandikwa kwenye *Sahih al-Bukhari na Sahih Muslim*; kwenye *Sahih Muslim* pia zimeongezwa hadithi zingine zilizosimuliwa naye kutoka kwa Uthman na Abu Mas'ud. Hadithi zake kwenye *Sahih Muslim* na *Sahih al-Bukhari* zimejulikana kupitia kwa mpwa wake, Ibrahim al-Nakha'i ambapo baadhi ya hadithi zake kwenye *Sahih Muslim* pia zimepokelewa kupitia kwa Abd al-Rahman ibn Yazid, Ibrahim ibn Yazid na Al-Sha'bi. Alifariki huko Kufah mwaka wa 62 A.H. (Mwenyezi Mungu airehemu roho yake.).

**61. Ali ibn Bidaymah:**

Dhahabi amemtaja yeye kwenye kitabu chake kiitwacho *Miizan* akimnukuu Ahmad Ibn Hanbal ili kuthibitisha kwamba: Alikuwa msimulizi mzuri wa hadithi, alikuwa mmoja wa viongozi wa Shia. Ibn Mu'in amethibitisha kwamba huyu mtu alikuwa mwaminifu; alijifunza hadithi kutoka kwa Akramah na wengineo, na Sha'bah na Mu'ammar wamejifunza kutoka kwake." Dhahabi pia amebuni ufupisho wa jina lake kwa sababu ya marejeo ya mara kwa mara yaliyofanywa kwenye hadithi zake na waandishi wa *Sunan*.

**62. Ali ibn al-Jad, (Abu al-Hasan al-Jawahari al-Baghdadi, mtumishi chini ya himaya ya Banu Hashim):**

Alikuwa mmoja wa washauri wa Bukhari, ambaye amechukua hadithi kadhaa kutoka kwake. Ibn Qutaybah amemuorodhesha yeye kwenye kitabu chake kiitwacho "*Kitab al-Maarif*" kama miongoni mwa Shia. Imeandikwa kwenye kitabu cha *Miizan* (cha Dhahabi) kwamba kwa kipindi cha miaka sitini alifunga swaumu kila baada ya siku moja. Ibn al-Qaysarani ameandika kuhusu yeye kwenye kitabu chake kuhusu maisha ya wasimulizi wa hadithi, kiitwacho *Al-Jama Bayna al-Rijaal al-Sahiihain*. Kitabu cha Bukhari kimejumuisha hadithi kumi na mbili zilizosimuliwa naye. Alifariki mwaka w 230 A.H. akiwa na umri wa miaka 96.

**63. Ali ibn Zayd ibn Abdullah ibn Zuhayr, Ibn Abu Malikah ibn Jadh'aan akijulikana kama Abu al-Hasan al-Qarashi al-Taymi al-Basri):**

Ahmad al-Ajali ameandika kuhusu yeye: "Alikuwa Shia." Na Yazid ibn Zarii' anasema: "Ali ibn Zayd alikuwa rafidhi;" hata hivyo pamoja na yote haya wanachuoni wengi wa kizazi kilichofuatia maswahaba

wa Mtume (*tab'iin*), kama vile Sha'bah na Abd al-Waarith, wamechukua hadithi kutoka kwake. Walikuwepo wanasheria wakubwa watatu kutoka Basrah majina yao ni: Qitadah, Ali ibn Zayd na Ash'ath al-Hadaani, na wote hawa walikuwa vipofu. Wakati Hasan al-Basri alipokufa, watu walimuomba Ali ibn Zayd kushika nafasi yake. Hii ilikuwa kwa sababu ya kujulikana kwa umashuhuri wake, vinginevyo watu wasingetoa pendekezo kama hilo. Siku hizo hapakuwepo na Shia wengi Basrah. Dhahabi ametaja mambo yote yaliyosemwa hapo juu kuhusu mtu huyu kwenye *Miizan* yake, na habari zake pia zinapatikana kwenye kitabu cha *Qaysarani* kiitwacho *al-Jama Bayna ali-Rijaal al-Sahihain* humo imeandikwa kwamba Muslim amechukua hadithi kutoka kwake ambazo zilipatikana kutoka kwa Thaabit al-Binaani na kwamba alisikia hadithi kuhusu *Jihad* (vita vya kuhami dini au kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu) kutoka kwa Anas ibn Malik. Alikufa mwaka wa 131 A.H. (Mwenyezi Mungu amrehemu).

**64. Ali ibn Saalih, ndugu yake Hasan ibn Saalih, (pia anajulikana kama Hasan ibn Hayy, angalia namba 21 hapo juu):**

Alikuwa miongoni mwa Ulamaa wa Shia wa mwanzoni, Muslim amemtegemea katika *Sahih* yake mlango wa 'mauzo' na Ali ibn Saalih amerudia hadithi zilizosikiwa na yeye kutoka kwa Salmah ibn Kuhayl, na Wakii anasimulia kutoka kwake (Ali) na wote wawili walikuwa Shia. Yeye na ndugu yake Hasan walikuwa mapacha, walizaliwa mwaka wa 100 A.H. na Ali ibn Saalih alifariki mwaka wa 151 A.H. (Mwenyezi Mungu amrehemu).

**65. Ali ibn Ghuraab, (Abu Yahya al-Fazard al-Kufi):**

Ibn Habaan amesema kwamba alikuwa Shia mwenye ghera kubwa na hii kwa maoni yangu ndio sababu ambayo imemfanya al-Jawzajaan amkatae. Abu Dawuud pia anasema kwamba hadithi zake zimeachwa. Lakini Ibn Mu'in na Darqutni wamekubali uaminifu wake; Abu Haatim amesema kwamba hakuna kasoro kuhusu mtu huyu; Abu Zarah amesema: "Kwa maoni yangu mtu huyu ni mkweli." Ahmad ibn Hanbal anadokeza: "Wakati wote nimemuona yeye kuwa mwaminifu;" na ibn Mu'in pia anakubali kwamba mtu huyu ni mkweli. Dhahabi amemtaja mtu huyu katika *Miizan* yake, akinukuu tofauti za maoni hayo hapo juu kuhusu mtu huyu miongoni mwa wanachuo watafiti na amebuni ufupisho wa jina lake; *Sin Qaf* kwa sababu ya marejeo ya kurudia rudia ambayo yamefanywa kwake na waandishi wa *Sunnah*. Amechukua hadithi zake kutoka kwa Hisham ibn Urwah na Ubaydullah ibn Umar. Ibn Sa'd amemtaja yeye kwenye *Tabaqaat* yake (Sehemu ya 6 ukurasa wa 273) akisema Isma'il ibn Rajaa amesimulia kutoka kwake ile hadithi ya Al-A'mash kuhusu Uthman." Alifia Kufah mwanzoni mwa mwaka wa 184 A.H. wakati wa utawala wa Harun al-Rashid. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**66. Ali ibn Qaadhim, Abu al-Hasan al-Khuzai al-Kufi:**

Shaykh Ahmad ibn al-Furaat, Yaq'uub al-Fasawi na baadhi ya wanachuoni wa hadithi walioshi wakati mmoja naye walijifunza hadithi kutoka kwake na walimtegemea. Ibn Sa'd anamtaja huyu kwenye kitabu chake kiitwacho *Tabaqaat*, akisema: "Alikuwa Shia mkereketwa." Kwa mtazamo wangu habari hii ni sababu ya Yahya kumtambulisha mtu huyu kama 'dhaifu.' Lakini Abu Haatim anasema: "Nafasi yake ni miongoni mwa wakweli." Dhahabi ameonyesha mambo yote hayo hapo juu kuhusu mtu huyu kwenye kitabu chake kiitwacho *Miizan* na amebuni kifupi cha jina lake; kwani Abu Dawuud na Tirmidhi wamechukua hadithi kutoka kwake kupitia kwa Sa'id ibn Abu Aruubah na wengineo. Alifariki mwaka wa 213 A.H. wakati wa utawala wa Ma'amum. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**67. Ali ibn al-Mundhir, al-Taraaifi:**

Mmoja wa walimu wa Tirmidhi. Nasa'I, Ibn Sa'id, Abd al-Rahman ibn Abu Hatiim na wengineo ambao waliishi wakati mmoja ambao wote wamechukua hadithi kutoka kwake na wakazitegemea hadithi hizo. Dhahabi

amemtaja huyu kwenye kitabu chake kiitwacho *Miizan* na amebuni kifupi cha jina lake: *Ta Sin Qaf* kuonyesha kwamba waandishi wa *Sunan* wamechukua hadithi kutoka kwake. Pia amenukuu maoni ya kutegemewa ya Nasa'i kwamba "Ali ibn Mundhir alikuwa Shia kamili na wa kuaminiwa." Na pia anamnukuu Ibn Hatim akisema kwamba 'Ali ibn Mudhir alikuwa "Mkweli na wa kutumainiwa" na kwamba "anasimulia hadithi kutoka kwa Ibn Fudhayl, Ibn Uyaynah na Waliid ibn Muslim." Ukweli kwamba wakati Nasa'i anakubali kwamba mtu huyu alikuwa Shia mkamilifu, kunyambulika kwa hadithi zake zilizomo kwenye Sahih yake lazima kuangaliwe kwa uangalifu na wale wabishanaji ambao huhamisha na kugeuza maneno. Ibn Mundhir alifariki mwaka wa 256 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**68. Ali ibn Hashim ibn Burayd (Abu al-Hasan al-Kufi al-Khazzaaz al-Aaidhi):**

Alikuwa mmoja wa washauri wa Imam Ahmad (ibn Hanbal). Abu Dawuud amemtaja mtu huyu kama "Shia Madhubuti," na Ibn Haban anasema "Ali ibn Hashim alikuwa Shia mwenye ghera kupita kiasi." Ja'far ibn Ibaan anasema: "Nimesikia kutoka kwa Ibn Namiir kwamba Ali ibn Hashim alikuwa na ghera ya kupita mpaka katika Ushia wake." Na Bukhari anasema: "Ali ibn Hashim na baba yake wote wawili walikuwa na ghera kupita kiasi kwenye itikadi zao." Kwa maoni yangu hii ni sababu ambayo imemfanya Bukhari aache hadithi zake. Hata hivyo, waandishi wengine wote watano wa vitabu vya *Sahih* wametegemea juu ya mtu huyu na Ibn Mu'in na wengineo wamechukua dhamana kwa ajili yake; Abu Dawuud amemweka mtu huyu miongoni mwa 'wasimulizi wa kuaminika,' na Abu Zar'ah amesema kwamba alikuwa mkweli. Nasa'i amekubali kwamba hakuna ubaya wowote kwa mtu huyu na Dhahabi amemtaja kwenye kitabu chake *al-Miizan* akitoa maoni yote yaliyosemwa hapo juu (katika *Taarikh* yake Jz. 12, uk. 116).

Khatib al-Baghdadi amemtaja Muhammad ibn Sulayman, ambaye anasema kwamba Ali ibn al-Madi'ini alisema: "Ali ibn Hashim alikuwa mtu mkweli na alikuwa Shia;" pia anamtaja Muhamamd ibn Ali al-Aajuri ambaye alisema: "Nilimuuliza Abu Dawuud kuhusu Ali ibn Hashim ibn Burayd na akasema aliulizia kuhusu mtu huyu kutoka kwa Isa ibn Yunus ambye alisema kwamba alitokea kwenye familia ya Kishia lakini kamwe hakuwahi kusema uongo." Khatib wa Baghdadi pia amemtaja Ibrahim ibn Yaq'uub al-Jawzajaan ambaye alisema: "Hashim ibn Burayd na mtoto wake wa kiume wote wawili walikuwa wakereketwa mno kwenye itikadi yao ya dini isiyofaa." Lakini hata baada ya haya yote, waandishi watano wa vitabu vya *Sahih* (isipokuwa Bukhari) wametegemea juu ya mtu huyu na kuna hadithi moja iliyosimuliwa naye kutoka kwa Hashim ibn Urwah kuhusu mada ya ndoa kwenye *Sahih Muslim,* na hadithi nyingine kuhusu kuomba ruhusa iliyochukuliwa kutoka kwa Talhah ibn Yahya. Kwenye *Sahih Muslim* Abu Mu'ammar, Isma'il ibn Ibrahim na Abdullah ibn Umar ibn Ibaan wameoneshwa kwamba wamesimulia hadithi kutoka kwake na Ahmad ibn Hanbal na watoto wa kiume wa Abu Shaibah na wengine wengi wa kizazi hicho pia wamesimulia hadithi kutoka kwake, kwani Ali ibn Hashim alikuwa mwalimu wao. Dhahabi anasema kwamba Ali ibn Hashim alifariki mwaka wa 181 A.H. Kwa hiyo, inawezekana alifariki wakati wa uhai wa Imam Ahmad. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**69. Ammaar ibn Zariiq al-Kufi:**

As-Sulayman amemuorodhesha mtu huyu miongoni mwa 'Rafidhi' kama ambavyo Dhahabi naye pia alivyofanya kwenye maelezo ya Ammaar katika *Miizan* yake. Lakini, pamoja na kuwa rafidhi, Muslim, Abu Dawuud na Nasa'i wametegemea hadithi zake. Hadithi zake katika *Sahih Muslim* zimesimuliwa kutoka kwa Al-A'mash, Abu Ishaq al-Sabii, Mansur na Abdullah ibn Isa pia na Abu al-Jawaab, Abu al-Ahwas Salaam, Abu Ahmad al-Zubayri na Yahya ibn Adam.

**70. Ammaar ibn Muawiyah, (Au ibn Abu Muawiyah, na wengine wanasema alikuwa mtoto wa Khabaab):**

Imesemekana kwamba Ibn Saalih al-Dahani al-Bajali al-Kufi alijulikana kama Abu Muawiyah. Alikuwa mmoja wa Mashujaa wa Kishia. Alipata mateso mengi kwa kufuata kwake njia ya kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hata nyayo zake mbili zilikatwa kwa sababu alikuwa Shia. Alikuwa Mwalimu wa wale Sufyan wawili na Sha'bah na Shariik na al-Abaar, na wamechukua hadithi kutoka kwake na wamemtegemea. Ahmad, Ibn Mu'in Abu Haatim na wengineo wamechukua hadithi kutoka kwake. Muslim na waandishi wa vitabu vinne vya *Sunnan*, wemchukua hadithi kupitia kwake, na Dhahabi ametaja mambo yote ya mtu huyu na amemtaja kwenye sehemu mbili katika kitabu chake *al-Miizan*, kwa kumuelezea kwamba alikuwa Shia na mwaminifu. Sijapata kuona lawama zozote dhidi ya mtu huyu isipokuwa kwenye maandishi ya Al-Aqiili, na humo pia mlikuwa hamna kikwazo isipokuwa kwamba alikuwa Shia. Kuna hadithi moja muhimu kutoka kwake kuhusu mada ya Hijja ambayo ipo kwenye *Sahih Muslim* kama alivyofundishwa na Abu Zubayr. Alifariki mwaka wa 133 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**71. Amr ibn Abdullah Abu Is'haq al-Sabi al-Hamadaani al-Kufi:**

Alikuwa Shia kulingana na chanzo cha Ibn Qutaybah (*Ma'rif*) na Shahristani kwenye kitabu chake *al-Milal wa al-Nihal.* Alikuwa mmoja wa wasimulizi wakubwa wa hadithi ambao imani na matendo yao ya kidini yamekataliwa na *ma-Naasibi,*[124] wakiwashutumu kwamba wao Mashia wamebuni mambo haya kwa sababu ya kuwapendelea Ahlul-Bayt na kwamba wanawafuata viongozi wao katika mambo yote yahusuyo dini. Hivyo, Jawzajaan anasema kwenye maelezo yake kuhusu Zubayd kwenye kitabu chake *al-Miizan*: "Palikuwepo kundi miongoni mwa watu wa Kufa ambao dini yao haikupendwa na watu, ingawaje walikuwa wasimulizi wakubwa wa hadithi wa Kufah, kama vile Abu Is'haq, Mansur, Zubayd al-Yaami, A'mash na wengineo wa aina yao.

Watu wanaamini ukweli wao kama wasimulizi wa hadithi ambapo wakisita kuzikubali riwaya zisizo za moja kwa moja zilizohusishwa kwao. Manasibii wanasita kuzikubali riwaya kama ile iliyopokelewa kupitia kwa Amr ibn Isma'il Hamadani (kama ambavyo imelezwa kwenye maelezo juu yake ndani ya *Miizan*) kwamba Abu Is'haq alisema kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Ali ni kama mti ambao shina lake ni mimi, na tawi yake ni Ali, matunda yake ni Hasan na Husayn na majani yake ni Shia." Mughayrah anasema; "Watu wa Kufa ni watu wenu na vivyo hivyo Abu Is'haq na al-A'mash bali kwa ukweli kwamba watu hawa ni Mashia na wafuasi waaminifu wa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.), wamekuwa wahifadhi wa sunnah na hadithi zinazohusiana na sifa za watukufu hawa. Walikuwa bahari za elimu na mabingwa katika njia ya Mwenyezi Mungu." Wakusanyaji wa vitabu vyote na vile vya *Sahihi Sita* na wengineo, wemetegemeza mafunzo yao juu ya hadithi zao. Isitoshe, hadithi za Abu Is'haq kama alivyojifundisha kutoka kwa Bara'a ibn Aazib, Yazid ibn Arqam, Haarithah ibn Wahab, Sulayman ibn Surd, Nu'man ibn Bashiir, Abdullah ibn Yazid al-Hatim na Amr ibn Maymuum, zimo kwenye vitabu vyote viwili *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim.* Hadithi zake zilizomo kwenye vitabu hivyo zinapatikana kupitia kwa Sha'ba, Al-Thawri, Zubayr na mjukuu wa Abu Ishaq – Yusuf ibn Ishaq. Ibn Khalikaani anasema kwenye maelezo yake kwenye *Wafayaat* kwamba alizaliwa miaka mitatu kabla ya kwisha kwa utawala wa Uthman (mnamo mwaka wa 37 A.H. – 652 A.D.) na alifariki mwaka wa 127, 128 au 129 A.H. Kufuatana na wasemavyo Yahya ibn Mu'in na Al-Madaaini, alifariki mwaka wa 132 A.H..

**72. Auf ibn Abu Jamiilah al-Basri, (Akiitwa Abu Sahl, ajulikanaye pia kama al-Araabi):**

Ingawa hakuwa Mwarabu (bedui) kwa asili, Dhahabi amemtaja kwenye *Miizan* yake akisema: "Alijulikana kama 'Auf wa kweli' na inasemekana kwamba alikuwa Shia. Wanachuoni kadhaa wamekubali

[124] Naasibi ni tapo la wafuasi wa Mu'awiyah wanachukulia kwamba hila zilizofanywa na Amr ibn Aas wakati wa tukio la suluhu (baada ya vita vya Siffin), lilimpatia Mu'awiyah haki ya ukhalifa.

kwamba alikuwa mkweli," na wamesimulia taarifa za kuwa kwake Shia kutoka kwa Ja'far ibn Sulayman, na kuwa kwake rafidhi kutoka kwa Bindaar.

Ibn Qutaybah amemuorodhesha yeye miongoni mwa Shia kwenye kitabu chake kiitwacho *Maarif*. Ruuh, Hawdhah, Sha'bah, Nadhr ibn Shumayl. Uthman ibn al-Haytham na wengineo wamechukua hadithi kutoka kwake, na waandishi wa vitabu sita vya *Sahihi* na wengineo wemetegemeza uamuzi wao kwenye hadithi zake. Hadithi zake zilizomo kwenye *Sahih al-Bukhari* zinatoka kwa Hasan, Said ibn Abdul-Hasan al-Basri, Muhammad ibn Siiriin na Sayyaar ibn Salaamah, na kwenye *Sahih Muslim* hadithi zake zinatoka kwa Nadhr ibn Shumayl. Hadithi zake kutoka kwa Abu Rajaa al-Utaaridi pia zinaweza kuonekana kwenye zile *Sahih* mbili. Alifariki mwaka wa 146 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**73. Fadhil ibn Dakiin:**

Jina la baba yake ni Amr ibn Hammad ibn Zuhayr al-Malai al-Kufi na alijulikana kama Abu Na'iim. Ametajwa kama mwalimu wa Bukhari katika *Sahih*. Baadhi ya wanachuo mashuhuri wamemuainisha kama Shia; kwa mfano, angalia kwenye kitabu kiitwacho *Ma'arif* kilichoandikwa na Ibn Qutaybah. Dhahabi pia amemtaja mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Miizan*, anasema: "Fadhil ibn Dakiin Abu Na'im ni mwandishi wa kutegemewa lakini yeye ni Shia." Mwandishi huyo huyo anaendelea kunukuu maandishi ya Ibn al-Junayd al-Khatli, ambaye amesema kwamba alimsikia Ibn Mu'in akisema kwamba wakati wowote Abu Na'im (Fadhil ibn Dakiin) alipomsifu mtu yeyote kwa kusema. "Mtu huyu alikuwa mashuhuri" mtu huyo alionekana kuwa ni Shia, na wakati wowote aliposema kuhusu yeyote, "Mtu huyu ni Murjii,[125] mtu huyo alijulikana kuwa ni Sunni na alikuwa hana dosari.

Dhahabi anamalizia kwenye maelezo yake kwamba Yahya ibn Mu'in alikuwa na mwelekeo wa u-Murjii. Inaonyesha pia kwamba Fadhil alikuwa ni Shia. Dhahabi anaendelea zaidi katika maelezo ya Khalid ibn Mukhallid kwenye kitabu *al-Miizan* kwamba Jawzajaan anamuona Abu Na'im kama ni wa "madhehebu ya watu wa Kufa" (yaani madhehebu ya Shia). Kwa kifupi, hapana shaka kwama Abu Na'im alikuwa Shia, na waandishi wa vitabu 6 vya *Sahih* wametegemea juu yake. Hadithi zake zimesimuliwa kwenye *Sahih al-Bukhari* kupitia kwa Hamaam ibn Yahya, Abd al-Aziz ibn Abu Salmah, Zakariya ibn Abu Zaaidah, Hisham ibn al-Dastwa'i, Al-A'mash, Musir, Thawri, Maalik, Ibn Uyaynah, Shaaban na Zuhayr, na kwenye *Sahih Muslim* hadithi zake zimesimuliwa kupitia kwa Abu Asim Muhammad ibn Ayyub al-Thaqafi, Sayf ibn Abu Sulayman, Isma'il ibn Muslim, Abu al-Amiis, Musa ibn Ali, Abu Shahaab Musa ibn Naafi', Sufyani, Hisham ibn Sa'd, Abd al-Waahid ibn Ayman, na Israil. Bukhari ameismulia hadithi moja kwa moja kutoka kwake na Muslim amesimulia hadithi zake kupitia kwa Hajjaj ibn al-Shaair, Abd ibn Hamiid, Ibn Abu Shaybah, Abu Said al-Ashaj, Ibn Namiir, 'Abdul Uah al-Daarimi, Is'haq al-Hanzali na Zuhayr ibn Harb. Alizaliwa mwaka wa 130 A.H. na alifariki huko Kufah tarehe 26 au 27 usiku wa mwezi wa Shaban mwaka wa 210 A.H. wakati wa utawla wa al-Mu'tasim. Ibn Sa'd amemtaja mtu huyu kwenye kitabu chake kiitwacho *Tabaqat,* sehemu ya 6 ukursa wa 279 akisema: "Ni mtu wa kutegemewa; mwaminifu na amesimulia hadithi nyingi na ni madhubuti.

**74. Fudhayl ibn Marzuuq:**

Pia anaitwa Abu Abd al-Rahman, alikuwa miongoni mwa viongozi walioheshimiwa sana wa Kufah. Dhahabi anasema kuhusu mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Miizan* kwamba alijulikana sana kama Shia na ametaja vyanzo vya Sufyan ibn Uyaynah na Ibn Mu'in kwamba Ibn Adi amesema kwamba hakuna dosari

[125] Tapo mojawapo la Khawariji wanaoamini kwamba mtu yoyote anayetenda dhambi kubwa anakuwa kafiri, lakini Waasil ibn Ata, mfuasi wa filosofia ya Mu'tazilah ana mtazamo ulio kinyume na huo, na kwamba wale wote wanaojiunga na mtazamo wa Waasil walijulikana kama *Murji'ah* – yaani, wale ambao wanachukulia kwamba yeyote yule ambaye anatenda dhambi kubwa habaki moja kwa moja kuwa mu'mini lakini pia hawi kafiri.

kwa mtu huyu. Dhahabi anaendelea kunukuu kutoka kwa Haytham ibn Jamiil kwamba Fudhayl ibn Marzuuq alikuwa mmoja wa viongozi wa dini kwa sababu ya uchamungu wake na hadhi. Muslim amezitegemea hadithi zake mtu huyu kwenye *Sahih* yake ambazo zimesimuliwa kutoka kwa Shaqiiq ibn Uqbah katika mada ya Swala, na kutoka kwa Adi ibn Thaabit katika mada ya Haki za Masikini. Hadithi zake kwenye *Sahih Muslim* zimesimuliwa na Yahya ibn Adam na Abu Usamah kuhusu mada ya Zakaat; na kuhusu Sunnah ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zimesimuliwa na Wakii', Yaziid, Abu Na'im, Ali ibn al-Ja'd, na wasimulizi wengine wa kizazi hicho. Zayd ibn al-Habaab anazichukulia hadithi zake kuhusu "*ta'miir"*[126] kuwa si za kweli. Alifariki mwaka wa 158 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**75. Fitr ibn Khaliifah, al-Hanaat al- Kufi:**

Abdullah ibn Ahmad ilitokea wakati fulani alimuuliza baba yake kuhusu Fitr ibn Khaliifah; alisema: "anaaminika ni msimulizi mzuri wa hadithi, simulizi zake ni simulizi za mtu mwenye akili lakini mtu huyu ni Shia." Abbas anasimulia kutoka kwa Ibn Mu'in kwamba Fitr ibn Khaliifah ni Shia mwaminifu. Ahmad anasema kwamba Yahya aliamini kwamba Fitr alikuwa mwaminifu lakini alihisi alikuwa mgumu na mwenye ghera zaidi. Ni kwa sababu hii Abu Bakr ibn Ayyash amesema: "Nimekataa riwaya za Fitr si kwa sababu nyingine isipokuwa imani yake mbaya," hapa ina maana kwamba mtu huyu hakuwa na kasoro isipokuwa tu kwa sababu yeye ni Shia.

Jawzajaan anasema: "Fitr ibn Khaliifah alikuwa Muasi," na Ja'far al-Ahmar alimsikia wakati wa ugonjwa wake akisema kwamba: "Si jambo dogo kwangu mimi kuwa na malaika wengi kama zilivyo nywele mwilini kwangu, kwa kumtukuza Mwenye Enzi kwa sababu ya mapenzi yangu kwa Ahlul-Bayt." Fitr amesimulia hadithi kutoka kwa Abu Tufayl, Abu Waail na Mujaahid, na miongoni mwa wale ambao wamejifunza (waliopata) hadithi kutoka kwake ni Abu Usaamah, Yahya ibn Adam na Qabiishah. Ahmad (ibn Hanbal) na wengineo wamemshuhudia kwa uaminifu wake; Abu Haatim amemwelezea mtu huyu kama ni msimulizi mzuri; Nasa'i anasema: "Hakuna dosari kwake;" Murrah anasema kwamba, "alikuwa mwaminifu, alikuwa na kumbukumbu nzuri na mwenye akili," Ibn Sa'd alikuwa na maoni kwamba, "alikuwa mwaminifu." Dhahabi ameingiza habari zake kwenye *al-Miizan* yake na amenukuu mambo yote yaliyotajwa hapo juu pamoja na maoni kuhusu mtu huyu. (kiangalie kitabu *Tabaqat* cha Ibn Sa'd sehemu ya 6 ukurasa wa 253) Ibn Qutaybah, amemjumuisha Fitr miongoni mwa Shia katika maelezo na maisha ya Mashia kwenye kitabu chake, *Ma'arif*. Bukhari ameandika kwenye *Sahih* yake Hadithi moja kama ilivyosimuliwa na Fitr kutoka kwa Mujaahid; Thawri amechukua hadithi kutoka kwa Fitr kuhusu 'tabia' (maadili), na waandishi wa vitabu vinne vya *Sunnan* na wengineo wamesimulia hadithi kutoka kwa Fitr. Alifariki mwaka wa 153 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**76. Maalik ibn Isma'il ibn Ziyad ibn Dirham, (Alijulikana pia kama Abu Ghassan al-Kufi al-Nuhdi):**

Alikuwa Sheikh wa Bukhari, kama ilivyotajwa kwenye *Sahih.* Ibn Sa'd ametoa maelezo ya maisha yake kwenye kitabu chake, *Tabaqat*, sehemu ya 6, uk. 282, akimalizia na maneno yafuatayo: "Abu Ghassan alikuwa mwaminifu, mkweli na Shia madhubuti," Dhahabi amemtaja kwenye kitabu chake *al-Miizan* kwa maneno yanayothibitisha uadilifu wake na heshima ya kipekee na anaonyesha kwamba alikubali imani ya Ushia kwa ushawishi wa mwalimu wake Hassan ibn Saalih. Ibn Mu'in anasema: "Hakuna hata mtu mmoja hapo Kufah ambaye ni mkamilifu na sahihi mno kuliko Abu Ghassan." Abu Haatim anasema: "Kamwe sikupata kumuona mtu yeyote hapo Kufah ambaye ni thabiti na mwenye usahihi hasa kuliko mtu huyu – hata Abu Na'im wala mwingine yeyote. Heshima na ucha-Mungu ndio sifa yake. Wakati wowote nilipomuona alionekana kama vile alikuwa ametokea kaburini akiwa na alama mbili za sijida kwenye paji la uso wake."

[126] "*Ta'miir"* – kuteuliwa kwa Hadharat Ali (a.s) na Mtume (s.a.w.w.) kama Amirul Muminin.

Bukhari anasimulia hadithi kwenye sehemu kadhaa kwenye *Sahih* yake ambazo alizichukua moja kwa moja kutoka kwake, na Muslim ameandika hadithi moja kutoka kwake kupitia kwa Harun ibn Abdullah inayozungumzia kuhusu adhabu. Kufuatana na taarifa ya Bukhari, alikuwa mwanafunzi wa Ibn Uyaynah, Abd al-Aziz ibn Abu Salmah na Israil. Bukhari na Muslim wamechukua hadithi kadhaa kutoka kwake kupitia kwa Zubayr ibn Muawiyah. Alifia huko Kufah mnamo mwaka wa 219 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**77. Muhammad ibn Khaadhim:**

Baadhi ya waandishi kwa makosa humuita Ibn Haazin, na kwa kawaida anajulikana kwa jina la Abu Muawiyah al-Dhariir al-Tamiimi al-Kufi. Dhahabi anasema kuhusu habari za mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Miizan*: "Muhammad ibn Khadhim (kifupi chake Ayn) al-Dhariir ni mtu thabiti kabisa; kamwe sijasikia lolote dhidi yake; nitakuwa na mengi zaidi ya kusema kuhusu mtu huyu kwenye sura inayozungumzia kuhusu majina ya ukoo." Abu Muawiyah al-Dharir ni mmoja miongoni mwa watu wenye elimu nyingi wa zama za mwanzo, na Hakim anasema kwamba "Masheikh wawili (Bukhari na Muslim) wamezitegemea hadithi zake, na ghera yake kubwa kuhusu imani yake ya Ushia ilikuwa inajulikana sana." Kwa hiyo imehakikishwa kwamba waandishi wote wa vitabu sita vya Sahih wanamwamini mtu huyu, na Dhahabi amebuni kifupi cha jina lake, kuonyesha kuungana kwa maoni yao kuhusu mtu huyu kuwa mkweli. Hadithi zake zinapatikana kwenye *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim* kutoka kwa msimuliaji zaidi ya mmoja ukimjumuisha na al-A'mash na Hisham ibn Urwah. Kwenye *Sahih Muslim* hadithi zake zimesimuliwa kupitia kwa Ali ibn al-Madiini, Muhammad ibn Salaam, Yusuf ibn Isa, Qutaybah, Musaddad, Said al-Waasti, Said ibn Mansur, Amr al-Naaqad, Ahmad ibn Sinaan, Ibn Namiir, Ishaqa al-Hanzali, Abu Bakr ibn Abu Shaybah, Abu Kurayb, Yahya ibn Yahya na Zuhayr. Musa al-Zaman amesimulia hadithi kutoka kwa mtu huyu ambazo zinapatikana kwenye *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim*. Abu Muawiyah alizaliwa mwaka wa 113 A.H. na alifariki mwaka wa 195 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**78. Muhammad ibn Abdullah, al-Dhubbi al-Tihaani al-Naisaburi:**

Anajulikana kama Abu Abdullah al-Haakim. Alikuwa wa mwamzo kabisa katika watu waliohifadhi Qur'ani na mwandishi wa hadithi wakati wa uhai wake, na mtunzi wa vitabu visivyopungua elfu moja. Alisafiri sana kwa ajili ya kutafuta elimu na aliwasikiliza walimu takriban 2000. Wanachuoni wenzake wa wakati wake kama vile al-Saluuki na Imam Ibn Fuurak, watu wasomi ambao walikiri ubora wake kuwazidi wao, walimheshimu kwa hadhi zake, walisisitiza kumfanyia heshima na kamwe hawakuacha kukubali uongozi wake. Wasimulizi wote wa hadithi wa Sunni ambao walikuja baada yake, walipata elimu kutoka kwake na alikuwa mmoja wa mashujaa wa Mashia na nguzo za Shari'ah. Mambo yote haya yanaweza kuhakikishwa kwenye maelezo yake kama yalivyoandikwa kwenye kitabu *Tadhkirat al-Huffadh* kilichoandikwa na Dhahabi. Mwandishi huyohuyo amesema kwenye kitabu *al-Miizan* pia kwamba; "Alikuwa Imam, mkweli," inaonyesha ushahidi kwamba "mtu huyu alijulikana sana kama Shia." Na anaendelea kusema kwamba "Nilimuuliza Abu Isma'il Abdullah al-Ansari kuhusu Haakim Abu Abdullah na alisema, 'alikuwa Imam katika somo la hadithi na rafidhi aliyepindukia.'" Dhahabi pia amenukuu tetesi nyingi kutoka kwake pamoja na usemi wake kwamba; "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alizaliwa akiwa tayari ametahiriwa na huku akitabasamu," na kwamba "Ali alikuwa mrithi wake," Dhahabi anaendelea kusema zaidi kwamba "kuhusu mtu huyu kuwa ni mkweli, iwe katika mambo ya binafsi au katika mambo ya kielimu, hilo ni jambo ambalo limekubaliwa kwa wote." Alizaliwa mwezi wa Rabi ul-Awwal mwaka wa 321 A.H. na alifariki mwezi wa Safar mwaka wa 405 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**79. Muhammad ibn Ubaydullah ibn Abu Raafi' al-Madani:**

Mtu huyu na Abu Ubaydullah na ndugu zake wote walikuwa wanachuoni wa kuheshimiwa. Abdullah alikuwa baba wa Ubaydullah, mjukuu wake alikuwa Abu Raafi', na ami zake walikuwa Raafi', Hasan, Mughayrah na Ali, ambaye watoto wake na wajukuu zake wote walikuwa ni watu watakatifu miongoni mwa vizazi vya mwanzo vya Mashia, na wameacha vitabu vingi ambavyo vinathibitisha kwamba walikuwa wafuasi madhubuti wa itikadi ya Shia. Maisha yao yameelezewa kwa kirefu kwenye sehemu ya 12 ya hotuba yangu ya pili kwenye kitabu changu "*Fusul al-Muhimmah*." Kuhusu Muhammad, ametajwa na Ibn Adi mwishoni mwa maelezo yake kwenye kitabu *al-Miizan* kama ifuatavyo: "Alikuwa mmoja wa Shia waliokuwa wanaishi Kufah." Kwenye *Miizan*, Dhahabi amebuni kifupi cha jina lake *Ta Qaf* kama waandishi wa Sunan walivyozikubali hadithi zilizosimuliwa na mtu huyu. Dhahabi anaendelea kusema zaidi kwamba alisikia hadithi kutoka kwa baba yake na babu yake, ambapo Mundla na Ali ibn Hashim walisimulia kwamba walisiia kutoka kwake.

Habaan ibn Ali, Yahya ibn Ya'li na wengineo pia wamesimulia hadithi zilizosikiwa na wao kutoka kwa Muhammad ibn Ubaydullah; na inawezekana kwamba Muhammad amesimulia kutoka kwa ndugu yake, Abdullah ibn Ubaydullah, kama ajulikanavyo na wale waliomfuata.

Tabarani anasimulia kwenye kitabu chake cha *Mu'jam al-Kabiir* kutoka kwa Muhammad ibn Ubaydullah, ambaye anasimulia kutoka kwa baba yake, ambaye anasimulia kutoka kwa babu yake kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Ali: "Nitakuwa wa kwanza kuingia Peponi na wewe, Hasan na Husein na dhuria wetu watakuja nyuma yetu, na Mashia wetu watakuja kutoka kushoto na kulia."

**80. Muhammad ibn Fudhayl, ibn Ghazwaan, (Anayejulikana kama Abu Abd al-Rahman al-Kufi):**

Ibn Qutaybah amemuorodhesha mtu huyu miongoni mwa Shia kwenye kitabu chake *al-Ma'arif*. Ibn Sa'd amesema kuhusu mtu huyu kwenye kitabu chake *Tabaqat*, Jz. 6, uk. 271 kama ifuatavyo: "Ni mtu wa kutegemewa na mkweli; amesimulia hadithi nyingi, yeye ni Shia; wengine miongoni mwao hawaweki hoja zao juu ya hadithi zake…" Dhahabi anasema karibu na mwisho wa *Miizan* yake kwamba "alikuwa mkweli na Shia," na mahali pengine katika kitabu hicho hicho anasema "Mkweli na ni maarufu." Pia anasema kwamba Ahmad (ibn Hanbal) anamuona mtu huyu kama "msimulizi mzuri wa hadithi na Shia," na kwamba Abu Dawuud anamfikiria mtu huyu kama "ni Shia na mwenye ghera sana," na anasema kwamba alikuwa msimuliaji wa hadithi na mtukufu na kwamba alisoma Qur'ani kwa ajili ya Hamzah, kwamba Ibn Mu'in amekubali kwamba ni mtu mkweli, kwamba Ahmad ibn Hanbal anamuona mtu huyu kama msimuliaji mzuri, na kwamba Nasa'i anasema: "Hakuna dosari yoyote kwake huyu."

Waandishi wa vitabu sita vya *Sahih* na wengineo wamemtegemea mtu huyu. Hadithi zake zimeandikwa kwenye *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim* kupitia kwa baba yake Fudhayl, na kupitia kwa A'mash na Isma'il ibn Abu Khalid na wengineo wa rika lake wa kizazi hicho. Bukhari amechukua hadithi zake kupitia kwa Muhammad ibn Salaam, Qutaybah, Imraan ibn Maysarah na Amr ibn Ali. Muslim amechukua hadithi zake kupitia kwa Abdullah ibn Aamir, Abu Kurayb, Muhammad ibn Tarayf, Waasil ibn Abd al-Ala, Zuhayr, Abu Sa'id al-Ashajj, na Muhammad ibn Abd al-Aziz ibn Umar ibn Aban.

Muhammad ibn Fudhayl alifariki kule Kufah mwaka wa 194 au 195 Hijiria, Mwenyezi Mungu amrehemu.

**81. Muhammad ibn Muslim, ibn at-Taaifi:**

Alikuwa mmoja wa wanafunzi mashuhuri wa Imam Abu Abdullah Ja'far as-Sadiq (a.s). Sheikh al-Taaifah Abu Ja'far al-Tuusi anamtaja mtu huyu kwenye kitabu chake chenye habari za maisha

ya wasimulizi wa Kishia. Hasan ibn Ali ibn Dawuud pia ameandika mambo kadhaa kuhusu mtu huyu kwenye kitabu chake *Mukhatasar* kwenye sura inayozungumzia wasimulizi wakweli. Hivyo hivyo Dhahabi anamtaja mtu huyu na kunukuu maoni ya Yahya ibn Mu'in na wengineo kuhusu kutegemewa kwake na kusema kuwa Qa'nabi, Yahya ibn Yahya na Qutaybah wamesimulia hadithi ambazo walijifunza kutoka kwake, pia anamtaja Abdul Rahman ibn Mahdi, ambaye anatuambia kwamba Muhammad ibn Muslim ni mwandishi wa vitabu vya kuaminika kuhusu hadithi na kwamba Ma'ruf ibn Waasil alimuona Sufyan al-Thawri akiandika hadithi zilizosimuliwa kwake na Muhammad ibn Muslim. Ni kweli kwamba kuna waandishi ambao wamemuona mtu huyu kama ni "dhaifu" kwa sababu yeye ni Shia, lakini maoni ya waandishi hawa hayawezi kumwondoa kwenye heshima yake madhubuti.

Hadithi zake kuhusu wudhu kama ilivyochukuliwa kupitia kwa Amr ibn Diinaar inapatikana kwenye *Sahih Muslim*, na Wakii' ibn al-Jarrah, Abu Na'im, Ma'n ibn Isa na wengineo wamejifunza hadithi kutoka kwake.[127]

Alifariki mwaka wa 177 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu. Katika mwaka huo huo wajina wake Muhammad ibn Muslim ibn Jammaaz pia alifia huko Madina. Ibn Sa'd anatoa maelezo ya watu hawa wawili kwenye kitabu chake "*Tabaqat"* sehemu ya 5.

**82. Muhamamd ibn Musa, ibn Abdullah al-Fitri al-Madani:**

Dhahabi amemtaja mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Miizan*, akitaja chanzo cha Abu Haatim kuhusu yeye kuwa Shia na kuandika maoni ya Tirmidhi kuhusu kuaminika kwake mtu huyu, ambapo Muslim na waandishi wa Sunan wamebuni kifupi cha jina lake hivyo kukiri kiwango ambacho kwacho kwamba wanamtegemea. Kwenye sura inayozungumzia juu ya vyakula katika *Sahih Muslim* – mwandishi anasimulia hadithi yake kama ilivyopatikana kupitia kwa Abdullah ibn Abdullah ibn Abu Talhah na pia kutoka kwa al-Maqbiri na kundi la wasimulizi wa kizazi hicho. Ibn Abu Fadiik; ibn Mahdi, Qutaybah na wengineo wa rika lake wamesimulia hadithi zilizosikiwa na wao kutoka kwa mtu huyu.

**83. Muawiyah ibn Ammaar, al-Dahani al-Bajali al-Kufi:**

Alikuwa mashuhuri miongoni mwa wasimulizi wetu na anasimama katika safu ya kwanza miongoni mwao; mtu mkubwa, mtu mwenye hadhi ya juu na mwaminifu. Baba yake, Ammaar, alikuwa mtu mwenye tabia ya kuigwa, ni mfano mzuri kwetu sisi sote wa kuiga. Imani yake katika ukweli wa imani za msingi ilikuwa hautetereki. Subira, ari na uvumilivu wake wakati wa kukabiliana na mateso iliweka mfano mzuri kwa ajili ya wale wote ambao wangevumilia mateso kwa ajili ya ukweli. Baadhi ya maadui waasi walikata nyayo zake kwa sababu ya imani yake ya Shia, kama ambavyo nimekwishataja kwenye habari zake, lakini hakusitisha wala hata kuyumba au kuonyesha udhaifu wowote mpaka hatimaye alipokwenda njia yake (yaani, kufa), mvumilivu, imara na thabiti katika msimamo wake.

Mtoto wake Muawiyah pia alifuata nyayo zake – mtoto afaaye wa baba afaaye, na sio kuongeza chumvi kusema kwamba huyu mtoto alikuwa kama baba yake. Alikuwa mwanafunzi wa Imam Ja'far as-Sadiq na Imam Musa al-Kazim (a.s) na akawa mwenezaji wa mafundisho yao. Ameandika vitabu ambavyo vimetufikia kutoka kwa watu waaminifu. Ibn Abu Umayr na wengine kutoka miongoni mwa wasimulizi wetu wanasimulia hadithi kutoka kwake na miongoni mwa Sunni, Muslim na Nasa'i wamepokea hadithi kuhusu Hija kutoka kwake kupitia kwa Yahya ibn Yahya na Qutaybah. Muawiyah kwa upande wake amepokea hadithi kutoka kwa baba yake, Ammaar na baadhi ya wasimulizi wa rika lake, na hadithi hizi zinapatikana kwenye vitabu vya kuaminika vya Sunni. Alifariki mwaka wa 175 A.H. Mwenyezi Mungu amrehemu.

[127] Tazama *Tabaqat* cha Ibn Sa'd, seh. 5, uk. 381

**84. Ma'ruuf ibn Kharbuudh, al-Karkhi:**

Wengine wanasema kwamba jina la baba yake lilikuwa Firus. Au Firuzan au Ibn Ali. Dhahabi amemtaja kwenye kitabu chake *al-Miizan* pamoja na maoni kwamba mtu huyu alikuwa mkweli na alikuwa Shia. Bukhari, Muslim na Abu Dawuud wamebuni kifupi cha jina lake kuonyesha kwamba mara kwa mara wanafanya marejeo kwenye hadithi zake. Dhahabi pia anasema kwamba Ma'ruuf al-Karkhi alisimulia hadithi kutoka kwa Abu Tufayl ambapo Abu Aasim, Abu Dawuud, Ubaydullah ibn Musa na wengineo wamesimulia hadithi kutoka kwake. Mwandishi huyo huyo amenukuu kutoka kwa Abu Haatim kwamba alikuwa akiandika hadithi zake.

Aidha, Ibn Khalikan anasimulia kwenye kitabu chake "*Wafayaat"* kwamba mtu huyu alikuwa mmoja wa w atumishi wa Imam Ali ibn Musa al-Ridha (Imam wa nane wa Shia), na katika maelezo yake anaendelea kusimulia kwamba Ma'ruuf alisema: "Nilitafuta ukaribu na Mwenyezi Mungu na nikasusa kila kitu kwa ajili yake, isipokuwa kumtumikia bwana wangu, Ali ibn Musa al-Rida, (a.s)."

Ibn Qutaybah amemtaja Ma'ruuf miongoni mwa wasimulizi wa Kishia kwenye kitabu chake *Ma'arif*. Muslim amemwamini mtu huyu na hadithi zake zinazohusu Hija zinapatikana kwenye *Sahih Muslim* kama zilivyochukuliwa kutoka kwa Ibn Tufayl.

Ma'ruuf alifia Baghdad mwaka wa 200 A.H. na kaburi lake ni mahali panapojulikana sana kwa Ziara. Sirri al-Saqti alikuwa mmoja wa wanafunzi wake.

**85. Mansur ibn Mu'tamar, ibn Abdullah ibn Rabi'ah al-Salmi al-Kufi:**

Alikuwa mmojawapo wa wanafunzi wa Imam Baqir (a.s) (Imam wa tano) na Imam Sadiq (a.s) (Imam wa Sita) kama ilivyotajwa na mwandishi wa kitabu cha "*Muntaha al-Maqaal Fi-Ahwaal al-Rijaal*." Ibn Qutaybah kwenye *Ma'arif* yake anamuainisha mtu huyu kama Shia, na Jawzajaan anasema kwamba "imani yake ya kidini na matendo yake hayakubaliwi na watu walio wengi, sababu ya utiifu wake kwa watu wa Nyumba ya Muhammad (s.a.w.w.)."[128]

Kwa nini wasimulizi wakweli kama hawa wanaepukwa? Ni kwa sababu tu ya kwamba wao ni wafuasi wa **'vitu viwili vizito,'** au kwa sababu wanapanda kwenye "Safina ya Wokovu" au kwa sababu wanaingia "Jiji la Elimu kupitia kwenye Lango lake," Lango la Toba, au kwa sababu wanatafuta hifadhi kwenye 'Kimbilio la dunia yote' au kwa sababu wanamtii Mtume kwa kuwatukuza watoto wake, au kwa sababu wanalia kwa sababu ya kumwogopa Mola wao kama ilivyodhihiri kwenye habari za maisha yao (wasifu)? Ibn Sa'd anasema kuhusu Mansuur kwenye kitabu chake kiitwacho '*Tabaqat*' Jz. 6, uk. 235. "Macho yake yalivimba kwa sababu ya kulia sana kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu, na alikuwa akifuta machozi yake kwa kutumia shati lake la kitambaa cha kukwaruza, na inasemekana kwamba aliswali na kufunga saumu kwa muda wa miaka sitini!" Inawezekanaje nafsi za wachamungu namna hiyo kukataliwa? Lakini tunapaswa kushughulika na watu wasiopima mambo kwa haki. **"Kwa hakika, sisi tu wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea."**

Ibn Sa'd anasema kwenye maelezo ya habari za Mansuur kutoka kwa Hammaad ibn Zayd: "Nilimuona Mansuur kule Makka, ninafikiri kwamba mtu huyu ni *khashbi* na sioni kama si mkweli." Angalia jinsi watu hawa waheshimiwa ambavyo wamenasibishiwabdharau, dhihaka, tuhuma na uadui kiasi kwamba waandishi wa baadaye imewabidi kufutilia mbali mashaka hayo kuhusu watu hawa, kama vile kuwa na mapenzi na watu wa Nyumba ya Muhammad (s.a.w.w.) ndio inakuwa sababu ya kumfanya msimulizi awe sio mkweli. Hivyo kwamba imekuwa lazima ielezwe kwa umahususia katika kila hali kwamba msimulizi fulani ibn fulani hakuwa muongo. Maadui wa Ali (yaani, Manasibi) kamwe hawataji jina la mfuasi wa Aali

[128] "Kuna watu miongoni mwa wasimulizi kutoka Kufah ambao itikadi zao hazikubaliwi na watu. Hawa ni Abu Is'haq, Mansur, Zubayd al-Yaami, A'mash na wengine. Lakini hata hivyo, wanatagemewa kutokana na ukweli wao kama wasimulizi." (tazama maelezo ya Zubayd al-Yaami katika *Miizan*.) Nukuu hiyo hapo juu imechukuliwa kutoka kwa Juzjaan, ambaye anairudia katika maelezo yake kuhusu Zubayd, A'mash na Abu Ishaq. Maoni hayohayo yameelezwa hapa pamoja na rejea kwa Mansuur pia."

Muhammad bila kumuita majina yafuatayo: *Za'ah*, au *Khashbi*, au *Turabi* au *Rafidhi*. Washabiki hawa wa kidini inaonyesha hawajawahi kusikia aya hii ya Qur'ani isemayo: "**Wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli); majina mabaya baada ya kuamini kweli ni uovu.**" Ibn Qutaybah anaelezea maana ya "*khashbi"* kwenye kitabu chake *Ma'arif* kama ifuatavyo: "Ni marafidhi wakati ambapo Ibrahim al-Ashtar alipokutana na Ubaydullah ibn Ziyad kwenye uwanja wa vita, askari wa Al-Ashtar walibeba *khushub*[129] kwa hali hiyo ndio sababu wanaitwa *khashbi*; ni jina la utani ambalo linatokana na dharau, kejeli na chuki. Lakini *Khashbia* hawa waliwaua warithi wa Manasibi na kulipa kisasi kuuawa kwa watoto watakatifu wa Mtume kwa kummaliza kabisa Ibn Marjanah na kwa ukamilifu kuwanyamazisha kabisa wale waasi, wauaji wa dhuria wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w). **"Kwa hiyo sehemu ya chini ya watu waliofanya maovu walikataliwa mbali. Sifa zimwendee Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu."**

Kwa hiyo hakuna dhara katika sifa hiyo mbaya kutumiwa na maadui zao dhidi yao. Kwa kweli ni cheo cha heshima kubwa kwa mtu yeyote kuitwa mlipiza kisasi wa damu isiyo na hatia ya watoto wa Mtume (s.a.w.w.). Kadhalika kuhusu madhara katika kuitwa *Turabiyah* kwa sababu ya fungamano na *Abu Turab* (Imam Ali) cheo mbacho alipewa Imam Ali na Mtume. Kinyume chake, ni heshima na fahari kufananishwa hivyo.

Lakini tukirejea kwenye mada ya mazungumzo yetu, kuna kukubaliana wote kwa pamoja juu ya maoni kuhusu kutegemewa kwa Mansuur, kwa hiyo ni kwamba waandishi wote wa vitabu sita vya *Sahih* ambao ni Sunni wameweka mategemeo yao juu ya mtu huyu na waandishi wengine wastahiki wamefanya hivyo pamoja na kujua kwao kwamba mtu huyu alikuwa Shia.

Zaidi ya hayo, hadithi zake zimeandikwa kwenye *Sahih Al-Bukhari* na *Sahih Muslim* kupitia kwa Abu Waail, Abu Dhuha, Ibrahim al-Nukhai na wengineo wa rika lao, ambapo Sha'bah, Al-Thawri, Ibn Uyaynah, Hammad ibn Zayd na watu wengine wasomi wa kizazi hicho hicho chao wamejifunza hadithi kutoka kwa mtu huyu kama walivyokubali Bukhari na Muslim.

Ibn Sa'd anasema kwamba Mansur alifariki mwishoni mwa mwaka wa 132 A.H. na anaongezea, "alikuwa msimulizi wa kutegemewa na muaminiwa wa hadithi nyingi na mtu wa maadili na tabia nzuri." Mwenyezi Mungu amrehemu.

**86. Minhaal ibn Amr al-Kufi:**

Alikuwa *Tabi'ina* mashuhuri na Shi'a, alikuwa akiishi Kufah. Hii ndio sababu iliyomfanya Jawzajaan kumuainisha mtu huyu kama 'dhaifu' akisema: "Ni mfuasi wa itikadi mbaya." Na Ibn Hazm na Yahya ibn Sa'id wanaidhinisha fikra hii. Ahmad ibn Hanbal anasema: "Ninampendelea Abu Bishr kuliko Minhaal, na ni wa kutegemewa zaidi." Anasema haya akijua fika kwamba alikuwa Shia na shughuli zake wakati wa Mukhtar,[130] lakini hata hivyo hawasababishi shaka kuhusu kuaminika kwa hadithi zake. Sha'bah, Mas'udi, Hajjaj ibn Artat na wengine wa kizazi hicho wamechukua hadithi kutoka kwake, na Ibn Mu'in, Ahmad al-Ajali na wengineo wamemthibitisha kwa uaminifu wake. Dhahabi amemtaja mtu huyu kwenye *Miizan* yake na alisimulia yote yale ambayo yamezungumzwa hapo juu kuhusu yeye, ambapo Bukhari na Muslim wamebuni kifupi cha jina lake, inaonyesha kwamba marejeo mengi hufanywa mara kwa mara kwenye hadithi za mtu huyu. Hadithi yake imeandikwa kwenye *Sahih al-Bukhari* kutoka kwa Sa'id ibn Jubayr, na pia kwenye sura ya Tafsiri (*Tafsir*) hadithi yake imesimuliwa na Zayd ibn Abu Aniisah, na katika sura kuhusu Mitume imo hadithi kama ilivyosimuliwa na Mansur ibn Mu'tamar.

**87. Musa ibn Qays, al-Hadhrami (Anafahamika kama Abu Muhammad):**

[129] Khushab huenda ina maana ya silaha zao, kama vile panga, pinde na mishale ambayo imechongwa vibaya na sio nzuri katika kumalizia kwao.

[130] Mukhtar ibn Abu Ubaydah al-Thaqafi; ambaye alinyanyua bango la uasi nchini Iraq dhidi ya Banu Umayyah na akawauwa wengi katika wale waliomuuwa Imamu Husein (a.s) kule Karbala.

Aqiili anamhesabu miongoni mwa rafidhi waliopindukia. Wakati mmoja Sufyan alimuuliza yeye kuhusu Abu Bakr na Ali, na alitoa jibu lifuatalo. "Ali ni mpendwa wangu zaidi." Anasimulia kutoka kwa Salmah ibn Kuhayl, ambaye alisikia kutoka kwa Ayadh ibn Ayadh ambaye alisikia kutoka kwa Maalik ibn Ju'unah, ambaye alisema: "Nilimsikia Umm Salmah akisema, "Ali yupo pamoja na haki, kwa hiyo yeyote amfuataye yeye anafuata haki na yeyote anayemkimbia anaikimbia haki, licha ya ahadi yenye taadhima." Fadhl ibn Dakiin amesimulia hili kutoka kwa Musa ibn Qays. Aidha, Musa amesimulia hadithi za kweli kuhusu ubora wa Ahlul-Bayt. Kwa hiyo Aqiil ana makosa katika kutengeneza hukumu hiyo aliyoitoa. Ibn Mu'in alimkubali Musa, na Abu Dawuud na Sa'id ibn Mansur waliweka misingi ya hoja zao kwenye hadithi zake zilizomo kwenye Sunan zao. Dhahabi ametoa maelezo na habari zake kwenye *Miizan* yake akieleza yote yaliyosemwa hapo juu. Zaidi ya hayo, hadithi zake zimo kwenye Sunnan kupitia kwa Salmah ibn Kuhayl na Hajr ibn Aniisah, ambapo Fadhl ibn Dakiin, Ubaydullah ibn Musa na wasimulizi wengine wa kuaminika wamesimulia hadithi zake. Alifariki wakati wa utawala wa Mansur (Khalifa wa Bani Abbasi). Mwenyezi Mungu amrehemu Musa ibn Qays.

**88. Nafi'i ibn Harith, Abu Dawuud al-Nakhai al-Kufi al-Hamadani al-Sabii:**

Aqiili anasema: "Alikuwa rafidhi mwenye kupindukia" na Bukhari anaeleza: "Ushia wake unazungumzwa sana." Lakini Sufyan, Hamam, Shariik na watu wengine kadhaa wasomi wa kizazi hicho wamechukua hadithi kutoka kwake. Tirmidhi ametegemeza hoja zake juu ya hadithi za Nafi'i kwenye *Sahih* yake, na waandishi wa Musnad wemetegemea hadithi zake. Hadithi zake zimeandikwa kwenye *Sahih Tirmidhi* na vitabu vingine kutoka kwa Anas ibn Malik, Ibn Abbas, Imran ibn Hasiin na Zayd ibn Arqam. Dhahabi amesimulia mambo yote yaliyokwisha semwa hapo juu kuhusu mtu huyu.

**89. Nuh ibn Qays, ibn Ribah al-Hadani al-Tahi al-Basri:**

Dhahabi anamueleza mtu huyu kwenye kitabu, *al-Miizan*, "Msimulizi mzuri;" anaongezea zaidi kwamba Ahmad na Ibn Mu'in wanamuona mtu huyu kama mwaminifu na Abu Dawuud anasema kwamba alikuwa Shi'a, ambapo Nasa'i anasema: "hakuna dosari kwa mtu huyu." Dhahabi amebuni kufupi cha jina lake inaonyesha kwamba Muslim na waandishi wa *Sunan* wameingiza hadithi zake kwenye vitabu vyao vya kuaminika. Hadithi moja iliyosimuliwa na mtu huyu imenukuliwa kuhusu mada ya 'Vinywaji' kwenye *Sahih Muslim* ambayo ameisimulia kutoka kwa ndugu yake Khalid ibn Qays. Hadithi za mtu huyu zimepatikana kwenye *Sahih Muslim* kupitia kwa Nasr ibn Ali na kwenye vitabu vingine kupitia kwa Abu al-Ash'ath na wengineo wa kizazi hicho; na Nuh anazo kupitia kwa Ayub, Amr ibn Malik na wengine.

**90. Harun ibn Sa'd, al-Ajali al-Kufi:**

Dhahabi amemtaja mtu huyu na Muslim amebuni kifupi cha jina lake, kwa kuonyesha kwamba yeye ni mmoja wa mabingwa ambaye amechukua hadithi kutoka kwake huyu na amemsifu kama ifuatavyo: "Kama mwanamume, alikuwa mkweli lakini alikuwa rafidhi aliyechukiwa." Abbas anasimulia kwa ushahidi wa Ibn Mu'in kwamba Harun ibn Sa'd alikuwa Shi'a wa kupindukia. Anasimulia kutoka kwa Abd al-Rahman ibn Abu Sa'id al-Khudri ambapo wale anaosimulia kutoka kwake ni pamoja na Abdurahman mtoto wa Abu Sa'id al-Khudri aliyekuwa sahaba wa Mtume (s.a.w.w.), Ibn Abu Hafs al-Attar, Mas'udi na Hasan ibn Hayy. Abu Haatim anasema: "Hakuna upinzani kwa mtu huyu… Kumbuka ile hadithi kutoka kwake ikielezea kuhusu Jahannamu, kama ilivyoandikwa kwenye *Sahih Muslim* ambayo imesimuliwa kupitia kwa Hasan ibn Saalih, ambaye alisimulia kutoka kwa Harun ibn Sa'id, kutoka kwa Hadhrat Salman.[131]

[131] Salman Farsy alikuwa mmoja wa masahaba mashuhuri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w)

**91. Hashim ibn al-Burayd ibn Zayd (Abu Ali al-Kufi):**

Dhahabi amemtaja mtu huyu, na Abu Dawuud na Nasa'i wamebuni kifupi cha jina lake, hapo ikionyesha kwamba amekubalika kama mmoja wa wasimulizi wa mkusanyiko wa *Sahih* zao. Dhahabi anakubali uaminifu wake kwa ushahidi wa Ibn Mu'in na wengineo, ambapo anakubali kwamba alikuwa rafidhi, na kwamba Ahmad (Ibn Hanbal) hana upinzani wowote kwa mtu huyu. Hashim anasimulia hadithi kutoka kwa Zayd ibn Ali.[132] na Muslim al-Batiin, ambapo wale wanaosimulia kutoka kwake ni pamoja na al-Khariibi na mtoto wa kiume wa Hashim, Ali ibn Hashim (ambaye ametajwa kwenye namba 68 hapo juu) na kundi la watu mashuhuri. Hashim alitokea familia ya Kishia iliyojulikana sana kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu kuhusu Ali ibn Hashim.

**92. Hubayrah ibn Bariim, al-Humayri:**

Sahaba wa Ali (a.s) (Imam wa Kwanza), mapenzi yake kwa Ali na walio karibu naye Amirul-Muminin ni sawa na Haarithi. Dhahabi amemtaja mtu huyu na waandishi wa *Sunan* wamebuni kifupi cha jina lake, kuonyesha kwamba wamemjumuisha mtu huyu miongoni mwa vyanzo vyao, Dhahabi pia amenukuu maoni ya Ahmad Ibn Hanbal: "Hakuna kasoro yoyote kwa mtu huyu kama msimulizi na anapendelewa zaidi ya Harith." Anaendelea kunukuu Dhahabi, "Ibn Kharraash anamuona mtu huyu kuwa 'dhaifu' kwa sababu alijiunga na jeshi la Ali kwenye vita vya Sufin." Jawzajaan anasema: "Alikuwa mfuasi wa Mukhtar,[133] akiwa amejiunga na walipiza kisasi kwenye Vita vya Khaazir," Shahristani, kwenye kitabu chake "*Milal wa al-Nihal,"* amemjumlisha mtu huyu na Mashia na hapana shaka kwamba alikuwa Shi'a. Hadithi zake zilizotoka kwa Ali zimeandikwa kwenye vitabu vya *Sunan*. Abu Is'haq na Abu Fakhtah ni miongoni mwa wale waliomsikia na kukariri hadithi hizo zilizotoka kwake.

**93. Hisham ibn Ziyad, (Abu al-Miqdaam al-Basri):**

Shahristani, kwenye kitabu chake *al-Milal wa al-Nihal,* amemjumuisha mtu huyu miongoni mwa Mashia. Dhahabi anamtaja yeye kwa jina kwa kutumia hefuri 'H' na pia kwa jila lake la Ubaba; Abu al-Miqdaam kwenye kitabu cha *Miizan*, na kubuni kifupi cha jina la mtu huyu *T, Qaf*, inayoonyesha kwamba waandishi wa *Sunan* walikuwa wanamwamini. Aidha, hadithi zake pia zinapatikana kwenye *Sahih Tirmidhiy* na wengineo kutoka kwa Hasan na al-Qardhi, ambapo wale ambao walikariri hadithi walizozisikia kutoka mdomoni mwake ni pamoja na Shaybani ibn Farukh, al-Qawariiri na wasimulizi wengine kadhaa.

**94. Hisham ibn Ammar, ibn Nasir ibn Maysarah (Abu al-Waliid):**

Kwa mujibu wa Al-Zafari al-Damishqi, alikuwa mwalimu wa Bukhari na imekubalika kama hivyo kwenye *Sahih*. Ibn Qutaybah amemuorodhesha mtu huyu miongoni mwa wasimulizi wa Kishia kwenye sura ya 'Madhehebu' katika kitabu chake *al-Ma'arif* ambamo amewataja baadhi yao. Dhahabi pia amemtaja kwenye kitabu chake *al-Miizan*, akimweleza mtu huyu kama Imamu wa Swala, khatwibu, msomaji wa Qur'ani, msimulizi fasaha wa hadithi, mwanachuo na mtu mkweli, ingawaje ana mapungufu yake…"

Bukhari amekariri hadithi alizojifunza moja kwa moja kutoka kwake chini ya kichwa cha habari 'Uuzaji' kwenye *Sahih* yake na kwenye sehemu zingine za kitabu, kama wasomaji wake wajuavyo vizuri. Najua kwamba hadithi zake zimeandikwa chini ya kichwa cha habari 'vita' 'vinywaji' na 'Sifa za masahaba wa Mtukufu Mtume.' Hisham anarudia hadithi alizojifunza kutoka kwa Yahya ibn Hamzah, Sadaqa ibn Khalid na Abdul Hamiid ibn Abdul Ushriin na wengine. Dhahabi anaendelea kusema kwenye *Miizan* yake: "Idadi kubwa ya watu wamesimulia kutoka kwa mtu huyu. Walikuwa wakija kutoka masafa marefu

[132] Zayd yule shahid (aliyekufa kifo cha kishahidi), ambaye kwaye madhehebu ya Zaydiyah wanachukuwa imani yao.
[133] Mukhtar ibn Abu Ubaydah al-Thaqafi (angalia tanbihi na. 35 hapo juu)

kwa makusudi ya kujifunza ufundi wa kusoma Qur'ani na kusikia hadithi kutoka kwake." Waliid ibn Muslim amesimulia hadithi kutoka kwake na alikuwa Sheikh wake; alipata ruhusa ya kusimulia hadithi kutoka kwa Ibn Lahii'ah. Abdaan anasema: "Hapakuwepo na mtu kama yeye hapa duniani." Mwanachuo mwingine anasema: "Hisham alikuwa msemaji fasaha, mwingi wa hoja za msingi na alikuwa na pumzi nyingi (wakati anasoma Qur'ani) na alikuwa na ujuzi mwingi." Aliamini maneno ya Qur'ani kwamba yaliumbwa na sio ya rika na Mwenyezi Mungu, maoni ambayo yanashikiliwa na Mashia wengine.

Ahmad ibn Hanbal anarejea kwenye hilo anaposema (kama ilivyoandikwa kwenye *Miizan*), "Nilimjua mtu huyu alikuwa na hasira sana. Mungu na amuuwe." Ahmad ibn Hanbal wakati mmoja alisimama kwenye kifungu cha maneno katika maandishi yaliyoandikwa na Hisham ambapo paliandikwa: "Sifa zote ni Zake Mwenyezi Mungu ambaye amejidhihirisha kwa njia ya uumbaji Wake." Hapa, Ahmad alisimama wima, aliunguruma na kuwaka kwa hasira na kuamuru wote wale ambao waliswali chini ya uongozi wa Hisham kuswali tena (kwani alizichukulia swala hizo kuwa ni batili), kwa sababu Hisham alikuwa anaamini kwamba Mungu haonekani, hafananishwi na yuko huru kutokana na hali zozote na hana mwanzo wala mwisho na alikwishatukuza dalili Zake miongoni mwa uumbaji Wake. Inaeleweka wazi kwa wanafalsafa kwamba maoni ya Hisham yaliegemezwa tu kwenye usemi wa uhakika wa theolojia. "Dalili za Mwenyezi Mungu zimo kwenye vitu vyote, ingawa Yeye ni Mkubwa na Mbora na wa juu zaidi kwa kila kimoja chao." Lakini wanachuo wa vizazi mbali mbali wameshikilia maoni tofauti tofauti kufuatana na utafiti wao. Hisham alizaliwa mwaka wa 153 A.H. na alifariki mwishoni mwa Muharram, mwaka wa 245 A.H.

**95. Hashim ibn Bashir, ibn Qasim ibn Diinar al-Salmi al-Wasiti (Jina la ukoo ni Abu Muawiyah):**

Kwa asili alitokea Balkh. Babu yake Qasim alikuja Wasit kwa madhumuni ya biashara. Ibn Qutaybah, kwenye kitabu chake *Ma'arif*, anamweka mtu huyu miongoni mwa Shi'a; alikuwa mwalimu wa Imam Ahmad ibn Hanbal na wote wa rika lake. Dhahabi anatumia kifupi cha jina la mtu huyu kuonyesha kwamba wakusanyaji wa vitabu sita vya *Sahih* wamemtegemea na amemweleza kuwa na cheo cha *hafidh* (aliyehifadhi Hadith kwa moyo). Halafu anaendelea kusema: "Alikuwa mmoja wa wanachuo wakubwa." Alijifunza hadithi kutoka kwa al-Zuhri na Hasiin ibn Abd al-Rahman. Yahya al-Quttaan, Ahmad, Yaqub ad-Dawraqi na idadi kubwa ya wasimulizi wamesimulia hadithi walizojifunza kutoka kwake. Hadithi zake zinapatikana kwenye *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim* kama zilivyosimuliwa na Hamiid al-Tawiil, Isma'il ibn Abu Khalid, Abu Ishaq al-Shaybani na wengine; na pia kutoka kwa Amr al-Naqid, Amr ibn Zararah, Sa'id ibn Sulayman; na kwenye Bukhari tu, kutoka kwa Amr ibn Awf, Sad ibn Nadhr, Muhammad ibn Nabahaan, Ali ibn al-Madiin na Qutaybah; na kwenye Muslim tu, kutoka kwa Ahmad ibn Hanbal, Shurayh, Yaq'uub al-Dawraqi Abdullah ibn Mutii, Yahya ibn Yahya, Sa'id ibn Mansur, ibn Abu Shaybah, Ismail ibn Salim, Muhammad ibn al-Sabah, Dawuud ibn Rashiid, Ahmad ibn Mani'i, Yahya ibn Ayub, Zuhayr ibn Harb, Uthman ibn Abu Shaybah, Ali ibn Hajar na Yazid ibn Harun. Alifia Baghdad mwaka wa 183 A.H. akiwa na umri wa mika 79. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**96. Wakii ibn al-Jarrah, ibn Maliih ibn Adi:**

Alipewa jina la ukoo kama baba wa Sufyan al-Rawaasi al-Kufi. Ibn Qutaybah amemuorodhesha kwenye kitabu *al-Ma'arif* miongoni mwa Mashia, na hivyo hivyo amefanya Al-Madini kwenye kitabu chake *Tahdhib*, akisema kwamba Wakii alikuwa mfuasi wa Shia. Marwan ibn Muawiyah hakuweza kupuuza ukweli kwamba Wakii alikuwa rafidhi; Yahya ibn Mu'in, alipomtembelea siku moja, alimuona na kibao kilichokuwa kimeandikwa majina mengi na maoni kuhusu majina hayo, na kwenye kibao hicho alisoma jina la Wakii na maelezo ya kuonyesha kuwa ni rafidhi. Ibn Mu'in alimuambia: "Wakii alikuwa bora kuliko wewe." "Bora kuliko mimi? Marwan ibn Muawiyah aliuliza kwa mshangao. "Ndio," alimjibu. Ibn Mu'in anasema: "Wakati kadhia hii iliposimuliwa kwa Wakii alisema, 'Yahya ni rafiki yetu.'"

Ahmad ibn Hanbal, alipoulizwa kama Wakii na Abd al-Rahman walikuwa tofauti na hayo tuliyoyasema alirejea kwenye riwaya ya Abd al-Rahman kuhusu tukio lililotajwa hapo juu, akiongezea kwamba wote wa kabla yake waliridhika na maarifa ya Abd al-Rahman isipokuwa Wakii ibn Al-Jarrah. Maandishi haya yanathibitishwa na Dhahabi kwenye maelezo yake kuhusu Hasan ibn Saalih ambapo anamsimulia Wakii akisema: "Ninamchukulia Hasan ibn Saalih kama Imam (Kiongozi)," na alipoambiwa kwamba Hasan hakuonyesha huruma kwa Uthman, alisema: Wewe unamhurumia Hajaj?" Hivyo alimlinganisha Uthman na Hajaj yule dhalimu.

Dhahabi amemtaja mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Miizan*, akisimulia mambo yaliyopita kuhusu yeye. Waandishi wote wa vitabu sita viitwavyo *Sahih* na wengine wengi wamemtegemea. Vitabu vya *Sahih al-Bukhari* na *Sahih Muslim* vina hadithi zake kama zilivyochukuliwa kupitia kwa A'mash, Al-Thawri, Sha'ba, Isma'il ibn Abu Khalid, Ali ibn Mubarak, Is'haq al-Hanzali na Muhammad ibn Namiir. Aidha, wasimulizi kwenye *Bukhari* ambao wamesimulia hadithi zake ni pamoja na Abdullah al-Hamidi, Muhammd ibn Salam, Yahya ibn Ja'far ibn A'yun, Yahya ibn Musa na Muhammad ibn Maqatil, ambapo kwenye *Muslim* ni pamoja na Zuhayr, Ibn Abu Shaybah, Abu Kurayb, Abu Sa'id al-Ashajj, Nasr ibn Ali, Sa'id ibn Azhar, Ibn Abu Umar, Ali ibn Khashram, Uthman ibn Abu Shaybah na Qutaybah ibn Sa'id. Alifia huko Fayd wakati anarudi kutoka Hija, Muharram mwaka wa 97 A.H. akiwa na miaka 68. Mwenyezi Mungu amrehemu.

**97. Yahya ibn al-Jazzar, al-Arani al-Kufi, (Mwanafunzi wa Amirul-Muminin (a.s):**

Dhahabi amemtaja mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Miizan* na amebuni kifupi cha jina lake kuonyesha kwamba Muslim na waandishi wa *Sunan* wamemtegemea. Anathibitisha ukweli wake na anasimulia kutoka kwa Hakam ibn Utaybah, ambaye amesema: "Yahya ibn al-Jazzar alikuwa Shi'a wa kupindukia." Ibn Sa'd pia amemtaja mtu huyu kwenye kitabu chake kiitwacho *Tabaqat* (Jz. 6, uk. 206) anasema: Yahya ibn al-Jazzar alikuwa Shia na aliongea kwa hamasa sana. Hata hivyo, wanasema kwamba alikuwa mwaminifu na amesimulia hadithi kadhaa."

Nimeona hadithi ambayo imesimuliwa na mtu huyu kutoka kwa Hadhrat Ali (a.s) kuhusu mada ya Swala kwenye *Sahih Muslim* na nyingine kuhusu mada ya imani ya kweli iliyosimuliwa na yeye kutoka kwa Abd al-Rahman ibn Abu Layla kwenye kitabu hicho hicho. Miongoni mwa wale wanaosimulia kutoka kwake kwenye *Sahih Muslim* ni Hakam ibn Utaybah na Hasan al-Arani.

**98. Yahya bin Said al-Quttan:**

Jina la ukoo Abu Said, aliyekuwa mtumwa wa Banu Tamiim wa Basrah. Alikuwa msimulizi wa Hadithi katika umri wake. Ibn Qutaybah amemuorodhesha mtu huyu kwenye kitabu chake *al-Ma'arif* miongoni mwa Shi'a. Hata hivyo, waandishi wa vitabu sita viitwavyo *Sahih* wamemtegemea na wengine pia wamefanya hivyo. Hadithi yake kama ilivyopatikana kupitia kwa Hishaam ibn Urwah, Hamiid al-Tawiil, Yahya ibn Sa'id al-Ansari na wengineo imehakikishwa kwenye vitabu vyote viwili *Sahih Muslim* na *Sahih al-Bukhari* kuwa ni kweli. Wale ambao wamerudia vile walivyosikia kutoka kwake kwenye vitabu vyote viwili ni pamoja na Muhammad ibn al-Muthanna na Bindaar; ambapo kwenye *Bukhari* ni pamoja na Musaddad, Ali ibn al-Madiini na Bayan ibn Amr na kwenye *Muslim*, Muhammad ibn Hatam, Muhammad ibn Khilad ul-Bahili, Abu Kamil Fudhayl ibn Husayn al-Jahadar, Muhammad al- Muqadammi, Abdullah ibn Hashim, Abu Bakr ibn Abu Shaybah, Abdullah ibn Said, Ahmad bin Hanbal, Yaq'uub al-Dauraqi, Abdullah al-Qawariiri, Ahmad ibn Abdah, Amr ibn Ali na Abd al-Rahman ibn Bishr. Alifariki mwaka wa 198 A.H. akiwa na umri wa miaka 78, Mwenyezi Mungu amrehemu.

**99. Yazid ibn Abu Ziyad, al-Kufi:**

Jina la ukoo Abu Abdullah, mtumwa wa Banu Hashim. Dhahabi amemtaja mtu huyu kwenye *Miizan* yake, na Muslim na waandishi wanne wa *Sunan* vilevile wametumia kifupi cha jina lake kuonyesha kuzitumia hadithi zake mara kwa mara. Dhahabi ameendelea kumnukuu Ibn Fudhayl, ambaye amesema: "Yazid ibn Abu Ziyd alikuwa mmoja wa viongozi mashuhuri wa Shia." Dhahabi amekubali kwamba mtu huyu alikuwa mwanachuo mashuhuri wa Kufah. Lakini pamoja na sifa zote hizo amekuwa akishambuliwa kila mara pamoja na kudharauliwa kwa sababu ya hadithi aliyoisimulia kutoka kwa Abu Barzah (au Abu Bardah) ambayo kwayo Dhahabi amesema kwamba: "Tulikuwa tumeketi na Mtukufu Mtume aliposikia sauti ya muziki, wakati Amr ibn al-Aas na Muawiyah walikuwa wanafanya karamu (sherehe) ya ulevi. Hapo hapo Mtukufu Mtume (ambaye alikuwa ameharamisha muziki) alisema: 'Ee Mwenyezi Mungu wahukumu wawili hawa na uwatupe kwenye Moto wa Jahanam." Pia amesimulia hadithi yenye mada kuhusu 'Chakula' ambayo imeandikwa kwenye *Sahih Muslim* kupitia kwa Abd al-Rahman ibn Abu Layla, ambaye alisikia kutoka kwa Sufyan ibn Uyaynah. Alifariki akiwa na umri wa miaka 90 mnamo mwaka wa 136 A.H. Mwenyezi mungu amrehemu.

**100. Abu Abdullah al-Jadali:**

Dhahabi amemtaja kwa jina lake la ubaba (jina lake mwenyewe hasa likiwa halijulikani kwa uhakika) na amebuni kifupi cha "D-T" kwa jina lake kuonyesha kwamba mtu huyu ni mmoja wa wasimulizi ambao wametegemewa na Abu Dawuud na Tirmidhi kwenye vitabu vyao viitwavyo *Sahih*. Anaendelea kumwelezea yeye kama "Rafidhi anayechukiwa" na anamnukuu Jawzajaan, ambaye anaamini kwamba alikuwa mbebaji bendera wa Mukhtar na pia anaamini ukweli wake kutokana na uthibitisho wa Ahmad (ibn Hanbal). Shahristani anamuanisha mtu huyu miongoni mwa Shia kwenye kitabu chake kiitwacho *Mila wa al-Nihal*, na ibn Qutaybah anamhesabu miongoni mwa 'rafidhi shupavu' katika *al-Ma'arif* yake.

Aidha, hadithi zake hupatikana kwa Tirmidhi na Abu Dawuud na *Musnad* zote za Ahlu Sunnah. Ibn Sa'd anamtaja katika kitabu chake kiitwacho *Tabaqat* Jz. 6, uk. 159, wakati jina lake linatajwa kama Abdah ibn Abd ibn Abdullah ibn Abu Ya'mir. na anasema: "Alikuwa shabiki mkubwa wa Shia". Watu wanasema kwamba alikuwa askari wa mbele wa Mukhtar ambaye alimuamuru kumshambulia Abdullah ibn Zubayr na askari mia nane; na alimlinda Muhammad ibn Hanafiyah kutokana na mpango wa Ibn Zubayr, kwa vile Ibn Zubayr alikuwa amemzingira Ibn Hanafiyah na Banu Hashimu wengine na alikuwa anapanga mkakati wa kuchoma moto ngome yao kwa sababu walikataa kutoa kiapo cha utii kwa Ibn Zubayr. Abu Abdullah al-Jadali, hata hivyo, aliwaokoa kutokana na janga hilo. Mwenyezi Mungu amlipe thawabu nzuri kwa kufungamana kwake na Mtume.

Hii inatufikisha mwishoni mwa mazungumzo yetu ya haraka, na taarifu yangu ambayo takriban yote ni kutoka kwenye kumbukumbu, kuhusu wasimulizi wa hadithi wa Kishia ambao wameaminiwa na waandishi mashuhuri wa Sunni. Wasimulizi mia moja wa namna hiyo wamezungumziwa habari zao katika barua hii. Wao ni mashujaa wa Kishia ambao wamekubaliwa kama vyanzo sahihi na Masunni; Wao ni chemchem za elimu ya Uislamu, wahifadhi wa hadithi za Mtukufu Mtume. Vitabu vya *Sahih, Musnad*, na *Sunan* vimetegemea juu ya riwaya zao. Nimewataja watu hawa kwa majina yao kamili na kutaja marejeo kutoka kwa waandishi wa Sunni ambao wamekiri kuambatana kwao na Ushia na bado waliwategemea, na nimeonesha rai za waandishi katika kila suala.

Baada ya kufanya hivyo, ninafikiri wale wakosoaji wangu watakubali makosa yao ya kudhani kwamba "waandishi wa Sunni hawakubali kuchukua hadithi zilizosimuliwa na Mashia." Sasa waelewe kwamba kigezo cha kuaminika kwa msimulizi ni ukweli wake. Unyofu wake na uaminifu wake, na sio kwa sababu yeye ni mfuasi wa madhehebu ya Sunni au Shia. Kwa hiyo, inaweza ikasemwa kwamba kama riwaya za wasimuliaji

wa Shia zingeachwa, hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) karibu zote zingetoweka – kama alivyokiri hilo Dhahabi -. Lakini unajua (Mwenyezi Mungu asaidie Ukweli kupitia kwako) kwamba miongoni mwa vizazi vya awali vya Shia, wapo wasimulizi wengi ambao walikuwa wakitegemewa na waandishi wa Sunni, mbali na hawa niliowataja hapa. Orodha kamili ya wasimulizi hao itakuwa na mamia kadhaa zaidi kuliko hii iliyotajwa hapo juu ya watu mia moja tu, wasimuliaji wenye uadilifu wa kiwango cha juu, idadi kubwa ya hadithi, ujuzi mpana, walioishi karibu na wakati wa Mtume na ambao ni imara zaidi kwenye itikadi yao ya Ushia kuliko wale ambao wametajwa hapa. Ni Mashia kutoka miongoni mwa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe, Mwenyezi Mungu na awaridhie wote hao.

Nimetaja majina ya baadhi ya hawa 'masahaba' mwishoni mwa kila mazungumzo muhimu na pia majina ya *'Tabi'in* kutoka miongoni mwa Mashia, ambao juu yao waandishi wenu wametegemea. Kila mmoja wao ni mwaminifu, wakiwa na kumbukumbu nzuri, waliojaa ufahamu mwingi, madhubuti katika itikadi na mabingwa, kwa mfano, wale waliopata kufa kishahidi kwa ajili ya dini wakati wanamsaidia Amirul Muminin (a.s) kwenye vita ndogo na vita kubwa vya Jamal na vya Sufin na Nahrwan; vile vya Hijaz na Yemen, wakati Basr ibn Artah alipoongoza mapambano katika maeneo mawili hayo; katika machafuko na uasi wa Hadhramut ambao ulienea kuelekea Basrah kwa uchochezi wa Muawiya; na kama mfano mkubwa kabisa, zile nafsi tukufu za watu waliokufa kama mashahidi wakati wakimhami Mfalme wa Vijana wa Pepo, Husein katika siku hiyo ya Karbala; au wale waliopata shahada wakati wanamhami mjukuu wa Husayn, Zayd ibn Ali, au wale waliotaka kulipa kisasi cha damu ya kizazi cha Muhammad kama kitendo cha utii; au waliokutana na kifo kwa subira, wakati wakiteswa na kulazimishwa kuhama nyumba zao; au wale waliolazimika kuficha utii wao kwa sababu ya kuhofia udhaifu wa miili yao kama vile Ahnaf ibn Qays, Asbagh ibn Nabaatah na Yahya ibn Ya'mur (mtu wa kwanza kutumia vidoti kwenye herufi za alfabeti). Khalil ibn Ahmad, mtu wa kwanza katika sanaa za kamusi, arudhi (sauti za mashairi) mizani (za mashairi), au Ma'adh ibn Muslim al-Harra', mtu wa kwanza kukusanya kanuni za sarufi na elimu ya kupanga maneno kwa sarufi.

Mazungumzo kuhusu maisha ya watu hawa yangeweza kujaza vitabu vingi vikubwa. Nakurejesha kwenye shutuma zilizofanywa dhidi yao na Manasibia (wale ambao chuki dhidi ya Ali ni sehemu ya dini yao), matokeo yake waandishi wa Sunni wamekataa hadithi zilizosimuliwa na wao. Wamo mamia juu ya mamia ya wasimulizi wenye kumbukumbu nzuri na wabebaji wa bendera za mwongozo kutoka miongoni mwa Mashia wa kizazi cha Muhammad, ambao Ahlu Sunah wamewaweka katika hali ya kusahauliwa, lakini wanachuoni wa Shia wamekusanya na kutengeneza orodha na enklopidia za wasifu zenye maelezo ya maisha yao. Kwa kuvisoma vitabu hivi unaweza ukafahamu matendo yao yanayong'ara katika huduma ya *Shari'ah* za 'Dini sahihi ya kuheshimika ya Uislamu'. Mtu yeyote anayetafakari yale yaliyomo humo atawaelewa kuwa ni mifano ya kweli na uaminifu, utii na uchamungu, kazi ya uaminifu katika kutoa ushauri mzuri kwa ajili ya Mungu Mwenye Enzi na kwa ajili ya Mjumbe Wake – rehema na amani ya Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na Kizazi chake – na kwa Kitabu chake kitakafitu, Qur'ani na kwa ajili ya Maimamu wa Waislamu na kwa ajili ya Umma wote. Mwenyezi Mungu atunufaishe kwa wingi wa ukarimu wao na kwa ukarimu wenu pia, kwani Yeye ni Mwingi wa Rehema.

Wassalaam,

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 17

## DHUL-HIJJAH 3, 1329 A.H.

**I. Kushukuru Upole wa Mjadili,**

**II. Kukubali Ukweli kwamba Hakuna Sababu kwa nini Sunni Wasitegemee Riwaya za Wanachuo wa Kishia,**

**III. Kuamini kwake Aya Zinazowahusu Ahlul-Bayt,**

**IV. Mshangao Katika Kulinganisha Kati ya Haya na Yanayoaminiwa na Waislamu.**

Napenda nikuhakikishie kwamba kamwe bado sijakutana na bongo safi, au uelewa mwepesi, akili makini mno, muono wa kina cha mbali, hali ya kiungwana yenye kujizuia, mwenye mfumo tulivu wa majadiliano kuliko wewe. Umepiga mbizi kwenye mapango ya ndani kabisa ya nafsi yangu kwa majibu yako yote, na umemiliki katika mazungumzo yako yote macho, masikio, ulimi na moyo. Na kuhusu barua yako ya mwisho, yale ni maandishi ambayo hapana shaka ndani yake yameshusha macho ya wenye hekima na busara, na yameinamisha vichwa vya wapotoshaji kwa ukweli uliomo ndani mwake.

Sunni hana tena sababu ya kutotegemea riwaya za ndugu yake Shia kama msimuliaji huyo ni muaminifu na mkweli. Maoni yako katika suala hili ni ukweli uliodhihirishwa, na kwamba maoni ya kinyume na haya sio chochote zaidi ya chuki na muono wa akili finyu. Wanachokisema juu ya kutotegemewa kwa wasimuliaji wa ki-Shia hukinzana na wanayoyafanya haswa, na vitendo vya ulamaa wao katika kuchagua wasimulizi havilingani na utetezi wao kuhusiana na hili. Matendo ya wasimulizi wao yamekuwa kinyume na kanuni hii isiyo na msingi ambayo wanaipendekeza, na wameshindwa kuthibitisha hoja yao wakati ambapo wewe umethibitisha ya kwako. Kwa muda mfupi kiasi hiki umekusanya tasnifu juu ya jambo ambalo ningepaswa kulichanganua katika barua ambayo ningekuandikia kwa jina la ‘Nafasi ya Vyanzo vya Shia kama msingi wa Sunnah.’ Tasnifu yako itachukuliwa kama neno la mwisho katika suala hili, hapawezi kuwa na hitimisho jingine mbali na kile ulichothibitisha na ninatumaini kuwa, Insha-Allah, italeta mabadiliko ya maoni yanayokubalika kwenye ulimwengu wa Kiislamu.

Tunaamini katika aya zote za Qur’ani, pamoja na zile zinazomhusu Amir wa Waumini, Ali ibn Abi Talib na Ahlul-Bayt wote (a.s.) ambazo ni aya zaidi ya ulizoonesha wewe.

Swali sasa ni sielewi kwa nini “Watu wa *Qibla* (Waislamu) waligeuka na kuacha kuwafuata Maimamu wa Ahlul-Bayt (as) na kuiacha itikadi yao kwenye *usul* na *furuu* au utekelezaji wake; na wameshindwa kuchukulia mafundisho yao kama kauli ya mwisho katika masuala ambayo kwayo wanahitalifiana? Au kwa nini wanachuo wetu hawatilii maanani mitazamo yao? Kwa nini badala yake wamepingana nao katika masuala ya kitheiolojia bila kusita? Na matokeo yake yakawa kwamba wengi wa Waislam, kizazi baada ya kizazi siku zote wamekuwa wakiendelea kuwategemea watu wengine mbali na Ahlul-Bayt kwa ajili ya mwongozo.

Kama kungekuwako katika aya za Qur’ani au riwaya za kutegemewa za Sunnah mwelekeo wowote wa wazi au maalum kama unavyodai, watu wa Qibla wasingegeuka na kuacha hekima za Maimamu wa Ahlul-Bayt, wala wasingemkubali yeyote badala yao. Lakini hawakuzielewa aya hizi za Qur’ani na riwaya hizo kama ni zenye kuthibitisha lolote zaidi ya kuwasifu Ahlul-Bayt, na amri ya kuwapenda na kuwaheshimu. Hivyo vizazi vya mwanzoni kabisa vya Waislam viko karibu zaidi na ukweli na kwenye

nafasi nzuri zaidi ya kuelewa maana ya Sunnah na Kitabu. Hivyo ni kwa nini usifuate mwongozo wao? Wassalaam.

**Wako Mwaminifu,S.**

# BARUA YA 18

## DHUL-HIJJAH 4, 1329 A.H.

**I. Shukurani kwa Maneno ya Upole,**

**II. Kosa la Kufunga Istilahi "Watu wa Qibla" kwenye Madhehebu Maalum,**

**III. Wanasiasa ndio Waliogeukia Mbali na Njia ya Ahlul-Bayt,**

**IV. Maimamu wa Ahlul-Bayt kwa Hali Yoyote sio Duni kwa Maimamu Wengine,**

**V. Hakuna Mtu Mwadilifu Anayeweza Kuwashutumu Wafuasi wa Ahlul-Bayt kwa Kupotoka.**

Asante kwa kunifikiria kwa hali ya juu kiasi hicho, licha ya mapungufu yangu, na nashukuru uamuzi wako wenye upole kwa kuridhika kabisa, na ninajiinamisha kwa unyenyekevu mbele ya upole huo na hapo nimetiishwa.

Kwa kurejea barua yako niliyonayo mkononi, ambamo umetaja ukengeukaji wa "watu wa Qibla" napenda nikukumbushe kwamba nusu ya watu wa Qibla, na hawa ninamaanisha Shia wa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.), kwa hakika hawakukengeuka na wala kamwe hawatakengeuka kwenye njia ya Ahlul-Bayt iwe ni kwenye mas'ala ya misingi ya dini au kwenye utekelezaji wake. Dini yao inawataka kutoa utii wa dhahiri kwenye mafundisho ya Maimam wao (as), kwa msingi wa Qur'ani na Sunnah. Hii kwa mujibu wao ndio imani tukufu wakati wote na katika hali yoyote. Hii imekuwa ndio kanuni mwongozo wa wahenga wao bora na halikadhalika ya vizazi vyao tangu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipofariki hadi leo hii.

(1) Wale ambao wamekengeuka na kuziacha imani za Ahlul-Bayt katika itikadi na vitendo ni wanasiasa na wale wenye uchu wa madaraka, wakati walipowanyan'ganya Ukhalifa, na kuufanya urithi huo kuwa jambo la uchaguzi wao huru, ingawa walijua kwa uhakika kwamba uliaminishwa kwa Amir wa Waumini Ali ibn Abu Talib (as). Waliona kwamba Waarabu hawatavumilia Ukhalifa huo kubakia katika familia moja maalum; kwa hiyo walitwaa maana tofauti ya maamrisho (ya Qur'ani na Sunnah) kuhusiana na hilo, wakalifanya ni suala la kutegemea uchaguzi ili kwamba kila mmoja wao aliye hai aweze kuwania nafasi hiyo ya juu mapema au baadae. Hivyo, uliendelea kwa kupokezana kwa huyu na kwa yule. Waliiunga mkono kanuni hiyo kwa nguvu zao zote walizoweza kumiliki, wakatoa muda mfupi kwa wale waliowapinga kukubaliana nao kabla hawajawaua. Matokeo yake ni kwamba ni dhahiri mazingira yaliwalazimisha watu kuitelekeza itikadi ya Ahlul-Bayt na kupotosha tafsiri za Qur'ani na Hadith zinazohusu umuhimu wa utiifu kwao. Lau wangefuata zile maana zilizo wazi za amri hizi, wote wangewaelekea Ahlul-Bayt ikiwa ni pamoja na watu wa kawaida na watu makhususi, wangewaelekea katika masuala yote ya itikadi na matendo ya dini, na wangeona kwamba ni wajibu wao kushikamana na kuwafuata Ahlul-Bayt, hivyo wangekuwa ni wafuasi wakubwa wa Ahlul-Bayt (a.s.). Lakini hili halikukubaliana na matamanio yao, na kufaa kwenye dhamiri zao za kufaidi utajiri wa kidunia na mamlaka ya kisiasa.

Katika kuleta fikra penyefu kwenye matukio haya, mtu hawezi kukosa kuona kwamba ukengeukaji huu wa watu kutoka kwenye njia ya Ahlul-Bayt katika mas'ala ya imani kulikuwa ni matokeo ya kukataa uongozi wa jumla ambao ulikuwa ni wao mara tu baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na kwamba tafsiri ya amri ya aya za Qur'ani na hadith kuwekewa mipaka kuwa unahusu familia yao tu

ilikuja baada ya kuufasiri kimakosa uimamu wao wa jumla, bila ya mazingira haya, kukubalika kwa haki za Ahlul-Bayt kusingeweza kuakhirishwa.

Mbali kabisa na maagizo ya Qur'ani na hadithi yaliyo wazi na yanayojieleza, yanayowateua wao kama warithi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), hebu tuwaangalie wao kama wafuasi wa kawaida tu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Je, wana kasoro yoyote? Je, wana ukosefu wowote katika elimu ya lazima, au uchamungu ama tabia njema? Je, wao ni wa kiwango cha chini katika kipengele chochote kati ya hivyo kuliko Imam Ash'ari au yeyote kati ya maimamu wanne wa Ahlus-Sunna? Kama hakuna kasoro yoyote kama hiyo kwao hao, basi ni kwa nini mtu mwingine yoyote afuatwe kuliko wao? Yuwapi hakimu anayeweza kuwashutumu wafuasi wa Ahlul-Bayt kuwa wamepotoka? Mtu anawezaje kudhaniwa kwamba amepotoka kwa sababu ya kung'ang'ania kwake kwenye kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Hakuna mfuasi wa madhehebu ya Ahlus-Sunna (aliye na akili salama) anayeweza kutoa hukumu kama hiyo dhidi yetu sisi.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 19

## DHUL-HIJJAH 5, 1329 A.H.

**I. Wafuasi wa Ahlul-Bayt Hawawezi Kuhukumiwa kama Waliopotoka,**

**II. Kufuata Imani yao ni Kutekeleza Wajibu Kunakotosha,**

**III. Inaweza Kusemwa Ahlul-Bayt ndio Wanaostahiki Zaidi Kufuatwa Kuliko Wengine,**

**IV. Kuomba Nususi Zisizo na Shaka Kuhusiana na Ukhalifa.**

Allama Sayyid Sharafud-Diin,

Assalaam Alaykum.

Hakika si lolote kabisa kuwaona wafuasi wa Ahlul-Bayt kama waliopotoka au waliokengeuka kutoka kwenye njia iliyonyooka. Wala haiwezi kusemwa kwamba Maimam miongoni mwa Ahlul-Bayt walikuwa na ustahiki mdogo wa kuongoza na kufuatwa kuliko wale Maimam wanne wa Ahlus-Sunna. Kwa kufuata itikadi ya Maimam miongoni mwa Ahlul-Bayt, mtu atachukuliwa kwamba ametekeleza wajibu wake kwa Allah swt. na anaweza kutarajia wokovu kama vile tu ambavyo mtu anaweza kuonekana kuwa ametimiza wajibu wake kwa kumfuata yeyote kati ya Maimam Wanne.

Inaweza kusemwa zaidi kwamba Maimamu miongoni mwa Ahlul-Bayt ni wenye kustahiki zaidi kufuatwa kuliko Maimamu hawa wengine wanne, kwa vile katika imani na itikadi za Maimam wote kumi na mbili ni hizo hizo zinafanana kwenye misingi na taratibu. Hakuna tofauti japo ndogo miongoni mwazo na maoni yao wote yana kitovu kimoja kinyume na yale ya Maimamu wanne ambao kutokubaliana miongoni mwao wenyewe kwa wenyewe kunajulikana kwa kila mtu. Ikiwa watu kumi na mbili baada ya kufikiria kunakostahiki juu ya jambo na wakafikia uamuzi mmoja unaofanana na kuunda maoni mamoja, na mtu mwingine akaleta maoni tofauti, ni dhahiri maoni yake ya pekee hayatakuwa na uzito wowote dhidi ya ile fatwa ya makubaliano ya pamoja iliyopita. Hakuna mtu mwadilifu anayeweza kulikataa hili. Lakini wapinzani wako wanakataa kwamba unafuata imani ya Ahlul-Bayt. Kwa hiyo ningekuomba tafadhali uonyeshe mwanga kwenye hoja hii na uthibitishe kwamba imani yenu mnayofuata ni sawa na ile ya Ahlul-Bayt waliyoiamini na kuitekeleza na kwamba ninyi mmerithi itikadi yenu kutoka kwao.

Na sasa nakuomba nususi bayana mlizodai kuwa zinathibitisha ukhalifa kwa Imam Ali bin Abi Talib (r.a.), zilete wazi wazi kwa njia ya Ahlus-Sunna.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# UIMAMU KWA UJUMLA

## (URITHI KWA MTUKUFU MTUME S.A.W.W) BARUA YA ISHIRINI DHIL-HIJJAH 9, 1239 A.H.

**I. Utajo Mfupi wa Nususi,**

**II. Nasu ya Siku ya Onyo kwa Jamaa wa Karibu,**

**III. Ahlus-Sunna Wameiandika na Kuisimulia Nasu hii.**

Kama mtu atachunguza wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), na kufuatilia mwenendo wake wa jinsi alivyoanzisha Dola ya Kiislamu, alivyoweka sheria, alivyoweka kanuni na taratibu kwa ajili yake na akazitekeleza sheria na kusimamia utawala kwa niaba ya Mwenyezi Mungu Aza wa Jallah…, ataona kwamba Ali (as) wakati wote alikuwa akimsaidia Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.), akishirikiana naye kwenye matatizo yake, msaidizi wake dhidi ya maadui zake, alipata elimu na kurithi hekima kutoka kwake, makamu wakati wa uhai wake, na Mtawala Mkuu baada ya kifo chake (s.a.w.w.). Katika upekuzi makini wa maneno na vitendo vya Mtume (s.a.w.w), kuanzia kwenye Tangazo la Kwanza la Utume hadi mwisho wa maisha yake, wakati akiwa nyumbani au safarini, atakuta kauli za wazi nyingi zilizosimuliwa kupitia vyanzo vya kuaminika kumuunga mkono Ali juu ya kushika Ukhalifa. Katika kila wakati uliofaa katika uhai wake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alionyesha kwa uwazi kabisa wa maneno na vitendo kwamba Ali (a.s.) ndiye aliyepaswa kuwa mrithi wake.

Hata kwenye lile tukio la mwanzoni lililotokea huko Makka, kabla ya kuwasili kwa Uislamu, pale Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipowaalika jamaa zake wa karibu linatoa tamko kama hilo.Wakati Mwenyezi Mungu alipoteremsha Aya: "**Na uwaonye jamaa zako wa karibu ….. (Qur'ani 26:214),**" Mtukufu Mtume aliwakaribisha kwenye nyumba ya ami yake, Abu Talib. Walikuwa watu arobaini, takriban. Miongoni mwao walikuwemo ami zake akina Abu Talib, Hamza, al-Abbas na Abu Lahab. Mwishoni mwa karamu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwahutubia waliohudhuria. Hotuba hiyo imeandikwa na kusimuliwa kwenye vitabu vya hadithi, historia na wasifu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani juu yake na kizazi chake. Hotuba hiyo ilikuwa na yafuatayo:

"Enyi wana wa Abdul-Muttalib! Ninaapa kwa jina la Allah kwamba simjui kijana miongoni mwa Waarabu ambaye amewaletea watu wake kitu kilicho bora zaidi kuliko kile nilichowaletea ninyi (Uislam). Nimewaleteeni kitu bora katika dunia hii na katika ile ijayo (Akhera), na Mweyezi Mungu ameniagiza niwaiteni kwenye hilo. Kwa hiyo ni nani miongoni mwenu atakayenisaidia mimi katika jambo hili, na ashirikiane nami katika kazi yangu, ili aweze kuwa ndugu yangu, wasii wangu, na Khalifa wangu miongoni mwenu?"

Walihudhuria wote, ukimuondoa Ali, ambaye alikuwa ndiye mdogo zaidi miongoni mwao, walinyamaza kimya. Ali alijibu kwa kusema: "Mimi, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, niko tayari kushirikiana nawe katika jambo hili."

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.) ndipo akamkamata Ali shingoni mwake na akasema: "Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu miongoni mwenu; kwa hiyo msikilizeni na mumtii." Wale walio hudhuria wakacheka na wakawa wanamwambia Abu Talib: "Loh! amekuamrisha kumsikliza na kumtii mwanao!"

Tukio hilo hapo juu limesimuliwa na idadi kubwa ya wanachuo wa kutambulika na wasimulizi wa hadith mashuhuri katika vitabu vyao kwa mfano; Ibn Is'haq, Ibn Jarir, Ibn Abu Haatim, Ibn Mardawayh, Abu Na'im

na al-Bayhaqi ambaye ameiandika katika vitabu vyake vyote: *Sunan* na *al-Dala'il*, wote, al-Thalabi na al-Tabari katika tafsiri zao maarufu za *Suratul-Shu'araa.* Tabari ameiandika hii katika Juz. 2 ya *Tarikh al-Umam wal Muluk,* uk. 217 kwa maneno tofauti kidogo, na Ibn Athir ameisimulia miongoni mwa hadithi zinazokubalika katika Jz. 2, uk. 22 ya kitabu chake: *Taarikh Al-Kamil* chini ya kifungu cha maneno: "Mwenyezi Mungu alimuamuru Mtume Wake kutangaza Utume wake." Abdul Fida ameliandika tukio hili katika Jz. 1, uk. 116 ya kitabu chake cha *Tarikh* alipokuwa akizungumzia ni nani aliyekuwa wa kwanza kuingia katika Uislamu, na Imamu Abu Ja'far al-Iskafi al-Mutazili ameisimulia katika kitabu chake "*Naqdhul-Uthmaniyyah"* akionyesha usahihi wake,[134] na Allama al-Halabi ameisimulia katika mlango unaozungumzia juu ya kujificha kwa Mtukufu Mtume na sahaba zake katika nyumba ya Arqam katika kitabu chake mashuhuri cha *sirah al Halabiyyah*[135]

Mbali na hayo hapo juu, takriban pamoja na maelezo yanayotofautiana kidogo lakini kwa maana ileile, Hadithi hii imesimuliwa na mabingwa wengi wa Hadithi na waandishi wenye kutegemewa zaidi kama vile al-Tahawi, Dhiyau al-Maqdasi katika kitabu chake cha *Mukhtara*, na Sa'id Ibn Mansur katika *Sunnan* yake. Lakini kwa lengo lako inakutosha kurejea kwenye kile alichoandika Ibn Hanbal kutoka kwa Ali (a.s) katika ukurasa wa 111 na 159 wa Jz.1 ya *Musnad* yake. Yeye pia ameelekeza mwanzoni mwa ukurasa wa 331 wa Jz. ya 1 ya *Musnad* yake, kwenye Hadithi muhimu sana kutoka kwa Ibn Abbas yenye sifa kumi ambazo zimemtofautisha Ali na kila mtu mwingine yeyote. Hadithi ile pia imechapishwa kwenye *Nasa'i* vile vile ameinukuu kutoka kwa Ibn Abbas, katika ukurasa wa 6 wa *Khasa'is al- Alawiyyah*, na katika Uk. 132, Jz. 3 ya *Mustaduk* ya Hakim. Tha'labi ameisimulia katika *Talkhis* yake, akichukua dhima juu ya uhakika wake. Rejea kwenye Jz. ya 6 ya *Kanz al-ummal* ambamo tukio hilo limeelezwa kirefu.[136]

Kama utarejea pia kwenye *muntakhabul Kanz al-Ummal* ambayo imechapwa kwenye tanbihi chini ya kurasa za *Musnad* ya Imam Ahmad, ukiyafuatilia yaliyomo kwenye tanbihi ya uk. 41 na 43 za Jz. 5 ya kitabu hiki, utaikuta hadith hii kwa kina. Hili tukio moja la onyo kwa jamaa wa karibu na hotuba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambayo imesimuliwa na takriban wanachuoni wote, wanahistoria na wasimulizi, inatoa uthibitisho wa kutosha na zaidi kuwa Uimam na Ukhalifa ulikuwa ni haki ya Ali (a.s.). Na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[134] Kama ilivyotajwa katika uk 263 wa Juz. 3, ya *Sharh Nahjul-Balaghah,* chapa ya Misri, kuhusiana na kitabu chake *Naqdhull-Uthmaniyyah*, kwa kweli haina kifani. Mwandishi amejadili kinaganaga kila kitu kinachohusiana na mwaliko huo katika Jz. 3, uk. 257 - 281, katika maelezo hayo katika kipande cha mwisho cha "*Khutbat ul Qasi'ia."*

[135] Rejea kwenye uk. 381 wa Jz. ya 1, ya '*Al-Sira al-Halabiyyah*.' Ile riwaya isiyo na uangalifu kabisa juu ya tukio hilo na maelezo pujufu ya Ibn Taymiyyah hayafai kuzingatiwa kutokana na msimamo wake unaofahamika sana. Hadithi hii imesimuliwa na mwandishi mjamaa wa Misri, Muhammad Husayn Haykal; rejea kwenye safu ya pili ukurasa wa tano wa kwenye toleo la 2751 la gazeti lake *As-Siyasat* la tarehe 12 Dhul-Qad, 1350A.H. na utaikuta hapo ikiwa imeelezewa kwa kina. Kama utarejea kwenye safu ya nne kwenye uk.6 wa toleo na 2785 la gazeti hilo hilo, utamkuta mwandishi akiisimulia hadithi hii (ya hotuba hiyo) kutoka *Sahih Muslim* na *Musnad* ya Ahmad, *Ziyadat al Musnad* ya Abdillah Ibn Ahmad, *Jam'a ul-Fara'id* ya Ibn Hajar Makki, *Uyun al-Akhbar* ya Ibn Qutaybah, *Al-Iqd al- Farid* ya Ahmad Ibn Abd Rabbih, Omar Ibn Bahr al Jahiz katika tasnifu yake juu ya kizazi cha Hashimu, na katika Tafsir ya Qur'an ya Imam Abu Ishaq Thalabi. Hadithi pia imesimuliwa na yule mwandishi wa Kiingereza George katika kitabu chake mashuhuri kiitwacho *A Treatise on Islam*, kilichotafsiriwa kwa Kiarabu na mkana uprotestanti anayejiita Hashim al-Arabi. Unaweza pia kuikuta Hadithi hiyo katika uk 79 wa tafsiri ya kiarabu ya kitabu hicho, toleo la sita. Kutokana na umaarufu ilionao Hadithi hii, waadishi wengi wa Ulaya, Wafaransa, Waingereza na Wajerumani wameiingiza kwenye vitabu vyao. Katika kitabu chake, Heroes and Heroworship, Thomas Carlyle ameinukuu kwa ufupi.

[136] Rejea Hadithi ya 6008 katika uk.392, na utaikuta imesimuliwa kutoka kwa Ibn Jarir, ambapo Hadithi ya 6045 katika uk 396 ikasimuliwa kutoka kwenye *Musnad* ya Ahmad na kutoka kwenye *Al-Mukhtara* cha al-Zia al-Maqdisi na kutoka kwa al-Tahawi na Ibn Jarir amethibitisha hilo. Vilevile rejea Hadithi 6056 katika uk 397 na utaikuta imenukuliwa kutoka kwa Ibn Ishaq, Ibn Jarir, Ibn Abu Haatim, Ibn Mardawayh, Abu Na'im, na al-Bayhaqi katika *Shu'abul-Imani*, na katika *Dala'il*, na hadithi 6102 katika uk 401 kutoka kwa Ibn Mardawayh, na Hadithi ya 6155 katika uk. 408 kutoka kwenye Musnad ya Ahmad na kutoka kwa Ibn Jarir na Al-Zia kwenye *Mukhtara*. Na katika *Kanz al-Ummal* Hadithi hii imesimuliwa katika sehemu zingine pia. Kama ukitazama uk. 255, Jz. 3 ya *Sharh Nahjul Balaghah* cha Ibn Abil Hadidi, utaikuta hadith hii kwa kirefu mwishoni mwa maelezo ya *Khtubatul-qasi'a*.

# BARUA YA ISHIRINI NA MOJA

## DHUL-HIJJAH 10, 1329 A.H.

**Hadithi Hiyo ina Mashaka Juu ya Ukweli Wake**.

Mpinzani wako ana wasiwasi sana juu ya kuaminika kwa hadithi hii (onyo kwa jamaa wa karibu na hotuba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na hayuko tayari kuipokea kama ni sahih kwa sababu Masheikh wakuu wawili (Bukharin na Muslim) hawakuiingiza katika Sahih zao, wala waandishi wa Sahih nyinginezo zinazoaminiwa na Sunni hawakufanya hivyo. Sidhani kwamba Hadithi hii imesimuliwa kutoka kwa msimuliaji yeyote wa kuaminika wa Sunni, na sidhani kwamba wewe mwenyewe waamini kwamba imethibitishwa na wanahadith wa Sunni. Na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu,Sh.**

# BARUA YA ISHIRINI NA MBILI

## DHUL HIJJAH 12, 1329

**I. Kutoa Ushahidi wa Usahihi wa Hadithi hii,**

**II. Kwa nini wao (Bukhari na Muslim) Wamekwepa Kuiandika,**

**III. Yeyote Anayewafahamu Masheikh hawa Hataona Ajabu.**

Ningekuwa sikuamini hadith hii kuwa halisi kwa mujibu wa vyanzo vya Sunni, nisingeitaja kwenye maudhui hii. Zaidi ya hivyo, hadith hii inafahamika sana kiasi kwamba Ibn Jarir na Imam Abu Ja'far al-Iskafi wamechukulia hadith hii kama inayokubali pote kwamba ni sahihi na halisi.[137]

Baadhi ya watafiti maarufu wengine miongoni mwa Sunni pia wameichukulia kwamba ni ya kweli. Usahihi wake umekubaliwa na kuthibitishwa na kundi lilelile la wanachuoni wa kutegemewa na kuaminika na wapokezi wa kuaminika ambao kauli zao hutegemewa na kukubaliwa kwa ridhaa kabisa na waandishi wa vitabu vya *Sahih* (yaani vitabu vya hadith vinavyokubaliwa kuwa ni *Sahih* na Ahlus Sunnah), na hadith hii imesimuliwa na wale wale wanachuoni wa kutegemewa ambao riwaya zao zimeingizwa ndani ya hizo *Sahih*. Zaidi ya hapo, tafadhali rejea uk.111 wa Jz. 1, ya *Musnad* ya Ahmad ambamo utaisoma Hadithi hii kama ilivyosimuliwa na As'wad Ibn Aamir,[138] kutoka kwa Shariik,[139] kutoka kwa al-A'mash,[140] kutoka kwa Minhal[141] kutoka kwa Ibbad ibn Abdullah al-Asadi,[142] aliyeipokea kutoka kwa Ali (a.s). Kila moja ya *Sanad* hizi za wapokezi inakubaliwa na mpinzani wangu kama ni chanzo, na wote ni wasimulizi wa kutegemewa ambao riwaya zao zimejumuishwa katika vitabu vya Sahihi bila ya wasiwasi wowote. Na Al-Qaysarani amewaelezea katika kitabu chake, *Al-Jama' Bayna Rijal us-Sahiihain*. Hakuna jinsi kwa hiyo ila kuikubali Hadithi hii (ya kuwaonya jamaa wa karibu) kuwa ni sahihi. Mbali na hivyo, hadith hii imesimulia kwa njia mbalimbali kila mmoja akimuunga mkono mwingine.

Sababu ya kwanini Masheikh wote wawili Bukhari na Muslim hawakuisimulia Hadithi hii kwenye *Sahih* zao ni kutokana na ukweli kwamba haikukubaliana na maoni yao binafsi kuhusiana na suala la Ukhalifa. Pia wamekwepa kwa makini sana idadi kubwa ya hadith sahihi ambazo zinasisitiza Ukhalifa wa Imam Ali (a.s.) kwa hofu kwamba Mashia watazitumia kama silaha mikononi mwao, kwa hiyo waliuficha ukweli kwa makusudi kabisa. Sio hawa wawili tu bali wapo Masheikh wengi sana pia miongoni mwa Ahlus-Sunnah (muhadithiina), Mwenyezi Mungu awasamehe, ambao vivyo hivyo wameuficha ukweli

[137] Rejea Hadithi ya 6045 katika *Kanz al-Ummal*, uk. 396, Juz. 6 ambamo utakuta Ibn Jariir ameichukulia Hadithi hii kwamba halisi. Kama ukirejea kwenye *Muntahhab al-Kanz*, pambizoni mwa uk. 44, Juz. ya 5 ya *Musnad* ya Ahmad, utakuta kwamba Ibn Jariir anaiona Hadithi hii kuwa ni halisi. Nakuhusu Abu Ja'fari al-Iskafi, anaiamini kwa nguvu zote kwamba ni hadith sahihi katika kitabu chake *Naqdhw al-Uthmaniyyah*, kwenye pambizo ya Uk. 263, Juz. 3 ya *Sharh Nahjul Balaghah* cha Ibn al-Hadid, chapa ya Misri.

[138] Wote, Bukhari na Muslim wamesimulia hadith zake katika *Sahihi* zao kama mtu mkweli. Shu'bah amewasikia Bukhari na Muslim wakisimulia hadith kutoka kwa Aswad na Abul-Aziz Ibn Abu Salma alimsikia Imam Bukhari akisimulia Hadithi kutoka kwake kupitia kwa Zuhayr Ibn Mu'awiyah na Humad Ibn Salmah alimsikia Imam Muslim akisimulia Hadith kutoka kwake. Sahih Bukhari ina hadith zilizosimuliwa kutoka kwake na Muhammad Ibn Hatim Bazii' na katika Sahihi ya Muslim, zimo zilizosimuliwa naye kutoka Harun Ibn Abdullah, Naqid ibn Abu Shaybah na Abuu Zuhayr.

[139] Muslimu ametegemea simulizi zake kwenye Sahih yake, kama tulivyoelezea katika maelezo yake kwenye Barua ya namba 16.

[140] Wote, Bukhari na Muslim wanazitegemea simulizi zake katika *Sahih* zao, husika kama tulivyoelezea wakati tukimjadili kwenye Barua ya namba 16.

[141] Bukhari amemnukuu ndani ya *Sahih* yake, kama tulivyoelezea wakati tulipomtaja kwenye Barua ya 16

[142] Jina lake kamili ni Ibbad Ibn Abdullah Ibn az-Zabayr Ibn al-Awwam al-Qarashi al-Asadi. Bukhari na Muslim wote wamesimulia kutoka kwake katika *Sahih* zao husika. Amesikia Hadithi hizo kutoka kwa Asma na Aisha binti wa Abu Bakr. Bukhari na Muslim wamenukuu riwaya zake katika *Sahih* zote kutoka kwa Ibn Abu Maliika na kwa Muhammad Ibn Ja'far Ibn az-Zubayr ibn Urrah.

kwa kufuata desturi yao. Wamekuwa wakificha kila kitu chenye asili hii na wanafahamika vema kwa choyo chao cha kuficha mambo yanayomhusu Amirul-Mu'minin Ali (a.s.) na Ahlul-Bayt (a.s.). Hafidh Ibn Hajar katika kitabu chake *Fath al-Bari* ameyasimulia haya kutoka kwao, na Imam Bukhari ameweka mlango maalum kwa ajili ya mada hii katika mlango wa "*Kitabul Ilm*," katika Jz. 1, uk. 25 ya Sahih yake, chini ya kichwa kidogo cha maneno, "Ugawaji wa Ilimu kwa kundi moja na kulinyima kundi jingine."

Yeyote anayejua tabia za Bukhari kwa Amirul-Muminin (as), na juu ya Ahlul-Bayt wote (a.s.), na pia akajua namna kalamu ya Bukhari wakati wote inavyokwepa kusimulia hadithi za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zinazohusu kuwapendelea wao, na kwamba wino wake hukauka kabla ya kusimulia sifa zao bora zinazowatofautisha, yeye hatashangaa kumuona anaikwepa Hadithi hii hasa na nyinginezo mfano wake, kwa hiyo, hakuna nguvu wala uweza ila kwa Mwenyezi Mungu, Muweza, Mtukufu, na amani iwe juu yako. Wassalam

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA ISHIRINI NA TATU

## DHUL-HIJJAH 14, 1329 A.H.

**I. Kukiri Usahihi wa Hadithi hii,**

**II. Hadithi Kutotumika kama Hoja ya Nguvu kwa Sababu ya Uchache wa Usimuliwaji wake,**

**III. Kwa Vyovyote Inathibitisha Urithi Maalum (wenye mipaka), sio Ukhalifa wa kila yeyote.**

**IV. Hadithi Imepewa Mbadala.**

Kwakweli, nimerejea na kusoma hadith hii katika uk. 111 wa Jz. 1, ya *Musnad* ya Ahmad na kuchunguza majina ya wapokezi wa hadith hii na kugundua kwamba wote ni wasimulizi wa kuaminika kabisa wa Sunni, na vyanzo vizuri vya hadith. Kisha nimegundua kwamba kuna maandiko katika usimuliaji wa Hadithi hii, kila moja ikiunga mkono nyingine katika maana. Kwa hiyo, nimejiridhisha mwenyewe kuamini kwamba usahihi wa hadithi hii umethibitishwa vya kuridhisha kabisa.

Isipokuwa wao hawatumii hadithi kuthibitisha uimamu isipokuwa inapokuwa *mutawatiri*, kwani Uimam, kulingana na falsafa yenu Shiah, ni moja ya mizizi ya dini, na ambapo Hadthi hii haiwezi kuchukuliwa kama ni "*mutawatir"* na kwa hiyo, haiwezi kutegemewa kama hoja yenye nguvu.

Inafikiriwa pia kwamba riwaya hii kwa vyovyote inathibitisha kwamba Ali ndiye mrithi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama mkuu wa kizazi chake Ahlul-Bayt peke yake, ambao ni urithi uliobainishwa. Lakini liko wapi sharti la wazi linalothibitisha urithi wake kama Khalifa juu ya Umma wote wa Kiislam?

Hadith hii inaweza kusemwa kwamba ilibatiliswa au kufutwa, kwa vile Mtukufu Mtume (s. a. w.w.) baadae hakujali kulilazimisha jambo lenyewe. Kwa hiyo, masahaba hawakuona kipingamizi kwa nini wasitoe kiapo cha utii kwa makhalifa watatu waongofu, Mwenyezi Mungu awawie radhi wote.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA ISHIRINI NA NNE

## DHUL- HIJJAH 15, 1329 A.H.

**I. Kwa nini Tumetoa kama Hoja Hadithi Inayosemwa kwamba si Mutawatir,**

**II. Urithi Wenye Mipaka ni Kinyume na Maoni ya Pamoja ya Wanachuoni wote wa Kiislam,**

**III. Hapa Ufutwaji ni jambo Ambalo Haliwezekani.**

Ahlus-Sunna wanategemea juu ya kila Hadithi sahihi katika kuthibitisha dhana yao ya urithi, iwe *mutawatir* au la. Kwa hiyo katika kujadiliana nao tunatwaa mbinu yao wenyewe ya mahojiano na kutoa hoja zile zile wanazoziona wao kwamba ni za kweli. Juu ya ni kwa nini tunarejea kwenye riwaya hii kama hoja ya kutetea Uimamu wa Ahlul-Bayt, tafadhali tambua kwamba sisi Shi'ah tunaichukulia riwaya hii kuwa sio tu kwamba ni sahihi bali imesimuliwa kwa *Mutawatir* kwa mujibu wa vyanzo vyetu wenyewe vya taarifu za kuaminika.

Madai kwamba riwaya hii kwa kila hali inathibitisha kwamba Ali (a.s.) alimrithi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kama kiongozi au Khalifa wa Ahlul-Bayt tu hayana maana kabisa kutokana na ukweli kwamba, wale wanaoamini kwamba Ali alikuwa ni Khalifa wa Mtume wa Allah swt. juu ya kizazi chake, wanaamini vilevile kwamba ndiye Khalifa wake kwa Umma wote wa Waislam, na wale ambao hawaamini kuwa yeye ndiye Khalifa wake kwa Umma vilevile hawaamini Ukhalifa wake juu ya Ahlul-Bayt wake. (Kwa maneno mengine ni kwamba wale wanaoamini katika Ukhalifa wake uliobainishwa au wenye mipaka wanaamini pia juu ya Ukhalifa wake wa jumla na kinyume chake). Kuna makundi mawili tu ya wanachuoni na maoni namna mbili tu juu ya maudhui hii. Ni nani anayeshikilia maoni hayo uliyoyaleta wewe, ambayo sio kwamba ni ya ajabu tu bali pia yanakwenda kinyume na makubaliano ya maoni ya pamoja ya wanachuoni wa Kiislamu wote?

Pia sio sahihi kusema kwamba hadithi hii imetaguliwa au ilifutwa, ambapo kisheria na kimantiki ya kielimu haiwezekani. Kama unavyojua maagizo ya kwenye ahadi hayafutwi kabla ya wakati wa utekelezwaji wake, jambo pekee kwa hiyo ambalo linaelekea kuunga mkono hoja yako juu ya ubatilishwaji wa riwaya hiyo ni kule kudhania kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) baadae hakujishughulisha na utekelezaji wa Hadithi hii. Bali kudhania huko ni kwa makosa. Hadithi yenyewe inathibitisha kwamba, yeye, rehema na amani juu yake na juu ya kizazi chake hakuzembea kusisitiza utekelezaji wake. Bali kinyume chake ni kwamba kuna riwaya nyingi zilizoandamana baadae nazo ni *Mutawatir* kuhusu jambo hili, zikiungana mkono zenyewe kwa zenyewe. Hata kama tukichukulia kwamba hakukuwa na riwaya nyingine za baadae zenye kuunga mkono na kuthibitisha hadithi ya asili, hilo linaweza kumwelekeza mtu kuamua kwamba Mtume (s.a.w.w.) alipuuza utekelezaji wa hadith hiyo au alibadili mawazo yake na akafuta maneno yake? **"Hawafuati ila mawazo na matamanio yao, baada ya kuwa uongofu kutoka kwa Mola wao umekwisha kuwafikia (Qur'ani 53:23).**

**Wako Mwaminifu, Sh**.

# BARUA YA ISHIRINI NA TANO

## DHUL-HIJJAH 16, 1329 A.H.

**I. Imani yake Juu ya Hadith,**

**II. Kuomba Utetezi zaidi (Juu ya Uimam wa Ahlul-Bayt).**

Ninaamini kwamba wewe umenielimisha vya kutosha katika yale yaliyokuwa kwangu yamejificha, na kwa kuweka wazi yale yenye utata. Mwenyezi Mungu amekufanya wewe kuwa moja ya dalili Zake na udhihirisho unaong'ara.

Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tafadhali nielimishe zaidi somo hili, na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA ISHIRINI NA SITA

## DHUL- HIJJAH 17, 1329 A.H.

**I. Hadithi za Wazi Zinazoorodhesha Sifa 10 za Ali (a.s.)**

**II. Uthibitisho wa Haki ya Ali ya Urithi Unaotolewa na Hadith hizo.**

Mbali na hadithi ya ‘kuwaonya jamaa wa karibu,’ rejea kwenye riwaya iliyosimuliwa na Imam Ahmad katika Jz. 1, uk. 330 ya *Musnad* yake, na Imam Nasa’i katika *Khasais al-Aulwiyah*, uk. 6, , na Hakiim katika Jz. 3, ya *Sahih Al-Mustadrak*, uk. 123, na Dhahabi aliyekiri usahihi wake katika *Talkhiis* yake, na wasimulizi wengine kupitia vyanzo vinavyokubaliwa kwa pamoja na Ahlus-Sunna kama ni sahihi. Umar ibn Maymum anasema “Wakati mmoja nilikuwa nimekaa mbele ya Ibn Abbas wakati machifu tisa walipomjia na kusema ‘Ewe Ibn Abbas! Ama usimame ufuatane nasi, au waambie hawa wafuasi waondoke wakuache peke yako kwa ajili ya mjadala wa faragha na sisi’ Ibn Abbas ambaye alikuwa bado hajapoteza kuona kwake alisimama na akaondoka nao na akawauliza kuhusu lile walilotaka kulisema. Palikuwa na mazungumzo kati yao ambayo sikuweza kuyasikia. Ibn Abbas aliporejea alikuwa anatingisha nguo yake na akasema: ‘Balaa liwashukie.’ Kisha akaendelea kusema: ‘Wanamzungumza kwa ubaya mtu ambaye ana sifa kumi bora ambazo hakuna mtu mwingine aliyenazo. Wanamtaja kwa ubaya mtu ambaye Mtukufu Mtume (s.a.w.w) amesema:

1. ‘Hakika kesho asubuhi nitamtuma mtu ambaye Mwenyezi Mungu kamwe hatamuabisha. Mtu anayempenda Allah na Mtume wake (s.a.w.w.) na yeye anapendwa na Allah na Mtume Wake.’ Masikitiko matupu yaliwakumba watu wengi walioitamani sifa hiyo. Mtukufu Mtume akauliza: ‘Yuko wapi Ali?’ Pale Ali alipomjia, macho yake yakiwa yamevimba kwa maradhi na alikuwa hawezi kuona chochote. Yeye Mtume (s.a.w.w.) akampulizia machoni mwake, na akaipepea bendera mara tatu kisha akaikabidhi kwa Ali ambaye alielekea kwenye uwanja wa mapambano wa Khaybr na alirejea na ushindi pamoja na Safiyya binti Hayi (na dada yake Marhab) ambaye alimkabidhi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).’
2. ‘Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimtuma mtu mmoja na Surat at-Tawba kwenda kuisoma mbele ya makafiri wa Makka. Mara baada ya hapo ilimbidi amtume Ali na akasema: ‘Yeye pekee ndiye awezaye kulitekeleza jukumu hilo kwani yeye anatokana na mimi, na mimi ninatokana naye.’ Ali alimfuata nyuma na kumkuta mtu huyo na akaichukua at-Tawba na akaisoma mbele ya makafiri.’
3. ‘Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), aliwauliza jamaa zake: ‘Ni nani miongoni mwenu ambaye yuko tayari kunisaidia katika kazi yangu ili awe ni walii wangu katika dunia hii na ya Akhera?’ Wote walinyamaza kimya, bali Ali ambaye alikuwapo hapo akasimama na akasema: ‘Mimi nitakusaidia ili niwe msaidizi wako katika dunia hii na ile ya Akhera.’ Ndipo Mtume (s.a.w) akasema: ‘Wewe kwa hakika, ni msaidizi wangu katika dunia hii na ile ya Akhera.’ Kisha akamwambia Ali (a.s.) aketi chini na akarudia tena: ‘Ni nani miongoni mwenu ambaye yuko tayari kunisaidia katika kazi yangu ili awe ni msaidizi wangu katika dunia hii na ya Akhera?’ Bado hapakuwa na jibu kutoka kwa wale wengine bali Ali (a.s.) alisimama na kusema: ‘Mimi nitakuwa msaidizi wako katika dunia hii na ile ya Akhera.’ ‘Wewe ni msaidizi wangu katika dunia hii na ile ya Akhera.’ Mtukufu Mtume alimwambia Ali.

4. Ibn Abbas anaendelea kusema kwamba: 'Ali alikuwa ndiye mtu wa kwanza kuukubali Uislamu baada ya Khadija, mke wa kwanza wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)'
5. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alichukua shuka yake mwenyewe na kuwafunika nayo Ali. Fatimah, Hasan na Husein, kisha akasoma ile Aya inayosema; **"Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondoleeni uchafu, enyi Ahhul Bayt na kuwatakasa kwa utakaso uliokamilika." (Qur'ani, 33.33)."**
6. 'Ali aliuza nafsi yake mwenyewe (katika njia ya Allah) alipojifunika shuka la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kulala katika kitanda chake wakati makafiri walikuwa wanamtupia mawe.'
7. 'Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w) aliondoka Madina kwenda safari maalum ya Tabuk akiandamana na watu wengine. Ali akamuomba: 'Je nijiunge na wewe?' Mtume wa Allah (s.a.w) akasema 'hapana,' hapo Ali akalia sana. Mtume (s.a.w.w.) ndipo akamuliza: 'Huridhiki wewe kwamba cheo chako kwangu ni kama kile cha Harun kwa Musa (a.s.), isipokuwa tu kwamba hakuna Mtume baada yangu? Sipaswi mimi kundoka mahali hapa kabla ya kukuweka wewe kama mwakilishi wangu.'
8. Mtume wa Allah (s.a.w) vile vile alimwambia haya yafuatayo: 'Wewe utakuwa mtawalia mambo kwa waumini wote wanaume na wanawake baada yangu.'
9. 'Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliifunga milango yote inayofungukia Msikitini isipokuwa ule mlango wa Ali ambaye alikuwa akipita msikitini humo hata pale alipokuwa kwenye hali ya janaba (yaani hata kabla hajaoga josho la wajibu au kutayammam), na hiyo ilikuwa ndio njia pekee ya kutokea na kurudia nyumbani kwake.'
10. Mtume wa Allah (s.a.w.w.) pia amesema: 'Ali ni bwana (mtawalia wa mambo) wa yule ambaye anaamini kwamba mimi ni bwana wake."'

Imam al-Hakim, akiwa amekwisha kutaja hadith ya "Ali ni bwana wa ……" anasema kwamba 'Hadithi hii ni sahihi na imesimuliwa kupitia vyanzo vinavyoaminika ingawa mashekhe wote wawili (Bukhari na Muslim) hawakuisimulia kwa njia hii." Na kwamba Al-Dhahabi ameinukuu katika *Talkhis* yake na akaielezea kuwa ni Hadithi sahih.

Katika hadithi hiyo hapo juu, kwa hakika utakuta hoja kwa ajili ya uthibitisho wa wazi unaong'ara ukisisitizia ukweli kwamba Ali alikuwa ndiye naibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wakati wa uhai wake na mrithi baada yake. Tafadhali hebu angalia jinsi Mtume (s.a.w) alivyomteua yeye kama *msaididzi* katika dunia hii na ile ijayo, na kumpendelea yeye juu ya ndugu zake wote, na jinsi alivyokichukulia cheo chake kuwa sawa na kile cha Harun kwa Musa, bila tofauti yoyote nyingine isipokuwa utume. Ile tofauti pekee ya Utume inathibitisha kwamba katika vipengele vyote vingine, nafasi ya Ali (kwa uhusiano na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa ni sawa na ya Haarun (katika uhusiano wake na Nabii Musa).

Na unaijua sifa maarufu ya kipekee ya Harun ilikuwa kwamba yeye alikuwa waziri na msaidizi wa Musa, mshiriki wake katika ujumbe na mwakilishi wake, kwamba utii kwake (Haarun) ulikuwa ni wajibu ulioshurutishwa kwa wafuasi wote wa Musa kama inavyoonekana katika maombi yake Musa: **Na nipe waziri katika watu wangu Harun ndugu yangu Niongeze nguvu zangu kwaye Na umshirikishe katika jambo langu. (20:29-32). "…Shika mahali pangu katika watu wangu, na utengeneze, wala usifuate njia ya waharibifu (Qur'ani, 7:142),"** na kukubaliwa maombi na Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Akasema: Hakika umepewa maombi yako ewe Musa. (Qur'ani 20:36)."**

Kulingana na maelezo hayo, ya hadith hii sahihi, Ali alikuwa ndiye mwandamizi wa Mtukufu Mtume juu ya wafuasi wake na waziri wake kutoka miongoni mwa ndugu zake, mshirika wake, katika kazi yake.

Huyu mwandamizi wake kwa hakika alikuwa ni mlezi na mtawala na sio kama Mtume, na alikuwa mbora zaidi kuliko wafuasi wake (Mtume) wote na alikuwa karibu naye alipokuwa hai na alipokufa kuliko watu wengine, na kama Waziri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) utii kwake yeye ulikuwa ni wajibu uliowekwa juu ya wafuasi wake hata wakati wa uhai wa Mtume, kama vile tu watu walivyopaswa kumtii Harun wakati wa uhai wa Musa.

Kwenye akili ya yeyote atakayesoma au kusikia Hadithi hii ya nafasi ya mahusiano (*Hadith al-Manzilah*) ya Ali bila shaka anajitokeza kwamba nafasi ya Ali ni sawa hasa na ile ya Harun katika nyanja zote (ukiachilia mbali ya Utume), na msikilizaji huyo anaachwa bila ya shaka yoyote kuhusu maana yake. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ameliweka hili wazi kabisa pale aliposema; "Kwa hakika mimi sipaswi kuondoka mahali hapa kabla ya kukuteua wewe kuwa naibu wangu." Na haya sio maelezo yenye kueleweka wazi tu bali ni tamko la dhahiri kabisa pia la Uandamizi wa Ali; kwa kuwa inaarifu kwamba kama Mtume (s.a.w.w.) angeondoka Madina bila kufanya hivyo, angekuwa na hatia ya kufanya kitendo kisicho sahihi. Na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) asingezungumza hayo bila ya kuamrishwa na Mwenyezi Mungu kumteuwa yeye kama mwandamizi wake kama ilivyothibitishwa na Aya isemayo:

**"Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe wake (hata kidogo). Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri. (Qur'ani 5:67)."**

Wale ambao wameyachunguza maneno haya "**basi hukufikisha ujumbe wake hata kidogo,"** na kuyalinganisha na maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) "Kwa hakika mimi sipaswi kuondoka mahali hapa (kuelekea Tabuuk) kabla ya kukuteuwa wewe kuwa naibu wangu," wamegundua kwamba zote (hii aya ya Qur'ani na hadith ya Mtume) zinaashiria kwenye lengo lile lile, kama ilivyo dhahiri kabisa. Unapaswa pia kuzingatia yale maneno ya Mtume (s.a.w.w.) katika Hadithi iliyotajwa hapo juu: "Wewe ni *Bwana* wa kila mumini baada yangu." Kwa hakika hii inathibitisha wazi kwamba yeye Ali alikuwa ndiye mtawala na mlezi na mwandamizi wa Mtume (s.a.w.w.) juu ya wafuasi wake wote, kama alivyomaanisha al-Kumail, Mwenyezi Mungu amuwie radhi, katika kumsifu Ali kwenye ubeti wa shairi lake;

"Wewe ndiye mtawala bora baada ya Walii wake (Mtukufu Mtume (a.s.w.w.)) ambaye ulikimbilia uchamungu na kuwa mwalimu bora wa nidhamu!"

Na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA ISHIRINI NA SABA

## DHUL-HIJJAH 18, 1329 A.H.

**Mashaka Kuhusu Usahihi wa Hadithi ya *Manzila*.**

"Hadithi ya *Manzila* ni sahihi na mashuhuri, lakini al-Amidi, ambaye ni mwanachuoni mchaguzi mgumu kuridhika, na ambaye anachukuliwa kwamba bingwa wa elimu ya *usul* katika zama zake, alikuwa na wasiwasi juu ya usahihi wa hadithi hii na uhakika wa vyanzo vyake. Utawashawishije wapinzani wako ikiwa watachukulia maoni ya al-Amidi? Na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA ISHIRINI NA NANE

## DHUL-HIJJAH, 19, 1329 A.H.

**I. Hadithi ya *Manzila* ni Moja kati ya zile Hadith Ambazo Usahihi wake Umethibitishwa sana,**

**II. Hoja Kuhusu Usahihi wake,**

**III. Hadithi Imesimuliwa na Wasimuliaji wa ki-Sunni,**

**IV. Kwa nini Al-Amidi Alikuwa Anashuku Usahihi wake.**

Al-Amidi aliifanya dhamira yake kuwa na hatia kwa kuendekeza shaka juu ya usahihi wa Hadithi hii, kwani hadithi ya Manzila ambayo ni moja kati ya maagizo yenye usahihi usio na maswali, na moja kati ya hadithi ambazo ubora wake umethibitishwa sana.

Hakuna mtu mwingine yeyote aliyetilia mashaka ukweli wake, wala haikuingia akilini mwa mtu yeyote kuhoji juu ya usahihi wake. Hata al-Dhahabi, - licha ya chuki yake na Ahlul-Bayt (a.s.) - amekiri wazi kabisa ukweli wake ndani ya *Talkhis Al-Mustadrak* yake.[143] Na yule mgomvi Ibn Hajar Makki, pamoja na upinzani wake, ameitaja ndani ya kitabu *chake as-Sawaiq al-Muhriqa* ameisimulia Hadithi hii katika *shubuhat* ya 12 akidondoa maelezo ya wasimuliaji wa Hadithi mashuhuri kabisa wanaochukuliwa na Ahlus-Sunna kama ni wapokezi maarufu na wa kutegemewa wa hadith katika uk. 29. Hadithi hii isingethibitishwa usahihi wake, basi al-Bukhari asingeiingiza kwenye *as-Sahih* yake kwani alikuwa mkali wakati wowote inapokuja kwenye kutaja sifa na mafanikio ya Ali na Ahulul-Bayt (a.s.).

Hata Muawiyah ambaye alikuwa ndiye kiongozi wa lile kundi lililoasi dhidi ya Amirul-Muminin Ali na aliyetangaza uadui na akapigana naye, akamlaani kutoka kwenye mimbari za waislamu na kwenye majukwaa, na akawaamuru wengine kufanya vivyo, kamwe hakuikataa au kutilia shaka usahihi wa hadithi ya *Manzila*. Wala hakulifuatilia lile jambo na kuingia kwenye ubishani na Sa'd Ibn Abu Waqqas ambaye, kwa mujibu wa Muslim, alipoulizwa na Muawiyah ni kwa nini alisita kumshutumu "Abu Turab," alijibu kwa kusema:[144] "Mimi sitamlaani kamwe wala kuzungumza maneno ya fedhuli madhali ninazikumbuka sifa bora tatu ambazo nimezisikia mimi mwenyewe binafsi kutoka kwa Mtukufu Mtume. Ningekuwa na moja tu ya hizo sifa zake za kipekee, ningeipenda na kuithamini sana kuliko kundi la ngamia wekundu. Nimemsikia Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.), ambaye wakati huo alikuwa anataka kufuatana na watu wachache katika baadhi ya kampeni zake za kivita bila ya Ali, akimwambia Ali: "Wewe hufurahii (huridhiki) kwamba cheo chako kwangu ni sawa na kile cha Harun kwa Musa isipokuwa tu kwamba hakutakuwa na Mtume baada yangu?"[145] Muawiyah alipigwa na bumbuwazi, lakini alijizuia kumshinikiza Sa'd.

Kinachovutia kwa nyongeza juu ya yote haya, Muawiyh mwenyewe amerejea Hadith hiyo, Ibn Hajar anasema katika kitabu chake, *Al-Sawa'iq al-Muhriqa:* "Ahmad ibn Hanbal amesimulia kwamba mtu mmoja alimwendea Muawiyah na akamuuliza maswali juu ya dini, na jubu lake lilikuwa: 'Peleka swali lako kwa Ali, kwa sababu yeye anayo elimu bora zaidi.' Bado yule mtu akasema: 'Ningependelea jibu

[143] Usahihi wa hadith hii umeelezwa katika barua ya 26.

[144] Hii inaonekana kwenye mlango unaozungumzia fadhila za Ali kwenye uk. 324, Juz. 2, ya *Sahih* yake

[145] Al-Hakim pia anasimulia riwaya hii mwanzoni mwa uk. 109, Juz. 3 ya *al-Mustadrak* yake, pia akiukubali usahihi wake kutokana na vipimo vya Bukhari na Muslim. Imam Thalabi pia ameinukuu kwenye *Talkhiis* yake na ameikubali kwamba ni sahihi.

lako wewe mwenyewe juu ya swali hili kuliko hilo atakaloweza kutoa Ali.' Muawiya alimfunga mdomo na kusema; 'Ni kauli mbaya hiyo ninayoisikia kutoka kwako. Unamchukia mtu ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa akimuandaa na kumfundisha kama ndege mlezi anavyolisha kinda kwa kumtumbukizia kwa mdomo wake punje baada ya punje [146] kinywani mwa kinda lake, na ambaye Mtukufu Mtume Yeye alimuambia:Una cheo sawa na kile cha Harun kwa Musa isipokuwa kwamba hakutakuwa na Mtume baada yangu, na ambaye kila wakati Umar alipochanganywa na jambo, alitafuta uvumbuzi kwake Ali…'"[147] Kwa ufupi Hadithi ya *Manzila* inafahamika mno, kwa kiasi kwamba Waislam wote, bila ya kujali Madhehebu yao na muelekeo wao, wanakubaliana kuhusu usahihi wake.

Watunzi wa *Al-Jama Baynas Sihah Al-Sitta na Al-Jami'Bayna as-Sahihain* wameinukuu, na imeingizwa katika *Sahih Bukhari* kuhusiana na vita vya Tabuk, na katika *Sahihi Muslim* katika mlango wa sifa za Ali, na katika *Sunan Ibn Majah* katika mlango wa ubora wa masahaba wa Mtume, na katika *al-Mustadrak* ya Hakim katika mlago wa sifa za Ali. Imam Ahmad ibn Hanbal ameisimulia katika *Musnad* yake kutoka kwa Sa'd ibn Waqqas na amenukuu vyanzo mbalimbali vinavyounga mkono. Vilevile ameisimulia hadith hii kwenye *Musnad* hiyo kutoka kwa Ibn Abbas, Asma bint Umais, Abu Sa'id al-Khudri, Muawiyah ibn Abu sufyan,[148] na masahaba wengine wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Al-Tabarani ameinukuu kama ilivyosimuliwa na Asma bint Umais, Umm Salamah, Jaish Ibn Janadah, Ibn Umar, Ibn Abbas, Jabir ibn Suumra, Zayd ibn Arqam, Baraa ibn Aazib, Ali Ibn Talib (as)[149] na wengine wengi. Al-Bazzar ameiweka ndani ya *Musnad* yake,[150] na vilevile Tirmidhi ndani ya *sahihi* yake[151] kwa njia ya hadithi ya Abu Sa`id al-Khudri, na Abdul Barr ameisimulia katika *al-Isaba* kwenye mlango unaomzungumzia Ali; kisha baada ya kuitaja akasema: "Hii ndio Hadithi sahihi zaidi kabisa na mashuhuri mno ya Mtume (s.a.w.w.) na imesimuliwa na Sa`d Ibn Abu Waqqas," na kisha anaongeza: "Hadithi iliyosimuliwa na Sa'd ibn Waqqas imenukuliwa na idadi ya watu wengi kama ilivyoelezwa na Ibn Abu Khaythamah na wengineo….. na imesimuliwa pia na Ibn Abbas, Abu Sa`id Khudri, Umm Salamah, Asma bint Umais, Jabri Ibn Abdullh na masahaba wengine wengi wa Mtukufu Mtume, ambao majina yao yameachwa kwa sababu ya ufinyu wa nafasi." Haya ni maneno ya Abdul Barr.

Wapokezi, waandishi wa wasifu na wanahistoria wote ambao wamesimulia juu ya vita vya Tabuk wameisimulia Hadithi hii bila ya tofauti yoyote. Na waandishi wa masuala ya makamusi, wa zamani na pia wa wakati huu, bila ya kujali ile mielekeo ya upendeleo wao wa kidini au kimadhehebu, wote wameisimulia Hadithi hii katika dondoo zao za kutoa wasifu wa Ali. Hadith hii inasimuliwa pia katika vitabu vyote vinavyosimulia juu ya fadhaila za Ahlul Bayt, au juu ya sifa za masahaba wa Mtume (s.a.w.w.) na waandishi mashuhuri kama vile Ahmad ibn Hanbal na wengine wa kabla na baada ya zama zake. Na hii ni moja ya Hadithi ambazo zinakubaliwa na Waislam wote wa vizazi vyote vya zamani na vya zama hizi.

Hakuna umuhimu wowote katika shaka iliyoonyeshwa na al-Amadi kuhusu usahihi wa Hadithi hii au vyanzo vyake. Elimu yake ya Hadithi mtu huyu ilikuwa mbovu sana, na hukmu yake juu ya usahihi wa hadithi hii au kuaminika kwa vyanzo vyake ni kama uamuzi wa watu wa kawaida wasiojua au kuelewa lolote kuhusu mada yenyewe. Na ilikuwa ni elimu yake kubwa juu ya ujuzi wa *usuli* ndio ambayo

[146] Hii ina tokeza kwenye Maqsad ya tano pale mwandishi anapojadili Aya 14 Sura ya 11, uk, 107 ya *Sawaiq al Muhriqah.*

[147] Allamah Ibn Hajar, baada ya kunukuu tukio hili amewanukuu wasimulizi wengine ambao baadhi yao wameongeza kwamba Muawiyah alimuamuru mtu huyo kusimama na kuondoka mbele yake na akasema: "Mwenyezi Mungu akufanye kilema! Kisha akaliondoa jina lake kwenye orodha ya wanaolipwa. Taz. *Sawaiq al-Muhriqah* uk. 107. Hii inaashiria kwamba, mbali na Ibn Hanbal, muhadithina wengi wamesimulia hadith ya Manzilah kutoka kwa Muawiyah.

[148] Maqsad ya tano ya Aya ya 14 sura 11, katika *al-Sawaiq al- Muhriqa*, uk. 107, kama kwenye tanbihi ya barua ya hapo juu.

[149] Kama Ibn Hajar anavyoelezea katika Hadithi ya kwanza ya zile arobaini zilizomo katika sura ya 9, uk. 72 wa Al-*Sawaiq al- Muhriqa* yake. As-Suyuti, amesema yafuatayo wakati alipokuwa anamjadili Ali (a.s.) katika *Tarikh Khulafa* yake kwamba: "Al-Tabarani ameisimulia Hadithi hii toka kwa watu wote hawa, ambapo Suyuti ameongezea juu yao jina la Asma binti Qays."

[150] As- Suyyati anaelezea hivyo wakati akimjadili Ali (a.s.) katika mlango wake juu ya makhalifa katika ukurasa wa 65.

[151] Tazama Hadithi ya 4 hadi ya 25 ya *Kanz al-Ummal*, uk. 152, Juz. 6.

imemuweka yeye kwenye mtanziko huo. Alipoiona Hadithi hiyo kuwa ni hoja ya wazi na isiyopingika ikiunga mkono uandamizi wa Ali bila kuacha namna mbadala mbali na kumkubali Ali kama mrithi wa haki wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), yeye alionyesha shaka juu ya usahihi wake ili aweze kukwepa uamuzi wake usiopingika (ila kwake yeye usiopendeza) wa mwisho. Umbali na ukweli ulioje! Na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA ISHIRINI NA TISA

## DHUL- HIJJAH, 20, 1329 A.H.

**I. Kuamini Hoja zetu Kuhusu Usahihi wa Hadithi ya Manzila,**

**II. Kutilia Shaka Matumizi yake ya Jumla,**

**III. Shaka juu ya Hadith kuwa Uthibitisho wa Uimam wa Jumla wa Ali.**

Yote uliyoyataja katika kuthibitisha usahihi wa Hadithi ya *Manzila* kwa kweli hayana hata chembe ya shaka yoyote ndani yake. Na Al-Aamidi amefanya kosa ambalo linaashiria kiwango chake na ujuzi wa Hadithi na wasimulizi. Mimi nimekusumbua kwa kutaja maoni yake (juu ya riwaya hiyo) ambapo umetaabika katika kufafanua kwa kirefu kuwa ni ya uongo. Hili ni kosa langu ambalo kwalo ninaomba msamaha wako nawe unaustahiki kuuombwa.

Nimekuja kujua kwamba wapo wengine mbali na al-Aamidi kutoka miongoni mwa wapinzani wako ambao wanadai kwamba Hadithi ya cheo (al-Manzila) haina matumizi ya jumla, na kwamba haithibitishi Uimam au Uandamizi wa jumla wa Ali. Inathibitisha tu uandamizi wake kwa ajili ya kutokuwepo kwa Mtume (s.a.w.w.) pale alipokwenda kwenye vita vya Tabuuk, na kwa kuunga mkono maoni yao wanarejea kwenye maneno ya Hadithi yenyewe na lengo lake. Wanasema kwamba maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w) yanastahili tu kwenye mazingira ya wakati, yaani pale alipomuacha yeye kama muandamizi wake hapo Madina wakati wa vita vya Tabuk. Imamu, amani iwe juu yake, alimuuliza: "Unaniacha mimi hapa miongoni mwa wanawake na watoto?" Ndipo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.") akamjibu kuwa: "Wewe huridhiki kwamba cheo chako kwangu ni sawa na kile cha Harun kwa Musa, isipokuwa kwamba hakutakuwa na Mtume baada yangu?" kana kwamba yeye (s a w) akielezea kwamba cheo chake kwake ni kama kile cha Harun kwa Musa pale tu Musa alipomuacha yeye amuwakilishe miongoni mwa watu wake wakati alipoelekea Mlima Sinai kwa mawasiliano ya siri na Mola Wake. Hivyo makusudio hasa ya maneno ya Mtume (s.a.w.w.) yalikuwa kwamba Ali ashikilie, kwa kuhusiana naye, nafasi kama ile mpaka atakaporejea kutoka Taabuk, kama Harun alivyokuwa kwa Musa wakati wa kuondoka kwenda Tuur (Mlima Sinai) kuwasiliana na Mola Wake."

Inaweza kusemwa kwamba hata kama Hadithi hii ikichukuliwa kama ya kutumika kijumla haitoi uthibitisho kamili (wa uandamizi wa jumla wa Ali) kwa sababu ilikuwa kwa lengo lile la tukio maalum na kauli ya jumla ambayo imeainishwa kwa lengo maalum, na kauli ya jumla huwa inapoteza ujumla wake unapopatikana umakhususi, na haiwezi kutumika kama ushahidi katika mas'ala mengineyo. Na amani juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA THELATHINI

## DHUL-HIJJAH 22, 1329 A.H.

**I. Wenye Asili ya Lugha ya Kiarabu Wanaiona ya Jumla, ya Kutumika pote,**

**II. Uongo wa Maoni Kwamba Riwaya ilihusu Tukio Maalum,**

**III. Kupingana kwa Maoni kwamba Riwaya hiyo siyo Ushahidi wa Uandamizi wa Jumla wa Ali.**

Kwamba riwaya hiyo ni ya matumizi ya jumla ama laa tunaliacha hilo kwenye uamuzi wa wale ambao lugha mama kwao ni Kiarabu na ambao wana ujuzi sana nayo. Wewe ni bingwa wa lugha ya Kiarabu na fasihi yake, ambaye uamuzi wako hauwezi kukataliwa wala kupingwa. Hivyo ni yapi maoni yako kuhusu suala hili? Na ni yapi maoni ya wazalendo wenzio Waarabu? Je wana shaka yoyote kuhusu ujumla wa Hadith al-Manzila? Mimi sidhani hivyo. Kwa bingwa wa lugha ya Kiarabu kama ulivyo haiwezekani kutilia shaka ujumla wa nyongeza ambayo ni nomino ya jumla na upana wake wenye kujumuisha maeneo yake yote. Kama wewe kwa mfano, ukiniambia. “Ninakupa wewe mamlaka yangu ya uhakimu,” mamlaka yako hivi yataishia kwenye baadhi ya masuala machache yasifike kwenye mambo mengine? Au kauli yako itakuwa ya jumla na yenye kuingiza mambo yote? Mwenyezi Mungu aepushilie mbali wewe kuona vinginevyo mbali na kuwa ya jumla, au kuifanya kuwa yenye mipaka katika upana na matumizi yake. Kama khalifa wa Waislam atamwambia mmoja wa maafisa zake; “Nimekuteua wewe kuwa mtawala mahali pangu juu ya watu,” au “utakuwa na cheo kama kile nilichokuwa nacho juu yao, au “nafasi yako kuhusiana na watu itakuwa sawasawa na yangu,” au “utaiendesha nchi yangu mahali pangu,” kitakuja akilini mwa mwenye kuambiwa kitu chochote mbali na kwamba utawala wake, cheo na nafasi au uendeshaji katika hali zote vitakuwa ni sawa na vile alivyokuwa khalifa? Au itamaanisha mipaka ya wakati na mahali katika utawala, cheo, nafasi na uendeshaji wa ofisa huyo? Kama mtu atadai kwamba mwenye kuambiwa atashika utawala, cheo, nafasi na uendeshaji katika mazingira maalum au katika masuala maalum, je hataonekana kwamba sio mtiifu au mwenye uchu?

Kama Khalifa wa Waislam atakuwa amemwambia mmoja wa mawaziri wake: “Wewe utashika nafasi ileile wakati wa utawala wangu, kama nafasi ile aliyoshika Umar wakati wa utawala wa Abubakr, bali wewe sio sahaba.” Sasa kwa mujibu wa matumizi ya Waarabu, kauli hii itaonekana, kulingana na kanuni za kawaida, kama yenye kudokeza kwamba huyo waziri atatekeleza mamlaka ya Umar katika baadhi ya mambo au mazingira maalum au kuelekea kwenye hatua fulani au kwenye mamlaka yote bila ya mipaka? Una maoni gani juu ya hili? Wallahi nina hakika utaichukulia kuwa ni utumikaji wa jumla. Na nina hakika kwamba utakiri kwamba hadith ya Mtukufu Mtume: “Cheo chako kwangu ni kama kile cha Harun kwa Musa,” nafasi ya Ali (a.s.) ilikuwa ni katika vipengele vyote kama ilivyokuwa kwa Haruni na Musa kama ilivyoelezwa kwenye mifano hiyo hapo juu. Inaunga mkono uandamizi wa Ali (a.s.), hususan pale alipouondoa Utume, (ambapo ina maana kwamba Ali alikuwa na haki zote na mamlaka kamili kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama ambavyo Harun alikuwa nayo kutoka kwa Musa bali Utume wake Harun ukiwa ndio upungufu). Tafadhali hebu tafakari juu ya hilo na pia waulize Waarabu kwani ndio majirani waliokuzunguka, iwapo wanaichukulia utumikaji wa hadith hiyo kuwa wa jumla au wenye mipaka.

Na kuhusu nadharia iliyotolewa na mpinzani wetu ya kwamba Hadihi hii imemwekea Ali haki na fursa za Harun wakati ule tu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa amekwenda Tabuuk, inapingwa kwa misingi miwili:

**Kwanza,** Hadithi yenyewe ni ya utumikaji wa jumla, kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Hata kama tukichukulia kwamba tukio la hadith kwamba ni makhsusi, haidhoofishi ujumla wa hadith, kwa sababu kikanuni, wakati mahususi wa kauli ya jumla haubadilishi utumikaji wa jumla wa kauli kuwa utumikaji maalum au uliyoainishwa. Chukulia kwamba umemuona mtu akiwa kwenye hali ya kunajisika (ana janaba) akigusa Ayatul-Kursiyu kwa mfano, na ukamwambia: "Hairuhusiwi mtu yoyote asiye tohara kugusa aya za Qur'ani Tukufu." Sasa katazo hilo litaishia kwa mtu huyo na Ayatul-Kursiyu tu basi, au itakuwa ni kwa jumla ya aya zote za Qur'ani na kwa watu wote wasio na tohara? Sidhani kama mtu yeyote ataelewa kwamba katazo hili linatumika kwenye Ayatul-Kursiyu tu, sio kwa aya nyingine za Qur'ani, na kwa mtu mwenye 'Janaba' tu wala sio kwa kila asiye na tohara. Kama mganga atamuona mgonjwa wake anakula tende na akamkataza kula vitu vitamu, kukatazwa huko kutachukuliwa kutumika kwenye wakati maalum na kwa tende tu au kutakuwa kwa nyakati nyingene za maradhi kama hayo na kujumuisha kila kitu chenye utamu pia? Sidhanii kwamba mtu yoyote atachukulia katazo hili kuwa ni la wakati ule maalum kwa kula tende tu, isipokuwa yule ambaye hana uelewa wa kanuni, asiyejua sarufi ya lugha ya Kiarabu, asiyetambua kabisa matumizi yake na mgeni kabisa kwenye dunia yetu hii hasa. Katika mifano hiyo hapo juu, utumikaji wa katazo ni wa jumla ingawa kauli yake ilitolewa kwenye tukio maalum. Kadhalika katika Hadithul-Manzila, ambayo iko sambamba kabisa na mifano hii, utumikaji wa tamko kuhusiana na nafasi ya Ali (a.s.) ni wa jumla, ingawa tamko lilifanywa kwenye tukio maalum la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuondoka Madina na kuelekea Tabuuk.

**Pili**, Hadithi hii haifungiki kwenye tukio la vita vya Tabuk tu, hivyo mpinzani wetu hawezi kuwa mkaidi na kushikilia maoni kwamba matumizi yake yalikuwa kwa wakati ule tu. Kuna hadith sahih na *mutawatir* kutoka kwa Maimamu miongoni mwa kizazi kitoharifu cha Mtume (s.a.w.w.) zinaothibitisha kwamba Mtukufu Mtume kwenye mahala pengine pengi pia amemtawaza cheo hicho. Wale wanaotaka kujiridhisha kuhusu jambo hili wanaweza kurejea kwenye vitabu vya hadith vya Shi'ah. Na wale wanaotaka kuyakinisha jambo hili pia wapekue vitabu vya hadith vya ki-Sunni ambavyo vinathibitisha riwaya zetu. Upinzani kwamba mafuhumu ya Hadithi hii ni ushahidi wa kutumika kwake kwenye tukio moja tu la vita vya Tabuk tu hayana msingi, na hayastahiki kutiliwa maanani.

**Tatu,** upinzani kwamba kauli ya jumla inayotokana na tukio maalum haiwezi kutumika kwenye matukio mengine ni makosa ya dhahiri kabisa na upotofu mbaya sana, na mtu anayezua upinzani wa (ujumla wa) hadith ambayo ndio mada ya mjadala wetu hana mantiki, ama yuko kwenye hali ya kuzimia au kama mtu anayempanda mnyama kwenye giza, au aliye kwenye usiku wa msukosuko. Tunamuomba Allah (swt) atuepushe na ujahilia huo, na tunamtukuza Yeye kwa kutuweka salama katika afya. Kwa kweli uainishaji wa kauli yenye utumikaji wa ujumla hauizuii kutumika kama hoja katika suala jingine kama hilo kama uainishaji huo si wa kauli jumuishi, hususan pale ambapo uainishaji huo ni wa kuungana na kauli ya jumla kama ilivyo kwenye hadithi hii iliyoko kwenye uchambuzi. Kwa maneno haya "bwana akimwambia mtumishi wake: "Leo mkirimu kila atakayenitembelea isipokuwa Zayd." Kisha mtumishi aache kumkirimu mtu asiyekuwa Zayd miongoni mwa waliomtembelea bwana wake, bila shaka watu wa kawaida watamuona mtumishi hana nidhamu na ameasi amri, na wenye hikma watamuona anastahili lawama, na watahukumu kiakili na kisheria kuwa anastahili adhabu kwa utovu wake wa nidhamu, na kwa wale wenye ufahamu wa matumizi ya lugha hawatasikiliza visingizio vyake kama atasema kauli hiyo ilitolewa katika hali maalum, na kwa hiyo imepoteza ujumla wake. Kwa upande mwingine watachukulia kisingizio chake kuwa kibaya zaidi kuliko kosa lake lenyewe. Hii si kwa sababu nyingine isipokuwa ni kwa kuwa utumikaji wa jumla kwa watu wengine unaonekana wazi.

Na wewe unajua kwamba Waislam na wengineo siku zote wamezoea kutoa kama hoja kauli ya jumla iliyoainishwa bila ya kipingamizi chochote kile. Hii imekuwa ni desturi iliyokubaliwa na watu huko

nyuma na masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na waliowafuatia *(tabiin)* na pia wale waliofuata baadaye, vivyo hivyo hadi leo. Na hususan hii ilikuwa ni desturi ya Maimamu wote miongoni mwa kizazi kitukufu cha Mtume (s.a.w.w.) na Maimamu wengine wote miongoni mwa Waislam, na hili ni suala ambalo haliruhusu kuzulia shaka yoyote ile. Na kwako wewe huu utakuwa ni ushahidi wa kutosha juu ya kauli ya jumla iliyoainishwa au mahususi kuwa yenye kutumika kwenye masuala mengine pia. Na kama isingekuwa hivyo, yaani kutoka kwenye umaalum kwenda kwenye ujumla, basi milango yote ya elimu ingebaki imefungwa kwa maimamu wanne wa Ahlus-Sunnah na wanachuoni wengine walioamua au kufikia sheria ndogo kutoka kwenye misingi ya sheria. Kwa hakika gurudumu la elimu linazunguka katika mhimili wa kutumia kauli za jumla, na hakuna kauli ya jumla isipokuwa ina ainisho lake, na kama kauli za jumla zitaachwa, basi jengo lote la elimu ya mwanadamu litaanguka chini na mlango wa elimu utafungwa. Tunaomba hifadhi kwa Allah (swt), na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 31

## DHUL-HIJJAH 22, 1329 A.H.

**I. Kuomba Matukio Mengine ya Hadithi hii.**

Hukutaja matukio mengine ya Hadithi hii kuwa imesemwa mahali pengine popote mbali na Tabuk. Ninayo shauku kubwa ya kujulishwa matukio mengine ya furaha (ambamo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amemfananisha Ali na Harun). Tafadhali nifikishe kwenye chemchemi za maji (yaani matukio mengine). Na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA 32

## DHUL-HIJJAH 24, 1329 A.H.

**I. Moja ya Matukio ni pale Mtume (s.a.w.w.) Alipokutana na Umm Saliim,**

**II. Suala la Binti wa Hamza,**

**III. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Kumuegemea Ali,**

**IV. Udugu wa Awali,**

**V. Kufunga Milango,**

**VI. Mtukufu Mtume Alitumia Kutoa Mfano wa Farqdain (Nyota mbili Angavu Karibu na Ncha ya Kaskazini ya Dunia Ambazo Wanamaji Hugundulia Mwelekeo) Kati ya Ali na Harun.**

Moja ya matukio muhimu sana ya hadithi hii ya cheo "*Hadithul-Manzila*" ilikuwa ni tukio la kule kukutana kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa mazungumzo na Umm Saliim.[152] Alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzoni kabisa kuingia kwenye Uislam na alikuwa mwanamke mwenye akili sana. Alifaidi hadhi ya hali ya juu kabisa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kutokana na kuwa miongoni mwa watu wa mwanzoni kabisa kuukubali Uislam, na kwa sababu ya uaminifu wake na nia zake nzuri na umadhubuti wa kustahimilia dhiki walizosababishiwa waumini wa Kiislam na makafiri. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alikuwa akimtembelea na kuzungumza naye nyumbani kwake mwenyewe. Siku moja Mtukufu Mtume alimwambia: "Ewe Umm Saliim! Nyama ya Ali ni nyama yangu, na damu yake ni damu yangu; yeye anayo nafasi kwangu kama Harun alivyokuwa kwa Musa."[153] Ni lazima utakuwa unajua kwamba Hadithi

[152] Yeye alikuwa ni binti ya Milhan Ibn Khalid al-Ansari na dada yake Haram Ibn Milhan. Baba yake na kaka yake waliuawa kishahidi wakipigana kwa niaba ya Mtukufu Mtume (s a w). Alikuwa ni bibi mwenye tabia tukufu mno na busara. Yeye alisimulia Hadithi nyingi za Mtukufu Mtume (s. a. w.w.), na mwanawe, Anas, pamoja na Ibn Abbas, Zayd Ibn Thabiti, Abu Salmah Ibn Abdul Rahman na wengineo wamesimulia riwaya alizozisimulia. Yeye alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo waliokubali kuingia na walinganiaji wa Uislam. Wakati wa kipindi cha ujahilia kabla ya Uislamu, alikuwa mke wa Maliki Ibn al-Nadhr ambaye kutoka kwake alimzaa Anas Ibn Maliki. Mwanzoni mwa Uislamu, aliwatangulia watu wengi kusilimu, na alimshawishi mume wake, Maliki kumwamini Allah na Mtume wake lakini alikataa; hivyo yeye akamuacha, na yeye, Malik kwa hasira zake akaondoka kwenda Syria ambako alifariki akiwa kafiri. Umm Saliim alimtua mwanawe ambaye wakati huo alikuwa na umri wa miaka kumi kumtumikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na Mtume aliukubali utumishi wake kwa ajili ya mama yake.Wanaume wengi wa Kiarabu wenye hadhi walimchumbia, lakini wakati wote alikuwa akisema: "Mimi sitaolewa mpaka Anas atakapofikia utu uzima na awe na uwezo wa kunganyika na wanaume." Hiyo ndiyo sababu Anas alikuwa akiesma: "Mwenyezi Mungu amzawadie mama yangu, kwani alikuwa mlezi wangu mzuri sana." Abu Talhah al-Ansari alisilimu na kuwa Mwislam mikononi mwa Umm Saliim. Yeye alimchumbia wakati akiwa bado ni kafiri, akamkatalia mpaka alipokubali kuingia Uislam kwa mfano wake na hivyo kusilimu kwake kukawa ndio mahari yake kwa mama huyu. Alipata mtoto wa kiume kutokana na Abu Talha, lakini mtoto alishikwa na maradhi na akafariki. Aliwaomba watu wake kwamba mtu yeyote asimtangulie katika kutoa habari za kifo chake kwa Abu Talha kabla yake. Wakati mume wake aliporudi nyumbani na kumuulizia kuhusu mwanawe, yeye alisema: "Yupo kwenye ametulia mno kuliko mwanza." Yeye akafikiria kwamba mtoto wao alikuwa amelala. Alimuandalia mumewe chakula cha jioni ambacho alikila. Kisha yeye akavaa mavazi yake mazuri kabisa na kujipamba na kuweka manukato kwa ajili ya mume wake, na mumewe akaenda kulala naye na kufanya jimai. Kesho yake akamwambia mumewe: "Mwanao amefariki." Abu Talhah aliisimulia habari hii kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambaye naye akamwambia."Mwenyezi Mungu aufanye usiku huo kuwa wenye baraka kwenu nyote. Mama huyu akaendelea kusema: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alimuomba Mwenyezi Mungu anijaalie mimi baraka na neema. Katika usiku ule ule alishika mimba ya Abdullah ibn Abu Talhah ambaye juu yake mwenyezi Mungu alimjaalia kumpata Ishaq ibn Abdullah ibn Abu Talhah, ambaye alikuwa na kaka zake tisa na wote ndugu kumi walikuwa wanachuoni mashuhuri wa elimu ya dini. Umm Salim alikuwa akishiriki katika misafara ya kivita ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Katika siku ya Uhud, yeye alikuwa na sime mkononi mwake ambayo angefumulia matumbo ya kafiri yoyote wa Makka ambaye angediriki kusogelea karibu yake. Alikuwa ndiye mwanamke bora katika kuhudumia Uislamu na kutangaza. Simjui mwanamke mwingine yeyote ambaye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akimtembelea nyumbani kwake mwenyewe na aliyekuwa pia akimzawadia Mtume. Yeye alikuwa anaitambua vyema hadhi na umuhimu wa jamaa wa karibu wa Mtume (s.a.w.w.) na mwenye ujuzi wa haki zao na fadhaili zao, rehema Zake Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote.

[153] Hadithi hii, yaani hiyo iliyosimuliwa na Umm Salim ni namba 2554 katika *Kanz-al-Ummal* kwenye Jz. 4, uk. 154. Imejumlishwa pia ndani ya *Muntakhab al-Kanz;* hivyo rejea kwenye mstari wa mwisho pembezoni mwa ukurasa wa 31 wa Jz. 5 katika *Musnad ya Ahmad*, ambapo hadithi hiyo inatokeza kwenye maelezo mafupi ya ziada.

hii ilikuwa ni tamko lisilo la kuandaliwa la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) lisilo na sababu dhahiri au rasmi ama tukio kwa ajili yake, isipokuwa kama tangazo au bishara njema ya ushauri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusiana cheo cha makamu wake wa jumla wakati wa uhai wake, na ambaye atachukua nafasi yake (ya mamlaka) mara atakapokuwa ameaga dunia. Kwa hiyo sio busara wala haki kuishia utumikaji wa hadithi hii ya cheo "*Manzila*" kwenye vita vya Tabuk tu.

Hadithi kama hiyo ilitamkwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika suala la binti wa Hamza ambaye kulikuwa na mzozano juu yake kati ya Ali, Ja'far na Zayd. Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) ndipo basi akasema: "Oh Ali! Wewe kwangu ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa….."

Kadhalika hadithi hii ilitamkwa wakati Abu Bakr, Umar, na Abu Ubaydah Ibn Jarrah walipokuwa pamoja na Mtume (s.a.w.w.) aliyekuwa amemuegemea Ali. Mtume (s.a.w.w.) alimpigapiga Ali mabegani na akasema: "Oh, Ali! Wewe ulikuwa ndiye muumini wa kwanza kushawishiwa na Imani na wa kwanza kuingia Uislamu, na unacho cheo kwangu kama kile[154] cha Harun alichokuwa nacho kwa Musa."[155]

Na ni moja ya zile Hadithi alizosimulia Mtukufu Mtume wakati wa tukio la Udugu wa Kwanza lililofanyika huko Makka kabla ya kuhama miongoni mwa Muhajirin, ambapo Ali (a.s.) alichaguliwa kama ndugu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwa kuwaacha wengineo.

Hadith hii ilirudiwa tena katika tukio la Udugu wa Pili, ambao ulisimamishwa huko Madina baina ya Muhajirin na Ansar, miezi mitano baada ya kuhama. Katika matukio yote haya, Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alijichagulia mwenyewe Ali kuwa ndugu yake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimtwaa Ali kama ndugu yake kuliko wengine wote,[156] na akimwambia: "Wewe kwangu ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa, lakini kwa hakika hapatakuwa na Mtume baada yangu." Idadi kubwa ya hadithi na mutawatir kuhusu suala hili zimesimuliwa kwetu na Maimam wa Ahlul-Bayt (a.s.). Kama ukitaka kuziona riwaya zilizosimuliwa na wengine kuhusu ule udugu wa kwanza, tafadhali rejea ile Hadithi iliyosimuliwa na Zayd Ibn Abu Awfih, ambayo pia imesimuliwa na Imam Ahmad Ibn Hanbal kwenye kitabu chake *Manaqib Ali* (yaani Sifa na Ubora wa Ali ibn Abi Talib), na Ibn Asakir katika *Tarikh* yake,[157] Al-Baghawi na Tabraniy katika *Mu'ajam* zao, al- Baruudi katika *al-Marifat*, na Ibn Adi[158] na wengineo. Hadithi hii ambayo ni ndefu sana na ambayo ina maelezo kamili kuhusu udugu huo inaishia na maneno aliyoyasema Ali:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nafsi yangu (kama) imekufa, na mgongo wangu (kama) umevunjika, baada ya kuona kwamba umeunga undugu miongoni mwa masahaba zako ambapo umeniacha mimi peke yangu. Kama hii ni kutokana na kutoridhika, basi ninakuomba msamaha kwa ukarimu wako na uilinde heshima yangu. Mimi nipo kwa ajili yako."

Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: 'Ninaapa kwa yule aliyenituma mimi kwa haki, sikukubakisha wewe ila kwa ajili yangu mwenyewe. Wewe kwangu ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa, isipokuwa

[154] Imam Nasa'i ameielezea hadith hii katika uk. 19 wa kitabu chake *Ikhtisasul Alawiya.*

[155] Hii imenukuliwa na al-Hasan ibn Badr na al-Hakim katika mlango wake juu ya *Kunniyat*, na al-Shirazi katika mlango wake wa *Alqaab*', na Ibn al-Najjar pia ameisimulia ambayo inatokeza mara mbili katika uk. 395 wa *Kanz al- Ummal* Jz. 6. ni Hadith ya 6029 na pia 6032.

[156] Akizungumzia kuhusu Ali (a s) katika *Istiiab* yake, Ibn Abd al-Birr anasema: "Mtume wa Allah, (s. a. w.w) Aliunga udugu miongoni mwa muhajiria, kisha kati ya Muhajiria na Ansar. Katika matukio yote haya, yeye (s. a. w. w) alimwambia Ali (a s) peke yake kwamba: "Wewe ni ndugu yangu katika dunia hii na Akhera," kisha akaunga udugu kati yake mwenyewe na Ali (a. s.)." Maelezo zaidi yamo kwenye vitabu vya wasifu wa Mtume (s.a.w.w.) na vya Hadithi kuhusu matukio haya mawili. Kwa maelezo zaidi juu ya udugu wa kwanza, rejea uk. 26, Jz. 2 ya *Al-sira al- Halabiyya*, na kwa undugu wa mara ya pili katika uk. 120 wa Jz. 2 pia ya *Al-Sira al-Halabiyya*, ambamo utakuta jinsi Mtume (s.a.w.w) alivyompendelea Ali (a s) katika matukio yote hayo kuliko mwingine yeyote katika udugu. Maelezo hay ohayo juu ya udugu wa kwanza na wa pili yanapoatikana katika *al-Sira Al-Dahlaniyya*, kama yalivyo katika *al-Sira al-Halabiyya*, na pia ameeleza kwamba ule udugu wa pili ulitokea miezi mitano baada ya kuhama (*Hijirah*).

[157] Hii imenukuliwa kutoka kwa Ahmad na kwa Ibn Asakir na kundi la wasimulizi waaminifu kama vile al-Muttaqi al-Hindi, tafadhali rejea kwenye Hadithi ya 918 ya *Kanz al-Ummal* yake, mwanzoni mwa ukurasa wa 40 wa Jz. 5. Na pia kwenye Hadithi ya 5982 katika uk. 390, Jz. 6 ambapo ameinukuu kutoka kwenye *Manaqib Ali* cha Imam Ahmad.

[158] Wanachuoni wengine waaminifu wameinukuu hadith hii kutoka kwa Maimamu hawa wa Ahlus-Sunnah, mmoja wao akiwa ni al-Muttaqi al-Hindi. Tafadhali rejea kwenye Hadithi Na. 919 mwanzoni mwa ukurasa wa 41 wa Jz. 5 ya kitabu chake cha *Kanz al-Ummal*.

hapatakuwa na Mtume baada yangu. Wewe ni Ndugu yangu, na mrithi wangu.' Ali (a.s) akamuuliza: 'Ni nini nitakachorithi mimi toka kwako?' Yeye Mtume (s.a.w) akamjibu: "Kile ambacho Mitume wa kabla yangu walikiacha kama urithi: Kitabu cha Mola Wao, na Sunnah zao wenyewe na wewe utakuwa pamoja nami na binti yangu Fatimah katika kasri langu ya peponi. Wewe ni ndugu yangu na mshirika wangu." Kisha Mtume (s.a.w.w.), rehema na amani iwe juu yake na juu ya kizazi chake, akasoma aya hii:

**"….. wawe ndugu, juu ya viti wakielekeana ….." (15:47)**

Kuhusu ule Udugu wa Pili tafadhali rejea kwenye Hadith iliyosimuliwa na Tabrani *Al-Tafsir Kabir* yake, na kusimuliwa na Ibn Abbas. Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alimwambia Ali (a s):

"Huna furaha kwa sababu nimeanzisha udugu baina ya Ansar na Muhajirnia na kwamba sikukuchagulia ndugu kutoka miongoni mwao? Huridhiki wewe kwamba nafasi yako kwangu ni kama ile ya Harun kwa Musa, isipokuwa hakutakuwa na Mtume baada yangu?"[159]

Hadithi hiyo hiyo pia ilisimuliwa pia wakati milango ya masahaba iliyokuwa imeeleke msikiti wa Mtume hapo Madina ilipoamriwa kufungwa isipokuwa ule wa Ali. Inakutosha nukuu ya riwaya ya Jabir Ibn Abdullah Ansar ambaye anasema: Mtume wa Allah, rehema na amani juu yake na juu ya kizazi chake, amesema; "Ewe Ali! Imeruhusiwa juu yako kufanya katika msikiti huu chochote kile ambacho mimi ninaruhusiwa, na wewe kwangu kwa uhusiano ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa, isipokuwa hakutakuwa na Mtume baada yangu." Hudhaifa Ibn Usaid ali-Ghiffari amesema kwamba: "Mtume (s.a.w) wakati mmoja alitoa khutuba katika tukio la kufungwa kwa milango hiyo, ambapo alisema: 'Kuna baadhi ya watu ambao wamehuzunika na kutokubaliana na kuuacha kwangu wazi mlango wa Ali na kufunga milango ya wengine. Sikumruhusu kwa mapenzi yangu binafsi Ali kubakia msikitini na kuwatoa wengine nje ya msikiti. Ninaapa Wallahi kwamba Allah ndiye aliyewatoa na kumbakisha Ali humo. Allah Mwenye kuheshimika na Mtukufu aliwasiliana na Musa na ndugu yake juu ya amri ya kujenga majumba katika mji (huko Misri) kwa ajili ya wafuasi wao na kuyafanya makazi yao kuwa Qibla na kutekeleza swala zao,' mpaka akafikia kusema: 'Nafasi ya Ali kwa kuhusiana na mimi ni kama Harun alivyokuwa kwa Musa, na yeye ni ndugu yangu, na hairuhusiwi kwa yeyote kulala na mwanamke ndani ya msikiti isipokuwa Ali.'"

Kuna matukio mengi ya Hadithi hii tunayojadili ambayo hayahitaji kutajwa katika barua fupi kama hii, hivyo ni matumaini yangu kwamba matukio niliyoyataja hapa yanatosha kubatilisha madai kwamba hii Hadithi ya cheo (*Manzila*) ilikuwa kwa tukio maalum la vita vya Tabuk tu. Kwa kuzingatia wingi wa matukio niliyotaja hapo juu, madai hayo yanapoteza nguvu na kuonekana hayana msingi kabisa.

Yeyote ambaye amechunguza vizuri na kwa makini wasifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), atajua kwamba yeye, rehema na amani ziwe juu yake na juu ya kizazi chake, alikuwa akiwafananisha Ali na

[159] Hii imenukuliwa na al-Muttaqi al-Hindi katika *Kanz al-Ummal* yake. Vilevile tafadhali rejea kwenye uk. 31 wa *Muntakhab* ya *Kanz al-Ummal* kwenye pambizo ya *Musnad Ahmad* Jz. 5, ambamo utaikuta neno kwa neno kama vile tulivyoitoa hapo juu. Hebu tazama hii hali ya usuhuba mzuri, upole, na upendo kama wa baba anayejaribu kutuliza hisia za mtoto wake, upendeleo na huruma ambavyo maneno haya "umedhika ….. " yanawasilisha. Pengine huenda ukazungumzia kwamba wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa tayari amekwishamteua Ali kama ndugu yake katika tukio la Udugu wa Kwanza, asingekuwa na mashaka pia katika utwaaji wake katika tukio la Udugu wa Pili na angefikiria hili tukio la baadae kwamba ni lenye kufanana na lile la mwanzo na akangojea kwa subira kabisa mpaka kumalizika kwa kadhia hiyo. Mimi ningesema kwamba hakuna kulinganishwa kati ya matukio haya ambako kungeweza kufanyika kwa sababu Udugu wa Kwanza ulikuwa baina ya Muhajir tu; na Muhajir mmoja akafanywa ndugu wa Muhajir mwingine, ambapo kwenye lile la safari ya pili ilikuwa ni baina ya Muhajirina na Ansari, Muhajir mmoja katika tukio la pili aliweza kuunganishwa na Ansar – na Ali kwa kawaida angetegemea udugu uunganishwe kati yake na Ansar na wala sio na Mtume (s.a.w.w) ambaye alikuwa ni muhajirina kama yeye. Pale Mtume wa Mwenyezi Mungu alipokuwa hakuunga udugu kati yake na Ansar yeyote, mashaka kidogo yaliitawala akili yake na akadhani kwamba amepuuzwa, kwa hiyo akawa na wasiwasi. Lakini Allah na Mtume Wake walikuwa wakimpendelea Ali kuliko Muhajir na Answari wote, na kwa hiyo Mtume wa Allah (s.a.w.w) akatwaa udugu, na Ali kinyume na mategemeo ya wengi.

Harun kama zile nyota mbili angavu (*farqadain*) ambazo zinafanana sana, hakuna moja inayotofautiana na nyingine. Na ni moja ya dalili za ujumla wa cheo hicho kilichotajwa kwenye Hadithi ya cheo. Hata kama dalili hizo zikipuuzwa, maneno yenyewe hasa ya hadith hii yanawasilisha akilini utumikaji wa jumla bila kisingizio chochote, kama tulivyoeleza hapo juu, na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 33

## DHUL- HIJJAH 25, 1329 A.H.

**I. Ni Lini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Aliwafananisha**

**II. Ali na Harun na Hizo Nyota Mbili (*Farqadain*)?**

Bado hakijabainika waziwazi kile unachomaanisha kusema kwamba yeye, rehema na amani ziwe juu ya kizazi chake alikuwa akiwalinganisha Ali na Harun na nyota mbili, *farqadain* zinazofanana sana; na ni lini alipofanya hivyo? Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 34

## DHUL-HIJJAH 27, 1329 A.H.

**I. Katika Siku ya Shabar, Shubayr, na Mushbir,**
**II. Siku ya Tukio la Kuunga Udugu,**
**III. Siku ya Kufunga Milango.**

Chunguza wasifu wa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake na kizazi chake, na utamkuta yeye akiwafananisha Ali na Harun kama nyota mbili angavu katikati ya mbingu, na macho mawili usoni. Hakukuwa na tofauti katika nafasi au cheo kilichoshikiliwa na wawili hawa katika umma zao husika.

Utaona ambavyo yeye Mtume, rehema na amani ziwe juu yake na juu ya kizazi chake, alivyokataa kuwaita watoto wa Ali majina isipokuwa kama yale yaliyofanana na ya watoto wa Harun, kwa kuwaita Hasan, Husein na Muhsin na akasema: "Nimewapa majina ya watoto wa Harun, Shabar Shabayr na Mushbir,"[160] akikusudia kwa hilo kukazia kule kufanana kikamilifu kati ya wawili hao katika hatua na mazingira ya hali zote. Kwa sababu hii, Mtume (saww) alimtwaa kama ndugu yake na akampendelea yeye juu ya wengine wote, ili kule kufanana kwa wote wawili kuhusiana na ndugu zao wahusika kuweze kuwa sawa kabisa, na alipenda pia kuhakikisha kwamba hapakuwa na jambo lolote la tofauti linaloachwa kati yao. Ni jambo linalofahamika sana kwamba yeye rehema na amani ziwe juu yake na juu ya kizazi chake, aliunga udugu miongoni mwa sahaba zake mara mbili, akimfanya Abu Bakr katika tukio la kwanza kuwa ndugu wa Umar, na Uthuman ndugu wa Abdul Rahman Ibn Auf. Katika udugu wa safari ya pili, Umar alifanywa kuwa ndugu wa Atban Ibn Malik. Lakini kama ujuavyo vizuri kabisa bado katika matukio yote, Ali alifanywa kuwa ndugu wa Mtume wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake na juu ya kizazi chake.

Kwa ukosefu wa nafasi hatuwezi kutoa hapa zile hadith sahihi zote juu ya suala hili ambazo zimesimuliwa kupitia kwenye vyanzo vya kuaminika kama vile Ibn Abbas, Ibn Umar, Zayd Ibn Arqam, Zayd Ibn Abu Aufi, Anas Ibn Malik, Hudhaifa Ibn al Yamani, Makhduuj Ibn Yazid, Umar Ibn al-Khattab, al-Bara Ibn Azib, Ali Ibn Abu Talib, na wengineo, ambamo Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.) anasimuliwa kwamba alimwambia Ali: "Wewe ni ndugu yangu katika dunia hii na dunia ya kesho Akhera." [161]

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliweka mkono wake juu ya kichwa cha Ali akisema: "Hakika huyu ni ndugu yangu na mtekeleza wasii wangu na mrithi wangu miongoni mwenu, kwa hiyo, msikilizeni na mtiini." Yeye, (s.a.w.w.) siku moja alitoka nje kuja kuungana na masahaba zake akiwa na tabasamu pana usoni mwake. Abdul Rahman Ibn Awf akamuuliza ni nini kilichomfurahisha sana hivyo. Yeye (s.a.w.w.) akamjibu;

---

[160] Kuhusiana na hili riwaya nyingi zimesimuliwa kwa mujibu wa vyanzo sahihi vya hadithi za Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Rejea ukurasa wa 265 na 168, Jz. 3, ya *al-Mustadrak*, na utaona juu ya suala hili, hadithi ya wazi kabisa ambayo ni sahih kwa mujibu wa vipimo vya Masheikh wote wawili (Bukhari na Muslim). Imamu Ahmad vilevile ameinukuu hadithi iliyosimuliwa na Ali kwenye uk 98, Jz. 1, ya *Musnad* yake. Na Ibn Abdul-Bar pia ananukuu katika tafsiri ya mjukuu wa Mtume al- Hasan (as) kwenye kitabu cha *Isti'ab*, na hata al-Dhahabi pia ameinukuu katika kitabu chake *Talkhis*, akiukubali usahihi wake, pamoja na ushabiki wake wa kidini na muonekano wa mkengeuko kutoka kwa Harun wa taifa lake, na kutoka Shabir na Shubair wake. Vilevile imenukuliwa na Baghawi katika kitabu chake *Mu'ajam*, na Abdul Ghani kutoka kwenye kitabu chake *Iidhah*, kama ilivyoandikwa kwenye ukurasa wa 115 wa *al-Sawa'iq al-Muhriqa*, kutoka kwa Salman na Abdul Ghani katika 'Asakir.'

[161] Al-Hakim ameinukuu kwenye ukurasa wa 14, Jz. 3, ya kitabu chake *Al-Mustadrika* kama ilivyosimuliwa na Ibn Umar akinukuu vyanzo viwili tofauti ambavyo vyote ni sahihi kwa viwango vya Masheikh wote wawili. Al-Dhahabi vilevile ameinukuu kwenye kitabu chake *Talkhis* huku akikubali usahihi wake. Al-Tirmidhi vilevile anainukuu kwa aliyenukuliwa na Ibn Hajar katika ukurasa wa 73 wa kitabu chake *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*. Na wanahistoria waandishi ambao wametoa maelezo juu udugu huu wa mara mbili wameiandika hadithi hii kama yenye usahihi unaokubalika.

"Nimepokea habari njema kutoka kwa Mola Wangu kuhusu ndugu yangu na binamu yangu, na pia kuhusu binti yangu kwamba Mwenyezi Mungu amemchagua Ali kuwa mume wa Fatimah." (Hadith hii imesimuliwa na Abu Bakr al-Khawarizmi kama ilivyoelezwa katika uk. 103 wa Sawaiq al-Muhriqah.)

Wakati Bibi wa mabibi alipotoka kuelekea kwa mume wake, Ali, mkuu wa kizazi cha Mtume (s.a.w.w.), Mtume (s.a.w.w) akasema: "Ewe Umma Ayman nenda ukamchukue ndugu yangu." Umm Ayman akauliza: "Huyu ni ndugu yako, kisha bado unamuozesha kwa binti yako?!" Yeye akasema: "Naam hakika ni hivyo ewe Umm Ayman." Yeye Umm Ayman akaenda kumuita Ali ambaye alikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)[162] ambaye mara nyingi sana Mtukufu Mtume alikuwa akizungumza na Ali huku akisema, "Huyu ni ndugu yangu binamu yangu mtoto wa ami yangu wa kiumeni, mkwe wangu na baba wa wanangu."[163] Wakati mmoja wakati wa maongezi na Ali alimwambia: "Wewe ni ndugu yangu na rafiki yangu."[164] Katika tukio jingine alimwambia: "Wewe ni ndugu yangu, rafiki yangu na sahaba yangu huko peponi."[165] Yeye, (s.a.w.w) wakati mmoja alizungumza naye wakati walipokuwa wamehitifiana kati yake na kaka yake Ja'far, Zayd Ibn Harithah, akisema: "Lakini Ewe Ali! Hakika wewe ni ndugu yangu na baba wa wanangu na wewe unatokana nami, na wewe ni wangu."[166] Siku moja alimwambia Ali: "Wewe ni ndugu yangu na waziri wangu. Utalipa madeni yangu, utatimiza ahadi zangu, na utatekeleza majukumu ama kazi zangu."[167] Na pale kifo kilipomkaribia, wazazi wangu wote wawili wewe kafara kwa ajili yake, yeye alisema: "Niitieni ndugu yangu." Wakamuita Ali akaingia chumbani. Yeye (s.a.w.w.) akamwambia: "Sogea karibu yangu;" Ali (a.s) akamsogelea karibu zaidi na akakiweka kichwa cha Mtume kwenye paja lake. Alibaki akimnong'oneza sikioni mwake mpaka roho yake tukufu ilipotoka mwilini mwake na kiasi cha mate ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yalimdondokea Ali (a.s.).[168]

Mtume wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake na juu ya kizazi chake vile vile amesema: "Imeandikwa katika mlango wa Peponi: 'Hakuna mungu isipokuwa Allah, Muhammad ni Mtume wa Allah, Ali ni ndugu wa Mtume wa Allah."[169] Na katika ule usiku wa Hijrah Mtume alipotoka Makka kwenda Madina, Mwenyezi Mungu aliwafunulia Jibrail na Mikaili: "Nimeunga udugu kati yenu na nimekadiria kipindi cha uhai wa mmoja wenu kuwa kirefu kuliko cha mwingine. Je, mko tayari kuhiari kupeana kama zawadi huo urefu wa ziada wa uhai kati yenu?" Lakini kila mmoja alijipendelea mwenyewe hayo maisha marefu zaidi. Mwenyezi Mungu akasema: "Kwa nini msiige mfano wa Ali Ibn Abu Talib, nimeunga udugu kati yake na Muhammad (s.a.w.w). Sasa hivi amelala kwenye kitanda cha Muhammad kwa ajili ya kuyalinda maisha ya Muhammad kwa kuyatoa muhanga maisha yake mwenyewe. Sasa shukeni duniani wote wawili mkamlinde kutokana na maadui zake." Wote wakashuka. Jibrail akasimama kichwani kwa Ali, na Mikaili akasimama miguuni. Jibrail akaguta" "Hongera!

[162] Hii imenukuliwa na al-Hakim katika uk. 159, Jz. 3, ya *al-Mustadrak* yake. Na Dhahabi ameinukuu katika kitabu chake *Talkhis* huku akikiri usahihi wake. Ibn Hajar anainukuu katika sura ya 11 ya *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*. Wote wale walioandika kuhusu harusi ya al-Zahra (as) wameitaja bila tofauti yoyote.

[163] Hii imeandikwa na al-Shirazi katika kitabu chake "*Alaqah*," na Ibn Hajjar ambaye anamnukuu Ibn Umar, na Al-Muttaqi al-Hindi ameinakili katika kitabu chake *Kanz al-Ummal* na katika *Al-Muntakhab* yake ameimbatanisha pambizoni mwa kitabu chake *Musnad*; tafadhali rejea kwenye msitari wa pili wa pambizo kwenye uk. 32, Jz. 5.

[164] Ibn Abdul-Bar ameisimulia hii katika maelezo yake juu ya Ali (a.s.) katika *Isti'aab* akinukuu mlolongo wa vyanzo hadi kwa Ibn Abbas.

[165] Khatiib ameiandika hii kama hadith ya 6105 katika uk. 402 Jz. 6 ya *Kanz ul-Ummal.*

[166] Al-Hakim anainkuu katika ukurasa wa 217, Jz. 3, ya kitabu chake *al-Mustadrak*, akinukuu chanzo ambacho usahihi wa wasimuliaji wake unathibitishwa na Muslim. Al-Dhahabi amekiri ukweli huo huo katika kitabu chake *Talkhis* kwa kipimo hichohicho.

[167] Tabraniy ameinukuu katika kitabu chake *Al-Kabir* kutoka kwa Ibn Umar, na imenakiliwa na al-Muttaqi al-Hindi katika kitabu chake *Kanz al-Ummal* halikadhalika katika *Al-Muntakhab*; hivyo, tafadhali rejea kwenye yaliyomo kwenye pambizi ya uk. 32, Jz. 5, ya '*Musnad'*.

[168] Hii imenukuliwa na Ibn Sa'd katika uk. 51, Sehemu ya pili, Jz. 2, ya kitabu chake *Tabaqat*, na vilevile inatokeza katika uk. 55, Jz. 4, ya *Kanz al-Ummal.*

[169] Hii imenukuliwa na Tabraniy katika kitabu chake *al-Awsat*, na al-Khatib katika kitab chake *Al-Muttafaq wal-Muftaraq*, na imewasilishwa na mwandishi wa *Kanz al-Ummal*; hivyo, rejea kwenye Muntakhab na tazama tanbihi iliyojumuishwa katika ukurasa wa 35, J. 5, ya Musnad ya Ahmad. Vilevile imewasilishwa na Ibn Asakir katika tanbihi yake ukurasa wa 46.

Hongera! Ewe mwana wa Abu Talib. Hakuna mwingine kama wewe. Hata mwenyezi Mungu (s.w.t) anajigamba juu yako kwa malaika wake." Kuhusiana na tukio hilo, ndipo ikashuka Aya ya:

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ

"Na katika watu yupo auzaye nafsi yake kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu ….."( 2:207).[170]

Ali mwenyewe alikuwa mara kwa mara akisema: "Mimi ni mtumwa wa Allah (s.w.t) na ndugu wa Mtume Wake, na mimi ndio mkweli mkuu (*swidiq al-Akbar*) wa wote. Hakuna mwingine yeyote awezaye kusema hivi isipokuwa muongo."[171] Na kisha akasema:

"Wallahi mimi ni ndugu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na rafiki yake na binamu yake na mrithi wa elimu yake, nani mwingine mwenye cheo bora zaidi cha kumrithi yeye kuliko mimi?"[172] Na katika siku ya *Shura* (ile inayoitwa mashauriano ya kumchagua Khalifa) alimwambia Uthuman, Abu Rahman Sa'd na Zubeir: "Muapieni Allah na mnijulishe kama kuna yeyote miongoni mwenu mbali na mimi, ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu aliunga udugu pamoja naye miongoni mwa Waislam?" Wao wakajibu: "Wallahi hakuna yeyote."[173] Wakati Ali alipopambana na al-Walid katika vita vya Badr, Walid alimuuliza: "Wewe ni nani?" Ali akajibu: "Mimi ni mtumwa wa Allah na ndugu ya Mtume Wake."[174] Pale Umar al-ipokuwa Khalifa, siku moja Ali alimuuliza[175] "Tuseme wana wa Israil fulani wanakujia wewe, na mmoja wao akakuambia kwamba yeye ni mtoto wa ami yake Musa, je, angepata kipaumbele juu ya masahaba wake (wa Musa)?" Umar akajibu: "Ndiyo, hakika." Ali akasema: "Mimi, Wallahi ni ndugu wa Mtume wa Allah na mtoto wa ami yake." Umar akavua joho lake na akalitandaza kama zulia, huku akisema: "Wallahi wewe hutakaa mahali pengine popote pale mbali na hapa juu ya joho langu mpaka hapo tutakapoachana." Ali alikaa juu ya joho hilo na akabakia hapo mpaka walipoachana, na Umar alibaki amekaa mbele yake. Hii ilikuwa ni kukiri kipaumbele cha ndugu wa Mtukufu Mtume na binamu yake.

Loh! kugeuka gani kwa kalamu yangu! Mada yetu ilikuwa ni juu ya kufungwa kwa milango inayoelekea msikitini. Mtukufu Mtume (s.a.w) aliamuru milango ya nyumba za sahaba zake wote inayoelekea Msikiti ifungwe moja kwa moja, kwa sababu ilikuwa hairuhusiwi kuingia Msikitini katika hali ya najisi kuu (janaba). Lakini akaruhusu mlango wa Ali kubakia wazi, na aliruhusiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kuingia au kukatiza msikitini kama vile tu alivyoruhusiwa Harun kuingia au kupita katikati ya msikiti akiwa katika hali ya janaba. Na hivyo kutoa uthibitisho mwingine wa ujumla wa kufanana kwa wao wawili, amani iwe juu yao. Ibn Abbas anasema: "Mtume wa Allah, (s.a.w) alikuwa ameamuru milango yote inayoelekea msikitini kufungwa isipokuwa ule wa Ali, ambaye alikuwa akiingia humo hata alipokuwa

[170] Waandishi wa vitabu vya hadithi wameisimulia hadith hii katika *Masanid* zao, na imetajwa na Fakhrul-Din Razi wakati akitafsiri aya hii. Tafadhali rejea maelezo ya Suratul-Baqarah, ukurasa 189, Jz.2, ya *Al-Tafsir-al-Kabir*

[171] Tafadhali rejea Jz. 3, uk. 126 wa Mustadrak. Na Dhahabi ameiandika kwenye Talkhiis yake ambamo amekiri kwamba ni hadith sahihi.

[172] Hii imenukuliwa na an-Nasai katika *Al-Khasa'is al-Alawiyya*, na al-Hakim mwanzoni mwa uk. 112, Jz. 3, ya kitabu chake *Al-Mustadrak*, na Ibn Abu Shaybah na Abu Aasim katika *Al-Sunnan* zao, na Abu Na'im katika *Al-Ma'rifat*. Vilevile imeandiwa na al-Muttaqi al-Hindi katika *Kanz al-Ummal* na pia katika *Muntakhab al-Kanz* yake. Rejea kwenye yale ambayo yamo katika pambizo ya ukurasa wa 40, Jz. 5, ya *Musnad Ahmad*.

[173] Hii inanukuliwa na Ibn Abd'l-Birr katika maelezo juu ya Ali katika *Isti'ab* yake. Wanachuoni wengine maarufu na wa kutegemewa wameisimulia pia.

[174] Hii imenukuliwa na Ibn Sa'd wakati anajadili vita vya Badr katika *Tabaqat* , uk. 15, Sehemu ya Kwanza, Jz. 2.

[175] Kama ambavyo Dar Qutni ananukuu katika Maqsad ya tano ya aya mapenzi kwa kizazi cha Mtume "Mawadda" **(43:23)**, na ni aya ya 14 kati ya aya ambazo Ibn Hajar amezijadili katika Sura ya 11 ya *Sawa'iq al-Muhriqa*; Tafadhali rejea uk. 107 wa *Sawa'iq al-Muhriqa*.

na hali ya janaba, kwa sababu ilikuwa ndio njia pekee ya kuingia na kutokea nyumbani kwake."[176] Umar Ibn al-Khattab anasimuliwa kuwa amewahi kusema:[177] "Ali Ibn Abu Talib alijaaliwa mambo matatu. Kama mimi ningeangukiwa na moja ya hayo basi ningelithamini hilo zaidi kuliko msururu mzima wa ngamia wekundu – kumpata kwake Fatimah binti ya Mtume wa Allah kama mke wake, makazi yake pale msikitini pamoja na Mtume wa Allah, na kuwa halali kwake humo msikitini ambayo hayaruhusiwi humo kwa mwingine yeyote, na kule kupata kwake bendera ya Uislam wakati wa vita vya Khaibar." Hadith hii ni sahihi na ya kutegemewa vilevile kwa mujibu wa vigezo vya masheikh wawili, Bukhari na Muslim.

Siku moja Sa'id ibn Malik alisimulia hadithi sahihi inayoorodhesha sifa za kipekee za Amirul-Mu'minin Ali na akasema: "Wakati Mtume wa Allah alipoifunga milango yote pale msikitini, pamoja na ule wa al-Abbas, ami yake, Al-Abbas akamwambia: "Unafunga milango yetu sisi inayofungukia msikitini na kubakisha mlango wa Ali" Yeye, rehema na amani ziwe juu yake na juu ya kizazi chake akajibu: "Mimi sijafunga milango yenu wala kubakisha wa Ali kwa kupenda kwangu. Bali Allah (s.w.t) amewatoeni nje na kumbakisha yeye ndani ya msikiti."[178]

Zayd ibn Arqam alisema: "Masahaba wachache wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) walikuwa na milango ya nyumba zao iliyokuwa ikielekea Msikitini. Mtume wa Allah (s.a.w.w) akasema: "Fungeni milango yenu yote isipokuwa mlango wa Ali." Mazungumzo ya kutilia shaka amri hiyo yakazunguka. Hivyo, Mtume wa Allah (s.a.w.w) siku moja akasimama na kuhutubia. Akamshukuru Allah (s.w.t) kisha akasema: "Nimeamriwa na Mwenyezi Mungu kufunga milango yote isipokuwa ule wa Ali. Baadhi yenu mnalipinga hilo. Wallahi mimi sijafunga mlango, wala kufungua kwa kupenda kwangu. mimi nimetekeleza kile nilichoamriwa na Mola wangu kufanya.'"[179]

at-Tabrani ameandika katika *Mu'ajam al-Kabiir* yafuatayo kama ilivyosimuliwa na Ibn Abbas: "Siku moja Mtume wa Allah (s.a.w.w) alisimama na akasema: 'Sikuwatoeni nje wala sikumbakisha yeye kwa matakwa yangu binafsi; bali Mwenyezi Mungu ndiye aliyewatoeni na kumuacha yeye. Mimi ni mja mtiifu na nimefanya tu, kile ambacho nilikuwa nimeamrishwa kukifanya. Mimi sifuati chochote ila kile kilichofunuliwa kwangu kutoka kwa Mola Wangu"[180] Na Mtume wa Allah, wakati mmoja alimwambia Ali (a.s): "Ewe Ali! Hairuhusiwi kwa mtu yoyote, mbali na wewe kubakia ndani ya msikiti akiwa katika hali ya janaba."[181] Sa'd Ibn Abi Waqqas, al- Baraa' Ibn Aazib, Ibn Abbas, Ibn Umar na Hudhaifa Ibn Usaid al-Ghaffari, wote wamesimulia kwamba Mtume wa Allah, (s.a.w) siku moja alitoka nje na kuja Msikitini na akasema: "Mwenyezi Mungu amenishushia *wahyi* wa siri na kuniamuru kujenga msikiti mtukufu ambao ndani yake hakuna anayeruhusiwa kuishi humo isipokuwa mimi na ndugu yangu Ali tu.''[182]

Nafasi haituruhusu hapa kuelezea hadithi sahihi nyingine nyingi juu ya somo hili kama zilivyosimuliwa na Ibn Abbas, Abu Sa'id al-Khudri, Zayd Ibn Arqam, swahaba kutokaa kabila la Khath'aam, Asma bint

---

[176] Hadithi hii ni ndefu sana, na humo zimeandikwa sifa kumi za pekee za Ali, na tumeinukuu katika Barua ya 26.

[177] Inapatikana katika ukurasa wa 125, J. 3, ya *al-Mustadrak*. Imenukuliwa na Abu Ya'li, kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 3, Sura ya 9, ya *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*; hivyo, rejea kwenye ukurasa wa 76 wa kitabu chake. Vilevile imenukuliwa katika maana hii takriban kwa maneno hayahaya na Ahmad ibn Hanbal wakati alipokuwa ananukuu hadithi za Umar na mwanawe Abdullah, na wasimuliaji wengi waaminifu wa hadithi kupitia maeneo mbalimbali.

[178] Tafadhali rejea ukurasa wa 17, Jz. 3, ya *Al-Mustadrak*. Hii ni moja ya hadithi iliyothibitishwa usahihi wake na imenukuliwa na muhadithina wengi mashuhuri na wa kutegemewa.

[179] Ahmad ameichukua kama ilivyosimuliwa na Zayd ibn Arqam katika ukurasa wa 369, Jz. 4, ya *Musnad*. Vilevile Zayd ameisimulia kama ilivyoelezwa katika *Kanz-al-Ummal* na *Muntakhab* yake; tafadhali rejea kwenye pambizo katika uk. 29 wa Jz. 5 ya *Musnad*.

[180] al-Muttaqi al-Hindi ameirudia kuitoa tena hii mwishoni mwa pambizo katika uk. 29 wa Jz. 5 ya *Musnad*.

[181] Kama ilivyonukuliwa na al-Tirmidhi katika *Sahih* yake na kunukuliwa kutoka kwake na al-Muttaqi al-Hindi kwenye *Mutakhab* yake katika pambizo ya uk. 29 Jz. 5 ya *Musnad*. Vilevile imenukuliwa na al-Bazzaz kutoka kwa Sa'd, kama ilivyoelezwa katika hadithi ya 13 katika Sura ya 9, ukurasa wa 73 kitabu *Al-Sawa'iq al-Muhriqah* cha Ibn Hajar.

[182] Ali ibn Muhammad al-Khatib, mwanachuo wa Shafi'i ambaye ni maarufu kwa jina la Ibn al-Maghazili, ameiandika riwaya hii katika kitabu chake *Al-Manaqib* kama walivyoisimulia wote hao akinukuu vyanzo mbalimbali, na kutoka kwake imeinakiliwa na mwanachuoni mtafiti mwenye kuaminika al-Balkhi katika sura ya 17 ya kitabu chake *Yanabi al-Mawddah*..

Umais, Umm Salamah, Hudhayfah Ibn Usaid, Sa'd ibn Abi Waqqas, Baraa ibn Aazib, Ali ibn Abi Talib, Umar, Abdullah ibn Umar, Abu Dharr al-Ghifari, Abu Tufail, Buraydah al-Aslami, Abu Rafi, mtumwa wa Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.), Jabir Ibn Abdullah al-Ansari na wengine. Ifuatayo ni du'a ya kimapokezi ya Mtume wa Allah (s.a.w.w.):

"Ee Mola! Ndugu yangu Musa alikuomba akisema**: 'Ewe Mola wangu! Nikunjulie kifua changu Na unifanyie wepesi jambo langu. Na ulifungue fundo lilo katika ulimi wangu Wapate kufahamu kauli yangu. Na nipe waziri katika watu wangu Harun ndugu yangu. Niongeze nguvu zangu Kwaye Na umshirikishe katika jambo langu.' (20:25-32).** Nawe ukamtia moyo, ukamjibu: **'Tutautia nguvu mkono wako kwa ndugu yako. Na tutawapa madaraka hawatawafikia.' Qur'ani 28:35).** 'Ee Mola wangu! Mimi ni mja na mtumishi wako Muhammaad. Nakuomba unikunjulie kifua changu Na unifanyie wepesi jambo langu na unichagulie kutoka miongoni mwa ndugu zangu, Ali kuwa waziri wangu,'"[183]

Al-Bazzaz halikadhalika amesimulia hadith kama hiyo kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikamata mkono wa Ali na akasema: "Musa alimuomba Mola Wake ruksa ya kupata msaada wa Harun katika kutakasa msikiti wake, na mimi nimeomba ruksa ya Mola Wangu kutaka msaada wako katika kuutakasa msikiti wangu." Kisha akatuma ujumbe kwa Abu Bakr akimuamuru kufunga mlango wake, na Abu Bakr akasoma aya hii "Hakika sisi sote ni wa Allah na Kwake tutarejea." Kisha akasema "Nimesikia na nimetii". Kisha akatuma ujumbe mwingine kwa Umar, na mwingine kwa al-Abbas kadhalika kwa madhumuni hayo hayo. Kisha yeye (s.a.w.w.), akasema: "Sikuifunga milango yenu, wala sikuubakisha ule wa Ali kwa mapenzi yangu mwenyewe; bali Allah ameuacha wazi mlango wake na kuifunga ya kwenu." (Hii ni hadith ya 6156 katika uk. 48, Jz. 6 ya *Kanzul-Ummal*).

Kiasi cha hadithi zilizotajwa hapo juu kinatosha kuthibitisha kwamba cheo cha Ali kinafanana na cha Harun katika mazingira yote na hali zote, na amani iwe juu yako.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[183] Hii imenukuluiwa na Imamu Abu Is'haq al-Tha'labi katika *Tafsiir al-Kabir* yake wakati akisherehesha aya iliyoko Suratul al-Maidah kama ilivyosimuliwa na Abu Dharr al-Ghifari. Na yule mwanachuoni mtafiti al-Balkhi amenukuu maneno hayo hayo kutoka kwa Imamu Ahmad katika kitabu chake cha *Musnad*.

# BARUA YA 35

## DHUL-HIJJAH 27, 1329 A.H.

**1. Kuomba Uthibitisho Zaidi.**

Allah akubariki! Uwazi na busara zilizoje katika hoja zako. ufasaha na shabaha zilizoje katika uchambuzi wako! Tafadhali endelea kujitokeza na hoja na maelezo yaliyobakia. Wassalamu Aleykum.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 36

## DHUL-HIJJAH 29, 1329 A.H.

**I. Hadith Zilizosimuliwa Kutoka kwa Ibn Abbas, Imran, Buraydah', Ali, Wahab, na Ibn Abu Aasim,**

**II. Hadithi ya Fadhila Kumi.**

Rejea kwenye hadithi aliyoandika Abu Dawuud al-Tayalasi, kama alivyosimulia katika *Isti'ab* kwenye maelezo kuhusu Ali kutoka kwa ibn Abbas ambaye anasema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alimwambia Ali Abu Talib: 'Wewe ndio Bwana (*mawla*) wa waumini wote baada yangu.'"[184]

Imran ibn Hasin imesimulia Hadith sahihi nyingine kama hii. Yeye anasema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alituma kikosi cha jeshi chini ya ukamanda wa Ali ibn Abu Talib. Kutoka kwenye *Khums* ambayo aliipata, Ali alijitengea mwenyewe msichana mtumwa kama mgao wake. Hili halikuwapendeza baadhi ya watu wake, na wanne wao wakaamua kwenda kulalamika kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) dhidi yake. Wakati waliporejea walimwendea Mtume (s.a.w.w.) na mmoja wao alisimama na kusema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Umeona jinsi Ali alivyofanya hivi na hivi?' Mtume (s.a.w.w.) alimgeuzia mbali uso wake. Wa pili alisimama na kuzugumza kama alivyosema mwenzake, na pia Mtuume (s.a.w.w.) alimpuuza. Watatu alisimama na akarudia yaliyosemwa na wenzake, na yeye pia alipuuzwa. Wanne akasimama akaelezea vilevile kama walivyoelezea wenzake. Hapo ndipo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aliwageukia huku akiwa na dalili za hasira usoni mwake na kusema: 'Mnataka nini kwa huyo Ali? Hakika Ali anatokana na mimi na mimi natokana naye, na baada yangu yeye ndiye bwana (*mawla*) wa waumini wote.'"[185]

Hadith kama hiyo imesimuliwa na Buraydah ambayo matini yake ya asili haswa yanatokeza katika ukurasa wa 356 wa Jz. 5 ya *Musnad* ya Ahmad. Yeye Buraydah anasema: "Mjumbe wa Allah alipeleka majeshi mawili kwenda Yemen. Mojawapo liliongozwa na Ali ibn Abu Talib (a.s.), na lingine liliongozwa na Khalid ibn al-Walid na akawaambia hivi: 'Wakati mtakapochanganya majeshi yenu, Ali awe ndiye kiongozi wa wote,[186] na mtakapotengana, basi kila mmoja ni kiongozi wa Jeshi lake.' Tulikabiliana na

---

[184] Hii imenukuliwa na Abu Dawuud na wasimuliaji wengine wa hadithi kutoka kwa Abu Awanah al-Wazzah ibn Abdallah al-Yashkari ambaye ameipokea kutoka kwa Abi Balaj Yahya bin Salim Alfazari kutoka kwa Umar ibn Maimuun al-Abdi kutoka kwa ibn Abbas; ambaye aliisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Watu wote hawa ni wapokezi waaminifu, na Bukhari na Muslim wamesimulia kutoka kwao ispokuwa Yahya ibn Salim ambaye yeye hawakumnukuu. Lakini wakosoaji maarufu na magwiji wa hadith wamekiri uaminifu wake. Na alikuwa mmoja kati ya wale waliotumia muda wao mwingi katika kumuabudu Allah zaidi. Al-Dhahbi katika kitabu chake *Al-Mizan*, anaeleza kwamba Ibn Mu'in, an-Nasai, Dar Qutni, Muhammad ibn Sa'd, Abu Haatim, na wengine wengi wote walimchukulia kwamba alikuwa mkweli na mwaminifu.

[185] Hii imenukuliwa na wandishi wengi wa vitabu vya hadithi. Imamu an-Nasai ameiandika katika kitabu chake *Al-Khasa'is al-Alawiyya,* Ahmad ibn Hanbal katika uk. 438, Jz. 4, ya *Musnad* yak echini ya kichwa "Hadith ya Imran." al-Hakim katika uk. 11, Jz. 11. ya *al-Mustadrak* yake, Allamah Dhahabi katika *Al-Talkhis al-Mustadrak* wote wakikiri usahihi wake kwa mujibu wa vipima vya Muslim. Imenukuliwa na Ibn Abu Shaybah na Ibn Jarir kutoka kwa yule ambaye Muttaqi wa India, ameinakili katika uk.400, Jz. 6, wa kitabu chake *Kanz al-Ummal*. Imenukuliwa na al-Tirmidhi kutokana na vyanzo vya kuaminika kama ilivyotajwa na al-Asqalani katika maelezo juu ya Ali katika kitabu chake *Al-Isabah*. Mwanchuoni ibn al-Hadid Mu'tazili ameinukuu katika uk. 450, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul Balaghah*, akieleza kwamba Abu Abdullah Ahmad ameiandika hadith hii katika *Musnad* yake katika kurasa zake kadhaa, na vilevile katika kitabu chake *Fadha'il Ali*, na imesimuliwa na wasimuliaji wengi wa hadithi.

[186] Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) katika uhai wake wote kamwe hakuweka Ali (a.s.) kuwa chini ya mtu yeyote bali kinyume chake, wengine waliwekwa chini yake yeye na alikuwa ndiye mbebaji bendera wake katika kila vita kinyume na wengineo. Abu Bakr na Umar walikuwa askari wa kawaida katika jeshi la Usamah aliyekuwa ameshika bendera. Na kuna makubaliano ya maoni miongoni mwa muhadhitina na wanahistoria kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaweka katika vikosi vilivyokuwa chini ya ukamanda wa Umar ibn Aas ambaye walikorofishana naye. Hakim anaeleza ugomvi wao huo katika uk. 43, Jz. 3 ya Mustadrak yake na al-Dhahabi amelisimulia tukio hilo

kabila la Banu Zubayda la Yemen na Waislamu walipata ushindi dhidi ya washirikina na tukawauwa wapiganaji wao na kuwateka wanawake wao na watoto. Ali alijitingea msichana mmoja mateka wa vita kwa ajili yake mwenyewe. Khalid alimuandikia barua Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), kumjulisha tukio hilo na akanipa mimi barua hiyo kuiwasilisha. Nilipokuja kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) nikamkabidhi barua na akaisoma. Niliona dalili za hasira machoni mwake; kwa hiyo, nilimsihi kwa kusema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nakuomba unisamehe; ulinituma mimi na mtu na ukaniamuru nimtii, na nimefanya hivyo tu katika kuileta barua hii.' Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akasema: 'Kamwe msimshutumu Ali, kwani yeye anatokana na mimi na mimi natokana naye, na yeye ndiye bwana wenu baada yangu.'" [187]

Maelezo ambayo Imam An-Nasai ameyaandika katika ukurasa wa 17 wa *Al-Khasa'is al-Alawiyyah* ni: "Ewe Buraydah! Usijaribu kunifanya mimi niwe adui wa Ali. Kwa hakika Ali anatokana na mimi na mimi natokana naye, na yeye ndiye bwana wenu baada yangu." Kwa mujibu wa Jarir maelezo yenyewe ni[188] "Buraydah alisema hivi: "Mara tu, uso wa Mtume ulibadilika na kuwa mwekundu na akasema:

"Kwa yeyote yule ambaye anaamini kwamba mimi ni *mawla* wake, na Ali pia ni *mawla* wake." Yale mawazo maovu dhidi ya Ali yalitoweka mara moja na nikasema: "Kuanzia sasa kamwe sitakuja kusema vibaya juu ya Ali." Tabraniy, vilevile, amenukuu hadithi hii kwa urefu. Yeye anaandika: "Wakati Buraydah aliporejea kutoka Yemen na akaingia msikitini, aliona kundi la watu wamesimama mbele ya mlango wa chumba cha Mtume (s.a.w.w.). Walimsalimia Buraydah na wakamwendea na kumuuuliza habari kuhusu Yemen. Akasema: "Ni habari nzuri. Allah amejaalia ushindi juu ya Waislamu." Walimuuliza: "Basi nini kilichokuleta hapa?" Akasema: "Kutokana na *Khums* iliyopatikana, Ali amejitengea mwenyewe msichana mtumwa. Na nimekuja hapa kumjulisha Mtume kuhusu tukio hilo." Wakasema: "Ndio, mjulishe juu ya hilo, mjulishe ili Ali aweze kuanguka kwenye mtazamo wake Mtume (s.a.w.w.)."

Mtume (s.a.w.w.), aliyasikia mazungumzo yao kutokea nyuma ya mlango. Kwa ajili hiyo alitoka nje akiwa amekasirika na kusema: "Kumetokea jambo gani kwa watu nyie? Kwa nini mnazungumza mabaya dhidi ya Ali? Yeyote yule anayemchukia Ali ananichukia mimi pia, na yeyote anayejitenga na Ali amejitenga na mimi. Hakika Ali anatokana na mimi na mimi natokana naye. Yeye ameumbwa kutokana na udongo wangu mwenyewe, na udongo wangu mimi ni wa Ibrahim, na hata hivyo mimi ni bora zaidi kwa Ibrahim,[189] Badhi

katika Talkhiis yake ambamo ameeleza wazi kwamba hadithi hiyo ni sahihi. Lakini Ali (a.s.) hajawahi kuwekwa chini ya ukamanda wa mtu yeyote yule isipokuwa Mtume mwenyewe (s.a.w.w.) tangu Tangazo la Utume hadi kufariki kwake yeye (s.a.w.w.).

187 Haya yaliyoandikwa na Ahmad kwenye ukurasa wa 356 kama yalivyosimuliwa na Abdullah ibn Buraydah ambaye anainukuu kutoka kwa baba yake. Na tena kwenye ukurasa wa 347, Jz. 5, ya *Musnad* yake, kama ilivyosimuliwa na Sa'id ibn Jubayr kutoka kwa Ibn Abbas ambaye alisimuliwa na Burydah akisema: "Katika vita vya Yemen mimi nilikuwa pamoja na Ali, na niliona tabia yake ilikuwa ya ukali. Wakati niliporudi kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) nilimlaamikia juu ya tabia ya ukali ya Ali. Niliona uso wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ukibadika rangi, na akaniambia: 'Ewe Buraydah je, mimi sio bwana mwenye mamlaka zaidi juu ya waumini kuliko wao wenyewe?' Nikajibu: 'Ndio, hakika, Ewe Mjumbe wa Allah.' Akasema: 'Ali ni bwana (*Mawla)* wa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* wake.'" Hadithi hii imenukuliwa na al-Hakim kwenye ukurasa wa 110, Jz. 3, ya kitabu chake *Al-Mustadrak*, na muhadithina wengi wameinukuu hadith hii. Na utaona wazi kabisa kwamba hadithi hii inathibitisha ukweli wa imani yetu. Ule utangulizi: Je, mimi sio bwana mwenye mamlaka zaidi…….….?' bila utata kabisa unaashiria kwamba neno "*Mawla*" katika hadithi hii lina maana ya "Bwana mwenye mamlaka zaidi." Hadithi nyingine sawa na hii imesimuliwa na wasimuliaji wengi wa hadithi. Imamu Ahmad ameisimulia katika uk. 483, Jz. 3, ya *Musnad* yake, kama ilivyosimuliwa na Umar ibn Shas al-Aslami ambaye alihudhuria vita vya Hudaybia. Yeye anasema: "Nilifuatana na Ali kwenda Yemen ambaye alinifanyia ukali wakati wa safari hiyo, kiasi kwamba sikumfurahia. Wakati niliporudi Madina, nililalamika dhidi yake msikitini. Taarifa zikamfikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Nilipoingia msikitini asubuhi iliyofuata, nilimkutaa Mjumbe wa Allah (saw) alikuwa ameketi katikati ya baadhi ya Masahaba. Mara tu aliponiona alinikazia macho kwa hasira. Nlipokaa chini yeye Akaniambia: 'Ewe Amr! Kwa jina Allah umenihuzunisha.' Mimi nikasema: 'Naomba hifadhi ya Allah kwa kukuhuzunisha wewe, Ewe Mjumbe wa Allah!' Akasema: 'Kwa hakika umenisababishia huzuni, zingatia kwamba yeyote mwenye kumsababishia huzuni Ali amenisababishia huzuni na mimi pia.'"

188 Kama ilivyonukuliwa na al-Muttaqi al-Hindi kwenye ukurasa 398, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*. Vilevile ameinakili katika *Muntakhab al-Kanz* yake.

189 Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema kwamba Ali ameumbwa kutokana na udongo wake mwenyewe, hivyo kwa hakika yey ni bora kuliko Ali. Isije ikawa maneno yake: "Na mimi nimeumbwa kwa udongo wa Ibrahim," yakifikiriwa kimakosa kuwa na maana kwamba Ibrahim ni bora kuliko yeye, amani iwe juu yake na kizazi chake, kauli ambayo hukinzana na ukweli wenyewe, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alieleza wazi kwamba yeye ni mbora kuliko Ibrahim (a.s.) katika kuzuia mapema tafsiri potovu.

yao ni kizazi cha wengine, na Allah ni Mwenye kusikia Mwenye Ujuzi. Ewe Buraydah! Hujui kwamba Ali anastahiki mgao mkubwa zaidi kuliko msichana mtumwa aliyemchukua? Na kwamba hakika yeye ni bwana wenu baada yangu?"[190] – Hakuna shaka yoyote kuhusu usahihi wa hadihti hii, na imesimuliwa kupitia vyanzo vingi mutawatir na vya kuaminika hadi kufikia kwa Buraydah mwenyewe.

al-Hakim amesimulia hadithi nyingine muhimu sawa na hii kutoka kwa Ibn Abbas ambamo anaorodhesha sifa kumi mahususi na za pekee za Ali. Ibn Abbas anasema: Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimwambia Ali hivi: "Baada yangu wewe ndiye bwana (*mawla* - mlezi) wa kila Mu'umin."[191] Halikadhalika, kuna hadithi nyingine kama hiyo ambamo yanaonekana maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Ewe Ali! Nimemuomba Allah akujaalie neema tano ambapo nne amezitakabalia na amekatalia moja……. Na amenikubalia hili la kwamba wewe utakuwa bwana (*Mawla)* wa waumini wote baada yangu."[192]

Hadithi kama hiyo inasimuliwa na Ibn al-Sakna kutoka kwa Wahab ibn Hamzah kama ilivyotajwa katika maelezo ya Wahab katika *Isaba.* Wahab anasema kwamba: "Siku moja nilisafiri na Ali na nikamuona ni mkali, kwa hiyo nikafikiria kumlalamikia juu ya ukali wake kwa Mtume wakati wa kurudi. Niliporejea nilitoa malalamiko kwa Mtume wa Allah dhidi ya Ali, ambapo yeye Mtume (s.a.w.w.) alisema: 'Kamwe usije ukasema tena maneno kama hayo kuhusu Ali, kwani baada yangu yeye atakuwa ndiye bwana wako.'" At-Tabrani ameisimulia hii katika kitabu *Mujma'al-Kabir,* akimnukuu Wahab kwamba: "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: Usiseme hivi kuhusu Ali, kwani baada yangu yeye atakuwa na mamlaka makubwa juu yako." [193] Ibn Abu 'Asim ameisimulia hadithi hii kama ilivyosimuliwa na Ali ambaye ameisikia kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe:

"Je mimi sio mbora zaidi kwa waumini kama bwana wa maisha yao wenyewe?" Watu wakajibu kwa kubali. Kisha Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Ali ni bwana (*mawla*) wa yeyote yule ambaye mimi ni bwana (*mawla*) wake. [194]

Kuna hadithi nyingi sahihi na *mutawatir* zilizosimuliwa kupitia kwa Maimamu miongoni mwa Ahlul-Bayt (as) kuhusiana na ubwana wa Ali (a.s.). Bali kilichoelezwa hapo juu kitaonekana kukidhi lengo letu. Zaidi ya hayo, ile aya ya ubwana (*al-wilayat*): **Hakika walii wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukui, (5:55),** iliyomo kwenye Kitabu Kitukufu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu pia nayo inaunga mkono kauli yetu. Shukurani ziwe kwa Allah, Mola wa walimwengu wote. Wassalam Aleykum.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

[190] Ibn Hajar amnakili hadithi hii kutoka kwa Tabrani kwenye ukurasa wa 103 Sura ya Pili ya kitabu chake *Al-Sawa'iq al-Muhriqa* wakati alipokuwa anashughulikia *maqsad* ya pili ya aya 14. Lakini wakati alipokuja kwenye kauli isemayo: "Je, hujui kwamba Ali anastahiki mgao mkubwa zaidi ya kijakazi (msichana mtumwa) aliyemchukua?" kalamu yake ikasimama. Hilo lilikuwa linachukiza kwake yeye na akamalizia kunakili kwa kuandika "…..hadi mwisho wa hadith! Hii sio ajabu kwa mkereketwa kama alivyokuwa yeye; na shukrani ziwe kwa Allah swt. aliyetuweka mbali na ushabiki huu.

[191] Hadithi hii inanukuliwa na al-Hakim mwanzoni mwa uk. 134, Jz. 3, wa *Al-Mustadrak*, na al-Dhahabi katika *Talkhis al-Mustadrak*, akikiri usahihi wake, na an-Nasai katika uk. 6 wa *Al-Khasa'is al-Alawiyya*, na Imamu Ahmad katika uk. 331, Jz. 1, ya *Musnad* yake. Tumeinukuu neno kwa neno mwanzoni mwa barua yetu ya 26.

[192] Hadithi hii ni Na. 6048 na inaonekana katika ukurasa wa 396, Jz. 6. ya *Kanz al-Ummal*,

[193] Hadithi hii ni Na. 6048 katika *Kanz al-Ummal*, ukurasa wa 155, Jz. 6.

[194] Hadithi hii imenakiliwa na al-Muttaqi al-Hindi kutoka kwa ibn Abu Asim katika uk. 397, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal.*

# BARUA YA 37

## DHUL-HIJJAH 29, 1329 A.H.

**I. *"Walii"* Ni Neno Lenye Maana Nyingi,**

**II. Sasa, Uko Wapi Ushahidi wa Wazi?**

Neno *"Walii"* ni neno lenye maana nyingi na lina maana ya msaidizi, rafiki, mpenzi, mkwe wa kiume, mfuasi, mshirika, jirani, au mlezi na kadhalika. Yeyote yule achukuaye usimamizi wa jambo la mtu mwingine ni *"Walii"* wake. Huenda neno Walii katika hadithi ambazo umezinukuu laweza kumaanisha tu: 'Ali ni msaidizi wenu, au rafiki yenu, au mpendwa baada ya Mtume;' sasa uko wapi ushahidi wa wazi juu ya urithi wa jumla?

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 38

## DHUL-HIJJAH 29, 1329 A.H.

**I. Maana Halisi Ya Neno *"Walii",***

**II. Vidokezo Vya Maudhui na Mpangilio wa Maneno.**

Moja kati ya maana kadhaa za neno *"Walii"* ulizozitaja katika barua yako ni 'yule anayesimamia mambo ya mtu mwingine, yeye anaitwa *"Walii"* wa mtu huyo.' Ni kwa maana hii ambapo neno *"Walii"* limetumika katika hadithi tulizozitaja katika barua yetu iliyotangulia na hiyo ndiyo maana ambayo huja akilini mara moja kwa mwenye kusikia neno '*Walii*' katika riwaya hizi. Tunasema: "Kwamba *"Walii"* wa mtoto mdogo ni baba yake kisha babu yake (mzaa baba), kisha ikiwa wote hawapo basi mrithi wa yeyote kati yao, na wakikosekana wote hao basi mtu au mwangalizi anayesimamia sheria za kidini." Hili neno 'Walii' kwa hiyo lina maana ya mtu anayesimamia mambo na anayetekeleza mamlaka kwa niaba ya mtu mwingine.

Vidokezo vinaashiria, kama watu wote wenye hekima wanavyojua, kwamba ni maana hii ndio iliyokusudiwa katika hadithi hizo, kwani maneno yake (s.a.w.w.), "Na ni *Walii* wenu baada yangu" kwa uwazi yanaweka ukomo na kuyafungia mamlaka yote kwa Ali (a.s.) ya kusimamia mambo yake yeye (s.a.w.w.) baada ya kufariki kwake. Hili linawajibisha kuchagua maana tuliyoainisha, na wala halikubaliani na matakwa mengine. Neno '*Walii*' haliwezi katika riwaya hizi kumaanisha vinginevyo na wala halikubali tafsiri yoyote ile, kwa sababu msaada, upendo, urafiki, na mambo kama hayo hayakomei kwa mtu mmoja. Waumini wanaume na wanawake wote wanapendana ni marafiki wa kila mmoja wao (wenyewe kwa wenyewe). Kama maana ya neno walii ni msaidizi na rafiki tu na sio kama tunavyoelewa na tulivyoeleza hapo juu basi kuna ubora gani au fadhila gani maalum ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimaanisha kumtunukia Ali (a.s.) au ni siri gani aliyotaka kudhihirisha kwa kumtangaza Ali kwa kusisitiza kabisa kwamba ni ndugu yake na *Walii* wake katika hadithi chungu nzima zilizotangulia kuelezwa?

Ni jambo liko mbali na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) la kuonyesha shauku kubwa ama kuweka umuhimu kiasi hicho kwa ajili tu ya kufafanua kile ambacho tayari kiko wazi, au kueleza jambo ambalo lilikuwa dhahiri, tena kiasi cha kurudia tangazo hilo mara kwa mara. Hikma yake kamilifu, umaasum imara na kumalizikia kwa utume, kwake yeye kunamfanya awe mbali kabisa na kuhusika katika kueleza chenye udhahiri, kusisitiza kilicho wazi na kufanya marudio yasiyo na msingi wowote. Isitoshe bado hizi hadithi zimeweka wazi kabisa kwamba Ali ndiye, au atakuwa ndiye bwana (*Mawla*) wa Umma baada ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Hili linafanya iwe ni muhimu na lazima zaidi kulielewa neno 'Walii' kwa maana hiyo na kulitengea maana hiyo hiyo kama ambavyo tumeieleza hapo juu. Haiingii akilini kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikusudia neno Walii kuwa na maana hiyo ya msaidizi, rafiki na mpendwa, na kadhalika, kwani Ali hakuwa msaidizi, rafiki na mpendwa wa Umma wa Waislamu wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Tangu kulelewa kwake na kukuzwa kwenye mapaja ya Mtume (s.a.w.w.), akawa imara na mwenye nguvu chini ya ulezi na usimamizi wake (s.a.w.w.), mpaka nyakati za mwisho za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Ali aliendelea kusaidia, kuwa rafiki na kumpenda Mtume na wafuasi wake. Na kama unavyojua, msaada wa Ali (a.s.) na urafiki wake kwa Waislamu haukuhifadhika kwa ajili ya kile kipindi cha baada tu ya kifo cha huzuni cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Miongoni mwa mambo mengine yanayoonyesha kwamba neno ‘Walii’ linawasilisha maana ileile tuliyoeleza hapo juu, tafadhali rejea riwaya ya Imamu Ahmad katika uk. 347 Jz. 5 katika kitabu chake *Musnad* kama ilivyosimuliwa na Said Ibn Jubayr ambaye ameisikia kutoka kwa Ibn Abbas aliyeisikia kutoka kwa Buraydah mwenyewe akisema: “Katika mashambulizi ya kuvamia Yemen, mimi nilikuwa pamoja na Ali. Niliiona tabia yake ilikuwa ya ukali. Hivyo wakati niliporejea kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), nilimlalamikia kuhusu tabia ya ukali wa Ali. Hapo nikaona mabadiliko makali kwenye uso wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Yeye akaniuliza: ‘Ewe Buraydah! Je, mimi sio bwana mwenye mamlaka zaidi juu ya waumini kuliko wao wenyewe?’ Nilijibu: ‘Hakika ndivyo Ewe Mjumbe wa Allah.’ Yeye (s.a.w.w.) kisha akasema: ‘Ali ni bwana (*mawla)* wa yeyote yule ambaye anaamini kuwa mimi ni *mawla* wake.’” Hadithi hii inanukuliwa pia na al-Hakim katika *Mustadirak* Jz. 3, uk. 110, ambako amekiri kuwa ni sahihi kutegemea juu ya vigezo vilivyowekwa na Muslim, na Al-Dhahabi ameinukuu katika kitabu chake *Talkhis*, akikiri usahihi wake kwa mujibu wa vigezo hivyo vya Muslim. Wewe mwenyewe unajua umuhimu wa swali: “Je, mimi sio bwana mwenye mamlaka zaidi juu ya waumini kuliko wao wenyewe?” na kukazia kabisa ukubalikaji wa Ubwana wake yeye mwenyewe kabla ya kutangaza huo Ubwana wa Ali (a.s.). Hili pia linathibitisha kwamba neno *Walii* au *Mawla* lilitumika katika riwaya hizo hapo juu kwa maana hiyohiyo tuliyoeleza sisi. Na yeyote atakayezisoma riwaya hizi kwa utulivu na uadilifu na akazichunguza kwa makini, kwa hakika yeye ataelewa maana zake halisi na makusudio yake na atakuwa hana shaka kuhusu haya tuliyoeleza. Shukurani zote ni za Allah.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 39

## DHUL-HIJJAH 30, 1329 A.H.

**I. Kuomba Aya ya *Wilayat* (Ubwana au Ulezi au Mamlaka ya Juu, ya Imam Ali (a.s.).**

Uchambuzi wako ni mzuri wa kushangaza sana, hoja zako zinagonga kwenye shabaha yenyewe kwa usahihi kabisa, mwenye umahiri wa ajabu usio na kifani katika kumfikisha mshindani wako kwenye hoja yako. Mpinzani wako hawezi kuhimili mashambulizi ya hoja zako zenye nguvu. Mimi sasa ninaamini kabisa kwamba hizi riwaya husika zinapendekeza akilini jambo lilelile kama ulivyoeleza wewe [na kuthibitisha kwamba mamlaka ya kusimamia mambo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yaliwekwa mikononi mwa Imam Ali (a.s.)]. Lau isingekuwa kulazimika kwetu kuwaamini masahaba na kufuata njia yao, basi ningekubaliana na maamuzi yako. Lakini inavyoonekana sisi haturuhusiwi kukengeuka kwenye njia yao na kutafsiri riwaya au kuelewa maana ya neno '*Walii*' au '*Mawla*' katika maana tofauti na ile ambayo wao masahaba wameielewa. Tunapaswa kufuata mfano mzuri wa wahenga wetu, Allah awe radhi nao wote! Mwishoni mwa barua yako ya 36 ulisema: "Aya ya wazi ya Wilayat pia inaunga mkono maelezo yako kuhusiana na hadithi hizi." Lakini hukuinukuu aya hiyo. Tafadhali hebu fanya hivyo sasa hivi. Mwenyezi Mungu akipenda tutaichunguza.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 40

## MUHARRAM 2, 1330 A.H.

**I. Aya ya *Wilayat* na Kushuka Kwake Kuhusu Ali,**

**II. Ushahidi Kuhusu Kushushwa Kwake,**

**III. Sababu ya Kuitumia Kama Hoja.**

Sawa, nakutolea tena ile aya ya wazi ambayo ni moja kati ya dalili za Allah Aza wa Jalah, katika ushahidi Wake wa kuvutia kabisa ambao ni Qur'ani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema.[195]

**"Hakika walii wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukui. Na atakayemtawalisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini, basi kundi la Mwenyezi Mungu ndio watakaoshinda."** (Qur'ani 5:55-56)

Wanakubaliana kwa pamoja kwamba aya hii iliteremshwa kuhusu Ali wakati alipotoa pete yake kama sadaka wakati akiwa kwenye rukuu ndani ya swala.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameelezea kushuka kwa aya hii kuhusu Ali wakati alipotoa sadaka pete yake wakati akiwa amerukuu katika swala. Lakini kwa ajili ya faida yako tunaelezea riwaya za wazi kuhusiana na hili zilizosimuliwa kutoka kwenye vyanzo vingine. Kuna riwaya iliyosimuliwa na Ibn Salam ambaye sanadi yake ya wapokezi inapanda hadi kwa Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Tafadhali rejea kwenye *Sahih* ya *Nisa'i*, au katika *al-Jami Bayna al-Sihah al-Sittah,* katika tafsiri ya *Surat al-Ma'ida*. Halikadhalika, hadithi kama hizo zimesimuliwa na Ibn Abbas na Ali (a.s.). Tafadhali rejea maelezo juu ya aya hii katika kitabu cha Imam al-Wahidi*, Asbab al-Nuzuul* ambamo imo riwaya iliyosimuliwa na Ibn Abbas. Al-Khatib ameisimulia katika *Al-Muttafiq.* Na tafadhali rejea kwenye hadithi iliyosimuliwa na Ali katika *Musnad* za Ibn Mardawwyh na Abul-Shaykh. Kama ukipenda irejee katika *Kanz al-Ummal.*[196]

Mbali na hayo ya hapo juu wanachuoni wote wa tafsiri ya Qur'ani Tukufu wanakubaliana kwa pamoja kwamba aya hii ilishuka kuhusu Ali na wanachuoni wengi wa Sunni, wametaja umoja wake au makubaliano ya maoni katika vitabu vyao. Miongoni mwao Allamah al-Qawshaji ameitaja hii katika *Sharh al-Tajrid* alipokuwa akishughulika na suala la Uimam. Katika Sura ya 18 ya *Ghayat al-Maram* kuna riwaya ishirini na nne kutoka vyanzo vingine mbali na vile vya Ahlul-Bayt, zote zikiunga mkono maelezo yetu kuhusu kushuka kwa aya hiyo. Kama si uchache wa nafasi, na pia kwa sababu suala hili liko wazi kama jua la mchana, tungelinukuu kwa ajili yako hadith zote sahihi zinazothibitisha kushuka kwa aya hii kuhusu Ali (a.s.). Lakini, sifa njema zote ni kwa Allah, hili ni suala ambalo ukweli wake hakuna aliyeutilia shaka yoyote ama kuukanusha. Licha ya hivyo, hatupendekezi kuimalizia barua hii bila kunukuu baadhi ya hadithi kuhusu hili zilizosimuliwa kupitia vyanzo mbali na vile vya Ahlul-Bayt (a.s.).

---

[195] Hivyo katika matumizi ya watu wa Syria "*Mutawali,*" inamaanisha mtu Shi'ah kwa sababu anaamini katika Ubwana (Mawla) ama serikali ya Allah na Mtume Wake, na wale Walioamini, yaani, wale ambao kwao aya hii imeteremshwa. Mashi'ah pia wanajulikana kama "*Wahid ul-Mutawali*". Wanaitwa hivyo kwa sababu wanaamini kwamba Ali na Ahl al-Bayt (as) ndio Mabwana na Watawala wao.

[196] Hii ni hadithi Na. 5991 katika *Kanz al-Ummal* uk 391, Jz. 6, na pia kwenye pambizo ya *Muntakhab ul-Kanz*, uk. 38, Jz. 5, ya *Musnad Ahmad*.

Tutajitosheleza wenyewe na ile riwaya ambayo inajitokeza kwenye tafsiri ya Qur'ani ya Imamu Abu Is'haq Ahmad ibn Muhammad ibn Ibrahim al-Nisaburi al-Tha'labi.[197] Alipoifikia aya hii alisimulia katika *Al-Tafsir al-Kabir* riwaya ifuatayo kutoka kwa Abu Dharr al-Ghiffari ambaye anasema: "Masikio yangu yote yawe kiziwi na macho yangu yapofuke kama ninasema uwongo. Nimemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: 'Ali ni kiongozi wa wachamungu na muuaji wa makafiri; yeyote anayemsaidia atakuwa mshindi na yeyote anayemtelekeza naye atatelekezwa.' Siku moja niliswali nyuma ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) wakati muombaji alipokuja msikitini na akaomba apatiwe sadaka, lakini hakuna aliyempa kitu. Ali alikuwa katika hali ya kurukuu katika swala. Aliashiria pete iliyokuwa kwenye kidole chake kwa muombaji huyo ambaye alimsogelea na kuchukua pete ile kutoka kwenye kidole cha Ali. Hapo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimuomba Allah *Aza wa Jalah* akisema: 'Ewe Mola Wangu! Ndugu yangu Musa alikuomba akisema: 'Ewe Mola Wangu nikunjulie kifua changu, na unifanyie wepesi kazi yangu, na ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu (yaani ili apate kuongea bila ya hofu), wapate kufahamu maneno yangu. Na nipe waziri miongoni mwa watu wangu, Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu. Na umshirikishe katika kazi yangu ili tukusabihi sana na tukukumbuke sana Wewe (na neema zako nyingi) kwa wingi sana. Hakika wewe unatuona.' (**Qur'ani Tukufu 20:25-35**) Hapo ukampa wahyi ukasema: 'Hakika umepewa maombi yako, ewe Musa.' (**Qur'ani Tukufu 20:36**). Ewe Mola wangu! Mimi ni mja na Mtume Wako; kwa hiyo, niondolee uzito, ifanye kazi yangu kuwa nyepesi kwangu, na nipe waziri kutoka miongoni mwa watu wangu, Ali, na uimarishe mgongo wangu kwa yeye.' Abu Dharr anaendelea: Wallahi, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa bado hajamaliza maombi yake Jibrail, mwaminifu akatokea na kumletea aya hii:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ
رَاكِعُونَ وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ

**"Hakika *Walii* (mlezi) wenu ni Allah na Mtume wake na walioamini, ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa katika rukuu. Na atakayemtawalisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wale walioamini, basi kundi la Mwenyezi Mungu ndio watakaoshinda.** (Qur'ani Tukufu 5:55-56)**.**

Na wewe ambaye Allah amekujaalia kuwa na "hisia za uadilifu," unajua kwamba katika aya iliyoko kwenye mjadala, neno *'Walii'* limetumika kwa maana ya mlezi au mtu ambaye ana mamlaka ya juu kabisa kwa watu wengine, kama katika mfano huo hapo juu 'Walii' lina maana ya mtu anayesimamia mambo ya wa chini yake, na wataalamu wa kamusi wameliweka hilo wazi kwamba yeyote yule anayechukua uangalizi wa mambo ya mtu mwingine, basi huyo ni *Walii* wa mtu huyo. Kwa hiyo maana ya aya hiyo ni kwamba wale ambao wanasimamia mambo yenu ni wabora kwenu na kwa hakika hao ni: Allah, Aza wa Jala, Mjumbe Wake, na Ali ambaye ana sifa zote hizi zilizotajwa kwenye aya hii, nazo ni imani, kusimamisha Swala, na kutoa sadaka katika hali ya kurukuu katika Swala, na ambaye kwake aya hizi zimeteremshwa.

Katika aya hizi, Allah Aza wa Jala wakati huohuo amethibitisha kwamba Ulezi au mamlaka makubwa ambayo yamo mikononi Mwake Mwenyewe na Mtume Wake (s.a.w.w.) na Walii Wake yapo katika mpangilio huohuo tu basi. Ulezi au mamlaka ya juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni ya jumla kwa wote, yaani ya ulimwengu mzima. Hivyo ndivyo ilivyo kwa ulezi au mamlaka ya juu ya Mtume na halikadha-

[197] Amekufa mwaka wa 337 A.H. Ibn Khallikan ametoa maelezo juu ya kifo chake katika *Wafiyyat al-Ayan* akisema: "Alikuwa mshereheshaji wa kipekee na mfasiri wa Qur'ani, na *Al-Tafsir al-Kabir* yake ni bora kupita tafsir nyinginnezo…..," na anaendelea kusema: "Alitajwa na Abdul-Ghafir ibn Isma'il al-Farisi katika kitabu chake *Siyaq e-Nisaburi* na anasema alikuwa ni wa kutegemewa."

lika ya *Walii* wake; hubeba maana hiyo hiyo. Haiwezekani neno hili kulitumia katika muktadha huu kwa maana ya msaidizi na rafiki nk., kwa vile msaada na urafiki havifungiki kwa hawa watatu tu. Waumini wote wake kwa waume ni marafiki wa kila mmoja wao kwa mujibu wa Kitabu. Nina hakika kwamba ni dhahirii kabisa kama jambo lolote lile kwamba neno 'Walii' katika aya hii lina maana ya Bwana, Mlezi, Mtawala, Mwenye mamlaka makubwa, na shukurani zote ni kwa Allah, Mola wa walimwengu.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 41

## MUHARRAM 3, 1330 A.H.

**Wale Walioamini "Waumini - yaani Waislam" ni Katika Uwingi.**

**Inawezaje Kutumika kwa Ajili ya Mtu Mmoja?**

Katika majibu yako umerejelea kwenye: "Wale walioamin ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa katika rukuu." Sifa hizi zimetumika kwenye muundo wa uwingi. Nini majibu yako endapo utaulizwa; "Ni vipi litumike kwa Imamu (a.s.), Mwenyezi Mungu amjaalie hadhi, ambaye ni mtu mmoja tu?

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 42

## MUHARRAM 3, 1330 A.H.

**I. Waarabu Hutumia Muundo wa Uwingi Kuashiria Mtu Mmoja,**

**II. Mfano wa Kutumia Uwingi kwa Ajili ya Mtu Mmoja,**

**III. Maoni ya Imam Tabrasi,**

**IV. Maelezo ya Zamakhshari,**

**V. Mtazamo Wetu Sisi Wenyewe.**

Jibu kwa swali lako ni kwamba Waarabu wakati mwingine hutumia wingi kwa kumaanisha mtu mmoja. Kuna nukta ya maana nzuri ndani yake.[198]

Mfano wa jambo hilo unaonekana kwenye maneno ya Alla Aza wa Jala katika Surat Al-Imran:

**"Wale ambao waliambiwa na watu: Hakika watu wamewakusanyikia kwa hivyo waogopeni." (Imani yao juu ya Allah na Mtume Wake ikaongezeka nguvu), "wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha na bora ya mwenye kutegemewa ni Yeye."** (Qur'ani 3:173)

Wafasiri, wanahadithi na wanahistoria wote wanakubaliana kwamba alikuwa ni Na'im Ibn Mas'ud al-Ashja'i peke yake aliyewataka wawaogope maadui zao. Lakini Allah Aza wa Jala ambaye yuko mbali na kasoro ya aina yoyote ile amelitumia kwake, mtu mmoja kwamba yeye ni muundo wa wingi kwa kuonesha tu heshima kwa wale ambao hawakusikiliza maelezo yake wala kujali wito wake wa kuwashawishi. Abu Sufyani alikuwa amempa ngamia kumi ili awavunje moyo na kuwatisha Waislamu kuhusiana na nguvu za washirikina, naye alitekeleza maelekezo yake, na miongoni mwa mambo mengine yeye aliwaambia Waislam: "Waogopeni maadui zenu ambao wameungana dhidi yenu na wamejikusanya kwa idadi kubwa ili kukushambulieni ninyi." Matokeo yake Waislamu wengi walisita kutoka kwenda vitani. Lakini Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alitoka akiwa na kikosi cha wapanda farasi sabini, na wote walirudi wakiwa salama. Aya hii ilishushwa kuwasifia waumini hawa sabini ambao walitoka pamoja na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) bila kujali maelezo ya vitisho ya Na'iim al-Ashja'i. Katika kutumia neno la wengi "watu" kwa ajili tu ya mtu mmoja, kuna nukta moja nzuri sana. Ni sifa fasaha kabisa ya watu wale sabini ambao walitoka na Mtume. Kusema kwamba watu waliwatishia lakini wao wakapuuza vitisho, ni fasaha zaidi kuliko kusema 'mtu mmoja aliwaambia hakika watu wamejikusanya.'

Kama ilivyo dhahiri, kuna mifano mingi katika Qur'ani Tukufu ya kutumia wingi kwa ajili ya mtu mmoja, kwenye hadithi na katika vitabu vya fasihi ya lugha ya Kiarabu. Allah Aza wa Jala anasema: **"Enyi ambao mmeamini! Kumbukeni neema ya Allah juu yenu wakati baadhi ya watu walipokusudia kuweka mikono yao (miovu) juu yenu, na akawalinda dhidi ya madhara yao."** Kwa kweli alikuwa ni mtu mmoja tu aliyekusudia kuweka mikono yake miovu. Baadhi ya wanachuoni wanasema kwamba alikuwa ni mtu kutoka katika kabila la Muharib anayeitwa Ghawarath ambapo wengine wanasema alikuwa Umar ibn Jahash wa Banu al-Nasiir ambaye katika tukio fulani ambalo limeelezwa na wapokezi na wanahistoria na wafasiri, yeye alichomoa upanga wake na akataka kumshambulia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini Allah Aza wa Jala alizima jaribio lake. Ibn Hisham amelitaja suala hili katika maelezo

[198] Neno hili la umoja kutumika katika wingi pia hutumika sana kwenye luhga nyingi ikiwemo Kiswahili hususan katika kuonyesha heshima. (Mtarujuma)

yake juu ya vita vya *Dhat al Ruqa* katika Jz. 3 ya *Sirah* yake. Allah swt. ambaye ameepukana na mapungufu yote ametumia neno '*Qaum*' (kundi au umma) kwa mtu mmoja kwa ajili tu ya kuonesha ukubwa wa neema Zake, Nguvu na Utukufu juu ya Umma wa Kiislamu katika muundo wa usalama wa Mtume wao (s.a.w.w.). Katika Aya ya Mubahala tena, Alitumia maneno '*Abnaa*' (watoto), '*Nisaa*' (wanawake) na 'Anfus' (watu wenye haiba kama ya mtu mwenyewe) yametumika. Maneno haya ni nomino za kawaida za wingi zenye kutumika kwa jumla lakini Waislam wote wanakubaliana kwa pamoja kwamba maneno hayahaya yana utumikaji mahususi kwa maana ya Hasan na Husein, Fatima na Ali. Hili limefanyika kudokeza hadhi za hali ya juu tu walizokuwa nazo - Allah awe radhi nao. Kuna mifano mingi ya matumizi ya muundo wa wingi kwa ajili ya mtu mmoja. Mifano michache iliyotolewa hapo juu yote inathibitisha kwamba kuna ruhusa ya kutumia muundo wa wingi wakati wakizungumzia mtu mmoja iwapo haja ya maelezo ya hoja fasaha inalazimu.

Allamah al-Tabrasi katika kufafanua Aya hii, katika *Tafsir al-Majma'ul Bayan*, anasema: "Muundo wa wingi umetumika kwa Amirul-Mu'minina Ali (a.s.) ili kuonyesha utukufu na ubora wake. Mabingwa wa lugha ya Kiarabu wanatumia muundo wa wingi juu ya mmoja kwa namna ya heshima, na matumizi kama hayo ni mashuhuri katika lugha yao kiasi ya kutohitaji uthibitisho."

Katika kitabu chake *Tafsiir al-Kashaf,* al-Zamakhshari anataja nukta nyingine nzuri wakati anaposema: "Kama utaulizia ni vipi neno hili la wingi limetumika kwa Ali (a.s.) ambaye ni mtu mmoja, nitakuambieni kwamba ingawa aya hii imeshuka kwa ajili ya Ali ambaye ni mtu mmoja anatajwa katika muundo wa wingi tu, ili kwamba watu washawishike kufanya kama yeye na kutoa sadaka kwa utayari kabisa kama Ali (a.s.) alivyofanya. Pia kuna maagizo mengine yaliyohusishwa kwamba waumini wanapaswa kujiweka wenyewe wakati wote katika kutafuta nafasi za vitendo vya huruma, ukarimu, na sadaka kwa masikini na wenye dhiki na kuwa tayari kufanya yenye kuhitajika bila ya kusubiri hadi kukamilika kwa hata jambo muhimu la wajibu kama swala.

Mimi nimejiwa na hoja ya kupendeza na nzuri zaidi. Katika kutumia muundo wa wingi badala ya umoja, Mwenyezi Mungu aliye Mkuu, amekuwa na hisani kwa watu wengi, kwa sababu maadui wa Ali na waliowachukia na kuwatakia mabaya Banu Hashim, halikadhalika na wale wanafiki wote, wenye wivu juu yake na wabinafsi wasingeweza kuvumilia ile sifa iliyokusudiwa ya Ali lau ingetajwa katika muundo wa umoja, kwani kwa hali hiyo wangeweza kupoteza matumaini ya kuridhisha uchu wao wa kukamata madaraka ya kiulimwengu baada ya kifo cha Bwana Mtume (s.a.w.w.), wangeweza papo hapo kwa uwazi kabisa kujitoa kwenye Uislam ambao walilazimishwa na mazingira kujiunga nao, na kwa kila aina ya uwezekano hili lingethubutu kuwa ni balaa kwa waumini wa Uislamu (ambao walikuwa ni wachache wa kusikitisha). Aya hii kwa hiyo iliteremshwa katika muundo wa wingi badala ya umoja; ili kuwaokoa wanafiki kutokana na kuvunjika moyo kabisa, na waumini kutokana na matokeo ya kusikitisha. Baada ya hapo zilifuata Aya nyingi zenye matini tofauti na katika matukio kadhaa, na kulikuwa na ufafanuzi wa pole pole wa kanuni ya '*Wilayat*' (Mamlaka au Utawala uliofungika kwa Mwenyezi Mungu, Mtume Wake na Ali) mpaka (Siku ya Ghadir) Allah alipokamilisha dini Yake na kutimiza neema Yake juu ya waumini wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipomtangaza waziwazi Imam Ali (a.s.) kuwa Mwandamizi (mrithi) wake na kwamba ndiye mbora kwa watu wote. Katika hili, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), alifanya kama watu wenye hekima na busara wanavyofanya katika kuweka wazi kwa watu kwa njia ya pole pole na sio ghafla kile ambacho ni chenye kushtua kwao. Lau Aya ingekuja katika makusudio ya muundo wa umoja, wangeweka vidole vyao kwenye masikio yao, wangechana wenyewe majoho yao ya unafiki na wakawa na ghasia zenye shari kubwa kabisa. Na kama unavyojua hii ni hekima ya msingi wa hali ya juu wa zile Aya zote za Qur'ani Tukufu ambazo ziliteremshwa ili kuonesha sifa za Amirul-Mu'minina na watu wengine miongoni mwa Ahlul-Bayit watukufu. kama ambavyo iko wazi kabisa. Katika vitabu vyetu

*Sabil al-Muminin* na *Tanzil al-Ayat* tumezitaja aya kama hizo na kuelezea mazingira ya kushuka kwao. Na tumefafanua maelezo haya na kuleta ushahidi usiopingika na hoja za wazi katika kuthibitisha kwamba Aya hizo ziko katika kumtukuza Imam Ali (a.s.) na Ahlul-Bayt wengineo. Na shukurani zote anastahiki Allah kwa Mwongozo Wake na msaada, Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 43

## MUHARRAM 4, 1330 A.H.

**Mwelekeo na Muktadha wa Aya Unaashiria Neno 'Walii' au 'Mawla' lina Maana ya Msaidizi au Rafiki au Watu Kama Hao.**

Allah awe mpole juu yako! Hakika umeondoa shaka zangu na kufuta wasiwasi wangu, na kuwasilisha ukweli kwa namna dhahiri kabisa. Bali kuna jambo moja bado halijafafanuliwa. Wanasema kwamba Aya husika imeshuka katika mwelekeo wa kukataza kufanya urafiki na washirikina kama ilivyo wazi kwenye muktadha, yaani Aya zilizoitangulia na zinazoifuatia na hili linapendekeza akilini kwamba maana ya neno "*Walii*" katika Aya hii ni msaidizi au rafiki au watu kama hao; hivyo, jibu lako litakuwa nini? Tafadhali elezea. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 44

## MUHARRAM 4, 1330 A.H.

**I. Muktadha Hauthibitishi Kwamba Neno ‘Walii’ Katika Aya hii lina Maana ya “Msaidizi” au Mfano Wake,**

**II. Muktadha Peke yake Haubebi Uzito Dhidi ya Hoja Sahihi.**

Uchunguza makini wa aya hii unaashiria kwamba haina uhusiano na Aya ambazo zimetangulia zinazokataza kufanya urafiki na makafiri. Somo la aya hii ni tofauti kabisa. Iko katika kumsifia Amirul-Mu’uminina Ali (a.s.) kuhusu kuteuliwa kwake kwenye Uchifu (Uongozi) na Uimamu, ambapo wahaini wameonywa juu ya nguvu na ushujaa wake wa kushangaza aliokuwa nao. Hii ni kwa sababu Aya iliyo kabla yake ni:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ۚ ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ

**“Enyi mlioamini! Atakayeritadi dini yake miongoni mwenu, basi Mwenyezi Mungu atawaleta watu anaoawapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa waumini, wenye nguvu juu ya makafiri, wenye kufanya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anayelaumu. Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, mwenye kujua.” (Qur’ani 5:54)** ambayo ni makhsusia kwa Amirul-Mu’minina (a.s.) na ambayo inaingiza kwa makafiri na washirikina hali ya kuhofia nguvu zake na zile za maluteni wake,[199] kama Amiru’l-Mu’minina (a.s.), mwenyewe alivyoeleza katika Vita vya Ngamia na amelisema waziwazi hili Imamu Al-Baqir na as-Sadiq (amani iwe juu yao wote).

Maana hiyo hiyo inatumiwa na al-Tha’labi katika kitabu chake *Tafsir al-Qur’ani*. Vilevile inasimuliwa na mwandishi wa *Maj’maul Bayan fi Tafsir al-Qur’ani* kutoka kwa Ammar; Hudhayfah, na Ibn Abbas. Imetafsiriwa katika njia hii kwa mujibu wa makubaliano ya pamoja (*ijma*) ya Shi’a ambao wamepokea kwa kufuatana kutoka kwa Maimamu wa kizazi kilichotoharishwa (as). Hivyo Aya ya *wilayat* imekuja baada ya kudokezwa *wilayat* yake na kuonesha ulazima wa kukubali uimamu wake. Hivyo muktadha

[199] Hii ni sawa katika maana kwenye hadithi ya Mjumbe wa Allah (saw), isemayo: “Jamaa zenu Makureishi hawataacha kuwepo mpaka Allah amteue mtu juu yenu ambaye ameujaribu moyo wake kwa mitihani migumu ya imani. Yeye atakata shingo zenu kwa upanga wake, wakati ambapo ninyi mnakimbia kwa woga kama kondoo wenye hofu.” Abu Bakr akauliza: “Je, mtu huyo ni mimi Ewe Mjumbe wa Allah.?” Akajibu: “Hapana.” Umar akauliza: “Je, ni mimi Ewe Mjumbe wa Allah?” Akajibu: “Hapana; bali ni yule ambaye sasa hivi anashona viatu.” Aliyasema haya wakati huo Ali alikuwa na viatu mkononi mwake ambavyo alikuwa anavishona kwa ajili ya Mjumbe wa Allah (saw). Muhadithina wengi wameiandika hadithi hii na ni Hadithi ya 610 katika ukurasa wa 393, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*. Mfano mwingine sawa na huu ni hadithi yake, (saw), “Miongoni mwenu yuko yule ambaye atapigana na kuua kwa ajili ya tafsiri ya Qur’ani kama ambavyo mmekuwa mkipigana kwa ajili ya kuteremshwa kwake.” Abu Bakr akauliza: “Ni mimi Ewe Mjumbe wa Allah” akajibu: “Hapana.” Umar naye akauliza kama hivyo hivyo, na Mtume aksema: “Hapana, bali ni mtu ambaye yuko ndani akishona kiatu.” Ambapo wakati huo Ali akatoka ndani huku ameshika kiatu cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akiwa amemeliza kukishona. Hadithi hii imenukuliwa na Ahmad ibn Hanbal katika *Musnad* yake kama ilivyowasilishwa na Abu Sa’id, na imesimuliwa na al-Hakim katika kitabu chake *Al-Mustadrak*, Abu Ya’li katika *Musnad* yake, na waandishi wengi wa vitabu vya hadithi. Al-Muttaqi al-Hindi amenukuu kutoka kwao kwenye ukurasa wa 155 wa Jz. 6 ya *Kanzul- Ummal* yake.

wake utakuwa ni maelezo ya kidokezo hicho, na ufafanuzi juu ya kidokezo ambacho kimeitangulia ambacho kinadokeza serikali yake; hivyo, itawezekanaje kusemwa kwamba Aya hii iliteremshwa katika muktadha wa kukataza kuwafanya makafiri kuwa ni marafiki?

Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) yeye mwenyewe amelinganisha hadhi ya Maimamu miongoni mwa kizazi chake kama ile ya Qur'ani Tukufu, na akabashiri kwamba vyote viwili kamwe havitatengana na kuachana, na kwamba kwa vile Maimam kutoka kwenye kizazi chake wako sawa katika umuhimu na Kitabu (Qur'ani) chenyewe, ile maana kamili ya aya hiyo ya Qur'ani yaweza kubainishwa kutoka kwao na tafsiri yao ya Kitabu inaweza kutegemewa kabisa. Maimam wa Ahlul-Bayt mara nyingi wameichukua Aya hii kama uthibitisho wa haki ya Uimam wao na wameweka maana hiyo hiyo ya neno *"Walii"* kama tulivyoeleza. Hata kama tukiuchukulia muktadha huo kuwa ni sahihi unapoteza umhimu wake pale unapokuwa hauendani na hoja sahihi ambazo ni nususi zao. Waislamu wote kwa pamoja wanakubaliana kwamba hoja sahihi ndio zinazofaa kuzingatiwa zaidi kuliko muktadha, na wakati wowote kama maana ya muktadha inapingana na maana ya hoja, huacha maana ya muktadha na kusalim amri kwenye hoja. Na siri katika hilo ni kwa sababu wana shaka juu ya aya kuteremka kwa ajili ya muktadha huo uliojitokeza.

Umma wote wa Kiislam unakubaliana kwamba wakati aya za Qur'ani zilipokusanywa ndani ya Kitabu Kitukufu chenyewe hazikupangwa katika mfuatano wa kuteremshwa kwao. Kwa hali hiyo, kuna Aya nyingi ambazo hutokeza katika muktadha usio wake. Chukua kwa mfano, Aya ya Tohara ambayo inatokeza katika maelezo ya wake za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) lakini kwa kweli ipo kwa ajili ya sifa ya watu watano ambao walifunikwa shuka (*Ahlul-Kisaa*) kama ilivyothibitishwa na mantiki na kukubalika kwa wote. Kwa kifupi, kuitafsiri Aya ya "**Hakika *Walii* wenu ni Allah na Mtume wake na walioamini, ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa katika rukuu."** katika njia ambayo inapinga muktadha wake uliopendekezwa hakuwi kinyume na mwelekeo wa kimuujiza wa Qur'ani Tukufu, wala hakuna madhara juu ya ufasaha wake, na kuwepo kwa hoja zake zenye kusadikisha hakuachi nafasi nyingine bali kuelewa kwamba neno 'Walii' katika aya hii lina maana ya bwana, mlezi, mtawala, mtu wa mamlaka ya juu na kadhalika, na wala sio msaidizi, rafiki na mengine kama hayo. Wassalaamu.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 45

## MUHARRAM 6, 1330 A.H.

### I. Ni Lazima Kutafsiri Aya Kinyume chake kwa Ajili ya Kulinda Heshima na Hadhi ya Wahenga Wetu.

Tafsiri yako ya aya ya "**Hakika *Walii* wenu ni Allah na Mtume wake na walioamini, ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa katika rukuu."** inavunja kabisa urithi wa makhalifa ambao ni Makhalifa wema. Lau isingekuwa hivyo, tusingekuwa na chaguo lolote bali kukubali mtazamo wako na kusalimu amri kwenye hukumu yako kuhusiana na kushuka Aya hii na maana hiyo. Lakini tafsir yako inatufanya tutilie shaka ukhalifa wao sahihi, Allah awawie radhi. Hivyo, ni muhimu kushikamana na tafsiri ambayo inalinda hadhi na heshima yao kama makhalifa wa haki, na halikadhalika hadhi na heshima ya wale ambao waliwakubali wao kama mabwana zao. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 46

## MUHARRAM 6, 1330 A.H.

**I. Sio Lazima Kutafsiri Aya Kinyume chake kwa Ajili tu ya Kulinda Heshima na Hadhi ya Wahenga,**

**II. Tafsir ya Kinyume Haiwezekani.**

Unapenda sana kulinda haki ya urithi wa wale Makhalifa watatu, Allah awe radhi nao. Lakini hii ndio maudhui ya mjadala na mada yenye utata. Si lolote bali ni kichekesho kuhalalisha msimamo wao na kuleta urithi wao kama hoja pinzani licha ya kuwepo hoja nzito dhidi yao.

Zaidi ya hayo, hakuna umuhimu wa kuitafsiri aya hiyo kwa njia tofauti ili kuunga mkono msimamo wao na msimamo wa wale waliowakubali hao kama mabwana zao. Njia mbadala ilikuwa ni kuwaacha badala ya kutoa au kukubali tafsiri potovu ya aya hiyo. Tutatoa ufafanuzi juu ya suala hili kama itakuwa lazima.

Kimsingi huwezi kutafsir kwa njia tofauti zile riwaya ambazo tumezitaja, ni muhali; na vivyo hivyo zile ambazo hatukuzitaja mpaka hapa, kama vile Hadithi ya "*Ghadir*" au ile hadithi ya Wosia, hususan wakati kunapokuwa na hadithi nyingi mno zenye muelekeo mmoja ambazo kila moja huunga mkono nyingine zinazowasilisha maana moja, hasa kama hadithi ni za wazi kabisa. Kama utaziangalia riwaya hizi zenye muelekeo mmoja bila upendeleo, utazikuta zenyewe ni hoja mkataa na ushahidi unaong'ara wa ukweli wa mambo. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 47

## MUHARRAM 7, 1330 A.H.

**Kuomba Hadithi Zenye Uthibitisho.**

Ingekuwa bora kama ungetufahamisha zile hadithi zinazounga mkono, kuthibitisha ambalo umedokeza. Tafadhalli tujulishe sasa. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA 48

## MUHARRAM 8, 1330 A.H.

**Riwaya Arobaini Zinazounga Mkono Ukweli wa Wazi wa Hadithi.**

Tunazikariri hapa riwaya arobaini tu zinazounga mkono hadithi za wazi kwa dhahiri kabisa na tunatarajia kwamba hizi zitatosheleza katika kukuondoa shaka juu ya imani yetu:

1. Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.), wakati akiwa ameweka mkono wake kwenye shingo ya Ali alisema: "Huyu ni kiongozi wa wachamungu, mfyekaji wa waovu, mwenye kushinda ni yeyote yule anayemsaidia, na yeyote yule mwenye kumtelekeza naye pia atatelekezwa." Yeye (s.a.w.w.) alipaza sauti yake wakati alipokuwa anayasema haya. Hakim ameipokea hii kama ilivyosimuliwa na Jabir katika ukurasa wa 129, Jz. 3, ya Al-Mustadrak,[200] na anasema: "Hadithi hii ni sahihi, lakini masheikh wawili Bukhari na Muslim hawakuiandika."

2. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mambo matatu yamefunuliwa kwangu kuhusu Ali, nayo ni: kwamba ni bwana wa Waislamu, kiongozi wa wachamungu na Imamu wa wale wasimamishao swala ambao wana vipaji vya nyuso vinavyong'ara." Hakim amesimulia hadithi hii mwanzoni mwa ukurasa wa 138, wa Jz. 3, katika Mustdrak [201] na akaongeza: "Hii ni hadith moja ambayo usahihi wake unathibitishwa na nyororo (sinad) yake yenyewe ya wasimuliaji, ingawa waandishi wote (wa vitabu vya sahih) hawakuiandika."

3. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Imefunuliwa kwangu kuhusu Ali kwamba ni bwana wa Waislamu, na rafiki wa wachamungu na kiongozi wa wale ambao wanasimamisha swala ambao paji zao za uso zinang'ara." Imeandikwa na Ibn al-Najjar,[202] na waandishi wengine wa hadithi.

4. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Ali (a.s.): "Karibu ewe bwana wa Waislamu, kiongozi wa wachamungu." Ameiandika Abu Na'im katika Hilyat al-Awliya." [203]

5. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mtu wa kwanza kuingia kupitia mlango huu ndiye kiongozi wa wachamungu, bwana wa Waislamu, mlinzi wa dini, wa mwisho wa mawasii na Imam wa wale wasimamishao swala ambao wana mapaji ya nyuso yanayong'ara." Halafu akaingia Ali (a.s.) katika mlango huo na yeye (s.a.w.w.) akasimama na kwa furaha sana akamkumbatia na kumfuta jasho la kwenye paji lake la uso huku akisema: "Wewe utakuja kulipa madeni yangu, kufikisha ujumbe wangu, na baada yangu utawaonyesha watu njia iliyonyooka utakapotokea mfarakano miongoni mwao." [204]

[200] Hii ni hadihi Na. 2527 katika *Kanz al-Ummal*, Jz. 6 uk. 153, na al-Tha'labi ameipokea kama ilivyosimuliwa na Abu Dharr wakati wa kutafsiri aya ya 'Mamlaka Makubwa' katika *Al-Tafsir al-Kabiir.*

[201] Vilevile imenukuliwa na al-Baarudi, Ibn Qani, Abu Na'im, na al-Bazzaz. Ni hadithi Na. 2628 katika *Kanz al-Ummal*, ukurasa wa 157, Jz. 6.

[202] Ni hadithi Na. 2630 katika *Kanz al-Ummal* ,ukurasa wa 157, Jz. 6.

[203] Hii ni hadithi Na. 11 kati ya zilizosimuliwa na Ibn Abul Hadid kwenye ukurasa wa 450, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul Balaghah,* na ni hadithi Na. 2627, katika *Kanz al-Ummal,* ukurasa wa 157, Jz. 6.

[204] Hadithi hii imenukuliwa na Abu Na'iim katika *Hilyat al-Awliya*, kutoka kwa Anas, na Ibn Abul Hadid ameinakili kwa kinaganaga katika

6. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Allah amenijulisha Ali kwamba yeye ndiye bendera ya mwongozo, kiongozi (Imamu) wa wafuasi wangu na nuru kwa wale wanaonitii na yeye ndio neno ambalo nimeliamuru juu ya wachamungu."[205]

Je huoni jinsi hadithi hizi sita zinavyoweka sharti la Uimamu wake na kukazia wajibu wa kumtii yeye (a.s.).

7. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimnyooshea mkono Ali huku akisema: "Huyu Ali ni wa kwanza kuamini Utume wangu, na atakuwa wa kwanza kupeana mikono na mimi Siku ya Hukumu, yeye ndiye mtu mkweli kabisa, na muamuzi (faruq) mwenye hekima sana katika umma huu. Atatofautisha kati ya haki na batili, na ndiye mtawala wa waumini."[206]

8. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:

"Enyi kundi la Ansar! Ngojeni nikuongozeni kwenye lile ambalo kama mnashikamana nalo, kamwe hamtapotea. Huyu ni Ali, mpendeni kama mnavyonipenda mimi, na mheshimuni kama mnavyonihshemu mimi, kwani haya ninayosema ni amri ya Allah Aza wa Ajala ambayo Jibrail amenifikishia." [207]

9. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.):

"Mimi ni jiji la ilmu, na Ali ni lango lake, yeyote anayetaka kupata ilmu, na aiendee kupitia mlango huo."[208]

10. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:

"Mimi ni nyumba ya hifadhi ya hikma na Ali ni mlango wake."[209]

11. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.):

"Ali ni lango la ilmu yangu, ambaye ataelezea kwa umma wangu baada yangu kile ambacho nimetumwa nacho; kumpenda yeye ni alama ya imani ya kweli, na kumchukia yeye ni unafiki." [210]

12. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.) kwa Ali:

---

uk. 450 wa Jz. 2, ya kitabu chake *Sharh Nahjul Balagha;* tafadhali rejea riwaya Na. 9 katika ukurasa huo.

[205] Abu Na'im ameiandika katika kitabu chake *Hilyat al-Awliya*, kama ilivyosimuliwa na Abu Barzat Al-Aslami na Anas ibn Malik, na Allamah Mu'tazili ameinakili katika uk. 449, wa Juz. 2, ya kitabu chake *Sharh Nahjul Balaghah*; tafadhali rejea riwaya Na. 3 katika ukurasa huo.

[206] Hii imenukuliwa na Tabrani katika kitabu chake *Kabiir*, kutoka kwenye hadithi iliyosimuliwa na Salman na Abu Dharr. Imenukuliwa na al-Bayhaqi katika *Sunan* yake, na Ibn Adiy katika *Al-Kamil* kutoka kwa Hudhaifa na ni hadithi Na. 2608 katika *Kanz al-Ummal*, Jz. 6, uk. 156.

[207] Hii imenukuliwa na Tabrani katika kitabu chake *Kabir*, na ni hadithi Na. 2625, katika Kanz al-Ummal, J. 6, uk. 157, nayo ni ya kumi katika ukurasa 450, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul Balaghah* cha Ibn Abul Hadid; hivyo tazama na uone jinsi walivyofanya mwongozo wao sahihi wa kimasharti juu ya kumfuata Ali; hivyo, wale ambao hawafanyi hivyo kwa hakika watapotea. Tazama jinsi alivyowaamrisha kumpenda yeye kama wanavyompenda Mtume (saw). Hii ni kwa sababu tu ya yeye kuwa mrithi, mtu atakayechukua mamlaka baada yake.

[208] Hii imenukuliwa na Tabrani katika kitabu chake *Kabir*, kutoka kwa Ibn Abbas kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 107 wa *Al-Jami al-Saghir* cha Suyuti. al-Hakim katika mlango wa Manaqib Ali, katika uk. 226, Jz. 3 ya Sahih yake *Mustadrak*, kutoka kwa wapokezi wawili mashuhuri, mmojawapo akiwa ni Ibn Abbas ambaye riwaya yake imesimuliwa kwa njia mbili tofauti za kuaminika, na mwingine ni Jabir ibn Abdullah al-Ansari. Imamu Ahmad ibn Muhammad ibn al-Siddiq al-Magharibi, wa Cairo ameandika kitabu kizima kwa ajili tu ya kuthibitisha usahihi wa hadithi hii na akakiita *Fath al-Malak al-Ali Bisihihati Hadith Babul Ibn Ali* kilichochapishwa Misr na Islamic Press.

[209] Hii imenukuliwa na al-Tirmidhi katika *Sahih* yake, kwa nyongeza ya Ibn Jarrir, na kutoka kwao imenukuliwa na waandishi mbalimbali kama vile al-Muttaqi al-Hindi katika ukurasa wa 401, Jz. 6, ya kitabu chake *Kanz al-Ummal*, ambako anamnukuu Ibn Jarrir akisema: "Hii ni hadithi ambayo sanadi yake ni sahihi na hakika kabisa." Vilevile Jalalud-Din al-Suyut ameinukuu kutoka kwa al-Tirmidhi wakati alipokuwa anajadili "*hamza*" katika lugha kwenye kitabu chake *Jami al-Jawami* na *Al-Jami al-Saghir*, hivyo, rejea kwenye ukurasa wa 170, Jz. 1, ya *Al-Jami al-Saghir*

[210] Huu imenukuliwa na al-Daylami kutoka hadithi ya Abu Dharr kama ilivyodondolewa katika ukuras wa 156, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*.

"Utafafanua kwa umma wangu mambo yote yale ambayo wanahitilafiana kwayo." Hii imeandikwa na al-Hakim katika ukurasa wa 122, Jz. 3, wa kitabu chake *Mustadrak,*[211] kama ilivyoripotiwa na Anas. Kisha mwandishi akafafanua: "Hii ni hadithi sahihi kwa mujibu wa vigezo vya masheikh wote wawili [Bukhari na Muslim], ingawa wenyewe hawakuinukuu." Kwa kweli yeyote yule atakayeichunguza hadithi hii na nyingine zilizo sawa na hii atakuja tambua kwamba hadhi na heshima ya Ali kwa Mjumbe wa Allah ni sawa na ile ya Mjumbe wa Allah kwa Aza wa Jala Mwenyewe, kwani Allah anamuambia Mjumbe Wake: "Tumekuteremshia wewe ufunuo Wetu ili tu kwamba uweze kufafanua kwa ajili yao mambo yote ambayo kwayo wanahitilafiana, na kama mwongozo na rehema kwa wale ambao wanaamini." Ambapo katika hadithi hii Mjumbe wa Allah anamwambia Ali: "Utafafanua kwa umma wangu mambo yote ambayo kwayo wanahitilafiana baada yangu."

13. Ibn al-Sammak amesimulia hadithi ifuatayo kama ilivyosimuliwa na Abu Bakr, ambaye alimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe akisema: "Hadhi ya Ali kwangu ni kama ile ya kwangu kwa Mola wangu." [212]

14. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.) kama ilivyoandikwa na al-Dar Qutni katika Al-Afrad ambamo anamnukuu Ibn Abbas akionesha simulizi ya Mtume (s.a.w.w.): "Ali Ibn Abi Talib ni mlango wa toba, yeyote yule anayeuingia huo ni muumini wa kweli, na yeyote anayetoka nje yake huwa kafiri."[213]

15. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.), katika siku ya Arafat wakati wa Hijjatul Wada (Hija ya Mwago): "Ali anatokana na mimi, na mimi natokana na Ali, na hakuna awezaye kutekeleza wajibu wangu isipokuwa mimi mwenyewe au Ali." [214] Hakika hiyo bila shaka ni kauli ya mjumbe mtukufu, Mwenye nguvu, mwenye cheo mbele ya Mwenye Arshi, Mwenye kutiiwa huko mwaminifu. Na mwenzenu si mwendawazimu.

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

**"Wala hatamki kwa matamanio. Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa."** (Qur'ani 53:3-4).

Sasa ni wapi mnakwenda? Na ni kipi mtakachosema kuhusu hizi hadithi sahihi na hoja zilizo wazi?

[211] Ameitoa tena Daylami kutoka kwa Anas kama ilivyo katika uk. 156 wa Jz. 6 ya *Kanz al-Ummal*.

[212] Hii imenukuliwa na Ibn Hajar katika Maqsad ya 5 katika maqsad ya aya ya 14, moja kati ya zilizojadiliwa katika ukurasa wa 11 wa kitabu chake *Al-Sawa'iq al-Muhriqa;* hivyo rejea ukurasa wa 106 wa kitabu hicho.

[213] Hii ni hadithi Na. 2528 miongoni mwa zilizo dondolewa katika *Kanz al-Ummal*, ukurasa wa 153, J. 6.

[214] Hii imenukuliwa na Ibn Majah katika mlango wa 'Fadhaili za masahaba wa Mtume' ukurasa wa 92, Jz. 1, ya *Sunan* yake, Tirmidhi na an-Nasai katika *Sahih* zao husika, na ni hadithi Na 2531 katika *Kanz al-Ummal*, ukurasa wa 153, Jz. 6. Vilevile imenukuliwa na Imamu Ahmad katika ukurasa wa 154, Jz. 4, ya *Musnad* yake kutoka hadithi iliyosimuliwa kutoka vyanzo mbali mbali sahihi na Habash Janadah. Na ukutosheleze ukweli kwamba imenukuliwa kutoka nyororo za wasimuliaji ambao ni pamoja na: Yahya ibn Adam kutoka kwa Isra'il ibn Yunus na babu yake Abu Is'haq al-Subay'i ambaye anamnukuu Habashi. Wote hawa ni waandishi wanaotegemewa na kuaminiwa na Masheikh wote wawili (Bukhari na Muslim) katika *Sahih* zao husika. Na atakayerejea kwenye hadithi hii ndani ya Musnad Ahmad atakuja kujua kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitamka hadith hii kwenye Hijja yake ya mwisho ambapo baada ya hapo aliishi muda mfupi tu hapa duniani. Kabla ya hili, yeye alimtuma Abu Bakr na aya kumi za Surat Tawba (9) kwenda kuwasomea watu wa Makka. Halafu akamwita Imam Ali (a.s.), na kama ilivyosimuliwa na Ahmad katika Jz. 1, uk. 151 wa Musnad yake: "Nenda ukamuwahi Abu Bakr, uchukue mswada alionao mara tu utakapomkuta na uende kwa watu wa Makka ukawasomee aya hizo." Ali (a.s.) alimkuta Abu Bakr mahali panapoitwa Juhfah na akayachukua mswada huo kutoka kwake, Imam Ahmad anasema: "Abu Bakr alirudi kwa Mtume (s.a.w.w.) na akamuuliza iwapo kama kuna aya yoyote iliyoshuka kwa ajili yake. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamjibu: Hapana. Bali malaika Jibril amenijia na kuniambia: 'Ama utekeleze kazi yako mwenyewe au ikabidhi kwa utekelezaji wake kwa mtu atokanaye na wewe.'" Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ali ambayo Ahmad Hanbal ameinakili uk. 150 wa Juz. 1 ya Musnad yake wakati iliposhuka Surat Tawba, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimwambia Ali (a.s.): Ama ni mimi mwenyewe au wewe ambaye ni lazima aende na aya hizi, na Ali akasema: "Kama ni hivyo basi mimi nitakwenda." Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: Basi ondoka na Mwenyezi Mungu atathibitisha matamshi yako na kuuongoza moyo wako.

Kama utatafakari kiasi hiki, ukachunguza sababu ya hikma ya kufanya matamshi kama hayo wakati wa Hijja ya Kuaga pale Arafah mbele ya mkusanyiko mkubwa wa mashahidi, ukweli utajitokeza kwako kwa utukufu wake kabisa. Na ukichunguza maneno ya hadith jinsi yalivyo machache, na jinsi maana yake ilivyopana na isiyo na utata, na masharti magumu aliyoyaweka Mtume (s.a.w.w.) kupitia maelezo haya yenye mkazo, basi utatambua kwamba hadith hii haimhusu mwingine isipokuwa Ali na kwamba yeye ndiye mwenye kufaa kushiriki na Mtukufu Mtume katika kutekeleza wajibu wake. Hivyo sio ajabu kwamba yule mtekelezaji wa wosia wa Mtume anaweza pia kutekeleza kazi ya Mtume (s.a.w.w.) na hakuna mwingine yeyote anayeweza kuchukua cheo hicho kikubwa cha Imam na kiongozi wa kweli wa Umma huu isipokuwa makamu na mwandamizi wake wa haki, shukurani ziwe kwa Allah Ambaye ametuongoza kwenye yote haya, kwani bila mwongozo wa Allah tusingeweza kuongozwa hivi.

16. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Yeyote yule ambaye ananitii mimi anamtii Allah, na yeyote yule ambaye ananiasi mimi anamuasi Allah; na yeyote yule anayemtii Ali ananitii mimi, na yeyote yule anayemuasi Ali ananiasi na mimi vilevile." Hii imeandikwa na al-Hakim katika ukurasa wa 121, Jz. 3, ya kitabu chake cha Mustadrak, na al-Dhahabi katika kitabu chake cha Talkhiis al-Mustadrak na wote wameelezea hadithi hii kuwa ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya Masheikh wawili (yaani, Bukhari na Muslim).

17. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Ewe Ali! Yeyote yule anayejitenga na mimi anajitenga na Allah; na yeyote anayejitenga na wewe anajitenga na mimi pia." Hii imeandikwa na al-Hakim kwenye ukurasa wa 124, Jz. 3, ya Sahih yake, ambako anafafanua kwa kusema: Hadith hii ni sahihi kupitia vyanzo sahihi, ingawa Masheikh wawili (Bukhari na Muslim) hawakuiandika."

18. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.), kama ilivyosimuliwa na Umm Salamah, amesema: "Yeyote yule mwenye kumlaani Ali ananilaani na mimi vilevile." Imeandikwa na al-Hakim ndani ya al-Mustadrak Jz. 3 uk. 121 ambaye amekiri usahihi wake kwa vipimo vya Masheikh wote wawili, Bukhari na Muslim na imesimuliwa na Dhahabi katika kitabu chake cha Talkhis na amethibitisha usahihi wake. Imeandikwa na Ahmad miongoni mwa hadithi zilizosimuliwa na Umm Salmah katika ukurasa wa 323, Jz. 5, ya Musnad yake, na an-Nisa'i uk. 17 wa Al-Khasa'is al-Alawiyya, na wasimuliaji wengine pia wameipokea. Na riwaya nyingine kama hiyo ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kama ilivyosimuliwa na Amr ibn Shash inaeleza hivi: "Yeyote yule anayemsababishia Ali huzuni, ananisababishia huzuni mimi vilevile."[215]

19. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Yeyote yule anayempenda Ali, basi ananipenda na mimi pia, na anayemchukia Ali basi amenichukia na mimi pia." al-Hakim imeisimulia Hadithi hii katika ukurasa wa 130, Jz. 3, ya Al-Mustadrak, na ambaye anakiri kwamba ni hadithi sahihi kwa vigezo vilivyowekwa na masheikh wawili, na imesimuliwa na al-Dhahabi katika kitabu chake Takhiis ambamo anakiri usahihi wake kwa vigezo hivyo hivyo. Kuna riwaya nyingine kama hiyo, ya Ali, ambaye amesema: "Naapa kwa Yule Ambaye ameuchipua mche kutoka kwenye mbegu na akaumba roho, Mtume Ummiy (s.a.w.w.) ameniahidi mimi kwamba hakuna mtu yeyote anipendae mimi isipokuwa muumini wa kweli, na hakuna mtu yeyote anichukiaye mimi isipokuwa munafiki." [216]

[215] Hadithi hii imetajwa katika Barua ya 36.

[216] Kama ilivyosimuliwa na Muslim katika *Sahih* yake Sura juu ya *Imamat* ukurasa wa 46, J. 1, Ibn Abd al-Birr anaelezea maana yake wakati ambapo anasimulia wasifu wa Ali katika Isti'ab kutoka kwenye kundi la masahaba. Hadithi ya Buraydah imenukuliwa katika Barua ya 36. Hadithi yake Mutume (saw): "Ee Allah! kuwa rafiki kwa yeyote yule mwenye urafiki na Ali, na kuwa adui wa yeyote yule mwenye uadui na Ali" imewasilishwa kwa mfululizo (*mutawatir*), kama ilivyokubaliwa na mwandishi Al-Fatawa al-Hamidiyya katika tasnifu yenye anwani "*Al-Salat al-Fakhira fi Ahadith al-Mutawatira."*

20. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Ewe Ali! Wewe ni kiongozi katika dunia hii na ile ya kesho Akhera; yeyote yule ambaye akupendae wewe hunipenda na mimi pia, na yeyote anipandae mimi anapendwa na Allah; adui yako ni adui yangu, na adui yangu ni adui wa Allah; ole wake yule anayekuchukia wewe baada yangu." Hii imeandikwa na al-Hakim mwanzoni mwa ukurasa wa 128, wa "Mustdrak" na amekiri kwamba usahihi wake umethitishwa na Masheikh wawili. [217]

21. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Ewe Ali! Habari njema kwa yule ambaye anakupenda na mwenye kuthibitisha maneno yako wewe, na ole wake yule ambaye anakuchukia wewe na kukukanusha wewe." Hii imeandikwa na al-Hakim katika ukurasa wa 135, Jz. 3, ya kitabu chake "Al-Mustadrak" ambamo anaongeza kwamba Hadithi hii ni sahihi na kwamba lakini Masheikh wote wawili hawakuisimulia."

22. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Yeyote yule ambaye anataka kuishi kama nilivyoishi na kufa katika njia ambayo nitafia na kukaa katika Bustani ya Milele (Peponi), ambayo imeahidiwa kwangu na Mola wangu, naamkubali Ali kama walii wake, kwani kwa hakika yeye kamwe hatakubali watu wapotee kutoka kwenye mwongozo, na kuangukia kwenye upotofu."[218]

23. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Namuamrisha yeyote yule ambaye ananiamini mimi na kunisadikisha kuwa makini na mamlaka ya Ali ibn Abi Talib, kwani yeyote yule ambaye anamkubali kama walii wake amenikubali mimi kama hivyo, na yeyote yule anayenikubali mimi kama walii wake hakika amemkubali Allah kama hivyo; na yeyote ampendaye yeye amenipenda mimi na anampenda Allah; na yeyote yule anayemchukia (Ali) ananichukia mimi pia, na yeyote anayenichukia mimi anamchukia Allah Aza wa Jala."[219]

24. Kwa kauli yake hii (s.a.w.w.): "Yeyote yule ambaye anaridhia kuishi maisha kama yangu na kufa kifo kama changu na kisha aje kuishi katika Bustani ya Eden iliyowekwa na Mola Wangu, basi naamfanye Ali kama walii wake baada yangu na akubali mamlaka ya yeyote yule ambaye amewekwa na Ali, na

---

[217] Hakim ameipokea kama ilivyosimuliwa na al-Azhar, na Abdul Razzaq kutoka kwa Mu'mmar, al-Zuhri, kutoka kwa Ubaydullah kutoka kwa Ibn Abas, wote walikuwa waandishi waaminifu. Kwa sababu hii al-Hakim, ameiita hadithi hii kuwa ni "sahih" kwa viwango vya masheikh wawili (Bukhari na Muslim), Abdul Azhar kwa mujibu wa mtazamo wa *ijma* ya Sunni ni mwaminifu, na kama mwandishi mwaminifu mmoja pekee anaposimulia riwaya, huwa inachukuliwa kama hadithi sahihi na Masheikh hao wawili. Kisha akaendelea kusema: "Nimemsikia Abu Abdullah al-Qarashi akisema kwamba amemsikia Ahmad ibn Yahya al-Halwani kwamba wakati Abul-Azhar alipokuja kutoka San'aa na akaisimulia hadithi hii kwa watu mjini Baghdad, Yahya ibn Mu'in aliikataa. Wakati wa kufungwa kikao fulani cha wapokezi wa hadith ambacho yeye alikuwa mwendeshaji wake, aliuliza kuhusu muongo wa Nishapur ambaye alisimulia hadithi hii alimnukuu Abdul Razaq, Abu al-Azhar alisimama na kusema ni yeye. Yahya ibn Ma'in alicheka kauli yake hiyo, alisimama na kumleta akae karibu naye na akamuuliza: Kwa vipi Abdul Razaq alikusimulia hadithi ambayo hajamsimulia mtu mwingine yoyote? Abul Azhar akasema: 'Ewe Abu Zakarriya (yaani Yahya ibn Mu'iin), tafadhali tambua kwamba punde tu nilipowasili San'a na kugundua kwamba Abdul Razzaq alikuwa yuko kwenye kijiji cha mbali, mimi nilielekea huko kwenda kumuona licha ya hali yangu ya maradhi. Nilipofika kwake aliniuliza kuhusu hali ya ya mambo ya Khurasani ambayo nilimjulisha. Kisha niliandika hadith alizozisimulia na nikarudi naye hadi San'aa. Wakati nilipokuwa namuaga, aliniambia kwamba anawiwa na mimi hadithi ya pekee ambayo hakuna mtu yeyote ambaye amewahi kuisikia kutoka kwake, na Wallahi alinisimulia hadithi hii kwa maneno haya haya.' Yahya ibn Mu'in aliithibitisha kauli ya Abul Azhar na akamuomba radhi kwa kumwita kwake muongo. Lakini Dhahabi, licha ya kukiri mategemeo ya vyanzo vyote vya hadith hii kwa jumla, na Abul Azhar haswa katika *Talkhiis* yake bado anatilia shaka riwaya hiyo ingawa hakuweza kuonyesha kasoro yoyote ya dhahiri juu yake. Hii ni kwa sababu ya chuki yake mbaya isiyo na aibu. Na kuhusu kwa nini Abdul Razzaq aliificha hadith hii kwa wengine ni kwa sababu ya kuwahofia wale madhalim ambao walikuwa na chuki dhidi ya Ahlul-Bayt (a.s.). Sa'iid ibn Jubair alikuwa na hofu kama hiyo wakati Malik ibn Diinar alipomuuliza: "Nani alikuwa mshika bendera wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?" Sa'iid alimtazama na akamwambia: "Wewe ni fedhuli na mzembe kabisa." Hili lilimuudhi sana Malik kiasi kwamba alilalamikia jambo hili washirika wa Sa'iid ambao walimuomba radhi kwa niaba yake na wakamwambia kwamba Sa'iid alikuwa akimuogopa Hajjaj na kwamba kwa mujibu wa Sa'iid mshika bendera huyo alikuwa ni Ali ibn Abi Talib (a.s.). Al-Hakim ameiandika hii katika Jz. 3, uk. 137 wa *Mustadrak* yake na akaongeza kwamba vyanzo vyake vyote ni vya kutegemewa lakini masheikh wawili hawakuiandika. – Hadithi hii imenukuliwa katika barua yetu ya 10.

[218] Tumeinukuu hadithi hii katika Barua yetu ya 10.

[219] Ibid,

afuate mfano wa kizazi changu baada yangu, kwani wao ni watoto wangu wameumbwa kutokana na udongo wangu (nilioumbiwa) na kubarikiwa na ujuzi wangu, kwa hiyo, ole wao wale katika umma wangu ambao wanakataa fadhaili zao, ambao wanakata mafungamano yao na wao; Allah kamwe asiwaruzuku uombezi (shufaa) wangu."

25. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Yeyote yule anayetaka kuishi maisha yangu na kufa kifo changu na kuingia katika Pepo ambayo Mola wangu ameniahidi, Pepo ya Milele, basi naamfanye Ali kuwa walii wake na kizazi chake baada yake, kwani wao hawatakutoeni nje ya mwongozo, wala kamwe hawatakutupeni kwenye upotofu."[220]

26. Mwanzoni mwa ukurasa wa 156, Jz. 6, ya Kanz al-Ummal, al-Daylami anamnukuu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akimwambia Ammar yafuatayo: "Ewe Ammar! Kama ukimuona Ali anatembea kwenye njia moja ambapo watu wengine wanatembea kwenye njia nyingine, tembea na Ali na waache watu hao wengine, kwani hatakuelekeza kwenye kuangamia, wala kamwe hatakutoa nje ya mwongozo."[221]

27. Kwa mujibu wa hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliyosimuliwa na Abu Bakr inasema hivi: "Mkono wangu na wa Ali ni sawasawa wakati tunapotekeleza uadilifu." Hii imenukuliwa na al-Hakim kwenye ukurasa 129, Jz. 3, ya Sahih al-Mustadrak, na imesimuliwa na waandishi wengine wa hadithi, wote wakithibitisha juu ya usahihi wake.[222]

28. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): Ewe Fatimah! Je, huridhii kwamba Allah wa Pekee Aza wa Jala ameangalia katika wakazi wa ardhini na akachagua miongoni mwao wanaume wawili mmoja wao ni baba yako na mwingine ni mume wako?" Dailami ameiandika riwaya hii kama ilivyosimuliwa na Ibn Abbas, na hii ni hadithi ya 2631 kwenye uk. 157 wa Jz. 6 ya Kanzul-Ummal.

29. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Mimi ni muonyaji na Ali ni muongozaji; na kutoka kwako Ewe Ali mwongozo utapatikana baada yangu." Tafadhali rejea barua yetu ya 34 na uiangalie kwa makini riwaya hii na zile nyingine zilizonukuliwa humo.

30. Kwa kauli yake hii (s.a.w.w.): "Ewe Ali! Hakuna anayeruhusiwa kuishi ndani ya msikiti akiwa katika hali ya janaba isipokuwa mimi na wewe." Halikadhalika hadithi hii imeandikwa na Tabrani kama ilivyonukuliwa na Ibn Hajar katika kitabu chake "Al-Sawa'iq al-Muhriqa" kama ilivyosimuliwa na Umm Salma, al-Bazzar, na Sa'id hivyo, rejea kwenye hadithi ya 13 ya Al-Arba'in al-Nawawiyya ambayo ananukuu katika sura ya 9. Huyu wa mwisho anamnukuu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Hakuna anayeruhusiwa kuwa katika hali ya janaba katika msikiti huu isipokuwa mimi na Ali." [223]

31. Na kauli yake hii (s.a.w.w.): "Mimi na bwana huyu (yaani, Ali) ni hoja katika taifa langu Siku ya Hukumu." Hii imeandikwa na al-Khatib kama ilivyosimuliwa na Anas.[224] Itakuwaje Abul-Hasan (as) kuwa hoja kama alivyokuwa Mtume (s.a.w.w.), kama hakuwa makamu na mrithi wake kwa mamlaka kamili baada yake? Tafadhali hebu litafakari hili.

---

[220] Rejea maelezo tuliyotoa kuhusu hadithi hii na iliyo kabla yake kwani tumekwishatoa maelezo katika barua ya 10.

[221] Dailami ameiandika riwaya hii kama ilivyosimuliwa na Ammar, naye Abi Ayyuub kama ilivyoelezwa mwanzoni mwa uk. 156, wa Jz. 6 ya *Kanz ul Ummal.*

[222] Hii ni hadithi ya 2539 iliyoandikwa katika ukurasa wa 153, Jz. 6, ya kitabu "*Kanz Ummal."*

[223] Rejea kwenye Barua ya 34 kwa ufafanuzi zaidi.

[224] Tabarani ameiandika katika *al-Ausat*, Khatiib katika *Muttafaq wal Muftaraq* kama ilivyoelezwa katika *Kanzul-Ummal*. Tumeirudia hadith hii katika barua yetu ya 34 na tukatoa hapo angalizo ambalo litakuwa na msaada sana kwa wanachuoni watafiti.

32. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): “Imeandikwa katika mlango wa Peponi: ‘Hakuna mungu ila Allah, Muhammad ni Mjumbe wa Allah, Ali ni Ndugu wa Mjumbe wa Allah,” [225] 3

33. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): Imeandikwa katika nguzo ya ‘Arsh: “Hakuna mungu ila Allah, Muhammad ni Mjumbe wa Allah, Mimi (Allah) Nimemuimarisha (Muhammad) kwa Ali, na nimemsaidia kupitia Ali.”[226]

34. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): “Yeyote yule ambaye anataka kutambua ari ya Nuh, ujuzi wa Adam, upole wa Ibrahim, busara za Musa, kujinyima (anasa za dunia) kwa Isa (sa), basi naamungalie Ali.” Hii imeandikwa na Bayhaqi katika “Sahih” yake na Imamu Ahmad ibn Hanbal katika “Musnad” yake.[227]

35. Katika kauli yake hii (s.a.w.w.): “Ewe Ali! Kuna kufanana kati yako wewe na Isa (a.s.) ambaye mayahudi walimchukia kwa kiasi kwamba walitilia shaka heshima ya mama yake, na kupendwa na Wakiristo kiasi kwamba walimhusisha na hadhi ambayo sio yake.” – Hakim ameisimulia hii katika uk. 122 wa Jz. 3 ya Mustadrak yake.

36. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Waumini wa mbele na mashuhuri zaidi ni watatu: Joshua mwana wa Nun [wa kabila la Ephraim] ambaye aliuamini zaidi Utume wa Musa (as), na yule muumini katika Surat Yasin (Sura ya 36 katika Qur’ani Tukufu) ambaye alimuamini zaidi Nabii Isa (as) na Ali Ibn Abu Talib (as) ambaye alikuwa mu’mini wa mbele kabisa wa Utume wa Muhammad (s.a.w.w.).”[228]

37. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): “Masiddiq (kushuhudia ukweli wa mitume) ni watatu: Habib al-Najjar, muumini wa Aali-Yasiin, ambaye alisema: ‘Enyi watu wangu wafuateni mitume (wa Mungu); Ezekiel, muumini katika Aali Firaun, ambaye alisema: ‘Je mnataka kumuuwa mtu kwa sababu tu amesema Mola wangu ni Allah?’; na Ali Ibn Abu Talib (a.s.) ambaye ni mbora wa juu zaidi kuliko wote.” [229]

38. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.) kwa Ali: “Umma utageuka na kukusaliti; ambapo wewe utadumu katika kushikamana na mila yangu na utauawa katika sunnah yangu; yeyote yule akupendaye wewe hunipenda mimi pia, na yeyote akuchukiaye wewe hunichukia mimi pia, na hizi (ndevu za Ali) zitaloweshwa na damu kutoka kwenye hiki (kichwa cha Ali).”[230] Ali (as) mwenyewe alisema:

[225] Tabrani katika kitabu chake *al-Kabiir*, Ibn Asakir ameipokea kutoka kwa Abil Hamra ambaye vyanzo vyake vinafikia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

[226] Ameipokea Tabrani katika al-Kabiir, na ibn Asakir kutoka kwa Abi Hamraa bila sanad, kama ilivyo katika uk. 158 wa Jz. 6 ya *Kanzul Ummal*.

[227] Hii imewasilishwa kutoka kwao wote na Abul-Hadid kama riwaya ya nne miongoni mwa riwaya zilizotolewa na yeye kwenye uk. 449, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul Balaghah*. Vilevile imenukuliwa na Imamu al-Razi wakati anajadili maana ya aya ya Mubahila katika kitabu chake *Al-Tafsir al-Kabir*, uk. 288, Jz. 2, na ameeleza tu usahihi wa hadithi hii kwamba umekubaliwa na wote kwamba ni sawa. Hadithi hii vilevile imenukuliwa na Ibn Battah kama hadithi iliyosimuliwa na Ibn Abbas, kama ilivyoelezwa kwenye uk. 34 ya *Fath al-Malik al-Ali Bi Sihhati Babi Madiinatul Ilm Ali* cha Imamu Ahmad ibn Muhammad ibn al-Sadiq al-Hassani al-Magharibi wa Cairo. Tafadhali rejea kitabu hicho. Na miongoni mwa waliokiri kuwa Ali ni ghala la elimu na siri za Mitume wote ni mkuu wa masufii (*Gnostics),* Muhiyd-Din ibn Arabi ambaye kutoka kwake Aarif Shirani ameinukuu katika mada ya 32 uk. 172 wa kitabu chake *al-Yuwaqiit wal Jawaahir.*

[228] Hii imenukuliwa na Tabraniy na Ibn Mardawayh kama ilivysimuliwa na Ibn Abbas. Na imenukuliwa na al-Daylami kutoka kwa Aisha, na hii ni hadithi maarufu.

[229] Hii imenukuliwa na Abu Na’im na Ibn Asakir kutoka kwa Abu Layla ambaye vyanzo vyake vinapanda hadi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.); na kunukuliwa vilevile na al-Najjar kutoka kwa Ibn Abbas aliyeisikia kutoka kwa Mtume mwenyewe. Tafadhali rejea kwenye hadithi ya 30 na 31 kati ya hadithi arobaini zilizodondolewa na Ibn Hajar katika Sehemu ya Pili kifungu cha 9, cha kitabu chake *Al-Sawa’iq al-Muhriqa*, mwishoni mwa uk. 74 na ukurasa unaoifuatilia.

[230] Hii imenukuliwa na al-Hakim katika ukurasa wa 147, Jz. 3, ya kitabu chake *Al-Mustadrak* ambako mwandishi anakiri usahihi wake. Al-Dhahabi ameinukuu kwenye kitabu chake *Talkhis*, akikiri usahihi wake.

"Moja ya utabiri wa Mtume (s.a.w.w.) ni kwamba taifa litanisaliti baada ya kufariki kwake." Ibn Abbas anamnukuu Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akimwambia Ali: "Kwa hakika utakabiliana na shida kubwa baada yangu."[231] Ali aliuliza: "Je, nitakuwa na uwezo wa kuiweka imara imani yangu?" na Mtume wa Allah akamjibu kwa kumuitikia.

39. Iangalie kauli yake hii (s.a.w.w.): "Miongoni mwenu kuna mtu atapigana kwa ajili ya tafsiri ya Qur'ani kama ambavyo mimi nimepigana kwa ajili ya kushuka kwake." Wasikilizaji walisisimkwa. Miongoni mwao alikuwepo Abu Bakr na Umar. Abu Bakr akauliza: "Je, mtu huyo ni mimi?" Jibu la Mtume lilikuwa la kukataa. Umar akauliza: "Je, ni mimi?" Mtume (s.a.w.w.) akajibu: "Hapana; bali ni yule anayeshona viatu (vilivyochanika)." Hapo akimaanisha Ali; kwa hiyo, tulimuendea Ali na kumpelekea habari hizo njema, lakini hakunyanyua hata kichwa chake, kana kwamba alikwishazisikia kutoka kwa Mtume wa Allah (s.a.w.w.).[232]

Simulizi kama hiyo ni hadithi iliyosimuliwa na Abu Ayyub al-Ansari wakati wa ukhalifa wa Umar. Kwa mujibu wa al-Hakim, ambaye anategemea juu ya rejea mbili ambazo anazionesha katika ukurasa wa 139 na ukurasa unaofuatia huo, Jz. 3, ya kitabu chake *Mustadrak*, Umar alisema kwamba Mtume wa Allah (s.a.w.w.), aliamuru kwamba wale ambao wanaritadi na wale wanaokaidi na wapinzani wapigwe vita. Ibn Asakir, kama ilivyo anaonesha katika hadith 2588 katika ukurasa wa 155, Jz. 6 wa *Kanz al-Ummal,* anaeleza kwamba Ammar Ibn Yasir alisema kwamba Mtume wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Ewe Ali! Genge la wakandamizaji litakupiga wewe vita; lakini uko katika njia iliyo sahihi (iliyonyooka); yeyote yule ambaye anajizuia kukusaidia wewe sio katika mimi." Na katika hadithi ya Abu Dharr al-Ghiffari (kama alivyoandika al-Daylami kama ilivyo mwishoni mwa ukurasa wa 155, Jz. 6 ya *Kanz al-Ummal*) amemnukuu Mtume wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Naapa kwa Yule ambaye mikononi mwake uko uhai wangu kwamba miongoni mwenu yuko yule ambaye atapigana baada yangu kwa ajili ya tafsiri ya Qur'ani Tukufu kama nilivyopigana na makafiri kwa ajili ya kushuka kwake." Na hadithi ya Muhammad ibn Ubaidullah ibn Abu Rafi'i, kama ilivyooneshwa na al-Tabari katika kitabu chake *Mujma al-Kabir* na kuoneshwa katika ukurasa wa 155 wa Jz. 6 ya *Kanz al-Ummal,* amemnukuu baba yake na babu yake Abu Rafi'i akisema kwamba Mtume wa Allah (s.a.w.w.) alimuambia hivi: "Ewe Abu Rafi'i! Kundi la watu litapigana na Ali baada yangu; Allah amehalalisha kwamba lazima wapigwe vita. Yeyote yule ambaye hana uwezo wa kupigana nao kwa mikono yake, na apigane nao kwa ulimi; kama ikiwa bado hana uwezo wa kufanya hivyo, basi kwa moyo wake." Al-Akhdhar al-Ansari[233] amemnukuu Mtume wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Napigana kwa ajili ya ufunuo wa Qur'ani wakati ambapo Ali atapigana kwa ajili ya tafsiri yake."

40. Yeye (s.a.w.w.) alisema: "Ewe Ali mimi ni bora kuliko wewe kwa sababu ya mimi kuwa Mtume, ambapo wewe ni bora kuliko watu wote kwa sababu ya sifa saba: Wewe ni wa kwanza miongoni mwao kumuamini Allah, mwadilifu zaidi katika kutekeleza ahadi ulizotoa kwa Mwenyezi Mungu, mtiifu zaidi katika amri za Allah, mgawaji mwadilifu zaidi, mwenye kufanya haki zaidi wakati

[231] Hadithi hii na ile iliyoitangulia, yaani hadithi ya Ibn Abbas, zimenukulia na al-Hakim katika ukurasa wa 140, Jz. 3, ya kitabu chake *Mustadrak*, na al-Dhahabi anamnukuu katika kitabu chake *Talkhis al-Mustadrak*. Wote waandishi hawa wanakiri usahihi wa hadithi hii kwa vigezo vya masheikh wawili.

[232] Hii imenukuliwa na al-Hakim kwenye 122, Jz. 3, ya Al-Mustadrak, akisema kwamba ni hadithi sahihi kwa mujibu wa vigezo vya masheikh wawili ambao hawakuijumuisha katika vitabu vyao Al-Dhahabi amekiri usahihi wake kwa sababu ileile katika kitabu chake *Talkhis al-Mustadrak*. Imamu Ahmad ameinukuu kutoka kwa Abu Sa'id katika ukurasa 82 na 33, Jz. 3, ya *Musnad* yake, na al-Bayhaqi ameinukuu kwenye kitabu chake *Sh'aab al-Iman*. Sa'id ibn Mansuur kwenye *Sunan* yake, Abu Na'iim katika Hilyatul-Auliyah na Abu Y'ali katika *Sunan* yake na hii ni hadith ya 2585 katika uk. 155, Jz. 6 ya *Kanzul-Ummal*

[233] Jina lake Ibn Abul Akhdhar, Ibn al-Sakan anamtaja na ananukuu hadithi hii kuhusiana naye kutoka kwa al-Harith ibn Hasirah kutoka kwa Jabir al-Ju'fi kutoka kwa Imamu al-Baqir (a.s.) kutoka kwa baba yake Zaynul-Abidin (a.s.) kutoka kwa al-Akhdhar kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.). Ibn al-Sakan anasema: "Sio maarufu sana miongoni mwa masahaba wa Mtume, na hadithi yake inahitaji kuthibitishwa." Hii imenukuliwa na al-Asqalani katika maandishi yake ya wasifu wa Akhdhar katika kitabu chake *Al-Isabah*. Al-Darqutni ameitoa hadithi hii kwenye kitabu chake *Ifrad*, akisema: "Hadithi hii imesimuliwa tu Jabir al-Ju'fi, ambaye ni Rafidhi."

wa kushughulika na umma, mwenye utambuzi zaidi katika masuala yenye utata, na mwenye kuvutia zaidi kwa ubora na hadhi ya juu zaidi katika macho ya Allah." Abu Sa'id al-Khudri anamnukuu Mtume wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Ewe Ali! Unazo sifa saba ambazo kwazo hakuna mtu anayeweza kupingana nawe; wewe ni muumini wa kweli wa kwanza wa Allah, mtiifu zaidi wa amri za Allah, mwenye huruma zaidi kwa umma, mjuzi zaidi wa masuala ya hukmu na mwenye kuvutia kwa ubora na hadhi zaidi miongini mwao."[234]

Hapa hakuna nafasi ya kunukuu hadithi zote kama hizo ambazo kwa ujumla kila moja huunga mkono nyingine na zote huonesha maana moja, nazo ni kwamba: 'Ali ni wa pili kwa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) katika umma wake, na kwamba ana mamlaka ya uongozi katika kuuongoza (umma) baada tu ya Mtume wa Allah (s.a.w.w.). Hadithi hizi huleta maana kama hiyo katika njia ya mutawatiri kimaana, hata kama maandiko yao hayakuripotiwa kama mutawatiri kilafudhi, na kiasi hiki kitatosha kama uthibitisho usio kanushika, Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[234] Abu Na'im ameinukuu miongoni mwa hadithi zilizosimuliwa na Ma'dh, halikadhalika na hadithi iliyofuatia, yaani, ile ya Abu Sa'id, katika kitabu chake *Hilyat al-Awliya*, na ziko kwenye ukurasa wa 156, Jz. 6, ya *Kanz al-Umamal*.

# BARUA YA 49

## MUHARRAM 11, 1330 A.H.

**I. Kukiri Sifa Bora za Ali,**

**II. Sifa hizo Hazihalalishi Cheo chake cha Ukhalifa.**

Imamu Abu Abdullah Ahmad Ibn Hanbal alisema: "Hakuna miongoni mwa Sahaba wa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) aliye na sifa nyingi kama alizonazo Ali ibn Abu Talib." Ibn Abbas alisema: "Hakuna aya za Qur'ani zilizoteremshwa kwa heshima ya mtu yeyote [mbali na Mtukufu Mtume] zilizo nyingi kama ilivyo kwa heshima ya Ali." Katika tukio jingine alisema: "Kiasi cha aya mia tatu za Qur'ani Tukufu zimeteremshwa kwa heshima ya Ali." Na bado katika tukio jingine alisema: "Wakati wowote Allah alipoteremsha, **'Enyi ambao mmeamini…'** Ali alidokezwa kama bwana wao na mwenye hadhi kubwa; na Allah amewakemea masahaba wa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) sehemu mbali mbali katika Kitabu Chake ambapo wakati wote humzungumzia Ali kwa uzuri." Abdullah ibn Ayyash ibn Abu Rabiyah anasema: "Ali ana ujuzi mkubwa katika elimu; na alikuwa wa kwanza katika kuukubali Uislamu; ana heshima ya kuwa mkwe wa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) na yeye pekee alikuwa na uwezo mkubwa wa kuilewa Sunnah yake (s.a.w.w.), tumaini la ushindi katika vita, na mkarimu mno wa kutoa."

Wakati fulani Imamu Ahmad Hanbal aliulizwa kuhusu Ali na Mu'awiyah, alisema: "Ali alikuwa na maadui wengi mno, maadui zake walijaribu sana kutafuta kasoro kwake lakini hawakufanikiwa kuona kitu. Walikuja kwa mtu mmoja ambaye alipigana naye, na wakamsifu mtu huyo kwa sababu tu ya kumchukia Ali na kushusha hadhi yake na kuwadanganya watu wa ulimwengu." Kadhi Isma'il, al-Nasa'i, Abu Ali al-Nisaburi na wengine wengi walisema kwamba hakuna mtu miongoni mwa Sahaba wote wa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) aliyesifiwa zaidi kama alivyosifiwa Ali.

Hakuna mjadala kuhusiana na yote haya, hata hivyo, bado mjadala unakuja kwamba ni lini Mtume (s.a.w.w.), wakati wa uhai wake alimteua kama khalifa wake? Riwaya zote ulizotaja hazitoi uthibitisho wa wazi wa kuteuliwa kwake kama Khalifa au Imam. Riwaya hizi hutaja tu sifa na nemsi zake tu, na kwa hakika idadi yake haina ukomo na ambazo haziwezi kuelezwa kwa ukamilifu hasa, na tunaamini kwamba yeye (Ali) Allah amemtukuza. Anazo sifa na ubora huu na zaidi. Lakini mengi uliyosema yako nje ya msitari. Vipo vidokezo, bila shaka, kuhusu kuteuliwa kwake kama Khalifa au Imam katika baadhi ya riwaya hizi. Lakini kama unavyojua, vidokezo ni vidokezo tu, wala havitengenezi amri rasmi ya kuteuliwa kama Khalifa. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 50

## MUHARRAM 13, 1330 A.H.

**I. Nususi Juu ya Sifa na Ubora wake, Zimetolewa Kama Hoja**

**II. Juu ya Uimam Wake.**

Haiwezekani kwa mtu mwenye akili ya kupenya kama wewe, ambaye hana kasumba ya upendeleo, na anayetambua vyema umuhimu wa tukio la kauli na hatua zilizo nyuma yake, aliyejaaliwa umaizi kwenye lengo na maana ya kauli, na mwenye elimu ya kimwanazuoni kuhusu Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.), anayeamini katika hekima madhubuti na umwisho wa utume wake, mwenye kutathmini ubora wake kupitia vitendo vyake na maelezo yake, na pia anayejua kwamba Mtume **"Hasemi kwa matamanio yake… (Qur'ani 53:3),"** kwa hakika awe amelikosa lengo la riwaya hizi. Na kwamba maana ya msingi na hitimisho lisilopingika, kulingana na mantiki na akili ya kawaida na matumizi, view vimefichika na ni siri kwake. Haiwezekani kwamba wewe, bingwa unayefahamika wa lugha ya Kiarabu (*athbat*)[235] na fasihi ushindwe kuelewa kwamba riwaya zote hizi zimempa Ali ile hadhi na heshima ya hali ya juu sana, ambayo Allah Aza wa Jala na Mitume Wake hawaitoi isipokuwa kwa warithi wa Mitume hao, kwa watu ambao wanawaamini zaidi kuwa waangalizi wa dini yao, na walezi wa dini hiyo. Hata kama riwaya hizo hazithibitishi kwa uwazi kuteuliwa kwa Ali kama khalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), hapana shaka yoyote kwamba zinahakikisha haki yake kwenye kujuzu hilo.

Matukio na mazingira ya riwaya hizi na maana zake za wazi, bila ubishi yanaelekeza kwenye hatma hiyohiyo. Bwana wa Mitume (s.a.w.w.) mkuu wa Ali, yuko mbali na kutoa cheo kama hicho cha juu kwa mtu yeyote asiyekuwa mtekelezaji wa wasia wake, mwandamizi wake baada yake na makamu wake wakati wa uhai wake. Kadhalika, kama ukiziangalia kwa makini riwaya zote hizi ambazo ni makhsusi juu ya Ali (a.s.) na kwa kufuata haki utahukumu kurudiwa kwake na kusimuliwa kwake mara kwa mara, utaona kwamba zote hizi, isipokuwa chache tu, zinathibitisha Uimamu wake wa jumla, ama kwa uwazi wa moja kwa moja, kama riwaya zilizonukuliwa katika barua zetu namba 20, 26, 36 na 40 na kama vile Tangazo la Ghadir, au kwa dalili ya mlazimiano, kama zile riwaya zilizoorozeshwa katika Barua ya 48. Chukua kwa mfano, kauli yake (s.a.w.w.): "Ali yuko pamoja na Qur'ani na Qur'ani iko pamoja na Ali; viwili hivi havitatengana mpaka vinifikie kwenye Birika (la Kawthar), mnamo Siku ya Kiyama."[236] Au kwa mujibu wa hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): 'Ali ana uhusiano na mimi sawa na ule uhusiano wa kichwa changu na mwili wangu."[237] Na hadithi iliyosimuliwa na Abdul Rahman ibn Awf:[238] "Naapa kwa Yule ambaye uhai wangu uko mikonono Mwake, mtathibitisha kusimamisha Swala, kutoa Zaka, au vinginevyo nitakutumieni mtu kutokana na mimi mwenyewe, au kama mimi mwenyewe," kisha Mtume (s.a.w.w.) alikamata mkono wa Ali na akasema: "Mtu mwenyewe ndiye huyu." Kuna riwaya nyingi zinazofanana na hii. Hii ni faida nzuri sana ya wazi ambayo kwamba inavutia nadhari ya wale wote wanaotafuta ukweli, na ya wale ambao huficha kile chenye utata, na wale wanaotafakari kwa kina na kujadili mambo wao wenyewe kwa kujitegemea. Wataelewa kile tu ambacho kimemaanishwa humo, alimuradi tu wanajiweka mbali na vishawishi na matamanio na kutoonyesha chuki binafsi. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

[235] "*Athbat*" ni wingi wa "*thabat*" na "*asnad*" ni wingi wa "*sanad*" na wamwisho humaanisha "*hujjah,*" yaani, thibitisho au mamlaka

[236] Hii imenukuliwa na al-Hakim kwenye uk. 124, Jz. 3, ya *al-Mustadrak,* halikadhalika na al-Dhahabi katika kitabu chake *Talkhis al-Mustadrak*. Waandishi wote hawa wanathibitisha usahihi wake.

[237] Hii imenukuliwa na al-Khatib katika hadithi iliyosimuliwa na al-Bara' ibn Aazib, na al-Daylami kama ilivyosimuliwa na Ibn Abbas. Inawasilishwa na Ibn Hajar katika ukurasa wa 75 wa kitabu chake *al-Sawa'iq al-Muhriqa*, hivyo rejea hadithi ya 35 katika arubaini alizo zinukuu katika Kifungu cha Pili, Sura ya 9, ya *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*.

[238] Ni hadithi ya. 6133, ukurasa wa 405, Jz. 6, katika *Kanz al-Ummal.* Na aya ya Mubahila hukutosheleza kwa ajili ya kuthibitisha kwamba nafsi ya Ali ni sawa na ile ya Mtume (s.a.w.w.) kwa kuitazama kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na al-Razi katika kitabu chake *Mafatih al-Ghayb*, ukurasa wa 488, Jz. 2, na rejea vilevile kwenye kile ambacho tumekitaja wakati tulipokuwa tunashughulikia aya hii.

# BARUA YA 51

## MUHARRAM 14, 1330 A.H.

**Hoja Pinzani Kwa Msingi wa Riwaya Zinazosifia Wengine.**

Washindani wako wanaweza kupinga madai yako kwa kuonesha riwaya ambazo zinazotaja sifa za Makhalifa watatu waongofu, na kuonesha riwaya nyingine zenye kusifu Waislamu wa mwanzo kutokana na Muhajirun na Answar; je utasemaje kwa hilo? Wassalam

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 52

## MUHARRAM 15, 1330 A.H.

**Kukataa Hoja Pinzani.**

Tunaamini juu ya sifa za wa mwazo kuukubali Uislamu miongoni mwa Muhajirun na Answar, Allah awe radhi nao na wao waridhie. Sifa zao ni nyingi mno zisizohesabika. Kuna aya nyingi za Kitabu (Qur'ani) na Sunnah sahihi juu ya sifa zao. Hizi pia tumezichunguza kwa kina. Lakini Allah ni Mwenye kujua zaidi, kwamba hatukuona hata kidogo zenye kulingana au kukinzana na aya au hadithi zenye kumsifia Ali (as), au sifa zao zozote zilizotajwa humo ambazo zinaweza kulinganishwa au kupingana na ubora wa Ali (a.s.). Lakini ulinganisho na ukinzanaji hauna nafasi hapa kwani mada ya mjadala wetu hapa ni Uimam au Ukhalifa na sio masuala ya ulinganishaji wa sifa zao. Ndiyo, wapinzani wetu wamesimulia hadithi ambazo zinawasifia masahaba fulani wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hadith ambazo hazina nafasi kwenye kumbukumbu zetu za hadithi na ambazo sisi hatuzichukulii kwamba ni sahihi. Kutumia kwao hadihti hizo kukanusha mitazamo yetu kunakataliwa na haitegemewi kutoka kwa yeyote yule ila asiye na misingi maalum na mkaidi. Zaidi ya hayo sisi kwa sababu yoyote hatufungwi katika kuzitegemea au kuzikubali hadithi kama hizo kuwa ni sahihi, ambazo hazikusimuliwa mwote katika rejea zetu. Wewe lazima utakuwa umeona jinsi ambavyo, ili kukuridhisha wewe, wakati wote tumenukuu riwaya ambazo zimesimuliwa na vyanzo vyenu wenyewe tu na ambazo zimepokewa kupitia vyanzo sahihi na vinavyokubalika na wasimulizi wenu, kama vile Hadith ya Ghadir au kama hiyo. Kadhalika tumezichunguza riwaya ambazo zinawasifia waliosilimu mwanzoni miongoni mwa Muhajirina na Ansari, na hatukuona dalili yoyote humo yenye kupingana na ubora wa Ali (a.s.) au ushahidi na uthibitisho wowote juu ya haki yao ya ukhalifa huo, wala kuwa na chochote chenye kudokezea hilo. Na hiyo ndio sababu kwamba hakuna yoyote aliyeziendea riwaya hizo ili kuthibitisha uhalali wa ukhalifa wa makhalifa watatu waongofu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 53

## MUHARRAM 16, 1330 A.H.

**Maombi Ya Hadithi ya Ghadir.**

Umerudia mara kwa mara kutaja Hadith ya Ghadir. Tafadhali simulia kisa chake kama kimesimuliwa kwenye vyanzo vya Sunni, ili tuweze kuiangalia. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh**.

# BARUA YA 54

## MUHARRAM 18, 1330 A.H.

**Mnyororo wa Hadith ya Ghadir Unaong'ara.**

Tabrani na wengine wamesimulia hadith iliyopokewa na Zayd ibn Arqam na kusimuliwa kupitia vyanzo vinavyokubaliwa kwa pamoja kwamba ni vya kuaminika na kutegemewa,[239] akisema: "Mtume wa Allah (s.a.w.w.), alitoa khutba mahali paitwapo Ghadir Khum chini ya kivuli cha miti michache akisema: 'Enyi watu naona kwamba hivi punde nitaitwa na ni lazima nijibu wito huo.[240] Mimi nitaulizwa juu ya majukumu yangu[241] nanyi mtaulizwa pia;[242] basi mwasemaje?' Wakasema: 'tunashuhudia kwamba umefikisha ujumbe, na umefanya juhudi kwa kila uwezalo katika kutuongoza [umma] kwenye njia iliyonyooka; na wakati wote ukitushauri. Kwa hiyo, Allah akulipe malipo mema.' Aliwauliza: 'Je, hamshuhudii vilevile kwamba hapana mola isipokuwa Allah na Muhammad ni mja na Mjumbe wake, kwamba Pepo ipo ni haki na kwamba moto upo ni haki, kwamba kifo ni haki, kwamba uhai baada ya kifo ni haki, kwamba Kiyama hakina shaka kitakuja, na Allah atawafufua waliomo makaburini?' Wakasema: "Ndiyo, hakika, tunashuhudia yote hayo."[243] Kisha akasema: 'Ewe Mola Mwenye nguvu zote! Shuhudia Nawe pia kwamba wameshuhudia.' Kisha akasema: 'Enyi watu! Allah ni Bwana *(Mawla)* Wangu, na mimi ni *Mawla* (Bwana) wa waumini. Nina mamlaka zaidi juu ya maisha yao kuliko walivyo wao wenyewe; kwa hiyo, kwa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* wake huyu (Ali) ni *mawla* wake.[244] Ee Allah! Kuwa rafiki kwa yule anayekuwa rafiki kwake, na kuwa adui kwa yule mwenye kujiweka adui kwake.'

---

[239] Waandishi wengi mashuhuri wamekiri usahihi wake. Hata Allamah Ibn Hajar anaelezea hivyo hivyo, akimnukuu Tabrani na wengine katika *Shuhba* Na. 11, moja ya ambazo zimetajwa katika ukurasa wa 25, kifungu cha 5 Sura ya 1, ya *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*.

[240] Kwanza kabisa alitangaza kwamba wakati wake wa kufariki unakaribia haraka. Hili lilikuwa ni tahadhari kwa watu kwamba wakati umefika wa kukamilisha ujumbe wake wa ki-mbinguni na kuhakikisha hali ya kiroho ya baadae juu ya wafuasi wake kwa kumteua mrithi wake, na kwamba ni jambo muhimu ambalo asingevumilia kuchelewesha kulifanya kwa kuhofia kwamba asije kufariki kabla ya kumsimamisha sawasawa mrithi wake katika kazi ya ujumbe huo.

[241] Kwa vile uteuzi wa ndugu yake ulikuwa haukubaliki kabisa kwa wenye ubinafsi, husuda, waovu na wanafiki, yeye Mtume (s.a.w.w.) aliona kwamba ni vema kabla ya kutoa tangazo hilo, kwanza atulize hisia zao na kuzipa wakati nyoyo zao kwa kutangulizia tangazo hilo la uteuzi maneno ya ziada ili kuepuka fursa yoyote ya kuonyesha hasira. Kwa hiyo alisema: "Mimi ni mwenye kuhojiwa na kuwajibika," ili kwamba waweze kuelewa kwamba yeye alikuwa kwenye amri ya Allah ya kufikisha kwao tangazo hilo; na kwamba atakuja kuulizwa kuhusu kulifikisha hilo na kwamba kulikuwa hakuna jinsi. Imamu al-Wahdi, ameeleza katika kitabu chake *Asbabul Nuzul*, kutoka vyanzo vya kutegewa hadi kufikia kwa Abu Sa'id al-Khudri akisema: "Aya ya 67 Sura ya 5; 'Ewe Mjumbe! Fikisha kile ambacho kimeteremshwa kwako kutoka kwa Mola Wako,' iliteremshwa Ghadir Khum kwa ajili ya Ali ibn Abu Talib (a.s.)."

[242] Kwa kusema "Ninyi pia ni wenye kuwajibika, mtaulizwa," yeye (s.a.w.w.), huenda alidokeza kwenye hadithi ilivyonukuliwa Daylami na wengine kama ilivyoelezwa kutoka kwa Abi Sa'iid na kuandikwa katika *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*, kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Waambie wasimame, watakuja kuulizwa kuhusu mamlaka makubwa na uongozi wa Ali." Na Imamu al-Wahidi anasema: "Wataulizwa kuhusiana na *wilayat* ya Ali na Ahlul Bayt." Hivyo, madhumuni ya msemo huu "na ninyi pia mtaulizwa" ni kuwatisha na kuwahofisha wale ambao wangepinga mamlaka ya *uwalii* na *wasii* wake.

[243] Khutba hii inahitajia kuizingatia vilivyo. Usomaji wa makini wa riwaya hii utafichua ukweli kwamba imani juu ya mamlaka makubwa na wilayat ya Ali ni moja ya kanuni za misingi ya dini, na hili ndilo Shi'ah wanaloamini. Mtume (s.a.w.w.) kwanza aliwataka waliohudhuria pale washudie kwamba hakuna mungu isipokua Allah, na kwamba Muhammad ni Mtumishi na Mjumbe Wake, na kwamba Saa (Qiyama) inakaribia; hakuna shaka kuhusu hilo, na kwamba hakika Allah atawafufua wale walioko makaburini. Na walipokuwa wameahidi kuyashuhudia yote haya na wakaonyesha imani yao katika hayo, aliwataka waamini kwamba Ali (a.s.) ni *Walii*, yaani Mlinzi wa Dini, Kamanda Mkuu wa waumini na kipenzi cha Allah ili kwamba kila mtu aweze kujua kwamba kuamini juu ya Wilayat ya Ali ni msingi muhimu wa imani kama uleule wa imani juu ya Upweke wa Allah (Tawhiid), Utume wa Muhammad (s.a.w.w.), kufufuliwa kwa wafu na katika Siku ya Kiyama, na kwamba mtu ataulizwa kuhusu hilo pia. Hii ni dhahiri kwa wale wote wenye kufuata mtindo wa khutba hii, ule uwekwaji sawa wa sentensi zilizomo na maana ya maneno watafikia uamuzi huo huo usiopingika.

[244] Maneno yake: "*Mimi ni mawla*" yanaashiria kwamba neno Maula maana yake ni mtu ambaye ni "*awla*" wa juu zaidi katika hadhi na ubora. Hivyo, alichomaannisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa sentensi hii ni: " Allah ni *awla* Mkuu kwa haki na nguvu juu yake, na yeye ni Mkuu kwa haki na nguvu kwa waumini, na yeyote mwenye kunichukulia mimi kama *mawla* wake kwake na Ali ni Mkuu kwa haki na nguvu hivyo hivyo.

Kisha akasema: 'Enyi watu! Mimi nawatangulieni, nanyi mtaungana nami kwenye Birika (la *Kawthar*) ambalo ni pana kuliko umbali wa kuanzia Basra mpaka San'aa; lina vikombe vya shaba vingi mno kama nyota, na nitawauliza mtakapoungana nami kuhusu Vizito Viwili, jinsi mtakavyoshughulika navyo baada ya kufariki kwangu. Kitu kizito zaidi ni Kitabu cha Allah, Aza wa Jala, ambacho ncha yake moja iko mikononi mwa Allah na ncha nyingine iko mikononi mwenu. Hivyo, shikamaneni nayo ili msije mkapotea, na msikibadilishe wala kukirekebisha. Na kizito kingine ni Ahlu'l-Bayt wangu, kwani Aza wa Jala, na Mwenye kujua zaidi amenijulisha mimi kwamba viwili hivyo havitatengana mpaka viungane nami kwenye Birika [la *Kawthar* ].'" [245]

Katika sehemu inayoshughulika na sifa za Ali katika *al-Mustadrak* uk. 109 wa Jz. 3*,* al-Hakim amesimulia kutoka kwa Zayd ibn Arqam[246] na kusimuliwa kupitia vyanzo viwili ambavyo vyote huchukuliwa kama vya kuaminika kwa vipimo vya Masheikh wote wawili (Bukhari na Muslim). Zayd ibn Arqam anasema kwamba wakati Mtume wa Allah (s.a.w.w.), alipokuwa anarudi kutoka kwenye Hijja yake ya Mwago, alisimama sehemu iitwayo Ghadir Khum na akawaamuru waumini kufagia sehemu ile chini ya miti michache mikubwa ambako mimbari ya matandiko ya ngamia ilitengenezwa kwa ajili yake. Alisimama na kusema:

"Inaonekana kana kwamba nimeitwa na nitaitikia wito huo, na nawaachia vizito viwili, kimoja ni kikubwa kuliko kingine, Kitabu cha Allah Mtukufu na Kizazi changu, angalieni jinsi mnavyoshughulika navyo baada yangu, kwani havitatengana mpaka viungane nami kwenye Birika [la kawthara]." Kisha akaongeza: "Allah Aza wa Jala ni Bwana *(Mawla)* wangu, na mimi ni *mawla* wa kila muumini." Kisha alishika mkono wa Ali na kuunyanyua juu na akasema: "Kwa yule ambaye mimi ni *mawla* wake huyu Ali [bila mwanya] ni *mawla* wake; Ewe Mola! Kuwa rafiki kwa yule mwenye kuwa rafiki kwake, na kuwa adui kwa mwenye kuwa adui kwa yeyote yule mwenye kumpinga yeye."

Imam Hakim ananukuu kikamilifu hadithi hii ndefu ambayo al-Dhahabi hakuitolea maelezo katika kitabu chake *Talkhis*. Al-Hakim vilevile, anainukuu kama ilivyosimuliwa katika mlango wa kumtaja Zayd ibn Aqram katika kitabu chake *Al-Mustadrik,* Jz. 3, uk. 533 huku akikiri usahihi wake. Lakini licha ya imani yake asilia, al-Dhahabi ameinakili katika *Talkhis* yake, kutoka kwenye maelezo ya Zayd, ambayo unaweza kurejea.

Imamu Ahmad ibn Hanbal amepokea katika *Musnad* yake Jz.4, uk. 372 hadithi hiyo iliyosimuliwa na Zayd ibn Arqam ambaye anasema hivi: "Tulikuwa tunafuatana na Mtume wa Allah (s.a.w.w.) wakati tuliposimama katika bonde liitwayo Wadi Khum, na akaamuru kila mtu kukusanyika kwa ajili ya Swala katikati ya joto la mchana. Kisha shuka kubwa ilitandazwa juu ya miti ya mkangazi kuweka kivuli kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) halafu akatutolea khutba. Alisema: 'Je, hamjui? Hamshuhudii ukweli kwamba nina haki iliyotangulia na mamlaka makubwa juu ya maisha ya waumini kuliko waumini wenyewe?' Wakajibu 'Ndio hakika, tunashuhudia hayo.' Akasema: 'Yeyote yule anayenikubali mimi kama *mawla* wake, Ali ni *mawla* wake pia, Ee Mola! Kuwa rafiki kwa yule mwenye kuwa rafiki wa Ali; na kuwa adui kwa yeyote yule mwenye kumpinga Ali.'"

Na Al-Nasa'i amepokea kutoka kwa Zayd ibn Arqam akisema kwamba wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa anarudi kutoka Hija yake ya mwago, na aliposimama Ghadir Khum, alituamuru sehemu ile chini ya miti michache mikubwa tuifagie na tutengeneze mimbari kutokana na matandiko ya ngamia. Akapanda juu ya mimbari hiyo na akasema: "Inaelekea kana kwamba nitaitwa hivi karibuni nami sina budi niitikie wito huo.

[245] Maneno haya ya hadithi yamenukuliwa kama yalivyo na Tabraniy, Ibn Jarir, al-Hakim al-Tirmidhi, kutoka wka Zayd ibn Aqram. Inasimuliwa na Ibn Hajar kutoka kwa Tabraniy katika ukurasa wa 25 wa na wengine katika maneno haya haswa, na kuelezea kwamba usahihi wake unakubaliwa na Waislam wote.

[246] Rejea kwenye ukurasa wa 21 wa *Al-Khasa'is al-Alawiyya*, ambako Mtume (s.a.w.w.) ananukuliwa akisema: "Kwa yeyote yule ambaye mimi ni *Walii* wake, huyu (Ali) ni Walii wake."

Ninakuachieni miongoni mwenu Vitu Viwili Vizito, kimojawapo ni kikubwa kuliko kingine; Kitabu cha Allah na Kizazi changu, watu wa nyumbani kwangu (Ahlul-Bayt). Hivyo, angalieni jinsi mtakavyoshughulika navyo vyote baada yangu, kwani viwili hivyo havitatengana mpaka viungane nami katika Birika [la *Kawthara*].” Kisha akaongeza: “Hakika Allah ni Bwana *(Mawla)* wangu, na mimi ni *mawla* (bwana) wa kila muumini.” (*Khasais Alawiyah* uk. 2(1). Huku akiuchukua mkono wa Ali aliongeza kusema: “Kwa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* (bwana wake) wake, huyu Ali ni *mawla* wake pia; Ee Mola! Kuwa rafiki kwa mwenye kuwa rafiki naye, na kuwa adui kwa wote wale wanaomchukia.”

Abul Tufail anasema: “Nilimuuliza Zayd: ‘Ulisikia maneno haya ya Mtume wa Allah (s.a.w.w.) wewe mwenyewe?”[247] alijibu kwamba wale wote ambao walikuwa pale chini ya miti mikubwa walimuona Mtume kwa macho yao na kumsikia kwa masikio yao wenyewe. Hadithi imeandikwa na Muslim katika mlango wa fadhail za Ali (a.s.) katika *Sahih* yake, kutoka kwa wasimuliaji mbalimbali tofauti ikiishia na Zayd ibn Arqam, lakini aliifupisha kwa namna ya kuikata, na hivyo ndivyo wafanyavyo baadhi ya watu wa aina yake kwa desturi yao kwenye masuala kama hayo.

Imamu Ahmad ibn Hanbal ameiandika hadithi hii kutoka kwa al-Baraa ibn Azib[248] kutoka vyanzo viwili tofauti, Baraa anasema: “Tulifuatana na Mtume wa Allah (s.a.w.w.). Tulisimama mahali paitwapo Ghadir Khum. Adhana kwa ajili ya Swala ya jamaa ilisomwa. Sehemu yenye miti miwili ilichaguliwa, na kisha pakafagiliwa kwa ajili yake. Aliswali swala za mchana kisha akamshika Ali mkono wake na akauliza mkusanyiko ule wa watu: ‘Je, hamjui kwamba mimi nina mamlaka zaidi juu ya kila muumini kuliko alivyo yeye mwenyewe?’ wakajibu: ’Ndio tunajua.’ Akauliza (tena): Je, mnajua kwamba nina haki zaidi juu ya kila muumini kuliko muumini mwenyewe?’ wakajibu kwa kukubali. Kisha akaushika mkono wa Ali na akasema: “Yeyote yule ambaye mimi ni bwana *(mawla)* wake, huyu Ali ni *mawla* wake pia; Ewe Mola! Kuwa rafiki kwa mwenye kuwa rafiki yake na kuwa adui kwa mwenye kuchagua kuwa adui yake.’ Kisha Umar (al-Khatab) punde tu akamwendea Ali na akasema: ‘Hongera, ewe mtoto wa Abu Talib! Asubuhi hii umekuwa bwana (mawla) wa kila muumini mwanaume na mwanamke.”’

An-Nasai amepokea kutoka kwa Aisha bint Sa’d akisema kwamba alimsikia baba yake akisema: “Nimemsikia Mtume wa Allah (s.a.w.w.) katika siku ya Juhfa, wakati akitoa khutba huku ameushika mkono wa Ali, akamshukuru Allah kisha akasema: ‘Enyi watu! Je, mimi sio *mawla* wenu.’ Wakasema: ‘Umesema kweli ewe Mtume wa Allah.’ Kisha akaunyoosha mkono wa Ali na akasema: ‘huyu ni *walii* wangu kwenu na atalipa madeni yangu kwa niaba yangu, mimi rafiki wa yeyote yule mwenye kumpenda na ni adui kwa yeyote mwenye kuchagua kuwa adui yake.’”

Sa’d huyu naye anasimulia akisema yeye alikuwa miongoni mwa waliofuatana na Mtume (s.a.w.w.). Wakati walipowasili Ghadir Khum, wale waliokuwa wametangulia walirudi na kujiunga naye, ambapo aliwangojea wale waliokuwa nyuma, mpaka watu wote wakakusanyika. Kisha akasema: ‘Enyi watu!

[247] Swali la Abu Tufayl ni dalili ya wazi ya kushangazwa kwake na upuuzaji wa umma huu maelekezo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na Ali licha ya kusimulia hadithi kutoka kwa Mtume wake (s.a.w..) kuhusu haki iliyotangulia na mamlaka makubwa ya Ali juu ya maisha ya waumini siku ile ya Ghadir, sawa na haki tangulizi na mamlaka ya Mtukufu Mtume mwenyewe. Ama alikuwa kama vile mwenye wasi wasi na usahihi wa hadithi hiyo kwa vile ummah umelimaliza suala la ukhalifa kwa kura mbele ya ukiukwaji wa dhahiri wa tangazo la Mtukufu Mtume, au kushangazwa na upuuzaji mkubwa wa wafuasi wa tamko muhimu la Mtume wao. Kwa hiyo aliendelea na kumuulizia Zayd kama yeye amemsikia akisema hivyo hivyo. Sauti yake ilikuwa ile ya mtu ambaye ameshangazwa, tatazika na mwenye kushuku. Zayd alimjibu kwamba licha ya kuwepo umati mkubwa wa watu kwenye tukio hilo kwa kweli walimuona Mtume kwa macho yao na kumsikia kwa masikio yao. Majibu ya Zayd yalimridhisha juu ya ukweli wa kile ambacho kilikuwa kimeelezwa na Kumait, mshairi maarufu ambaye alitunga mashairi ya kumsifu Ali (a.s.) katika mistari ifuatayo: “Katika bonde la Ghadiir, Mtume (s.a.w.w.) alimtangaza Ali (a.s.) kuwa mrithi wake.Ummah ungekubaliana na kutii tangazo hilo! Lakini waliliamua suala la urithi kwa kiapo cha utii.
Sijawahi kushuhudia upigaji kura wa kiapo cha utii kuhusu jambo nyeti kama hilo. Wala sijashuhudia siku nyingine muhimu sana kama siku ya Ghadiir. Wala sijaona ubomoaji mbaya wa haki kama huu!

[248] Hii imetokea kwenye ukuras wa 281 wa kitabu chake Al-Khasa’is al-Alawiyya, katika sura inayoshughulika na cheo cha Ali katika katika macho ya Allah, Aza wa Jallah, na vilevile katika ukurasa wa 25 wa sura nyingine inayoamuru kukubali wilayat yake na kuonya dhidi ya kuwa adui kwake.

Ni nani *walii* wenu?' wakajibu: 'Allah na Mtume Wake.' Kisha akaushika mkono wa Ali, akaunyoosha, na akasema: 'Yeyote yule ambaye amemfanya Allah na Mtume Wake kama *walii* wake, huyu Ali ni *wali* wake; Ee Mola! Kuwa rafiki kwa yeyote mwenye kuwa rafiki naye na mchukie yeyote mwenye kumchukia na kumfanya aduai yake.'"

Kuna hadithi nyingi zisizo na idadi kuhusu kadhia ya Ghadiir ambazo zote zinathibitsha wazi kwamba Ali ni makamu na mrithi wa Mtume kama vile ambavyo al-Fadhli ibn al-Abbas Abu Lahab alivyosema katika shairi lake maarufu.[249] "Ali alikuwa mwandamizi wa Muhammad baada yake na mwenza na mshiriki wake wa karibu mno katika kila tukio." Wassalaam

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[249] Hili ni moja miongoni mwa mashairi yaliyotungwa na Fadhl Ibn Abbas ibn Abu Lahabi kama majibu kwa al-Walid ibn Uqbah ibn Abu Mu'iit, kama yalivyonukuliwa na Muhammad Mahmuud al-Rafi'i katika utangulizi wake kwenye *Sharh al-Hashimiyyat*, ukurasa wa 8.

# BARUA YA 55

## MUHARRAM 19, 1330 A.H.

**Kwa nini Riwaya hii Imetumika Kama Ushuhuda, Ingawa Haikusimuliwa Mfululizo (*mutawatir*).**

Shi'ah wanakubaliana kwa pamoja kwamba riwaya moja kama hiyo inaweza kutolewa kuunga mkono na kuutetea Uimamu, kama tu itasimuliwa kwa mfululizo wa mutawatir, kwani Uimam ni moja ya kanuni za msingi wa imani yao. Kwa hiyo basi, haieleweki ni kwa nini hadithi ya Ghadir imetolewa katika kuunga mkono hoja yako ingawa hadithi hiyo haikuwasilishwa kwa mfululizo wa mutawatir ingawa imesimuliwa kupitia vyanzo sahihi vya kutegemewa na inachukuliwa kuwa ni sahihi na muhadithina wa Kisunni.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 56

## MUHARRAM 23, 1330 A.H.

**I. Uhalisia wa Mambo Unaifanya Hadith Ya Ghadir Kuwa Mutawatir,**

**II. Ilikuwa ni Fadhila Maalum za Mwenyezi Mungu Mtukufu,**

**III. Mtume Wa Allah (s.a.w.w.) Aliipa Umuhimu Maalum,**

**IV. Amirul Muminin (a.s.) Aliipa Umuhimu Maalum,**

**V. Al-Husein (a.s.) Aliipa Umuhimu Maalum,**

**VI. Maimamu Miongoni mwa Ahlul-Bayt (As) Waliipa Umuhimu Maalum,**

**VII. Shi'ah Waliipa Umuhimu Maalum,**

**VIII. Imesimuliwa Mfululizo (Mutawatir) Kwa Maoni ya Umma wa Kiislam.**

Katika barua ya 24 hapo juu, tayari tumekwisha kuelezea kwa kirefu sababu za kuleta kwetu hadithi hii kama hoja katika kuunga mkono Uimam.

Zaidi ya hayo, maumbile ya kibinadamu yanathibitisha uwasilishwaji wa mfululizo (*Tawatur*) wa hadithi ya Ghadir. Kama ilivyo kwa matukio yote ya kihistoria yenye umuhimu wa ki-umma ambayo yanakuwa ndio gumzo la umma, na yanasimuliwa kutoka kizazi hadi kizazi, hadithi ya Ghadir imekuwa siku zote ndio mazungumzo ya Umma mzima wa Kiislam na imesimuliwa kwa wingi sana hadi leo hii. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alifanya maandalizi yasiyo ya kawaida kwa ajili ya usimuliaji wa hadithi hii. Kadhia yenyewe ilikuwa ni safari yake ya kurejea kutoka kwenye Hijja yake ya mwisho iliyokuwa imetangazwa kabla ya hapo. Aliweka kituo wakati wa mchana kwenye njia ndogo ya kwenye ardhi hame isiyo na kivuli mbali na kile kilichotolewa na miti michache ya mikangazi, kwa ajili ya ule umati mkubwa wa wafuasi uliotoka sehemu mbalimbali na maeneo ya mbali. Hiyo sehemu ya mkusanyiko ilikuwa ni katika njia panda ya njia ziendazo pande kadhaa tofauti. Alikuwa mwangalifu haswa katika kuhakikisha kwamba wale waliokuwa wamemtangulia wanarejea na waliokuwa nyuma wanamkuta ili idadi kubwa kabisa iwezekanayo ya Waislam iweze kusikia na kushuhudia lile tangazo muhimu ambalo lilitolewa kabla hawajatawanyikia miongoni mwa njia zao tofauti. Isitoshe, waliagizwa kulifikisha tangazo hilo kwa wengine kwenye maeneo wanakokwenda. Ni vipi tangazo lililotolewa katika mazingira kama hayo lionekane kama hadithi iliyosimuliwa au kuandikwa na watu wachache na isiwe imesimuliwa kwa wingi? Tangazo hili ni lazima litakuwa limetangazwa na kuenea kote katika ulimwengu wa Kiislam, nchi kavu na baharini papo kwa papo kama miale ya jua linalochomoza inavyoenea kila mahali juu ya ardhi na kwenye maji. **"Na kamwe hutaona tofauti katika utaratibu wa Allah (Qur'ani, 33:62)."**

Ndio kusema kwamba Hadithi ya Ghadir ni chechem ya fadhila na utukufu. Ni Mwenyezi Mungu ambaye alimfunulia Mtume Wake (s.a.w.w.) hadithi hii, akaielezea katika Qur'ani ambayo inasomwa na Waislamu wakati wa usiku na mchana, katika hadhara na katika faragha, katika maombi yao na dua, katika Swala zao, katika hotuba juu ya mimbari zao na katika adhana juu ya minara:

**"Ewe Mtume fikisha kile ambacho kimeteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako, na kama hutafanya hivyo, basi utakuwa hukifikisha ujumbe Wake kabisa, na Allah atakulinda kutokana na watu (waovu)…"** (Qur'ani 5:67)[250]

[250] Tuna hakika kabisa kwamba aya hii ilishuka kuhusu *wilayat* ya Ali siku ya Ghadir Khum, na hadithi katika kumbukumbu zetu juu ya suala

Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa amefikisha ujumbe huu wa Mwenyezi Mungu (uliodokezwa katika aya hii), wa kumteuwa Ali kama Imamu wa wafuasi wake, Allah Aza wa Jalah siku hiyo hiyo alimteremshia aya ifuatayo:

**"Siku ya leo nimewakamilishieni dini yenu, na kuwakamilishieni neema yangu juu yenu, na nimewaridhieni Uislamu kuwa dini yenu…"** (Qur'ani 5:3)[251]

Hivyo, hongera juu ya hongera kwa Ali; hii ni neema ya Allah; humpa yeyote yule amtakaye. Yeyote yule ambaye ataangalia aya hizi kwa makini hatasita kuzikubali hizo fadhila maalum za Allah.

Wakati Mwenyezi Mungu alikuwa makhsusia kama hivyo kuhusu tangazo hilo, hakuna ajabu kwamba suala hilo likaonesha umuhimu mkubwa machoni kwa Mtume wa Allah (s.a.w.w.). Na ilikuwa hivyo. Pale alipohisi kwamba mauti yake yamekaribia, aliamua kwa mujibu wa amri ambayo amepokea kutoka kwa Allah Aza wa Jalla kutangaza *wilayat* ya Ali wakati wa Hijja yake kubwa, mbele ya kundi kubwa la masahaba wake, ingawa alikuwa amekwishamtangaza Ali kuwa mrithi wake wakati wa kutangaza Utume wake, kama katika riwaya ya kuwaonya ndugu wa karibu huko Makka ndani ya nyumba ya Abi Talib, na katika matukio mengine ya baadae ambayo baadhi yake mpaka sasa tumekwisha kuyaeleza. Lakini hakuridhika na matangazo haya ya hapa na pale. Kwa hiyo, Mtume (s.a.w.w.) alifanya maandalizi ya tangazo la hadhara mapema kabisa kwamba atakwenda katika Hijja yake ya mwisho kabisa. Matokeo yake waumini walimiminika kutoka sehemu zote, za mbali na karibu na walikuwepo zaidi ya watu laki moja wakati alipoondoka Madina kuelekea Makka.[252] Katika siku ya kisimamo cha Arafah mwezi 9 Dhil-Hijjah, kwenye hotuba yake aliwajulisha waliohudhuria kwamba: "Ali anatokana na mimi, na mimi natokana na Ali, na hakuna mtu yeyote awezaye kutekeleza jukumu langu kama Mtume isipokuwa mimi mwenyewe au Ali"[253]

Na wakati alipokuwa anarudi kutoka kwenye Hijja yake hiyo wote laki moja na zaidi alikuwa nao. Alipowasili katika bonde la Khum, malaika Jibrail alimshukia akiwa na *"Ayat Tabligh,"* aya ya kufikisha ujumbe kutoka kwa Mola wa walimwengu. Mtume s.a.w.w. alishuka pale na kusubiri mpaka wale waliokuwa nyuma yake wakafika, halikadhalika na wale waliokuwa mbele yake waliporejea kwake. Wakati wali-

hili ni nyingi mno na mutawatir kupitia Maimam katika kizazi kitoharifu cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini kwa ajili ya rejea kwenye simulizi yake kutoka vyanzo vingine, rejea kwenye kile ambacho Imamu al-Wahidi amekinukuu katika ufafanuzi wa aya hii ya Surat al-Ma'idah ukurasa wa 50 wa kitabu chake *Asbabul Nuzul* ambamo ameipokea hadith ya Ghadiir kutoka vyanzo viwili vya kuaminika: Atiyyah na Abu Sa'id al-Khudri. Huyo wa kwanza alimsikia huyu mwingine akisema: "Aya hii; **'Ewe Mtume, fikisha ulichoteremshiwa kutoka kwa Mola wako….. (5:67)** iliteremshwa Siku ya Ghadir Khum kwa ajili ya Ali ibn Abu Talib (as)." al-Hafidh Abu Na'im wakati anafafanua tafsiri ya aya hii katika *Nuzal al-Qur'ani* ameandika hadith hii kama ilivyosimuliwa na vyanzo viwili, mmoja ni Abu Sa'id na mwingine ni Abu Rafi. Vilevile imesimuliwa na Imam Ibrahim ibn Muhammad al-Hamawaini al-Shafi'i katika kitabu chake *Al-Fara'idus-Simtain* kutoka kwa vyanzo mbali mbali vikiishia na Abu Hurayrah. Imenukuliwa na Imamu Abu Is'haq al-Tha'labi wakati anafafanua maana ya aya hii katika kitabu chake *Al-Tafsir al-Kabir* kwa mategemeo ya vyanzo viwili vya kuaminika. Isitoshe, inatupasa kuzingatia kwamba Swala ilikuwatayari imekwishasimamishwa kabla ya kushuka kwa aya hii, Zaka ilikuwa imekwishafanywa ni wajibu na ilikuwa inalipwa, Saumu ya Ramadhani ilikuwa inatekelezwa, Hija ya Makka inatekelezwa kila mwaka, maamrisho na makatazo ya dini yamefafanuliwa, Shariah tayari zilikuwa zimeagizwa. Sasa basi, kama sio tangazo kuhusu suala la Khalifa na Muandamizi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni ujumbe gani mwingine tena wa mbinguni ambao ulikuwa bado haujafikishwa ambao Allah bila mpenyo alimuamuru Mtukufu Mtume kuufikisha, bila ya kumpa hiari na kumruhusu kulicheleweshа, na mhimizo wenye ulazimishaji wa kuufikisha ambao takriban umekuwa kama tishio? Na kuhusu nini zaidi kuliko Ukhalifa, ambao katika kuufikisha Mtume (s.a.w.w.) alihofia fitina na vurughu, na kuhitaji msaada na ulinzi wa Mwenyezi Mungu dhidi ya madhara yoyote ambayo yanaweza kujitokeaza kutoka kwa watu?

[251] Kuna hadithi Sahih na mutawatir katika kumbukumbu zetu kutoka kwa Ahlul-Bayt (a.s.) zenye kuthibitisha kauli yetu kwamba aya hii ilishuka mwezi 18 Dhil-Hijjah hapo Ghadir Khum na riwaya hizo hazina shaka. Ambapo Bukhari anasema imeteremshwa siku ya Arafat, mwezi 9Dhil-Hijjah, lakini watu wa nyumba ya Mtume wanajua zaidi mambo yanayowahusu wao kuliko mtu wa nje.

[252] Sayyid Ahmad Zayni Duhlan, katika sura juu ya Hija ya Muago katika kitabu chake *Al-Sirah al-Nabawiyya* anaandika: "Kwa mujibu wa chanzo kimoja, kulikuwa na watu elfu tisini pamoja na Mtume (s.a.w.w.) wakati alipoondoka Madina, ambapo kwa mujibu wa kingine, walikuwa mia moja na ishirini elfu, ambapo wengine wanasema ni wengi zaidi ya hao. Hiyo ndio idada ya waliofuatana naye (s.a.w.w.) kutoka Madina. Wengine walijiunga naye humo njiani na hivyo idadi ya waliohiji pamoja naye ilikuwa ni kubwa zaidi ya hii." Hii inaashiria kwamba idadi ya walifika naye Ghadir walikuwa zaidi ya elfu mia moja, na wote walishuhudia Mtume akiitoa hadthi ya Ghadir.

[253] Tumenukuu hadithi hii katika kifungu cha 15 cha barua yetu ya 48, ambayo inastahili uchunguzi makini. Tafadhali rejea.

pokusanyika wote, aliongoza Swala za jamaa ya Dhuhr kisha akatoa khutba juu ya mimbari iliyotengenezwa kwa matandiko ya ngamia na kama alivyoamriwa na Allah, kwa uwazi kabisa akamtangaza Ali kuwa mrithi wake kama ilivyokwisha kuelezwa hapo kabla kwa kiasi fulani ambacho yapasa kikutosheleze. Na wale watu wote waliokuwa pamoja naye Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) pale siku ile waliisikia riwaya hiyo kutoka kwake na wakaondoka na taarifa hiyo, na wanakadiriwa kuwa zaidi ya mahujaji laki moja kutoka sehemu mbali mbali za nchi. Hivyo Hadith ya Ghadir, licha ya vikwazo na vizuizi vyote katika kuipokea imesimuliwa kwa wingi mfululizo, kwani sunna ya Allah Aza wa Jalla inayotawala vitendo vyote vya binadamu na ambayo haipatwi na mabadiliko yoyote inalazimu tukio hili liwe mutawatiri. Hata hivyo bado Maimamu wa Ahlul Bayt (as) walifuata njia zao wenyewe za kuineza na kuitangaza kwa busara kabisa.

Tukio moja tu katika Ukhalifa wa Amirul Muminin, Ali (as), linatosha kukuridhisha kuhusu kusimuliwa kwa wingi na utawatir wa hadithi hii. Wakati mmoja Ali (as) kuwakusanya watu kwa idadi kubwa katika uwanda wa Rahba. Kisha akawahutubia akisema: "Nasimamia kiapo kwa Jina la Allah kila Mwislamu aliyesikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akitoa tangazo katika Siku ya Ghadir asimame na ashuhudie kile alichosikia. Asisimame mtu yeyote isipokuwa wale tu waliomuona Mtume kwa macho yao na kumsikia kwa masikio yao." Masahaba thelethini, wakiwemo kumi na mbili miongoni mwao walioshiriki vita vya Badr, walisimama na kushuhudia kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliushika mkono wa Ali na akawauliza waliohudhuria: "Mnajua kwamba ninayo haki tangulizi na mamlaka makubwa juu ya waumini kuliko walivyo waumini wenyewe?" Walijibu kwa kukubali, 'Hakika ndivyo.' Mtume (s.a.w.w.), kisha akasema: "Kwa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* wake huyu (Ali) ni *mawla* wake; Ewe Mola! Kuwa rafiki kwa mwenye kuwa rafiki naye, na kuwa adui kwa mwenye kuwa adui naye." Unajua kwamba haikubaliki kimantiki kwamba masahaba thelethini walikubaliana kwa siri kusema uongo kwa pamoja. Ushuhuda wa hawa watu thelathini bila shaka unathibitisha kusimuliwa kwa mfululizo na kwa mutawatir.

Wale wote ambao walikuwepo pale Rahba waliisikia Hadithi hiyo kutoka kwa masahaba hao thelathini na wakati huo waliisambaza kwa watu wengine baada ya kutawanyika kwao, kwenye vijiji na miji mbalimbali, hivyo kuipatia utangazaji mpana mno. Yapasa ukumbuke kwamba tukio la Rahba lilitokea wakati wa Ukhalifa wa Amirul Muminin Ali (as) takriban miaka 25 baada ya Tangazo la Ghadir ambalo lilitokea wakati wa Hijja ya Kuaga, 10 A.H. kwani watu walichukua kiapo cha utii kwa Amirul-Mu'minin katika mwaka wa 35 A.H. alipokuwa mtawala aliyekubalika. Na ile robo karne iliyoingilia kati baina ya matukio haya mawili ilionekana kuwa na vita vingi vilivyopiganwa na utekaji nyara mwingi kufanyika, na ghasia na machafuko mengi yaliyoambatana wakati wa utawala wa makhalifa watatu wa mwanzo, na pia maangamizi ya ugonjwa wa tauni ya kuteketeza. Masahaba wengi wazee walikuwa wamefariki dunia, halikadhalika na vijana wengi wenye ghera walikufa katika medani za vita wakiwa na shauku kubwa ya kupata fadhila maalum za Mola Wao na Mtume Wake, (s.a.w.w.). Hivyo wengi kati ya wale waliofuatana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika hijja yake ya mwisho na wakashuhudia lile tangazo la Ghadir walikuwa hawapo tena duniani, na wale wachache waliokuwa wamebakia hai walitawanyika sehemu mbalimbali katika nchi tofauti. Na bado masahaba thelathini, ukiacha wanawake, na ukijumuisha masahaba kumi na mbili miongoni mwao walioshiriki vita vya Badr, ambao walikuwa pamoja na Amirul Muminin (a.s.) nchini Iraq walisimama na kutamka kwamba wao walimuona Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na walisikia hadithi ya Ghadir moja kwa moja kutoka kwake.

Kwa nyongeza ya hao mashahidi thelathini kulikuwa na masahaba wa kiume wengine ambao chuki yao na Amirul-Mu'minin iliwazuia kusimama na kushuhudia kama walioona kwa macho, kama vile Anas ibn Malik[254] na wengine ambao waliangukia chini ya laana ya Amirul Muminin (a.s.). Lau ingewezekana

[254] Wakati Imamu Ali (a.s.) alipomuambia Anas: "Kwa nini husimami pamoja na masahaba wengine na kushuhudia kile ulichosikia kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) siku ya Ghadiir?" Alijibu: "Ewe Amirul Mu'minin! Nimekuwa mzee, na sasa sikumbuki." Hapo Ali (a.s.) akasema:

kwa wale masahaba wote wanaume na wanawake walioshuhudia tukio la Ghadir ambao walikuwa hai wakati huo wakiishi sehemu mbalimbali kukusanyika pale Rahba, na Ali kuwahutubia kwa njia hiyo hiyo ambayo aliitumia, zaidi ya mashahidi thelathini wangeshuhudia. Na kama Ali angewataka kutoa ushahidi miaka ishirini kabla huko Hijaz, idadi ya mashahidi ingekuwa kubwa zaidi. Kama utaangalia kwa makini juu ya kadhia hii ya Rabha utaiona yenye uthibitisho wa nguvu ikithibitisha uwasilishaji wa mfululizo wa hadithi ya Ghadir.

Tukio hili la Rahba limeelezewa katika vitabu kadhaa vya hadithi. Imamu Ahmad bin Hanbal ameandika katika ukurasa wa 370, Jz. 4, ya *Musnad* yake hii hadith ya Ghadiir kama ilivyopokelewa kutoka kwa Zayd bin Arqam na kusimuliwa na Abul Tufail ambaye alisema: "Ali aliwakusanya watu katika uwanda wa Rahba, kisha akawaambia: 'Nakuapisheni kwa Jina la Allah kila Mwislamu ambaye alisikia lile tangaza ambalo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alilitoa katika Siku ya Ghadir asimame na ashuhudie kile alichokisema Mtume (s.a.w.w.).'" Hapo watu thelathini walisimama, na kwa mujibu wa Hafidh Abu Na'iim, watu wengi walisimama na kutoa ushahidi kwamba Mtume (s.a.w.w.) aliushika mkono wa Ali na akawauliza watu: 'Je, mnajua kwamba ninayo mamlaka zaidi juu ya waumini kuliko waumini wenyewe?' Walijibu: 'Ndio tunajua, Ewe Mjumbe wa Allah!' Kisha akasema: 'Huyu Ali anayo mamlaka makubwa juu ya maisha ya wale ambao wanaamini kwamba mimi nina mamlaka makubwa juu maisha yao; Ewe Mola! Mpende yeyote yule anayempenda Ali na mchukie yeyote yule anayemchukia.'" Abu Tufail anasema kwamba ilikuwa ni katika hali ya mkorogo wa akili hivyo aliondoka kwenye lile bonde la Rahba, kwani umma ule wa Waislam haukutekeleza maagizo ya hadithi hii. Kwa hiyo alikutana na Zayd ibn Arqam na akamuambia kile alichokisikia kutoka kwa Ali (a.s.), Zayd akamtaka asitilie shaka hilo kwani yeye mwenyewe alimsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akiitoa hadithi hiyo.

Kama ukiongeza ushuhuda wa Zayd ibn Arqam mbele ya Abu Tufail, kwenye ushuhuda wa Masahaba thelethini wa Rahba, na maelezo ya Ali katika siku ya Rahba, idadi ya Masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walioshuhudia kwa macho yao hadthi hii ya Ghadiir itapanda na kuwa thelathini na mbili. Imam Ahmad ameiandika katika ukurasa wa 119, Jz. 1, ya *Musnad* yake hadithi kama ilivyosimuliwa na Abdul Rahman ibn Abu Layla ambaye anasema alimshuhudia Ali kule Rabha akiwaapisha watu kwenye uwanda wa Rahba. Nawaapiza wale tu ambao Wallahi walimsikia Mtume (s.a.w.w.) mnamo siku ya Ghadir akisema: "Ali ni Maula wa yule ambaye mimi ni Maula wake,' wasimame na kutoa ushahidi. Wale ambao sio mashahidi wa kuona hawana lazima ya kusimama." Abdul Rahman anaongeza: "Hapo masahaba kumi na mbili ambao walishiriki vita vya Badr walisimama. Tukio hilo bado nalikumbuka vizuri sana. Walisema: "Tunashuhudia kwamba tulimsikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pale Ghadir akisema; 'Je, mimi sina mamlaka makubwa juu ya maisha ya waumini kuliko waumini wenyewe, na wake zangu sio mama zao?'" Wakajibu: "Ndio, hakika, Ewe Mjumbe wa Allah!" Kisha akasema: "Ali ni Maula wa yule ambaye mimi ni Maula wake; Ewe Allah! Mpende mwenye kumpenda na mchukie mwenye kumchukia!"

Mwishoni mwa ukurasa huo huo Imam Ahmad imeandika hadithi nyingine ya ushahidi huo ambayo kulingana nayo Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Ewe Mola! Mpende anayempenda na mchukie yule anayemchukia; msaidie yeyote yule anayemsaidia, na mtelekeze yule anayemtelekeza." Na kwamba mashahidi wote walisimama na kuthibitisha isipokuwa watatu ambao walikuwa chini ya laana ya Ali. Kama utamuongeza Ali na Zayd ibn Arqam kwenye mashahidi kumi na mbili, basi idadi ya mashahidi wa kuona katika tukio la Rahba, ambao walishiriki katika vita vya Badr itafikia kumi na wanne.

---

"Kama unasema uwongo, basi Allah akuweke alama ya baka jeupe lisilofichika (la ukoma) kwa kilemba chako." Kabla hajanyanyuka pale alipoketi uso wake ulipata baka kubwa. Baada ya hapo mara kwa mara Anas alikuwa akisema: "Niko chini ya laana ya Mtumishi wa Haki wa Allah." Imam ibn Qutaibah Dainuur ameliandika tukio hili katika maelezo juu ya Anas miongoni mwa walemavu katika uk. 14 wa al-Ma'arif yake. Imamu Ahmad ibn Hanbal amethibitisha tukio hili katika uk.119, Jz. 1, ya *Musnad* yake, ambamo anasema: "Wote walisimama kushuhudia isipokuwa watu watatu, ambao wote waliathiriwa na laana hii ya Imam Ali (a.s.)."

Na kama utazingatia riwaya chungu nzima kuhusiana na tukio la Rahba kama zilivyo kwenye vitabu vya hadith na maandiko kadhaa, huwezi kukwepa kukubali hekima iliyoko nyuma ya hoja hii kwa utangazaji na uenezaji mkubwa iwezekanavyo wa Amirul-Mu'minin wa hadithi hii ili kwamba kila mtu aweze kuitambua haki yake ya kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Bwana wa mashahidi, Abu Abdullah Husein (as) ametumia tukio sawa na lile la Rahba wakati wa utawala wa Mu'awiyah wakati ambapo kwa mara nyingine tena ukweli ulikuja kujulikana kwa mapana kabisa. Ilikuwa ni katika viwanja vya Arafah wakati wa msimu wa hijja, ambapo Husein (a.s.), alihutubia akiwa amezungukwa na maelfu ya mahujaji hotuba ambayo haina kifani katika fasaha yake. Alimsifu babu yake, baba yake, mama yake na kaka yake. Hakuna sikio ambalo kamwe limesikia khutba ya mpangilio na fasaha kama hiyo, hakuna jicho ambalo limeshuhudia uwasilishaji kama huo na hakuna moyo ambao uliguswa na kung'arishwa na khutba kwa kiasi kama hicho. Khutba yake ilisikilizwa kwa mazingatio na kufuatiliwa kwa makini sana na kubakia kwenye kumbukumbu za vichwani, ambayo ilikumbusha tena umma lile tukio la Ghadir. Hii ilikuwa ni hatua ya busara na kubwa katika ulinganiaji na uenezaji wa hadithi ya Ghadir kwa mapana.

Maimam tisa wa dhuria yake Imamu Husein, walichukua hatua mbalimbali lakini zilizojaa hikma za hali ya juu katika kuendeleza kutangaza na kueneza hadithi hiyo hiyo na wakaipa muundo unaotambulika kwa kawaida kabisa. Waliitumia siku ya mwezi kumi na nane Dhul-Hijjah kila mwaka kama siku ya sherehe kubwa maalum kwa ajili ya kula na kufurahia na kupongezana wenyewe kwa wenyewe, wakiomba radhi zaidi kwa Allah Aza wa Jalla, kwa swala za ziada na kufunga, wakisoma kaswida na marsia za kimapokezi na du'a na maombi kwa Mwenyezi Mungu, na kutenda huruma na ukarimu wa ziada katika kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwaneemesha na Siku ambayo Amirul Muminin Ali (a.s.) alitangazwa kuwa mrithi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kuteuliwa kuwa Imamu wa umma wa Kiislam. Katika siku hii walizoea kutoa zawadi kwa ndugu zao na marafiki, kuzipa familia zao na watu wa nyumbani mwao mambo ya kuwafurahisha. Kuwatembelea jamaa na marafiki zao na kukidhi haja za majirani zao, na kuwaagiza wafuasi wao na marafiki kusherehekea siku hiyo hali kadhalika.

Kwa sababu hii, siku ya mwezi kumi na nane Dhul Hijjah ya kila mwaka imekuwa ikisherehekewa na Mashia kama sikukuu kwa kila zama na kwa kila hali.[255] Katika siku hii, huwa wanaswali Swala za wajibu na za sunna katika misikiti yao, na kusoma Qur'ani Tukufu, na kusoma nyuradi za kimapokezi na dua mashuhuri zaidi kama tendo la shukurani kwa Allah Aza wa Jalla kwa kukamilisha dini Yake na kukamilisha neema Yake juu yao kwa kumteua Amirul Muminin (a.s.) kama Imamu [katika masuala ya dini na halikadhalika masuala ya kidunia]. Ndio hapo tena wanatembeleana na kwa furaha huombeana kheri, wakitafuta radhi za ziada kwa Allah kwa kufanya matendo mema na ukarimu wa ziada, kwa kuwaridhisha jamaa na jirani zao. Katika siku hiyo kila mwaka wanatembelea kuba la Amirul Muminin (a.s.), ambako mamia ya maelfu ya Mashi'ah hufanya ziara wakitokea kila sehemu ulimwenguni. Huko, humuabudu Allah katika siku hiyo kwa njia ileile waliyoitumia Maimamu wao watoharifu kumuabudu Allah kwa kufunga, kuswali wakitafuta kufutiwa madhambi na Allah. Wanaomba kuwa karibu na Allah kwa kufanya matendo mema na kutoa sadaka kwa ukarimu sana. Hawarejei mpaka wang'ang'anie kuba hilo tukufu na kusoma hotuba za du'a na maombi za kimapokezi zilizopendekezwa na kuandikwa na baadhi ya Maimamu wao.

Husimulia mazingira ya Shahada ya Amirul Muminin, matendo yake mashuhuri na vipaumbele vyake, juhudi zake kubwa katika kuimarisha misingi ya kanuni za dini, huduma yake ya kipekee na stahilifu kwa

[255] Wakati Ibn al-Athir anasimulia matukio muhimu yaliyotokea mwaka 352 A.H. katika kitabu chake *Kamil*, anasema yafuatayo katika ukurasa 181, Jz. 8, ya kitabu chake *Taarikh al-Kamil* kwamba katika mwezi kumi na nane Dhul Hijjah (mfunguo tatu) wa mwaka huo, Mu'izz ud-Dawla aliamuru mji wa Baghdadi upambwe na kung'arishwa. Kulikuwa na burudani za kila namna. Maduka na masoko yalifunguliwa wakati wa usiku kama ilivyo kawaida wakati wa usiku wa sikukuu za Iddi. Mienge iliwashwa, ngoma zilipigwa na matarumbeta yalipulizwa, yote haya kwa ajili ya kusheherekea Idd-ul-Ghadir, siku ya kumbukumbu.

Bwana wa Mitume na Wajumbe (s.a.w.w.), na nemsi na haki zake maalum, miongoni mwazo ikiwa ni pamoja na kuteuliwa kwake na Mtume (s.a.w.w.) kama mrithi wake, na tangazo la Siku ya Ghadir kama mwandamizi wake. Hii imekuwa ni sura ya desturi ya Mashia ya kila mwaka. Makhatibu wao kila mahali, tangu lilipotolewa tangazo la Ghadir na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wamekuwa kila ifikapo siku hii wakirejea kuwahutubia waumini wenzao yale mazingira ya tangazo hilo, wakielezea athari na matokeo yake wakinukuu rejea za kihistoria na kutoa hoja za kimantiki. Kadhalika washairi wao wa zamani na wa sasa wamezoea kutunga mashairi ya ukumbusho wa tangazo la Ghadir wakisifia ubora na sifa za Ali na huduma zake zenye thamani kubwa kwa Mtukufu Mtume wa Uislam (s.a.w.w.).[256]

Kwa hiyo, hapawezi kuwa na sababu ya kuwa na mashaka kuhusu kusimuliwa kwake kwa mfululizo kutoka kwenye vyanzo vya Ahlul Bayt (as), na Shi'ah wao wanaichukulia kuwa yenye umuhimu wa juu kabisa na ambao wamekuwa makini sana katika kuyahifadhi matini ya asili ya riwaya hiyo, na wamefanya juhudi kubwa za kuitangaza na kuisambaza kwa mapana kiasi iwezekanavyo. Kama utachukua usumbufu wa kurejea kwenye vitabu vinne vya mapokezi na halikadhalika rejea sahihi nyingine za Shi'a, usimuliaji *mutawatir* wa hadithi hii, kwa mujibu wa vyanzo vya Shi'ah, utakuwa dhahiri kama mwanga wa mchana.

Kama kanuni ya kawaida inavyohukumu, hadithi hii imesimuliwa kwa mfululizo kupitia vyanzo vya Sunni vilevile kama ulivyosikia tayari; "**Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini ya sawasawa, lakini watu wengi hawajui.." (Qur'ani 30:30).** Mkusanyaji wa *Al-Fatawa al-Hamidiyya,* licha ya Usunni wake halisi, anakubali usimuliaji wa mfululizo wa hadithi katika mukhtasari wa tasnifu yake iitwayo *Al-Salawat al-Fakhira fil Ahadith ul-Mutawatirah*. Na Suyyuti na wanachuoni wengine wa tafsir kama yeye, wote wameihifadhi hadithi hiyo na wameieleza kwamba imesimuliwa kwa tawatiri. Mbali na yeye, Muhammad ibn Jariir Tabari, mwandishi mashuhuri wa vitabu vya *"Tafsir"* na *"Tarikh,"* na Ahmad ibn Muhammad ibn Sa'id ibn Aqdah, Muhammad ibn Ahmad ibn Uthman al-Dhahabi, wote wameiona hadithi hii ya Ghadir kuwa ya muhimu sana kiasi kwamba kila mmoja ameandika kitabu kizima juu ya hadithi hii pekee na wamekusanya matini mbalimbali za hadithi hii na wameorodhesha vyanzo vyake vyote humo. Ibn Jarir ameandika katika kitabu chake hadithi hiyo kama ilivyopokelewa kupitia vyanzo sabini na tano tofauti na ibn Aqdah kama ilivyopokelewa na vyanzo mia moja na tano.[257]

Allamah Al-Dhahabi, licha ya kuwa mwenye imani halisi ya Sunni, ameshuhudia au kuthibitisha ukweli wa vyanzo vyake vingi.[258] Katika sura ya kumi na sita ya *Ghayat al-Maram* kuna kiasi cha hadithi themanini na tisa zilizosimuliwa kupitia vyanzo vya Sunni ambazo zote zinalitaja tukio la kumbukumbu la Ghadir nazo ni kwa nyongeza ya zile zilizoandikwa na Tirmidhiy, an-Nasai, Tabraniy, al-Bazzar, Abu Ya'li, na wandishi wengine wengi wa hadithi. Suyyuti ananukuu hadith hii wakati anamjadili Ali katika kitabu chake *Tarikh al-Khulafa* iliyowasilishwa na Tirmidhiy, akiongeza: "Hadith hii vilevile imeandikwa na Ahmad kama ilivyosimuliwa na Ali (a.s.), Abu Ayyub al-Answari, Zayd ibn Arqam, Umar na Dhiimar,[259] na Abu Ya'li anainukuu kutoka kwa Abu Hurayrah, na Tabraniy kutoka kwa Ibn Umar na

---

[256] Tumenukuu kwa mshairi maarufu, Al-Kumail ibn Zayd baadhi ya m ashairi yake, katika mojawapo alisema: "Siku ya dawh, siku ya dawh ya Ghadir, Ukhalifa ulidhihirishwa kwa ajili yake; Wallahi kama wangelitii tangazo hilo!" Mshairi mwingine maarufu, Abu Tamam katika moja ya mashairi yake anasema: "Mnamo Siku ya Ghadir haki ilidhihiri wazi, na iligeukia kwa mwenye kustahiki katika uwanda huo bila pazia wa kifuniko."

[257] Mwandishi wa *Ghayat al-Maram* anasema karibu na mwisho wa Sura ya 16 ukurasa wa 89 wa kitabu chake: "Ibn Jarir ameinukuu hadithi ya Ghadir kama ilivyopokelewa kwenye vyanzo 95 katika kitabu ambacho amekitoa kwa ajili ya suala hili, akakiita *Al-Wilayat*, na Ibn Aqdah ameinukuu kutoka kwenye vyanzo mia moja na tano katika kitabu chake ambacho vilevile naye amekitoa kwa ajili ya suala hili tu. Imamu Ahmad ibn Muhammad ibn al-Siddiq al-Maghribi ameeleza kwamba wote al-Dhahabi na Aqdah wametoa vitabu maalumu kwa ajili ya hadithi hii pekee." Hivyo, rejea kwenye kitabu maarufu kiitwacho *Fath al-Mulk al Ali Bi shat e Hadiith e Babi Madinat ul- Ilm Ibn Ali.*

[258] Ibn Hajar Amelieleza hili katika sehemu ya 5 Sura ya 1, ya *Sawa'iq* yake.

[259] Sina budi kuonyesha kwamba ameisimulia pia katika uk. 131, Jz. 1 ya *Musnad* yake kama ilivyosimuliwa na ibn Abbas na kisha katika

Malik ibn Hawairas, Habash bin Janada, Jariir, Sa'ad ibn Waqqas, Abi Sa'iid al-Khudri na Anas; na Bazar ameiandika kama ilivyosimuliwa na Ibn Abbas na Buraydah."

Miongoni mwa ushahidi mwingine wa uenezwaji mpana wa hadithi hii ni hadithi iliyosimuliwa na Imamu Ahmad katika *Musnad* yake kutoka kwa Riyah ibn al-Harith kama ilivyopokelewa na vyanzo viwili. Anaeleza kwamba kikundi cha Waislam wakati fulani walikuja kwa Ali (a.s.) na wakamsalimia: "Amani iwe juu yako, ewe *Mawla* wetu." Imamu akawauliza wao ni kina nani, walimjibu: "Sisi ni wategemezi wako, ni watumishi wako, ewe Amirul-Mu'minin." Imamu akawauliza: "Mimi nawezaje kuwa *mawla* wenu, ninyi Waarabu?" Wakasema: "Tulimsikia Mjumbe wa Allah, (s.a.w.w.), Siku ya Ghadir akisema: 'Kwa yule ambaye mimi ni mawla wake, na huyu Ali ni mawla wake.'" Riyah anasema kwamba wakati walipoondoka, aliwafuatilia na akaulizia wao walikuwa ni kina nani, akajulishwa kwamba walikuwa ni baadhi ya Answari wa Madina na kwamba Abu Ayyub al-Answari alikuwa ni mmoja wao."

Miongoni mwa thibitisho zingine za kusimuliwa mfululizo na mutawatir kwa hadith ya Ghadir ni riwaya ya Abu Is'haq al-Thalabi wakati anaelezea Surat al-Ma'arij katika kitabu chake cha Tafsir, akitegemea juu ya vyanzo viwili vyenye kuheshimika mno, kwamba katika Siku ile ya Ghadir, Mtume wa Allah (s.a.w.w.), aliagiza kupitia wapigambiu, watu wakusanyike. Walipokwisha kukusanyika kisha akauchukua mkono wa Ali na akasema: "Ali ni *mawla* wa yule ambaye mimi ni *mawla* wake." Habari za tangazo hili zilisambaa haraka katika maeneo ya mijini na vijijini kote. Pale Harith bin Nu'man al-Fahri alipopata kuifahamu habairi hii, alimpakia ngamia wake, akaenda Madina kukutana na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Huku akimkalisha ngamia wake na akashuka, alisogelea kwa Mtume na akasema: "Ewe Muhammad! Umetuamrisha sisi kushuhudia kwamba hakuna mola isipokuwa Allah na kwamba wewe ni Mjumbe wa Allah, na tumetii; kisha ukatuamrisha kuswali swala tano kwa siku, na tukakubali; kisha ukatuamrisha kutoa Zaka, na tukakubali; kisha ukatuamrisha kufunga mwezi wa Ramadhani na tukakubali; kisha ukatuamrisha sisi kuhiji Makka na tukakubali; kisha, kana kwamba yote haya hayatoshi, umemnyanyua binamu yako kwa mkono wako na kumuweka juu yetu sisi kama bwana wetu kwa kusema: 'Ali ni *mawla* wa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* wake;' je, hili latokana na amri yako wewe mwenyewe, au ni amri ya Allah?'" Yeye Mtume (s.a.w.w.) akajibu: "Naapa kwa Yule Mmoja na Mungu wa Pekee kwamba hii ni amri ya Allah, Aza wa Jallah." Kuyasikia hayo al-Harith aliondoka akielekea aliko ngamia wake huku akinung'unika taratibu mwenyewe: "Ewe Mola! Kama Muhammad (s.a.w.w.) anayosema ni kweli, basi turushie jiwe kutoka angani na itushukie adhabu kali na mateso." Hakudiriki kumfikia mnyama wake ambapo Allah aliye mbali na kila aina ya mapungufu alimrushia jiwe kupiga kichwa chake, likapenya mwilini mwake na kutoka kwenye utupu wake wa nyuma, na kumuacha akiwa amekufa pale pale. Ilikuwa ni katika tukio hili ambapo Allah Aza wa Jallah aliteremsha aya tatu za mwanzo za sura ya 70, Surat Ma'arij zifuatazo:

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ لِلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُ دَافِعٌ مِنَ اللَّهِ ذِي الْمَعَارِجِ

**"Mwenye kutaka alitaka adhabu itakayotokea. Kwa makafiri, hapana awezaye kuizuia. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye daraja.** (Qur'ani, 70:1-3)[260]

uk. 281 wa Jz. 4 ya *Musnad* yake kama ilivyopokelewa kutoka kwa Bara'a ibn Aazib.

260 vmHii imenukuliwa na kutoka al-Tha'labi na kikundi cha wanachuo wa Sunni wenye kuheshimika kama vile Allammah al-Shiblanji wa Misr katika wasifu wa Ali kwenye kitabu chake *Nurul Absar*; hivyo, unaweza kurejea kwenye ukurasa wa 11 wa kitabu hicho ukipenda.

Hivi ndivyo hadith hii ilivyonukuliwa kwa maneno yake haswa na al-Tha'labi.[261] Wanachuoni wengi wa Sunni wameiweka hadithi hii katika kundi moja na zile riwaya. zinazokubaliwa Usahihi wake na kujulikana kwa wote. Wassalaam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[261] Rejea kwenye kile ambacho al-Halabi amekinukuu kuhusiana na Hijja ya Muago katika kitabu chake cha wasifu cha *Al-Sira al-Halabiyya* na utaiona hadithi hii mwishoni mwa ukurasa wa 214, Jz. 3.

# BARUA YA 57

## MUHARRAM 25, 1330 A.H.

**I. Tafsiri ya Hadith Al-Ghadir,**

**II. Uwezekano wa Ukweli wa Tafsiri hiyo.**

Kuamini kwetu kwamba masahaba walikuwa katika upande sahihi kunatulazimisha kuitafsiri hadith al-Ghadir kwa namna tofauti kabisa, ama iwe imesimuliwa kwa mfululizo au vinginevyo. Kwa sababu hii, Sunni wanasema kwamba "*mawla*" imetumika katika maana mbali mbali na imetokeza katika sehemu moja ndani ya Qur'ani Tukufu ikiwa na maana ya "mwenye kustahiki," au "mwenye kufaa" kama ambavyo Allah Aza wa Jallah anasema wakati anawazungumzia makafiri: **"Makazi yenu ni ya motoni; ndio bora kwenu,"** ikimaanisha: "panapokufaeni zaidi," na mahali pengine kwa maana ya: "Mlinzi" au "Msaidizi," kama katika maneno ya Allah aliyetukuka Jina Lake, anasema: **"Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa walioamini, na makafiri hawana mlinzi." (47:1(1)** au katika maana ya: "Mrithi," kama katika kauli ya Allah Aza wa Jallah: **"Kwa kila mmoja tumemuwekea warithi wa yale waliyoyaacha wazazi na jamaa (zake)," (4:33),** au katika maana ya "kundi" au "chama" kama katika aya ifuatayo ya Allah Aza wa Jallah: **"Na hakika mimi nawahofia jamaa zangu baada yangu," (19:5)** au katika maana ya "rafiki," kama aya hii inavyodokeza: **"Siku ambayo rafiki hatamfaa rafiki kwa chochote, wala hawatasaidiwa." (44:4(1),** au katika maana ya mlezi, mtu ambaye ana haki ya juu zaidi ya kushughulikia masuala ya mtu mwingine wa chini yake, kama tunavyoweza kusema: "Bwana fulani ni mlezi wa fulani (mdogo)," na vilevile katika maana ya "msaidizi" na "Mpendwa." Kwa hiyo Ahlus-Sunnat wanasema: "Maana haswa ya hadith hii yaweza kuwa kwamba Ali alikuwa 'msaidizi' ama 'rafiki' kwa yule ambaye Mtukufu Mtume alikuwa msaidizi wake. Kama tukishikamana na maana hii ya hadith ya Ghadir tunaweza kudumisha sifa na heshima waliyoifaidi wahenga wazuri, na pia kuokoa uimamu wa makhalifa watatu wa kwanza waongofu, Allah awe radhi nao wote.

Kadhia iliyosimuliwa hapa chini inaunga mkono kwenye tafsiri hii ya riwaya hii. Baadhi ya wale Waislam ambao waliandamana na Imam Ali kwenda Yemen waliona utendaji wake kwao ulikuwa mkali mno. Waliporejea Madina walimlalamikia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) juu ya hilo. Hili lilimfanya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amsifie Imam Ali na kufanya maandalizi yote hapo Ghadir na kuzama kwa kirefu kiasi juu ya sifa na ubora wake ili watu waweze kutambua cheo chake kitukufu na kuheshimika kwake na pia kumuondolea na kuwakatisha tamaa maadui zake. Hii ndio maana Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika hotuba yake alisisitiza sana juu ya ubora wake Ali (a.s.) kwa umakhsusia na akasema: "Ali ni rafiki au msaidizi wa yule ambaye mimi ni msaidizi na rafiki yake," na wa Ahlul-Bayt (a.s.) kwa jumla aliposema: "Ninawaachieni nyuma yangu vizito viwili vyenye thamani – Kitabu cha Allah na kizazi changu, Ahlul Bayt wangu;" Hotuba hii, yaani hadith hii kwa hiyo ilikuwa katika namna ya wosia kwa umma hususan kwamba lazima uwe na mahusiano mema na Ali (a.s.) kwa ajili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na uhusiano mzuri wa kawaida kwa ajili ya Ahlul-Bayt wake kwa ujumla. Na kwa hiyo Ahlus-Sunnah wanadai kwamba hadithi ya Ghadir haikuwa ni tangazo la urithi na hivyo sio hoja ya kuunga mkono Uimamu wa jumla wa Ali (a.s.). Wassalaam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 58

## MUHARRAM 27, 1330 A.H.

**I. Hadith ya Ghadir Haikubali Tafsri Nyingine.**

**II. Uwezekano wa Tafsiri Tofauti ni Maongezi Yasiyo na Mpango Maalum na ni ya Upotoshaji kwa Hakika.**

Nina hakika kwamba haujaridhika moyo wako bado na kile ambacho wewe mwenyewe umekielezea, na hivyo hata akili yako bado haiko tayari kukubali tafsiri uliyopendekeza wewe mwenyewe! Unaamini katika hekima kamilifu, uma'sumu usio na shaka na utume wa mwisho wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kwamba alikuwa kiongozi wa wenye hekima wote, na kamilisho la mitume:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ {4} عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ

**"Hasemi kwa matamanio yake; si kingine bali ni ufunuo uliofunuliwa; amefundishwa na Mmoja Mwenye nguvu zote."** (Qur'ani, 53:3-5)**.**

Chukulia kwamba mwanafalsafa asiyekuwa Mwislam anakuuliza wewe: "Kwa nini Mtume (s.a.w.w.) katika Siku ya Ghadir awasimamishe mamia ya maelfu yote yale ya mahujaji wanaorejea kutoka Makkah? Kwa nini akawazuia kwenye joto kali la jua la mchana? Kwanini akawaita waliotangulia, na kuwasubiri wale waliochelewa nyuma? Kwa nini aliwaamuru kuweka kituo cha safari yao kwenye sehemu ya wazi kwenye uwanda ambako hakuna maji wala hakuna hata kijani kisha awahutubie kama alivyoagizwa na Mwenyezi Mungu katika sehemu zinapogawanyika njia kuelekea maeneo mbalimbali na kuwaagiza kuufikisha ujumbe kwa wale ambao hawakuwepo hapo. Na kwa nini, kama utangulizi wa khutba yake akazungumzia kuhusu kifo chake mwenyewe na hali ya muda ujao karibuni tu, pale aliposema: 'Nahisi kwamba hivi karibuni nitaitwa kwa Mola Wangu na nitaitikia mwito huo; na nitaulizwa na nyie halikadhalika mtaulizwa.' Na ni ujumbe gani muhimu ambao atakuja kuulizwa kuhusu ufikishwaji wake na ambao umma utaulizwa kuhusu utekelezwaji wake? Na kwa nini alisema: Je, ninyi hamshuhudii kwamba hakuna mungu isipokuwa Allah na kwamba Muhammad (s.a.w.w.) ni mja na Mjumbe wake, na kwamba Pepo ni haki, na Moto Wake ni haki, kwamba kifo ni haki na uhai baada ya kifo ni haki, na kwamba Siku ya Kiyama haina shaka inakuja, kwamba Allah atawafufua wote walioko makaburini?' Wao wakasema: " Ndio, tunayashuhudia yote hayo."

Kwa nini mara moja akauchukua mkono wa Ali, na kuunyanyua juu kabisa mpaka weupe kwenye kwapa ukaonekena, na kisha akasema: 'Enyi watu! Allah ndiye *Mawla* wangu, na mimi ni *Mawla* wa waumini.' Na alielezea maneno haya: 'Mimi ni maula wa waumini' kwa kusema, "mimi nina haki iliyotangulia na mamlaka makubwa zaidi juu ya maisha yao." Kisha kwa nini alisema, wakati akiwa amekwishatoa maelezo hayo: "Yeye huyu ni *mawla* wa yule ambaye mimi ni *mawla* wake;" au "ni walii wa yule ambaye mimi ni walii wake. Ee Mola! mpende mwenye kumpenda yeye na kuwa adui kwa yeyote yule anayekuwa adui na msaidie yeyote yule anayemsaidia na umkane yeyote yule anayemkana

yeye,?" na kwa nini alifanya makhususi kwa ajili ya Ali tu ile dua ambayo ilifaa tu kwa maimamu wa haki na warithi wa kweli? Na kwa nini alitaka washuhudie kwa kuwauliza: 'Je, mimi sina mamlaka zaidi juu yenu kuliko mliyonayo ninyi wenyewe?' na walijibu kwa kukubali; kisha akasema: "Ali ni *mawla* kwa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* wake,' au 'Kwa yeyote yule ambaye mimi ni *walii* wake, Ali ni *walii* wake,' na kwa nini aliweka muungano usiotenganishika baina ya Qur'ani na kizazi chake Ahlul-Bayt, na akavitangaza viwili hivyo kama viongozi wa kweli kwa waumini kufuata mpaka Siku ya Hukumu? Ilikuwa ni kwa nini ambacho huyu Aalim Adhiim, Mtukufu Mtume alikuwa na shauku kubwa nacho na akaweza kuchukua hatua za tahadhari ya hali ya juu, na mipango isiyo ya kawaida? Na ilikuwa ni kazi gani muhimu ambayo alikusudia kuikamilisha mbele ya mkusanyiko mkubwa kama huo? Ni ujumbe gani mkubwa ambao Allah Aza wa Jallah alimuagiza kwa masharti kabisa kuufikisha wakati aliposema:

يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۖ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ۚ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ
النَّاسِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ

**'Ewe Mjumbe! Fikisha kile ambacho kimeteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako, na kama hutafanya hivyo, basi utakuwa hukufikisha ujumbe Wake (kabisa), na Allah atakulinda kutokana na watu (waovu)** (Qur'ani 5:67).'

Na ni ujumbe gani huo wenye umuhimu wa haraka ya kufikishwa kiasi hicho ambao Allah alitoa maagizo yenye masharti makali mno na himizo la uwasilishaji ambao ulikuwa ni karibu na tishio? Ni maagizo gani ambayo kutangazwa kwake kumekuwa kama ni amri yenye tishio lenye hatari ya maasi ambalo lilihitaji ulinzi kutoka kwa Allah dhidi ya madhara kutoka kwa wanafiki?" Kama utaulizwa maswali yote haya, utayajibu kwa kusema kwamba lengo na himizo lenye shuruti la Allah Aza wa Jallah, na huo mpango usio wa kawaida na tahadhari za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilikuwa ni kwa ajili ya kutangaza kwamba Ali alikuwa msaidizi na rafiki wa Waislamu? Sifikirii hata chembe kama ungeweza kutoa jibu kama hilo. Na sidhani kwamba ungeweza kusema maneno kama hayo kuhusu Mtukufu Allah, au kuhusu bwana wa watakatifu wenye busara, na mwisho wa manabii na mitume. Nina hakika wewe uko mbali na kushikilia fikira kwamba makusudio yaliyokuwa nyuma ya mpango na tahadhari iliyochukuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kutuliza akili zake kwa makusudi hasa yalikuwa ni tangazo la jambo ambalo linafahamika vema na kutohitajia tangazo maalum na maelezo ya kile ambacho chenyewe kiko dhahiri na cha kueleweka kwa akili za kawaida. Sina shaka kwamba unaamini kwamba matendo na kauli za Mtume (s.a.w.w.) ziko mbali kabisa na kile ambacho watu wenye hisia za kawaida wanaweza kukichukia au kubeza na wenye hekima na wanafalsafa waweze kulaumu au kukosoa. Hakuna shaka yoyote kwamba unatambua kwamba kauli zake na matendo yake ni katika hekima na uhakika usiokosolewa.

**Allah Aza wa Jallah amesema:**

مُطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُونٍ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ

**"Kwamba hakika hii ni kauli ya Mjumbe mtukufu, mwenye nguvu na mwenye cheo kwa huyo Mwenye Kiti cha Enzi, anayetiiwa tena muaminifu, na wala huyo mwenzenu hana wazimu."** (Qur'ani, 81:19-22)**.**

Hivi tutaweka umuhimu sana kwenye ufafanuzi wa kile ambacho kilikuwa kiko wazi, au kuelezea juu ya kile ambacho kilikuwa dhahiri, na kufanya mipango isiyo ya kawaida na kuchukua tahadhari kubwa mno kwa ajili kutangaza jambo ambalo tayari lilikuwa dhahiri wazi kabisa. Hilo halina maana kabisa na haliwezekani. Allah na Mjumbe Wake wako mbali kabisa kuweza kuzungumza upuuzi na kufanya mambo madogo madogo yasiyo na umuhimu. Na wewe ambaye Allah amekujaalia kuwa na maamuzi sahihi unatambua vizuri kwamba lengo lake la muhimu katika maneno yake na vitendo katika siku ya Ghadir katika joto la jua kali la mchana, katika uwanda huo usio na maji, mbele ya mkusanyiko mkubwa wa mahujaji katika makutano ya njia panda halikuwa ni jingine zaidi ya kukamilisha kazi yake na uteuzi wa makamu wake baada yake. Dhahiri ya maneno yake na mantiki vyote vinaelekeza kwenye hitimisho lisilopingika la kwamba katika siku ile Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakukusudia chochote mawazoni mwake kuliko uteuzi wa Ali kama makamu wake wakati wa uhai wake na mrithi wake baada yake. Hadithi hii, pamoja na mapendekezo yake na maana zake, na tafsiri na maana za maneno yanayoungana nayo ni uthibitisho wa wazi wa ukhalifa wa Ali, na haikubali maana na ufafanuzi wa aina nyingine. Hadithi yenyewe iko wazi dhahiri kabisa kwa mtu ambaye **"Hakika katika hayo kuna ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye ni shahidi. (50:37)**

Uwezekano wa tafsiri tofauti uliyodokezea wewe ni mazungumzo yasiyo na utaratibu wala yenye kuhusika, yenye kuchanganya akili na kubadilisha mambo kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) alimtuma Ali kwenda Yemen sio mara moja bali mara mbili, mara ya kwanza ilikuwa mwaka wa 8 A.H. na ilikuwa ni wakati wa kurejea kutoka kwenye safari hii ambapo baadhi ya watu fitna waliokuwa wameandamana na Ali walilalamika kwa Mtume (s.a.w.w.) kuhusu tabia yake ya ukali, ambapo yalimchukiza sana mtume (tafadhali rejea barua yetu ya 36) kiasi kwamba dalili za hasira zilionekana kwenye uso wake; na baada ya hapo hakuna aliyethubutu kulalamika tena dhidi ya Ali (a.s.). Mara ya pili ilikuwa ni mwaka wa 10 A.H. ule wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipomkabidhi Ali bendera ya Uislam, na akamfunga kilemba kichwani mwake kwa mikono yake mwenyewe, na akamwambia: "Endelea na kazi yako tu bali usije kuzingatia jambo jingine lolote," na kwa utayari kabisa Ali (a.s.) akaanza kama alivyoelekezwa, na huko akaweza kumudu kusimamia mambo ya Mtume (s.a.w.w.) kwa mafanikio, kisha akarudi na kuungana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika hija ya kuaga ya Mtume (s.a.w.w.). Alimkaribisha kwa shangwe sana na Mtukufu Mtume na wengineo, na Mtume (s.a.w.w.) akamshirikisha pamoja naye katika kutoa dhabihu. Wakati huu hakuna fisadi yeyote au adui aliyetoa malalamiko au taarifa mbaya isiyofaa dhidi yake. Inawezaje kusemwa kwamba taarifa mbovu za fitna kutoka kwa maadui zake zilikuwa ndio sababu ya msingi ya kile Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alichokitangaza kuhusu Ali pale Ghadir Khum, au kwamba tangazo hilo lilikusudiwa kukanusha au kupinga malalamiko yoyote au taarifa potovu kama zilivyoeleweka vibaya?

Hata hivyo, upinzani tu kwa Ali hauwezi kuwa sababu tosha ya tahadhari hiyo na ulundikaji wa matandiko ya ngamia kama mimbari, na utoaji sifa tele zenye mkazo na msisitizo juu yake kuhusu Ali kutoka kwa Mtukufu Mtume katika Siku ya Ghadir. Ni wale tu wanaokubaliana na tafsiri hiyo uliyorejea, ndio wanaomchukulia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Allah aepushilie mbali, kwamba alikuwa na pupa na uzembe katika matendo na kauli yake mwenyewe, uchungu na maamuzi yake. Lakini ubora wake na akili yake komaavu iko mbali na hilo, kwani Allah Aza wa Jallah, anasema:

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ ۚ قَلِيلًا مَا تُؤْمِنُونَ وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ ۚ قَلِيلًا مَا تَذَكَّرُونَ
تَنْزِيلٌ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Ni kauli ya Mjumbe mtukufu; sio kauli ya mshairi; ni kuchache mno mnakoamini; wala sio kauli ya mwenda wazimu; ni kuchache mno mnako kumbuka; bali ni kauli kutoka kwa Mola wa walimwengu."**

(Qur'ani, 69:40-43)

Lau lingekuwa lengo lake ni kuwafanya watu watambue ubora na daraja za Ali, au kukanusha malalamiko yoyote dhidi yake, yeye (s.a.w.w.) angesema tu: "Huyu ni binamu yangu, mkwe wangu, baba wa kizazi changu, Mkuu wa watu wa nyumba yangu; kwa hiyo, msinichukize kwa utovu wa nidhamu wenu kwake," au mambo mengine kama hayo yenye kuelezea sifa zake na kuonyesha hadhi yake tukufu kabisa. Isitoshe, kutokana na maneno ya hadithi hii (hususan kwa mtazamo wa vidokezo vya kimantiki na kihistoria tulivyovitaja) halijitokezi akilini jambo jingine mbali na tuliyoyaeleza. Na kuingizwa kwa Ahlul-Bayt (a.s.) katika hadithi ya Ghadir kunatilia nguvu tu ile maana ya kile tulichokieleza, kwani ndani yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesisitiza uhusiano wa milele wa baina ya Ahlul-Bayt na Kitabu Kitukufu Qur'ani na akavipendekeza kwa Umma kama mifano ya kuigwa kwa ajili ya muongozo kwa kusema: "Nakuachieni miongoni mwenu vitu viwili, ambavyo kama mtashikamana navyo, kamwe hamtapotea: Kitabu cha Allah na kizazi changu, watu wa nyumbani kwangu."

Alifanya hivyo ili umma uweze kutambua kwamba hauna kimbilio lolote kwao baada ya Mtume isipokuwa viwili hivi, na kwamba hapakuwa na mwingine wa kutegemewa kwa ajili ya mwongozo baada ya Mtukufu Mtume mbali na Qur'ani na Ahlul-Bayt. Unaweza kuamua juu ya hali ya umuhimu na wajibu wa utii kwa Maimam katika kizazi chake kitukufu kwa ule ukweli kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwatangaza kwamba wameunganishwa milele na Kitabu cha Allah ambacho hakiwezi kufikiwa na batili kutoka mbele wala nyuma. Kama vile tu ambavyo haiwezekani kurejea kwenye kitabu kingine mbali na Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na aliye mbali na mapungufu yote, halikadhalika hairuhusiwi kumfuata Imamu mwingine yoyote mbali na Maimamu watokanao na kizazi chake (s.a.w.w. ) kitoharifu (a.s.).

Na katika maneno yake Mtume (s.a.w.w.), "Viwili hivi havitafika mwisho" au "Kamwe viwili hivyo havitatengana mpaka vitakaponifikia kwenye Birika (la Kauthara);" ni uthibitisho wa wazi kwamba ardhi kamwe haitakuwepo bila kuwa na Imamu kutokana na kizazi chake ambaye atadumisha lile fungamano. Kama utaichunguza kwa makini hadithi hii utakuja kujua kwamba urithi wa Mtume au ukhalifa umethibitika kwa Maimamu kutoka kizazi kitoharifu cha Mtume (s.a.w.w.). Na hadithi iliyosimuliwa na Zayd ibn Thabit na kunukuliwa na Ahmad katika Musnad yake mwanzoni mwa ukurasa wa 122, Jz. 5 inaunga mkono hilo na inaeleza kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema:

"Ninakuachieni miongoni mwenu warithi wawili: Kitabu cha Allah, ambacho ni kamba iliyoning'inia kuanzia mbinguni mpaka aridhini, na watu wa nyumbani kwangu Ahlul-Bayt wangu. Na viwili hivyo kamwe havitatengana mpaka viungane nami katika Haudhi (ya kauthara)." Ni hoja madhubuti inayounga mkono urithi wa Maimam katika kizazi chake, amani juu yao wote. Na wewe unafahamu kwamba masharti juu ya utii kwa kizazi chake kama wajibu ni hoja isiyoweza kushambuliwa, kwamba utii kwa uongozi wa Ali ni wajibu, kwani yeye kwa hakika ndiye Mkuu wa kizazi chake na Imamu mwenye kutiiwa wa nyumba yake. Kwa hiyo, hadithi ya Ghadir na nyingine kama hizo zinazoagiza utii kwa kizazi

cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama ni wajibu, wakati huo huo zinathibitisha ile haki ya urithi ya Ali na utii kwake kuwa ni wajibu kama Mkuu wa Ahlul-Bayt ambao Allah na Mjumbe Wake walivyowapa hadhi ileile sawa na Qur'ani, ambapo kwa mujibu wa riwaya nyingine ambazo zinazungumzia shakhsia yake kubwa na sifa na ubora usio na mshindani zinathibitisha kwamba Ali alikuwa Walii yaani alikuwa bwana na kiongozi wa wale wote ambao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alikuwa Bwana na Mlezi wao. Wassalaam,

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 59

## MUHARRAM 28, 1330 A.H.

**I. Ukweli Wadhihiri,**

**II. Kukwepa.**

Kamwe sijaona mtu yeyote ambaye ana uwezo wa kujieleza kwa utulivu, uwazi wa kueleweka na kuendesha mjadala kielimu kabisa kama wewe. Sasa ukweli umedhihiri wenyewe kupitia dalili ulizoelezea na pazia la shaka limeondolewa kutoka kwenye sura ya uhakika. Kumebakia hakuna shaka tena kwamba maneno *"walii"* au *"mawla"* katika hadithi al-Ghadir yana maana ya "Mbora" au "Bwana" na wala sio msaidizi au rafiki au mambo kama hayo. Vinginevyo yule muombaji asingeomba adhabu iumizayo ya haraka kwa ajili ya makafiri. Ninakubali kwamba maelezo yako juu ya maneno "Walii" na "mawla" ni sahihi kabisa.

Laiti ungekubali tafsiri ya hadithi ya Ghadiir kwa namna ambavyo imetafsiriwa na kundi la maulamaa wasomi, kama Imamu Ibn Hajar katika kitabu chake *Al-Sawa'iq al-Muhiriqa*, na Halabi katika kitabu cha *Sirat* ambamo wanasema: "Tunakubali kwamba yeye Ali (a.s.) alikuwa na haki kubwa kwenye uimamu, lakini hii ilikusudiwa kwa baadae; lasivyo ingemaanisha kwamba alikuwa ni Imamu wakati wa uhai wa Mtume na hili sio sahihi na halikubaliki kabisa. Hivyo ilikusudiwa pale atakapokuja kuchaguliwa na watu kama mrithi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na sio kwa wakati wa Mtume (s.a.w.w.), hivyo hakuna kizuizi na madhara yeye kutanguliwa na wale makhalifa watatu wa kwanza, na kwa maana hii hadhi na heshima ya watangulizi wa haki, Mwenyezi Mungu Mtukufu awe radhi nao wote, itahifadhiwa.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 60

## MUHARRAM 30, 1330 A.H.

**Kukanusha Ukwepaji na Matumizi Mabaya.**

Mwenyezi Mungu akuongoze kwenye ukweli! Umetutaka tuwe tumeshawishika kutokana na hadithi al-Ghadir kwamba Ali alikuwa na haki ya juu zaidi kwa Uimamu kwa baadae kabisa wakati umma wa Waislamu walipomchagua na kula kiapo cha utii kwake kama hivyo, sio mara baada ya tangazo la Ghadir, au kwa maneno mengine, Ali alistahiki ubora au ubwana wakati wa baadae na sio hasa katika Siku ya Ghadir. Umependekeza tafsiri hii ili kwamba ule urithi wa ukhalifa wa maimamu watatu waliomtangulia uonekane kuwa haugongani na hadithi ya Ghadir kwa jina la kufuata taratibu, haki, Ukweli na Uadilifu, tafadhali tufafanulie tuelewe kwamba wewe mwenyewe utashikilia tafsiri ya Ibn Hajar na Halabi na kwamba hutayumba kwa hilo, ili nasi tufuate mwelekeo wa hoja yako na kuegemeza majadiliano zaidi juu ya tafsiri hiyo iliyotajwa. Je sasa utakubali hiyo kuhusishwa na wewe, ili tuweze kukubaliana na kufikia maelezo yanayokubaliana? Nadhani haielekei kabisa kwamba utathibitisha kukubaliana na hili. Najua kwa hakika kabisa kwamba wewe mwenyewe unashangazwa na tafsiri hii na unastaajabu kuhusu wale ambao ni watoaji wa tafsiri kama hiyo ambayo maneno ya hadithi hii hayapendekezi hivyo wala hayatokezi kabisa kwenye akili ya mtu katika kuyasikia, wala hayahusishwi na akili ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wala hayaafikiani na maneno yake yenye maamuzi makini, wala hayaendani na mpango angalifu na tahadhari na maneno mazito ya Siku ya Ghadir. Tafsir hiyo haiendani na ishara na uwezekano ambao tumeueleza hapo juu, wala na maana ya hadithi kama ambavyo ameielewa al-Harith ibn Nu'man al-Fihri, na kama ambavyo imedhihirishwa na Allah au ilivyokusudiwa na Mjumbe Wake (s.a.w.w.), halikadhalika na kueleweka kwa masahaba wote.

Zaidi ya hayo, maneno ya hadithi hii hayaashirii kwamba ubora wa Ali (as) haukuwa wa wakati huu bali wa wakati wa baadae, kwani katika hali kama hiyo Ali asingekuwa *mawla* wa makhalifa watatu wa mwanzo ama wa mwislamu yeyote ambaye alifariki wakati wa utawala wao, jambo ambalo ni kinyume kabisa na maagizo ya Mtume (s.a.w.w.) ambaye alisema: "Je, mimi sio mbora zaidi juu ya waumini kuliko walivyo kwa nafsi zao wenyewe?" na watu wakamjibu kwa kukubali; kisha yeye (s.a.w.w.) akasema: "Ali ni *mawla* kwa yeyote yule ambaye mimi ni *mawla* wake," yaani wa wafuasi wake wote bila kumbagua yoyote yule, na ndio sababu ya Abu Bakr na Umar baada ya kusikia tangazo hilo kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) siku ile ya Ghadir, wakamwambia Ali; "Ewe mtoto wa Abu Talib umekuwa maula wa kila muumini wa kiume na wa kike." Na haya yamesimuliwa na Darqutni kama yalivyoelezwa katika sehemu ya mwisho ya sura ya 1, Jz. 5 ya *Sawaiq al-Muhriqa* ya Ibn Hajar, tafadhali rejea ukurasa wa 26 humo. Riwaya nyingine nyingi zimesimuliwa kutoka kwenye chanzo hicho. Na Imam Ahmad amenukuu maneno ya Umar kama yalivyosimuliwa na Baraa bin Azib katika uk. 281, Jz. 4 ya Musnad wake kama tulivyoeleza katika barua yetu ya 54, wakisema hivi "Ewe mwana wa Abu Talib, sasa umekuwa bwana (*mawla)* wa waumini wote." [262] Hivyo wote wamebainisha kwamba Ali alikuwa bwana wa kila muumini mwanaume na mwanamke katika Siku hiyo ya Ghadir.

---

[262] Hadithi hii imenukuliwa na Da Qutni, kama ilvyoneshwa karibu na Kifungu cha 5, Sura ya kwanza, ya *Al-Saw'iq al-Muhriqa* cha Ibn Hajar, hovyo, rejea kwenye ukurasa wa 26. vilevile imesimuliwa na wasimuliaji wengi wa hadithi, kila mmoja kutoka kwenye chanzo chake mwenyewe, na katika vitabu vyao wenyewe vya hadithi. Ahmad amenukuu kitu kama hicho kutoka kwa Umar kilichosimuliwa na al-Bara ibn Azib katika ukurasa wa281, J. 4, ya kitabu chake cha Musnad, ambacho tayari tumeinukuu katika Barua yetu ya 54 hapo juu.

Wakati mmoja Umar aliulizwa; kama ilivyoelezwa katika *Dar Qutni* katika ukurasa wa 36 katika kitabu cha *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*: "Ni vipi mwenendo wako kwa Ali unaonekana kuwa tofauti kabisa na ule wa kwa masahaba wengine wa Mtume (s.a.w.w.)." Umar alijibu kwa kusema: "Yeye ni *mawla* wangu," Huku ni kukiri kwa dhahiri kwamba Ali alikuwa bwana wake kwa wakati huo ingawa yeye (Ali) alikuwa bado hajachaguliwa kuwa Khalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wala hajapokea kiapo cha utii kutoka kwao. Hii inathibitisha kwamba Ali alikuwa ni *mawla* wake na *mawla* wa kila waumini wote, mwanaume na mwanamke tangu wakati huo wa Mtukufu Mtume, akamtangaza kama Mawla wake kulingana na amri ya Allah (s.a.w.w.), iliyoshuka katika Siku ya Ghadir.

Wakati mmoja mabedui wawili waliokuwa na ugomvi kati yao walifika kwa Umar kutaka uamuzi wake. Umar alimuomba Ali ahukumu katika kesi hiyo iliyoletwa mbele yake, hapo mmoja wao akauliza: "Huyu ni nani kutuamulia kati yetu?" Mara moja Umar alimrukia, akamkamata mtu yule shingoni na akamwambia: "Ole wako! Unajua mtu huyu ni nani? Yeye ni *mawla* wako na *mawla* wa waumini wote; na yeyote yule asiyemuamini kuwa ni *mawla* wake kwa hakika sio Mwislamu." Kuna ushahidi mwingi kutoka kwa waandishi wengi katika kuunga mkono maana hii ya hadithi hii. Na wewe ambaye Allah aza wa Jallah amekujaalia na uamuzi wa haki unajua kwamba lau kama falsafa ya Ibn Hajar ikikubalika na kufuatwa kuhusiana na hadithi ya Ghadir, basi mpango wote na tahadhari iliyochukuliwa na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) siku ile, itaonekana kuwa ni upuuzi na isiyo na malengo yoyote, Mwenyezi Mungu atuhifadhi! na ataonekana kuwa – tunaomba kinga kwa Allah dhidi ya kufikiria namna hiyo – aliyejisahau, mwenye kupayuka na kuweseseka katika maneno yake na matendo.

Kwa mujibu wa Ibn Hajar na Allamah Halabi, lengo zima, mpango na tahadhari ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika hali mbaya ile ya pale Ghadir ilikuwa ni kutoa tangazo tu kwamba watakapokuwa wamechaguliwa Ali kama khalifa wake na akapokea viapo vya utii kutoka kwao, ndipo atapokuwa mawla na bwana wao. Hata mtu zumbukuku ataicheka tafsiri kama hiyo. Haileti upambanuzi wowote kati ya Amirul-Mu'minin na wengine wote, na haimteui kama mwenye kuonekana zaidi katika hali yoyote miongoni mwa Waislamu wote, kwani mtu anapochaguliwa kwenye Uimam na viapo vya utii kwake vikapokelewa kutoka kwenye Umma basi atakuwa ndiye bwana na mlezi wa Umma huo kwa ubora wake, iwe ni Ali au sahaba mwingine yoyote wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), au hata Muislam asiyekuwa sahaba wa Mtume pia. Kama kulikuwa hakuna sifa maalum au haki yoyote ya kumtofautisha Ali na masahaba wengine waliobakia pamoja na Waislamu wengine wa mwanzoni kabisa, ni kitu gani basi alichokusudia Mtume (s.a.w.w.) pale kukitangaza kuhusu yeye katika Siku ile ya Ghadir baada ya mipango yote ile isiyo ya kawaida na tahadhari ya hali ya juu? Tafsiri hii inashindwa kulieleza hilo na kwa uhakika ni isiyo na maana yoyote kabisa.

Ibn Hajar na Halabi wanadai kwamba lau kama Ali akichukuliwa kama Mawla wa Umma tangu wakati wa tangazo la Ghadir, ingeelekeza kwenye hitimisho lisilokubalika la kwamba yeye alikuwa Imamu wakati wa uhai wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Huu ni upuuzaji wa ajabu sana na tafsiri mbaya ya mambo na upotoshaji usio na kifani. Wamejifanya kutokuwa na utambuzi wa mwenendo wa Mitume wote, makhalifa, wafalme na watawala wengine tangu zama za kale kabisa za kuamua kuhusu suala la urithi na utajaji wa wale watakaoshika nafasi zao baada yao wakati wa uhai wao. Wamejifanya kutojua maana ya hadithi: "Ewe Ali! Nafasi yako kwangu wewe ni kama ile ya Harun alivyokuwa kwa Musa isipokuwa hakutakuwa na mtume baada yangu," na kujifanya wasahaulifu wa hadithi ya onyo kwa ndugu zake wa karibu wakati alipowaonya akisema: "Kwa hiyo, msikilizeni [Ali] na mtiini," na riwaya nyingine nyingi zenye maana hii. Zaidi ya hayo hata kama tukichukulia kwamba Uimamu wa Ali wakati wa uhai wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), kuwa usiokubalika, basi ni muhimu kumkubali yeye kama Imam wa wote mara tu baada ya kufariki kwake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), bila ya mwanya wowote kwa kufuata

kanuni mashuhuri iliyowekwa na wasemaji na mafasaha wazuri kwamba inapokuwa ni vigumu au kutowezekana kuelewa neno katika maana yake ya asili, basi inapasa lieleweke kwa maana yake ya kilugha au ya kidesturi.

Na kuhusu heshima ya watangulizi wema, tafadhali baki na uhakika kwamba itabaki kama ilivyo salama hata bila ya tafsiri iliyotolewa na Ibn Hajar na Halabi kama tutakavyoeleza kama ikionekana kuwa ni muhimu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 61

## SAFAR 1, 1330 A.H.

**Maombi ya Riwaya Zilizosimuliwa na Vyanzo vya Shi'ah.**

Almradi heshima na hadhi ya wahenga waongovu inahifadhiwa bila ya tafsiri iliyotolewa na Ibn Hajar na Halabi na kadhalika, basi hakuna pingamizi lolote la kukubali tafsiri yako ya hadithi ya Ghadir na nyingine zote zinazomhusu hasa Imamu (as), na hakuna haja pia ya tafsiri nyingine tofauti.

Inawezekana pia kwamba kuna hadithi nyingine katika kumbukumbu zenu kuhusiana na suala hili ambazo kwamba hazimo kwenye elimu ya Ahlus-Sunnah. Hivyo, tutakushukuru sana kama utazisimulia ili kwamba tuweze kupata faida ya kuelemika nazo. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 62

## SAFAR 2, 1330 A.H.

**Hadithi Arobaini za Wazi Kabisa.**

Ndio, zipo katika kumbukumbu zetu hadithi nyingi za wazi kabisa ambazo kwamba hazijulikani kwa Ahlus-Sunnah. Hizi zimesimuliwa kwa mfululizo kupitia kwa jamaa wa kizazi kitoharifu cha Muhammad (s.a.w.w.), ambazo kwamba hapa tutakusimulia arobaini miongoni mwazo.[263]

(1) al-Saduq Muhammad ibn Ali ibn al-Husein ibn Babawayh al-Qummi amesimulia katika kitabu chake *Ikmal al-Din wa Itmam al-Naymat*, akinukuu vyanzo sahihi hadi kwa Abdul Rahman ibn Samrah, ambaye anasema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: "Ewe mwana wa Samarah! Kama malengo yakiwa mbalimbali na maoni yakigongana, basi, mfuate Ali ibn Abu Talib, kwani yeye ni Imamu wa Umma wangu na mrithi wangu juu yao baada yangu."

(2) Katika rejea hiyo hiyo, yaani *Ikmal*, al-Suduq anamnukuu Ibn Abbas akisimulia hadithi moja ambayo kwayo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), anasema: "Allah Mtoaji wa rehema na Mtukufu zaidi, alitupa jicho kwa wakazi wa ardhi na akanichagua mimi kutoka miongoni mwao kuwa Mtume, kisha alitupa jicho la pili na akamchagua Ali kama Imamu na akaniamrisha kumchukua kama ndugu na rafiki yangu, na kwamba nimteue kama mtekelezaji wa wasia wangu, *walii* na waziri."

(3) Vilevile al-Saduq katika *Ikmal*, kuna hadithi moja kutoka kwa Imamu as-Sadiq (as) ambaye yeye ameipokea kutoka kwa wahenga wake, kizazi baada ya kizazi, kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: "Malaika Jibril ameniambia kama alivyoelekezwa na Mola Mwenye uwezo, kwamba: 'Yeyote yule atakayetambua kwamba hakuna mungu isipokuwa Mimi, na kwamba Muhammad ni Mja na Mjumbe Wangu, na kwamba Ali ibn Abu Talib ni muwakilishi Wangu na kwamba Maimamu kutokana na kizazi chake ni Hoja Zangu (*Hujjat*), basi nitamfanya aingie Peponi kwa Rehema Yangu."

(4) Al-Saduq vile vile katika hiyo *Ikmal*, anasimulia hadithi nyingine yenye sanadi hadi kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) ambaye ameipokea kutoka kwa baba yake na baba yake ameipokea kutoka babu yake na kadhalika kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: "Maimamu baada yangu ni kumi na mbili: wa kwanza wao ni Ali na wa mwisho wao ni *al-Qaim* [al-Mahdi]; wote hao ni warithi wangu na watekelezaji wa wosia wangu."

(5) Katika kitabu hicho hicho *Ikmal*, as-Saduq amesimulia hadithi nyingine kupitia vyanzo mpaka kwa al-Asbagh ibn Nabatah ambaye anasema: "Siku moja Amirul-Mu'minina Ali ibn Abu Talib (as)

[263] Tumechagua idadi hii kwa sababu kwenye rekodi zetu kuna hadithi iliyosimuliwa na Amirul Mu'minin Ali Ibn Abu Talib (as), Abdullah Ibn Abbas, Abdullah Ibn Mas'ud, Abdullah Ibn Umar, Abu Sa'id al-Khudri, Abu Dardaa, Abu Hurayrah, Anas Ibn Malik, Ma'adh ibn Jabal, na kusimuliwa kupitia vyanzo mbali mbali pamoja na tofauti kidogo ya maneno, kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Mfano wa wafuasi wangu atakayehifadhi hadithi arobaini zinazo husiana na mambo ya dini, Allah atamfufua Siku ya Hukumu pamoja na *ma-faqih* na wanachuoni." Riwaya moja inasema: "Allah atamfufua kama mwanachuoni msomi." Kwa mujibu wa Abu Dardaa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mimi nitakuwa muombezi na shahidi wake Siku ya Kiyama." Kwa mujibu wa Ibn Mas'ud, yeye alisema: "Atapewa hiari ya kuingia Peponi kupitia mlango wowote atakaopenda." Na kwa mujibu wa Ibn Umar, "Atahesabiwa miongoni mwa wanachuoni na atafufuliwa pamoja na Mashahiid." Na kwetu sisi, ile hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) "Mwenyezi Mungu ausafishe uso wa yule anayesikiliza maneno yangu, akayahifadhi na kuyasimulia kwa wengine vile hasa alivyoyasikia tu," ni mamlaka tosha ya kuhifadhi hadith hizi arobaini. Maagizo kama hayo yamo kwenye hadithi: "Wale walionisikia mimi nikizungumza wayafikishe maneno yangu kwa wasiokuwepo hapa."

alitujia na mkono wake ulikuwa katika mkono wa mwanawe, Imam al-Hasan (a.s.), na akasema: Mjumbe wa Allah wakati mmoja alitujia na mkono wake ulikuwa katika mkono wangu kama hivi, huku akisema: 'Ndugu yangu huyu ndiye mbora wa viumbe baada yangu, na ndiye bwana wao, yeye ni Imamu wa kila Mwislamu, jemedari (*Amiir*) wa kila muumini baada yangu."

(6) Pia, al-Saduq katika *Ikmal*, anafuatilia hadithi nyingine mpaka kwa Imamu al-Ridha (as) ambaye anawanukuu baba zake wakieleza kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: "Yeyote yule anayetaka kushikilia dini yangu na kupanda kwenye Safina ya Wokovu baada yangu, na afuate mfano wa Ali ibn Abu Talib, kwani ni mtekelezaji wa wosia wangu, na makamu juu ya umma wangu wakati wa uhai wangu na baada ya kufa kwangu."

(7) Vilevile al-Saduq katika *Ikmal*, anasimulia hadithi nyingine ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), baada ya kutaja vyanzo kadhaa hadi kwa Imamu al-Ridha (a.s.) ambaye ameipokea kutoka kwa baba yake, ambaye naye ameisikia kutoka kwa wahenga wake na kupanda hadi kwa Mtume (s.a.w.w.) ambamo alisema: "Mimi na Ali ni baba (wawili) wa Umma huu; yeyote yule anayetutambua hivyo, huyo anamuamini Allah, na ambaye hatutambui kihivyo hamuamini Allah, Mtukufu, Mwenye Nguvu. Na kutoka kwa Ali ni wajukuu zangu al-Hasan na Husein, ambao ni mabwana wa vijana wa Peponi, na kutoka kwenye kizazi cha Husein watakuwepo Maimamu tisa ambao utii kwao ni sawa na kunitii mimi, na yeyote yule anayewaasi wao ananiasi mimi; wa tisa wao ni *Qa'im* wao na Mahdi."

(8) Kwenye kitabu hicho hicho *Ikmal*, al-Saduq anasimulia hadithi nyingine kupitia *isnad* mpaka kwa Imamu Hasan al-Askari (a.s.) ambaye ameipokea kutoka kwa baba yake, naye kutoka kwa wahenga wake mpaka kufikia kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Ewe Ibn Mas'ud, Ali ibn Abi Talib ni Imamu wako baada yangu; na mrithi wangu kwenu wote."

(9) Ndani ya *Ikmal* hiyo hiyo, al-Saduuq baada ya kutaja mfululizo wa wapokezi ananukuu hadithi moja iliyosimuliwa na Salman akisema kwamba wakati mmoja alimtembelea Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), na akamuona al-Husein ibn Ali (as) amekaa katika mapaja yake, na Mtume alikuwa anabusu kinywa chake huku akisema: "Wewe ni bwana, mtoto wa bwana, ni Imamu na mtoto wa Imamu, ndugu wa Imamu, baba wa Maimamu na wewe ni Hoja (*Hujjat*)wa Allah, mtoto wa Hoja Yake, na baba wa Hoja tisa kutoka kwenye kiuno chako. Wa tisa wao ni *Qa'im* wao."

(10) al-Saduq vile vile katika *Ikmal*, amesimulia na kuungwa mkono na baadhi ya rejea hadithi nyingine ndefu kutoka kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), kama ilivyosimuliwa na Salman ambamo mna maneno: "Ewe Fatimah! Je, hufahamu kwamba sisi ndio Ahlul Bayt ambao kwao Allah ameifanya Akhera kuwa ni bora zaidi kuliko dunia hii, na Allah Aza wa Jallah, alitupia macho kwa wakazi wa ardhi na akanichagua mimi kutoka miongoni mwa viumbe Wake; kisha akatupa macho kwa mara ya pili na akamchagua mume wako na akaniteremshia wahyi nikuozeshe kwake na kumchukua kama rafiki na nimteuwe kuwa waziri wangu, na kumfanya mrithi wangu juu ya Umma wangu. Hivyo, baba yako ni mbora wa Mitume wote, mume wako ni mbora wa mawasii (warithi wa mitume), na wewe utakuwa ndiye wa kwanza kuungana tena nami (baada ya kufa kwangu)."

(11) al-Saduq, vilevile katika kitabu hicho *Ikmal*, ananukuu hadithi ndefu ambamo imeelezwa kwamba wakati mmoja katika kipindi cha Uthman, mkutano wa watu zaidi ya mia mbili kutokana na Muhajirun (wahamiaji kutoka Makka) na Answar (wenyeji wa Madina) walikuwa wamekusanyika msikitini. Walikuwa wanazungumzia masuala ya dini (fiqhi) na matawi mengine ya ilmu wakati walipoanza kujigamba wenyewe kuhusu elimu zao. Lakini Ali (as) ambaye alikuwemo humo pia, yeye alinyamaza kimya. Walimuuliza: "Ewe Abu al-Hasan, kwa nini wewe hushiriki kwenye ma-

zungumzo yetu?" Katika kujibu swali lao, yeye (as) aliwakumbusha tu kauli ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ambayo kwayo alisema: "Ali ni ndugu yangu, waziri, mrithi, mtekelezaji wa wosia, mrithi wangu juu ya Umma wangu, na bwana (*walii*) wa waumini wote baada yangu." Wote wakakiri kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyazungumza yote haya kuhusu yeye.

(12) Vilevile al-Saduq katika kitabu chake *Ikmal,* ananukuu hadithi iliyosimuliwa na Abdullah ibn Ja'far, al-Hasan, al-Husein, Abdullah ibn Abbas, Umar ibn Abu Salmah, Usamah ibn Ziyad, Salmaan, Abu Dharr al-Ghifari, na al-Miqdad ambao wote wanasema kwamba wamemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Nina mamlaka zaidi juu ya waumini kuliko waumini wenyewe waliyo nayo; ndugu yangu Ali baada yangu anayo mamlaka zaidi juu ya waumini kuliko waumini wenyewe waliyo nayo."

(13) al-Saduq vilevile katika kitabu chake *Ikmal*, anasimulia riwaya ya al-Asbagh ibn Nabatah ambaye ameisikia kutoka kwa Ibn Abbas akisema kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Mimi, Ali, al-Hasan, Husein na wengine tisa kutoka kizazi cha Huseini ni watoharifu na watoharishaji."

(14) Vilevile al-Saduq amesimulia kutoka kwa Abayah ibn Rab'i katika kitabu chake *Ikmal* riwaya ambayo ameisikia kutoka kwa Ibn Abbas akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amesema: "Mimi ni bwana wa mitume, ambapo Ali ni bwana wa *wasii* (warithi wa mitume)."

(15) al-Saduq pia amenukuu katika kitabu hicho *Ikmal* hadithi moja iliyowasilishwa kwa sanadi hadi kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) aliyeipokea kutoka kwa jadi zake ambao wameisikia kutoka kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ambaye alisema: "Allah Aza wa Jallah, amenipendelea mimi juu ya mitume wote, na kutoka kwangu amemchagua Ali kuwa mbora juu ya mawasii wote, na akamchagua kutoka kizazi cha Ali, Hasan na Husein, na akachagua kutoka kizazi cha Husein mawasii ambao wataondoa katika dini uharibifu na upotoshaji wa wazushi, wizi wa wahubiri waongo, na tafsiri mbaya za wapotoshaji."

(16) al-Saduq, vilevile katika kitabu chake *Ikmal* anamnukuu Ali (a.s.) akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Maimamu baada yangu ni kumi na mbili: Ewe Ali, wewe ni wa kwanza wao na wa mwisho wao ni *al-Qa'im* ambaye kupitia kwake Allah Aza wa Jallah ataifungua Mashariki ya ardhi na halikadhalika Magharibi yake."[264]

(17) Katika kitabu chake kingine, *Aamali* al-Saduq vilevile amenukuu hadithi iliyosimuliwa na as-Sadiq (a.s.) ambayo ameipokea kutoka kwa babu zake walioisikia kutoka kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), ambamo yeye (s.a.w.w.) amesema: "Ali anatokana na mimi na mimi natokana na Ali ambaye ameumbwa kutokana na udongo uleule nilioumbiwa mimi; anasuluhisha migogoro ya watu inayohusiana na Sunna na maagizo yangu; ni Amiir wa waumini, na ni Imam wa wale Wenye Nyuso Zinazong'ara (*Imamul-Muttaqiin*), na Mbora wa Mawasii wote."

(18) al-Saduq vilevile katika kitabu chake *Aamali* amenukuu hadithi nyingine ndefu iliyosimuliwa na Ali (as) ambayo ameisikia kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akisema: "Ali ni Amir wa Waumini. Allah, Aza wa Jallah amemteua kuwa Walii kwenye mbingu ya juu kabisa na kuwafanya malaika washuhudie na kwa kweli 'Ali ni mwakilishi wa Allah na Uthibitisho (*Hujjatullah*); na ni Imamu wa Waislamu wote.'"

---

[264] Hadithi hii na nyingine kumi na tano kabla ya hii zimeandikwa chini ya kichwa cha maneno: "Hadithi za wazi za Mkutuku Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na *Qa'im* (Mahdi) na kwamba atakuwa ndiye Imam wa kumi na mbili katika mpangilio wa Maimamu," katika Sura ya Ishirini na nne ya *Ikmal ad-Din wa aimam al- Ni'mah*, uk. 148 - 167.

(19) al-Saduq vilevile katika *Aamali* yake, ameandika riwaya iliyosimuliwa na Ibn Abbas akielezea kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: "Ewe Ali! Wewe ni Imamu wa Waislamu wote, Amir wa Waumini, kiongozi wa wenye Nyuso zenye Kung'ara, ni uthibitisho (hujjat) wa Allah baada yangu, na bwana wa Mawasii wote."

(20) al-Saduq vilevile katika *Aamali* yake, amesimulia riwaya nyingine kutoka kwa Ibn Abbas akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: "Ewe Ali! Wewe ni mrithi wangu juu ya Umma wangu, na wewe ni kama Shith alivyokuwa kwa Adam."

(21) Katika kitabu hicho hicho *Aamali,* sl-Saduq vilevile, baada ya kunukuu vyanzo kadhaa amesimulia kutoka kwa Abu Dharr al-Ghifari akisema kwamba wakati fulani alikuwa pamoja na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) msikitini kwake wakati aliposema: "Mtu atakujieni kupitia mlango huu ambaye yeye ni Amir wa Waumini na Imamu wa Waislamu." Mara akatokeza Ali ibn Abu Talib pale mlangoni, na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akapiga hatua mbele na kumkaribisha, kisha akageuzia uso wake mtukufu kwetu na akasema: 'Huyu ni Imamu wenu baada yangu."[265]

(22) Katika kitabu chake; *Aamali* al-Saduq ameisimulia hadith hii kama alivyoipokea Jabir ibn Abdullah al-Answari akimnukuu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Ali ibn Abu Talib alikuwa wa kwanza kukubali Uislamu, na ni mwenye ilmu zaidi kuliko wote"… na akamalizia kwa kusema "Yeye ni Imamu na Khalifa baada yangu."

(23) Katika *Aamali* yake hiyo, al-Saduq vilevile baada ya kutaja vyanzo kadhaa amesimulia hadithi moja sahihi kutoka kwa Ibn Abbas ambaye anamnukuu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Enyi watu! Ni nani ambaye maneno yake ni bora kuliko ya Allah? Mola wenu Jalal Jallaaluhu, ameniamrisha kumsimamisha Ali juu yenu kama mwongozo, khalifa wangu na wasii wangu, na kwamba lazima mumchukulie kama ndugu yangu na waziri."

(24) Katika *Aamali* yake, as-Saduq vilevile baada ya kutaja vyanzo kadhaa, ameandika hadithi moja iliyosimuliwa na Abu Ayyash ambaye anasema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) wakati fulani alipanda juu ya mimbari na akatoa khutba ambayo kwayo alisema: 'Binamu yangu Ali ni ndugu yangu, waziri, na ni Khalifa wangu na mlingania dini kwa niaba yangu."

(25) Vilevile katika *Aamali* yake, as-Saduq amenukuu hadithi moja sahihi kwa sanadi hadi kwa Amirul-Mu'minina Ali ambaye anasema: "Wakati fulani Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alituhutubia akisema: "Enyi watu wangu! Mwezi wa Allah umekaribia,' na akaendelea na khutba yake akihadithia neema za mwezi wa Ramadhani. Nilimuuliza Mjumbe wa Allah ni kitendo gani ambacho ni bora katika mwezi huu. Yeye akajibu: 'Ni kukaa mbali na chochote kile ambacho Allah amekuharamishia.' Kisha aliangua kilio. Hivyo nikamuuliza: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni nini kinachokuhuzunisha?' na alijibu: 'Ewe Ali ninalia juu ya udhalimu wa kutisha utakaotendewa wewe ndani ya mwezi huu…..' Akamalizia kwa haya: 'Ewe Ali, wewe ni *wasii* wangu, baba wa watoto wangu, na khalifa wangu juu ya Umma wangu wakati wa uhai wangu na baada ya kifo changu. Amri yako ni amri yangu, na hivyo hivyo katazo lako ni katazo langu.'"

(26) Katika *Aamali* yake, al-Saduq amenukuu hadithi nyingine iliyosimuliwa na Ali (a.s.) ambaye anasema: "Mjumbe wa Allah alisema: 'Ewe Ali! Wewe ni ndugu yangu na mimi ni ndugu yako; mimi nimechaguliwa kwa Utume ambapo wewe ulichaguliwa kwa Uimamu. Amri za Mwenyezi Mungu zinateremshwa kwangu na wewe utachukua jukumu la kuzitafsiri. Na wewe ni baba wa Umma huu. Ewe Ali! Wewe ni wasii na makamu wangu, waziri wangu na mrithi na baba wa kizazi changu.'"

[265] Hadithi hii, pamoja na nyingine nne zilizoitangulia, zimenukuliwa kutoka kwenye kitabu *Amali* cha al-Saduq ndani ya Sura ya 9 ya *Ghayat al-Maram* cha Sayyid ul-Bahraini ambamo ndio tumezinukuu kuweka vyanzo ili kufupisha nafasi. Ama kuhusu hadithi ambazo zimefuatilia hizi, yaani namba 22 hadi 40, zitapatikana katika Sura ya 13 ya *Ghayat al-Maram.*

(27) Katika *Aamali* yake, al-Saduq vilevile ananukuu hadithi moja ambayo sanad yake inapanda mpaka kwa Ibn Abbas ambaye anasema kwamba siku moja Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa katika msikiti wa Quba katika mkusanyiko na Maansari wa Madina na akasema: "Ewe Ali! Wewe ni ndugu yangu na mimi ni ndugu yako; na wewe ni wasii wangu na khalifa wangu na Imamu wa umma wangu baada yangu. Allah ampende yeyote yule anayekupenda wewe, na Awe adui kwa yeyote yule atakayekufanyia uadui.'"

(28) Katika *Aamali* yake, al-Saduq vilevile kanukuu hadith ndefu iliyosimuliwa na Umm Salamah (mke mchamungu wa Mtume) ambayo kwayo mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimuambia: "Ewe Umm Salamah! Nisikilize na uwe shahidi: Huyu Ali ibn Talib ni mtekelezaji wa wosia wangu; ni Khalifa wangu baada yangu na mtimizaji wa ahadi zangu na muondoshaji wa wanafiki kwenye birika langu la al-Kawthar."

(29) Katika *Aamali* hiyo hiyo, al-Saduq amenukuu riwaya iliyosimuliwa na Salman al-Farisi baada ya kutaja vyanzo vinavyoishia kwake akisema kwamba amemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Enyi Muhajirun na Answar! Je, nikuongozeni kwenye kile ambacho kama mtashikamana nacho, kamwe hamtapotea baada yangu?' Wakasema: 'Ndio Ewe Mjumbe wa Allah!' Yeye (s.a.w.w.) akasema: "'Huyu Ali ni ndugu yangu na mtekelezaji wa wosia wangu, waziri wangu, mrithi na khalifa wangu; ni Imamu wenu; kwa hiyo, mpendeni sana kama mnavyonipenda mimi, na mheshimuni sana kama mnavyoniheshimu mimi, kwani Jibril ameniamuru niwaambie hivyo.'"

(30) Katika *Aamali* yake al-Saduq, vilevile amenukuu hadithi moja iliyosimuliwa kwa sanadi inayofika kwa Zayd ibn Arqam ambaye anasema: Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amenukuliwa akisema: "Je, nikuongozeni kwenye kile ambacho kama mtashikamana nacho kitawakinga dhidi ya kuangamia na kupotea? Imamu wenu na *walii* ni Ali ibn Abu Talib; kwa hiyo, fanyeni mumsaidie katika kazi yake, mumtakie heri, sikilizeni ushauri wake, na muwe na imani kwake, kwani Jibril ameniamuru kuwambia hivyo."

(31) Katika *Aamali* yake, al-Saduq ananukuu hadithi moja iliyosimuliwa na Ibn Abbas, ambayo kwayo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Ewe Ali! Wewe ni Imamu wa Umma wangu na khalifa wangu baada yangu."

(32) Katika *Aamali* yake, al-Saduq anamnukuu Ibn Abbas akisimulia hadithi moja ambayo kwayo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) anasema: "Allah Aza wa Jallah amenifunulia mimi kwamba atachagua kutoka miongoni mwa Umma wangu ndugu na mrithi na khalifa na mtekelezaji wa wosia wangu: Niliuliza: 'Ewe Mola! Ni nani huyo?' Akajibu: 'Ni Imam wa Umma wako na Hujja Yangu kwao baada yako." Nikauliza tena: 'Ewe Mola Wangu, ni nani huyo?' Yeye akanijibu: 'Ni yule ambaye Mimi nampenda naye ananipenda mimi na …' Wahyi uliishia na maneno: 'Ni Ali ibn Abu Talib,'"

(33) Katika *Aamali* hiyo hiyo, al-Saduq ananukuu hadithi nyingine kama iliyosimuliwa na Imam as-Sadiq (a.s.) aliyeipokea kutoka kwa wahenga wake kutoka kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ambaye anasema: "Wakati nilipochukuliwa kwenda mbinguni *isra* (Miraji), Mola Wangu Mtukufu, alinijulisha kuhusu Ali kwamba yeye ndiye Imamu wa wachamungu, kiongozi wa wale wenye nyuso zinazong'aa na ni fahari ya waumini."

(34) Katika *Aamali* yake, as-Saduq ananukuu hadithi moja kwa sanad mpaka kwa Imamu al-Ridha (a.s.) ambaye anawanukuu wahenga wake waliomsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Ali anatokana na mimi, na mimi natokana na Ali; Allah awalaani wale ambao wanapigana dhidi ya Ali, hakika yeye ni Imamu wa viumbe wote baada yangu."

(35) Shaykh at-Ta'ifah Abu Ja'far Muhammad ibn al-Hasan al-Tuusi, katika *Aamali* yake baada ya kutaja vyanzo kadhaa, ananukuu hadithi moja iliyosimuliwa na Ammar ibn Yasir ambaye anasema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimuambia Ali: "Allah amekupamba kwa sifa bora na ishara maridadi zenye kupendeza mno Kwake kuliko ambazo amempamba nazo mwingine yeyote kati ya waja Wake. Amekupamba kwa utawa na ghera ya kidini na kwa kuipa nyongo dunia na anasa zake (*zuhud*) ambavyo hakuna kinachoweza kupungua kwako na ambavyo hakuna anayeweza kukulaumu kamwe. Na amekujaalia wewe mapenzi kwa mafukara, akakufanya mwenye kukubalika kwenye ufuasi wao, na akawafanya wakubaliane na Uimamu wako. Amebarikiwa yeyote yule mwenye kukupenda wewe na kuthibitisha na kuunga mkono maneno yako, na ole wake yeyote yule anayekuchukia na kukanusha ukweli wa maneno yako."

(36) Shaykh at-Ta'ifah Abu Ja'far Muhammad ibn al-Hasan al-Tuusi katika *Aamali* yake, baada ya kunukuu vyanzo kadhaa mpaka kwa Ali (a.s.), amesimulia hadithi kwamba wakati mmoja Ali alikuwa anahubiri kwenye mimbari huko Kufa akisema: "Enyi watu! Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amenitunukia fadhila kumi maalum ambazo ni bora zaidi kwangu kuliko kitu chochote chini ya jua. Yeye (s.a.w.w.) ameniambia: Ewe Ali! Wewe ni ndugu yangu katika dunia hii na katika ile ya Akhera, na wewe uko karibu mno na mimi miongoni mwa viumbe wote katika Siku ya Ufufuo; makazi yako katika Pepo yako mbele ya makazi yangu; wewe ni mrithi wangu, mtekelezaji wa wosia wangu katika ahadi nilizotoa mimi na ndani ya familia yangu, na wewe ndio mlinzi wa Ahlul-Bayt wangu baada yangu. Na wewe ni Imamu wa Umma wangu; utakuwa mtoaji wa haki miongini mwa wafuasi wangu. Na rafiki yako ni rafiki yangu na rafiki yangu mimi ni rafiki wa Allah; adui yako ni adui yangu, na kwa hakika adui yangu ni adui wa Allah."

(37) Katika kitabu cha al-Saduq kiitwacho *Al-Nusuus 'ala al-A'imma*, baada ya kutaja wasimuliaji hadi kwa Imam, Hasan ibn Ali (a.s.) ambaye amesema kwamba amemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akimwambia Ali: "Wewe ni mrithi wa ilmu yangu na mhifadhi wa hekima zangu na ndiwe Imamu baada yangu."

(38) Vilevili katika *an-Nusuus* hiyo, baada ya kunukuu majina ya wapokezi, al-Saduq amesimulia kutoka kwa Imran ibn Hasiin ambaye amesema: "Nimemsikia Mjumbe wa Allah akimuambia Ali (as): 'Na wewe ndiye Imamu na Khalifa baada yangu.'"

(39) Vilevile katika kitabu hicho hicho, al-Saduq amesimulia baada ya kunukuu majina ya wapokezi hadi kwa Ali (a.s.) ambaye amesema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimuambia: "Ewe Ali! Wewe ni mtekelezaji wa wasia juu ya wale ambao wamekufa miongoni mwa familia yangu, na khalifa wa wale ambao wa hai miongoni mwa Umma wangu."

(40) Vilevile katika rejea hiyo hiyo hapo juu, al-Saduq amenukuu wapokezi hadi kwa Husein ibn Ali (a.s.) ambaye amesema kwamba wakati Allah alipoteremsha aya hii: **Na ndugu wa tumbo wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe katika Kitab cha Mwenyezi Mungu…' (Qur'ani 8:75).** Nilimuomba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aitafsir aya hiyo, na akasema: "Ninyi ndio ndugu wenye cheo bora. Wakati nitakapofariki, baba yako Ali, ambaye ndiye wa karibu sana na mimi, ana cheo bora zaidi kuliko mtu mwingine yoyote kwa ajili ya kunirithi mimi. Wakati baba yako akifariki kaka yako Hasan ana nafasi bora zaidi kwa cheo cha baba yako; na atakapofariki Hasan, basi wewe ni bora zaidi kwa cheo chake."

Riwaya hizo hapo juu ambazo zimenukuliwa katika hali hii ya haraka zina uwiano sawa na hadithi sahihi zilizobaki (kuhusiana na Uimam wa jumla wa Imam Ali) kama vile ua moja kwenye shada zima la

maua yote yaliyo bakia, au tone la maji kwenye bahari. Lakini bado hata hivyo chache hizo zitatosheleza (kukuridhisha juu ya ukweli wa imani yetu). Sifa zote ni za Allah Mola wa walimwengu wote. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 63

## SAFAR 3, 1330 A.H.

**I. Riwaya Zilizosimuliwa na Shi'ah Pekee Hazikubaliwi kama Hoja,**

**II. Kwa nini Wasio Shi'ah Hawakuzisimulia?**

**III. Maombi ya Riwaya Zaidi Zilizosimuliwa na Kuandikwa na Sunni.**

Riwaya ulizonukuu wewe sio hoja za kuridhisha dhidi ya Ahlul-Sunnah ambao hawaziamini kuwa sahihi.

Kwa nini wengine (wasiokuwa Shi'ah) hawakuzisimulia na kuziandika kama riwaya hizo zimethibitishwa kuwa ni sahihi?

Tafadhali egemeza majadiliano ya baadae juu ya hadithi zilizosimuliwa na muhadithiina wa Sunni katika suala hili. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 64

## SAFAR 4, 1330 A.H.

**I. Tumenukuu Riwaya Hizo Kulingana na Maombi Yako,**

**II. Riwaya Zilizonukuliwa Kabla Kutoka Kwenye Vitabu Vyenu Vya Hadithi Sahih Zinatosha Kuridhisha Walio Wengi,**

**III. Kwa nini Hawakusimulia Hadithi Hizi Sahihi Zilizo Kwenye Kumbukumbu Zetu,**

**IV. Kutajwa kwa Hadithi ya Urithi.**

Riwaya tulizodondoa katika barua yetu iliyopita zilikuwa ni kwa ajili ya taarifa yako kama ulivyotaka kwenye ombi lako mwenyewe.

Riwaya ambazo tumezisimulia kabla kutoka kwenye vitabu vyenu wenyewe vya Hadithi Sahihi zinatosheleza kukuridhisha juu ya maoni yetu.

Ilikuwa ni desturi mashuhuri ya kundi la Mafiraun wa wakati wa mwanzo kabisa wa Uislamu ambao nyoyo zao zilikuwa ngumu kwa Aali Muhammad (s.a.w.w.) na ambao wameficha kwenye vifua vyao chuki na uadui wao na kinyongo dhidi ya Ahlil-Bayt (a.s.) ambavyo viliwazuia kuandika hadithi hizi Sahihi kwenye vitabu vyao. Wale ambao waliokuwa kwenye mamlaka na utawala wakati huo, waliutawala Umma kwa mapesa yaliyotumika kianasa kutoka kwenye Baytul-Mal na hazina za watu binafsi ili kuficha zile sifa na tabia bora na kuzima nuru ya Ahlul Bayt. Kwa hali na mtazamo huu, wao walifanya kila kilichokuwepo kwenye mamlaka yao. Waliwazuia watu kwa vishawishi na kulazimisha katika kuzungumzia kuhusu sifa bora za kichwa na moyo wa Ahlul-Bayt. Walitoa pesa, wakalipa mishahara na wakatoa nafasi za kazi za kiheshima kabisa kwa wale ambao wangeweza kutumika katika kuwatimizia malengo yao, na wakati mbinu hizi ziliposhindwa walitumia mijeledi na panga zao kikatili kabisa. Wale ambao walisema uwongo juu ya Ahlul-Bayt au wanaokanusha ukweli wa maneno yao walifanywa kuwa vipenzi, ambapo wale ambao walizungumza juu ya sifa zao na kuthibitisha ukweli wa maneno yao walitolewa kwenye majumba yao, kuwahamisha au waliuawa.

Wewe hujui kwamba hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na Uimamu, na warithi wake, kwa asili yake hasa, zilikuwa ni chanzo cha hofu na wasiwasi wa kudumu kwa wale walioingia madarakani baada yake. Walikuwa wanaogopa kubomoka kwa utawala wao na kudhoofika ufalme wao. Kwao wao usalama ulikuwa katika kuzuia uenezaji wa zile hadithi na kuufanya Umma usiwe na habari nazo. Kwamba riwaya hizo zilizishinda jitihada zao hatari na zikaishi zaidi ya waporaji na wenye kujipendekeza kwao, na kutufikia kupitia vyanzo vingi vya kuaminika ni uthibitisho usiopingika wa Ukweli na muujiza wa Haki. Wale madhalimu ambao walikuwa wamepora haki za Ahlul-Bayt na kujitwalia wao wenyewe au wasaidizi wao bila haki zile fadhaili na heshima ambazo Mwenyezi Mungu alizitoa kwa Ahlul-Bayt (a.s.), walizoea kutoa adhabu kali kwa yeyote yule ambaye alishutumiwa kuonesha mapenzi au heshima kwa Ahlul-Bayt. Walimnyoa ndevu zake, kumpandisha juu ya mgongo wa punda na kuzungushwa sehemu za madukani na sokoni kama wahalifu wenye hatia za kulaumiwa, kisha kuwadhalilisha, kuwakemea na kuwanyima haki zao za kiraia. Walinyimwa hata haki ya kukata rufaa au kutafuta msaada wa kisheria, na wakatengwa kabisa na jamii.[266]

[266] Rejea kwenye ukurasa wa 15, J. 3, ya *Sharh Nahjul Balaghah* cha Ibn Abul Hadid, na utaona ukatili ule waliofanyiwa Ahlul Bayt (as) na Mashia wao wakati wa zama za Bani Umayyah na Bani Abbas. Maelezo yanaishia na nukuu kutoka kwa Imamu al-Baqir (as) ambayo wachuoni wa utafiti wanayafahamu vizuri.

Mtu yeyote anayekutwa anazungumza lolote linalokubalika kuhusu Ali (as), alikuwa hakubaliwi na serikali, anawekwa wazi kwenye uadui na damu yake inakuwa ni halali kumwagwa, anaporwa mali yake na ananyongwa. Ndimi nyingi zimeng'olewa kwa sababu tu ya kumsifu Ali. Macho mengi yamenyofolewa kwa kumuangalia yeye kwa heshima. Ni mikono mingi iliyokatwa kwa kuelekezea sifa yoyote bora ya Ali. Miguu mingi iliyokuwa ikitembea kwa mapenzi ama hisia za urafiki kuelekea kwa Ali ilikatwa. Nyumba nyingi za wafuasi wake zilichomwa moto na mashamba yao ya mitende kuharibiwa. Na hatimaye ama walinyongwa kwenye miti na kuuliwa au kufukuzwa kwenye nyumba zao, kunyang'anywa ardhi na mali zao na kuteswa kwa njia za namna mbalimbali.

Muhadithina wengi na wanahistoria walikuwa ni watu ambao waliwaabudu wafalme hao na madhalimu halikadhalika na watawala wao badala ya kumuabudu Allah Aza wa Jallah, na walikuwa wakiwadanganya kwa kubadilisha, matamshi na tafsiri zenye kupotosha hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilizo na mwelekeo wa kuhatarisha maslahi yao binafsi, kwa kuzifanya hadith sahihi zionekane zenye mashaka, kama vile tu tunavyowaona wengi siku hizi wenye kujipendekeza miongoni mwa masheikh, wanachuoni wa kulipwa, majaji wabaya ambao hufukuzana kuwaridhisha watawala kwa kuthibitisha sera zao, na hatua zao za kiutawala, ziwe ni za kiadilifu zenye manufaa au za kidhalimu na mabavu, na kutetea na kushikilia amri zao, ziwe zinafaa kwa usalama ama machafuko, na watawala wanapotaka hukumu yenye kuunga mkono amri zao au kunyamazisha wapinzani wao, wao wanaharakisha kutoa hukumu kulingana na matakwa yake, na zenye kusaidia kutimiza sera zake za kisiasa, hata kama zinapingana na mwelekeo wa Kitabu (Qur'ani) na Sunna, au kuvunja *ijma* ya Umma waziwazi. Wanachojali tu ni kulinda nafasi zao na hofu ya kufukuzwa endapo mtawala atakasirika, au matumaini ya kupata zawadi endapo mtawala atafurahi. Kuna ulimwengu wa tofauti baina ya hawa wanachuoni wetu wa sasa na hao wa enzi zile. Wanachuoni wa sasa hawaheshimiwi na serikali zao, ambapo katika zama zile watawala waliwahitaji mno wanachuoni na walitafuta kwa hamu sana huduma zao, wakawaajiri kwenye nafasi za heshima na kuwafanya wawe na maisha ya anasa kwa sababu ilikuwa ni kupitia kwao hao ambapo watawala walipigana dhidi ya Allah na Mjumbe Wake. Wanachuoni walipewa heshima maalumu ya hali ya juu, na maneno yao yalisikilizwa na kuzingatiwa; kwa hiyo; walipata ushawishi mkubwa, wakawa na mali nyingi mno na wakaishi maisha ya kifahari. Kazi yao ilikuwa ni kugeuza, kukanusha au kwa msisitizo kabisa kuzikosoa na kuziita kama zenye mashaka hadithi sahihi zote zenye kumsifia Ali (a.s.) au mtu yeyote kati ya Ahul-Bayt moja kwa moja kwa mzunguko. Hilo lilipokuwa haliwezekani walizitafsiri vibaya hadithi hizo. Kama hadithi haikukubali tafsiri potovu basi wangewatangaza wasimuliaji, waandishi na wapokezi wa hadithi hizo kuwa marafidhi, na kwa mujibu wa maoni yao, Rafidhi ni uovu mbaya mno. Hii ndio sera yao kwa hadithi zinazomsifia Ali, hususan kama zinachukuliwa kwa heshima kubwa na Mashia.

Ama kuhusu hawa wanachuoni wanaojipendekeza, hawa walikuwa na mawakala na watu wa kupita nyumba hadi nyumba katika kila mji na kijiji ambao husifia mno mafanikio ya kiuanachuo ya mabwana zao. Miongoni mwao walikuwamo wanachuoni wa kidini wenye hamasa za kisekula ambao hutangaza maoni na mitazamo na hukumu za kisheria za wakuu wao, ni wafuasi wenye kudhihirisha utawa na ibada, ni viongozi wa makabila na makundi vilevile. Wakati mawakala hawa wanapokuja kuzijua hukumu potovu za wanachuoni hawa wenye kujipendekeza, juu ya hadithi sahihi kuhusu Ali au yeyote kati ya Ahlul-Bayt (a.s.) watazichukua na kuzieneza kama hoja zenye nguvu miongoni mwa watu wa kawaida na wajinga na wahuni, na kuzifanya mashuhuri sana katika mji wote na kuzitumia kama kanuni za imani yao na mfano kwa ajili ya baadaye. Kulikuwa kuna kundi lingine la wasimulizi siku hizo ambao hofu ya ulinzi wa mali na maisha yao walilazimika kujizuia kusimulia au kuandika zile hadithi zinazomhusu Ali na Ahlul-Bayt (as) ambazo ni mutawatir. Wakati masikini watu hawo wakitakiwa kutoa maoni yao kuhusu mawazo au hukumu potovu za hawa watu wanaojipendekeza kuhusu sifa za Ali na Ahlul-Bayt (as), au kukataa kwao moja kwa moja riwaya kama hizo wanaogopa na kuhofia mlipuko wa ghafla wa hisia za

umma na vurugu za wasio wastaarabu dhidi yao. Wasingethubutu kuwapa majibu sahihi, wangekimbilia kutafuta hifadhi nyuma ya yale maelezo ya maoni pinzani. Walilikwepa hilo kwa kuhofia kuvamiwa na wale wenye kujipendekeza walioajiriwa, hususan wale mawakala wao na wale wanaopita nyumba kwa nyumba, na walihofia pia makelele na misisimko ya ghafla ya umma na vurugu za wahuni dhidi yao. Wasingethubutu kutoa majibu sahihi na wangejihami kwenye yale maelezo ya maoni ya kinyume chake.

Watawala na magavana wao, na maafisa wa ngazi za juu waliwaamuru watu vikali kumshutumu na kumlaani Amirul-Muumini Ali ibn Abu Talib na walihakikisha makubaliano magumu ya amri hizo kwa kupitia ahadi, zawadi na vitisho vya hatua za kijeshi. Walikuwa wakiwalazimisha watu kumshutumu, kumdharau na kumkosoa Ali. Katika taarifa na nyaraka zao walimsawiri vibaya au walichora picha za kuwafanya watu wamchukie. Waliongea mambo ambayo yanakarahisha na kuudhi masikioni. Kumlaani Ali na kumuombea mabaya juu ya mimbari na majukwaa ya Umma ilikuwa ni kitendo kilichopendekezwa husasan wakati wa Swala za Ijumaa na Iddi zote mbili. Nuru ya Allah isingekuwa ni isiyoweza kuzimwa, na sifa bora za mawalii Wake hazifichiki; sio hadithi sahihi na za wazi kuhusu urithi wa Ali wala riwaya kuhusu sifa zake bora ambazo zingeweza kutufikia kupitia vyanzo vya kuaminika vya makundi yote ya Sunni na Shi'ah. Hakuna maandiko ambayo yamesimuliwa kwa mfululizo zaidi kama maandiko juu ya sifa zake, na mimi Wallahi, nashangaa ni mng'aro wa kupumbaza kiasi gani ulikuwa nazo sifa ambazo Allah amezijaalia makhsusi juu ya Ali ibn Abu Talib, mtumishi Wake na ndugu wa Mjumbe Wake, na jinsi nuru yake ilivyopenya kwenye mrundikano wa giza la mapazia mengi, na kushinda mawimbi ya dhoruba inayounguruma ya ukandamizaji, na kuufanya ulimwengu wote kung'ara kama mwanga wa mchana!

Kwa nyongeza juu ya riwaya zilizokwisha kusimuliwa ambazo ni hoja zisizo na shaka katika kuunga mkono urithi na Uimam wa jumla wa Ali ibn Abi Talib, tunakurejesha kwenye Hadithi ya Urithi, ambayo yenyewe ni hoja kubwa isiyokanushika. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 65

## SAFAR 5, 1330 A.H.

**Maombi Ya Hadithi Inayohusiana Na Urithi.**

Tafadhali tusimulie hadithi ya urithi kama ilivyowasilishwa pia na Masunni. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh**.

# BARUA YA 66

## SAFAR 5, 1330 A.H.

**Ali (a.s.) ni Mrithi wa Mtume (s.a.w.w.).**

Hakuna shaka kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimteua Ali (a.s.) kuwa mrithi wa ilmu na hekima kama ambavyo mitume waliwateua mawasii wa kutekeleza wasia wao. Ilikuwa ni kuhusiana na hili kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Mimi ni Jiji la ilmu na Ali ni mlango wake. Kwa hiyo, yeyote yule anayetaka kupata ilmu, basi anapaswa kupitia kwenye mlango huo."[267]

Yeye (s.a.w.w.), alisema: "Mimi ni ghala la hekima na Ali ni mlango wake… Ali ni lango la ilmu yangu, ni mwenye kuelezea baada yangu ujumbe ambao nimetumwa kuufikisha; kumpenda yeye ni dalili ya imani, na kumchukia yeye ni unafiki." Kwa mujibu wa Zayd ibn'Awfah, yeye (s.a.w.w.) alimuambia Ali hivi: "Wewe ni ndugu na mrithi wangu,"[268] wakati ambapo Ali aliuliza: "Na utanirithisha nini?" Yeye (s.a.w.w.) alijibu: "Chochote kile ambacho mitume kabla yangu waliwarithisha mawasii wao." Katika hadithi nyingine kutoka kwa Buraydah, bila utata inaeleza kwamba Ali ibn Abi Talib alikuwa ndio mrithi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)."[269] Vilevile rejea kwenye hadithi katika siku ya kuwaonya ndugu wa karibu ambayo ni hoja ya kutosha kuunga mkono urithi wa Ali (a.s.). Wakati wa uhai wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) Ali (a.s.) alikuwa akisema: "Kwa jina la Allah mimi ni ndugu yake, mrithi wake na binamu yake, na mrithi wa ilmu yake. Basi nani mwenye haki bora zaidi ya kumrithi yeye kuliko mimi mwenyewe?"[270]

Wakati fulani Ali aliulizwa: "Imekuaje umemrithi binamu yako licha ya kuweko ami yako?" Alijibu: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aliwakusanya watoto wa Abdul Muttalib, ambao walikuwa kundi kubwa, na kila mmoja wao alikuwa anapaswa kula mkono mzima na kunywa bakuli zima la maziwa. Lakini alitayarisha kwa ajili yao kibaba cha chakula (kiasi cha ratili moja na robo tatu au kilo moja na robo); bado wote walikula mpaka wakashiba, na chakula hicho kikabaki kama kilivyokuwa kana kwamba hakikuguswa. Kisha yeye (s.a.w.w.), alisema: 'Enyi watoto wa Abdul Muttalib! Nimetumwa hususan kwenu na kwa watu wote kwa ujumla; basi nani miongoni mwenu atanipa kiapo cha utii cha kuwa ndugu, swahiba na mrithi wangu?' Hakuna aliyesimama kujibu; hivyo, mimi nilisimama, ingawa nilikuwa ndio mdogo kabisa miongoni mwa waliohudhuria. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliniamuru nikae chini. Alirudia kauli yake mara tatu, na kila wakati, nilikuwa mimi tu niliyesimama, na kila wakati aliniambia nikae chini. Mara ya tatu, alinipa mkono; hivyo ndivyo nilivyotokea kumrithi binamu yangu licha ya kuwepo ami yangu (Abbas).'" [271]

---

[267] Tumenukuu hadithi hii na nyingine mbili baada ya hii katika Barua yetu ya 48. Tafadhali rejea pia kwenye hadithi ya 9, 10 na 11, kwenye barua hiyo na usipuuze uzingatie tanbihi yake.

[268] Hadithi hii tumeinukuu katika Barua yetu Na. 32.

[269] Rejea Barua Na. 68.

[270] Maelezo haya ni tafsiri yenyewe haswa ya maneno asilia ya Ali ambayo yamenukuliwa na al-Hakim kwenye ukurasa wa 126, Jz. 3, ya kitabu chake *Al-Mustadrak* kupitia vyanzo viliyothibitishwa na al-Bukhari na Muslim. Al-Dhahbi, katika kitabu chake *Talkhis al-Mustadrak,* amekiri maneno haya kuwa ni halisia.

[271] Hadithi hii inasimama juu ya misingi imara, na ni hadithi ndefu. Imenukuliwa na Ziya al-Muqaddasi katika kitabu chake *Al-Mukhtara*, na Ibn Jarir katika kitabu chake *Tahdhib al-Athar*. Ni hadithi Na. 6155 katika ukurasa 408, Jz. 6, ya *al-Kanz al-Ummal.* Vilevile imenukuliwa na an-Nasai katika ukurasa 18 wa kitabu chake *Al-Khasa'is al-Alawiyyat,* na imewasilishwa na Ibn Abul Hadid kutoka *Tarikh al-Tabarani* karibu na mwisho wa ufafanuzi juu ya khutba ya "*qasi'a*", ukurasa wa 255, Jz. 3, wa *Sharh Nahjul Balaghah.* Pia rejea ukurasa wa 159, Jz. 1, ya *Musnad* ya Imamu Ahmad ibn Hanbal ambako utaona hadithi yenye maana kama hii.

Kwa mujibu wa al-Hakim katika *Al-Mustadrak* [272] na al-Dhahabi ameinukuu katika *Talkhis,* ambao wote wanathibitisha usahihi wake. Inasema kwamba Qutham bin Abbas wakati fulani aliulizwa: "Imekuaje Ali akamrithi Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na sio wewe?" Alijibu: "Ni kwa sababu yeye alikuwa wa mwanzo kabisa miongoni mwetu katika kumfuata yeye (Mtume), na kwa kuambatana naye zaidi kuliko yeyote katika sisi."

Ninaona kwamba kila mtu alijua kwamba mrithi wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa ni Ali na sio ami yake Abbas au mtu mwingine yeyote wa ukoo wa Hashim. Walikuwa wakilizungumzia hilo kama ukweli uliothibiti, ingawa hawakufahamu sababu ya kwa nini Ali, ambaye alikuwa ni binamu yake Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alikuwa ndiye mrithi na sio Abbas ambaye ni ami yake (s.a.w.w.), au binamu mwingine yeyote au ndugu wa Mtume (s.a.w.w.). Kwa sababu hii walimuuliza Ali (a.s.) wakati fulani na Qutham wakati mwingine, na umeyasoma majibu yao katika mistari ya hapo juu. Na yalikuwa majibu ya kuridhisha kwa uelewa wa wale waulizaji na wale wenye akili kama zao. Lakini majibu halisi yalikuwa kwamba, Allah Aza wa Jallah aliangalia juu ya watu wa ardhi na akamchagua Muhammad (s.a.w.w.) na akamfanya kuwa Mtume, kisha akatupa tena jicho na akamchagua Ali na kupitia *wahyi* alimwagiza Mjumbe Wake (s.a.w.w.) kumteua Ali kama mrithi na mtekeleza wasia wake.

Katika ukurasa wa 125, J. 3, wa *Al-Mustdrak,* al-Hakim, akiwa anamnukuu Qutham akielezea hadithi hiyo hapo juu, anaandika kwamba Kadhi Mkuu [Jaji mkuu au Mufti mkuu], Abul-Hasan Muhamaad ibn Saalih al-Hashimi alimwambia kwamba wakati fulani alimsikia Abu Umaral Qadhi akisema kwamba, baada ya kutajwa majibu ya Qatham bin Abbas mbele yake, Isma'il ibn Is'haq al-Qadhi alisema kwamba: "Msingi wa urithi kwa mwingine ni ama undugu wa damu au uhusiano mwema, utiifu na nia njema, na wanachuoni hawapingi ukweli kwamba [chini ya mazingira ya kawaida] binamu hawi mrithi wakati ami [baba yake] yuko hai. Kwa mujibu wa makubaliano haya ya wote, Ali alirithi ilmu ya Mtume kuliko wao." Kusema kweli, riwaya zinazohusu hili ni mutawatiri, hususan zilizopatikana kupitia njia ya kizazi kitoharifu, na watutosha Wosia na maandiko yake bayana, Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[272] Hadithi hii inapatikana ukurasa wa 125 wa Jz. 3, ambapo imenukuliwa na Abu Shaybah, na ni hadithi Na. 6084 uk. 400, Jz. 6, wa *Kanz al-Ummal*.

# BARUA YA 67

## SAFAR 6, 1330 A.H.

**Kuuomba Wosia Wa Mtume.**

Ahlus Sunni hawafahamu wosia wowote ulioachwa kwa ajili ya Ali, wala hawajui chochote kuhusu hadithi ya wazi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.); hivyo tafadhali kama utatueleza kisa chake tutakushukuru sana, wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 68

## SAFAR 9, 1330 A.H.

**Hadithi za Wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)**
**Kuhusu Urithi wa Ali (a.s.).**

Hadithi zinazohusiana na wosia ni mutawatir kama zilivyosimuliwa kupitia Maimamu wa kizazi kitoharifu (as). Rejea kwenye kifungu cha 11 katika barua ya 20 kuhusiana na kilichoelezwa na watu wengine juu ya hili. Hapo tumenukuu hadithi ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), ambaye alikamata shingo ya Ali (as) na akasema: “Huyu ni ndugu yangu na wasii wangu na Khalifa wangu juu yenu, kwa hiyo msikilizeni na mumtii.”

Muhammad ibn Hamid al-Razi ananukuu riwaya kama ilivyosimuliwa na Salmatul al-Abrash, kutoka kwa Ibn Is’haq, kutoka Abu Rabi’ah al-Ayadi, aliyeisikika kutoka kwa Ibn Burayda, kutoka kwa baba yake, Burayd aliyemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akisema: “Kwa kila Mtume kulikuwa na wasii na khalifa; wasii na khalifa wangu ni Ali ibn Abu Talib.”[273]

Na Tabraniy katika kitabu chake *al-Kabir* kwa kutaja sanadi mpaka kwa Salman al-Farisi, ambaye amesema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: “Wasii na mrithi wangu, msiri wangu na mbora zaidi wa wote watakaobaki nyuma yangu, na mtimizaji wa ahadi zangu na mlipa madeni yangu ni Ali ibn Abu Talib (as).”[274] Hadithi hii inathibitisha wazi kwamba Ali alikuwa ndiye wasii wa Mtume, na ni ushuhuda wa wazi kwamba yeye alikuwa ndiye mbora wa watu mwenye kuheshimika zaidi baada ya Mtume (s.a.w.w.). Kufikiria kwa makini zaidi hadithi hii pia kutaonyesha kwamba yeye alikuwa ndiye mrithi wa jumla, na utii kwake ulikuwa ni wajibu wa lazima kwa Umma mzima. Hafiz Abu Na’im, katika *Hilyat al-Awliya*,[275] anamnukuu Anas akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimuambia: “Ewe Anas! Wa kwanza kuingia katika mlango huu ni Imamu wa wachamungu, Kiongozi wa Waislamu, mlinzi wa dini (*Ya’asub al-Diin*), muhuri wa mawasii wa mitume, na kiongozi wa wale wenye nyuso zinazong’ara.” Anas anasema kwamba mara tu Ali akaingia kupitia mlango ule, na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akasimama kwa furaha sana, akapiga hatua moja mbele na kumkumbatia Ali na akamwambia: “Utalipa madeni yangu na kutekeleza majukumu yangu, utafikisha sauti yangu kwa watu, na kuelezea yale yote ambayo watahitilafiana baada yangu.”

Tabraniy amesimulia katika kitabu *Al-Kabir* yake akinukuu vyanzo vya kutegemewa hadithi kutoka kwa Abu Ayyub al-Answari ambaye anasema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimuambia Fatimah hivi: “Ewe Fatimah! Je, unajua kwamba Allah Aza wa Jallah, aliwatupia jicho wakazi wa ardhi na

---

[273] Al-Dhahbi ameinukuuhadthi hii wakati anajadili wasifu wa Shariik katika *Mizan al-I’tidal*, anaithibitisha na anamuona kwamba Shariik ni muongo na kwamba hakuisikia hadithi kutoka kwa mtu yoyote. Anasema pia kwamba: “Muhammad ibn Hamiid al-Razi sio muaminifu.” Jibu letu kwa shutuma hizo za Dhahabu ni kwamba Imamu Ahmad ibn Hanbal, Imamu Abul Qasim al-Baghwi, Imamu ibn Jarir al-Tabari, Imamu wa kukosoa na mthibitishaji Ibn Ma’in, na wengine wa rika lake, wote wamemuamini Muhammad ibn Hamiid na wamesimulia hadithi zake, hivyo yeye ni mshauri wao na wa kuaminika. al-Dhahabi mwenyewe anakiri uaminifu wake kwenye wasifu wa Muhammad ibn Hamiid katika kitabu chake *al-Mizan,* Mtu huyu hakuwahi kushutumiwa na Urafidh (mwenye kuwakataa makhalifa watatu wa mwanzo) au Ushia.Muhammad bin Hamiid pia ni mhenga wa al-Dhahabi. Inapokuwa anaonekana mwaminifu kwa muhadithina wakubwa, hivyo hakuna sababu ya kuanzisha shutuma kuhusiana na hadthi hii.

[274] Hadithi hii imesimuliwa kwa maneno yanayofanana na vyanzo vinavyofanana pia, ni hadithi ya. 2570 mwishoni mwa uk. 155, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*, na mwandishi anainukuu tena katika kitabu chake *Muntakhab al-Kanz;* iliyochapwa kwenye tanbihi ya *Musnad.* Tafadhali rejea uk. 32, Jz. 5, ya *Musnad Ahmad.*

[275] Kama ilivyoelezwa katika uk. 450, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul Balaghah*, na tumeinukuu Hadithi hii katika Barua ya 48.

akamchagua baba yako kutoka miongoni mwao na akamtuma kama Mjumbe Wake, kisha akatupa jicho mara ya pili na akamchagua mume wako na akaniteremshia wahyi nikuozeshe kwake na akamteua kuwa wasii wangu.?"[276]

Tazama jinsi Allah baada ya kumteua Mtume wa Mwisho, alivyomteua Ali (as) kutokana na wakazi wote wa ardhini, na kwamba aliteua wasii kama vile alivyomteua Mtume Wake na vilevile tazama jinsi Allah anavyomteremshia Mtume Wake wahyi kumwamuru kumuoza binti yake na kumteua kuwa wasii wake. Zingatia zaidi kwamba mitume waliotangulia walikuwa hawakurithiwa na wengine mbali na wale mawasii wao wenyewe. Je, ni sawa kumpa kipaumbele mtu mwingine na kumuweka kando [wakati linapokuja suala la kumchagua khalifa] mtu ambaye Allah amemteua miongoni mwa waja Wake, na ambaye alikuwa *Wasii* wa Bwana wa Mitume Wake? Je, ni sawa kwamba mtu mwingine achukue mamlaka na amtawale Wasii wa Mtume (s.a.w.w.) na amfanye tu kama mtu wa kawaida na raia wake? Je, unaweza kimantiki kutarajia kwamba mtu aliyeteuliwa na Allah kama vile alivyoteuliwa Mtume Wake, ni wajibu kwake kumtii au kutoa kiapo cha utii kwa mtawala aliyechaguliwa na watu? Je, ni sahihi kwetu sisi kwamba tumchague mtawala na kiongozi mbali na yule ambaye Allah Mwenyewe na Mjumbe Wake wamemchagua?

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا

**"Haiwi kwa muumini mwanaume wala muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, wakati Allah na Mtume Wake wanapokata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Allah na Mtume Wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi."** (Qur'ani, 33:36.)

Kuna hadithi na riwaya zilizosheheni zenye kueleza kwamba mara tu wale wanafiki na wenye husda, na wenye kutafuta masilahi walipofahamu kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), atamuozesha binti yake Fatimah az-Zahra (a.s.), Bibi wa wanawake wa Peponi na aliye sawa tu na Mariam (as) kwa Ali, walihuzunika sana na wakamuonea wivu, hususan wale ambao waliwahi kumposa na wakakataliwa na kukatishwa tamaa.[277]

Walisema kwamba hiyo ndoa ya Ali na Fatimah ilikuwa ni dalili ya kutunukiwa Ali hadhi ambayo hakuna mtu yeyote ambaye angeweza kuifikia, na hakuna ambaye angeweza kuwa na tamaa ya kuipata. Na walikusanya propaganda zao zote na kula njama ya kumfanyia hila. Waliwatuma wanawake zao kwa Bibi wa wanawake wa Ulimwengu (Fatimah) wakijaribu kumfanya amdharau na kumchukia Ali (a.s.). Katika yale waliyomwambia ni pamoja na kwamba Ali alikuwa mtu masikini asiye na kitu cha maana katika miliki yake. Lakini yeye, Fatima (a.s.) hakutikisika kwani alifahamu kabisa hila na njama zao na nia zao

[276] Hadithi hii imesimuliwa kwa maneno yanayofanana, na kwa msingi wa vyanzo vinavyofanana pia kama hadithi Na. 2541 ukurasa wa 153, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*, na pia imenukuliwa katika *Muntakhab al-Kanz*; hivyo rejea kwenye kitabu hicho kilichochapwa kwenye pambizo ya *Musnad Ahmad* uk. 31, Jz. 5.

[277] Ibn Abu Haatim amemnukuu riwaya kutoka kwa Anas ambaye amesema: "Abu Bakr na Umar walikuja kwa Mtume kumposa Fatimah, lakini Mtume alikaa kimya na hakuwapa jibu lolote; hivyo, walikwenda kwa Ali kumjulisha hili. Walimwambia Ali aende kumposa Fatimah. Muhadithina wengi wameinukuu kutoka kwa Ibn Abu Haatim. Ibn Hajar ameiandika mwanzoni mwa Sura ya 11 ya kitabu *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*. Mahali hapohapo amenukuu riwaya kama hiyo kutoka kwa Ahmad kwa nyororo ya wasimulizi mpaka kwa Anas. Na kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 12 ya Sura 11 ya *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*, Abu Dawuud al-Sajiastan amesimulia riwaya yenye maana kwamba Abu Bakr alimposa Fatima, na Mtume akageuzia mbali uso wake, kisha Umar naye akafanya kama hivyo, Mtume akageuzia mbali uso wake vilevile. Wote wakamwambia Ali naye akatoe posa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Ali amenukuliwa akisema: Abu Bakr na Umar walimposa Fatima kutoka kwa Mjumbe wa Allah, lakini yeye (s.a.w.w.) aliwakatalia. Kisha Umar akasema: 'Ewe Ali! Yule ni wa kwako.'" Hadithi hii imenukuliwa na Ibn Jariir ya Ali na amethibitisha kwamba ni sahihi, Al-Duulabi ameinukuu pia, huku akikiri usahihi wake katika kitabu *Dhurriyyatit-Tahira*, na ni hadithi Na. 6007 katika uk. 392, Jz. 6, wa *Kanz al-Ummal*.

mbaya na halikadhalika na zile za wanaume zao kutokana na kauli zao za usingiziaji. Licha ya yote haya, hakuwakosea katika njia yoyote ile, kwani hakuwapa jibu lolote lile. Mpaka lile walilomtakia Allah Aza wa Jallah na Mjumbe Wake liwe lilipotimia na akaolewa na Ali, hapo ndipo alipoona ni wakati muafaka kufanya hadhi, ubora na sifa a Amir wa Waumini (a.s.) zijulikane kwa watu wote ili kuwaaibisha na kuwafedhehesha maadui zake Ali (a.s.). Hivyo akasema: "Ewe Mjumbe wa Allah! umeniozesha kwa mwanaume masikini ambaye hamiliki chochote?" Yeye (s.a.w.w.) akamjibu katika njia iliyoelezwa hapo juu.

"Wakati Allah akitaka kutangaza wema wa mtu uliofichika Huuamrisha ulimi wa adui yake kuwa chanzo cha muonekano wake."

Al-Khatib ananukuu katika kitabu chake '*Muttafaq*' riwaya iliyoko katika msingi wa vyanzo vya kukubalika iliyosimuliwa na Ibn Abbas, akisema: "Wakati Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa anafungisha ndoa ya Fatima na Ali, Fatima alisema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Umeniozesha kwa mtu masikini ambaye hana kitu chochote.' Mtume (s.a.w.w.) akamuambia: 'Je, hufurahi kwamba Allah amechagua kutoka miongoni mwa wakazi ardhini watu wawili mmoja wao akiwa ni baba yako na mwingine ni mume wako?[278] Akizihesabu sifa za Ali, Al-Hakim, katika ukurasa wa 129, J. 3, wa kitabu chake *Al-Mustadrak*, anamnukuu Sariiji ibn Yunus akimpokea Abu Hafs al-Abar, ambaye amemnukuu al-A'mash kutoka kwa Abu Saalih, na akaishia na Abu Hurairah ambaye anamnukuu Fatima (as) akisema: "Ewe Mjumbe wa Allah! umeniozesha kwa mtu masikini ambaye hamiliki chochote?" Yeye (s.a.w.w.) akamjibu: "Ewe Fatimah! Je, hufurahi kwamba Allah Aza wa Jallah, aliwatupia jicho wakazi wa ardhi na akachagua watu wawili mmoja wao akiwa ni baba yako na mwingine ni mume wako?" Ibn Abbas vilevile amesema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimwambia Fatimah: "Hufurahi kwamba nimekuozesha kwa mtu ambaye ni wa kwanza kabisa miongoni mwa Waislamu katika kuukubali Uislamu na mtu ambaye amejaaliwa kuwa na ilmu zaidi yao wote na kwamba wewe ni Bibi wa wanawake wa umma wangu, kama Mariamu alivyokuwa Bibi wa umma wake? Je, hufurahi, Ewe Fatimah, kwamba Allah alitupa jicho kwa wakazi wa ardhi na akachagua watu wawili kutoka miongoni mwao; mmoja wao ni baba yako na mwingine ni mume wako?"[279]

Baada ya hapo ilikuwa ni desturi ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kwamba wakati wowote Bibi wa wanawake wa ulimwengu alipopatwa na shida yoyote alimkumbusha neema ya Allah na Mjumbe Wake waliyotunukiwa yeye kwa kumuoza kwa mtu mwema na bora kabisa wa Umma wake ili kumliwaza na kumuwezesha kustahimili kwa subira kabisa matatizo na dhiki zake na kusahau mabadiliko ya maisha. Na ikutosheleze wewe kwa ajili ya ushuhuda juu ya suala hili kile ambacho Imamu Ahmad amekieleza katika ukurasa wa 26, Juz. 5, wa kitabu chake *Musnad* ambako ananukuu hadithi moja makhususi iliyosimuliwa na Ma'qil bin Yasar ambayo kwayo Mtume (s.a.w.w.) inaripotiwa kwamba alimtembelea Fatima (a.s.) wakati alipokuwa anaumwa na akamwambia: "Unajisikiaje mpendwa wangu?" Yeye akajibu:

"Kwa jina la Allah, matatizo yangu yameongezeka, ufukara wangu umezidi kuwa mbaya kwa kiwango kisichovumilika, na ugonjwa wangu umeendelea kwa muda mrefu." Yeye (s.a.w.w.) akamwambia: "Bado hujaridhika kwamba nimekuozesha kwa mtu ambaye ni wa kwanza kuukubali Uislamu, mtu ambaye amejaaliwa ilmu zaidi, na mvumilivu kuliko wote?" Hadithi zinazohusiana na suala hili ni nyingi mno, na hakuna nafasi ya kuzieleza zote katika barua hii, Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

[278] Hadithi kwa maneno yanayofanana, pamoja na rejea zinazofanana, imeandikwa kama hadthi Na. 5992 uk. 391, Jz. 6, ya Kanz al-Ummal, miongoni mwa ubora na sifa za Amirul-Mu'minin (a.s.) na mkusanyaji ameeleza kwamba imesimuliwa kupitia vyanzo vya kuaminika.

[279] Hadithi hii kwa maneno yanayofanana, pamoja na nyororo ya wasimuliaji inayofanana, ni hadithi Na. 2543 uk. 153, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal,* ambako imenukuliwa kutoka kwenye nyororo hadi kwa Ibn Abbas na Abu Hurayrah. Na pia imenukuuli kukota Tabraniy na kutoka kwa al-Khatib ambaye anamnukuu vyanzo hadi kwa Ibn Abbas. Tafadhali rejea msitari wa kwanza wa tanbihi uk.39, Jz. 5, ya *Musnad* ya Ahmad. Na ibn Abil-Hadiid ameinukuu kutoka kwenye *Musnad Ahmad* kwenye uk. 451 Jz. 2 ya *Sharh Nahjul-Balaghah*.

# BARUA YA 69

## SAFAR 10, 1330 A.H.

**Hoja Inayokataa Kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Ameacha Wosia.**

Ahlus-Sunnah wal-Jama'ah wanakataa kwamba Mtukufu Mtume aliacha wosia wowote kuhusu mrithi wake na kwa kuunga mkono kanusho lao wanarejea kwenye kile alichokisimulia al-Bukhari katika *Sahih* yake ambapo anamnukuu al-Aswad akisema: "Wakati fulani ilisemwa kwa Aisha (ra) kwamba Mtume (s.a.w.w.) amefanya wosia kuhusiana na Ali,[280] na akajibu kwa mshangao: 'Nani kasema hivyo? Nilimuona Mtume (s.a.w.w.) wakati wa kifo chake. Nilikuwa namsaidia kifuani mwangu. Aliomba aletewe dishi la kunawia na akaliegemea; na akafariki bila mimi kuelewa. Je kweli ilikuwa ni rahisi kwa mazingira kama hayo kufanya wosia kwa fadhila ya Ali?'"[281] Na Bukhari tena amesimulia katika Sahih yake kwa wakati mwingine Aisha alikuwa akisema: "Mjumbe wa Allah alipumua pumzi yake ya mwisho akiwa baina ya tumbo na chini ya kidevu changu," na mara kwa mara amenukuliwa akisema: "Alifariki wakati akiwa amejinyoosha kifuani kwangu," na aliweza kusema: "Kichwa chake kiko juu ya mapaja yangu wakati Malaika wa mauti alipomshukia."[282] Katika mazingira haya, kama Mtume angetoa wosia, basi Aisha lazima angeufahamu. Katika *Sahih Muslim*, katika Kitabu cha wosia uk.14, Jz. 2, mwandishi anamnukuu Aisha akisema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) hakuacha dinari wala dirham, wala kondoo au ngamia, wala hakuacha wosia wowote." Katika *sahihi* zote mbili, Bukhari na Muslim zimesimulia kwamba Talha ibn Masrif alimuuliza Abdullah ibn Awfah: 'Je, Mtume (s.a.w.w.) aliteua wasii yoyote?' Alijibu: 'Hapana.' Nikamuuliza: 'Imekuwaje hivyo?" Talha akaendelea kusema: 'kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaamrisha watu kuandika wosia wao wakati yeye mwenyewe hakufanya hivyo?' Ibn Awfi akajibu: 'Yeye alitoa wosia wake kuhusiana na Qur'ani, Kitabu cha Allah.'"

Kwa vile hadithi hizi zimeandikwa na Muslim na Bukhari, na kwamba zenyewe ni sahihi zaidi kuliko ulizoonesha, kwa hiyo umuhimu na mategemeo lazima viwekwe mbele katika kuamua mzozo huu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

[280] Hadithi hii imeandikwa kwenye *Sahih Bukhari*, Mlango wa Wasia Jz. 2, uk. 83 na pia kwenye Mlango wa Maradhi na Kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Jz. 3, uk. 64. Na katika *Sahih Muslim*, Kitabu cha Wasia, Jz. 2, uk. 14.

[281] Unaweza uwe hutambui kwamba katika hadithi hii Masheikh wawili hawa (Bukhari na Muslim) wameurejea wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu Ali (a.s.) bila ufahamu kabisa. Wangefanya fikra japo kidogo wangeiacha moja kwa moja hadithi hii, kwani wale watu ambao walitaja wosia wa Mtukufu Mtume kwa fadhila za Ali mbele ya Aisha hawakuwa nje ya Uislam. Walikuwa ama ni Masahaba au wafuasi wao na walikuwa na ujasiri wa kutaja mbele ya Ummul-Mu'minin Aisha yale yasiyompendeza na yaliyo kinyume na mwelekeo wa kisiasa wa wakati ule. Aisha, Mungu amrehemu, kwa hiyo alifadhaika kwa kutajwa wasia huu na ili kuupinga kabisa au kuufanya uonekene usio wa kweli, yeye alianza kutoa kauli zisizo na maana na msingi wowote. Kuhusiana na hili tafadhali rejea maelezo juu ya hadithi hii, yaliyotolewa na Imam as-Sadiq (a.s.) ndani ya *Sunan Nisai* Jz. ya 6, uk. 241 iliyochapwa Matbat ul Misriya, Azhar. Yeye anasema:Naifahamike kwamba hadithi hii haimaanishi kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alifariki ghafla hivyo au bila kutegemea na kwamba hakuweza kupata muda wa kutoa wasia. Hilo ni jambo lisilofikirika kabisa. Na kwa nini iwe hivyo wakati yeye (s.a.w.w.) alikibashiri kifo chake kabla ya maradhi yake, na halafu akaja akaugua na akajua kwamba anazo siku chache bado za uhai duniani hapa. Kama ukiipitia kwa uangalifu makala hii utaikuta timamu kabisa na yenye kudhihirisha ukweli.

[282] Maneno ya Aisha kwamba: "Alivuta pumzi zake za mwisho magotini kwangu" na "alifarika akiwa ameegea kwenye shingo na kifua changu" yanakutikana katika mlango wa 'Maradhi na Kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)' ndani ya *Sahih Bukhari*, ambapo maneno "Kichwa chake kilikuwa juu ya paja langu pale Malaika wa Mauti alipomshukia" yanatokeza mara tu katika mlango unaofuatia "Maneno ya mwisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)" katika kitabu hichohicho.'"

# BARUA YA 70

## SAFAR 11, 1330 A.H.

**1. Kufanya Wosia kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Hakukanushiki,**
**II. Sababu ya kukataliwa Wasia,**
**III. Riwaya ya Talha bin Masrif ndani ya Bukhari sio hoja Dhidi yetu,**
**VI. Mantiki na Kipawa cha Kufikiri Vinathibitisha kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Alitoa Wosia.**

Kwamba Mtukufu Mtume aliacha Wosia wa kuhusu Ali ni jambo ambalo haliwezi kukanushwa kwa hali yoyote. Hili limethubutu bila shaka kwamba Mtukutu Mtume (s.a.w.w.) baada ya kumtangaza Ali (a.s.) kama mrithi wa ilmu na hekima yake,[283] alichukua ahadi kutoka kwake kwamba atakuja kukosha maiti yake, kuivisha sanda na kuizika,[284] na kulipa madeni yake, na kutekeleza ahadi yake kwa niaba yake, kuchukua wajibu na majukumu yake baada ya kifo chake[285] na katika kuhitalifiana

[283] Tafadhali rejea barua yetu ya 66 ambamo utakuta maelezo ya jinsi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alivyomteua Ali (a.s.) kuwa mrithi wa elimu na hekima zake.

[284] Katika ukurasa wa 61, Sehemu ya Pili, Ibn Sa'd katika kitabu chake *Tabaqat* anasimulia kwamba Ali (a.s.) alisema: "Katika wosia wake, Mtume (s.a.w.w.) kwangu mimi ameniamuru kwamba hakuna mtu yeyote isipokuwa mimi ndio nimuoshe [josho la maiti]." Wote Abul Sheikh na Ibn Hajjar, kama ilivyoelezwa katika uk. 54, Jz. 4, ya *Kanz al-Ummal*, wamemnukuu Ali akisema: "Mjumbe wa Allah (saw) ameniusia mimi akisema: 'Wakati nitakapokufa uje unioshe kwa tumia viriba (vya ngozi) saba vya maji." Katika maelezo yake juu ya josho lake la mwisho la Mtume (s.a.w.w.), Ibn Sa'd katika uk. 63, Sehemu ya Pili ya Jz. 2, ya *Tabaqaat* yake, amenukuu riwaya ya Abdul Walid bin Abu Awanah akisema kwamba wakati Mjumbe wa Allah (saw) alipoangushwa na maradhi kabla ya kifo chake alisema: "Ewe Ali! Nitakapokufa unioshe wewe." Amemnukuu Ali pia akisema: "Hivyo nilishughulika mimi katika kumuosha, na kila sehemu ya mwili wake niliyokusudia kuinyanyua ilijiinua mara moja kwa mguso wangu." Wote al-Hakim katika uk. 59, Jz. 3, ya *Al-Mustadrak*, na al-Dhahabi katika *Talkhis al-Mustadrak*, baada ya kunukuu mfululizo wote wa vyanzo wamesimulia na kuthibitisha kwamba ni riwaya ya Ali ambaye amesema: "Nilimuosha Mjumbe wa Allah josho lake la mwisho. Nilikuwa na shauku ya kuona kama maiti yake itakuwa kama maiti nyinginezo lakini sikuona lolote kama hilo; mwili wake ulinukia manukato kama ulivyokuwa ukunukia wakati wa uhai wake." Hadithi hii imenukuliwa na Sa'id bin Mansuur katika *Sunan* yake na al-Maruuzi katika kitabu chake *Jana'iz*, Abu Dawd katika *Murasiil,* Ibn Ma'ni, Ibn Abu Shaibah katika *Sunan* zao, na ni hadithi ya 1094, katika uk. 54, Jz. 4, ya *Kanz al-Ummal*; Al-Bayhaqi, katika Sunan yake, anamnukuu Abdullah ibn al-Harith akisema: "Ali alimuosha Mtume (s.a.w.w.) josho lake la mwisho wakati mwili wake ukiwa umevalishwa kanzu" na hii ni hadithi ya 1104, uk. 55, Jz. 4 ya *Kanz al-Ummal,* na Ibn Abbas ananukuliwa akisema: "Ali ana sifa nne ambazo hakuna mtu aliyekuwa nazo: alikuwa wa kwanza kuswali pamoja na Mjumbe wa Allah; alikuwa kamanda wa vita vyote wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.); alibaki naye na kumlinda wakati wengine walikimbia kuokoa maisha yao, na ndiye aliyemuosha (Mtume) josho lake la mwisho na kumlaza kaburini." Hii imenukuliwa na Ibn Abd al-Birr katika maelezo yake juu ya Ali kwenye kitabu chake, *Isti'ab*, na al-Hakim katika ukurasa wa 111, Jz. 3, ya *Al-Mustadrak*. Vilevile anamnukuu Abu Sa'id al-Khudri akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), amemuambia Ali: "Ewe Ali! Wewe ndiye utakayeniosha, kulipa madeni yangu, na kuniweka kaburini." Hii pia imenukuliwa na al-Daylami, na ni hadthi ya 2583, uk. 155, Jz. 4, ya *Kanz al-Ummal*. Umar ananukuliwa akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amemuambia Ali: "Ewe Ali! Utaniosha na kunizika," hadithi hii imapatikana katika uk. 393, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*. Katika tanbihi ya ukurasa wa 45, Jz. 5, *Musnad* ya Imamu Ahmad Hanbal, Ali ananukuliwa akisema: "Nimemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: 'Nimepewa mambo matano ndani ya Ali ambayo hakuna Mtume yeyote kabla yangu aliyepewa, la kwanza ni kwamba yeye ndiye atakayelipa madeni yangu na kunizika…" mpaka mwisho wa hadithi iliyonukuliwa mwanzoni mwa ukurasa wa 403, Jz. 6 ya *Kanz al-Ummal*. Na wakati baada ya josho na kukafiniwa mwili wa Mtukufu Mtume ulipowekwa kwenye jeneza na watu wakataka kumswalia, Ali akasema: "Hakuna mtu yeyote atakayekuwa Imamu wa swala hii, kwani yeye Mjumbe wa Allah ni Imamu wenu akiwa hai na maiti." Watu waliingia kwa makundi na kuswali wakimama katika safu bila ya Imamu. Walisoma takbira '*Allahu Akbar'* wakati Ali akiwa amesimama karibu na jeneza la Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akisema: "Amani iwe juu yako, Ewe Mtume, na rehema na baraka za Allah zikushukie wewe. Tunashuhudia, Ewe Mola kwamba ametufikishia kile ulichomtuma nacho kwetu, amefanya kila aliloweweza kwa ajili ya ustawi wa umma, na amejitahidi na kupigana katika njia ya Allah mpaka Yeye Aza wa Jallah akaiimarisha imani yake aliyoilingania, na akakamilisha neno lake (Wito wa dini). Ewe Mola! Tujumuishe sisi miongoni mwa wale ambao wanafuata amri zako ulizoteremsha kupitia kwake, tufanye imara baada yake, na ziunganishe nafsi zetu kuwa pamoja naye." Na watu waliitikia "Amin, Amin." Hii iliendelea mpaka wanaume walipomaliza swala zao, kisha wanawake, kisha watoto. Hadithi imenukuliwa kwa maneno yanayofanana na Ibn Sa'd katika kuelezea josho la mwisho la Mtukufu Mtume *Tabaqat* yake. Wa kwanza kuingia kumswalia ni Bani Hashim, kisha *Muhajirun* (wahamiaji kutoka Makka) kisha *Answar* (wenyeji wa Madina), kisha watu wengine. Watu wa kwanza ambao waliswalia jeneza ni Ali na al-Abbas ambao walisimama kila mmoja katika safu na wakasoma takbira tano.

[285] Simulizi kuhusiana na hili zimewasilishwa kwa mfululizo wa kufuatana kutoka kwa kizazi kitoharifu (a.s). Lakini kwa riwaya zilizosimuliwa

maoni[286] baada yake kuwaeleza watu kuhusiana na amri na maamrisho ya Allah Aza wa Jallah na sheria zote za dini. Vilevile aliuaminisha umma kumchukua Ali (a.s.) kama *Maula* wao,[287] na kwamba Ali alikuwa ni ndugu yake,[288] baba wa watoto wake,[289] waziri wake[290] msiri wake,[291] mtekelezaji wa wosia

---

na kuandikwa kwenye vyanzo mbali na vya Ahlul-Bayt (a.s.) ikutoshe tu riwaya iliyonukuliwa katika *Mu'ajami Kabir* ya Tabraniy kutoka kwa Ibn Umar, na riwaya iliyoandikwa na Abu Ya'ali katika *Musnad* yake kutoka kwa Ali (as). Kwa mujibu wa Tabrani, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amesema: "Ewe Ali! Wewe ni ndgu yangu na waziri wangu, na utalipa madeni yangu kwa niaba yangu, na kutekeleza ahadi, wajibu na majukumu yangu." Unaweza kuiona hadithi hii kwenye uk. 155, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal* ikinukuu vyanzo hadi kwa Ibn Umar, tena katika uk. 404 wa rejea hiyo hiyo, Ali (a.s.) ananukuliwa akisema hivyo hivyo. Katika sehemu hiyohiyo imeelezwa kwamba Allamah Busairi amethibitisha kwamba wasimuliaji wote wa hadithi hii ni waaminifu. Na kama ilivyoelezwa kwenye uk. 155 wa Jz. 6 ya *Kanz ul Ummal*, Ibn Mardawayh na al-Daylami, wamesimulia hadithi kama ilivyopokelewa na Salman Farsi akisema kwamba Mjumbe wa Allah (saw) alisema:*** "Ali ibn Abu Talib atatekeleza wajibu wangu kwa niaba yangu na analipa madeni yangu." Riwaya kama hiyo imesimuliwa na Al-Bazzaz, kutoka kwa Anas ilivyoelezwa katika uk. 153, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*, Vilevile imenukuliwa na Imamu Ahmad ibn Hanbal kwenye uk. 164, Jz. 4, ya *Musnad* yake kutoka kwa Habashi ibn Janadah ambaye anasema: "Nimemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Hakuna mtu yeyote alipaye madeni yangu ispokuwa mimi mwenyewe au Ali." Ibn Mardawayh kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 401, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*, anamnukuu Ali (as) akisema kwamba wakati aya ya **"waonye jamaa zako wa karibu"** ilipoteremshwa, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akasema: "Ali atalipa madeni yangu na kutekeleza ahadi yangu kwa niaba yangu." Sa'd anasema kwamba katika siku ya Juhfa Mjumbe wa Allah (saw) akiwa amemshika Ali kwa mkono wake, alitoa khutba; alimshukuru na kumtukuza Allah, kisha akasema: "Enyi watu! Mimi ni *Walii* (mlinzi) wenu." Wakasema: "Umesema kweli, Ewe Mjumbe wa Allah." Kisha akanyoosha mkono wa Ali na akasema: "Huyu ndiye mtu aliyechaguliwa kuwa *walii* wangu; atalipa madeni yangu kwa niaba yangu." Umeisoma riwaya hii mwishoni mwa barua ya 54. Na Abdur Razzaq ameandika katika Jam'ii riwaya kutoka kwa Muammar aliyeisikia kwa Qatadah kwamba amesema: "Ali ametekeleza majukumu fulani baada ya Mtume (saw) (kwa niaba ya Mtume) mengi ya hayo yalikuwa ni ahadi na mikataba ya Mtume (s.a.w.w.). Nadhani alitaja deni lenye thamani dirham laki tano ambazo Ali alizilipa." Abdul-Razaq aliulizwa: "Je, Mtume (s.a.w.w.) aliacha wosia kuhusiana na jambo hili?" Alijibu: "Ndio. Sina shaka kabisa na hilo, kwamba Mtume (s.a.w.w.) kwa kweli aliacha wosia kwa Ali, vinginevyo hakuna mtu yeyote ambaye angemuacha alipe madeni yote ya Mtume yeye mwenyewe." Hadithi hii imenukuliwa na mwandishi wa *Kanz al-Ummal* kwenye ukurasa wa 60, Jz. 4, ambayo ni hadthi ya 1170.

286 Kuna hadithi sahihi zinazothibitisha kwamba Mtume (s.a.w.w.) ameusia kwamba baadaa yake Ali (a.s.) atawaongoza watu na kuufafanulia umma wake masuala yenye utata wowote wanapohitilafiana katika masuala ya dini. Ikutoshe tu kwa ajili ya uthibitisho hadithi namba 11 na 12 zilizonukuliwa katika Barua ya 48. kuna riwaya nyingi ambazo zinaunga mkono ukweli huu ambazo baadhi tayari zimekwishanukuliwa, halikadhalika na nyingine hatukuzinukuu kutokana na kuwa kwao mashuhuri.

287 Hii imeelezwa katika Barua ya 36, 40, 54 na 56 hapo juu.

288 Undugu kati ya Mtume na *wasii* wake umethibitishwa *(mutawatir)* vya kutosha katika Barua ya 32 na 34 ambazo unaweza kuzirejea tafadhali

289 Kuwa kwake baba wa watoto wake kunaungwa mkono na weledi. Mtume (s.a.w.w.) alimuambia Ali (as): "Wewe ni ndugu yangu, na baba wa watoto wangu, utapigana kwa ajili ya utetezi wa *Sunnah* yangu." Hadithi hii imenukuliwa na Abu Ya'li katika *Musnad* yake, kama ilivyoelezwa kwenye uk. 404, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*, na kama ilivyoelezwa na al-Busairi wasimuliaji wake wote ni waaminifu. Vilevile imenukuliwa katika *Manaqib* ya Ahmad, kama ilivyoelezwa katika hitimisho la Sehemu ya Pili ya Sura ya 9 uk. 75, wa *Al-Sawa'iq* ya Ibn Hajar. Mtume (s.a.w.w.) vilevile amesema: "Allah ameweka kizazi cha kila Mtume katika kiuno chake mwenyewe, ambapo ameweka cha kwangu katika kiuno cha Ali." Hadithi hii imenukuliwa na Tabraniy katika *Mu'ajam Al-Kabir* kama ilivyosimuliwa na Jabir, na al-Khatiib katika *Tarikh* kutoka kwa Ibn Abbas. Ni hadithi ya 2510, uk. 152, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*. Na Mtume (saw) pia alisema: "Watoto wa mwanamke hunasabishwa kizazi cha kiumeni isipokuwa kizazi cha Fatima, kwani mimi ni mlezi na jadi ya kiumeni na baba yao." Hii imenukuliwa na Tabraniy kutoka kwa al-Zahra (a.s.) na ni hadithi ya 22, Sehemu ya Pili, Sura ya 11, uk. 121 wa *al-sawa'iq al-Muhriqa* ya Ibn Hajar. Vilevile imenukuliwa na Tabraniy kutoka kwa Ibn Umar kama ilivyotajwa kwenye ukurasa huohuo. Al-Hakim ananukuu hadidhi kama hiyo katika uk. 164, Jz. 3, ya *Al-Mustadrak*, kutoka kwa Jabir na akiongeza kwamba wasimuliaji wa hadithi hii ni waaminifu, ingawa Bukhari na Muslim hawakuiandika. Mtume (s.a.w.w.) amesema katika hadithi moja iliyonukuliwa na al-Hakim katika *Al-Mustadrak*, na al-Dhahabi katika *Talkhis al-Mustadrak*, wote wanakiri usahihi wake kwa vipimo vya Masheikh wote wawili [Bukhari na Muslim] kuhusiana na (kauli ya Mtume) "Ewe Ali, kwa hakika u ndugu yangu na baba wa watoto wangu, wewe watokana na mimi na kwa ajili yangu." Kuna hadithi sahihi nyingi kuhusiana na mada hii.

290 Miongoni mwa ushahidi unaoridhisha juu ya Ali kuwa waziri ni kauli yake Mtume (s.a.w.w.): "Wewe kwangu una cheo sawa na kile cha Harun kwa Musa," kama tulivyoeleza katika Baru ya 26 na kadhalika. Na hadithi ya "Kuwaonya watu wa nyumbani kwake;" ambamo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Nani basi, miongoni mwenu atakayenisaidia katika kazi yangu hii?" Ali alijibu: "Mimi hapa, Ewe Mjumbe wa Allah, nitakuwa msaidizi wako katika suala hili," kama ilivyonukuliwa katika Barua yetu ya 20. Allah ambariki Imamu al-Busairi kwa shairi lake zuri ambalo beti zake zina maana kwamba Ali alikuwa mshirika katika kazi mashuhuri na Tukufu ya binamu yake na alikuwa ni waziri aliyefaa na kustahiki kabisa. Imani yake ilikuwa kamilifu, na kufunuliwa mapazia kusingeweza kuisahihisha au kuiongeza. Yeye mwenyewe alikuwa ni jua lisilokuwa na au kujua mapazia..

291 Umma wote wa Kiislam unakubaliana kwa pamoja kwamba kuna aya moja katika Kitabu cha Allah ambayo haikutekelezwa na yeyote isipokuwa Ali mpaka Siku ya Hukumu. Ni aya ya *Najwa* (yaani siri) katika Surat al-Mujadila; 58:12. Hii fatwa inayokubaliwa na wote marafiki zake na wapinzani wake ambao wananukuu kuhusiana na hili, riwaya nyingi zinazochukulia kuwa ni sahihi kwa mujibu wa masheikh wote wawili, Bukhari na Muslim, ambazo zinajulikana kwa wachamungu au wakware miongoni mwa Ummah. Na kuhusiana na hili tafadhali rejea kile ambacho kimenukuliwa na al-Hakim kwenye uk. 482, Jz. 2, ya *al-Mustadrak* yake, na al-Dhahabi katika ukurasa huo huo katika *Talkhis al-Mustadrak*. Vilevile rejea kwenye vitabu vya tafsir vilivyoandikwa na Thalabi, al-Tabari, al-Suyyuti, al-

wake,[292] mlango wa mji wa ilmu yake,[293] Mlango wa ghala ya hekima yake,[294] mlango wa maghfira kwa ajili ya umma huu[295] na usalama wake, na jahazi la wokovu[296] na kwamba kumtii Ali ni wajibu wa lazima kwa Umma kama kumtii Mtume mwenyewe: kumuasi yeye kunaangamiza[297] sawa na kumuasi Mtume kunavyoangamiza Kumfuata yeye Ali ni sawa na kumfuata Mtume; kujitenga na yeye ni sawa na kujitenga na Mtume,[298] na kwamba yeye (Mtume) yuko katika amani na yeyote yule ambaye yuko katika amani na Ali, na ana uhasama na yeyote yule ambaye ana uhasama[299] na yeye Ali, ni rafiki wa yeyote yule ambaye ni rafiki yake na adui wa yeyote yule ambaye ni adui yake;[300] ambaye anampenda yeye amempenda Allah na Mjumbe Wake (s.a.w.w.), na anayemchukia Ali amemchukia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (s.a.w.w.).[301] Na yeyote yule aliye rafiki yake ni rafiki wa wote pamoja, na yeyote anayempinga kwa kweli huwapinga wote pamoja,[302] na yeyote anayemdhuru yeye anawadhuru wote pamoja[303] pia; yeyote anayemtusi, kumshutumu na kumfedhehesha kwa kweli anamtusi Allah na Mjumbe Wake (s.a.w.w.).[304] Yeye kwa hakika ni Imamu wa wamchao Mungu na muangamizaji wa waovu; yeyote mwenye kumsaidia atakuwa mshindi, na ambaye anamtelekeza atakuwa ni mwenye kushindwa.[305] Ni bwana wa Waislamu na Imamu wa watu wema, kiongozi wa wale wenye nyuso angavu kuelekea Peponi.[306] Ni bendera ya mwongozo, kiongozi wa mawalii na vipenzi wa Allah, na mwanga kwa ajili ya watiifu wa Allah, na ndio neno ambalo Allah ameliamuru kama ni wajibu juu

Zamakhshari, al-Razi na wengine. Katika Barua ijayo ya 74 utazikuta hadithi mbili zilizosimuliwa na Umm Salamah na Abdullah bin Umar kuhusu minong'ono ya siri kati ya Mtume (s.a.w.w.) na Ali (a.s.) punde tu kabla ya kufariki kwa Mtume. Inawezekana ukaelewa kwamba yalikuwepo majadiliano ya siri kama hayo kule Ta'if na kauli ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) wakati huo: "Sio mimi niliyemnong'oneza bali ni Allah ndiye aliyefanya hivyo, ambaye mimi nimeitii amri Yake," na vilevile tutaonyesha kwamba kulikuwa na mnong'ono wa siri kati yao kuhusu Aisha.

292 Na kuhusu Ali kwamba ni *wasii* na rafiki yake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) utakuta uthibitisho wa kutosha katika riwaya iliyosimuliwa na Ibn Abbas na imetajwa kwenye Barua ya 26: "Wewe ni *wasii* na rafiki yangu katika dunia hii na ya Akhera." Hadithi hii inatambulika sana miongoni mwa Waislamu, kwa hiyo, hakuna haja ya kuendelea kueleza kwa urefu. Na kuhusu utekelezaji wa wosia wake, tafadhali rejea hadithi kuhusu hili iliyotajwa kwenye Barua ya 68.

293 Tafadhali rejea hadithi ya 9 katika barua ya 48 na tanbihi yetu hapo.

294 Tafadhali rejea hadithi ya 10 katika barua ya 48.

295 Tafadhali rejea hadithi ya 14 katika barua ya 48.

296 Kama ilivyothibitishwa na hadithi zilizonukuliwa katika barua ya 48.

297 Kama ilivyothibitishwa na hadithi ya 16 iliyonukuliwa kwenye barua ya 48.

298 Kama ilivyothibitishwa na hadithi ya 17 iliyonukuliwa katika barua ya 48.

299 Imamu Ahmad Hanbal imenukuuu katika uk. 442, Jz. 2, ya *Musnad* yake hadithi moja kutoka kwa Abu Huraira ambaye anasema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimtazama Ali, Fatima, al-Hasan na al-Husein, amani iwe juu yao wote, kisha akasema: "Mimi ni adui kwa yeyote ambaye ana uadui kwenu ninyi, na nina amani kwa yeyote yule aliyeko kwenye amani na ninyi." Katika hadithi nyingine sahihi, Mtume (s.a.w.w.) vilevile alisema wakati walipowafunika na shuka (Kisaa): "Mimi ni adui kwa yeyote yule anayepigana nao, na amani juu ya yule ambaye yuko kwenye amani nao." Hadithi hii imewasilishwa na Ibn Hajar wakati alipokuwa anaelezea aya ya kwanza kati ya zile alizoorodhesha juu ya fadhaili na heshima ya Ahlul-Bayt (a.s.) katika Sehemu ya kwanza, sura ya 11 ya *Al-Sawa'iq al-Muhriqa*, Na maneno ya Mtume (s.a.w.w.): "Kupigana na Ali ni kupigana na mimi, na kufanya amani na Ali ni kufanya amani na mimi." Ni maarufu sana

300 Rejea kwenye hadithi ya 20 katika barua ya 48. Zaidi ya hapo, kauli yake ya mfululizo: "Ewe Mola! Mpende yeyote mwenye kumpenda yeye, na umchukie mwenye kumchukia yeye" ni uthibitisho tosha juu ya hilo. Sifa njema zote ni zake Allah. Umeona kwenye Barua ya 36 kauli yake (s.a.w.w.) kama ilivyonukuliwa na Buraydah: "Yeyote mwenye kumchukia Ali ananichukia mimi pia, na yeyote mwenye kujitenga na Ali amejitenga na mimi pia." Hadithi nyingine *mutawatur* ni kauli yake (s.a.w.w.): "Hakuna yeyote ampendaye Ali isipokuwa muumini, na hakuna yeyote amchukiaye isipokuwa mnafiki," imesimuliwa mfululizo na ni maarufu inayoaminika kwamba ni sahihi. Wallahi hili limehakikishwa na Mtukufu Mtume Ummi (s.a.w.w.)

301 Kama ilivyothibitishwa na hadithi ya 19, 20 na 21 katika barua ya 48 na kadhalika.

302 Kama ilivyothibitishwa na hadithi ya 23 katika barua ya 48. pia maneno yake "Ewe Allah! Mpende yule anayempenda Ali na mchukie mwenye kumchukia" yanathibitisha hilo.

303 Iangalie kauli yake (s.a.w.w.), ambayo imenukuliwa na Umar ibn Shas: "Yeyote yule anayemuumiza Ali huniumiza mimi pia," ambayo imenukuliwa na Ahmad katika uku. 483, Jz. 2, ya *Musnad* yake, na al-Hakim katika ukurasa wa 123, Jz. 3, ya *Al-Mustadrak*, na al-Dhahabi katika *Talkhis al-Mustadrak* ambako anakiri usahihi wake. Al-Bukhari ameinukuu katika kitabu cha *Tarikh*, Ibn Sa'd katika *Tabaqat* yake, Ibn Abu Shaybah katika *Musnad* yake, na Tabraniy katika *Mu'ajam al-Kabir*, pia ipo kwenye uk. 400, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal.*

304 Kwa mujibu wa hadithi ya 18 yaliyoorodheshwa katika barua ya 48 na kadhalika.

305 Kwa mujibu wa hadithi ya kwanza iliyooneshwa katika barua 48 na kadhalika.

306 Tafadhali rejea kwenye hadithi ya 2 hadi ya 6 katika barua ya 48.

ya wachamungu.[307] Na yeye ni *Siddiq* mkuu, mbainishaji (*Faruuq*) wa haki na batili wa Umma, na Amiir wa waumini.[308] Yeye ni Upambanuzi Mkuu *(Furuqan Adhim)* na Ukumbusho wa Hekima[309] na ana cheo kwa Mtume (s.a.w.w.) kama alivyokuwa Harun kwa Musa.[310] na yeye kwa Mtume ni kama vile Mtume alivyo kwa Mola Wake,[311] na ni kama kichwa katika mwili,[312] na kwa hakika yeye ni kama nafsi au roho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).[313] Allah Aza wa Jallah alitupa jicho kwenye wakazi wa Ardhi na akawachagua wao[314] (Muhammad na Ali ) kutoka miongoni mwao.

Tafadhali hebu tafakari juu ya meneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyoyasema kule Arafat wakati wa Hija Mwago kwamba: "Hakuna mtu yeyote mwingine awezaye kutekeleza wajibu wangu (kama Mtume) isipokuwa mimi mwenyewe au Ali.[315] Mbali na hayo hapo juu kuna hadithi nyingine nyingi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambamo amemtaja Ali kwa sifa nyingi moja moja zinazomfanya awe si mwingine ile ni bali ni *wasii*, na zinazomstahiki tu mwakilishi ama mrithi. Anaweza vipi mtu yeyote mwenye busara kuzipuuza riwaya hizi, na ni vipi kimantiki atakataa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuacha wosia huo kwa fadhila ya Ali na kumteua kama mrithi wake? au kuwa mkaidi kiasi cha kuishikilia kwamba haina maana? Na wosia ni jambo la umuhimu wa hali ya juu.

Sababu ya Ahlus Sunnah kuukataa wosia huu ni hofu yao kwamba urithi wa makhalifa watatu wa kwanza hauendani na imani iliyoko kwenye wosia huo unaompendelea Ali (a.s.).

Hatuwezi kuiamini kwamba ni sahihi ile riwaya iliyosimuliwa na al-Bukhari kutoka kwa Talha ibn Masrif kwamba alimuuliza Abdullah bin Awfah kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliacha wosia wowote, na Abdullah akajibu kwamba hapana hakuacha, hapo Talha bin akaonyesha mshangao kwamba vipi Mtume (s.a.w.w.) aliwaamrisha watu kuandika wosia wao wakati yeye mwenyewe hakufanya hivyo, na Abdullah akajibu kwamba alifanya wosia wake kuhusu Kitabu cha Allah, Qur'ani. Hadithi hii haikusimuliwa wala kuthibitishwa kupitia vyanzo vya Shi'ah, hivyo kwamba haiwezi kusimamishwa kama hoja sahihi dhidi yetu. Badala yake imeelezwa vibaya kwa hadithi na utoaji wa hadithi bandia za ubunifu uliofanywa kwa shinikizo la baadhi ya wanasiasa waliokuwa madarakani. Zaidi ya hayo kuna hadith *sahih* za kizazi kitoharifu ambazo ni *mutawatir* zinazothibitisha suala hili; kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliacha wosia wa urithi kuhusu Ali. Kwa hiyo tunazikataa kauli zote pinzani. Kadhalika suala la Mtume kuacha wosia kwa ajili ya Ali ni mashuhuri sana na halihitaji hoja zaidi. Kwa upande mwingine mantiki na upeo wa fikra[316] vyote vinathibitisha kwamba yeye (s.a.w.w.) aliacha wosia. (Kama mtu atarefusha kitu, husimama chenyewe. Kwani sifa za mwanga wa jua huondoa batili).

---

[307] Tafadhali rejea kwenye hadithi ya 6 katika barua ya 48.

[308] Kwa mujibu wa hadithi ya 7 katika barua ya 48 na kadhalika.

[309] Umekwisha kusoma hadithi sahihi zinazothibitisha hili katika barua ya 8. Kwa mtu mwenye umaizi, kuzipitia hadithi hizi hakuachi nafasi yoyote ya shaka. Na katika barua ya 50 imenukuliwa pia hadithi ya: "Ali yuko pamoja na Qur'ani, na Qur'ani ipo pamoja na Ali. Viwili hivi havitatengana.

[310] Kama ilivyofafanuliwa katika barua ya 26, 28, 30, 32 na 34.

[311] Kwa mujibu wa hadithi namba 13 katika barua ya 48.

[312] Kwa mujibu wa hadithi tuliyoinukuu katika barua ya 50, Tafadhali irejee hadithi hiyo.

[313] Kwa mujibu wa aya ya Mubahala na hadithi iliyosimuliwa na Ibn Awf ambayo tumeinukuu katika barua ya 50.

[314] Kama ilivyo wazi katika hadithi za wazi kabisa ambazo tumezinukuu katika barua yetu ya 68.

[315] Tafadhali rejea kwenye hadithi ya 15 iliyonukuliwa katika barua ya 48.

[316] Ni kinyume na akili kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliwaamuru wafuasi wake wote kwa nguvu kabisa kuacha wosia, lakini yeye mwenyewe akawa hakuacha wosia wowote ule. Ilikuwa ni muhimu zaidi kwa Mtume kuacha wosia kwa sababu hakuna mtu mwingine kamwe ambaye aliacha mali au mayatima wanaohitaji hasa mlezi au wasia na kadhalika kama ilivyokuwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), jambo ambalo ni sharia na hukumu ya kidini. Ilikuwaje kwa hiyo kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwaacha bila kushughulikiwa na vipi angewaacha yatima na wajane wake (yaani wafuasi wake wote) kuhangaika huku na kule bila ya kiongozi au msimamizi kiasi kwamba wafanye mambo kwa matakwa na hiari zao. Akili na tafakari vyote vinatuambia kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa hakika aliacha wosia kwa fadhila ya Ali (a.s.). Ndio maana yeye Ali aliuosha mwili wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), akaandaa mazishi yake, akalipa madeni yake na dhima zake, akaonyesha njia ya haki kwa waumini wakati walipokhitilafiana. Mtukufu Mtume vilevile aliwajulisha watu kwamba Ali (a.s.) ndiye kiongozi (Bwana) baada yake. Kadhalika alionyesha upekee mwingine na sifa za Ali kwa Waislam wote kama ilivyoelezwa kirefu mwanzoni mwa barua hii.

Ama kuhusu riwaya iliyosimuliwa na Ibn Abu Awfih na kuandikwa na al-Bukhari kwamba Mtume (s.a.w.w.) ameacha Kitabu cha Allah kama wosia wake sisi tutaonyesha kwamba bila shaka hilo ni kweli lakini hadithi hiyo imefupishwa kwa fitina. Ukweli ni kwamba, yeye (s.a.w.w.) alitoa wosia kuuamrisha umma wake kushikamana na Vitu Viwili Vizito hivyo moja kwa moja, akiuonya na hatari ya kupotea kama haukufanya hivyo. Akiujulisha kwamba Viwili hivyo havitatengana mpaka vimfikie kwenye Birika la Kauthar. Vitabu vyetu vya hadithi na vinginevyo vimesimulia juu ya suala hili kwa mfululizo wa moja kwa moja kutoka kwenye vyanzo vya kizazi kitoharifu. Kwa hadithi zilizosimuliwa na kupokewa kuhusiana na suala hili unaweza kurejea kwenye riwaya zilizonukuliwa katika barua ya 8 na 54. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 71

## SAFAR 12, 1330 A.H.

**Kwanini Umekataa Hadithi ya Ummul Muuminiin, Ambaye ni Mke bora wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?**

Limekufika lipi? Allah akusamehe! Aisha ni Mama wa Waumini, na mbora wa wake za Mtume, lakini umegeuka mbali na yeye na ukaitupa hadithi yake, kana kwamba haina maana kabisa, ambapo kauli yake ni ya mwisho na hukumu yake iko kwenye misingi ya haki. Bado unashikilia maoni ya kinyume kuhusu yeye! Pamoja na hili, unaweza kutupa msimamo wako wa kutokubaliana naye na kuikataa riwaya yake ili tuweze kufikiria. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 72

## SAFAR 12, 1330 A.H.

**I. Aisha Hakuwa Mke bora Zaidi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),**
**II. Mke bora Alikuwa ni Bibi Khadija (s.a.),**

**III. Maelezo Mafupi juu ya Sababu ya Kuikataa Hadithi yake.**

Mama wa waumini Aisha kweli alikuwa anao ubora wake na hadhi maalumu, lakini hakuwa ndiye mzuri au mbora zaidi kati ya wake za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na atakuwaje mbora wakati hadithi yake moja sahihi inapingana na hilo. Yeye anasema: "Mjumbe wa Allah siku moja alimkumbuka Khadija, nami sikulipenda hilo na nikasema alikuwa mzee, na alikuwa hivi na hivi. Sasa Allah amekupa wewe mwingine aliye bora kuliko yeye [yaani, yeye mwenyewe]. Akasema [Mtume]: 'Hata kidogo; Allah hajanipa aliye bora kama yeye. Yeye aliamini Utume wangu wakati wengine walikataa kuniamini, na alithibitisha na kuyaunga mkono maneno yangu wakati wengine waliyapinga; aliweka utajiri wake mikononi mwangu wakati watu walininyima, na Allah amenineemesha watoto kupitia kwake na sio kupitia kwa mke mwingine yeyote.'" [317]

Aisha ananukuliwa vilevile akisema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kamwe hakutoka nyumbani kabla ya kumtaja Khadija na kumsifu. Siku moja alimtaja, na nikahisi wivu, nikasema: Yeye hakuwa ila ni mwanamke mzee tu, ambapo Allah amekubadilishia kwa kukupa mwingine aliye bora kuliko yeye?' Alichukizwa mno kiasi kwamba nywele zake za mbele zilitetemeka kwa hasira, kisha akasema: 'Kwa jina la Allah, hapana! Allah hakunibadilishia kwa yeyote aliye bora kuliko yeye! Aliniamini wakati watu waliponikana; alinisadiki wakati watu waliponikadhibisha; alinipa mali yake wakati watu waliponinyima, na Allah ameniruzuku watoto kupitia kwake wakati ameninyima watoto kupitia kwa wanawake wengine. …'" [318] Kwa hiyo, mbora wa wake za Mtume (s.a.w.w.) ni Khadija al-Kubra, mkweli wa kwanza wa umma huu, wa kwanza katika kumuamini Allah na Kitabu Chake, na katika kumliwaza Mtume Wake. Na ilikuwa ni kuhusu yeye kwamba Allah alimteremshia wahyi Mjumbe Wake (s.a.w.w.) kufikisha habari nzuri kwake kwamba anayo nyumba katika Pepo iliyojengwa kwa nguzo za fedha, na kwamba Mtukufu Mtume alimwelezea kama mkewe bora zaidi pale aliposema: "Wanawake bora kabisa wa Peponi ni Khadija bint Khuwaylid, Fatima bint Muhammad, Asia bint Muzahim, na Mariamu bint Imran," Yeye (s.a.w.w.) pia alisema: "Wabora wa wanawake wote wa ulimwengu ni wanne, nao ni Mariamu bint Imran, Khadija bint Khuwaylid, Fatima bint Muhammad na Asia bint Muzahim mke wa Fiaruni." Kuna hadithi nyingine nyingi ambazo ni miongoni mwa zilizo sahihi zaidi na za kutegemewa zinazosisitizi suala hilohilo.[319]

Hali kadhalika haiwezi kusemwa kwamba Aisha alikuwa bora miongoni mwa mama wa waumini wengineo ukiachilia mbali Khadija. Kwani watu wenye elimu na wasomi wanajua kwamba zipo hadithi za kuaminika na maelezo yaliyoandikwa kupinga ubora wake yeye juu ya wakeze wengine wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wakati mwingine alifikiri mwenyewe kuwa yeye ni bora kwa wengine wote, lakini wakati wote Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akimpinga, kama inavyoonekana kwenye tukio la Safiyya bint Huyay. Wakati Mtume (s.a.w.w.) siku moja alipoingia chumbani kwake akamkuta analia. Alimuuliza: "Kitu gani kinakuliza?" Alijibu: "Nimekuja kufahamishwa kwamba Aisha na Hafsa wananisema vibaya

---

[317] Hadithi hii na inayoifuatia ni miongoni mwa hadithi sahihi mashuhuri. Utazikuta hadithi hizi zimeandikwa kwa maneno yanayofanana na yale tuliyoyaeleza katika *Istii'ab* ya Ibn Abdul-Bar katika maelezo yake kuhusu Khadija al-Kubra (s.a.). Hadithi hizi mbili zimenukuliwa na al-Bukhari na Musilim katika *Sahih* zao takriban kwa maneno hayohayo.

[318] Kama ilivyosimuliwa na al-Bukhari katika Mlango wake juu ya 'Wivu wa mwanamke na mapenzi yaliyopituka mipaka,' karibu na mwisho mwa tasinifu yake juu ya ndoa, ukurasa 175, Jz. 3, ya *Sahih* yake. (Rejea gazeti la "Kisiwa cha Maarifa," la 8-10-2012, Dar es Salaam, kwa taarifa kama hii - **Mhariri**)

[319] Tumeinukuu katika ibara ya pili ya maelezo yetu maarufu, na yeyote ambaye anapenda kufanya utafiti arejee humo.

na wanajaribu kunifanya mimi nidharaulike, na kusema kwamba wao ni bora zaidi kuliko mimi." Yeye (s.a.w.w.), akasema: "Kwanini usiwaambie kwamba: 'Ninyi sio wabora kuliko mimi, kwa sababu mimi baba yangu ni Harun, na ami yangu ni Musa, na mume wangu ni Muhammad?"[320] Yeyote atakayefuatilia saikolojia na mwenendo wa mama wa waumini Aisha atakuta kwamba tuliyoeleza hapa kuhusu yeye ni ya kweli tupu.

Na kuhusu sababu iliyotufanya tusiizingatie hadithi yake kuhusiana na wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) tunaweza kukujulisha kwa kifupi kwamba sisi hatumtegemei yeye na hatuichukulii hadithi yake kama ni hoja halali. Nakuomba tuliache suala hili hapo na tafadhali usiombe ufafanuzi wake. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[320] Hii imenukuliwa na al-Trimidhi kutoka kwa Kananah, kijakazi wa Ummul-Mu'minina Safiyya, na imepokelewa na Ibn Abd al-Birr katika maelezo juu ya Safiyya katika *Istii'ab.* Ibn Hajar katika wasifu wa Safiyya katika *Al-Isabah,* na Sheikh Rashid Ridha mwishoni mwa uk. 589, Jz. 12, ya kitabu chake *Manar*. Wapokezi wa hadithi wengi wameisimulia riwaya hii.

# BARUA YA 73

## SAFAR 13, 1330 A.H.

**Kuomba Maelezo ya Kukataa kwetu Hadithi za Aisha.**

Wewe sio miongoni mwa wale watu ambao hawalaghaiwi, wala kudanganya wengine, wala wewe huna ajizi ya kuuficha ukweli au mawazo ya ndani yaliyojificha, wala hukwepi mjadala wenye busara na umeepukana na chuki na utoaji shutuma zisizo na msingi. Na kwa rehema zake Allah, mimi sio miongoni mwa wale wanaoshutumu, wanaokosoa wala kujadili jambo lolote kwa ajili tu ya malengo kama hayo, wala sioni aibu kutafuta habari au kufuatilia mjadala wenye busara; mimi natafuta ukweli, na kwa hiyo, nakuomba unipatie majibu ya kina kuhusiana na kukataa kwako hadithi ya Aisha, siwezi kuondokana na hili na ni wajibu juu yako kukubaliana na maombi yangu ambayo kwa kuyaunga mkono na kurejesha kwenye aya hii ya Qur'ani:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنْزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَالْهُدَىٰ مِنْ بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ ۙ أُولَٰئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّاعِنُونَ

**“Hakika wale wanaoficha tuliyoyateremsha, katika ubainifu na uwongofu, baada ya Sisi kuyabainisha kwa watu Kitabuni, hao anawalaani Mwenyezi Mungu, na wanawalaani wanaolaani.** (2:159)**.**

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 74

## SAFAR 14, 1330 A.H.

**I. Sababu za Kuzikataa kwetu Hadithi ya Aisha,**

**II. Akili Inathibitisha Mtume Aliacha Wosia kwa Fadhila ya Ali,**

**III. Madai yake Kwamba Mtume Alifariki Akiwa Ameegemea juu ya Kifua Chake sio ya Kweli.**

Nilikuomba usiulizie sababu za kukataa kwetu hadithi yake lakini umekataa. Allah akusaidie! Umenilazimisha na kusisitiza kwamba nikupatie maelezo ya sababu zetu za kukataa, ambazo hazina umuhimu sana kwako kwa sababu tayari unajua kwamba tumeanzia hapa, na hapa ndipo ulipofia wosia, na hapa ndipo yalipofia maandiko ya wazi, na hapa ndipo ilipofia khums, mirathi na zawadi, na hapa ndipo chimbuko la fitna, na hapa ndipo chimbuko la fitna, na hapa ndipo chimbuko la fitna,[321] ambapo (Aisha) alikwenda kumpiga vita Amirul-Mu'minina kwa kukusanya wapiganaji kutoka miji mbalimbali, na akaongoza jeshi kubwa katika kuipora serikali yake na kutokomeza mamlaka yake.

Yakatokea yaliyotokea; ambayo mimi sitayataja; Kuwa na dhana nzuri; na wala usiulize habari zake.

Kukataa wosia kwa fadhila ya Ali sio hoja halali. Yeye alikuwa adui yake mkali mno, na kwa hiyo mtu mwadilifu hawezi kutarajiwa kutegemea juu ya maneno yake kuhusiana na wosia huo. Yeye alikuwa ni chanzo cha matatizo kadhaa kwa Ali (a.s.). Kukataa na kujaribu kuuzima wosia kwa maslahi ya Ali sio tatizo pungufu kuliko Vita Ndogo ya Ngamia[322] na Vita Kubwa ya Ngamia ambamo yeye alijitokeza kwa picha yake halisi na ambavyo vilionyesha wazi hadharani ule uadui na wivu wake kwa Ali (a.s.). Alibakia kuwa adui mbaya wa Ali (a.s.) ambaye alikuwa ni kiongozi wake mwenyewe, na *wasii* wa Mtume wake baada ya vita hivyo viwili kama alivyokuwa kabla ya hapo, na walipomletea habari za kifo cha Ali alisherehekea na akafanya sijda kumshukuru Allah (kwa kuuliwa kwake shahidi) na akatunga beti hizi:[323]

Aliweka chini fimbo yake, na kisha akatulia, Moyo wake umejaa furaha yake, akili yake imetulia, Kama msafiri anayerejea kwake, mizigo kajipumzikia, Katu usiseme Ali kufa kwake, Aisha kahuzunishwa.

Kama unataka, naweza kunukuu kwa ajili yako mfano wa hadithi zake chache kwa ajili ya kukuwezesha kuamua ukubwa wa uadui wake. Alisema: "Wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alipokuwa anaumwa sana, na maumivu na usumbufu vikazidi mno, alitoka nje huku akiwa amewaegemea watu wawili na

[321] Kama ilivyokuja katika hadithi sahihi. Tafadhali rejea kwenye Mlango wa "Nini kilikuja katika nyumba za wake zake Mtume" katika Kitabu '*Jihad wa siir'* katika uk. 125 wa Jz. 2, ya *Sahih Bukhari* ambamo utakuta maelezo kwa kirefu.

[322] Mapambano ya Vita vya Ngamia yalipiganwa mnamo mwezi 25 ya *Rabi'ul-Thani* [mfunguo saba] 36 A.H., kabla ya kuwasili Amirul-Muminin (a.s.) huko Basra wakati Aisha akifuatana na Talha na al-Zubeir waliliposhambulia mji wa Basra ambako Uthman ibn Hanif al-Ansar alikuwa gavana kwa niaba ya Ali. Alisababisha Shi'ah arobaini wanaomuunga mkono Ali (a.s.) wakauawa msikitini humo, na wengine sabini sehemu nyingine. Uthman ibn Hanif, ambaye alikuwa mmoja wa masahaba wenye elimu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ali (a.s.) alichukuliwa mateka. Watekaji wake walitaka kumuuwa pia lakini wakaogopa ulipaji kisasi kutoka kwa ndugu yake Suhayl na marafiki wengine; hivyo, walimnyoa ndevu zake, masharubu, nyusi na kichwa, na wakampiga, wakamtia jela kwa siku kadhaa, kisha wakamfukuza kutoka Basra. Walipigwa vita na Hakim ibn Jablah, aliyekuwa mkuu wa kabila la Abdul Qays na aliyekuwa mtu mwenye elimu na busara na aliyehifadhi Qur'ani alifuatana na kundi la Banu Rabi'a na wakakabiliana na jeshi la Aisha. Walipigana bila kukata tamaa mpaka kila mmoja wao akauawa shahidi. Mtoto wa Hakim Ashraf pamoja na kaka yake waliuliwa mashahidi na Basra ikaanguka mikononi mwa jeshi wavamizi. Wakati Ali (as) alipowasili na jeshi lake, alilazimika kupambana na jeshi la Aisha, na hivyo ndivyo Vita vikubwa vya Ngamia vilivyoanza. Maelezo ya vita vyote viwili yamehifadhiwa katika vitabu vya historia vilivyoandikwa na Ibn Jariir, Ibn al-Athiir na waandishi wa wasifu na wanahistoria wengine.

[323] Kama ilivyonukuliwa na muhadithina na wanahistoria waaminifu kama vile Abdul-Faraj al-Asfahani mwishoni mwa mjadala wake kuhusu Ali katika kitabu chake *Maqatil al-Talibiyyin.*

miguu yake ikiburuza chini; wasaidizi hao walikuwa ni Abbas ibn Abdul-Muttalib na mtu mwingine."[324] Msimuliaji wa hadithi hii, Ubaydullah bin Utba bin Mas'ud anaongeza kusema: "Nilimsimulia Abdullah ibn Abbas kuhusu riwaya hii naye akajibu akaniambia: 'Unajua huyo mtu mwingine ambaye Aisha hakumtaja jina alikuwa ni nani?' nikasema: 'Hapana.' Ibn Abbas akasema: 'Alikuwa ni Ali ibn Abi Talib.'" Msimuliaji aliendelea kusema "Hakuna kheri yoyote juu ya Ali ambayo Aisha alipendezewa nayo.[325]

Nasema, kama hakuna kheri yoyote ya Ali ambayo ilikubaliwa na Aisha na hakuweza hata kutaja jina la Ali miongoni mwa wale ambao walitembea hatua chache na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) (akiwaegemea), vipi angetegemewa kustahimili kutaja wosia wa urithi wa Nabii ambao ni kwa fadhila ya Ali, ambao kwa kusema kweli ndio kigezo cha ustahilifu wake? Imamu Ahmad katika uk. 113, Jz. 6, ya *Musnad* yake amenukuu riwaya ya Aisha kama ilivyopokelewa kutoka kwa Ata ibn Yasaar akisema: "Mtu mmoja alikuja kwa Aisha na akamuongelea vibaya Ali na Ammar. Aisha alijibu kwa kusema: 'Ama kuhusu Ali, sina la kukuambia; lakini kuhusu Ammar, nimemsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akisema kwamba wakati wowote Ammar inapomtokea kuchagua kati ya vitu viwili, yeye huchagua kile kilicho bora zaidi kwa mtazamo wa mwongozo mzuri na wokovu.'"

Nashangaa sana! Mama wa waumini anamuonya mtu huyo kuhusu kumkashifu Ammar kwa sababu ya maneno ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.); "wakati wowote Ammar inapomtokea kuchagua kati ya vitu viwili, yeye huchagua kile kilicho bora zaidi kwa mtazamo wa mwongozo mzuri na wokovu," wakati ambapo anajizuia kutokana na kumuonya dhidi ya kumkashifu Ali ambaye alikuwa ni ndugu na walii wa Mtukufu Mtume, Haruun wake na msiri wake, mwadilifu mno miongoni mwa umma wake, lango la jiji la elimu yake, aliyempenda sana Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na yeye akapendwa sana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wa kwanza kuamini ujumbe wake, mtu ambaye ndiye mwenye elimu na mwadilifu zaidi katika Umma. Nashangaa! Kama vile hajui hadhi ya Ali mbele ya Allah Aza wa Jallah, au nafasi yake katika moyo wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), au hadhi yake katika Uislamu, juhudi zake kubwa katika kuuendeleza, na michango yake mikubwa. Kama vile hajasikia hata aya moja katika Kitabu cha Allah wala hadithi ya Mjumbe Wake (s.a.w.w.) katika kumtukuza. Hicho ndio kiasi cha uadui na wivu juu ya Ali kiasi kwamba alimchukulia hata kutolingana na Ammar na hakumzuia mtu huyo kumkashifu Ali (a.s.)!

Wallahi! Kushangaa kwangu kunapita mipaka wakati ninapofikiria juu ya kauli yake: "Nilimuona Mtume (s.a.w.w.) (wakati wa kifo chake). Nilikuwa nimemshikilia kifuani kwangu. Aliagiza aletewe beseni la kunawia; akaliegemea na kufariki bila mimi kutambua. Hivi ingewezekana katika mazingira kama hayo, kufanya wosia kwa fadhili ya Ali?" Sijui ni kipengele gani cha riwaya hii ambacho ni chakukosoa, ambacho ni chenye mashaka kutoka pembe mbalimbali. Natamani kama mtu yeyote angeweza kunielezea jinsi gani kifo chake, kama anavyokielezea yeye, kinathibitisha kwamba alikufa bila kuacha wosia. Alifikiri kwamba wosia unakuwa halali iwapo tu umetolewa muda mchache tu kabla ya kufa?! Nina hakika kwamba hapana mtu mwenye akili timamu anayeweza kufikiria hivyo. Lakini hoja ya mtu mwenye kupinga ukweli ni batili kwa vyovyote awavyo mtu huyo, wakati ambapo Allah amesema katika Kitabu Chake Kitukufu, akimuambia Mjumbe Wake Mtukufu (s.a.w.w.): **"Mmeandikiwa mmoja**

[324] Kama ilivyonukuliwa na al-Bukhari kuhusiana naye katika sehemu ya maradhi ya Mtume (saw) na kifo chake, ukurasa 62, J. 3, ya *Sahih* yake.

[325] Bukhari amesimulia tu ile hadithi kama ilivyosimuliwa na Ubaidullah bila ya kuongeza maneno ya Ibn Abbas: "Hakuna kheri yoyote juu ya Ali ambayo Aisha alipendezewa nayo" Huu ni mwenendo wa Bukhari unaofahamika sana. Lakini waandishi wengi wa hadithi wameinukuu kupitia vyanzo vya kuaminika, kwa mfano Ibn Sa'd ambaye ameinukuu riwaya hii na akaongeza mwishoni maneno ya Abdullah bin Abbas katika uk. 29, Sehemu ya Pili, Jz. 2, ya *Tabaqat* yake, kutoka kwa Ahmad bin al-Hajjaj kutoka kwa Abdullah ibn Mubarak kutoka kwa Yunus na Mu'ammar ambaye ameisikia kutoka al-Zuhri kutoka kwa Ubaydullah bin Atbah bin Mas'ud, ambaye ameyasikia maneno yenyewe hayo kutoka kwa Ibn Abbas. Wapokezi wote hawa na wasimuliaji wa hadithi hii wanachukuliwa kuwa ni watu waaminifu.

**wenu anapofikiwa na mauti, kama akiacha mali afanye wosia…(Qur'ani, 2:180 na 5:106).”** Je, mama wa waumini aliwahi kumuona Mtume (s.a.w.w.), akienda kinyume na maelekezo ya Kitabu cha Allah au kupuuza maamrisho yake? Mungu aepushie mbali. Alimuona hasa akifuata mwongozo wake, akishikamana na aya zake, akifanya hima kutii amri zake na makatazo yake, akifikia raghba ya mwisho kabisa ya kushikamana na maamrisho yake yote. Hakuna shaka katika akili yangu kwamba lazima alimsikia akisema: “Kama Muislam yeyote anayejua kwamba anaacha kitu nyuma yake haruhusiwi kulala hata kwa siku mbili bila kuandika wosia wake.”[326] Atakuwa pia amesikia kutoka kwake amri nyingine kama hiyo vilevile. Hakuna shaka kwamba amri zake kuhusiana na wosia zilikuwa kali sana. Na hayo ndio mafundisho yao. Haiwi sawa kwake au kwa Mtume yeyote, baraka za Allah ziwashukie wote, kuwaambia watu kitu bila ya kukifanya yeye mwenyewe, au kukataza kitu huku yeye akifanya kinyume chake; Allah yuko mbali kutokana na kumteua mtu kama huyo kufikisha ujumbe Wake.

Ama kuhusu kile ambacho Muslim na wengine wamemnukuu Aisha akisema: “Mjumbe wa Allah hakuacha dinar wala dirham, wala ngamia dume au jike, wala hakuacha wosia wowote,” iko mbali na ukweli na isiyokubalika kama tu hadithi yake iliyopita. Kama alichomaanisha ni kwamba yeye (s.a.w.w.) hakuacha kitu chochote kabisa na kwamba alikuwa hana chochote kilichohitaji kufanyiwa wosia kabisa, bado sio sahihi kabisa. Kwa kweli, bila shaka hakuacha kama watu wengine vitu vinavyochukuliwa kama ni fahari ya ulimwengu huu. Kwani yeye alikuwa ndiye mtu aliyejitoa zaidi kidini duniani kote na aliyejitenga zaidi na starehe za kidunia. Alipofariki na kujiunga na Mola wake Aza wa Jallah, akiwa ameacha madeni kidogo yaliyohitaji kulipwa,[327] ahadi kadhaa na wajibu wa kutimizwa, na vitu vilivyowekwa amana kwake na watu wengine ambavyo vilihitaji wosia. Vilevile aliacha mali yake mwenyewe na vitu ambavyo vingesaidia kulipia madeni yake, na kutekeleza ahadi yake, mabaki ya vitu vyake binafsi ambavyo ni mrithi wake kwa ajili ya binti yake Fatima az-Zahra (as), jambo ambalo linaungwa mkono na madai yake ya mali akiwa mrithi wa baba yake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).[328]

Kadhalika Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), aliacha vitu ambavyo ni muhimu sana ambavyo hakuna mwanadamu mwingine duniani ambaye amewahi kuviacha hapo kabla au baada yake ambapo kuhusu hivyo ilikuwa ni muhimu sana kuacha wosia, yaani, aliacha dini ya kweli iliyonyooka ya mbinguni, ambayo ilizaliwa karibuni tu na ipo katika uchanga wake na ambayo ilikuwa na thamani kabisa na yenye mahitaji makubwa zaidi ya mrithi kiongozi na mlezi kuliko ilivyo kwa dhahabu na fedha, nyumba au mali isiyohamishika, ardhi au mifugo. Aliacha mayatima na wajane katika Umma wake, ambao wote walikuwa na shauku ya kuona kwamba kuna mrithi na mwandamizi wake atakayekuwa ndiye bwana na kiongozi wao, atakayechukua nafasi ya kushughulika na uendeshaji na usimamizi na mwongozo wa mambo yao ya kidini na kiulimwengu. Na ilikuwa haiwezekani kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) angeliiacha ulinganiaji dini ya Allah, wakati bado ikiwa katika uchanga wake (kwenye susu), kwenye mawazo ya ajabu ajabu na matakwa ya watu, au kutegemea makisio na maoni ya kubahatisha ya watu binafsi kwa ajili ya uhifadhi na ulinzi wa kanuni na sheria za kidini bila ya kuteua mrithi atakayeyasimamia masuala yao ya kidini na halikadhalika na ya kiulimwengu, mtu ambaye juu yake watu wanaweza kumtegemea na kumuamini kabisa kama walivyofanya kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Yuko mbali na kuwaacha yatima wake, yaani Umma wote ambao wanaishi katika mapana na marefu ya dunia, kama kondoo wanaohangaika katika usiku wa kipupwe wenye mvua, bila ya mchungaji yeyote wa kuwaangalia.

[326] Kama ilivyonukuliwa na al-Bukhari mwanzoni mwa tasinifu yake juu ya wosia (kwa ujumla) katika *Sahih* yake, ukurasa 83, Jz. 2; vilevile imenukuliwa na Muslim katika Kitabu cha Wosia, uku. 10, JZ. 2, ya *Sahih* yake.

[327] Mu'ammar anamnukuu Qatadah akisema kwamba Ali (as) alichukua usimamizi wa masuala fulani baada ya kifo cha Mtume (saw), mengi yake ambayo yalikuwa ni baadhi ya ahadi zilizohitaji kutimizwa, madeni yanayokisiwa kuwa kiasi cha dirham laki tano kwa mujibu wa Qatadah; hivyo, rejea kwenye hadithi kwenye ukurasa wa 60, Jz. 4, ya *Kanz Al-Ummal*, na ni hadithi ya 1170.

[328] Kama ilivyonukuliwa al-Bukhari mwishoni mwa Mlango juu ya kampeni ya Vita vya Khaibar katika Sahih yake, uk, 37, Jz. 2. Na Muslim katika Mlango juu ya maneno ya Mtume: “Hatuachi mirathi, kile tunachokiacha ni sadaka na zaka,” katika “*Kitab Jihad*” katika *Sahih* yake, Jz. 2, uk.72.

Na Mwenyezi Mungu atuhifadhi na kudhania kwamba yeye alishindwa kufanya wosia, hususan baada ya kupokea maagizo mengi kuhusiana na hilo kutoka kwa Mola Wake na hivyo kwa mkazo kabisa akaamrisha Umma wake kufanya hivyo. Kwa hiyo sio mantiki kuwaamini wale wenye madai kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alishindwa kuandaa wosia wa urithi, hata kama madai hayo yanatolewa na mtu mwenye kuheshimiwa sana.

Wakati wa mwanzo kabisa wa Uislamu, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alifanya wosia wa mrithi kwa fadhila ya Ali (a.s.) katika mwaliko wa awali kabisa kwenye Uislam, hata kabla ya ujumbe wake haujatangazwa mjini Makka, mara tu Mwenyezi Mungu, ambaye yuko mbali na mapungufu yoyote alipoteremsha aya isemayo: **"Na uwaonye jamaa zako wa karibu (26:214),"** kama tulivyoeleza katika Barua ya 20. Baada ya hapo aliendelea kurudia wosia wake tena na tena, akiusisitiza katika njia mbalimbali na sehemu mbalimbali kupitia hadithi za kutegemewa ambazo tumezitaja ndani ya kitabu hiki. Na pale alipohisi mkono wa Malaika wa Mauti unamsogelea (wazazi wangu wawe muhanga kwa ajili yake), alinuia kuweka kumbukumbu kwa kuandika wosia wake huo juu ya Ali (a.s.) ili kuthibitisha kuimarisha matangazo yake ya mdomo na kauli za mara kwa mara kuhusiana na suala hili. Yeye (s.a.w.w.) aliagiza: "Nileteeni kalamu, karatasi na wino ili nikuandikieni wosia (wa mwongozo) ili msije kupotoka kwenye njia iliyonyooka baada ya kifo changu." Lakini, badala ya kutii maagizo yake, wao walianza kuzozana, ingawa hawakupaswa kufanya hivyo mbele ya Mtume (s.a.w.w.), na baadhi ya masahaba waliokuwepo pale wakasema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) anaweseseka." [329] Baada ya kusikia kauli hiyo ya kukirihisha na kushusha hadhi, Mtume (s.a.w.w.) alitambua kwa uhakika kwamba kuandika kwake wosia baada ya kauli hizo hakutakuwa na athari yoyote mbali na kusababisha uovu mkubwa. Kwa hiyo, aliwaambia waondoke chumbani kwake, akijisikia kutosheka na matangazo ya mdomo na kauli za mazungumzo ambayo aliyafanya hapo kabla kuhusiana na hilo.

Hata hivyo, licha ya yote hayo, bado alitoa kauli za wosia tatu kwa wafuasi wake kabla ya kifo chake; ambazo ni kumtii Ali kama mrithi kiongozi na imam wao; kwamba lazima wawatoe washirikina nje ya Rasi ya Bara Arabu na waendelee kutuma wajumbe kwa watawala wa kigeni kama alivyokuwa akifanya yeye (s.a.w.w.). Lakini serikali zilizoanzishwa baada yake na hali za kisiasa za wakati huo hazikuwaruhusu muhadithina kusimulia wosia wake wa kwanza, wakajidai kwamba wameusahau (wosia huo). Tafsiri ya neno kwa neno ya alichokisema Al-Bukhari mwishoni mwa hadithi yenye maneno "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) anaweseseka" ni hii "Na wosia wake (s.a.w.w.) wakati wa kifo chake ulikuwa na maelekezo matatu: Kuwatoa washirikina nje ya rasi ya Arabia; kuendelea kutuma wajumbe kama alivyokuwa akifanya yeye …, na la tatu nimelisahau."[330] Hivi ndivyo Muslim pia alivyoandika katika *Sahih* yake, na vivyo hivyo kwa waandishi wengine wa *Sunan* na *Musnad.* Wote wameusahau wosia huo wa tatu.

Na kuhusu madai ya Mama wa Waumini kwamba wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alipokutana na Mola Wake (yaani alipofariki) alikuwa ameegemea juu ya kifua chake yanapingana na hadithi sahihi zinazoeleza kwamba yeye (s.a.w.w.) alikutana na Mola wake wakati akiwa juu ya paja la ndugu yake na rafiki yake Ali ibn Abu Talib (a.s.). Hili limeelezwa katika simulizi zote sahihi zilizosimuliwa kwa mfululizo kutoka kwa Maimamu wa kizazi kitoharifu ambazo zinaungwa mkono na sahih za waandishi wa *Sunni* na utazikuta riwaya hizo katika kumbukumbu za kwenu kama utachukua usumbufu wa kufanya utafiti, Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

329 Hii imenukuliwa kwa maneno yake haswa na Muhammad ibn Isma'il al-Bukhari katika sehemu yake juu ya "ukarimu kwa wajumbe" katika kitabu chake *Al-Jihad wal siyar*, ukurasa wa 118, J. 2,

330 Rejea kwenye sura inayoshughulika na "ruhusa ya kutuma wajumbe" katika cha "*Al-Jihad wal Siyar"* uk. 118, Jz. 2 ya Sahih yake.

# BARUA YA 75

## SAFAR 17, 1330 A.H.

**I. Mama wa Waumini Hatawaliwi na Chuki au Hisia Katika Kusimulia Hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),**

**II. Yenye Kupendeza au Kuchukiza Yanaamuliwa kwa Sheria ya Dini,**

**III. Kuna Riwaya Yoyote Inayopingana na Madai ya Mama wa Waumini?**

Ulichoeleza kuhusu Mama wa Waumini Aisha na hadithi yake sahihi inayokataa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuacha wosia kimeegemea kwenye dhana mbili.

1. Moja ni shutuma yako kwamba chuki yake ya kutompenda Imamu, ilimfanya akatae wosia unaompendelea yeye. Majibu yetu ni kwamba, uchunguzi wa mtindo wake wa maisha unaonyesha kwamba katika kusimulia hadithi ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alikuwa hatawaliwi na chuki, hisia au sababu za kibinafsi. Hawezi kulaumiwa kwa upendeleo wakati anaponukuu hadithi aliyosikia kwa Mtume, hata kama hadithi hiyo inamhusu mtu anayempenda au asiyempenda. Mungu aepushie mbali kwamba alitawaliwa na sababu za kibinafsi katika kuhusisha kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) jambo ambalo hakulisema.

2. Jambo lingine ni dhana yako kwamba akili peke yake inakataa kabisa, kama unavyofikiri kuunga mkono hadithi yake, kwa sababu inachodokeza hakina mantiki na kwa hiyo hakiwezekani. Unasema hairuhusiwi kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kuiacha dini ya Allah Aza wa Jallah, katika uchanga wake, ambapo waja wa Allah walikuwa bado ni wageni kwenye Jamii ya Kiislam na kushikiliwa kwao na umma za kipagani zilizopita na desturi zao zikiwa bado zina nguvu, bila ya kuwateulia mrithi atakayeangalia mambo yao. Jibu kwa madai yako ni kwamba dhana hii imetegemea juu ya imani kwamba uzuri na ubaya unaamuliwa na akili. Lakini Masunni hawaamini hilo kuwa ni hivyo. Kwa mujibu wao kimsingi akili haiwezi kupambanua iwapo kitu ni kizuri au kibaya; bali, wanaamini kwamba mamlaka ya kisheria ndio yenye kuamua uzuri au ubaya wa kitendo na si vinginevyo. Wanaamini kwamba chochote kinachoamuliwa na sheria ya dini kuwa ni kizuri, huwa ni kizuri, na chochote kinachoelezewa na sheria kuwa ni kibaya, huwa ni kibaya. Uamuzi wa uzuri au ubaya wa jambo hautegemei kabisa juu ya akili.

Ama kuhusu kile ulichotaja mwishoni mwa Barua yako ya 74, kuhusiana na kukataa kwako madai ya Mama wa Waumini kwamba Mtume alifariki juu ya kifua chake, yanapingwa na kukanushwa na wanahistoria wengine, hatuna ujuzi na hadithi yoyote iliyosimuliwa na Masunni ambayo inalikana hilo; hivyo, kama unafahamu hadithi yoyote, tafadhali tufahamishe tuijue. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 76

## SAFAR 19, 1330 A.H.

**I. Alitawaliwa na Hisia Kali za Moyoni,**

**II. Uthibitisho wa Uzuri na Ubaya Kuamuliwa na Akili,**

**III. Hadithi Sahih Zakanusha Madai ya Ummul-Mu'minin,**

**IV. Hadithi Iliyosimuliwa na Umm Salama ni Bora Zaidi Kuliko yake.**

Katika kujibu sehemu ya kwanza ya barua yangu umeeleza kwamba kutokana na uchunguzi wa tabia ya Mama wa Waumini Aisha ni kwamba anaposimulia hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kamwe hatawaliwi na hisia wala hashawishiwi na sababu za kibinafsi. Tafadhali nakuomba ujifungulie mwenyewe pingu za desturi, mazoea na hisia kali (za upendeleo) na kwa umakini na uangalifu uutafiti mwenendo na tabia yake katika kushughulika na wale ambao aliwapenda, na halikadhalika na wale ambao alikuwa hawapendi. Utafiti wa uhakiki na uchunguzi makini utakuwezesha kuziona kwa udhihirisho mno hisia, chuki na upendeleo wake. Tafadhali kumbuka tabia yake kwa jinsi alivyoshughulika na suala la Uthman ibn Affan kwa maneno na vitendo,[331] na tabia yake ya uadui wa dhahiri dhidi ya Ali, Fatima, Hasan na Husein (as), na tabia yake kwa Mama wa Waumini wengine (yaani wake za Mtume); hasha, hata kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) mwenyewe; kwani katika haya mna udhihirisho mkubwa wa hisia zake kali za moyoni na ubinafsi.

Kwa mfano, tafadhali hebu rejea kwenye kadhia ya Bibi Maria na mtoto wake Ibrahim (a.s.) ambayo inaonyesha alivyokuwa dhaifu na mwenye chuki. Wakati waovu fulani walipomtuhumu visivyo kweli Ummul-Mu'minina Maria. Aisha aliwaunga mkono watuhumu hao na akijaribu bila mafanikio kuthibitisha lawama hizo bandia. Lakini Mwenyezi Mungu aliwasafisha na shutuma hizo za uovu kupitia kwa Amirul Muminina (a.s.).[332]

وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَنَالُوا خَيْرًا ۚ

**"Na Mwenyezi Mungu aliwarudisha nyuma makafiri juu ya ghadhabu yao; hawakupata kheri yoyote….."**

(Qur'ani, 33:25)."

Kama unataka kusikia zaidi juu ya udhaifu wake, tafadhali rejea maneno ambayo siku moja alimwambia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.): "Ninapata harufu ya *maghafir* [maua ya mti yenye harufu mbaya] kutoka kwako."[333] Aliyasema haya ili amzuie kutembelea nyumba ya Ummul-Mu'minina Zainab bint Jahsh (ra)

[331] Rejea kwenye uk.77, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul-Balagha* ya mwanachuo wa Mutazili, na uk. 457 na baadae uk.497 wa juzuu hiyo hiyo, na utaona tabia yake kwa Uthman, Ali na Fatima kwamba iliegemea kwenye hisi za upendeleo mbaya.

[332] Yeyote anayependa kujua habari za tukio hili la kuchukiza anapaswa arejee kwenye maelezo ya Bibi Maria [Mwenyezi Mungu amuwie radhi], katika ukurasa wa 30, Jz. 4, ya *Al-Mustadrak* cha al-Hakim, au *Talkhis al-Mustadrak* cha al-Dhahbi.

[333] Kutokana na kile al-Bukhari alichonukuu katika maelezo yake ya Sura al-Tahrim katika *Sahih* yake, ukurasa wa 136, Jz. 3; ambayo tafadhali hebu irejee na ushangazwe. Katika sehemu hiyohiyo kuna hadithi nyingi zilizonukuliwa kutoka kwa Umar zinazoeleza kwamba wale wanawake wawili ambao walikuwa wakorofi na wasumbuvu kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ni Aisha na Hafsa. Hadithi hizi

na kula asali huko. Kama lengo lisilo na muhimu kama hili limeweza kumchochea kuwa mbinafsi kiasi cha kusema uongo mbaya kama huo kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), mbele yake, itakuwa haishangazi kwamba akiukataa wosia wa Mtume (s.a.w.w.) kwa fadhila ya Ali (a.s.). Vilevile kwa ushahidi mwingine wa kuchochewa kwake na sababu za ubinafsi na kupotoka kwenye haki, tafadhali rejea kwenye suala la Asma bint al-Nu'man. Alipokuwa anaongozwa kama bibi harusi kwenda kwa mumewe, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Aisha alimwambia kwamba Mtume anapendezewa sana na mwanamke ambaye anapomwendea atamsikia akisema: "Naomba kinga ya Allah dhidi yako."[334] Kwa hilo akilenga kumfanya Mtume (s.a.w.w.) amchukie na kumdharau mkewe huyo mpya na kumfanya masikini mwanamke yule aangukie kwenye mtazamo wake yeye. Ni kana kwamba Ummul-Mu'minina anahalalisha maneno kama hayo kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), ili kufanikisha malengo yake ya ubinafsi, bila kujali kama madhumuni yake yalikuwa na umuhimu mdogo au mabaya ama hata ni yanayokatazwa na sheria ya dini. Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alimtuma akusanye taarifa fulani kuhusu mwanamke fulani. Taarifa alizowasilisha kwa Mtume (s.a.w.w.) sio zile alizokusanya bali akamjulisha taarifa potovu zilizochochewa na sababu za ubinafsi.[335] Siku moja alimlalamikia Mtume (s.a.w.w.) mbele ya baba yake, tena akiwa ameathiriwa na hisia zake, akasema: "Kuwa mwadilifu." [336] Baba yake alimzaba kibao kikali kiasi kwamba alitoka damu iliyodondokea kwenye nguo zake. Tukio hili linaonyesha jinsi alivyokuwa akitawaliwa na hisia zake. Siku moja akiwa amekasirika, alimwambia Mtume (s.a.w.w.) "…na ni wewe unadai kuwa ni mjumbe wa Allah…"[337] Na kwa nyongeza utaikuta mifano ya matukio mengi kama hayo ya kutawaliwa na hisia zake na chuki ambayo nafasi haitoshelezi hapa kuitoa, na mifano michache tuliyonukuu hapa itosheleze haja ya lengo letu.

Katika kujibu nukta ya pili umesema kwamba Ahlus-Sunnah hawaamini kwamba wema na ubaya unaamuliwa na akili. Mimi siko tayari kuamini kwamba mtu msomi mwenye elimu kama yako anaweza kuwa na imani ya ajabu kama hiyo. Hii inafanana sana kama imani ya wapotoshaji ambao wanakataa hata ukweli unaotambulika. Kwa sababu katika matendo yapo ambayo tunayafahamu kwa uhakika kwamba ni mema na mazuri, na tuna hakika kwamba yanastahiki sifa na malipo kwetu, kwa sababu ubora ndio sifa yao ya msingi, kama vile ukarimu na uadilifu. Ambapo kuna mengine ambayo tunayajua kwamba ni mabaya au maovu, na tunayo hakika kwamba vitendo hivyo vitaishia kushutumiwa na kuleta adhabu juu yetu, kwa sababu ubaya au uovu ndio sifa yao ya msingi, kama vile tabia mbaya, dhulma na uonevu. Kila mtu mwenye busara anajua kwamba ni akili ambayo inaamua uadilifu na ukarimu kuwa ni vitendo vya wema au vizuri, na tabia mbaya, dhulma na uonevu kuwa ni vitendo vibaya na viovu. Watu wenye busara wana hakika kuhusiana na uzuri na ubaya kuamuliwa na akili, kama walivyo na hakika kwamba moja ni nusu ya mbili. Welevu na umaizi wa haraka siku zote hubainisha tofauti kati ya mtu rahimu na dhalimu. Ni akili inayoamua kitendo cha mtu mwadilifu na rahimu kuwa ni kizuri na kumchukulia mtendaji wa kitendo hicho kuwa mwenye kustahiki kusifiwa na kulipwa thawabu, na kitendo cha mtu dhalimu au mtu muovu kuwa ni kibaya na chenye kufaa kushutumiwa na adhabu juu yake. Yeyote mwenye kukanusha hili ni muasi dhahiri katika tabia yake isiyo na busara.

zinafuatiwa na hadithi moja ndefu inayoshughulika na suala hili.

[334] Kama ilivyonukuliwa na al-Hakim katika wasifu wa Asma katika kitabu chake cha *Al-Mustadrak*, ukurasa wa 37, J. 4; na imenukuliwa na Ibn Sa'd ambaye anajadili wasifu wake katika ukurasa wa 104, J. 8, wa kitabu chake *Tabaqat*, na tukio hili ni mashuhuri sana. Imesimuliwa katika wasifu wa Asma na waandishi wote wa *Isti'ab* na *Al-Isabah*, na imenukuliwa na Ibn Jarir na wengine.

[335] Habari za tukio hili zimehifadhiwa katika vitabu vingi vya hadithi na historia; hivyo. Tafadhali rejea kwenye uk. 294, Jz. 6, wa *Kanz al-Ummal,* au uk. 115, Jz. 8, wa *Tabaqat* cha Ibn Sa'd ambako vilevile ameelezea wasifu wa Sharaf bint Khalifah

[336] Suala hili limenukuliwa na waandishi wengi wa hadithi na historian a wakusanyaji wa *Musnad*; hivyo rejea kwenye hadithi ya 1020 kati ya moja zilizosimuliwa katika *Kanz al-Ummal*, uk. 116, Jz. 7, na limenukuliwa na al-Ghazali katika Sura ya tatu ya tasinifu yake juu "Adabi za Ndoa" katika uk. 35, Jz. 2, ya *Ahya'ul-Ulum*. Vilevile imenukuliwa katika Sura ya 94 ya kitabu chake *Mukashafatul Quluub*, mwishoni mwa ukurasa wa 238.

[337] Kama ilivyonukuliwa na al-Ghazali katika sehemu zote za vitabu vilivyodondolewa hapo juu.

Lau kama wema au uovu haviamuliwi kwa akili, bali kama usemavyo wewe, ni kwa sheria ya dini basi wale ambao hawaamini katika dini ya kimungu kama vile mazandiki na wakanamungu wanaamua vipi kuhusu wema na uovu wa jambo lolote? Licha ya kutoamini kwao dini, wanachukulia uadilifu na ukarimu kama ni wema na urahimu, kwa ajili hiyo wanamuona mtu huyo mwadilifu na mkarimu kuwa ni mwenye kustahiki kutukuzwa na kupata malipo bora, na hawana shaka kabisa kwamba dhulma na tabia mbaya au uonevu ni mambo mabaya na maovu, na mwenye hatia ya matendo kama hayo anastahili kuchukiwa na kuadhibiwa. Kigezo chao katika hukumu yao si chochote mbali na akili; hivyo, usiwaendekeze sana wale ambao ni madhubuti sana katika ukaidi na wapinga matumizi ya akili na umaizi na wanaokataa kile ambacho watu wote wenye busara wanaamini kuwa ni kweli na wanafanya maamuzi ama kufikia hitimisho ambalo ni kinyume na kile ambacho huamuliwa na silika zao au tabia. Allah, Aza wa Jallah, aliyeepukana na mapungufu ya namna yoyote ile amewaumba waja Wake kwamba waweze kupata elimu ya kutambua mambo kwa uwezo wa fikra zao, yaani akili kama vile wanavyopata elimu ya mambo mengine kwa kupitia miguso na hisia. Hivyo basi, maumbile yao ya asili huwasukuma wao wapate kujua uzuri wa uadilifu na kadhalika ubaya wa dhulma na uonevu kupitia ujuzi wa fikra zao, yaani akili kama vile wanavyojua utamu wa asali au uchungu wa shuburi kupitia hisia zao za muonjo, au manukato ya miski au harufu ya maiti iliyooza kupitia hisi zao za kunusa, au ulaini, unyororo na ugumu wa vitu kwa hisia zao za kugusa, na kwa uwezo wao wa kuona wanaweza kutofautisha kati ya sura au mandhari inayopendeza na sura au mandhari mbaya kwa hisi zao za kuona (wa macho), na kwa uwezo wa hisi za kusikia wanaweza kutofautisha kati ya sauti zenye mvuto za filimbi na mazumari na mlio wa punda usiovutia.

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

**"Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini, ndio umbile la Mwenyezi Mungu alilowambia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini ya sawasawa, lakini watu wengi hawajui.** (Qur'ani 30:30)**."**

Wakati *Ashaira* walipoamua kuwa wakakamavu sana katika kuonyesha imani yao ya Uislam na umakini mkali kabisa kwenye kutekeleza amri zake zote walianza kukataa maamuzi ya akili na wakasema: "Hakuna maamuzi yapasayo kutiiwa mbali na maamuzi ya sheria ya dini" na wakazisahau zile kanuni za kimantiki na zinazokubaliwa kote. Kila kitu kinachotawaliwa na mantiki huwa kinatawaliwa na dini pia, yaani, maamuzi ya busara yanakubaliana kabisa na maamuzi ya dini. Haikuwaingia akilini kwamba kwa kubuni kanuni mpya kiushabiki juu yao walikuwa wanaingilia kati njia yao kwa ajili ya kujitoa. Hata kama tukikubaliana na imani kwamba kizuri na chema ni kile tu kinachotangazwa na dini, na kwamba kibaya ni kile tu kinachotangazwa na dini, basi ni kitu gani kitakachothibitisha kwamba kufuata dini na kuridhia amri zake zote kwamba ni wajibu wa lazima? Kama mtu atauliza swali: "Kwa nini ni vizuri kuamini dini iliyoteremshwa, na kutekeleza amri zake zote chanya na hasi, na kwa nini ni vibaya kutoiamini na kutotekeleza amri zake? Nawe unajibu kwamba dini inatangaza kwamba imani katika dini na kutekeleza amri za dini hiyo kuwa ni wema, na kutoiamini na kutotekeleza amri zake kwamba ni uovu, hakika hali hiyo itakuwa ni kubishana ndani ya duara. Bila ya mantiki kujadili jambo kwa misingi ya nukuu tu za kidini itakuwa ni kanuni isiyo na uthibitisho. Ni akili au mantiki pekee inayomlazimisha mtu kumuabudu Mwenyezi Mungu na

kumsaidia kupata elimu na ujuzi kumhusu Yeye swt. Bila ya nguvu ya muongozo ya mantiki hakuna kiumbe mmoja ambaye angemuabudu Mwenyezi Mungu au ambaye angeweza kupata elimu yoyote kuhusu Yeye. Utakuta mijadala ya kina katika vitabu vilivyoandikwa na wanachuoni wetu mashuhuri juu ya mada hii.

Ama kuhusu madai ya Mama wa Waumini kwamba Mtume (s.a.w.w.) alifariki juu ya kifua chake, ni dai ambalo linapingana na mfululizo wa hadithi sahihi zilizosimuliwa kupitia kwa Maimam wa Ahlul-Bayt (a.s.). Kwa riwaya zilizosimuliwa na wengineo, unaweza kurejea kwenye hadithi ya Ali kama ilivyonukuliwa na Ibn Sa'd,[338] akitaja vyanzo mfululizo hadi kwa Ali (a.s.) ambaye amesema: "Katika dakika za mwisho za uhai wake, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: 'Niitieni ndugu yangu,' hivyo nilifika kwake na akanitaka nisogee karibu naye, na nilifanya hivyo; ndipo hapo akaniegemea. Aliendelea kuniegemea hivyo huku akizungumza nami, kwa kiasi kwamba mate yake mengine yalinidondokea, kisha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akapumua pumzi yake ya mwisho." Hafidh Abu Na'iim katika *Hilyatul Awliyai*, Abu Ahmad al-Fardhii katika kitabu chake *Nuskha* na waandishi wengine wengi wa vitabu vya hadithi wote wamemnukuu Ali (as) akisema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alinifundisha (wakati wa ugonjwa wake) milango elfu moja ya ilmu ambayo kila mmoja ulinifungulia milango mingine elfu moja."[339]

Kila wakati alipoulizwa Umar ibn Khattab (ra) kuhusu kitu chochote kinachohusiana na dakika za mwisho za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wakati wote alikuwa akijibu: "Kamuulizeni Ali, kwani yeye alikuwapo na Mtume wakati wa dakika za mwisho za uhai wake ndiye anayeweza kulishughulikia hili." Jabir ibn Abdullah al-Answari ananukuliwa akisema kwamba Ka'b al-Akhbar siku moja alimuuliza Umar: "Ni yapi yalikuwa maneno ya mwisho ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)?" Umar akajibu: "Muulize Ali." Ka'b alifanya hivyo, na Ali (as) akasema: "Nilimuacha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aegemeze kichwa chake juu ya kifua changu. Aliweka kichwa chake kwenye bega langu kisha akasema: 'Swala! Swala!'" Ka'b akasema: "Hakika, huu ndio wito wa mitume wote (kwa wafuasi wao). Wameamrishwa na Mwenyezi Mungu kuwashauri wafuasi wao, na hilo ndio lengo la kutumwa kwao kama Mitume." Kisha Ka'b alimuuliza tena Umar nani aliyeukosha mwili wa Mtume, na jibu lake tena lilikuwa: "Muulize Ali." Wakati Ka'b alipomuuliza Ali (a.s.) Ali alijibu: "Ni mimi niliyemuosha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)."[340]

Ibn Abbas wakati fulani aliulizwa: "Wanasema kwamba kichwa chake Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipokufa kilikuwa juu ya mapaja ya mtu fulani; wewe unasemaje kuhusu hilo?" Ibn Abbas alijibu: "Alifariki akiwa ameegemea juu ya kifua cha Ali." Aliambiwa kwamba Urwah anasimulia hadithi kutoka kwa Aisha akisema kwamba yeye Mtume (s.a.w.w.) alifariki akiwa ameegemea juu ya kifua chake, na Ibn Abbas akaikataa, akamuuliza yule mtu aliyeuliza swali lile: "Je, wewe unaliamini hilo?! Wallahi, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alifariki huku akiwa ameegemeza kichwa chake juu ya kifua cha Ali, na Ali ndiye aliyemkosha." [341]

Ibn Sa'd amesimulia riwaya ya Imamu Muhammad Ali bin Husein Zainul Abidiin (a.s.) akitaja vyanzo kadhaa hadi kufikia kwake, ambaye amesema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipumua pumzi yake ya mwisho wakati kichwa chake kikiwa katika mapaja ya Ali." [342]

Ngoja nionyeshe wazi kwamba kuna hadithi nyingi mutawatir kutoka kwa Maimamu wa kizazi kitoharifu, Ahlul-Bayt (a.s) zenye kuthibitisha kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alivuta pumzi ya

[338] Katika uk. 5 Sehemu ya 2, Jz. 2 ya *Tabaqat* katika Mlango wa "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alifia kwenye mapaja ya Ali" na hii ni hadithi ya 1107 katika uk. 55, Jz. 4 ya *Kanz al-Umaal*.

[339] Hii ni hadithi Na. 6009, iliyonukuliwa mwisho wa ukurasa wa 392, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal.*

[340] Ibn Sa'd ameisimulia katika uk. 51, Sehemu ya Pili, Jz. 2, ya *Tabaqat*, na ni hadithi Na 1106 katika uk. 55, Jz. 4 ya *Kanz al-Ummal*

[341] Ibn Sa'd ameiandika katika ukurasa huohuo wa 51, Sehemu ya 2 ya Juz. 2 ya *Tabaqat*, na ni hadithi Na. 1108 katika uk. 55, Jz . 4 ya *Kanz al-Ummal,*

[342] Tafadhali rejea uk. 51, Sehemu ya 2 ya Jz. 2 ya *Tabaqat*

mwisho kifuani kwa Imam Ali (a.s.). Hata miongoni mwa wale waliokengeuka kutoka kwenye njia ya Ahlul-Bayt pia, kuna wapokezi na wanahistoria ambao wameukubali ukweli huu. Ibn Sa'd amepokea kutoka kwa al-Shu'bi kutoka vyanzo mfululizo hadi kwake kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alifariki dunia wakati kichwa chake kilikuwa katika mapaja ya Ali; na Ali ndiye ambaye alimkosha.[343] Na Amirul Muuminin (as) alikuwa na desturi ya kuueleza ukweli huu kwa uwazi kwenye mikusanyiko mikubwa ya watu. Tafadhali hebu rejea kwenye maneno yake yafuatayo katika moja ya khutba zake:

"Masahaba wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) wanajua sana kwamba kamwe sikuyumba katika kutekeleza amri za Allah, wala kurudi nyuma katika kutekeleza maagizo ya Mtume Wake. Mimi nilimsaidia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) dhidi ya maadui zake kwa kuwa imara katika nyakati za hali ya hatari kabisa, wakati hata mashujaa wa hali ya juu wa Arabia walipofyata na kuyumba kwa hofu au kwa kutojiamini walirudisha nyuma hatua zao, na nilimsaidia kwa mafanikio makubwa kabisa kwa nguvu ambazo Mwenyezi Mungu amenijaalia nazo. Na yeye (s.a.w.w.) alipumua pumzi yake ya mwisho wakati kichwa chake kikiwa juu ya kifua changu, na hata mate yake yalidondokea kwenye mikono yangu, ambapo nikayapangusa kwenye uso wangu, ni mimi niliyekosha mwili wake nikisaidiwa na Malaika, ambao sauti zao ziliijaza nyumba yote na uwanja wake. Makundi ya malaika wakishuka na kupanda kutoka nyumbani hapo kuelekea mbinguni mmoja baada ya mwingine, na nilizisikia sauti zao. Walikuwa wakimswalia swala ya maiti na wakimuombea rehema za Allah juu yake, mfululizo mpaka nilipomlaza kwenye kaburi lake. Hivyo, nani mwenye haki bora zaidi yangu kwake, ya kumrithi wakati wa uhai na wa kifo chake kuliko mimi?" Sawa na hayo ni yale maneno yake[344] aliyoyatamka wakati anamzika mke wake, Bibi wa Wanawake (*Saiyidat un Nisa*) – Fatima (s.a.). Alisema:

"Amani iwe juu yako, Ewe Mjumbe wa Allah, kutoka kwangu na kutoka kwa binti yako ambaye sasa amekuja na kuwa jirani yako, na karibuni ataungana nawe… Ewe Mjumbe wa Allah, kifo cha mteule binti yako Mtukufu kimeniumiza sana na kudhoofisha nguvu yangu ya subira. Ni yale mawazo tu ambayo bado ni machungu, ya kutengana kwako na sisi, na msiba mkubwa uliotuangukia kwa kifo chako ndio yanayonipa matumaini na nguvu ya kuvumilia kwa subira huu msiba wa sasa. Nilikulaza kwenye kaburi lako kwa mikono yangu mwenyewe, na ulivuta pumzi ya mwisho ukiwa umepumzika juu ya kifua changu. Baada ya kukabiliana na msiba ule mkubwa, basi balaa lolote linaloniangukia mimi sasa hivi linaweza kustahimilika kwa wepesi. Hakika, sisi ni wa Allah na Kwake lazima tutarejea ……………."

Umm Salamah vilevile amesimulia hadithi sahihi inayosema: "Wallahi naapa kwa Mungu Mmoja wa pekee, Ali alikuwa wakati wote karibu zaidi na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kuliko mtu mwingine na alibakia naye hadi wakati wa kifo chake. Sisi tulimtembelea siku ya kifo chake. Aliuliza tena na tena: 'Je, Ali amekuja? Je, Ali amekuja?' Binti yake Fatima (as) akajibu: 'Huenda umemtuma kazi ya muhimu.' Baadaye, muda mfupi Ali akaja na nilidhani kwamba huenda alikuwa anahitaji faragha pamoja na Ali. Hivyo, wote tulitoka nje ya chumba hicho." Umm Salma anaendelea: Mimi nilikaa karibu sana na mlangoni kuliko wengine. Niliona kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimwegemea Ali na akaendelea kumnong'oneza kwa siri mpaka alipofariki. Hivyo, Ali alikuwa mtu pekee aliyemhudumia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mpaka wakati wa kifo chake."[345]

---

343 Tafadhali rejea uk. 51, Sehemu ya 2 ya Jz. 2 ya *Tabaqat*

344 Rejea uk. 207, Jz. 2, ya *Nahajul Balagha*, na vilevile katika uk. 590, J. 2, wa *Sharh Nahjul Balaghah* ya Ibn al-Hadiid.

345 Hakim ameinakili hadithi hii mwanzoni mwa uk. 139, Jz. 2 ya Sahih Mustadrak na ameongeza kwamba hadithi hii ni sahihi na vyanzo vyake vyote ni vya kutegemewa, lakini Bukhari na Muslim hawakuinakili hii. Inanibidi kuonyesha kwamba Allama Dhahabi ameikubali hadithi hii kuwa ni sahihi kwa kuinakili kwake katika Talkhiis al-Mustadrak yake. Ibn Abi Shaibaj ameinakili katika Sunan yake na hii ni hadithi ya 6096 mwishoni mwa uk. 400, Jz. 6 ya Kanz ul-Amaal.

**Abdullah ibn Umar anasimulia yafuatayo:**

“Wakati wa ugonjwa wake, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alitaka aitiwe ndugu yake, hivyo, Abu Bakr akaingia ndani, lakini Mtume (s.a.w.w.) akageukia kando na akaendelea kusema: “Niitieni ndugu yangu.” Safari hii Uthmani aliletwa ndani aliko Mtume (s.a.w.w.). Mtume (s.a.w.w.) pia aligeuka mbali naye. Kisha mtu mmoja akamuita Ali kwa ajili yake. Mtume (s.a.w.w.) alimfunika na joho lake mwenyewe na akamuegemea. Wakati alipotoka nje ya shuka lile watu wakamuuliza kile ambacho Mtume (s.a.w.w.) amemuambia, naye Ali (a.s.) alijibu: ‘Amenifundisha milango elfu moja ya elimu ambapo kila mmoja kati ya hiyo ulinifungulia milango mingine elfu moja.’”[346]

Unajua kwamba mambo kama hayo ni stahili ya Mitume. Lakini anayoyasema Aisha yanawafaa watu wanaotawaliwa na tamaa zao. Kama mchunga kondoo anakufa juu ya kifua cha mke wake, au kati ya kidevu na kitovu chake, au juu ya mapaja yake…, na asiusie kuhusu uangalizi wa mifugo yake, kuisimamia ama kulitoa kundi lake la kondoo kwa hakika atakuwa mwenye hasara na mzembe wa maslahi yake. Allah amsamehe Mama wa Waumini Aisha. Kama angeamua kutoihusisha heshima ya kumsaidia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye kifua cha Ali wakati wa kufariki kwake, basi angeihusisha heshima hiyo kwa baba yake, ambayo ingekuwa ndio inafaa zaidi kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuliko kusema kwamba alivuta pumzi yake ya mwisho akiwa kifuani au mapajani mwake yeye. Lakini hilo hakuweza kulifanya kwa sababu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa amemjumuisha baba yake tayari kwenye jeshi lililoandaliwa kwa ajili ya vita na kuwekwa chini ya ukamanda wa Usama bin Zayd ambalo lilikuwa limepiga kambi nje kidogo ya Madina. Kwa hali yoyote, madai yake kwamba yeye Mtume (s.a.w.w.) alifariki juu ya mapaja yake hayakuthibitishwa na yeyote yule isipokuwa Aisha, wakati ambapo madai ya kufa kwake Mtume (wazazi wangu wawe muhanga kwa ajili yake) akiwa juu ya mapaja ya Ali imethibitishwa na wote – Ali (a.s.), Ibn Abbas, Umm Salamah, Abdullah bin Umar, al-Shu’bi, Ali ibn Husein (a.s), na Maimamu wote wa kizazi cha Muhammad (a.s.), hivyo kuifanya hadithi yenye kufaa zaidi na kulingana na hadhi ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.).

Lau kama kusingekuwa na hadithi inayopingana na kauli au riwaya ya Aisha mbali na ile ya Umm Salamah peke yake, bado hata hivyo kauli au hadithi ya Umm Salamah ingependelewa zaidi kuliko ya Aisha na kuchukuliwa kwamba ni sahihi kwa sababu nyingi mbali na hizo zilizotajwa hapo juu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

[346] Kama ilivyoelezwa katika riwaya ya Abu Ya’li iliyonakiliwa baada ya kusikia kutoka kwa Kamil bin Talha, aliyeipokea kwa Ibn Lahi’yah, kutoka kwa Hay bin Abdul-Maghafiri, kutoka kwa Abu Abdul-Rahman al-Habli, kutoka kwa Abdullah ibn Umar ambaye ameisikia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe na ambayo imenakiliwa na Hafidh Abu Na’im katika kitabu chake *Hilyat al-Awliyat*, Abu Ahmad al-Fardhi katika ‘*Nuskha*’ yake mwenyewe kama ilivyoelezwa katika uk. 392, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal.* Tabraniy, katika kitabu chake *Al-Muajam al-Kabiir,* ameelezea kwamba wakati kampeni ya vita vya Ta’if ilipokuwa mbioni, Mtume (s.a.w.w.) alichukuwa muda katika faragha na Ali kiasi kwamba wakati Abu Bakr alipopita karibu nao, alisema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Mazungumzo yako ya siri na Ali yamechukua muda mrefu sana.” Yeye (s.a.w.w.) akasema: “Sio mimi niliyenong’ona naye bali ni Allah aliyenong’ona naye…” Hii ni hadithi ya 6075, ukurasa 399, Jz. 6, ya *Kanz al-Ummal*. Mara kwa mara alikaa na Ali (as) na kuzungumza naye (juu ya siri za kimbingu au matukio ya baadae) wakati kukiwa hakuna mtu wa tatu pamoja nao au aliwasiliana naye kwa mnong’ono. Wakati mmoja Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa katika mazungumzo ya siri na Ali wakati Aisha alipoingia. Aisha akasema: “Ewe Ali! Mimi napata siku moja kati ya tisa [kuwa na mume wangu]; hivyo, kwanini ewe mtoto wa Abu Talib huniachii mwenyewe nikaifurahia siku hiyo kwa amani?” Kuyasikia maneno haya, uso wa Mtume mara moja ukageuka mwekundu kwa hasira. Rejea kwenye tukio hili mwanzoni mwa uk. 78, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul-Balaghah* ya al-Hamidiy.

# BARUA YA 77

## SAFAR 20, 1330 A.H.

**Kuomba Sababu za Kupendelea Hadithi za Umm Salamah.**

Mwenyezi Mungu akujaalie kuwa na amani! Hukuridhika na kutegemea hadithi ya Umm Salamah kuliko ile ya Aisha (Allah awe radhi nao wote). Umedai pia kwamba kuna sababu nyingi zaidi ya ulivyokwishaonesha. Ni sababu zipi hizo? Zieleze, rehema ya Allah iwe juu yako, bila kujali hata zikiwa ngapi, na usiache hata moja, kwani lengo letu ni kutafiti na kujifunza na kupata fursa ya kunufaika. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 78

## SAFAR 22, 1330 A.H.

**Sababu za Kupendelea Hadithi ya Umm Salamah kwa Nyongeza ya Zile Zilizokwisha Tangulia.**

Qur'ani Tukufu haionyeshi upotovu wowote kutoka kwenye wajibu kwa upande wa Bibi Umm Salamah na haikumuamuru kutubia,[347] na hakuna aya katika Qur'ani inayomuonya kwa utovu wa adabu kwa Mtume (s.a.w.w.) na kamwe hakuwa na vurugu ya kuwa muasi kwa warithi wake,[348] wala Mwenyezi Mungu hakumkumbusha juu ya msaada Wake kwa Mtume dhidi yake wala juu ya msaada wa Jibril, wa muumini na wa malaika, wala Allah hakumtishia talaka wala kumtishia kumbadilisha kwa mke bora kuliko yeye,[349] wala Allah hakumfananisha na wake za Nuh na Lut,[350] wala yeye kamwe hakumzuia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kufanya au kutumia kitu chochote ambacho Mwenyezi Mungu amehalalisha kukifanya au kukitumia.[351] wala Mtume (s.a.w.w.) hajahutubia siku yoyote na kuelekeza kidole chake kwenye nyumba yake na kusema: "Humo ndimo imelala fitina, Humo ndimo imelala fitina …; kutoka humo pembe ya shetani itachomoza."[352] Wala tabia yake haikumruhusu kunyoosha miguu yake mbele ya Mtume wakati alipokuwa anaswali na kuweka unyayo wake kwenye sehemu yake ya kusujudia bila kuuondoa ili kumheshimu yeye na swala yake, hakufanya hivyo na wala hakusubiri mpaka aminywe mguu wake na wala hakuunyoosha tena mguu huo na kuweka unyayo wake palepale mara tu Mtume aliposimama kwa ajili ya rakaa nyingine baada ya kusujudu.[353]

Umm Salma hakueneza taarifa za kukarahisha kuhusu Uthman na kupendekeza auwawe, wala hakumpachika jina la "Na'thal," wala hakusema "*Uqtul Na'thal faqad kafar!"* Muuweni Na'thal kwani amekuwa kafiri.[354] Umm Salma hakutoka nje ya nyumba yake, ambamo Allah Aza wa Jallah

---

[347] Hii ni marejeo kwenye aya ifuatayo katika Sura al-Tahrim: **"Kama ninyi wawili (Aisha na Hafsa) mtatubia kwa Mwenyezi Mungu, basi nyoyo zenu zimekwishaelekea kwenye haki. Na mkisaidiana dhidi yake Mtume, basi hakika Mwenyezi Mungu Ndiye kiongozi wake, na zaidi ya hayo Malaika pia watasaidia (dhidi yenu)." (66:4)**

[348] Aisha alikuwa muasi dhidi ya Ali (a.s.) na alikataa kuwa kwake mrithi wa Mtume (s.a.w.w.). Baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) yeye aliendelea kuwa adui mbaya na chuki naye muda wote alioishi. Ama kuhusu ukaidi wake kwa Mtume (s.a.w.w.), hili linathibitishwa na aya iliyotajwa kwenye tanbihi iliyotangulia ambayo kwa mujibu wake Mola Wake, na pia Jibril na watu wema miongoni mwa waumini, na hata malaika watamsaidia dhidi ya Aisha na Hafsa.

[349] Hiki ni kidokezo cha kwenye aya: **"Akiwapa talaka, asaa Mola Wake atampa wake wengine badala yenu ninyi, walio bora kuliko ninyi, wanyenyekevu, waumini, watiifu, waliotubu, wenye kushika ibada, wafanyao kheri, wajane na wanamwali." (66:5)**

[350] Hii inadokezea kwenye kauli ya Allah Aza wa Jallah: **"Allah amepiga mfano kwa wale wasioamini kwa mke wa Nuh na mke wa Lut."** Mpaka mwisho wa sura.

[351] Hii inadokezea kwenye aya: **"Ewe Nabii! Kwa nini unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? unatafuta radhi za wake zako! Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira Mwenye kurehemu" (Qur'ani 66:(1).**

[352] Hii inanukuliwa na Bukhari katika *Sahih* yake mlango wa "Kilichotokea kwenye nyumba za wake wa Mtume" katika tasnifu yake juu ya vita vitakatifu na wasifu wa Mtume. Vilevile iko katika *Sahih* yake ukurasa wa 125, Jz. 2, baada ya Mlango wa *khums* na malipo yake. Katika Maneno ya *Sahih Muslim* ni kama ifuatavyo: "Mjumbe wa Allah alitoka nje ya nyumba ya Aisha na akasema: "Humu ndimo mlimo kichwa cha usaliti ambamo pembe ya shetani itatokeza katika sehemu hii," Rejea kwenye uk. 502, Jz. 2 ya *Sahih Muslim*.

[353] Rejea kwenye Mlango wa "Matendo yanayoruhusiwa ndani ya swala," uk. 143, Jz. 1. ya *Sahih ya Bukhari*

[354] Aisha alieneza habari za kukarahisha kuhusu Uthman na kuvishukutumu vitendo vyake vingi, kumuita majina mabaya, na kauli yake: "Muuweni Na'thal, kwani amekuwa kafiri," ni maarufu sana kiasi hakuna kjitabu chochote cha historia kinachoshughulika na hali na matukio ya kipindi cha Uthman ambacho hakikunakili habari hizo. Utayakuta maneno haya katika vitabu vya historia vya *Tariikh Tabari* cha Ibn Jariir at-Tabari, *Tariikh Kamil* ya Ibn al-Athir (pamoja na maelezo ya kina kuhusu chuki yake dhidi ya Uthman) na wengine. Baadhi ya watu wa wakati wake huo walimuasa kuhusu tabia yake hiyo na pia wakamkemea ana kwa ana usoni mwake. Ibn Athiir katika uk. 80, Jz. 3 ya al-Kamil amenukuu baadhi ya beti kuhusu yeye kuhusiana na vita vya Jamal kama ifuatavyo: "Ni wewe uliyeanzisha mfarakano na uadui na ukaendelea kubadilisha rangi. Pepo zikavuma na mvua za ngurumo zikatoka upande wako. Ulituamuru kumuua Khalifa; Ukidai amegeuka na kuwa kafiri."

alimuamru kubakia humo,[355] na akapanda ngamia aitwaye *Askar* kama alivyofanya Aisha na akaongoza jeshi,[356] akipanda mlima au kushuka mabonde hadi mbwa wa sehemu ya karibu na chemchem ya Hawab wakambwakia ambapo ni jambo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alilokwisha kumuonya nalo mapema.[357] Hata hivyo, bado hakukubali ushauri bali alisisitiza kuongoza jeshi kubwa alilokusanya na kuliandaa kupigana na Imamu. Kwa hiyo, kauli yake kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alifariki akiwa juu ya kifua chake, unaweza kuiweka daraja moja na kauli yake: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aliwaona Wasudani wakicheza ngoma ndani ya msikiti wakiwa na mikuki na ngao zao, na akaniuliza, je unataka kuwatazama mchezo wao? ambapo nikasema 'Ndio, oh!' Nikasimama nyuma yake, mashavu yangu juu ya mashavu yake, na akasema: 'Zidisheni, zidisheni enyi Bani Arfada, endeleeni!'" Nilipochoka akaniuliza umetosheka? Nilipomuitikia akawaambia waache na mimi niondoke.[358]

Au unaweza kuiweka daraja moja na maneno yake: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) siku moja aliingia nyumbani kwangu wakati nilikuwa na vimwana wawili wakiimba kwa ajili yangu. Alilala kitandani. Wakati huohuo Abu Bakar akaingia na alipowaona waimbaji wale akanikaripia akisema: 'filimbi ya shetani inapulizwa mbele ya Mtume wa Allah?' Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akamgeukia na kumuambia: "Waache waendelee kuimba." [359] Au unaweza kuifananisha na hadithi yake kwamba "Siku moja mimi na Mtume tulifanya mashindano ya kukimbia pamoja naye na mimi nikamshinda. Baada ya muda wa siku kadhaa niliongezeka uzito na tukashindana tena. Safari hii alinishinda. Halafu akaniambia: 'Sasa nimelinganisha matokeo, tuko sare sasa!'"[360] Au iweke kundi moja na kauli yake: "Nilizoea kucheza na wasichana. Marafiki zangu wa kike walikuwa wakija kucheza na mimi, na Mjumbe wa Allah mwenyewe alikuwa akiwaleta kwa ajili ya kucheza na mimi."[361]

Au na hadithi yake nyingine: "Ninamiliki sifa saba[362] ambazo hakuna mwanamke ambaye amejaaliwa nazo isipokuwa sifa moja ambayo tumechangia na Mariamu bint Imran: "Malaika walishuka katika umbo langu; Mjumbe wa Allah amenioa mimi nikiwa bikira, hakuna mke mwingine wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliyeolewa akiwa bikira; kulikuwa na wakati ufunuo ukishuka yeye na mimi tukiwa katika shuka moja; mimi nilikuwa kipenzi zaidi kati ya wake zake; aya mbalimbali za Qur'ani ziliteremshwa kuhusu mimi ambazo kulikuwa na hofu ya kuangamia kwa umma; mimi nilimuona Jibril ambapo hakuna mke yeyote mwingine wa Mtume aliyemuona; na alivuta pumzi yake ya mwisho akiwa nyumbani kwangu ambapo kulikuwa hakuna mtu yeyote aliyekuepo humo isipokuwa mimi na malaika mauti."[363]

---

[355] Hii inadokezea aya ya Qur'ani anayosema: "**Na kaeni majumbani mwenu wala msidhihirishe mapambo** kwa madhihirisho yakijahiliya ya zamani. (Qur'ani, 33:33).

[356] Ngamia ambaye Aisha alimpabda wakati wa tukio la Basra alikuwa akiitwa *Askar*. Ngamia huyu aliletewa na Ya'li bin Umaiyya, na alikuwa mkubwa mwenye misuli ya nguvu. Wakati alipomuona alimpenda, lakini alipokuja kujua kwamba jina lake ni *Askar*, alibadilisha mawazo yake na akasema: "Mrudisheni, kwani sina haja naye," Alieleza kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimtabiria jina hilo na akamkataza asije akampanda; hivyo,. Walimrudisha, walibadilisha hatamu zake na wakamrudisha tena kwake na kusema: "Tumekuwa na bahati ya kumpata huyu mwingine mkubwa zaidi kwa ajili yako." Hivyo, alipendezewa naye na akamchukua. Tukio hili linatajwa na idadi ya waandishi wa historia na wasifu. Unaweza kurejea kwenye ukurasa wa 80, Jz. 2, ya *Sharh Nahjul-Balaghah* ya Ibn Abil-Hadid Mutazili.

[357] Riwaya kama hiyo ambayo inajulikana sana ni moja ya dalili za Utume wa Muhammad (s.a.w.w.) na nguzo ya alama ya Uislam. Imam Ahmad bin Hanbal ameinakili katika namna ya ufupisho katika riwaya ya Aisha kwenye *Musnad* yake Jz. 6. uk. 52 na 97. Imam Hakim pia amefanya kama hivyo wakati akiinakili kwenye uk. 120, Jz. 3 ya *Sahih al-Mustadrak* na Dhahabi amekiri ukweli wake kwa kuinakili katika *Talkhiis al-Mustadrak*.

[358] Hadithi hii kuhusu yeye haikanushiki. Imenukuliwa na Masheikh wote wawili [Bukhari na Muslim] katika *Sahih* zao; hivyo, unaweza kurejea kwenye *Sahih Bukhari*, mwanzoni mwa *Kitab Iidain* "Iddi mbili", uk. 116, Jz. 1, na rejea kwenye *Sahih* ya Muslim, Mlango juu ya "michezo inayoruhusiwa wakati wa sherehe za Iddi sio haramu," uk. 327, Jz. 1. Vilevile rejea kwenye *Musnad* ya Ahmad, uk. 57, Jz. 6.

[359] Hii imenukuliwa na Bukhari, Muslim na Imamu Ahmad bin Hanbal katika vitabu vyao kwenye Milango hiyohiyo na kurasa hizo hizo kama ilivyotajwa hapo juu.

[360] Kama ilivyo katika hadithi ya Aisha iliyonukuliwa na Imamu Ahmed katika uk. 39, Jz. 6 ya *Musnad* yake.

[361] Kama ambayo imenukuliwa na Imamu Ahmed katika uk. 75, Jz. 6, ya *Musnad* yake.

[362] Ibn Abi Shaybah ameinukuu na ni riwaya ya 1017 katika Jz. 5 ya *Kanz al-Ummal*.

[363] Inakubaliwa kwa pamoja kwambaMtume (saw) alifariki wakati Ali (as) akiwepo mbele yake na kwamba Ali (as) alikuwa akimuuguza na kumsaidia; hivyo, itawezekanaje kuwa sahihi kudai kwamba alifariki wakati hakuna mtu yeyote aliyekuwepo pale isipokuwa Aisha

Kuna Hadithi nyingine nyingi za Aisha zinazodai yeye kuwa na orodha kubwa ya sifa maalum ambazo ziko katika muundo huohuo.

Ama kuhusiana na Umm Salamah, alitosheka tu kuwa na ushirikiano kamili na *walii* wake na *wasii* na mrithi wa Mtume wake. Alikuwa na hekima iliyokomaa na pia alikuwa na uwezo wa maamuzi ya busara. Ushauri wake kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika siku ya Hudaibiyya ni ushahidi tosha ambao huthibitisha uwezo wa akili yake tambuzi, uamuzi wake wa busara, na hadhi yake ya hali ya juu; rehema na huruma za Allah ziwe juu yake. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

na malaika wa mauti? Ali (as) na Abbas walikuwa wapi? Na Fatima (as) na Safiyya alikuwa wapi? Au walikuwa wapi wake zake wote Mtume (saw) na kizazi chote cha Hashim? Vipi walimuacha kwa Aisha peke yake? Pia ni wazi kabisa kwamba Mariamu (as), kwa hakika hakuwa na sifa yoyote katika sifa saba ambazo mama wa waumini amehusishwa nazo, hivyo, ni busara gani ya yeye kumtumia yeye [Mariamu] kama mwanamke pekee tu.

# BARUA YA 79

## SAFAR 23, 1330 A.H.

**Makubaliano ya Wote Pamoja (*Ijmai*) Yalithibitisha Ukhalifa Wa Siddiq.**

Hata kama tukiyaitikia yote uliyosema kuhusu wosia wa urithi kwa fadhila za Ali kuwa ni ya kweli, halikadhalika tukakubaliana na ushahidi chungu nzima kwamba ni sahihi, basi utapuuza vipi kuhusu ukweli kwamba umma wote kwa pamoja (*ijmai*) ulikubaliana kutoa kiapo cha utii kwa [Abu Bakr] Siddiq? Makubaliano ya maoni ya pamoja (*Ijmai)* ya umma ni jambo zito lenye uamuzi kwa masharti ya kauli yake (s.a.w.w.): "Ijmai ya umma wangu kamwe haiwezi kuwepo kwenye jambo lolote la kimakosa," na kauli yake (s.a.w.w.): "Hakutakuwa na makubaliano ya umma wangu katika kupotoka kwenye njia iliyonyooka." Hivyo, utakuwa na lipi la kusema kuhusu hilo? Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 80

## SAFAR 24, 1330 A.H.

**Hakuna Makubaliano ya Pamoja – (*Ijmai*).**

Tunasema kwamba tunachokielewa kutokana na kauli ya (s.a.w.w.): "Hakutakuwa na Ijmai ya umma wangu kamwe juu ya jambo la kimakosa," na "Umma wangu kamwe hautakuwa na Ijmai katika kupotoka kwenye njia iliyonyooka," ni kwamba hakutakuwa na kosa, au upotoshaji kutoka kwenye njia ya haki katika lile ambalo umma kwa pamoja na kwa uhuru kabisa, unalitolea uamuzi baada ya majadiliano ya pande zote mbili. Hili ndilo linalojitokeza akilini mara tu baada ya kusikia au kusoma juu ya hadithi hizi, na si kingine chochote. Ama kuhusu suala ambalo huamuliwa na kikundi cha watu wachache ambao hatimaye wanaamua kuwalazimisha hata wale wenye kauli na hekima miongoni mwa jamii na kupitia kwao umma unalazimishwa kulikubali, hilo usahihi wake haujathibiti. Kiapo cha utii kilichochukuliwa pale Saqifa Bani Sa'ida hakikuwa ni suala lililoamuliwa kwa ushauriano wa pamoja wa umma wote. Bali kilikuwa ni uamuzi wa ghafla wa Khalifa wa pili akiungwa mkono na Abu Ubaydah na kundi la marafiki zao, ambao mara tu wakawasitukiza na kuwalazimisha wale raia ambao kwa hakika ndio wenye maamuzi na hekima hapo Madina kuukubali, na wakisaidiwa na mazingira yaliyoibuka wakati ule na hivyo wakafanikiwa kutekeleza mpango wao. Abu Bakar mwenyewe alikiri kwamba kiapo cha utii ambacho amepewa hakikuwa katika maafikiano na ushauriano angalifu wala busara. Alisema hivyo wakati alipokuwa anatoa khutba mwanzoni tu mwa ukhalifa wake ambayo kwayo aliuomba radhi umma kwa kusema: "Kiapo nilichopewa kilikuwa tukio la haraka ambalo Allah ametukinga na matokeo yake yenye madhara, ingawa nilikuwa na wasiwasi mkubwa usije ukatokea mgogoro na mfarakano wenye ghasia mbaya."[364] Umar alithibitisha habari hiyohiyo mbele ya umati mkubwa. Siku ya Ijumaa, mwishoni mwa Ukhalifa wake wakati alipokuwa akitoa khutba yake juu ya mimbari ya Mtume. Hii ni khutba ambayo ni maarufu sana ambayo Bukhari ameijumuisha katika *sahihi* yake.[365] Na kama ushahidi napenda niinukuu hapa kwa lafudhi yake haswa:

"Mtu mmoja [366] kati yenu amesema kwamba kama Umar akifariki, atatoa kiapo cha utii kwa fulani; kwa vile kiapo cha utii kwa Abu Bakr kilikuwa ni tukio la ghafla lakini hatimaye lilipita. Kusiwepo na kutoelewana kokote juu ya hilo. Bila shaka kiapo cha utii kwake kilitushukia kama mtelezo wa ghafla ambao mwishowe ulikubaliwa na wote na Allah akatukinga na matokeo yake maovu….." Kisha akaendelea: "Kama mtu atatoa kiapo cha utii kwa mtu yeyote bila ya ushauriano wa awali na umma, basi mwenye kutoa kiapo na yule mpokeaji wote wanaweza kuuliwa.[367] Akiendelea zaidi akasema: "Hali ambamo tuli-

[364] Hii imenukuliwa na Abu Bakr Ahmad ibn Abdul-Aziz al-Jawhari katika kitabu chake *Al-Saqifa* ambayo Ibn ul Hadid ameinakili katika uk. 132, Jz. 1, ya kitabu chake *Sharh Nahjul Balaghah*.

[365] Tafadhali rejea *Sahih* yake, Mlango wa 'Makatazo na Adhabu zake juu ya makafiri na wenye kuritadi,' ukurasa wa 119, Jz. 4 ambamo utaiona hotuba hiyo pamoja na vitangulizi vyake. Vilevile imenkuliwa na waandishi mbalimbali wa hadithi na historia kama vile Ibn Jarir na al-Tabari katika Tarikh yake ambamo anajadili matukio ya mwaka wa 11 H.A, na inawasilishwa na Ibn Abul-Hadid katika ukurasa 122, Jz. 1, ya kitabu chake *Nahjul-Balaghah*.

[366] Mtu aliyetoa kauli hii alikuwa ni Zubair. Alikuwa amesema: "Wallahi mara tu Umar atakapofariki, nitakula kiapo cha utii kwa Ali." Umar alipokuja kulitambua hilo alikasirika sana, na alitoa khutba hiyo iliyotajwa. Tukio hili limeelezwa na wafafanuzi wengi wa *Sahih al-Bukhari*. Rejea kwenye maelezo ya hadithi hii katika *Sharh* ya al-Qastalani, uk. 352, Jz. 11, ambaye ameinakili kutoka kwenye '*al-Ansab'* ya Baladhuli na amekiri usahihi wa hadithi hii kwa mujibu wa kuthibitishwa na masheikh wote wawili (Bukhari na Muslim).

[367] Ngoja nitoe maoni kwamba ule uadilifu ambao kwamba umemfanya Umar awe maarufu sana ulimtaka yeye mwenyewe kutumia kanuni ileile kwake yeye na rafiki yake Abu Bakr kama alivyoitangazia hadhara; yaani, mtu atakayetoa kiapo cha utii kwa mwingine bila ya kutanguliwa na mashauriano ya Ummah na vilevile yule anayepokea kiapo hicho lazima wauawe na yeyote kati yao asikubaliwe kuwa

jikuta tukiwemo sisi wenyewe wakati Allah alipomchukua Mjumbe wake (s.a.w.w.) kutoka kwetu ilikuwa kwamba Answar walitofautiana na sisi katika mitazamo yao; wote walikusanyika pale Saqifa [ukumbi wa] Bani Sa'idah. Ali (a.s.) na Zubair, na wafuasi wao, wao walitupinga sisi." Kisha akarejea kile kilichotokea kule kwenye ukumbi wa Saqifa, tofauti za maoni, makelele na mabishano na kisha akasema: "Yote haya yangeishia katika mgawanyiko katika umoja wa Uislam." Ilikuwa ni katika mazingira haya ambapo Umar alikula kiapo cha utii kwa Abu Bakr.

Kumbukumbu za kihistoria na hadithi zinaonyesha kwamba hakuna hata mtu mmoja wa Nyumba ya Mtume (s.a.w.w.), walinzi wa Ujumbe, aliyehudhuria hapo Saqifa. Wote walikuwa katika nyumba ya Ali pamoja na Salman, Abu Dharr al-Ghifari, al-Mikidad ibn al-Aswad al-Kindi, Ammar bin Yasir, al-Zubair bin al-Awwam, Khuzaymah bin Thabit, Abi bin Ka'b, Farwah bin Amr bin Wadqah al-Answari, al-Bara bin Azib, Khalid bin Sa'd bin al-Aas al-Amawi, na wengine wengi. Hivyo inawezakana vipi kuitwa kwamba ni makubaliano ya maoni ya pamoja ambapo hakuna yeyote kati watu hawa, pamoja na kizazi cha Muhammad (a.s.) ambaye alikuwa amehudhuria hapo Saqifa, ambapo Ahlul-Bayt kwa umma ni kama kichwa na mwili, au macho kwa ajili uso, wapendwa wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na vifua vya hifadhi ya ilmu, wanaolingana na Kitabu cha Allah, pia ni wasafiri wenza wa Kitabu cha Allah, safina ya wokovu, na mlango wa msamaha kwa usalama wa Umma wake dhidi ya kupotoka kwenye imani ya kweli, na bendera za mwongozo wake, kama tulivyothibitisha hapo juu…,[368] hawakuhudhuria [kule Saqifa], ingawa hadhi yao na sifa zao hazihitaji utambulisho wala uthibitisho. Katika mazingira haya basi, inawezekanaje kimantiki kuthibitishwa kwamba Ukhalifa wa Abu Bakr ulianzishwa kwa makubaliano ya maoni ya Umma?

Wote Bukhari na Muslim[369] katika *sahih* zao, kwa nyongeza ya wengine wengi wa wasimuliaji wa hadithi mashuhuri na wanahistoria, wote wamethibitisha ukweli kwamba Ali (a.s.) hakushiriki kula kiapo cha utii kwa Abu Bakr, na kwamba hakufanya maafikiano na kufanya amani isipokuwa baada ya miezi sita Bibi wa mabibi wa ulimwengu, Fatimah (s.a.) alipofariki na kuungana na baba yake (s.a.w.w.) [Peponi], na baada ya kiapo kwa Abu Bakr huko Saqifa, akilazimishwa haswa na mazingira magumu na masilahi ya Uislamu wakati huo, na haja shinikizi ya uwasilishaji sahihi wa Uislam na ufafanuzi wa misingi yake, ndipo Ali (a.s.) alipokubali kutoa ushirikiano wake kwa serikali na kutoa huduma alipotakiwa kufanya hivyo au ilipobidi. Ushuhuda wa habari hizi unatolewa na Aisha mwenyewe ambaye anasema: "Az-Zahra (s.a.) hakuwa radhi na Abu Bakr na alimsusia hata kuongea naye baada ya kifo cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) mpaka alipokufa, na wakati Ali (as) alipofanya maelewano ya amani nao, aliwalaumu kwa kumnyima nafasi yake katika ukhalifa." Hadithi hii kama unavyoona haitaji chochote kuhusu kula kwake kiapo cha utii kwa Abu Bakr wakati wa maelewano hayo. Kauli yake inathibitishwa na malalamiko makali wakati aliposoma beti mbili zenye maana kama ifuatavyo:

"Wewe ulitoa madai yako juu ya kumrithi Mtume (s.a.w.w.) kwa kuwaambia wapinzani wako kwamba una nasaba naye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kama nasaba na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilifanywa kuwa msingi wa urithi, basi mimi nina haki bora zaidi ya kumrithi Mtume na kustahikiv zaidi kwa sababu ndiye ndugu wa karibu sana naye. Na kama ukisema kwamba ulichaguliwa kusimamia mambo ya Umma kwa makubaliano ya maoni ya pamoja (*Ijmai*), Yalikuwa wapi basi makubaliano ya maoni ya wale wenye maamuzi bora na maoni makini waliokuwa hawapo pale Saqifa?!"[370]

---

Imam. Umar mwenyewe alitoa kiapo cha utii kwa Abu Bakr kwa ghafla tu bila ya ushauriano wa Ummah. Yaliyomo kwenye hotuba yake hiyo aliyoitoa hadharani yameandikwa vitabuni na waandishi wengi wa matukio ya kihistoria. Unaweza kumrejea mwanachuoni Ibn Abul-Hadid katika kitabu chake *Sharh Nahjul-Balaghah* uk. 123, Jz. 1.

[368] Rejea Kwenye Barua ya 6 na zile zinazofuatia mpaka mwisho wa Barua ya 12, na utafahamu utukufu na umuhimu wa Ahlul Bayt (a.s.).

[369] Rejea *Sahih Bukhari* uk. 39, Jz. 3 mwishoni mwa Mlango juu ya Vita vya Khaibar. Vilevile rejea *Sahih Muslim*, kwenye Mlango juu ya kauli ya Mtume: "Hatuachi mirathi, kwani chochote tunachokiacha ni kwa ajili ya sadaka" katika '*Kitab Jihad'*, katika uk. 72, Jz. 2, na utaliona suala hili kwa urefu kama tulivyolieleza.

[370] Beti zote hizo za kimashairi zimejumuishwa katika *Nahjul-Balaghah.* Ibn Abul-Hadid amesema hivyo wakati akizifafanua katika kitabu

Abbas ibn Abdul Muttalib wakati fulani alihoji suala la urithi vivyo hivyo. Wakati wa mahojiano kati yake na Abu Bakr[371] alisema: "Kama ulirithi kama Khalifa kwa msingi wa uhusiano wako na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), basi umepora haki yetu sisi kwani sisi ndio ndugu wa karibu kabisa, na kama umeupata Ukhalifa kwa msingi wa kuchaguliwa na Waislamu, basi uchaguzi huo ulikuwa ni batili madhali sisi ambao ni wa mwanzo kabisa katika Uislam hatukushiriki uchaguzi huo na hatukubali matokeo yake." Wakati ammi yake Mtume (s.a.w.w.) na binamu yake wa kiumeni ambaye ni ndugu yake mpendwa, Ali (a.s.) na familia yote ya Ahlul-Bayt na wafuasi wao wamethibitisha wazi madai ya Abu Bakr juu ya urithi ni ya bandia, inawezekana vipi kusemwa kwamba kuchaguliwa kwake kulipatikana kupitia makubaliano ya maoni ya pamoja ya Umma?

**Wako Mwaminifu, Sh.**

chake *Sharh Nahjul-Balagha*, uk. 319, Jz. 4, akiongeza: "Kauli yake inaelekezwa kwa Abu Bakr, kwani Abu Bakr alibishana na Ansar kule Saqifa, akisema: 'Sisi tuna haki bora ya kumrithi Mtume wa Allah (s.a.w.w.) kwa sababu alikuwa wa kabila moja naye na kinasaba alikuwa anahusiana naye pia.' Hivyo wakala kiapo cha utii kwake dhidi ya Answari na akawa juu ya mambo ya Ummah kwa msingi wa uhusiano wake na Mtume wa Allah (s.a.w.w.). Hivyo Ali (a.s.) alimwambia Abu Bakr kwamba wakati yeye akiwa wa kabila moja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yeye Ali alikuwa ni ndugu yake wa karibu zaidi na kwa kwa hiyo alikuwa na haki bora zaidi kuliko yeye. Ama kuhusu hoja yake nyingine ya kuteuliwa na ummah, ambao umeridhia kumkubali kama Khalifa, Ali (a.s.) alimjibu kwamba wakati wengi wa masahaba mashuhuri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hawakuwepo kule Saqifa na hawakushiriki katika mchakato wa kula kiapo, huo unaoitwa uchaguzi na hatimaye kukubaliwa na Ummah vyote vilikuwa ni batili na hoja hiyo ni dhaifu mno. Haikuwa ni *ijma* ya Ummah. Sheikh Muhammad Abduuhu, Mufti mkuu wa Misri ametoa maelezo juu ya beti hizi mbili katika pambizo ya Nahjul-Balaghah.

[371] Tafadhali rejea uk. 16 wa kitabu *Al-Imama wal Siyasa* chake Ibn Qutaybah.

# BARUA YA 81

## SAFAR 28, 1330 A.H.

**Makubaliano ya Maoni ya Pamoja Yalijitokeza Yenyewe tu Wakati Upinzani Ulipokoma.**

Ahlus-Sunni hawakatai ukweli kwamba kiapo cha utii kwa Abu Bakr hakikutokana na ushauriano wa kabla au makubaliano ya maoni ya Umma wala kutokana na tafakari makini. Bali wanakiri kwamba ilitokea kwa ghafla na bila kutegemewa. Wanakiri kwamba Answar walipinga uchaguzi huo na walitaka kumteua Sa'd mtu wao waliyempendelea kuwa Khalifa. Zaidi ya hayo wanakiri kwamba Bani Hashim na wafuasi wao kutoka miongoni mwa Muhajirun na Answar walipinga uchaguzi huo na walitaka kumuona Imamu Ali (a.s.) kama mrithi na Khalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini hata hivyo wanasisitiza kwamba hatimaye ukhalifa wa Abu Bakr ulikuwa ni jambo lililokwisha kupitishwa na kukubaliwa na kila mtu kama Imamu wake wakati mgogoro ulipotulia, mfarakano ukaisha, na kila mmoja akaamua kumuunga mkono na kumsaidia al-Siddiq katika kutekeleza kazi yake nzito na wakamtakia mema faraghani na hadharani. Hatimaye wote walipigana vita na yeyote aliyepigana naye, na walifanya amani na aliyekuwa na amani naye na wakatekeleza amri zake na makatazo yake. Hakuna mtu yeyote aliyekwenda kinyume naye, hivyo makubaliano ya maoni ya pamoja (*ijmai*) hatimaye kwa ujumla yalipatikana, na urithi wa Abu Bakr ukathibitishwa. Sifa zote ni za Allah kwani kulikuwa na umoja kamili katika Umma baada ya mfarakano na mgawanyiko, na nyoyo zao zikaridhiana baada kuhasimiana. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 82

## SAFAR 30, 1330 A.H.

**Hayakuwapo Makubaliano ya Maoni ya Pamoja (*Ijmai*), na Ugomvi na Mgawanyiko Havikwisha.**

Kwamba watu mwishowe walikubaliana kumuunga mkono al-Saddiq katika utendaji kazi wake na kuanza kumtakia mema faraghani na hadharani ni kitu kimoja; na kuhakikishwa au kuthibitishwa kwa ukhalifa kwa *ijmai* (makubaliano ya pamoja) ni kitu kingine kabisa. Havina uhusiano wa kiakili au kisheria, na uhusiano mmoja hauwi sharti au kigezo cha mwingine. Kila mmoja anafahamu msimamo wa Ali na wa Maimamu wote maasum watokanao na kizazi chake (a.s.) kwa watawala wa Waislamu wa zama zao. Msaada wao wa thamani na wa kujitolea ulikuwa ukipatikana kwa ajili ya watawala wa Waislam wakati wowote walipokuwa na matatizo. Wakati wowote msaada wao ulipohitajika kwa ajili ya kutatua matatizo magumu wao waliutoa kwa hiari kabisa. Na huo ndio msimamo wetu pia. Ninatoa hapa majibu ya kina katika kujibu kile ambacho umekielezea.

Maimam watukufu wakati wote walishikilia maoni kwamba Umma wa Kiislamu kamwe hauwezi kustawi na kutawala heshima ya umma nyinginezo, isipokuwa iwe na nguvu ya kutosha ya kuwakusanya Waislam wote chini ya bendera moja na wabaki wameungana, kuondosha vurugu na ghasia katika kundi lao, kuziba ufa wowote kwenye muundo wake, kulinda mipaka yake, na kuweka jicho la uangalifu juu ya watu na mambo yao. Na dola haiwezi kuwa madhubuti na tulivu isipokuwa iwe raia wanashirikiana nayo na wanaiunga mkono kwa uhai na mali zao. Kama dola ikiongozwa na mtawala halali yaani mrithi wa Mjumbe wa Allah, ambaye anashikamana hasa na Sunnah zake katika uendeshaji wake wa siku hadi siku basi yeye ndiye mrithi halali wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ndiye atakayesimamia serikali hiyo. Lakini kama hili haliwezekani, na hatamu za serikali zikinyakuliwa na mtu mwingine yeyote kwa mabavu, basi ni wajibu wa lazima juu ya Umma kushirikiana naye na kumuunga mkono katika masuala yote ambayo yatapelekea kwenye uendelezwaji wa mamlaka na utukufu wa Uislam, ulinzi wa mipaka ya dola yake na kudumisha amani na usalama wa dola.

Hairuhusiwi kwa mtu yoyote kuleta faraka miongoni mwa Waislamu na kusababisha mgawanyiko miongoni mwao kwa kusimama katika uasi dhidi ya mtawala na hivyo kuudhoofisha Umma na kuugawa katika makundi. Na haliishii hapo tu. Bali ni wajibu juu ya Umma kwenda na kiongozi huyo kama ambavyo wangefanya makhalifa wa haki katika kulipa kodi na mapato *(khira'ji)* ya ardhi na zakat ya ng'ombe na kadhalika. Umma una haki ya kukubali mauzo na manunuzi ya mali inayohamishika iliyopatikana kwa njia ya tuzo, zawadi ama njia nyingine za halali.

Huu ulikuwa ndio msimamo wa Ali na Maimamu watoharifu (a.s.) watokanao na kizazi chake. Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alisema: "Baada yangu kutakuwepo na ubinafsi, uhalifu wa kishenzi na matukio ya kuchukiza." [372] Watu walimuuliza Mtume (s.a.w.w.): "Ewe Mjume wa Allah! Unamuamrisha afanye nini mmoja wetu atakapo yashuhudia hayo?" Yeye (s.a.w.w.) alijibu: "Tekeleza wajibu wako kama raia mwema na umuombe Allah kwa ajili ya kupatikana ulinzi wa haki yako." Abu Dharr al-Ghiffari (r.a) alikuwa mara kwa mara akisema:[373] "Mpendwa wangu, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alinishauri kumsikiliza na kumtii kiongozi hata akiwa ni mtumwa ambaye mikono yake na miguu imekatwa."

[372] Hii inajitokeza katika hadithi moja iliyosimuliwa na Abdullah bin Mas'ud ambayo imenukuliwa na Muslim katika uk. 118, Jz. 2, ya *sahih* yake, pia kusimuliwa na waandishi wengi wa *sahih* na muhadithina.

[373] Muslim ameinakili katika *Sahih* yake Jz. 2, na ni miongoni mwa hadithi maarufu sana

**Salmat ul-J'afi alisema:**

"Ewe Mjumbe wa Allah! Je, kama tukitawaliwa na wale ambao wanatutaka sisi tutekeleze wajibu wetu kwao ambapo wao wenyewe wanakataa kutupa haki zetu, unatushauri kufanya nini?" Yeye (s.a.w.w.) alimjibu akisema: "Wasikilizeni na muwatii, kwani wao watawajibika juu ya kazi zao, nanyi mtaulizwa juu ya matendo yenu." Na kwa mujibu wa hadithi ya Hudhaifah al-Yamani (ra), [374] Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Kutakuwepo watawala baada yangu ambao hawatawaongozeni kwenye njia yangu, wala kufuata Sunna yangu; na mara tu watakuwepo viongozi ambao wana nyoyo za shetani ndani ya miili ya kibinadamu." Hudhaifah anasema nikamuuliza Mtume (s.a.w.w.): "Basi nifanye nini, Ewe Mjumbe wa Allah! kama ikitokea kuyashuhudia haya?" Yeye (s.a.w.w.) alijibu: "Utamsikiliza mtawala huyo na kumtii; kama akikutia majeraha na kutaifisha mali yako, bado [huna jinsi] utaendelea kumsikiliza na kumtii." Hadithi inayofanana na hii ni ile iliyosimuliwa na Umm Salamah hivi:[375] "Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema mara tu watakuwepo watawala [waovu] juu yenu ambao watatoa amri zinazokubalika na mbovu na makatazo pia. Wale ambao wanaoitambua amri na katazo kuwa sio ya halali (na hawana shaka juu ya uharamu wake) wataokolewa na dhambi hiyo ya uridhikaji, kwa kupinga na kukataa amri hiyo ama katazo kwa kivitendo au kwa ulimi na hayo yakishindikana basi waidharau na kuichukia amri potovu kwa mioyo yao. Yule ambaye hajui (juu ya uharamu wake) atakuwa hafanyi dhambi kwa kuitekeleza amri hiyo."[376] Walimuuliza (s.a.w.w.): "Je, hatupaswi kuwapiga?" Akajibu: "Hapana, maadamu wanasimamisha swala zao za kila siku."

Kuna hadithi nyingi *sahih* na mutawatir kuhusiana na suala hili, hususan zile zilizopokelewa kupitia kizazi kitoharifu cha Mtukufu Mtume (a.s). Na ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba Maimamu hawa wa Ahlul-Bayt watoharifu walidumu katika subira na kujizuia na kutenda lolote dhidi ya watawala waovu na katili, licha ya kizazi hicho kutokutulia kama mtu aliyetupiwa vumbi machoni na kukwamwa na mfupa kooni. Lakini walitekeleza kwa makini kabisa maagizo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) bila ya kutetereka wala kuyumba hata katika mazingira magumu kabisa na yaliyothubutu kwa sababu yeye Mtume (s.a.w.w.) aliwaelekeza kivitendo na kwa msisitizo kuhimili kwa subira madhara yoyote au balaa na kupuuza maudhi yote na usumbuvu utakaosababishwa kwao ili kwamba utulivu wa akili wa watawala hao usitibuliwe, na usalama na utukufu wa taifa viweze kudumishwa. Waliendelea kutoa ushauri mzuri kwa watawala Waislamu licha ya kwamba wao wamewapora haki yao wao, na mazingira yao ni ya shida na licha ya ukweli kwamba aliyepanda kwenye usimamizi wa mambo ya taifa ametengeneza vikwazo vizito katika njia yao ya muongozo sahihi kwa Umma. Kope za macho yao zilikuwa zinauma na nyoyo zao zilikuwa na maumivu makali kwa sababu ya mandhari mabaya ya ukandamizaji na dhulma, bado waliendela tu kutekeleza ushauri wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kutimiza majukumu yao kwa kadri Sharia inavyohusika. Walishikamana na utiifu madhubuti wa yaliyokuwa halali na ya lazima kimsingi juu yao katika mtazamo wa ustawi wa dola na Umma kuliko haki zao wenyewe hata kulipokuwa na mgongano wa maoni.

Ilikuwa ni kwa sababu ya sera hii kwamba Amirul Muminin (a.s.) aliwatakia kheri kwa uaminifu kabisa na alikuwa akiwapa ushauri makhalifa wote watatu wa kwanza. Yeyote yule mwenye kuchunguza sera na tabia ya Imam Ali (a.s.) wakati wa kipindi chao atafahamu kwamba hata baada ya kupoteza matumaini yote ya kupata haki yake ya urithi wa mara moja kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), kwa hiyari alitwaa njia ya kuwapendelea heri na amani wale waliokuwa

[374] Hii imesimuliwa na Muslim katika ukurasa wa 120, Jz. 2, ya *Sahih* yake, ambayo inasimuliwa pia na wana hadithi wakubwa wote .

[375] Hadithi hii imesimuliwa na Muslim katika uk.122 wa Jz. 2 ya *Sahih* yake

[376] Hadithi hii imenukuliwa na Muslim katika ukurasa wa 122, J. 2, wa *Sahih* yake. Maana ya usemi wake (saw) "Yeyote aujuae hana hatia" ni kwamba yeyote ajuaye kuchukiza kwake na akautambua kama hivyo, atapata njia iongozayo kwenye kujitenga na uovu wake na adhabu yake kwa kuubadisha (uovu huo) kwa mkono wake mwenyewe au kwa ulimi wake, lakini kama hawezi, basi naauchukie kwa moyo wake.

kwenye mamlaka. Aliona kwamba taji lake aliloahidiwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) likiwa kwenye mikono yao, bado hakupigana nao wala kuwapinga, wala kujaribu kuwaondoa kwa sababu alipendelea amani ya umma na usalama wa taifa na usalama wa dini kuliko yeye mwenyewe. Aliyapuuza ya wakati uliopo na akatupa macho yake kwenye ya baadae. Aliteseka kwa machungu ambayo hakuna yeyote aliyeyajua. Alikuwa na mizigo miwili ya kuchosha mabegani mwake; ukhalifa wenye nususi na matamko kwa upande mmoja, ambayo yalikuwa yanapiga kelele ya kutaka kumsaidia, huku yakimvuta kwa sauti yao kali iliyochoma moyo wake na kwa mkoromo ambao ulitikisa maini yake. Na upande wa pili kulikuwa na ghasia kubwa na maasi yaliyojitokeza, mambo ambayo yalikuwa yamejaa hatari ya uwezekano wa kuvipoteza visiwa vya Bara Arabu, kuleta mapinduzi katika nchi na kuangamiza moja kwa moja Uislam. Kulikuwa pia na hatari ya njama kutoka kwa wanafiki wa Madina ambao walikuwa waovu vibaya sana, na ya Waarabu mabedui wa vitongojini ambao kwa mujibu wa Qur'ani wameitwa "*Munafiqiin*" ambao walikuwa wauovu zaidi katika ukafiri na unafiki wao, na ambao kwa kiasi kikubwa walibaki hawajui kile ambacho Allah amekiteremsha kwa Mjumbe Wake (s.a.w.w.).

Kufariki kwa Mtume (s.a.w.w.) kuliwapa nguvu mabedui hawa katika unafiki wao na ukawa unaongezeka taratibu wakati hali ya Waislamu ilikuwa ni kama ya kondoo anayekimbia katika usiku wa kipupwe wenye giza nene kati ya mbwa mwitu na wanyama wakali wa mwituni. Manabii wa bandia kama vile Musailamatul-Kadhab, Tulayha bin Khuwailid na Sajah binti Haras walijichomoza na wao pamoja na marafiki na wafuasi wao walikuwa imara katika harakati zao za kuifuta dini ya Uislamu na kuwaangamiza Waislamu. Kaisari wa Roma na ma-Khusruu wa Uajemi nao kadhalika walikuwa wanangojea fursa ya kuivamia dola ya Kiislam. Walikuwa katika mtego wa uvamizi pamoja na vikundi vingine vingi vya wote ambao walikuwa na chuki dhidi ya Muhammad (s.a.w.w.), na walikuwa na hisia za kulipa kisasi dhidi ya Muhammad na kizazi chake na masahaba wake Muhammad wa kweli. Makundi haya yalikuwa na uadui na husda juu ya 'ujumbe wa Uislamu; yaani ule wa "Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah na Muhammad ni Mtume Wake," na walipania kuuhujumu na kuing'oa mizizi yake. Nguvu zote hizi zilikuwa zina juhudi sana na harakati ya kuuangamiza. Waliona kwamba wakati umewadia wa kutimiza matarajio yao na kuondoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kumewapatia fursa. Walidhamiria kutoruhusu fursa hiyo iwaponyoke na kutumia vizuri nafasi hiyo ya machafuko na ghasia zilizotokea baada ya kifo chake kabla hazijayeyuka na kurudisha utaratibu wa nidhamu, na utukufu wa Dola ya Kiislamu ukarejea. Hizi ndio hatari mbili mbaya sana katika kila upande wa Amirul Muminin Ali (a.s.), kutwaliwa kwa haki yake na kupitishwa Ukhalifa kwenye mikono isiyostahiki kwa upande mmoja, na kazi yote na juhudi zote za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kupotea bure na kuharibika na Uislam kuzimwa, kwa upande mwingine. Tabia yake ilimsukuma kutafuta usalama na kulinda uhai wa Uislam, na kuboresha hali za watu kwa kuzitoa muhanga haki zake mwenyewe.

Hivyo aliamua kupuuza zile tofauti kati yake na Abu Bakar kuhusu ukhalifa na kukomesha ukatikaji wa mahusiano kati ya kundi lake na kundi la Abu Bakr. Uamuzi huu wa Imam Ali (a.s.) ambao ndio mnaouchukulia kama ushahidi wa makubaliano ya maoni ya pamoja ya Umma ulichukuliwa kwa ajili ya kulinda Uislamu kutokana na maangamizi na kuwaokoa Waislam kutokana na upotevu. Hivyo, yeye, pamoja na watu wote wa nyumbani kwake, wafuasi wake kutoka Muhajirun na Answar, walistahimili kwa subira uporwaji wa haki zao na matokeo ya huzuni na mateso yoyote, ingawa walikuwa wamemwagiwa vumbi machoni mwao na mifupa kukwamishwa kwenye makoo yao. Mazungumzo na khutba za Ali (a.s.) baada ya kuondoka Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) vinabeba ushahidi wa kutosha kuhusu suala hili. Na kuna riwaya nyingi zilizosimuliwa kwa mfululizo (mutawatir) kutoka kwa Maimamu wa kizazi toharifu cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Lakini kiongozi mkuu wa Answar, Sa'd bin Ubadah, hakusikilizana kamwe na makhalifa wawili wa mwanzo, na hakukusanyika hata katika Swala za jamaa za Ijumaa ama katika zile za sherehe za Idd. Na kamwe hakuwajali kabisa wao wenyewe wala maneno yao. Amri zao na makatazo yao hayakuwa na athari kwake. Alishughulikiwa kuuliwa kwa siri huko Huurani wakati wa kipindi cha Khalifa wa pili, na wauaji wake wakadai kwamba ameuawa na majini. Alitoa maelezo yenye kumbukumbu wakati wa kadhia ya Saqifa, lakini hatuoni haja ya kuyanukuu hapa.[377]

Ama kuhusu marafiki zake kama vile Haban ibn Mundhir[378] na Answar wengine, hawa bila ya hiyari walisalimu amri kwa kuogopa nguvu za wale waliokuwa madarakani, na wakajinyenyekeza kwenye shinikizo lao. Kitendo chao kilikuwa ni matokeo ya hofu ya kuuliwa kwa upanga au nyumba zao kuchomwa moto. [379] Hivi utii wao katika mazingira kama hayo ni kiapo cha uaminifu kweli? Maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) "Hakutakuwa na makubaliano ya pamoja katika makosa miongoni mwa Umma wangu" yanaweza kutumika katika hii inayoitwa *"ijmai"* ya maoni ya Umma? Tunaliacha hili kwenye uamuzi wako mwenyewe; Allah akulipe. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

377 Sa'd bin Ubadah, ambaye anajulika pia kama Abu Thabit, alikuwa miongoni mwa wale waliochukua kiapo cha utii kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kule Aqaba. Vilevile alishiriki Vita vya Badr na vita nyingine. Alikuwa ni kiongozi na mkuu wa kabila la Khazraj, mtu maarufu aliyekulikana kwa ukarimu wake. Vitabu vya wasifu na historia vimejaa kauli zake ambazo tumezidokeza. Kuhusu hili unaweza kurejea kile ambacho Ibn Qutybah amekisema katika kitabu chake *Imamat wa al-Siyasat*, Ibn Jarir al-Tabari katika *Tarikh* yake, Ibn al-Athir katika *Taarikh al-Kamil,* Abu Bakr Ahmad bin Abdul-Aziz al-Jawahir katika *Al-Saqifa,* na wengineo.

378 Habib alikuwa mmoja wa wakuu wa Ansar na alishiriki vita vya Badr na Uhud, mtu mkarimu na sifa njema aliyeheshimiwa sana. Yeye alikuwa akisema: "Mimi ni [mwenye nguvu na imara] kama shina la mti ambalo ngamia hujikunia miili yao, na ni nguzo inayotumiwa kwenye mtende uliolemewa na matunda na kuwezesha kuhimili ule uzito wa ziada." (Hii ina maana kwamba ushauri wake mzuri unaweza kuponya maradhi na kuondoa mateso na mabalaa) Mimi ni simba kwenye tundu lake mwenyewe; na Wallahi naweza kula karamu ya watu wenye ujana na nguvu, kama mkipenda." Alitoa kauli nyingine kali zaidi, na tumeona ni busara kujizuia tusizinukuu hapa.

379 Umar alitishia kuichoma nyumba ya Ali. Tishio hili linathibitishwa na riwaya sahihi na *tawtur* kamili. Angalia alichosema Imamu Qutaybah mwanzoni mwa kitabu *al-Imamat wa al-Siyasat*, Imamu al-Tabari katika sehemu mbili ambako alijadili matukio ya mwaka wa 11 A.H., katika kitabu chake mashuhuri cha *Tarikh*, Ibn Abd Rabbih al-Malik katika kitabu chake *Iqd al-Fariid* Jz. 2 chini ya kichwa cha maneno "*Saqifa"* na Abu Bakr Ahmad bin Adul Aziz al-Jauhari kitabu kitabi chake *As-Saqiifa* kama ilivyonukuliwa katika Jz. 1, uk. 134, wa *Sharh Nahjul Balaghah* cha al-Hamiid al-Hadiidi, na al-Mas'udi katika *Muraj al-Dhahab* akimnukuu Urwah bin al-Zubeir wakati alipoomba radhi kwa niaba ya ndugu yake Abdullah ambaye alipendekeza kuchoma moto nyumba za kizazi cha Hashim kwa sababu walisusa kula kiapo cha utii kwake,alirejea tisho la Umar kwa Ali (a.s.) na kuchoma nyumba yake kama mfano. al-Shahristani ambaye anamnukuu al-Nizam katika kitabu chake *Al-Mial wal-Nihal* kuhusiana na maelezo juu ya kundi la Nizamiya. Abu Mikhnaf ameelezea kwa kina tukio la Umar kuchoma moto nyumba ya Ali ndani ya kitabu chake kwenye kichwa cha maneno 'Taarifa za Saqifa' tukio ambalo tumelidokezea. Tukio hili maarufu limezungumziwa katika beti tatu za mshairi mashuhuri wa Bonde la Mto Nile, al-Hafidh Ibrahim katika shairi lake mashuhuri juu ya Umar. Beti hizo zina maana:

Kauli ya Umar kwa Ali kumuambia; hivyo kidogo fikiria;
Wasikilizaji wake waisifia, mheshimu mzungumzaji na zingatia,
Nitaichoma yako nyumba, na lundo la majivu kuifanya
Kama mkaidi utakuwa, na kiapo kukataa kula
Nitaichoma hata kama bint wa Mustwafa, yuko ndani humo sikia
Si mwingine msemaji aliyekuwa, bali ni Abu Hafsa
Akimuambia shujaa wa Adnani na mlizi…

Hivyo ndivyo walivyomfanya Imamu (a.s.) ambaye bila makubaliano yake, mapatano ya pamoja, kwa mujibu wa maoni yetu kamwe hayawezi kuwa (kiapo) cha kutiiwa na sisi kukiamini. Mbali na kutoshauriana naye, nguvu za kikatili zilitumika juu yake kama ulivyosoma hapo juu. Sasa vipi utasema kwamba Abu Bakr alichaguliwa kumrithi Nabii (s.a.w.w.) kwa makubaliano ya pamoja ya Ummah? Kweli hii ni Ijmai?

# BARUA YA 83

**Rabi'ul Awwal 2, 1330 A.H.**

**Utathibitishaje Kwamba Masahaba wa Mtume, kwa Kujua Hasa,**

**Walipuuza Hadithi Zake na Bado Wakawa Hawana Hatia ya Upotofu?**

Wale ambao wamejaaliwa ujuzi makini na akili zenye kupenya huwaona masahaba kama watu walioepukana na kukosa utii kwa Mtume (s.a.w.w.) katika chochote anachoamrisha au kukataza. Hakuna chochote isipokuwa utii usio na masharti kwake na utekelezaji wa hiari wa amri zake ndio ungeweza kutegemewa kutoka kwao. Kwa hiyo, haiwezekani wawe wamesikia au kujua hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na uteuzi wa Imam (yaani Ali) kama mrithi wake na bado hawakumchagua kama Khalifa wa kwanza, wa pili au hata wa tatu. Na vipi masahaba hao wachukuliwe kuwa huru na makosa, yaani hawakosei, licha ya kukiuka kwao kwa makusudi amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Je unaweza kuzioanisha kauli hizi mbili?

i. Masahaba walizijua hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) za kumteua Ali (a.s.) kama Khalifa wake lakini hawakuzitekeleza; na

ii. Masahaba hawakuwa na hatia ya upotofu wa aina yoyote ile.

Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 84

## RABI'UL AWWAL 5, 1330 A.H.

**Uoanishaji wa Kauli hizi Mbili, Sababu za Imamu Kukataa Kudai Haki Yake.**

Uchunguzi juu ya wengi wa masahaba unatuelekeza kufikia uamuzi wa kwamba wao [masahaba] walikuwa wakitekeleza hadithi kama hizo za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kutii amri zake zile ambazo hususan zilishughulika na imani na kwa mujibu wa hizo, zilikuwa na faida tu kwenye maisha ya Akhera, kwa mfano hadithi ya wazi au amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kizazi chake kwamba wajibu wa kufunga [saumu] ni wakati wa mwezi wa Ramadhani badala ya mwezi mwingine wowote, kuelekea tu *qibla* wakati wa kuswali na si kwingineko ilikuwa ni suala la lazima, au idadi ya swala za wajibu wakati wa mchana na usiku, au idadi ya rakaa katika kila swala, halikadhalika na jinsi ya kuziswali, au kuhusu kuizunguka Nyumba *Ka'ba* (*tawaf* ) mara saba. Walikuwa wakifuata na kutii hadithi na amri nyingine kama hizo ambazo walifikiri kwamba zina manufaa tu katika maisha yajayo [Akhera].

Ama hawakuona kama ni jambo la muhimu kufuata na kutii hadithi na amri zake ambazo hushughulika na masuala ya kisiasa kama vile uteuzi wa magavana na maafisa wengineo, kuunda kanuni na taratibu kwa ajili ya serikali, taarifa na mapitio ya mambo ya utawala, kuandaa na kutuma majeshi kwenye vita. Hawakutaka kutegemea moja kwa moja katika kufuata ushauri wake katika mambo yote. Walitaka wawe huru na kupata uwanja wa kufuata maoni yao na kutumia busara na akili zao. Kama wakiona kumkhalifu kutawainua au kunufaisha utawala wao, humpinga. Wanaweza hata kuitafsiri ridhaa ya Mtume kwa kufanya hivyo. Walikuwa na wasiwasi kwamba Waarabu hawatakubali utawala wa Ali wala kufuata hadithi na amri za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika suala la Ukhalifa wa Ali, kwa sababu yeye Ali aliwauwa katika njia ya Mwenyezi Mungu (Jihad) idadi kubwa ya wahenga wao makafiri na kwa upanga wake kumwaga damu yao huku akiliwezesha neno la Allah kusimama imara. Alifichua, kuzuia na kuvunjilia mbali mipango miovu ya makafiri ya kutaka kubomoa imani ya kweli, mpaka dini ya Allah ikayashinda matatizo yote licha ya vurugu zote za makafiri. Hivyo, Waarabu wasingemtii Ali (a.s.) kwa hiyari isipokuwa kwa kutumia nguvu, na wasingezitii hadithi na amri dhahiri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu yeye isipokuwa kutumia mabavu katika kufanya hivyo. Walikuwa wamedhamiria kulipiza kisasi kwa kila damu iliyomwagika wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w.w.), kwa mujibu wa mila na desturi zao za kulipiza kisasi, kwani baada ya Mtukufu Mtume hakukuwa na yeyote anayestahiki kulipizwa kisasi cha damu hizo katika ukoo wa Mtume isipokuwa yeye Ali, hiyo ni kwakuwa kisasi kilikuwa kinalipizwa kwa ndugu wa karibu zaidi au yeyote yule ambaye alikuwa ndiye maarufu zaidi katika familia ya muuaji. Walijua kwamba yeye Ali alikuwa ndiye mbora miongoni mwa ukoo wa Hashim, baada ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), kwa hiyo walitaka walipe kisasi cha damu yote iliyomwagika juu ya Ali ambaye bila shaka yoyote au ubishani alikuwa ndiye bora baada ya Mtume. Kwa sababu hii, Waarabu walingojea fursa ya mapinduzi ipatikane na walileta mabadiliko katika mazingira. Walikuwa na chuki kubwa mno vifuani mwao dhidi yake na kizazi chake, na walisababisha hasara kubwa isiyo na ukomo ya uhai na mali juu yao, hatimaye kile kilichotokea kilienea katika angahewa lote na kubadili rangi ya ardhi na mbingu yote. Kila mtu anajua kilichotokea ni nini.

Kuna sababu nyingine: Waraabu hususan Makuraishi kwa ujumla walikuwa na dhamira ya madhara juu ya Ali (a.s.) ambaye angeweza kuwakanyaga kanyaga maadui wa Allah na angeweza kutoa adhabu

chungu kwa wale ambao wanachupa mipaka ya amri za Allah au kukiuka chochote kile alichoharamisha au watakaonajisi sehemu takatifu yoyote ya Mwenyezi Mungu. Waarabu waliogopa kuwa kama Ali angechaguliwa kushika Ukhalifa au kuwa mtawala angehakikisha utekelezwaji mkali wa matakwa yote ya dini na uzuiaji kamilifu wa machukizo na maovu yake. Walihofia pia uadilifu wake katika kushughulika na raia wote na angewatendea wote kwa usawa katika mambo yote. Hakuna mtu ambaye angetegemea kutendewa upendeleo wowote ama huruma maalum. Wenye uwezo na hadhi walikuwa kwake ni wanyonge hadi achukue haki ya Umma au ya watu binafsi kutoka kwao, na wanyonge na wenye kuonewa walikuwa wenye nguvu na kuheshimika madhali madai na haki zao hazijalipwa kwao. Hivyo, vipi Waarabu watajisalimisha kwa hiyari kwa mtu kama huyo:

وَمِمَّنْ حَوْلَكُم مِّنَ الْأَعْرَابِ مُنَافِقُونَ ۖ وَمِنْ أَهْلِ الْمَدِينَةِ ۖ مَرَدُوا عَلَى النِّفَاقِ لَا تَعْلَمُهُمْ ۖ نَحْنُ نَعْلَمُهُمْ ۚ

**"Na miongoni mwa mabedui walio pambizoni mwenu wamo wanafiki na katika wenyeji wa Madina wako waliobobea katika unafiki. Huwajui, Sisi tunawajua….." (9:101).**

Na miongoni mwao wako pia wale ambao kwa nje ni Waislam lakini kwa ndani ni wanafiki hawasiti kufanya chochote katika kuuangamiza Uislam na Waislam.

Bado kuna sababu nyingine. Makuraishi na Waarabu kwa ujumla walizoea kumhusudu kwa sababu Mwenyezi Mungu amekuwa mkarimu hasa katika kumjaalia Ali neema Zake bora kwa wingi. Alikuwa na cheo cha hali ya juu katika elimu na matendo mbele ya Allah, Mjumbe Wake na wenye busara, ambacho washiriki wake na maadui zake hawakuweza kufikia, na kupitia huduma zake za namna yake za awali na sifa zake zisizo na mfano, amepata kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hadhi ambayo kupatikana kwake kulikuwa kukitamaniwa kwa shauku kubwa na nyoyo zote. Matokeo yake nge wa husuda dhidi yake walianza kunyemelea nyoyo za wanafiki na mafasiki, Nakithiina (walipigana naye vita vya Jamal), Qasitiina (waliungana na Mu'awiya huko Sifiin) na Mariqiina (walipigana naye huko Nahrawan), wote walijizatiti katika kutengua ile ahadi iliyotolewa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ya kumtii Ali na waliacha nyuma ya migongo yao zile Hadith zote za dhahiri kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kuhusu hili, na kuzifanya zisahaulike kana kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuzitamka kamwe hadithi na amri hizo.

**Yametokea yaliyotokea, kamwe mitazamo sitajadili; Fikra nzuri shughulikia, usiulizie kuhusu habari.**

Vilevile, Makuraishi na Waarabu wengine wote wakati huo walitamani utawala wa kisiasa upatikane kwa ajili ya makabila yao mbalimbali, na kila mojawapo likawa na ulafi mkubwa juu ya hilo. Kwa hiyo, waliamua kutupilia mbali ahadi waliyoitoa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na utii kwa Ali kama khalifa wake na wakaamua kukiuka viapo vyao. Wote kwa pamoja wakaamua kupuuza hadithi na amri za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu suala hili na wakaahidi kutozikumbuka kabisa kamwe. Wote walikubaliana kutouruhusu ukhalifa kufika mikononi mwa yule Khalifa na kiongozi aliyeteuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wakaufanya wa kiuchanguzi na uteuzi, ili kwamba kila moja kati ya makabila yao liweze kuwa angalau na matumaini ya kushika ukhalifa kupitia mmoja wa ndugu yao, hata ingawa

ni baada ya muda. Lau wangetii hadithi na amri za wazi juu ya suala hili na wakampendelea Ali kuliko wengine kama Imam na Khalifa wao akimrithi Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), basi ukhalifa huo ungebakia daima kwenye kizazi chake, Ahlul-Bayt (a.s.), kwani katika Siku ile ya Ghadir na katika sehemu nyingine Mtume (s.a.w.w.) alilinganisha Ahlul-Bayt na Kitabu cha Allah, na pia akatangaza kwamba viwili hivyo havitenganishiki na akivielezea kama ni vigezo kwa ajili ya wenye akili na hekima mpaka Siku ya Hukumu. Lakini ilikuwa ni vigumu sana kwa Waarabu kuweza kuvumilia ukhalifa kuwekwa kwenye ukoo mmoja, hususan kwa vile makabila yote yalikuwa yakiukodolea macho na nafsi zote hai zikiutamani.

"Kwa hakika amedhoofika mpaka kwa udhaifu huo kila kitu kimeonekana,

na mpaka kila muflisi kamtamani,

Mifupa mitupu isiohitajika, hata na ambaye hazinaye yakaushwa."

Vilevile, kwa yeyote anayejua historia ya Kureishi na Waarabu wakati wa mwanzo wa Uislamu ataelewa kwamba hawakukubali Utume wa Bani Hashim isipokuwa baada ya kuangamizwa, wakiwa nguvu zimewaishia kuweza kuleta upinzani. Hivyo basi, vipi wangekubali kwamba kizazi cha Hashim wahodhi Utume pamoja na Ukhalifa vilevile? Umar bin Khattab wakati fulani wa mazungumzo kati yake na Ibn Abbas alimuambia: "Makureishi walichukia kuona kwamba Utume na Ukhalifa vyote viwe vimewekwa kwenye familia yenu (Bani Hashim) kwa hofu kwamba mngeweza kudhuru maslahi ya watu wengine."[380]

Hivyo wahenga wazuri wasingeweza kuwalazimisha watu wale kuzitii na kuzifuata hadith na amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa hofu kwamba kuwalazimisha huenda kukasababisha warejee kwenye hali ya ukafiri wa awali. Vilevile walihofia kwamba kama tofauti au mgawanyiko katika mazingira yale ungeruhusiwa kuendelea matokeo yake yatakuwa ya kutisha na kujutia sana. Unafiki ulijitokeza dhahiri mara tu baada ya kufariki kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), na nguvu ya wanafiki iliongezeka kwa haraka sana. Makafiri walicharuka kwa uadui, misingi ya imani ikadhoofika, na mioyo ya Waisilamu ikashitushwa, kwani kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kiliwashusha mpaka kwenye hali ya kuwa kama kondoo anayezurura katika usiku wa baridi na giza katikati ya mbwa mwitu na wanyama wakali wengine bila ya mchunga. Makundi kadhaa miongoni mwa Waarabu yaliritadi na mengine yakitaraji kufanya hivyo, kama tulivyoeleza kwa kirefu katika Barua yetu ya 82 hapo juu. Chini ya mazingira hayo Ali (as) alihofia matokeo ya hali kuwa mbaya zaidi na kuangamia kwa hivi punde tu kwa Uislam endapo kama angeamua kuchukua hatamu za utawala, huku akijua jinsi ilivyovunjika mioyo ya Waislam. Wanafiki walikuwa wanazidi kupata nguvu siku baada ya siku, wakiuma midomo na vidole vyao kwa hasira, na uasi kwenye dini ukiendelea, na ukafiri ukiwa unainukia kuja juu zaidi. Answar wametofautiana na kuwageuka Muhajirun, wamejiweka mbali nao wakisema: "Kiongozi mmoja atoke kwetu na mmoja kutoka miongoni mwenu, n.k." Kwa maslahi ya Imani ya dini, Ali alijizuia kuutwaa ukhalifa kwa nguvu kwani alijua kwamba kutahatarisha kuugawa Umma na kupuuzia mambo yao, hatari kwa Umma na kuharibika kwa usalama wa imani. Kwa hiyo aliamua kutoa muhanga maslahi yake mwenyewe binafsi kwa kuweka mbele masilahi na usalama wa Uislamu, na ustawi wa taifa, na usalama na utulivu wa watu, na akapendelea ya baadae kuliko ya wakati wa karibu. Hakuna mtu mwingine aliyeonyesha roho nzuri mno na moyo wa muhanga wa nafsi kama huo kuliko yeye.

Kwa hiyo, alibakia nyumbani, huku akikataa kutoa kiapo chake cha utii kwa Khalifa aliyechaguliwa huko Saqifah mpaka alipotolewa kwa mabavu. Hii ilikuwa ni kuhifadhi haki yake ya urithi na kutoa upinzani wa kimya kimya dhidi ya wale waliogeuka wasaliti kwake. Lau angekimbilia kutoa kiapo chake

[380] Hii imenukuliwa na Ibn Abul-Hadid katika ukurasa wa 107, Jz. 3, ya kitabu chake cha *Sharh Nahjul Balaghah*, kuhusiana na suala moja lenye kuhitaji utafiti na tafakari ambalo vilevile linajadiliwa na Ibn al-Athir karibu na mwisho wa wasifu wa Umar ukurasa 24, Jz. 3, ya kitabu chake *Tarikh Al-Kamil* katika maelezo juu ya Umar kabla ya kujadili kisa cha 'ushauriano' (*shu'ra*).

cha utii, asingekuwa na hoja nzito na yenye kukubalika katika kuunga mkono haki yake ya Ukhalifa na uthibitisho wa malalamiko yake. Bali yeye kwa kufanya hivyo, alilinda kwa usalama yote mawili; aliiokoa dini kutokana na kuangamia, na pia haki yake mwenyewe ya kuwa Imam na kiongozi wa waumini. Hii inatupatia uthibitisho wa uasili wa hali ya maamuzi yake mazuri, wingi wa subira yake, ukarimu wa nafsi na moyo wa muhanga binafsi katika kuweka mbele masilahi ya Umma. Ukarimu wa dhati na kweli katika balaa kubwa kubwa na katika jambo muhimu kama hilo huwa unashuka kutoka kwa Allah kwa yule ambaye yuko katika daraja la juu kabisa la uchamungu na utii kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hakika kile alichokifanya kilikuwa ni chenye manufaa sana katika mazingira yaliyopo na kwa ajili ya kurudisha hali ya kawaida. Hekima yake ya kipimo kikubwa kama hicho ilikuwa ni kutokana na ukaribu wake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ama kuhusu wale makhalifa watatu na wafuasi wao, hawa pia walianza kutoa tafsir potofu za hadithi na amri za dhahiri kuhusiana na Ukhalifa wa Ali kwa sababu ambazo tayari tumezionesha hapo juu. Hili halikuwa ni jambo la kushangaza kabisa kutoka kwao kwani kama ilivyokwisha kutajwa, wao walikuwa na desturi ya kutumia akili zao wenyewe na kutafsiri kwa njia zao wenyewe zile hadithi na amri zote za Mtume (s.a.w.w.), kuhusiana na masuala ya siasa, uteuzi wa magavana na maafisa wa serikali, uundaji wa sheria na kanuni kwa ajili ya serikali, taarifa na mapitio ya uendeshaji wa dola n.k. Pengine hawakuliona suala la Ukhalifa kuwa ni suala la kidini na hiyo ndio maana hawakuweka umuhimu wowote na kuzingatia kwa vitendo zile riwaya zinazohusu Ukhalifa. Hatimaye hali ilipotengamaa na ukawaida kurejea, walijaribu kwa tahadhari sana kupuuza na kusahau riwaya hizo, na kuwafanya watu wengine wapuuze na kusahau hadithi zote hizo na wakaanza kuwaadhibu wale ambao wanaotaja au hata kuzirejea hadithi hizo. Wakati utulivu ulipopatikana, uenezaji wa dini ya Uislamu, upanuaji wa taifa, upatikanaji wa utajiri na nguvu, na kujitenga na machafu, yote hayo yaliwanyanyua na kuwafanya wazikoge nyoyo za watu, kwa kuaminiwa na kupendwa. Watu wakaanza kuvutiwa nao na kuwapenda na pia kufuata mfano wao katika kupuuza na kusahau, na kuwafanya wengine wapuuze na kusahau zile hadithi zote zihusianazo na suala hilo. Hatimaye hatamu za serikali zikaangukia mikononi mwa Bani Umayyah ambao lengo lao kubwa lilikuwa ni kuwaangamiza Ahlul-Bayt wa Mtume na kuing'oa hadhi yao. Walifanya kila waliloweza kwenye mamlaka yao kufuta kutoka kwenye akili za watu, sio hadithi zinazohusu Ukhalifa wa Ali tu, bali pia zile zinazozungumzia sifa na ubora wa Ahlul-Bayt. Licha ya yote haya, hadithi sahihi na amri za wazi zimetufukia na kuhifadhiwa katika vitabu sahihi vya hadthi; na hizi zinatutosha kutuelekeza kwenye haki na kweli. Shukurani zote ni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu! Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 85

## RABI'UL AWWAL 7, 1330 A.H.

**Maombi ya Mifano ya Maeneo Ambayo Masahaba Hawakutii Amri na Hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).**

Nimepokea barua yako na kuiona ya kimuujiza katika kuthibitisha uwezekano wa kile tulichodhania kuwa hakiwezekani. Umewasilisha picha ya kushangaza kwa wazi katika uelezeaji wake wa kitamathali katika ufafanuzi zaidi. Shukurani ziende kwa Yule ambaye amejaalia juu yako uwezo wa kuleta hoja laini kabisa lakini zenye kukinahisha na akakupa uwezo wa kuelezea na kufafanua mambo kwa ufanisi. Umenifikishia taarifa ambazo kwangu zilikuwa hazipatikaniki na umefanikiwa kunipatia hoja ambazo nilikuwa nikizihitaji sana lakini nikahisi kwamba zinakosekana, hazipo. Nilidhani kwamba ilikuwa ni vigumu kiasi kwamba isingewezekana kwa wewe kuzioanisha kauli mbili hizo (zilizomo kwenye barua ya 83) na kuthibitisha kwamba masahaba walikuwa hawana hatia ya upotofu licha ya kupuuza kwa kujua kabisa zile amri na hadithi za wazi kuhusu Ukhalifa wa Ali na kwamba ilikuwa haiwezekani kwa wewe kudharau kile ambacho kilikuwa dhahiri na kukabiliana na changamoto niliyokutupia. Hata hivyo, bado natamani ungeelezea matukio ambayo kwayo masahaba hawakutii amri dhahiri na hadithi za wazi za Mtume (s.a.w.w.), ili kwamba sababu za kutokutii ziweze kuyakinishwa na njia ya mwongozo mzuri idhihirike wazi. Kwa hiyo, nakuomba ufafanue kwa kina juu ya matukio hayo ili niweze kuyachunguza kwa mwanga wa maelezo yaliyosimuliwa kihadithi juu ya maisha na tabia zao, na nichunguze muonekano na mielekeo yao kwa kuangalia kilichoandikwa katika vitabu vya historia. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 86

## RABI'UL AWWAL 8, 1330 A.H.

**Msiba Mkubwa wa Alhamisi, Sababu Iliyomfanya Mtume (s.a.w.w.) Asiandike wosia.**

Matukio ambayo kwayo amri na hadithi za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilipuuzwa na kutotiiwa ni mengi. Miongoni mwao, chukua kwa mfano lile la "Msiba wa Alhamisi," ambalo ni moja kati ya matukio mashuhuri zaidi na ambalo ni janga kubwa mno lililoushukia Uislam. Linasimuliwa na waandishi wote wa *Sahih* na *Sunan*, na wasimuliaji wengine wa hadithi na kunakiliwa na takriban wanahistoria na waandishi wote wa wasifu. Hadithi iliyosimuliwa na Bukhari[381] kutoka kwa Ubaydullah bin Utbah bin Mas'ud akinukuu vyanzo kadhaa hadi kwake inatutosha sisi. Kwa mujibu wa Abdullah bin Abbas anasema: Wakati wa kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): ulipokaribia kulikuwa na watu wengi ndani ya nyumba. Miongoni mwao alikuwepo Umar bin Khattab. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Nileteeni kalamu na karatasi ili niweze kuwaandikia wosia ambao hamtapotea kamwe baada yangu." Hapo Umar akasema: "Kwa hakika Mtume ana maradhi makali juu yake, mnacho Kitabu cha Mwenyezi Mungu miongoni mwenu na Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinatutosha." Baadhi ya wale waliokuwemo ndani mle walitofautiana na Umar na zogo likazuka hapo. Kuna waliosema 'mleteeni Mtume vifaa vya kuandikia ili awaandikie huo waraka ambao utawakinga kutokana na kupotoka baada yake.' Wengine ambao walikuwa ndio wengi wakamuunga mkono Umar. Walipoanza kutupiana maneno makali na ugomvi ukaendelea mbele ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), yeye akawaambia: "Ondokeni mbele yangu hapa mniache peke yangu." Ibn Abbas alikuwa amezoea kusema: "Msiba mkubwa kushinda misiba yote, ni ule uliomzuia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kuandika wosia aliotaka kuwaandikia, kutokana na kuzozana kwao na kelele zao."

Hakuna ubishani kuhusiana na usahihi wa hadithi hii na uaminifu wa wapokezi wake. Al-Bukhari amelisimulia tukio hili sehemu mbali mbali katika tasnifu yake "*Kitabul-ilmu,*" katika Jz. 1, uk. 22, ya *Sahih* yake. Muslim vilevile, analinukuu tukio hili mwishoni mwa Mlango wa "Wosia wa Mtume" katika *Sahih* yake Jz. 2, uk. 14, Ahmad anasimulia hadithi ya Ibn Abbas katika *Musnad* yake, uk. 325 wa Juzuu ya kwanza. Tukio hili limesimuliwa na takriban waandishi wote wa hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini wote wameihariri bali bado maana yake inabakia ileile. Maneno ya asili yaliyotamkwa na Umar yalikuwa ni "*Yahjur*" yakiwa na maana kwamba: "Kwa hakika Mtume anaweweseka" au "ana mawenge." Lakini muhadithina hao wanasema kwamba Umar alisema: "Mtume (s.a.w.w.) amezidiwa na maradhi." Walisema hivyo ili tu kuisafisha kauli hiyo na kuifanya ionekane ya kiungwana na yenye adabu ili kupunguza bezo na dharau inayomaanishwa na neno "weweseka." Kauli yangu hii inaungwa mkono na kile ambacho Abu Bakr Ahmad ibn Abdul-Aziz al-Jawhari amekinakili katika kitabu chake kiitwacho *Al-Saqifah,* akinukuu riwaya ya Ibn Abbas kutoka vyanzo vyote sahihi akisema: "Wakati wa kifo cha Mjumbe wa Allah ulipokaribia, walikuwepo watu katika nyumba yake, miongoni mwao akiwemo Umar bin Khattab. Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akasema: "Nileteeni wino na kibao cha kuandikia ili niwaandikie kitu ambacho kitawalinda salama dhidi ya kupotea baada yangu." Hapo Umar alizungumza maneno ambayo yana maana: 'Hakika Mtume ana hali ngumu ya maradhi juu yake.' Kisha akaongeza kusema: 'Tunayo Qur'ani pamoja nasi. Kinatutosha sisi Kitabu cha Mwenyezi Mungu.' Hii

[381] Tafadhali rejea mlango wa "Maneno ya Mgonjwa:" "Nyanyukeni na mniondokee hapa" katika Kitabu juu ya Mgonjwa katika uk. 5, Jz. 4, ya *Sahih Bukhari.*

ilisababisha kutofautiana miongoni mwa wale waliokuwepo nyumbani kwake na wakazozana wenyewe kwa wenyewe, baadhi yao wakisema 'Mleteeni Mtukufu Mtume vifaa vya kuandikia ili awaandikie huo wosia,'ambapo wengine walirudia kile alichosema Umar. Wakati ubishani na mzozo ulipozidi, Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alikasirika na akasema: "Ondokeni mbele yangu."

Simulizi hii inaonyesha wazi kwamba wasimuliaji hawakuleta tena yale maneno yaliyosemwa hasa na Umar katika kujibu maombi ya Mtume ya kutaka vifaa vya kuandikia, wamenukuu ile maana yake tu. Hii inathibitishwa zaidi pia na ule ukweli kwamba pale ambapo wasimuliaji wa hadithi hawakutaja jina la mtu ambaye alipinga maombi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wamenukuu ile kauli ya upingaji kwa maneno yenyewe hasa. Katika mlango wa 'Ruhusa ya Kuteua Naibu,' katika '*Kitab Al-Jihad wal Siyar*, uk. 118, Jz. 2, al-Bukhari anasema:[382]

"Qubaysah alitusimulia hadithi kutoka kwa Ibn Ayinah, Salman al-Ahwal, na Sa'id ibn Jubayr, wote kwa mfululizo wanamnukuu Ibn Abbas akisema: 'Siku ya Alhamisi, ilikuwa siku ya msiba ulioje hiyo ya Alhamisi…;' na aliangua kilio mpaka machozi yake yakalowesha ardhi, kisha aliendelea kusema: "Siku ya Alhamisi maradhi ya Mjumbe wa Allah yalizidi; hivyo, alituamrisha 'Nileteeni vitu vya kuandikia ili niwaandikie waraka ambao kwa huo mtakingwa dhidi ya upotofu baada yangu', lakini watu wakazozana, wakijua kwamba wasingepaswa kuleta mzozano mbele ya Mtume na wakasema: 'Mjumbe wa Allah anaweweseka.' Yeye Mtume (s.a.w.w.) akasema: 'Ondokeni mbele yangu, kwani hali ya maradhi niliyonayo ni bora zaidi kuliko ile mnayotaka kuniingiza.' Na alishauri katika wosia wake kabla ya kufariki kwake mambo matatu; kuwaondoa wanafiki nje ya bara Arabu, kuendelea kutuma manaibu kwenye nchi za nje kama vile yeye (s.a.w.w.) alivyokuwa akiwatuma,….. na nimesahau lile la tatu."[383]

Hadithi hiyo hiyo imesimuliwa pia na Muslim mwishoni mwa sura inayoshughulika na wosia katika *sahih* yake, na Imam Ahmad miongoni mwa hadithi za Ibn Abbas katika *Musnad* yake Jz. 1, uk. 222, na wasimuliaji wengine wote wa hadithi pia. Katika sura juu ya wosia, katika *Sahih* yake, Muslim anamnukuu Ibn Abbas katika njia nyingine pia kama ilivyosimuliwa na Sa'id ibn Jubayr ambaye kwa mujibu wake yeye, Ibn Abbas amesema: "Alhamisi ile, Oh! Ilikuwa ni Alhamisi ya balaa ilioje siku ile." Na macho yake yalijaa machozi na yakatiririka mpaka yakaonekana kama uzi wa lulu, kisha akaendelea kusema: "Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alisema: 'Nileteeni ubao wa kuandikia na kidau cha wino,' au kibao na kidau cha wino, 'ili niwaandikie waraka ambao kwamba baada yake kamwe hamtapotea;' lakini wakasema: 'Mjumbe wa Allah anaweweseka.'"[384]

Mtu yeyote aliyechunguza mazingira ya tukio hili la msiba mkubwa katika vitabu sita vya *Sahih* anajua kwamba mtu wa kwanza kusema kwamba 'Mjumbe wa Allah anaweweseka' si mwingine bali ni Umar bin Khattab. Maneno yake yalikaririwa na baadhi ya waliokuwepo pale kwenye kivuli cha maoni yake. Katika hadithi ya kwanza umesikia Ibn Abbas akisema:[385] "Wale waliokuwepo nyumbani kwake walitofautiana miongoni mwao wenyewe na wakazozona, baadhi yao wakisema: 'Mpeni Mtume vifaa vya kuandikia ili aweze kuwaandikieni waraka ambao kwamba baada ya huo hamtapotea kamwe.' Wengine walirudia kile alichosema Umar, yaani, "Mjumbe wa Allah anaweweseka." Katika hadithi nyingine iliyosimuliwa na Tabraniy, katika kitabu chake *Awsat*,[386] Umar mwenyewe ananukuliwa akisema:

[382] Kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 20, Jz. 2, ya *Sharh Nahajul Balaghah* ya Allamah Mutazili [Ibn Abu Hadid].

[383] La tatu si lingine bali ni lile suala ambalo Mtume (saw) alitaka kuandika ili kuwalinda dhidi ya upotofu, lakini hali ya kisiasa ya wakati huo ikawalazimisha wapokezi na wasimuliaji wa hadithi kujifanya wasahaulifu kuhusu hili, kama ilivyoelezwa na Mufti wa ki-Hanafi wa Syria, Haji Dawud al-Dadah.

[384] Hadithi hii inanukuliwa kwa maneno yake yenyewe na Ahmad ibn Hanbal katika ukurasa 355, Jz. 1, ya *Musnad* yake, kama nyongeza ya (vitabu) vingine vingi vya kutegemewa vya waandishi wa hadithi.

[385] Hiki ndicho ambacho al-Bukhuri amenukuu kutoka kwa Ubaydullah ibn Abdullah ibn Mas'ud kutoka kwa Ibn Abbas na vilevile imenukuliwa na Muslim na wengine.

[386] Tafadhali rejea katika ukurasa wa 138, Jz. 3, ya *Kanz al-Ummal*.

"Wakati Mtume alipokuwa anaumwa, alisema: 'Nileteeni karatasi na kidau cha wino ili nikuandikieni kitu ambacho baada yake kamwe hamtapotea.' Hapo, wanawake waliokuwa nyuma ya pazia wakasema: 'Je, hamkusikia anavyosema Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)?' Mimi nikasema: 'Ninyi ni kama wanawake wa wakati wa Yusuf; wakati Mjumbe wa Allah anapoumwa mnaminya machozi kutoka kwenye macho yenu, na wakati akiwa mzima, mnampanda shingoni!' Vilevile aliendelea kusema: "Kisha Mjumbe wa Allah akasema: 'Msitoe shutuma dhidi ya wanawake hao, kwani wao ni bora kuliko ninyi.'"

Unaweza kuona kwamba katika tukio hili masahaba hawakutii mwongozo amri ya wazi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lau wangemtii, wangejiokoa wenyewe dhidi ya upotofu daima. Laiti wangeishia tu kwenye kutokukubaliana na amri yake na sio kumjibu kwa kusema: "Kitabu cha Allah kinatutosha," kana kwamba yeye alikuwa hajui usahihi wa nafasi na umuhimu wa Kitabu cha Allah, au wao walikuwa na ujuzi zaidi kuliko yeye kuhusu sifa za msingi na faida za Kitabu hicho. Laiti wangetosheka na kauli hii ya dharau na kutomsababishia mfadhaiko zaidi kwa kauli ya ukorofi: "Mjumbe wa Allah anaweweseka." Walitumia maneno haya yenye maudhi makali wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa katika hali ya kufariki. Walitumia maneno haya ya kusikitisha wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa anawatoka daima! Hawakuitii amri ya Mtume kwa sababu ya kisingizio chao cha kutosheka kwao na Kitabu cha Allah, kama vile hawajasoma aya ya onyo la milele:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا ۚ

**"Anachokupeni Mtume, kichukueni, na chochote anachokukatazeni jiepusheni nacho, (Qur'ani, 59:7)."**

Maneno yao kwamba "Mjumbe wa Allah anaweweseka," yanaonyesha kwamba hawajasikia:

a) maneno haya ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ مُطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ
وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُونٍ

"**Kwa hakika hiyo bila shaka ni kauli ya mjumbe mtukufu, mwenye nguvu, mwenye cheo mbele ya Mwenye Arshi, Mwenye kutiiwa, tena muaminifu. Na Mwenzenu si mwendawazimu. (Qur'ani, 81:19-22)."**

b) kauli yake Aza wa Jallah:

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ ۚ قَلِيلًا مَا تُؤْمِنُونَ وَلَا بِقَوْلِ
كَاهِنٍ ۚ قَلِيلًا مَا تَذَكَّرُونَ

**"Kwa hakika ni kauli ya mjumbe mwenye heshima, wala si kauli ya mshairi. Ni machache mnayoyaamini. Wala si kauli ya kuhani. Ni machache mnayoyakumbuka, (Qur'ani, 69:40-43)."**

Na c) kauli Yake Allah Aza wa Jallah:

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ
عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ

"**Mwenzenu hakupotea, wala hakukosea, wala hatamki kwa matamanio, hayakuwa haya ila ni wahyi uliotolewa, amemfundisha Mwenye nguvu sana." (Qur'ani, 53:2-5).**

Kuna aya nyingi nyingine za Qur'ani ambazo zinaonyesha wazi kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amehifadhiwa na kuwa huru kutokana na aina zote za maongezi ya upuuzi. Kusema kweli hata hivyo, ni kwamba masahaba walijua kwa hakika kwamba, kwa kudai vifaa vya kuandikia, yeye Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alitaka kuimarisha ahadi ya ukhalifa, na kuthibitisha tangazo lake alilolitoa kwenye matukio mbalimbali kuhusu urithi wa Ali na baada yake wa Maimamu kutoka miongoni mwa kizazi chake kitoharifu; na kwa hivyo, walisimama kama kikwazo kumzuia kufanya hivyo (yaani kuandika wosia), kama alivyokiri mwenyewe Khalifa wa pili katika moja ya mazungumzo yake na Ibn Abbas…! Ipo katika msitari wa 27, ukurasa wa 114, Jz. 3, ya *Sharh Nahjul Balaghah* ya Ibn Abul Hadid.

Kama utaifikiria kwa makini kauli yake, (s.a.w.w.), "Nileteeni vifaa vya kuandikia ili nikuandikieni kitu ambacho kwacho kamwe hamtapotea baada yangu." Na kauli yake katika hadithi ya Vizito Viwili: "Nakuachieni pamoja nanyi vile ambavyo, alimradi mnashikana navyo, kamwe havitawafanya mpotee; Kitabu cha Allah na kizazi changu, Ahlul Bayti wangu," utakuja kuelewa kwamba madhumuni yake katika hadithi hizi mbili zote ni moja, na kwamba yeye (s.a.w.w.) wakati akiwa kwenye kitanda anachougulia, awaandikie na kuweka kumbukumbu maelezo ya wajibu alioweka juu yao kupitia hadithi ya Vizito Viwili *[al-Thaqalain]*.

Sababu ambayo ilimfanya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) asiandike waraka huo (licha ya upinzani wa Umar na wafuasi wake) ilikuwa kwamba kauli yao ya upinzani mkali na dharau (Mtume anaweweseka) ilimsababishia maumivu makali ya akili ambayo yalimfanya akalazimika kuyatelekeza mawazo yake ya kuandika wosia huo. Kwani baada ya kauli hiyo ya kifidhuli kutoka kwa wengi wa masahaba kulikuwa na matumaini madogo sana ya waraka huo uliopendekezwa kutokuwa na maana yoyote. Kwa upande mwingine, kulikuwa na kila uwezekano kwamba waraka huo ungeishia katika kuzua utengano, mizozo na upotovu baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwani wale watu waliopitisha kauli ya kifidhuli wakati alipoomba vifaa vya kuandikia wangeropoka maneno kuhusu waraka huo: 'Mtume (s.a.w.w.) hapa ameandika upuuzi' (Mungu atuepushe mbali na kufuru kama hii). Wengine wangewapinga hawa na mgogoro ungekuwa mkubwa zaidi kama walivyofanya hata mbele yake mwenyewe, na wakati akiwa bado anayaona mambo, kiasi kwamba hakuweza kuwaambia neno zaidi ya kuwaambia waondoke mbele yake, kama ulivyosoma hapo juu. Lau angesisitiza katika kuuandika (wosia huo), wangekuwa wakaidi zaidi katika kuuita upuuzi na wafuasi wao wangekwenda mbali zaidi kuthibitisha madai yao kwamba maandishi hayo yalikuwa ni upuuzu mtupu. Mwenyezi Mungu atuhifadhi. Kwa ukaidi wangejaza vitabu vyao na tuhuma kama hizo, na kufanya uandikwe kwenye vitabu vya historia pia upingaji wao wa wosia huo ambapo matokeo yake ni kwamba hakuna ambaye angeweza kuunukuu wosia huo kama rejea.

Kwa sababu hizi, kwa busara zake nzuri aliamua kuachana na wazo la kuandika wosia huo kwa kuhofia wale wanaopinga matakwa yake, na wafuasi wao kwamba wanaweza kufungua mlango wa kukanusha wosia huo na kuleta kashfa kuhusu Utume wenyewe. Tunaomba hifadhi kwa Allah na kutegemea malipo kutoka Kwake. Yeye (s.a.w.w.), alikuwa na hakika kwamba Ali (a.s.) na wafuasi wake watafuata yale yaliyomo kwenye waraka huo uliopendekezwa, yaani kutii amri yake na kushikamana na Ahlul-Bayt wake (a.s.) na Kitabu cha Mwenyezi Mungu, iwe ameyaandika au la, wakati ambapo wengine kwa hali yoyote hawatatii au kuheshimu amri hiyo hata kama itaandikwa. Kwa hiyo, busara katika mazingira haya ililazimisha aachane na wazo la kuandika wosia huo, kwa sababu sio tu kwamba hautakuwa na athari kabisa baada ya upinzani wenye dharau bali pia utasababisha kuwaelekeza wakataaji na wafuasi wao kwenye upotofu na ukosa imani kama ilivyokwisha kuelezwa tayari. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 87

## RABI'UL AWWAL 9, 1330

**Udhuru Katika Tukio la Msiba Mkubwa, Na Mjadala Muhimu juu ya Udhuru huo.**

Wakati yeye (s.a.w.w.) alipowaamrisha wamletee karatasi na kidau cha wino, huenda hakukusudia mahususi kuandika chochote, alikusudia tu kujaribu uaminifu na utii wao. Kwa hiyo, Allah alimuongoza al-Faruq, miongoni mwa masahaba wote waliokuwemo ndani ya nyumba hiyo, na aliweza kuelewa lengo lililokuwa nyuma ya ombi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kwa hiyo aliwakataza kumpatia vifaa hivyo vya kuandikia nao wakatii kukatazwa huko. Kwa hiyo ukatazaji wa Umar unapaswa uchukuliwe kuwa ni upendeleo na moja ya fadhila maalum alizojaaliwa na Mola Wake Mtukufu. Haya ndio majibu ya baadhi ya wanachuoni mashuhuri. Lakini kwa haki haswa, majibu haya hayaendani na kauli yake Mtume (s.a.w.w.): "…kamwe hamtapotea baada yake," ambayo ni majibu mengine tu ya amri yake na ina maana "Kama mkiniletea kidau na kipande cha karatasi na nikawaandikieni waraka (wosia), hamtapotea kamwe baada ya hapo." Kwa kuzingatia uhakikisho huu ni wazi kwamba sio sahihi kusema kwamba lengo la kutaka vifaa vya kuandikia lilikuwa ni kuwajaribu tu masahaba zake. Maneno ya Mitume (a.s.) kama kanuni, ni lazima yawe huru kutokana na makosa ya aina yoyote ile, na kwa hakika ilikuwa ni bora kwao kumpatia kidau, kalamu na karatasi kuliko kumkatalia, kama walivyofanya. Zaidi ya hayo, majibu haya ni ya kukataliwa kutokana na mitazamo mingine vilevile, na wangepaswa kutoa visingizio vingine. Ambacho sana sana wangeweza hasa kusema ni kwamba amri yake ya kuletewa vifaa vya kuandikia haikuwa ya wajibu hasa ambayo ingepaswa kutiiwa mara moja, na ambayo haikustahili kujadiliwa au kufanyiwa mabadiliko, na kwamba yeyote atakayeijadili atakuwa na hatia ya utovu wa utii na adabu na ukaidi.

Kwa upande mwingine lilikuwa ni pendekezo ambalo lilikuwa wazi kwa ajili ya ushauriano, kwani masahaba walizoea mara kwa mara kumjadili Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika baadhi ya amri zake, na hususan Umar ambaye alijiamini kwamba ana uwezo zaidi wa kupima kati ya mazuri na mabaya ya pendekezo lolote lile, na kuamua faida na mapungufu ya amri au maelekezo kuliko wengine, na kwamba amejaaliwa msukumo na Allah Aza wa Jallah. Alitaka tu kumpunguzia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) usumbufu mwingine zaidi ambao ungetokana na matokeo ya kuandika waraka aliokusudia licha ya maradhi na machungu anayoyapata, na yeye Umar alifikiria kwamba itakuwa bora wasilete karatasi na kidau cha wino. Pia huenda alihofia kwamba Mtume huenda akaandika amri ambazo wanaweza kuwa hawana uwezo kabisa wa kuzitii au kuzitekeleza, na hivyo kuwafanya wastahili adhabu, kwa sababu chochote atakachoandika kitakuwa ni amri yenye nususi ambayo kwamba haihusiki na kanuni za ijtihad. Au huenda alihofia kwamba wanafiki wangeweza kutia mashaka kuhusu usahihi wa waraka huo kwa ajili ya Mtume kuuandika akiwa katika hali ya maradhi, hivyo kuwa chanzo cha fitina kubwa; kwa hiyo, akasema: "Kitabu cha Allah kinatutosha," kwa mtazamo wa aya ya Mwenye nguvu zote Allah:

مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِن شَيْءٍ

**"Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote (bila kukielezea)." (Qur'ani, 6:38),**

na vilevile pia,

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ

**"Leo nimewakamishia dini yenu kwa ajili yenu** (Qur'ani, 5:3),"

kana kwamba Umar alikuwa na uhakika kwamba Umma hautapotea kwa sababu Allah alikuwa ameukamilisha dini Yake na kukamilisha neema Zake juu yake na kwa hiyo wosia huo ulikuwa hauna lazima.

Hayo ndio majibu yao na unayaona jinsi yasivyokuwa imara. Kusema kwake Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): "…Kamwe hamtapotea….." huonesha nia na mwelekeo bayana kwamba kutaka kwake vifaa vya kuandikia ilikuwa ni amri thabiti, ya maamuzi na ya lazima na haina fursa ya kuchunguzwa, kubadilishwa au ya ushauri. Bila shaka ni wajibu wa lazima kufanya kila juhudi juu ya kukubaliana na kile ambacho kinahakikisha usalama dhidi ya makosa na upotofu. Kuhisi kutofurahi kwake Mtume (s.a.w.w.) katika kutotii amri yake na kuwaambia waondoke mbele yake ni ushahidi na uthibitisho kwamba lengo la amri yake ni kutekelezwa kwake na sio tafakari na ushauriano juu yake.

Wanaweza wakauliza kwamba kama kuandika huko kulikuwa ni wajibu wa lazima kwake ni kwa nini Mtume (s.a.w.w.) hakuandika wosia huo licha ya upinzani wa masahaba, kama vile ambavyo hakuacha kuwasilisha Ujumbe Mtukufu licha ya upinzani mkubwa wa makafiri? Kwa kuyajibu haya, tunasema: 'Kama maneno hayo ni timilifu basi yanatuelekeza kwenye uamuzi kwamba kuandika wosia huo hakukuwa wajibu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini hili bila ya shaka halimaanishi kwamba haikuwa wajibu kwa masahaba kumletea karatasi na kidau cha wino wakati alipowaamrisha kufanya hivyo, hususan kwa vile aliwaeleza wazi kwamba utakuwa ni ulinzi kwa ajili yao dhidi ya upotofu na chanzo cha mwongozo endelevu daima. Nukta muhimu ni kwamba kimsingi wale ambao wanapewa amri ni wajibu wao kutii na kuitekeleza na sio wajibu kwa mtoaji amri, hususan wakati faida itakuwa moja kwa moja kwa yule mwenye kupokea amri. Suala la mjadala kwa hiyo ni iwapo kwamba ilikuwa ni wajibu kwa masahaba kutekeleza uletaji wa vifaa vya kuandikia au hapana na sio kwamba ni iwapo ilikuwa ni wajibu juu yake (s.a.w.w.) kuandika wosia huo.

Hata kama ilikuwa wajibu juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuandika wosia huo, wajibu huo uliondoka, haukumlazimu tena kwa sababu ya ukaidi wao na kauli yao ya kumtweza kwamba 'Mtume anaweweseka.' Kwani kama angeandika waraka huo, pamoja na yote hayo, wangeliishia kwenye mfarakano na kuzusha kashfa na uasi.

Vilevile baadhi ya watu wametoa udhuru na kusema kwamba Umar bin Khattab alishindwa kuelewa jinsi ambavyo wosia huo uliokusudiwa ungeweza kumkinga kila mtu katika Umma huu kutokana na kupotea na kwamba hakuna hata mtu mmoja atakayepotoka baada ya kuandikwa kwa waraka huo uliokusudiwa. Isipokuwa alielewa kutokana na maneno "…kamwe hamtapotea" kwamba Umma wote kwa jumla hautapotea, na kwamba kupotoka na kukengeuka njia iliyonyooka baada ya maandishi hayo, hakutapanuka hadi kuufikia Umma wote kwa jumla. Na tayari yeye (Umar) alikuwa anajua kwamba Umma wote mzima usingeweza kupotoka, hivyo aliona kwamba kuandikwa kwa wosia huo hakukuwa na umuhimu wa lazima. Alifikiria kwamba lengo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) lilikuwa tu ni kuchukua

tahadhari ya ziada kutokana na tabia yake asilia ya wingi wa huruma na upole na kwamba amri yake juu ya vifaa vya kuandikia haikuwa ya kimamlaka na ya wajibu bali ni huru kwa ushauriano na marekebisho. Ilikuwa ni shauku yake ya huruma na upole wa kipekee ambayo ilimfanya aitishe vifaa vya kuandikia kwa ajili ya kuandika wosia wa kutulinda zaidi kutokana na upotovu. Ni hisia na mawazo haya yaliyomfanya Umar kutoa kauli ile na kuzuia utoaji wa vifaa vya kuandikia kwa Mtume (s.a.w.w.).

Hizi ndio nyudhuru mbalimbali ambazo zimetolewa kama sababu ya kauli hiyo ya hamaki na kitendo cha Umar bin Khattab na wafuasi wake. Lakini katika kuangalia kwa makini visingizio vyote hivi vinaonekana vya kimakosa na kutokuwa na maana, kwa sababu maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), "…hamtapotea kamwe" yanaonyesha dhahiri kwamba ile amri yake ilikuwa ni wajibu wa lazima na sio ya hiari au yenye fursa ya mashauriano. Na kukasirika kwake kauli hiyo yenye maudhi na ubishi wao ni uthibitisho kwamba walikuwa na hatia ya kuacha wajibu wa lazima. Kwa hiyo, majibu sahihi yanayofaa zaidi yangekuwa kwamba, kauli hii ya dharau na kukataa kwao kumpatia vifaa vya kuandikia ilikuwa ya bahati mbaya kinyume na mwenendo wao, ni kujikwaa na mtelezo wa ghafla kwa upande wao, na kupotoka kusiko kwa kawaida ambako hatukuoni kuwa na maana yoyote. Allah ndiye Mwongozaji kwenye Njia Iliyonyooka, Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 88

## RABI'UL AWWAL 11, 1330 A.H.

**Visingizio na Maelezo ni Batili na Bandia.**

Inamfaa mtu mwenye elimu na busara kama wewe kuukubali ukweli na kuzungumza kilicho sawasawa. Umepingana na vile visingizio, nyudhuru na maelezo mbalimbali yaliyotolewa na wanachuoni wako wa Sunni kwa ajili ya kauli ya dharau iliyotolewa na Masahaba na kutokutekeleza ombi lake Mtukufu Mtume la vifaa vya kuandikia. Bado kuna vipengele vingine kuhusiana na nyudhuru hizi na maelezo ambavyo havijachunguzwa bado. Nadhani ni jambo linalofaa kwa mimi kutoa maelezo yangu kuhusu hivyo na kuliacha jambo hili juu ya uamuzi wako wa kisomi.

Katika maelezo yao ya kwanza wamesema kwamba huenda Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipowaagiza kuleta karatasi na kidau cha wino kwa kweli hakukusudia kuandika kitu bali alitaka kuwapima uaminifu na utii wao tu basi. Tunasema kwa nyongeza ya uliyoyaeleza wewe kwamba; kauli hiyo ilitolewa, na amri yake haikutiiwa, wakati akiwa kwenye sakaratil-mawt, na alikuwa atoe pumzi zake za mwisho muda mfupi tu baadae, kama hadithi yenyewe inavyoeleza. Kwa hiyo ulikuwa ni muda wa kutoa tahadhari na onyo na kwa hakika sio wa kuwapima masahaba wake. Ilikuwa ni muda wa kutoa wosia wenye kuhusu masuala muhimu na kutoa ushauri wa mwisho kwa ajili ya Umma wake. Mtu yeyote ambaye yuko kwenye fadhaa ya kifo kwa hakika yuko mbali na mizaha au utani na kuonyesha namna yoyote ya vichekesho; atakuwa anajishughulisha na nafsi yake mwenyewe, mambo yake muhimu na masuala ya familia yake, marafiki, na ya Umma hususan mtu huyo aliyeko kwenye kitanda cha mauti akiwa yeye ni Mtume. Kama yeye, muda wote alioishi hakuwajaribu uaminifu na utii wao, kwa nini awapime wakati akiwa yu karibu ya kufa?

Kauli yake (s.a.w.w.), kuwaambia waondoke mbele yake wakati walipopandisha sauti na kubishana mbele yake, kwa hakika ni dalili ya kuchukizwa nao. Lau wale ambao walimpinga walikuwa na haki, angekubaliana na ukatazaji wao na angeonyesha kuridhika kwake kutokana na hilo. Mtu yeyote anayechunguza vipengele mbalimbali vya hadithi hii, hususan kauli yao kwamba Mjumbe wa Allah alikuwa anaweweseka, atakuwa ameridhika kwa hakika kwamba walikuwa wanatambua kile alichokusudia kuandika ni kitu ambacho wanakichukia, ndiyo maana wakamsababishia maumivu makali ya akili kwa kauli hiyo yenye kuudhi na wakaendelea kupandisha sauti, kubishana na kuzozana mbele yake. Hivyo katika kukumbuka tukio hili, Ibn Abbas alilia sana na kuliita tukio hili msiba mkubwa, vilevile hii inathibitisha kukosa maana kwa maelezo hayo.

Maelezo ya pili kwamba Umar kiroho alikuwa amejaaliwa na mwongozo wa kimungu na kwamba alikuwa na uwezo wa kuamua kati ya ubora na mapungufu ya jambo na kwamba alikuwa na msukumo kutoka kwa Allah, hayastahili kupewa mazingatio yoyote kwa sababu hii itamaanisha kwamba Umar alikuwa na haki katika kukataza Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kupewa vifaa vya kuandikia na sio Mtukufu Mtume katika kudai vifaa hivyo, na kwamba ule unaoitwa "msukumo" wake wa kiroho aliokuwa nao siku ile ulikuwa ni sahihi na wa kufaa zaidi kuliko ufunuo *(wahyi)* ambao ulitawala matamko na kauli zote za Mtume (s.a.w.w.); Mkweli na Mwaminifu. Wameeleza kwamba Umar alimhurumia Mtume (s.a.w.w.) na alimuokoa na kero ambazo zingeweza kupatikana kwa kuandika waraka huo licha maradhi na maumivu aliyokuwa nayo. Lakini wewe, (ambaye Mwenyezi Mungu amekujaalia uamuzi sahihi),

unatambua kwamba kuandikwa kwa waraka huo kungemletea Mtume furaha na kuridhika, kutuliza moyo wake, kustarehesha macho yake na kumfanya mwenye imani ya kinga kutokana na kupotoka kwa wafuasi wake. Amri yake ilipaswa kutiiwa na kutekelezwa sio kupuuzwa. Wakati ilikuwa ni lengo lake kupata kipande cha karatasi na kidau cha wino; na pia alikuwa ametoa amri ya kupatiwa vifaa hivyo, hakuna mtu aliyestahili kupinga matakwa yake:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ
يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ
ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا

**"Haiwi kwa muumini mwanamume wala muumini mwanamke, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapoamua jambo, kuwa na hiyari katika jambo lao. Na yeyote mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi amepotea upotevu ulio wazi."** (Qur'ani, 33:36).**"**

Zaidi ya hayo, upinzani wa Umar na wafuasi wake katika suala muhimu mno kama hilo, na kupandisha kwao sauti, kubishana na kuzozana mbele yake, ilikuwa kwake ni usumbufu na maumivu makali kuliko kule kuandika alichotaka kuandika ambacho kingeulinda Umma wake dhidi ya upotofu. Vipi itakuwa kwa mtu yeyote ambaye asingetaka kumuona Mtume (s.a.w.w.) akikerwa na kusumbuliwa kwa kuandika kitu athubutu na kujasiri kumpinga na amshitukize ghafla kwa kusema; "alikuwa anaweweseka."?

Wanasema pia kwamba Umar alifikiri kwamba kutokumpatia karatasi na kidau cha wino ilikuwa bora na busara zaidi. Haya ni maelezo yanayoshangaza, ya ajabu na yenye mushkeli kabisa. Uzuiaji huo utakuaje bora na wa busara kuliko utekelezaji wa matakwa yake, licha ya amri dhahiri ya Mtume (s.a.w.w.)? Je, Umar alifikiri kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa akitoa maamrisho ambayo kuyafuta au kuyatekeleza kwake kungekuwa ni bora zaidi kuliko kuyakazia na kuyatekeleza papo hapo?

Na bado kinachoshangaza zaidi ni hoja yao kwamba Umar alihofia kwamba Mtume huenda akaandika amri ambazo zingeweza kuwa ngumu kwa watu kuzitii na kuziacha kwake kungewafanya wastahili adhabu. Vipi ilihofiwa licha ya kauli ya Mtume (s.a.w.w.) ya uhakikisho kwamba: "…kamwe hamtapotea baada ya wosia huo?" Je, Umar alikuwa na ujuzi zaidi wa matokeo ya waraka huo kwa usahihi zaidi kuliko Mtume mwenyewe? Hivi yeye alikuwa na wasiwasi wa uchungu zaidi kuhusu ustawi wa Umma na kwamba alikuwa na huruma na upole kwa Umma huu kuliko Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe? Kwa hakika sivyo.

Vilevile wamesema kwamba Umar alihofia kwamba wanafiki wangeweza kukataa na kutilia shaka usahihi wa waraka ulioandikwa wakati wa maradhi ya Mtume (s.a.w.w.), na kwamba hali hiyo itasababisha kashfa na kusababisha kufuru na uasi. Wewe, (Allah asaidie ukweli kujuliakana kupitia watu wako), unatambua kwamba kisingizio kama hicho kilikuwa ni muhali wakati Mtume, (s.a.w.w.) alikwishasema: "…kamwe hamtapotea" ambayo ina maana kwamba wosia huo ungekuwa ni chanzo cha usalama wa Umma kutokana na mkengeuko. Hivyo ni vipi yatakuwa ni sababu ya kashfa ya kijamii na kutiliwa shaka na kukosolewa na wanafiki kuhusu usahihi wake? Lau yeye [Umar] angehofia wanafiki hao na kutia kwao shaka kuhusu usahihi wa kile ambacho Mtume alitaka kuandika, kwanini alipanda mbegu ya shaka

hiyo yeye mwenyewe wakati alipopinga na kukatalia kuletwa kwa vifaa hivyo na hata akasema kwamba Mtume alikuwa anaweweseka?

Wakati wakitafsiri maneno yake Umar: “Kitabu cha Allah kinatutosha” wamerejea aya ya Qur’ani:

مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ

**“Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote…..” (Qur’an, 6:38),”**

Na

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ

**“Leo nimewakamilishia dini yenu….” (Qur’ani, 5:3).**

Rejea hizi sio sahihi, ni za kimakosa, kwani hakuna aya inayodokeza usalama wa daima wa Umma dhidi ya upotofu, wala aya zote hizo hazihakikishi mwongozo wa Umma kwenye njia iliyonyooka. Hivyo, ni vipi, kwa msingi wa aya hizi na kutokujali waraka uliokusudiwa au kutouheshimu kukubalike? Lau kuwepo kwa Qur’ani Tukufu ingekuwa ndio chanzo cha usalama dhidi ya upotofu, basi kusingekuwa na upotofu na mfarakano uliopo sasa hivi katika Umma huu ambao kuondolewa kwake kunaonekana takriban kuwa kamwe ni jambo lisilowezekana.[387]

Katika maelezo yao ya mwisho, kwa niaba ya Umar, wamesema kwamba Umar hakuelewa kutokana na amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba wosia huo uliokusudiwa ungemlinda kila mtu katika Umma wake kutokana na upotofu. Bali kwamba, yeye alielewa kwamba baada ya kuandikwa, wosia huo ungewakinga umma mzima kukubaliana katika jambo la makosa au mkengeuko katika njia ya haki. Wanadai kwamba Umar, Allah awe radhi naye alikwishajua kwamba kamwe haitatokea umma mzima kukubaliana katika jambo la makosa, japo waraka huo uandikwe ama usiandikwe, na kwa sababu hii alizuia vifaa vya kuandikia visiletwe kwake na akaleta upinzani. Pamoja na kile ulichoeleza tunaweza

[387] Wewe (Allah asaidie ukweli kupitia kwa watu wako) unajua kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakusema kwamba lengo la kutaka vifaa vya kuandikia lilikuwa ni kutaka kuandika sheria au maelekezo ambayo yangeweza kujibiwa kwa maneno “Kinatutosha Kitabu cha Allah Aza wa Jallah.” Hata kama tukichukulia kwamba alitaka kuandika amri na maelekezo kama hayo, bado kupewa vifaa vya kuandikia vingetolewa kwake kwa sababu kuandikwa kwa waraka huo huenda kungekuwa ni chanzo cha usalama wa Ummah dhidi ya upotofu. Kwa hiyo, kulikuwa hakuna sababu ya kutotii amri yake ya kutaka vifaa vya kuandikia na kutosheka na Qur’ani peke yake kwa ulinzi na mwongozo. Kama maandiko aliyotaka kuandika hayakukusudiwa hasa kuuokoa Ummah dhidi ya upotofu, basi kuyaepuka na kutegemea juu ya Kitabu cha Allah peke yake labda kungekuwa ni sawa. Lakini unajua haja shinikizi ya Ummah wa Waislamu kuhitajia maagizo na amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ulazima wa maagizo hayo licha ya Kitabu cha Allah, kama sharti la msingi. Hata kama Qur’ani ikiwa imeingiza kila kitu na kukamilika kabisa, haiwezekani kwa kila mtu kupata maamuzi na matoleo kutoka humo (Kitabuni) sio rahisi kwa kila mtu wa kawaida. Lau Kitabu cha Allah kingekuwa kinajitegemea chenyewe pamoja na ufafanuzi na maelezo yenye maoni ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), basi Allah Aza wa Jallah asingemuamuru kuifafanua kwa watu wakati aliposema:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

**“Na tumekuteremshia ukumbusho ili uwabainishie watu yale waliyoteremshiwa wapate kufikiri.” (16:44)**

kuongeza kwamba Umar hakuwa na upungufu wa kielimu kiasi cha kutoelewa hadith ya maombi ya vifaa vya kuandikia ambayo ilikuwa wazi kwa watu wote, na wakazi wa mjini na wale wa majangwani walielewa kwamba kama waraka huo ungeandikwa ungeweza kuwa ni chanzo kamili kwa ajili ya ulinzi wa kila mtu dhidi ya makosa na upotofu.

Hii ndio maana ya hadithi hii ambayo hujitokeza mwanzo kwenye akili ya kila mtu anapoisikia. Na Umar alijua kwa hakika kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alikuwa hana wasiwasi kuhusu Umma wake kuwa na makubaliano ya pamoja katika mitazamo ya makosa au ukengeukaji kutoka kwenye njia ya sawa, kwa vile Umar (ra), alimsikia Mtume (s.a.w.w.), mara kadhaa akisema: "Umma wangu hautakuwa pamoja katika upotofu wala makosa" na kauli yake (s.a.w.w.): "Kundi moja kutoka katika Umma wangu siku zote litasimama kupigania haki na kuiunga mkono" na alikuwa anajua maneno ya Mwenyezi Mungu yanayosema:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ
كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا

**"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale ambao wameamini na wakatenda mema kuwa hakika atawafanya makhalifa katika ardhi, kama alivyowafanya waliokuwa kabla yao. Na kwa yakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea na hakika atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi….." (Qur'ani, 24:55).**

Amesoma katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kusikia kutoka kwa Mtukufu Mtume aya nyingi kuhusiana na hili kwamba Waislam, wote bila kubagua, kamwe hawatakubaliana katika makosa ama upotovu. Hivyo, si yamkini, licha ya yote haya, kwamba hakuna anayeweza kuamini kwamba iliingia akilini mwa Umar au yeyote yule mwingine kwamba Mtume (s.a.w.w.), alitaka aletewe karatasi na kidau cha wino kwa sababu alikuwa ana wasiwasi kuhusu Umma wake wote kuja kupotea. Ilikuwa ni katika uhakika wa mambo kwamba Umar alipaswa kuwa ameelewa kutoka kwenye madai ya Mtukufu Mtume ya kutaka vifaa vya kuandikia kile kinachoonekana kwenye akili za wengine na sio kile kinachopingwa na aya sahihi za Qur'ani na Hadith sahihi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Lakini zaidi ya hayo, kuchukizwa kwa Mtume (s.a.w.w.), kuliko wazi katika maneno yake, "Simameni na muondoke mbele zangu," ni uthibisho wa kufanya kwao kosa la kuacha kwao kile ambacho ni wajibu wao wa lazima na kuwa na hatia ya kutotii amri yake ya kutaka vifaa vya kuandikia. Lau kama kauli ya dharau ya Umar na kukataza kwake kuletwa vifaa vya kuandikia kungekuwa kwa sababu ya kutoelewa, kama wanavyodai baadhi ya watetezi wake, basi Mtume angemsaidia kuondoa kutokuelewa kwake, na angemfafanulia lengo lake la kuandika wosia huo. Angeweza pia kumlazimisha yeye na wafuasi wake kumletea vifaa na kuandika waraka huo licha ya upinzani wao. Lakini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakujaribu kuwaondolea mushkeli wao wala kuwawekea ulazima wowote juu yao. Aliwaamuru tu watoke nje kwa sababu yeye alijua kwamba kauli hiyo ya twezo na kutokubaliana na amri yake viliegemea sio kwenye kutoelewa kokote kule bali kulisababishwa na fikra nyingine tofauti. Tena machozi ya Ibn Abbas na uchungu na wasiwasi katika kukumbuka tukio hili la kimsiba ni ushahidi wa nguvu kabisa wa ukweli wa maelezo yetu.

Kwa hakika tukio hili la kimsiba haliruhusu kisingizio chochote. Lau ingekuwa ni kujikwaa tu au kuteleza kwa nadra kidogo tu kwa upande wa masahaba kama ulivyosema, hilo lingechukuliwa kwa wepesi na uvumilivu mkubwa; ingawa tukio hili lilithibitisha kuwa ni msiba wa kuenea na wenye kishindo. Hakika, sisi sote ni wa Allah na Kwake ndio marejeo. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 89

## RABI'UL AWWAL 14, 1330 A.H.

**I. Kukiri kwa Visingizio na Maelezo kuwa Dhaifu,**

**II. Maombi ya Kadhia nyingine za Masahaba Kukaidi Amri na Hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).**

Umewazingira kutoka pande zote watetezi wa Umar na wafuasi wake, ukaziba njia zao zote na hukuwaachia njia mbadala na umesimamisha ukuta kati yao na matamanio yao. Ulichokieleza hakiruhusu nafasi yoyote ya kutoeleweka na hakuonekani sababu ya kutilia shaka ukweli wa mahitimisho yako.

Hivyo, tafadhali endelea kuelezea zaidi mada iliyoko kwenye mjadala na ulete kadhia zingine ambazo kwazo Masahaba hawakutii amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kwa kudhamiria kabisa wakitafsiri kinyume Hadithi ya wazi ya Mtume. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 90

## RABI'UL AWWAL 17, 1330 A.H.

**Jeshi La Usamah.**

Kama kweli umeukubali ukweli, bila kuogopa lawama yoyote, basi wewe ni mhimili ambao unasaidia mti wa mtende unaolemewa na mzigo wa matunda, na ni fimbo mti inayotumika kwa farasi mwenye muwasho katika kuuondoa muwasho wake huo (yaani, akili yako kali mno na uamuzi wa busara unaondoa matatizo na kuponya maradhi ya wengine). Kwa cheo uko juu sana kuweza kupamba uongo uonekane ni ukweli, na kwa nafasi yako uko juu sana kuweza kuficha ukweli. Na uko juu hata zaidi ya mambo haya. Wewe ni mcha-Mungu na mwaminifu.

Wewe (Mwenyezi Mungu akujaalie nguvu), umenitaka nikusimulie kadhia zote zingine ambamo masahaba walipendelea kufanya mambo kwa mujibu wa maamuzi yao wenyewe kuliko kunyenyekea kwenye amri za kiungu za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Kuhusiana na hili, unaweza kuangalia ile kadhia ya jeshi la Usamah bin Zayd bin Haritha lililoandaliwa kutumwa kwenda Asia Ndogo. Ilikuwa ni msafara wa kijeshi wa mwisho ulioandaliwa wakati wa Mtume (s.a.w.w.) ambaye (wazazi wangu wawe kafara kwa ajili yake) alijishughulisha nalo sana katika kuliandaa kwa uangalifu mkubwa. Aliwaamrisha masahaba zake kujiandaa kwa msafara huo wa kivita. Kwa ari kubwa aliwahimiza wote kwenda na msafara huo na yeye binafsi alilitayarisha jeshi hilo na kuwakusanya ili kuwapa moyo na kuimarisha dhamira zao. Walikuwamo katika kikosi hicho akina Abu Bakr, Umar,[388] Abu Ubayda, Sa'd na mfano wao. Hakuacha hata mtu mmoja maarufu kutoka miongoni mwa Muhajirun wala Answar, katika kuorodhesha.[389]

Kikosi hiki kilikusanywa mnamo mwezi 26 Safar, 11 A.H. Siku iliyofuatia alimuita Usamah na akasema: "Nenda kwenye sehemu ambako baba yako aliuawa. Wakanyagekanyage hadi uwauwe. Nimekuteua wewe kuwa Kamanda Mkuu wa jeshi hili. Washambulie watu wa Ubna[390] wakati wa asubuhi. Pandeni farasi wanaotembea kwa kasi. Safirini kwa mbio kali ili muweze kufika kabla ya taarifa ya kuwasili kwako. Kama Allah atakupa ushindi, basi usikae huko muda mrefu. Chukua waongozaji wa njia pamoja nawe; tuma watu wa ramani, wapelelezi na wakusanya taarifa kabla yako."

---

[388] Waandishi wote wa wasifu na wasimulizi wa hadithi kwa pamoja wamekubaliana kwamba Abu Bakr na Umar (Allah awe radhi nao), walijumuishwa kwenye jeshi hilo. Wamelieleza hili kwenye vitabu hivyo miongoni mwa riwaya ambazo kwa kawaida zimekubalika kwamba ni sahihi na za kweli. Kwa hiyo, rejea kwenye kitabu chochote ambacho kina taarifa za jeshi hili makhususi kama vile *Tabaqat* cha Ibn Sa'd, *Tarikh al-Tabari* na *Tarikh al-Kamiil* ya Ibn al-Athir, *Al-Sira al-Halabiyya, Al-Sira al-Dahlaniyya,* na vinginevyo. Wakati Halabi alipokuwa anaelezea juu ya jeshi hili katika Jz. 3 ya *Siirat ul-Halabiya* (kitabu cha wasifu), anataja kisa kimoja cha kweli cha kuvutia (ambacho kimetafsiriwa kwa uaminifu kabisa hapa chini):

"Wakati Khalifa al-Mehdi wa Bani Abbas alipoingia Basra ilitokea akamuona Ayas bin Mu'awiyah, ambaye alifahamika sana kwa uhodari wake wa akili, akiwa bado kijana mdogo akiongoza swala ya watu wazima kiasi cha watu mia nne na wenye ilmu wakiwa nyuma yake. al-Mehdi akasema: 'Wasiokuwa na haya wenye ndevu hawa! Hivi hakuna yeyote kati ya watu wazima hawa anayeweza kuongoza swala badala ya huyu kijana?' Kisha akamgeukia Ayas akamuuliza 'Una umri gani ewe kijana? Akajibu: 'Allah arefushe uhai wa Amirul Muminin (yaani, al-Mehdi)! Mimi nina umri kama uleule wa Usamah ibn Zayd ibn Harithah wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipomteua kuongoza kikosi ambacho miongoni mwa watu wengine, walikuwemo pia Abu Bakr na Umar.' Al-Mehd akasema: 'Shikilia nafasi yako hapo mbele, Allah akubariki sana.'" Wakati huo Usamah alikuwa na miaka kumi na saba."

[389] Umar alikuwa akimuambia Usamah: "Wakati wa kifo cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) wewe ulikuwa mkubwa wangu (kamanda)." Inanukuliwa kauli yake hii na kundi la wanachuoni wengi mashuhuri wa hadith na historia kama vile Allamah al-Halabi wakati alipokuwa anaelezea juu ya jeshi la Usamah katika kitabu chake Al-Sira al-Halabiyya.

[390] Ni eneo jirani ya Balqa huko Syria, iko kati ya Asqalan na Ramla karibu na Mauta ambako Zayd ibn Harithah na Ja'far ibn Abi Talib at-Tayyar (wa mbawa mbili katika Pepo, amani juu yake) waliuawa shahidi.

Mwezi 28 Safar, maradhi ya mwisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yaliongezeka, na alikuwa na joto kali (wazazi wangu wawe kafara juu yake) na kuumwa sana na kichwa. Mnamo mwezi 29 Safar, aliwagundua kwamba ni wazito na hawataki kuondoka; kwa hiyo, alitoka nje na akawasihi kuondoka mara moja. Yeye (s.a.w.w.) aliifunga bendera kwenye nguzo yake kwa mikono yake mitukufu na kumkabidhi Usamah ili kuchochea dhamira zao za jihadi na kuwatia nguvu. Kisha akasema: "Shambulia kwa jina la Allah, pigana katika Njia ya Allah, na uwauwe wale ambao hawaamini katika Allah." Usamah akatoka na bendera ile ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akamkabidhi Buraydah. Jeshi likapiga kambi sehemu iitwayo Jurf nje kidogo ya Madina ambapo Waislam walizurura kigoigoi na hawakuondoka, licha ya kauli zote za wazi na maelekezo ya Mtume (s.a.w.w.) kuwahimiza kuondoka mapema iwezekanavyo, tena kwa kasi kama ilivyo katika maagizo yake: "Wavamieni watu wa Ubna wakati wa asubuhi," na "muwasili mapema kabla ya taarifa za kufika kwenu," na maagizo mengine yenye amri kama hayo. Masahaba walipuuza maagizo haya na kamwe hawakuyatekeleza. Aidha, baadhi yao walianza kupinga kuteuliwa kwa Usamah kuwa kiongozi wao katika jeshi hilo, kama walivyopinga ule uongozi wa baba yake huko nyuma. Walisema mambo mengi yasiyopendeza juu ya Usamah licha ya kushuhudia wao wenyewe Mtume (s.a.w.w.) akimpa madaraka hayo, na kusikia kwao Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Nakuchagua kama Kiongozi Mkuu (Jemadari mkuu) wa jeshi hili," na kuona kwao akifunga bendera kwa ajili yake, kwa mikono yake mitukufu, licha ya kuwa Mtume alikuwa na homa kali, na kuikabidhi kwa Usamah.

Yote hayo bado hayakuwazuia kupinga kuchaguliwa kwa Usamah kama kamanda wao. Tabia hii ya masahaba ilimchukiza sana Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kiasi kwamba alitoka nje ya nyumba yake na kwenda msikitini kichwani akiwa amefunga kitambaa,[391] huku akiwa amejifunika shuka la kitambaa laini, na mwenyewe akisumbuliwa na homa kali. Hii ilikuwa ni siku ya Jumamosi, mwezi 10 *Rabi'l-Awwal,* siku mbili tu kabla ya kufariki kwake. Akapanda juu ya mimbari akamshukuru Allah na kumtukuza, kisha akatoa hotuba ambayo imeandikwa na kurudiwa na wanahistoria, na wanachuoni wote wa Kiislam wanakubaliana kwa pamoja kwamba alitoa hotuba ifuatayo:

"Enyi watu! Nimearifiwa kwamba baadhi yenu mnapinga kumchagua kwangu Usamah kama Kamanda Mkuu wa kikosi hiki. Mnapinga kuteuliwa kwake sasa kama mlivyofanya hapo kabla wakati nilipomteuwa baba yake kuwa Kamanda Mkuu. Naapa Wallahi baba yake kwa hakika alikuwa mwenye ufanisi kwa cheo hicho, na baada yake mwanawe ni hodari wa kustahiki cheo hicho."

Kisha akawahimiza waanze safari bila ya ucheleweshaji tena, na kwa kweli masahaba hao walianza kumuaga na kuondoka kuelekea kwenye kambi ya jeshi hilo iliyokuwa hapo Jurf. Aliendelea kuwahimiza kufanya haraka ya kuondoka mpaka maradhi yake yakachukua hatua kali zaidi. Lakini bado aliendelea kuwahimiza akisema: "Jeshi la Usamah! Kamilisheni kazi ya jeshi la Usamah! Pelekeni jeshi la Usamah!" Aliendelea kurudia rudia kutoa amri lakini masahaba walikuwa bado ni magoigoi hawataki kuondoka.

Siku iliyofuatia, yaani mwezi 12 Rabi'ul-Awwal, Usamah alitoka kambini kwake pale Jurf na kumtembelea Mtume (s.a.w.w.) ambaye alimuamuru kuanza safari yake mara moja, akisema: "Kesho kwa baraka za Allah Aza wa Jallah, ondoka mapema asubuhi," hivyo alimuaga na kuelekea kambini. Lakini alirejea akiwa amefuatana na Umar na Abu Ubaydah. Watu watatu hawa walimkuta Mtume ambaye alikuwa anakaribia kuvuta pumzi yake ya mwisho. Alifariki siku hiyohiyo (nafsi yangu na zile za walimwengu zitolewe muhanga kwa ajili yake). Jeshi lilirudi mjini Madina pamoja na bendera hiyo. Sasa wakaamua kuahirisha safari hiyo ya kijeshi. Wakati Abu Bakr alipokuwa Khalifa walimtaka kwa

[391] Wasimuliaji wote wa hadithi na mwandishi wa wasifu na vitabu vya historia ambao wametoa maelezo juu ya jeshi la Usamah vilevile wametaja upinzani wa masahaba juu ya uteuzi uliofanywa na Mtume kumteuwa Usamah kama kamanda juu yao, na kwamba Mtume (s.a.w.w.) alitoka nje akiwa amekasirika mno kama tulivyoeleza, kwa hiyo, alitoa khutba ambayo tumeinukuu mapema. Tafadhali rejea kwenye sura juu ya 'Jeshi la Usamah' katika *Tabaqat* ya Ibn Sa'd, *Siirat ul- Halabiya* na *Siirat al-Dahlani*, na vitabu vingine vinavyoshughulika na mada hii.

msisitizo wote walioweza kuwa nao kuivunja kabisa safari hiyo, licha ya kushuhudia kwa macho yao Mtume (s.a.w.w.) akifanya mipango ya kampeni hiyo na kuvitayarisha vikosi yeye mwenyewe, wakiwa wamesikia amri yake kwa marudio kwa uwazi wa kuharakisha kulipeleka jeshi katika hali ya haraka ili kuwafanya watu wa Ubna wasijue kuhusu habari zake, wakiwa wameziona juhudi zake kubwa kuliandaa jeshi hilo yeye mwenyewe binafsi, akamteuwa Usamah kuwa kiongozi wake, na akafunga bendera kwa mikono yake mitukufu akiwa na uchungu wa kifo, akisema: “Ondokeni mapema asubuhi kesho kwa baraka za Allah, Aza wa Jallah.” Na kama si Khalifa basi wangeamua kuifuta kampeini ile na kulirudisha jeshi na kuikunja bendera, lakini Abu Bakr hakuliruhusu hilo. Walipomuona amedhamiria kuitekeleza kampeini hiyo, Umar alimfuata na kumuomba kwa niaba ya Answar kumuondoa Usamah kutoka kwenye nafasi ya uongozi wa jeshi na amchague mtu mwingine mwenye uwezo kama kamanda mkuu, ingawa si muda mrefu tangu wamkasirishe Mtume na kumhuzunisha kwa kutokupendezwa kwao na uteuzi wake wa Usamah kama kamanda wa jeshi, na kutoka kwake nje ya nyumba yake kwa sababu hii hii, akiwa anaumwa sana na homa kali, akiwa amefunga kitambaa kichwani kwa maumivu, na huku akiwa amejifunika blangeti, na kuyumba katika kutembea kwake kutokana na udhaifu na mwili kutetemeka kwa hasira na kule kupanda kwake kwenye mimbari, akipumua kwa nguvu, na shauku ya kutaka msafara huo uondoke haraka, alisema:

“Enyi watu wangu! Nimeambiwa kwamba baadhi yenu mnapinga uteuzi wangu wa Usamah kama kamanda wa jeshi hili. Mnapinga kuteliwa kwake sasa kama kamanda mkuu kama mlivyopinga kumteuwa kwangu baba yake kabla yake, Naapa Wallahi baba yake kwa hakika alikuwa mwenye ufanisi kwa cheo hicho, na baada yake mwanawe ni hodari wa kustahiki cheo hicho.”

Hivyo ndivyo alivyofanya, Mtume (s.a.w.w.), kusisitizia hotuba yake kwa kuapia jina la Allah, na akakazia zaidi kwa kutumia neno ‘*Inna*’ kwa maana ya ‘Hakika’ na herufi thibitishi ‘Lam’ ya Kiarabu ili kuwafanya waachane na upingaji wao uteuzi wa Usamah kama Kamanda Mkuu wa jeshi hilo. Lakini wapi! Hawakuacha kufanya hivyo, na wakamuudhi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Khalifa Abu Bakr alikuwa mkaidi sana katika kukataa kusalimu amri kwenye shinikizo lao la kumuondoa Usamah kwenye nafasi yake. Aliruka na kukamata ndevu za Umar huku akisema: “Akulilie mama yako na akukose ewe mwana wa Khatab! Na uangamie wewe! Unanishinikiza nimuondoe Usamah ambaye ameteuliwa na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kuwa Kamanda Mkuu wa jeshi hili!”[392] Waliendelea kukataa uteuzi wa Usamah. Hatimaye Usamah alianza safari hiyo akiwa na idadi ya wanajeshi elfu tatu, ukijumuisha pamoja na askari wa farasi elfu moja.[393] Idadi kubwa ya masahaba ambao walioorodheshwa na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) mwenyewe walijitoa kwenye jeshi hilo, ingawa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa amesema, kama ilivyoandikwa na Shahristani kwenye utangulizi wa nne kwenye kitabu chake *Al-Milal wal Nihal*: “Harakisheni kuondoka na jeshi la Usamah; Mwenyezi Mungu amlaani yule atakayejitoa kwenye jeshi lake.”

Unaona kwamba wakati wa uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) masahaba walikuwa magoigoi katika kuanza safari ya jeshi hilo; kisha baada ya kifo chake wakajitoa kwenye jeshi hilo, ili waweze kuanzisha kwa uimara kabisa serikali yao. Hivyo walipendelea kuanzisha serikali yao na usalama wa utawala wao kuliko kutii amri ya wazi ya Mtume (s.a.w.w.). Walijua kwamba safari hiyo ya kijeshi haitaachwa kutokana na uzembe na uzito wao na mbinu zao za ucheleweshaji au kwa kujitoa kwao kwenye jeshi, na walifikiria

392 Hadithi hii imenukuliwa katika *Sirat al-Halabiya* na *Sirat al-Dahlani* na Ibn Jarir al-Tabari wakati anajadili matukio ya mwaka wa 11 A.H. katika kitabu chake cha *Tarikh* (historia), kwa nyongeza ya waandishi wengine wa vitabu vya historia.

393 Usamah alishambulia Ubna, akachoma nyumba zao, na kuharibu mazao yao, na kuuwa wapanda farasi wao kwenye uwanja wa vita, wakawaua wale wote walijitokeza kupigana na kuwakamata mateka wale waliojisalimisha, vilevile akamuua yule aliyekuwa amemuua baba yake. Miongoni mwa wale waliuawa alikuwa ni muuajiwa baba yake. Hakuna yeyote aliyeuawa miongoni mwa Waislamu mpaka hapa. Sifa zote ni za Allah Mola wa walimwengu. Wakati huo Usamah alikuwa amepanda farasi wa baba yake na wito wake likuwa: “Ya Mansuur Ummat” (Enyi Ummah wenye ushindi), ambalo ulikuwa ndio wito wa Mtume (s.a.w.w.) wakati wa Vita vya Badr. Aliwapa kila askari wa farasi mafungu mara mbili ya ngawira na kila askari wa miguu na mgao mmoja, na yeye mwenyewe akachukua mgao mmoja.

kwamba kama wangeondoka Madina na wakaenda kushiriki kwenye jeshi la Usamah kabla ya kifo cha Mtume (s.a.w.w.) kwa hakika wangeikosa daima ile fursa waliyokuwa wakiisubiri kwa muda mrefu, ya kuanzisha serikali ya kundi lao. Yeye (s.a.w.w.) alitaka kwamba Madina iondokane na masahaba wakaidi ili kwamba baada ya kuondoka kwa jeshi hilo, suala la Ukhalifa lingemalizwa kwa utulivu na amani kwa upande wa Amirul Muminin Ali ibn Abi Talib (as). Hivyo, wakati wakirudi, watakuja kugundua kwamba Ukhalifa wa Ali bin Abi Talib (a.s.) kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) tayari umekwishathibitishwa na kiapo cha utii kuchukuliwa na watu wengi, na kutakuwa hakuna nafasi ya mgogoro na mfarakano.

Mtume alimteuwa Usamah, ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi na saba,[394] kuwa Kamanda Mkuu kwa lengo tu la kuwadhibiti baadhi ya masahaba ambao walikuwa na kiburi sana cha kutomtii kikamilifu, na kusahihisha fikra za wale wenye kigeugeu, na vilevile kuweka kigezo kwa ajili ya baadae na kuzuia upinzani na mgogoro katika kuchaguliwa mtu aliye na umri mdogo kama kiongozi au mtawala juu ya wale wenye umri mkubwa kuliko yeye. Lakini masahaba hao walitambua lengo la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.); hivyo, walipinga uteuzi wa Usamah kuwa kiongozi, wakawa walegevu na kutopenda kufuatana naye, na hawakuondoka Jurf mpaka roho ya Mtume (s.a.w.w.) iliporejea kwa Mola Wake, walipokuwa na shauku ya kuivunja kampeini hiyo na kuifungua bendera ya jeshi na hatimaye kumuondoa Usamah. Aidha, wakati jeshi hilo lilipoondoka kambini hapo kuendelea na safari, wengi wao wakajitoa, kama tulivyokwisha kueleza. Sura za kuzingatia juu ya kadhia hii ya jeshi la Usamah ni:

(a) Hawakutii amri za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.);

(b) Katika masuala ya kisiasa, wao walipendelea kufanya kulingana na mawazo na uamuzi wao wenyewe kuliko kutii amri zake Mtume (s.a.w.w.) za wazi na dhahiri;

(c) Walipinga kumchagua kwake Usamah kama Kamanda Mkuu ;

(d) Baada ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walijaribu kila walivyoweza kufanya ile safari ya kijeshi itelekezwe moja kwa moj; na

(e) Walipokuwa hawakufanikiwa kufanya safari ivunjwe walianzisha njama zisizofanikiwa za kumuondoa Usamah kwenye uongozi wa jeshi.

Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[394] Hii ndio kauli yenye nguvu, baadhi wanasema alikuwa ana umri wa miaka kumi na nane, wengine wanasema kumi na tisa, na bado wengine wanasema ishirini, na hakuna aliyesema kwamba alikuwa mkubwa zaidi ya hiyo.

# BARUA YA 91

## RABI'UL AWWAL 19, 1330 A.H.

**I. Utetezi wa Masahaba Kutokwenda na Jeshi la Usamah,**

**II. Kukosekana Hadith Sahih, *Mutawatir* Inayowalaani wale Ambao Hawakujiunga na Jeshi hilo.**

Ni kweli kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aliwahimiza kuanza mapema safari ya jeshi lililoongozwa na Usamah, akiwaamuru wafanye kila haraka iwezekanayo kuondoka, kama ulivyotaja. Amri yake ilikuwa ni ya kulazimisha. Alipomteua Usamah kama kiongozi na Jemedari Mkuu wa kikosi hicho alimtaka kuwavamia watu wa Ubna wakati wa asubuhi, na hakumruhusu angojee mpaka jioni, na akimuambia "Safiri kwa haraka." Hakuna kingine isipokuwa kwenda kwa haraka tu, na safari ya kasi tu ndio ingemridhisha yeye (s.aw.w.). Lakini yeye (s.a.w.w.) baada ya hapo, maradhi yake yalizidi. Masahaba hawakuwa tayari kwenda safari hiyo kwa sababu hawakuweza kustahimili kutengana na Mtume wakati akiwa katika hali ya mashaka kiafya. Walikaa Jurf wakisubiri kupata taarifa kuhusu hali ya afya yake, na hii ni kwa sababu ya uambatanaji wao wa upendo kwake na mapenzi makubwa juu yake (s.a.w.w.). Kwa hiyo, lengo la kuchelewesha kwao safari hiyo lilikuwa kusubiri apate ahueni, ili wapate kupoza macho yao kwa kumuona akiwa katika afya ya kawaida tena, au hadi kifo chake ili wapate heshima ya kushiriki maziko yake na kusafisha njia kwa ajili ya uanzishaji madhubuti na tulivu wa serikali ya mrithi wake. Kwa hiyo mwenendo wao katika kuchelewesha kuanza kwa safari hiyo ya kijeshi na kusubiri mabadiliko katika hali yake haukuwa ni jambo la vurugu au la kukirihisha bali ni jambo la kusameheka na lisilo na hatia.

Ama kuhusu kupinga kwao uteuzi wa Usamah kama Jemadari mkuu wa jeshi hilo kabla ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), licha ya kusikia kwao amri yake ya wazi na onyo lake kuhusiana na hili, na kuona shauku yake yenye nguvu katika uteuzi huo, sababu ilikuwa kwamba baadhi ya masahaba walikuwa na umri wa kati na wengine walikuwa wazee, wakati Usamah alikuwa kijana mdogo bado, Na watu wa umri wa kati na wenye umri mkubwa kwa tabia yao hawako tayari kuwa chini ya kijana mdogo na huona vigumu sana kutekeleza amri zake. Kutofurahia kwao uteuzi wa Usamah kama Jemadari mkuu kwa hiyo, hakukuwa ni uzushi au ukaidi kwa upande wao, bali shauku ya tabia na maumbile ya kibinadamu; ambavyo naomba uvizingatie hivyo.

Ama kuhusu madai yao baada ya kifo cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ya kumuondoa Usamah, baadhi ya wanachuoni wanasema kwamba, masahaba walitegemea kwamba Abu Bakr Siddiq angekubaliana nao walidhani kwamba kuondolewa kwa Usamah kungekuwa ni jambo la busara na kwa maoni yao ni kwa masilahi ya Umma. Bado hata hivyo, kwa ajili ya uadilifu, mimi binafsi sioni mantiki ya ombi lao la kutaka kumuondoa Usamah baada ya kuona jinsi gani Mtume (s.a.w.w.) alivyoonyesha kukasirika kwake kukubwa wakati walipokataa uteuzi wake kwa kutoka nje, huku akiwa na homa kali, akiwa amefunga kitambaa kichwani na kujifunika shuka, na kupanda juu ya mimbari kutoa khutba yake akishutumu kukataa kwao na kuthibitisha uteuzi wake, ambalo ni jambo linalojulikana kihistoria. Hivyo tena, ni kwa nini wamekataa uteuzi wake haswa licha ya yote haya, Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anayejua.

Ama kuhusu ombi lao la msisitizo la kumshinikiza kwao al-Siddiq kuahirisha safari hiyo, pamoja na kuona jinsi gani Mtume alivyokuwa na shauku kubwa juu ya safari ya jeshi hilo, kuhusika kwake

mwenyewe kuliandaa, kuhimiza kuondoka kwake mapema iwezekanavyo, halikadhalika kusikia amri zake za kurudia rudia kuhusiana na hilo, si lolote bali ni kwa mtazamo wa ulinzi wa Waislamu kutokana na washirikina waliozunguka kwenye vitongoji vya Madina. Kwa kufariki Mtume (s.a.w.w.), mara tu wanafiki walijitokeza nje, Mayahudi na Wakiristo walirudisha sehemu ya nguvu yao iliyokuwa imepotea, na kundi miongoni mwa Waarabu waliritadi, wakati kundi lingine lilikataa kulipa zaka. Kwa hiyo masahaba wa Mtume walizungumza na bwana wetu al-Siddiq na wakamuomba amkataze Usamah asiende safari hiyo ya kivita ambapo alikataa na akasema: "Ni bora kwangu mimi nibebwe na ndege wa mawindo kuliko kuanza kufanya jambo lolote kabla ya kutekeleza lile ambalo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ametuamrisha kufanya ."

Hivi ndivyo wanachuoni wetu walivyosema kuhusiana na al-Siddiq. Ama kuhusu maombi ya masahaba wengine ya kutaka kwao kusimamisha kampeini za jeshi la Usamah, lengo lao halikuwa chochote bali ni kuulinda usalama wa Uislamu. Ama kuhusu sababu ya Abu Bakr, Umar kutokwenda na jeshi la Usamah, ilikuwa kwamba walikuwa wanashughulika na kuweka misingi ya serikali ya Kiislamu, kuimarisha dola ya Muhammad (s.a.w.w.), na kuilinda serikali, ambayo bila hiyo dini haingekuwa salama wala waumini wake.

Ama kuhusu ile hadith uliyoinukuu kutoka kitabu cha Shahristan *Al-Milal wal Nihal,* tumeona kwamba bila jina la msimuliaji, ambapo wote al-Halabi na Sayyid al-Dahlani, katika vitabu vyao husika vya wasifu, wamesema kwamba kwa kweli hakuna hadithi kama hiyo kabisa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na hilo. Kama wewe katika elimu yako unayo hadith iliyosimuliwa kutoka njia ya Sunni kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), basi tafadhali tujulishe. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 92

## RABI'UL AWWAL 22, 1330 A.H.

**I. Kisingizio kwa Niaba ya Sahaba Hakipingani na Maelezo yetu,**

**II. Hadithi ya Shahristani Imethibitishwa na Wanahadith Mashuhuri.**

Mwenyezi Mungu akujaalie amani! Umekiri kwamba masahaba walichelewesha safari ya jeshi la Usamah na kwamba walionyesha ulegevu pale Jurf na hawakuondoka kambini hapo kuendelea na safari licha ya kuamriwa na Mtume (s.a.w.w.) kuondoka kwa haraka kiasi iwezekanavyo. Vilevile umekiri kwamba kwa kweli walipinga kuteuliwa kwa Usamah kama Jemadari Mkuu licha ya shauku ya Mtume (s.a.w.w.) waliyoona katika maneno na matendo kuhusu kuteuliwa kwake kama Kamanda Mkuu.

Umeendelea kukiri kwamba, kwa kweli masahaba walimuomba Abu Bakr aifute safari hiyo ya kijeshi hata baada ya kuona jinsi Mtume (s.a.w.w.) alivyokasirika juu ya kupinga kwao kule kumsimika Usamah kwa kutoka kwake nje huku akiwa na homa kali, akiwa amefunga kitambaa kichwani kwa sababu ya maumivu, huku akiwa amejifunika shuka mwilini mwake, akiwahutubia kutoka juu ya mimbari, khutba ambayo wewe mwenyewe umeielezea kwamba ni mambo ya kihistoria na kuthibitisha uteuzi wa Usamah katika nafasi hiyo.

Umeukubali pia ukweli kwamba idadi kubwa ya masahaba walimuomba Khalifa Abu Bakr kulivunja jeshi lililoandaliwa na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) mwenyewe, na kwamba alikuwa amewaamuru watu kwenda kwenye kampeni hiyo chini ya ukamanda wa Usamah; na pia umekiri kuondoka kwao kwenye jeshi hilo na kutokwenda kwenye safari hiyo.

Umekiri kwamba mambo yote haya kuwa ni mambo ya kweli kama vile tu wanahistoria, wasimuliaji wa hadithi na waandishi wa wasifu walivyoandikwa katika vitabu vyao na wakayakiri kwamba ni mambo ya kweli.

Na umesema kwamba masahaba wanasameheka kuhusu hili, hawafai kulaumiwa. Kiini cha yale uliyosema ni kwamba masahaba walipendelea kufanya masuala hayo kwa masilahi ya Uislamu kwa mujibu wa maoni yao badala ya yale aliyowaamrisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuyafanya. Na hiki ndio tulichokuwa tukithibitisha katika nyingi ya barua zetu zilizopita, mada ya msingi ya majadiliano yetu ilikuwa ni iwapo kama masahaba walitii amri za Mtume bila kuchagua au la. Ulishikilia maoni ya kwanza kwamba walitii kila amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambapo sisi tumechagua ya pili; kwamba hawakutii amri zake zote. Na sasa umekiri kwamba masahaba hao hawakutii amri zake za wazi katika masuala hayo hapo juu na hivyo umeangukia kwenye msimamo wetu na kuunga mkono uthibitisho wetu. Kuwa masahaba walikuwa wanasameheka kwa kutotekeleza amri zake au la, hilo kwa dhahiri liko nje ya mjadala wetu wa sasa.

Sasa umeridhishwa kwamba katika kadhia ya jeshi la Usamah, masahaba walifanya kile walichoona kwa uamuzi wao, badala ya kutii amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kwamba ni kwa masilahi ya Uislamu kuliko yale aliyoamrisha yeye. Basi kwa nini husemi vivyo hivyo kwamba katika suala la ukhalifa wa Mtume (s.a.w.w.) masahaba walifanya kile kilichokuwa ni kwa maslahi ya Uislamu kulingana na uamuzi wao kuliko kutii amri za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama zilivyoelezwa katika hadithi yake ya Ghadir na nyingine kama hizo? Umeeleza kwamba masahaba walipinga uteuzi wa Usamah kama Kamanda Mkuu wa jeshi kwa sababu ya umri wake mdogo, na umeeleza kwamba watu wenye umri mkubwa kwa

kawaida na kimaumbile huwa hawataki na hawakubali kuwa chini ya amri ya kijana mdogo. Kwa nini hutumii hoja hiyo hiyo kuhusu kuasi kwao na kutotii ile hadithi mashuhuri na tukufu ya Ghadir inayomtaja Ali (a.s.), ambaye alikuwa bado ni kijana, kwa ajili ya Ukhalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Kwa nini husemi kwamba masahaba waliokuwa na umri wa kati na wengine wazee hawakukubali uteuzi wa Ali (a.s.) kama Khalifa kwa sababu alikuwa ni kijana bado? Walipinga uteuzi wa Ali (a.s.) kama Khalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na mtawala wao wakati wa kifo cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), kama tu walivyopinga uteuzi wa Usamah wa Mtume (s.a.w.w.) alipomteuwa kama Kamanda wao katika jeshi na ofisa juu yao. Na kuna tofauti ya ukubwa wa dunia nzima kati ya ukhalifa na uongozi wa muda wa kikosi cha jeshi! Wakati hawakukubali kumtii kijana katika jambo moja la pekee licha ya amri za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), walikuwa na sababu nzito zaidi ya kutokukubali kuwa chini uongozi na kutii amri za kijana maishani mwao katika masuala yao yote ya dunia hii na ya Akhera.

Umeeleza kwamba nyoyo za watu wa umri wa kati na watu wazima kwa kawaida huchukizwa na kutii amri kutoka kwa vijana. Inaweza kuwa hivyo kwa baadhi au idadi kubwa ya masuala. Lakini sio ukweli ulioenea kote. Nyoyo za wale waaminifu hasa miongoni mwa watu walio na umri mkubwa hawachukii kumtii katika masuala yote, kijana ambaye kama utii kwake ni sawa na utii kwa Allah swt. na Mtume Wake:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا
يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

**"La! Naapa kwa Mola wako! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utakayotoa, na wanyenyekee kabisa.** (Qur'ani, 4:65)**."**

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا

"….. na anachowapeni Mtume kichukueni, na anachokukataza jiepushni nacho ….." (Qur'ani, 59:7)."

Maneno kuhusu wale waliotoka katika jeshi la Usamah, ambayo Allamah al-Shahristani ameyasimulia bila kutaja vyanzo vyake sio hadith huru isiyokuwa na wapokezi. Maneno hayo yanatokeza katika hadithi moja sahihi na mutawatir. Abu Bakr Ahmad ibn Abdul-Aziz al-Jawhari ameinukuu katika kitabu chake *Al-Saqifa*. Tunatoa hapa chini maelezo yake kuhusu jeshi la Usamah. Anasema:

"Ahmad ibn Ishaq ibn Saalih ametusimulia hadithi kutoka kwa Ahmad ibn Siyyar na yeye kutoka kwa Sa'id ibn Kathiir al-Ansari naye kutoka kwa watu wake walioisikia kutoka kwa Abdullah ibn Abdul-Rahman akisema kwamba wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) aliposhikwa na maradhi muda mfupi kabla ya kifo chake, alimteuwa Usamah ibn Zayd ibn Harithah kuchukua mamlaka ya Jemadari Mkuu wa jeshi ambamo waliorodheshwa Muhajirun na Answari wote mashuhuri, miongoni mwao walikuwa: Abu Bakr, Umar, Abu Ubaydah bin al-Jarrah, Abdul-Rahman ibn Awf, Talhah na Zubair na kadhalika. Alimuamuru Usamah kuvamia Mut'a, ambako baba yake, Zayd aliuliwa, na pia kuvamia bonde la Palestina. Usamah alionyesha dalili za kulegalega, ambako kuliwafanya wengine waliobaki katika jeshi kumuakisi.

Afya ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) wakati fulani ilionyesha dalili za kuboreka na wakati mwingine dalili za kuzidiwa vibaya. Hata hivyo aliendelea kusisitiza kuondoka kwa jeshi hilo haraka. Hatimaye Usamah akamwambia: "Ewe Mjumbe wa Allah! Wazazi wangu wawe fidia juu yako! Tafadhali niruhusu nibakie kwa muda siku chache mpaka Allah Aza wa Jallah atakapokuponya?" Mtume akajibu: 'Kaendelee na safari, Mwenyezi Mungu akubariki.' Usamah akasema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Kama nikiondoka na hali unaumwa kama hivyo, nitakwenda na moyo uliojaa maumivu.' Yeye (s.a.w.w.) akasema: 'Kaanze safari yako. Mwenyezi Mungu akusaidie na akujaalie ushindi!' Usamah akasisitiza: 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, itakuwa inanikera sana kuwauliza kila mara wasafiri kuhusu hali yako.' Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: 'Fanya kama nilivyokuamrisha.' Kisha yeye (s.a.w.w.), akashikwa na hali ya kuzimia na Usamah akaondoka mbele yake na akajitayarisha kuondoka. Wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipozindukana, mara moja aliuliza kuhusu kuanza kwa safari ya Usamah, na akaambiwa kwamba yeye na watu wake wanajitayarisha kuondoka. Akasema (s.a.w.w.): "Pelekeni jeshi la Usamah mara moja; Mwenyezi Mungu amlaani yule atakayekataa kwenda na jeshi la Usamah." Aliyarudia maneno hayo tena na tena mpaka hatimaye Usamah akautoka mji, bendera ikipepea juu ya kichwa chake, akiwa amezungukwa na masahaba. Walipofika Jurf akashuka na pamoja naye wakashuka Abu Bakr, Umar, na wengi katika Muhajirun, na Usaid bin Khuzair, Bashir bin Sa'd na wengine miongoni mwa Answari walio maarufu. Wakati huohuo akatokea mjumbe aliyetumwa na Umm Ayman ambaye alimtaka aharakishe kurudi mjini kwa sababu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa anakaribia kufa. Mara moja alirudi Madina pamoja na bendera yake ambayo aliikita mbele ya nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye alifariki kabla tu ya muda huo."

Hii imeandikwa na kundi la wanahistoria miongoni mwao akiwa ni Allamah Mu'tazili Ibn Abul-Hadid ambaye ameiandika mwishoni mwa ukurasa wa 20 na ukurasa uliofuatia katika Jz. 2 ya *Sharh Nahjul Balaghah*. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh**.

# BARUA YA 93

## RABI'UL AWWAL 23, 1330 A.H.

**Maombi ya Matukio Mengine ya Sahaba Kukiuka Amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).**

Mazungumzo yetu kuhusu suala la jeshi la Usamah yamekuwa marefu kama yale mazungumzo juu ya 'Msiba wa Alhamisi.' Ukweli sasa umedhihiri na uwongo umejitenga, na mwanga umewashukia wale wenye umaizi. Tafadhali sasa hebu natusikie kuhusu matukio mengine ambayo Masahaba walikiuka amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wassalam.

**Wako Mwaminifu, S.**

# BARUA YA 94

## RABI'UL AWWAL 25, 1330 A.H.

**Amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ya Kumuuwa Mhaini.**

Tafadhali ichunguze riwaya iliyoandikwa na kundi la wanachuoni mashuhuri na maimamu wa hadithi. Imamu Ahmad ibn Hanbal ameandika katika ukurasa wa 15, Jz. 3, ya *Musnad* yake hadith kutoka kwa Abu Sa'd al-Khudri akisema kwamba Abu Bakr siku moja alikuja kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na akasema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Nilikuwa napita katika lile bonde fulani nikamuona mtu mtanashati akiwa anaswali tena kwa hushui kubwa." Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akamuambia: "Nenda ukamuuwe mtu huyo." Hivyo Abu Bakr akaenda kule, na akamkuta mtu yule katika hali ile ya kuswali kwa heshima zote, hakutaka kumuuwa; kwa hiyo alirudi kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), bila kutekeleza amri yake. Mtume, (s.a.w.w.), akamuambia Umar, "Nenda ukamuuwe," na Umar akaenda kule na akamuona katika hali kama ile ile ambayo Abu Bakr alielezea, na yeye, pia akarudi bila kumuuwa mtu yule na akasema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Nimemkuta anaswali swala zake kwa makini sana; hivyo, niliona vibaya kumuuwa." Kisha Mtume (s.a.w.w.) akamuambia Ali: "Ali wewe nenda ukamuuwe," ambapo Ali alikwenda kwenye bonde lile lakini hakumkuta mtu yule hapo. Akarudi kwa Mtume (s.a.w.w.), na kusema: "Ewe Mjumbe wa Allah! Sikumkuta mtu huyo pale. Alikwishaondoka." Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Mtu huyo na rafiki zake wataisoma Qur'ani lakini haitashuka kwenye makoo yao [kupendeza tu watu]. Watapotoka kwenye imani kwa haraka kama mshale unavyotoka kwenye upinde, ambao hautarudi tena kwenye upinde. Wauweni hao, kwani ndio watu waovu kabisa miongoni mwa viumbe wote."

Katika *Musnad* yake, Abu Ya'la ameandika hadith kutoka kwa Anas ibn Malik kama ilivyoelezwa na Ibn Hajar katika kitabu chake *Isaba* katika maelezo juu ya Dhul-Thadya. Anas anasema kwamba: "Katika siku zile za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kulikuwa na mtu ambaye ibada zake za uchamungu na jitihada zake zilikuwa zinashangaza. Tulimuongelea na tukataja jina lake mbele ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), lakini hakumjua. Tulieleza alivyo kimaumbile lakini Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) bado hakumtambua. Tulikuwa bado tunazungumza kuhusu mtu huyo wakati alipotokeza mbele yetu na tukamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba huyu ndiye yule mtu tuliyekuwa tunamzungumzia. Yeye (s.a.w.w.) akasema: 'Mnanizungumzia kuhusu mtu ambaye shetani ameupaka rangi uso wake?' Mtu yule akaja mpaka akasimama mbele ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) lakini hakumsalimia, ambapo Mtume akamwambia: 'Apia kwa jina la Allah na unijulishe kama ni wewe ambaye wakati ulipokuwa katika swala ya jamaa ulijisemea: 'Hakuna mtu katika Umma wote aliye Mtukufu na bora kuliko mimi!?' Yule mtu akasema: 'Ndio Wallahi hakika nimesema,' kisha akaingia na akaanza nyuradi na dua zake. Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), akauliza ni nani atakayemuuwa mtu huyu? na Abu Bakr akasema "Mimi nitamuuwa." Wakati Abu Bakr alipomwendea, alimkuta mtu yule amejishughulisha katika swala. Hivyo akamwambia: "Mwenyezi Mungu ameepukana na mapungufu yote! Nitawezaje kumuuwa mtu ambaye anaswali?" Akarudi kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ambaye alimuuliza alichofanya, alijibu: 'Sikutaka kumuuwa wakati yuko kwenye swala, na wewe umetukataza tusiwauwe wale walioko kwenye swala.' Mtume akataka mwenye kujitolea na akauliza tena: "Nani atamuuwa mtu huyu? Wakati huu Umar akajitolea, Umar aliingia ndani na akamkuta mtu yule anasujudu, Umar akajisemea mwenyewe: 'Abu Bakr ni bora kuliko mimi; kwa nini mimi nimuuwe mtu huyu ambapo yeye hakumuuwa'? Akarudi kwa Mtume bila kumuuwa. Wakati

Mtume (s.a.w.w.) alipomuuliza kama ametekeleza amri yake. Umar alimuambia: ‘Nilimkuta mtu yule ameweka paji la uso wake juu ya ardhi akimsujudia Allah, hivyo sikutaka kumuuwa.’ Mtume (s.a.w.w.) akauliza mara nyingine. ‘Nani atamuuwa mtu huyu?’ Ali (a.s.) akajibu: ‘Mimi nitamuuwa.’ Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akasema: “Ndio, alimuradi ukimkuta.” Na wakati alipomwendea akakuta kwamba amekwishaondoka; hivyo, alirudi kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ambaye alimuuliza nini kimetokea na Ali (a.s.) akamwambia kwamba hakumkuta mtu yule, alikwishaondoka. Ilikuwa tena kwamba Mtume (s.a.w.w.) akasema: ‘Lau mtu huyu angeuawa, kusingekuwa na watu wawili miongoni mwa Umma wangu ambao wangetofautiana wenyewe kwa wenyewe.’”

Tukio hili limeandikwa na al-Hafiz Muhammad bin Musa al-Shirazi katika kitabu chake ambacho ni mkusanyiko wa fasili na matoleo kutoka kwenye tafsiri ya Qur’ani ya Ya’qub bin Sufyan, ya Maqatil bin Sulaiman, ya Yusuf ul Qattan, ya Qasim bin Salam, ya Maqatil bin Hiyan, ya Ali bin Harb, ya al-Sadi, ya Mujahid, ya Qatadah, ya Wakii, na ya Ibn Jariih. Idadi kubwa ya wanachuoni wategemezi wameipokea hadithi yenye usahihi usio na shaka bila kunukuu wasimulizi wake au vyanzo vyake. Imamu Shihabud-Din Ahmad, ambaye anajulikana zaidi kama Ibn ‘Abd Rabbih al-Andalusi, ameinukuu hadith hii mwishoni mwa mazungumzo yake kuhusiana na wale ambao hufuata matamanio yao wenyewe (*Ashab ul-Ahwaa*) katika jalada la kwanza la kitabu chake *Al-Iqd al-fariid*, na mwishoni mwa maelezo ya tukio hili ameongeza maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Hili ni pembe la kwanza (la shetani) linalochomoza kwenye Umma wangu. Lau mngemuuwa, hakuna watu wawili ambao wangetofautiana wenyewe kwa wenyewe. Wana wa Israil waligawanyika katika makundi sabini na mbili, na Umma wangu huu utagawanyika katika makundi sabini na tatu ambayo yote yatakwenda motoni isipokuwa moja”.[395]

Hadithi nyingine iliyo karibu na hii ni ile iliyosimuliwa na Ali (a.s.) na kuandikwa na waandishi wengi wa hadithi[396] ambao wanamuonesha Ali (as) akisema: “Baadhi ya watu kutoka Kuraishi walikuja kwa Mtume (s.a.w.w.) na wakasema: ‘Ewe Muhammad! Sisi ni jirani zako na washirika wenzako. Baadhi ya watumwa wetu wamekuja kwako si kwa kuipenda dini au kutaka kujifunza. Wamekuja kama wakimbizi baada ya kukwepa kulima ardhi zetu na kuwa wasimamizi wa bidhaa zetu. Hivyo, tafadhali warudishe kwetu.’” Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitaka maoni ya Abu Bakr: “Unasemaje kuhusu jambo hili?” na Abu Bakr akasema: “Wanachosema ni kweli. Hawa ni majirani zako,” Dalili za kuudhika zikajitokeza kwenye uso wa Mtume (s.a.w.w.). Kisha akamuuliza Umar: Unasema nini kuhusu hili.” Umar akasema: “Wanasema kweli. Hao ni jirani na wenzio.” Uso wake ukabadilika rangi tena kwa kuchukia na akawaambia Makuraishi: ‘Enyi watu wa Kureishi! Ninaapa Wallah! Mwenyezi Mungu atawateulia mtu ambaye imani na uaminifu wake Yeye amevijaribu. Ataipigilia dini katika vichwa vyenu.” Hapo Abu Bakr akauliza: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mtu huyo atakuwa ni mimi? Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akajibu “Hapana.” Kisha Umar akauliza: “Ewe Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)! Labda mtu huyo atakuwa ni mimi? Jibu lake lilikuwa ‘Hapana sio wewe, bali ni yule mtu anayerekebisha viatu.” Mtume (s.a.w.w.) alikuwa amempa Ali (a.s.) viatu vyake avishone. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[395] Madhehab kwa kiarabu maana yake ni *“Firqa”* neno alilotumia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na maneno ‘F*irqa*’ na *“Shi’ah”* kwa mujibu wa Jumal, yana thamani sawa ya kinumerali ya 385, ambayo kutokana nayo hiyo baadhi ya watu hupata hisia za Nyota njema kuliko neno ‘Firqa.’ (Madhehebu) maana yake ni ile madhehebu ya Shi’ah ambayo haitaingia Motoni.

[396] Huyo ni Imamu Ahmad bin Hanbal ambaye ameinukuu karibu na mwisho wa ukurasa wa 155, Jz. 1, ya *Musnad* yake. Sa’id bin Mansur katika *Tahdhiib ul Aathar* yake, Allamah al-Muttaqi al-Hindi ameithibitisha usahihi wake na amenakili kutoka kwao wote katika ukurasa wa 396, Jz. 6, ya kitabu chake *Kanz al-Ummal.*

# BARUA YA 95

## RABI'UL AWWAL 26, 1330 A.H.

**Kisingizio cha Kutokumuuwa Mhaini.**

Wao, Allah awe radhi nao, huenda walifikiri kwamba kuitekeleza amri hiyo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ya kumuuwa mhaini huyo ilikuwa ni pendekezo tu na sio ya wajibu, na hii ndio sababu ya kwa nini hawakumuuwa mtu huyo. Au pengine walifikiri kwamba kumuuwa kulikuwa ni '*Wajib al-Kifaya*' (wajibu unaotosheleza hata kwa mtu mmoja tu kwa niaba ya jamii). Hivyo walijizuia kumuua kwa kuamini kwamba sahaba mwingine wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) atakuja kumuua nao watajumuika kwenye wajibu wa kumuua. Na pale Abu Bakr na Umar waliporudi bila ya kumuua, hawakuwa na sababu ya kuhofia kwamba ile amri ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ya kumuuwa mhaini huyo ingeweza kupita bila kutiiwa kwa sababu ya kutoweka mtu huyo kwenye sehemu hiyo, kwa sababu walikuwa hawakumjulisha juu ya kazi ambayo iliwapeleka kwake. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 96

## RABI'UL AWWAL 29, 1330 A.H.

**Kupingwa kwa Kisingizio.**

Amri kwa kweli ni wajibu, na kutokana na amri hakuna kinacho gonga kwenye akili ya mtu yeyote mbali na kuelewa kuwa ni wajibu wa lazima.  Na ni makosa kuchukulia utekelezaji wa amri kwamba ni pendekezo la kufaa tu, isipokuwa labda kuwe na maelezo au mazingira ya ziada yanayoonyesha kwamba ni ya pendekezo tu. Lakini hakuna maelezo wala mazingira ya nyongeza katika suala hili yanayoonyesha kwamba ni pendekezo linalofaa tu. Kwa upande mwingine, mazingira na maelezo ya ziada katika suala hili yanaashiria kwamba amri ya kuua ilikuwa katika maana yake halisi, na kwamba kutekeleza amri hiyo kulikuwa ni wajibu wa lazima na sio pendekezo la kufaa tu au wajibu wenye kutosheleza '*wajib al-Kifaya*.' Kwa kuangalia kwa uangalifu hadithi hiyo utagundua ukweli wa kile tunachokisema. Tafadhali rejea tena kauli ya Mtume (s.a.w.w.): "Mtu huyo na rafiki zake wataisoma Qur'ani lakini haitashuka kwenye makoo yao [kupendeza tu watu]. Watapotoka kwenye imani kwa haraka kama mshale unavyotoka kwenye upinde, ambao hautarudi tena kwenye upinde. Wauweni hao, kwani ndio watu waovu kabisa miongoni mwa viumbe wote." Na vilevile kauli yake, (s.a.w.w.): "Lau angeuawa, kusingekuwa na watu wawili miongoni mwa Umma wangu ambao wangetofautiana wenyewe kwa wenyewe." Baada ya kauli hizo na ule uhimizaji wenye msisitizo mkubwa wa kumuuawa mhaini huyo, hakuna mtu anayeweza kufikiri kwamba utekelezwaji wa amri hiyo haukuwa ni wajibu wa lazima.

Kama utarejea hadithi hii hii kwenye *Musnad* ya Ahmad Hanbal, utaona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimgeukia Abu Bakr akamuamuru yeye mahususi kumuuwa mhaini yule. Aliporejea bila kumuuwa, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimuamuru mahususi Umar kwenda kumuua mtu huyo. Wakati mtu anapoamrishwa mahususi kufanya jambo fulani, ni vipi utekelezaji wa amri hiyo uchukuliwe kama ni wajibu unaotosheleza kufanywa na mtu mmoja yoyote kwa niaba ya jamii (*wajib al-kifaya*)?

Isitoshe iko wazi kutokana na hadithi hii kwamba Abu Bakr na Umar waliepuka kumuuwa mhaini yule kule bondeni sio kwa sababu nyingine mbali na ile ya kwamba alikuwa anashughulika na swala na maombi kwa unyenyekevu sana. Hivyo hawakutaka kumuuwa ingawa Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe alitaka na akaamuru kuuawa kwa mtu yule licha ya kushughulika kwake na swala. Hawakuchagua kufanya kama walivyoamrishwa.

Kwa hiyo, hili ni moja ya matukio yanayothibitisha kwamba masahaba walipendelea kufanya mambo kulingana na maoni na maamuzi yao wenyewe kuliko kutii maagizo ya wazi ya Mtume (s.a.w.w.) ambayo kwao wao hayakuwa na uzito wowote kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 97

## RABI'UL AWWAL 30, 1330 A.H.

**Maombi ya Kadhia Zote Ambamo Masahaba Walikaidi Amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).**

Tafadhali simulia hadithi zote zilizobakia za matukio ambamo masahaba walikaidi amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Tafadhali usiache hata moja hata kama itachukua mlolongo mrefu kuzieleza zote, ili kwamba tusije kuomba hadithi nyingine tena. Wassalam

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 98

## RABI'UL THANI 1, 1330 A.H.

**I. Dokezo Kwenye Baadhi ya Matukio Ambamo Masahaba Hawakutekeleza Amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.),**

**II. Kugusia Matukio Mengine ya Masahaba Kutenda Kulingana na Maamuzi yao Binafsi Kuliko Kutii Amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).**

Kwa mujibu wa matakwa yako ya kutaka kujua matukio mengine ambamo humo masahaba walipuuza au kupinga amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Nakurejesha kwenye mkataba wa Hudaybiya, mgawanyo wa ngawira ya vita vya Hunayn, uchukuaji wa fidia kutoka kwa mateka wa vita vya Badr. Walitofautiana na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au kumpinga katika kadhia hizi. Wakati kulipokuwa na upungufu mkubwa wa chakula wakati wa Vita vya Tabuk na watu wake wakawa na njaa Mtukufu Mtume(s.a.w.w.) aliamuru wachinjwe ngamia wachache ambapo wao wakampinga. Kwenye vita vya Uhud walikaidi maelekezo ya wazi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Siku ya Abu Hurayra wakati alipotangaza habari njema kwa wale wote watakaofika mbele za Mwenyezi Mungu kama waumini katika *Tawhiid* ya Allah, na pia katika ile siku ya kumswalia mnafiki swala ya jeneza. Walishutumu ugawaji wake wa *sadakat* na wakadai mgao mkubwa kuliko wanavyostahili. Walimpinga kwa tafsiri potofu ya aya kuhusu *Khums* (Moja ya tano ya mapato ya mwaka kama fungu la Mtukufu Mtume na kizazi chake) na *Zakat,* na aya kuhusu *mut'a* mbili [ndoa ya muda – *Mut'a ul-Nisa*; na *Mut'a ul-Hajj*], na aya kuhusu talaka tatu, tafsiri potofu juu ya hadithi zinazohusu swala za Sunnah katika mwezi wa Ramadhani na namna ya kuziswali na idadi ya rakaa zake, na kwa kubadilisha muundo wa Adhana, idadi ya takibira wakati wa swala ya jeneza.

Matukio ya masahaba kupinga au kupuuza amri na maagizo ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) orodha yake ni ndefu sana kuweza kushughulikiwa hapa, kama hili la upinzani wao kuhusiana na suala linalofungamana na Hatib bin Balta'ah, upinzani wao kwa kile alichofanya Mtume (s.a.w.w.) kwenye *Maqam* Ibrahim ndani ya Ka'ba, kutwaa nyumba za baadhi ya Waislamu kuziingiza msikitini, kutokubaliana na uamuzi wake kuhusiana na fidia ya damu ya Abu Kharash al-Hadhliy kulipwa na watu wa Yemen, kufukuzwa [mjini] kwa Nasr bin al-Hajjaj al-Salmi, na kumuadhibu Ja'dah bin Saliim,[397] kukadiria kodi juu ya sehemu za malisho ya Umma, kubadilisha amri ya *Jizya* (kodi inayolipwa na wasiokuwa Waislam kwa ajili ya kupata ulinzi), kuamua suala la Ukhalifa kwa ushauriano (*shura*), kuweka ulinzi usiku, kupeleleza na kujaribu kujua siri za wengine, dhulma na uonevu katika suala la urithi. Kuna orodha ndefu ya masuala mengi ambayo kwayo masahaba walipuuza au kukaidi amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kutenda kwa mujibu wa maamuzi yao binafsi, mabavu au ushawishi kwa faida zao wenyewe ama kwa maslahi ya jamii. Tumetenga Mlango mzima kwenye kitabu chetu *Sabiil al-Mu'minin*[398] kwa ajili ya kushughulika na maudhui hii.

Mbali na matukio tuliyoyarejea hapo juu, hata hivyo, bado kuna matukio mengi mengine ya masahaba kutokutekeleza amri na hadith za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hususan zile zinazomhusu Amirul-Mu'minin

[397] Rejea kwenye maelezo juu ya Umar katika *Tabaqat* ya Ibn Sa'd na utaona kwamba alimuadhibu Ja'dah ambaye alishutumiwa kwa uzinifu na Warda peke yake bila ya shahidi wala ushahidi wowote. Mshairi ambaye hakutajwa jina aliandika beti za shairi juu ya "Shutuma za Uzinzi dhidi ya Ja'dah" ambazo zimeandikwa katika *Tabaqat*.

[398] Kama hukupata bahati ya kusoma *Sabil al-Muminin,* jitahidi usikose kusoma *Al-Fusul al-Muhimma*, kwani ina manfaa yene thamani ambayo hakuna kitabu kingine kilicho nayo. Tumetoa sura nzima kwa wale ambao wanaoitarjuma; ni Sura ya 8, ukurasa wa 44-130 wa toleo la pili, ambako masuala hayo yanaelezewa kwa urefu.

Ali na kizazi kitoharifu (as) mbali na zile hadithi kuhusu Ukhalifa wake na, kama ambavyo wanachuoni watafiti walivyogundua, walikwenda kinyume na hadithi zake. Wakati ambapo hawakutii amri zake na wakatenda kinyume na hadithi zake waziwazi zinazohusu urithi wake, hivyo hakuna cha kushangaza kuona kwamba, ama walipinga au kuzipuuza kabisa riwaya za fadhila za Ali na wanawe. Walitoa tafsiri potofu juu ya hadith kama hizo na wakatenda mambo kulingana na maamuzi yao kuliko kumtii Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kukubaliana na hadithi zake, kama vile ambavyo wametoa tafsiri potofu kwenye hadith kuhusu urithi wake na wakafanya mambo kuhusiana na maamuzi yao kuliko kutii amri na hadithi zake. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 99

## RABI'UL THANI 5, 1330 A.H.

**I. Katika Matukio Hayo Walipendelea Kufanya kile Kilichokuwa ni kwa Masilahi ya Umma,**

**II. Maombi ya Matukio Yaliyobaki.**

Mtu yeyote aliyejaaliwa busara hawezi kuwa na wasiwasi kwamba mifano yote hii masahaba walifanya kwa nia zao na kama wametenda kulingana na maamuzi yao na kupuuza amri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa ni kwa nia ya kufanya ambalo kwa maoni yao lilikuwa ni kwa masilahi ya Umma. Nia zao katika matukio yote hayo zilikuwa ni kwa yale waliyofikiria kwamba yalikuwa ni kwa faida au ya kuutengeza vizuri zaidi Umma wa Kiislam na kwa ajili ya nguvu zake. Hivyo kulikuwa hakuna madhara katika kile walichotenda. Kama wamefuata amri na hadith zake au wametoa tafsiri potofu katika hizo au kuzipuuza, hilo halina maana ya msingi.

Tulikuomba uchukue usumbufu wa kutusimulia matukio yote ya masahaba kutotii au kupuuza amri na hadithi za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Umesimulia idadi kubwa ya hadith kama hizo. Mwishoni mwa barua yako umeeleza kwamba mbali na Hadith ya Ghadiir kuhusu Ukhalifa wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) masahaba walichagua kutenda katika masuala mengi kulingana na maamuzi yao wenyewe kuliko kukubaliana na hadith za wazi za yanayomhusu Imamu Ali na kizazi chake (a.s.). Tunaomba tafadhali ututajie hizo hadith ambazo ni kwa fadhila ya Ali na kizazi chake ambazo masahaba walikataa kuzitii au walizipuuzia. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 100

## RABI'UL THANI 8, 1330 A.H.

**I. Masahaba Hata Wawe Wametenda kwa nia na Azma Njema, Hilo Liko Nje ya Mada ya Mjadala,**

**II. Kukubali Maombi.**

Umekiri kwamba katika masuala yote tuliyoorodhesha hapo juu masahaba walikiuka amri za wazi na hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na hivyo umethibitisha kile tulichosema. Shukurani zote zinamstahikia Mwenyezi Mungu! Kwamba walitenda kwa nia njema au laa, na kwamba kutokutii au kupuuza kwao amri na hadith zake kulichochewa na shauku yao juu ya ustawi wa jamii au kwa kupenda kwao marekebisho na utengenezaji wa Umma na kuimarisha nguvu yake, au kwa sababu yoyote ile iwayo, kama unavyojua wewe vizuri tu, huku ni kutoka nje ya mada yetu iliyoko kwenye mjadala sasa hivi.

Katika barua yako ya mwisho, umeomba kuorodhesha hadithi sahihi zinazomhusu hasa Ali (a.s.) mbali na hadithi kuhusiana na Uimamu wake ambazo masahaba walizipuuza au hawakuzitii. Wewe ni Imamu wa hadithi unayeongoza katika zama zetu. Umehangaika sana na kufanya utafiti mpana na wa maana sana kwa ukusanyaji na uchunguzaji wa hadithi. Hakuna mtu yoyote anayeweza, kwa busara kabisa, kufikiri kwamba anajua zaidi kuliko wewe katika yale maelezo ya kile tulichokitaja kwa ufupi au anayeweza kufanya vipimo kwenye yale tuliyodokeza. Je, kuna yeyote anayeweza kushindana na wewe au kupingana na elimu yako mahiri ya Sunnah? Hakika hakuna; bali suala ni kama usemi usemavyo: "watu huuliza kuhusu mambo fulani licha ya kwamba wana ujuzi nayo."

Unajua kwa hakika kwamba kuna masahaba wengi sana walimchukia Ali na walikuwa maadui zake. Walimtelekeza, wakamsumbua, walimkashifu, wakamtukana na kumuonea, wakahasimiana naye na wakapigana dhidi yake. Walichomoa panga zao juu yake na juu ya Ahlul-Bayt wake halikadhalika na kwa wafuasi wao, kama inavyotokeza kutoka kwenye uchunguzi wa wasifu zao na historia ya nyakati zao.

Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) amesema: "Yeyote mwenye kunitii mimi amemtii Allah, na yeyote mwenye kuniasi mimi anamuasi Allah; yeyote yule anayemtii Ali amenitii mimi, na yeyote asiyemtii Ali hanitii mimi pia."

Na amesema pia: "Yeyote mwenye kujitenga nami amejitenga na Allah, na ewe Ali! mwenye kujitenga na wewe, amejitenga na mimi pia."

Na amesema pia: "Ewe Ali! Wewe ni kiongozi katika dunia hii na ni kiongozi katika Akhera; nampenda yeyote mwenye kukupenda wewe, na ninayempenda mimi anapendwa na Allah; adui yako ni adui yangu, na adui yangu mimi ni adui wa Allah; ole wake yeyote mwenye kukuchukia wewe baada yangu."

Na amesema pia: "Yeyote mwenye kumtukana Ali ananitukana mimi pia, na yeyote mwenye kunitukana mimi anamtukana Allah."

Na amesema pia: "Yeyote mwenye kumuudhi Ali ananiudhi mimi, na yeyote mwenye kuniudhi mimi anamuudhi Allah."

Na amesema pia: "Yeyote mwenye kumpenda Ali ananipenda mimi, na yeyote mwenye kumchukia Ali ananichukia mimi."

Na amesema pia: "Ewe Ali! Hakuna atakayekupenda, isipokuwa ni muumini wa kweli, na hakuna atakayekuchukia wewe isipokuwa ni Mnafiki."

Na amesema pia: "Ewe Allah! kuwa rafiki kwa mwenye kuwa rafiki naye, na adui kwa mwenye uadui juu yake; msaidie yeyote mwenye kumsaidie yeye, na mtelekeze yeyote mwenye kumtelekeza yeye."

Siku moja yeye (s.a.w.w.), alimwangalia Ali, Fatima, Hasan na Husein (a.s.) na akasema: "Niko kwenye hali ya kupigana na yeyote yule mwenye kupigana na ninyi, na niko kwenye hali ya amani na yeyote aliyeko kwenye amani na ninyi." Akiwa amewafunika na shuka, yeye (s.a.w.w.) alisema: "niko katika hali ya mapigano na yeyote mwenye kupigana na hawa na kwenye amani na yeyote mwenye amani nao; mimi ni adui wa yule ambaye ni adui yao." Kuna hadithi nyingine nyingi kama hizi ambazo masahaba wengi kabisa hawakuzitekeleza. Kwa upande mwingine, masahaba hao walitenda kinyume na hadithi na wakapendelea kutimiza matamanio yao wenyewe na walitafuta kukamilisha malengo yao ya kilafi.

Wale ambao wana elimu na utambuzi makini wanajua kwamba semi na hadithi zote mashuhuri za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zenye kumsifia Ali ambazo zinazidi mamia kadhaa kwa idadi, ni sawa na zile riwaya za wazi zinazoamrisha Umma mapenzi na utii kwake kama wajibu wa lazima, au zinazokataza uadui juu yake, na riwaya zote hizi ziwe za urafiki au uadui juu yake zinaonyesha thamani yake kuu, cheo chake kikubwa na hadhi yake ya juu, na kwenye nafasi yake ya juu mbele ya macho ya Allah na Mjumbe Wake.

Tumesimulia idadi kubwa kati ya hizo katika barua zetu zilizopita, na kuna riwaya nyingine nyingi ambazo hazikusimuliwa. Na sifa zote njema ni zake Allah! Wewe ni miongoni mwa wale ambao wana ujuzi mkubwa wa hadithi na riwaya za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na umezichunguza kwa kina maana zake na kuhusika kwake. Je, umekutana na hadithi yoyote japo moja ambayo inaamrisha hasama ya Umma kwake na kupigana dhidi ya Ali (a.s.), au inayoruhusu kumdhuru au chuki na uadui dhidi yake yeye, au inayoruhusu ukandamizaji na ukatili juu yake yeye, au kumtukana yeye kutoka kwenye mimbari za Misikiti ya Waislamu, na si hivyo tu bali pia kuieleza kwamba ni jambo linalopendekezwa na lenye malipo huko Akhera kwa makhatibu wa swala za Ijumaa na Iddi mbili? Hakika jibu lako litakuwa ni hapana. Lakini ukweli ni kwamba wale masahaba (ambao waligeuka kuwa maadui wa Ali, waliopigana dhidi yake, waliokuwa na uhasama, ukandamizaji na waliomtukana) hawakuzingatia chochote kwenye hadithi hizo licha ya wingi wake na usimuliaji wa mfululizo. Hakuna yoyote iliyowazuia kutekeleza na kufanikisha malengo yao ya kisiasa. Masahaba hao walijua kwamba Ali alikuwa ni ndugu na rafiki wa Mtume (s.a.w.w.), mrithi na msiri wake, kiongozi wa kizazi chake, Haarun wake juu ya umma wake, pekee anayelingana na sehemu muhimu ya mwili wake (yaani binti yake Fatimah), baba wa watoto wake, Mwislamu wa kwanza, mnyofu mno katika dini kati yao, mjuzi zaidi yao, mwenye nguvu zaidi kuliko wao katika uchamungu, mwenye subira mno kuliko wao, mwenye nguvu sana kati yao katika imani, mwenye bidii zaidi katika shughuli za Uislam, mwenye moyo thabiti katika kukabiliana na matatizo, mwenye kustahiki sifa mno zaidi kati yao, wa mbele zaidi kwa ubora kuliko wao, mlinzi makini wa Uislamu, ndugu wa karibu sana kwa Mjumbe wa Allah, mwenye kufanana kwa karibu sana na Mtume (s.a.w.w.) katika mwongozo, tabia, na mwenendo wa maisha, na kigezo bayana kabisa cha kuigwa katika vitendo na maneno, na ukimya…

Lakini sababu za ulafi wao wa masilahi binafsi zilishinda juu ya hoja nyingine yoyote. hivyo, haishangazi kwamba katika suala la Uimam walipendelea kufanya kulingana na maoni yao binafsi kuliko kutii hadithi ya wazi na dhahiri ya Ghadiir. Na, hadithi ya Ghadir ni moja tu katika mamia mengi mengine ya hadith Tukufu ambazo wamezitolea tafsiri potofu, na wakapendelea kutenda kulingana na hiari na maamuzi yao na kulingana na masilahi yao kuliko kuzitii riwaya na hadith hizo. Maslahi yao binafsi yalikuwa na

uzito zaidi kuliko hadith za Mtukufu Mtume wao (s.a.w.w.). Na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alikuwa amesema: "Nawaachieni vizito viwili miongoni mwenu. Kama mtashikamana navyo vyote hamtapotea kamwe kwenye njia iliyonyooka, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, Ahlul-Bayt wangu. Na amesema vile vile: "Mfano wa Ahlul-Bayt wangu miongoni mwenu ni kama ule wa Safina ya Nuh; mwenye kuingia humo ameokolewa, na mwenye kuipa mgongo ameangamizwa," na "Mfano wa Ahlul-Bayt wangu miongoni mwenu ni kama ule wa Lango la wokovu (*Babe Hitta*) kwa Wana wa Israil wenye kuingia kupitia humo husamehewa dhambi zake." Yeye (s.a.w.w.) vilevile amesema: "Nyota ni chanzo cha usalama wa wakazi wa ardhini dhidi ya kupotea njia, na Ahlul-Bayt wangu ni chanzo cha usalama wa Umma wangu dhidi ya mfarakano na upotofu; hivyo, kama kabila lolote la Kiarabu likiwapinga wao, au kutowatii Ahlul-Bayt wangu watageuka kuwa kundi la shetani." Kuna hadthi nyingi sahihi kama hizi ambazo zote hazikutiiwa kabisa au kufuatwa na masahaba… wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 101

## RABI'UL THANI 10, 1330 A.H.

**Kwa nini Imamu Hakumpinga Abu Bakr na Wafuasi wake Dhidi ya Kuchaguliwa na Kula Kiapo Kwake Huko Saqifa kwa Msingi wa Hadithi Yoyote ya Wazi Inayohusu Ukhalifa na Urithi Wake?**

Ukweli umedhihiri kabisa sasa. Shukuran zote ni zake Allah, Mola wa walimwengu! Kumebakia suala moja tu la mwisho sasa kuelezewa, ambalo umelipita na kuliacha halijatamkwa. Nalitaja hilo ili uweze kuondoa pazia na kufanya siri yake ijulikane. Na hili ni kwamba, Imamu hakumpinga Siddiq (mkweli, yaani Abu Bakr) wakati wa siku ya Saqifa pamoja na wale waliochukua kiapo cha utii kwake, na hakutaja riwaya yoyote kati ya zile za dhahiri kuhusiana na ukhalifa na urithi wake kama hoja, riwaya ambazo ninyi mmezishikilia. Je, ninyi ni wajuzi wa makusudio ya riwaya hizo kuliko yeye? Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 102

## RABI'UL THANI 11, 1330 A.H.

**I. Sababu ya kwa nini Imamu Hakupinga Mnamo Siku ya Saqifa,**

**II. Dokezo Fupi la Upinzani wake na ule Upinzani wa Wafuasi wake na Vikwazo Katika Njia yao.**

Kila mtu anajua kwamba si Imamu wala yeyote katika wafuasi wake miongoni mwa kizazi cha Hashim na wengine walioshuhudia kiapo hicho kwa Abu Bakr. Hakuna yeyote aliyeingia katika ukumbi huo wa Saqifa siku hiyo. Walijitenga mbali na wale waliokusanyika ndani ya Saqifah na shughuli zake. Walikuwa wameshughulishwa sana na ule msiba mkubwa uliowapata wa kifo cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Walikuwa wanashugulika kusimamia matayarisho muhimu ya josho la maiti na sanda na mazishi ya Mtume (s.a.w.w.). Hawakuzingatia kitu kingine chochote zaidi. Wakati mwili wake Mtukufu ulipokwisha kuzikwa katika kaburi lake tukufu, wale waliokuwa Saqifa walikuwa tayari wamekwishamaliza uchaguzi wa khalifa, na ili kufanya kiapo cha utii kwa Abu Bakr kuthibitishwa na mkataba wa kiapo hicho kuidhinishwa, wao wakaungana na kudhamiria kuzuia mazungumzo yote au vitendo vyovyote ambavyo vingeweza kudhoofisha au kuharibu kiapo hicho, au kuvunja mkataba wao, au kusababisha vurugu katika fikra za Umma. Imam angeweza vipi katika mazingira kama hayo kuleta upinzani siku ile dhidi ya kilichotokea ndani ya Saqifah kiapo cha utii kwa Siddiq na wale waliokula kiapo kwake? Pengine unasahau kwamba ilikuwa haiwezekani kwa Imam au yeyote kati ya wafuasi wake kufanya upinzani baada ya kiapo cha utii kuchukuliwa kwa Abu Bakr na watu wenye ushawishi [katika hilo] katika kundi lenye mamlaka, na tayari marafiki na wafuasi wao wamechukua hatua zote za tahadhari na wamekimbilia kutumia nguvu na ukatili, au kuzuia shutuma zozote zisizopendeza juu ya mpango huo mpya na upinzani wowote kwa kundi lenye mamlaka. Je, itakuwa ni rahisi kwa mtu yeyote katika zama hizi kuipinga serikali na kukiondoa chama tawala kwenye madaraka? Je, hilo kundi la watawala litamuacha mtu huyo atimize malengo yake bila kipingamizi au vikwazo? Haiwezekani kabisa. Kundi linalotawala litafanya kila kitu kuzuia mishughuliko yake na kutwaa mali yake na litamtupa yeye na wafuasi wake ndani ya gereza au kuwahukumu kunyongwa. Ali (a.s.) na wafuasi wake wangepatishwa kila aina ya ushurutishwaji na mabavu na hata kunyongwa kama wangefanya mgomo wowote ule baada ya kuthibitishwa kiapo kwa Abu Bakr, kwani tabia ya wanadamu wakati wote na mahali pote huwa ni hiyohiyo, haibadiliki.

Bado Ali (a.s.) alijua kwamba upinzani wake wakati wa hatua kama hiyo ungesababisha kuenea kwa vurugu, mfarakano na maasi. Hivyo alipendelea kuona maslahi yake binafsi yakitolewa muhanga badala ya kuona Umma ukisambaratika na 'Neno la Imani' (Tamko la kuamini upweke wa Allah na utume wa Muhammad (s.a.w.w.)) kusahaulika kama tulivyoeleza katika barua yetu iliyopita, kwamba wakati huo alikuwa anapitiwa na msukosuko mgumu kabisa ambao haujapata kupitiwa na mtu mwingine tena. Alikuwa na mizigo miwili mizito juu ya mabega yake. Upande mmoja, anasikia sauti ikimwita kwenye ukhalifa kupitia hadithi zote za wazi, riwaya na wosia wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), sauti iliyokuwa inaufanya moyo utokwe na damu na ini lake kudunda. Na kwa upande mwingine kulikuwa ni wimbi kali la machafuko yaliyokuwa yanatishia kupotea kwa rasi yote ya Arabia, uwezekano wa mapinduzi makubwa katika nchi na kuangushwa kwa Uislamu na wanafiki wa Madina, ambao walikuwa ndio "Mashupavu zaidi katika Unafiki" (9:10(1) miongoni mwa wakazi wa vitongoji vya Madina ambao Qur'ani imewataja kama ni wanafiki kwa mujibu wa maneno ya Kitabu cha Allah:

الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا حُدُودَ مَا أَنزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ

**"Mabedui wamezidi sana katika kufuru na unafiki na wameelekea zaidi kutojua mipaka ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume….."** (9:97)**.**

Hawa wamekuwa na nguvu kwa kuondoka Mtume (s.a.w.w.), wakati Waislamu walipokuwa kama mifugo iliyotishwa katika usiku wa kipupwe, wakizungukwa na mbweha na wanyama wakali wa porini. Na kulikuwa na Musailamatul-Kadhab, Tulayha ibn Khuwailid ul-Affak na Sajah bint wa al-Harath ud-Dajalah na wafuasi wao waovu na wakatili ambao walikuwa wamejitolea kwa kila liwezekanalo kuufuta Uislamu na kuwasaga Waislamu. Na Waroma, wafuasi wa Kisra na Caesar, mbali na wengine wengi, walikuwa wamejificha ili kuwavamia Waislamu na kuuangamiza Uislam. Kulikuwa na makundi mengine mengi ambayo yalikuwa maadui wakubwa wa Muhammad (s.a.w.w.), kizazi chake na masahaba zake wa kweli, na yalikuwa na chuki na uovu dhidi ya Uislamu na yalikuwa yamedhamiria kung'oa mizizi ya Uislamu. Wote hawa walikuwa wamejiandaa kikamilifu na shauku kubwa ya kupigana vita dhidi ya Waislam. Waliuchukulia kwamba ni muda muafaka wa kukamilisha malengo yao maovu, na kwamba ni fursa nzuri iliyoletwa na kufariki kwa Mtume (s.a.w.w.). Muda umewadia kwa ajili yao na walinuia kutumia fursa hiyo kabla ya kwisha kwa vurugu na ghasia zilizokuwepo katika kundi la Waislam na kurejea kwa umadhubuti wa Uislam na nguvu mpya ya sheria na taratibu. Ali (a.s.) alikuwa na hatari mbadala mbili tu, ama kuvumilia kunyimwa haki yake ya Ukhalifa, yaani kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au akabiliane na kuangamia kwa Uislamu na Waislam, matunda ya kazi ngumu ya uhai mzima wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Yeye kwa kawaida kabisa alipendelea kuona haki yake binafsi ikitolewa muhanga ili kwamba Uislam, ambao ulikuwa na thamani sana kwake kuliko uhai, na Waislam waweze kuishi na kujitahidi.[399] Lakini ili kuhifadhi haki yake kwenye Ukhalifa na haki ya upinzani dhidi ya wale waliogeukia mbali na yeye, alielezea utaratibu wa harakati ambao utazuia mgawanyiko wowote miongoni mwa Waislamu, na kuzuia vurugu na uasi miongoni mwao, ambao utadhoofisha Umma na kuwachochea maadui wake kuchukua fursa ya hali hiyo ya machafuko. Kwa hiyo, alibakia nyumbani kwake na alitoka nje tu pale watu walipomshinikiza kutoka nyumbani bila mapigano. Uamuzi wa haraka haraka usingempatia upinzani wowote dhidi ya wale waliokuwa wapinzani wake au waliomgeuka, na usingewapa wafuasi wake hoja isiyopingika ya kuwa kwake mrithi halali na wa haki ambaye alishikilia manufaa ya Uislam kuwa yenye thamani zaidi kuliko maslahi yake binafsi hata katika mazingira magumu kiasi gani. Kwa kitendo chake hicho, aliulinda Uislam na pia kuihifadhi haki yake mwenyewe ya kutawala juu ya Wasilamu. Wakati alipoona kwamba ulinzi wa Uislamu na kuwashinda maadui wake wakati huo ulitegemea juu ya utakia heri na maelewano na kundi tawala, alijiandalia yeye mwenyewe njia ya heri na kwa maslahi ya usalama wa Uislam, ulinzi wa Umma na kwa mapenzi ya dini, alipendelea mustakbali wa baadae kuliko wakati huo, na kutoa kipaumbele kwa lile ambalo kisheria na kimantiki lilikuwa na mkazo zaidi na wajibu muhimu, alifanya maelewano na kundi linalotawala. Kwani kwa wakati ule, upinzani wa silaha wala wa maneno ulikuwa haustahili na haushauriwi.

[399] Yeye, Ali (as), alitamka hivyo katika barua ambayo aliipeleka kwa watu wa Misri iliyokabidhiwa kwa Malik al-Ashtar wakati alipompa ugavana. Alisema (kwenye barua hiyo): "Shukurani zote anastahiki Allah, amemtuma Muhammad (s.a.w.w.) kama dalili na muonyaji kwa walimwengu na bwana wa Mitume wote. Wakati yeye (s.a.w.w.) alipoutoka ulimwengu huu, Waislamu walizozana miongoni mwao juu ya uongozi yaani Khalifa baada yake. Wallahi, kilichotokea akilini mwangu ni kwamba baada ya Mtume (s.a.w.w.) Waarabu watainyanyasa Ahlul Bayt yake kwa sababu ya Ukhalifa wao (a.s.), na kwamba baada yake watanigeuka na kunikimbia. Hakuna kilichonitisha mimi zaidi isipokuwa ni kuelekea kwao kwa mtu yule na kula kiapo cha utii kwake; hivyo, nilijizuia mpaka nilipowaona watu wanaondoka kwenye Uislamu na kuwalingania wengine kwenye kuifuta dini ya Muhammad. Kwa hiyo, mimi nikaogopa kwamba kama sikuusaidia Uislamu na Waislamu, itakuwa nimeshindwa katika wajibu wangu, wakati nimeshuhudia mfumo wa Uislamu unapasuka au kuvunjwa, ambapo ilikuwa ni msiba mkubwa kwangu kuliko kuikosa serikali yenu ambayo si chochote bali furaha ya muda mfupi ambayo baada yake itatoweka kama mazigazi, au kutoweka kama mawingu ya kiangazi. Nilikuwa katika mazingira hayo mpaka uhalifu ukaondolewa, na dini ikajikita kwa kina na ikatulia……." Kwa barua hii rejea kwenye *Nahjul Balaghah*.

Licha ya yote haya, Ali mwenyewe na kizazi chake (a.s.), na wasomi miongoni mwa wafuasi wake, kwa busara sana walitaja urithi wake kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kila wakati uliofaa, na waliandaa utangazaji mpana lakini kwa tahadhari sana, wa hadithi zote za wazi na muhimu, za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zinazomtaja Ali kama kiongozi na Khalifa kama ambavyo wanachuoni watafiti wanavyotambua vyema. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 103

## RABI'UL THANI 12, 1330 A.H.

**Ni Lini Ali na Wafuasi wake Walifanya Malalamiko?**

Ni lini Imamu Ali (a.s.) alifanya malalamiko dhidi ya wale waliomnyang'anya haki yake ya kumrithi Mtume (s.a.w.w.)? Na lini wamefanya hivyo kizazi chake na wafuasi wake? Tafadhali tujuvye tufahamu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 104

## RABI'UL THANI 15, 1330 A.H.

**I. Idadi Kubwa ya Matukio ya Upinzani wa Imamu na Wafuasi wake,**

**II. Malalamiko ya Zahra (as).**

Imamu alikuwa makini kabisa katika kutangaza hadithi zote na riwaya za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na urithi wake yeye. Bali aliepuka kwa uangalifu sana mizozo yoyote na maadui zake kwa ajili ya ulinzi wa Uislamu na usalama wa Waislam na kwa umadhubuti na sifa ya serikali. Mara kwa mara alikuwa akijizuia kuidai haki yake katika yale mazingira magumu sana na siku zisizo kuwa na utulivu. Wakati mmoja alisema: "Hakuna mtu wa kulaumiwa kwa kutoa madai yaliyokawia au kucheleweshwa; lawama iko kwa yule ambaye anachukua kitu ambacho hana haki nacho."[400]

Mbinu alizotwaa katika mazingira yale yasiyopendeza kwa kueneza na utangazaji mpana wa hadithi hizi Tukufu zinaakisi hekima zake kubwa na busara. Kuhusiana na hili tafadhali kumbuka lile tukio la Rahba. Ilikuwa ni wakati wa ukhalifa wake wakati alipowakusanya watu wengi hapo Rahba (Iraqi) kuwakumbusha lile Tangazo la Ghadir. Aliwaambia: "Namuapisha kwa jina la Mwenyezi Mungu kila Mwislamu kati yenu hapa, ambaye alimsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akitoa lile Tangazo pale Ghadir, asimame na ashuhudie kile alichosikia, na asisimame mtu yeyote isipokuwa wale tu ambao waliomuona na kumsikia." Masahaba thelethini, wakiwemo kumi na wawili waliopigana chini yake katika vita vya Badir, walisimama na kuthibitisha kuwa waliisikia hadithi ya Ghadir kama tulivyoonesha hapo juu katika Barua ya 56.

Hiki ni kiasi cha hali ya juu ambacho aliweza kufanya chini ya mazingira haya magumu kufuatia mauwaji ya Uthman, machafuko, uchochezi na maasi huko Basra na Syria. Naapa kwa uhai wangu, haya ni malalamiko ya kilele cha busara na wakati huohuo yenye nguvu yaliyowezekana katika siku hizo zenye mazingira magumu mno. Mtu hawezi kufahamu vya kutosha hekima na busara ya Ali ambaye kwa namna hii iliihuisha na kuipatia utangazwaji upya na wenye nguvu ile hadithi ya Ghadir kwa kukusanya ushahidi wa kundi kubwa la kwenye bonde la Rahba kama vile tu Mtume (s.a.w.w.), akiwa amenyanyua mkono wa Imam Ali, alivyofanya katika Siku ya Ghadir Khum na akawahutubia wafuasi wake zaidi ya laki moja, kutoa tangazo kwamba baada yake, Ali (a.s.) alikuwa ndiye bwana na kiongozi wao. Hivyo, hadithi ya Ghadir ikawa ni maarufu sana miongoni mwa hadithi za mfululizo yenye kuaminika. Tafadhali hebu tafakari juu ya hekima ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambaye alitoa tangazo hilo mbele ya mashahidi wengi kiasi kile pale Ghadir-Khum, baada ya kupokea uthibitisho wao wenyewe, kwamba yeye anayo mamlaka juu yao kuliko waliyonayo wao wenyewe, na pia tazama hekima ya huyu wasii na mrithi wake ambaye baada ya kusimamia kiapo kwa wale wote waliokuwa wamekusanyika pale Rahba, alipata ushahidi wa wale walioshuhudia tukio la Ghadir na binafsi zao walisikia tangazo la Ghadir kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe. Ukweli ni kwamba, hadithi ya Ghadir na hali ya Ali (a.s.) kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ilithibitishwa kwa uangalifu mkubwa sana uliowezekana chini ya mazingira magumu yale. Imam (a.s.) alitetea haki yake ya ukhalifa kwa amani kabisa kwani amani ya watu na usalama wa Umma vilikuwa na thamani sana kwake kuliko maslahi yake binafsi, au hata uhai wake. Huu ulikuwa ndio msimamo wake maishani mwake kuhusiana na utangazaji wa hadith za Mtukufu Mtume

[400] Hii ni kauli fupi inayoshughulika na lengo lake tukufu, na imejumuishwa katika *Nahjul Balaghah*. Rejea kwenye kile ambacho mwanachuoni wa Mu'tazili alichosema wakati anaielezea katika ukurasa wa 324, Jz. 4, wa *Sharh Nahjul Balaghah*.

(s.a.w.w.) kuhusiana na urithi wake kama Khalifa. Ili kuandaa uenezaji wa hadithi hizi miongoni mwa wale ambao hawazitambui riwaya hizi, alizitwaa kwa hekima kabisa mbinu kama hizo kwani zilikuwa haziwezi kusababisha makelele au vurumai wala chuki yoyote au machukizo.

Kuhusiana na hili angalia ile hadithi ya Ali (a.s.) kuhusu ile karamu iliyoandaliwa na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), katika nyumba ya mkuu wa watu wa Makka (yaani Abu Talib), katika siku ya ‘Kuwaonya jamaa zake wa karibu.’ Ni hadithi ndefu na muhimu sana iliyosimuliwa takriban na muhadithina wote. Tayari tumeitaja katika Barua ya 20. Watu siku zote wamekuwa wakiichukulia hadith hii kama moja ya ishara za Uislam na utambulisho muhimu wa utume wa Muhammad (s.a.w.w.) kwani inazungumzia muujiza wa Mtume ambaye alilisha idadi kubwa ya watu kwa chakula kidogo sana. Hadith inahitimishwa kwa maneno haya: “Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimchukua Ali kwa kumshika shingoni na akasema: ‘Huyu ni ndugu yangu, mtekelezaji wa wosia wangu, na khalifa wangu kwenu; hivyo, msikilizeni na mtiini.’” Alizoea mara nyingi sana kurejea maneno aliyosema Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akimuambia: “Wewe ni *Walii* [mlinzi] wa kila muumini baada yangu,” na vilevile mara kwa mara alikuwa akisimulia kauli hii ya Mtume (s.a.w.w.): “Cheo chako kwangu ni kama kile cha Harun kwa Musa, isipokuwa hakutakuwa na Mtume baada yangu,” na alikuwa kila mara akisimulia hadith ya Ghadir Khum: “Je, mimi sina mamlaka zaidi juu ya maisha ya waumini kuliko waliyo nao waumini wenyewe?” Wakasema: “Ndio, hakika.” Kisha akasema: “Kwa yeyote yule ambaye mimi nilikuwa *walii* na kiongozi wake, huyu Ali ni *walii* na kiongozi wake.” (Yaani Ali sasa ana mamlaka juu ya Waislam wote kama aliyokuwa nayo Mtume - katika maneno ya Ibn Abu Asim, kama tulivyoeleza kwenye hitimisho la Barua ya 23). Kwa nyongeza alikuwa akitangaza riwaya nyingi kama hizo zenye usahihi usiokanushika miongoni mwa watu wenye kutegemewa sana. Hivi ndivyo tu Ali (a.s.) alivyoweza kufanya wakati wa mazingira hayo magumu katika kuwakumbusha watu juu ya hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu haki yake ya Ukhalifa bila kuchafua amani na umoja wa Umma kwa hali yoyote ile.

وَلَقَدْ جَاءَهُم مِّنَ الْأَنبَاءِ مَا فِيهِ مُزْدَجَرٌ حِكْمَةٌ بَالِغَةٌ فَمَا تُغْنِ النُّذُرُ

**“Na bila shaka zimewajia habari zenye makaripio. Hikma kamili, lakini maonyo hayafai.”** (54:4-5)

Na katika Siku ya Shuura (siku ya kamati ya mashauriano ya kumteua Khalifa baada ya kifo cha Khalifa wa pili, Umar), aliwabana sana wapinzani wake kwa hoja zake kiasi kwamba hawakuweza kupata udhuru wowote wenye nguvu na alifanya kila lililowezekana kuwaonya juu ya adhabu ya Siku ya Kiyama, na kuwafanya wahofie ghadhabu ya Mwenyezi Mungu swt. Aliorodhesha fadhila na sifa zake bora zote katika kuthibitisha madai yake ya kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na wakati wa ukhalifa wake, mara kwa mara alikuwa akizungumzia uporwaji wa haki yake na akilalamika kuhusu dhulma mbaya aliyofanyiwa. Kwa uchungu akitaja malalamiko yake juu ya mimbari, ya mateso na huzuni ya kunyimwa haki yake akisema: “Amma! Wallahi fulani, ameuvaa (Ukhalifa) hali akiwa yuajua kuwa nafasi yangu kuhusiana nao ni sawa na mahala pa muhimili wa jiwe la kusagia nafaka. Chemchem za elimu zinamiminika kutoka kwangu. Kubuni hakuwezi kupaa juu kufikia kiwango cha cheo changu. Lakini nilikishushia pazia na nikajiweka mbali naye. Kulikuwa na chaguzi mbili tu mbele yangu; nipigane kwa mkono butu, au nilivumilie giza linalopofusha (la maonevu), ambalo litamgeuza mtoto kuwa mzee, na mzee humo kuwa kikongwe dhaifu, na kumlazimsha muumini kutaabika humo mpaka mwisho wa maisha yake, nikaona kuivumilia hali na kuwa na subira ndio bora ya maovu mawili hayo, basi nikaweka subira ingawa jichoni mwangu mlikuwa na utongotongo, na kooni kuna

mfupa uliokwama kwani niliona uporwaji wa haki yangu na kutwaliwa kwa nguvu Ukhalif…" mpaka mwisho wa khutba yake ya *shaqshaqiya,* ambayo ni khutba ya 3 katika *Nahjul Balaghah*, uk. 25, Jz. 1.

Mara kwa mara alikuwa akiomba: "Ee Allah! Naomba msaada Wako dhidi ya Kuraishi na wale ambao wanawasaidia, ambao wamekata minofu yangu (wamekata mahusiano na mimi), wameshusha cheo changu, na kupunguza umaarufu wangu na wameshirikiana miongoni mwao na kuzozana na mimi kuhusu kile ambacho kinanistahiki mimi tu na ambacho nina haki pekee nacho." Kisha wakamwambia: 'Hivi hupendi wewe kukirejesha kile ambacho una haki nacho na ambacho mpaka sasa kiko mikononi mwa wengine?'" Na mtu mmoja akamwambia: "Ewe mwana wa Abu Talib! Wewe una uchu na Ukhalifa." (Rejea khutba 187 ya *Nahajul Balaghah).* Ambapo yeye alimjibu: "Lakini Wallahi, wewe una ulafi nacho zaidi kuliko mimi. Ninadai kilicho haki yangu ambapo wewe unaniingilia kati kwacho na kuweka vikwazo katika njia yangu." Wakati mmoja yeye (a.s.), vilevile alisema: "Kwa jina la Allah tangu wakati Allah alipochukua uhai wa Mjumbe Wake (s.a.w.w.), hadi leo, nimekuwa kila siku nasukumwa mbali na haki yangu, ambapo wengine wanapendelewa zaidi yangu tangu Mwenyezi Mungu alipomchukua Mtume Wake hadi leo." Hii ni kama ilivyo katika khutba ya 5, uk. 37, Jz. 1, ya *Nahjul Balaghah.*

Yeye, Ali (a.s.), alisema: "Hii ni haki yetu; kama tukiipata ni vema, vinginevyo kama hatuipati, tutapanda ngamia wazee hata kama safari ni ndefu."[401] Yeye (a.s.) alisema katika barua aliyoandika kwa ndugu yake Aqil: "Yule Ambaye hutenda kwa uadilifu na anilipizie kwa niaba yangu dhidi ya Kureishi ambao wamenitenganisha na ndugu yangu mwenyewe na kuninyima nguvu ya ndugu yangu wa kuzaliwa." Pia yeye (a.s.) mara kwa mara alikuwa akisema: kama ilivyoelezwa katika barua 36, uk. 67, Jz. 3, katika *Nahajul Balaghah*: "Niliangalia kila upande na sikuona msaidizi yeyote mbali na Ahlul-Bayt wangu ambao nilikuwa sipendi kuwaona wakitolewa muhanga. Kulikuwa na mwiba kwenye macho yangu na mfupa wa huzuni ukinikwama kooni, niliuvumilia. Na kwa subira niliziridhisha hisia zangu na kimya kimya nikapatwa na matatizo mengi machungu zaidi kuliko tango chungu." Kama ilivyo katika khutba 25, uk, 62, wa Jz. 1, ya *Nahajul Balaghah*.

Mmoja kati ya wafuasi wake wakati fulani alimuuliza: "Kwa nini kikundi cha watu wamekuweka mbali na kwenye nafasi ya Ukhalifa wakati wakijua kwamba wewe una haki zaidi kuliko mwingine yeyote?" Yeye, kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 79, Jz. 2, wa *Nahjul Balagha*, kama semi ya 157, alijibu: "Ewe ndugu yangu kutoka Banu Asad! Una haraka ya kutaka kujua siri ya kuniweka kwao mbali na Ukhalifa. Umeuliza swali kiovyo ovyo bila kujizuia. Wewe ni ndugu (wa kabila moja na Ummul-Mu'mini Zainab), na kwa hiyo una haki ya kuuliza swali kama hilo. Sasa kwa vile umeuliza juu ya sababu yenyewe, napaswa kukwambia kwamba, wao walijipendelea wenyewe kwa kazi hii kuliko sisi, ingawa sisi ni wa ukoo na kizazi bora zaidi na tuko karibu sana kwa uhusiano wa kidamu na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Tamaa yao ya kujikweza binafsi iliwafanya wawe mabakhili na walafi wa nafasi hiyo (ambayo waliikamata) wakati wengine (mimi na kundi langu) tulivumilia kwa ustahimilivu mkubwa dhulma yao. Mwenyezi Mungu ataamua suala letu hili, ambaye Kwake sisi sote tutarejea Siku ya Hukumu. Sasa tafadhali tuliache suala hili la ukandamizaji na uporaji ambao ulikuwa ni janga baya sana."

Yeye, (a.s.) vilevile akasema:[402] "Wako wapi wale wanaodai kwamba wamezama sana katika ilmu kuliko sisi? Ni waongo. Wao wanafanya maasi dhidi yetu sisi. Allah amenyanyua cheo chetu na kuwaacha katika nafasi duni. Ametujaalia sisi neema Zake na akawanyima wao, na ametuingiza kwenye rehema Zake ambapo amewatoa wao nje. Mwongozo unapatikana kupitia kwetu na macho ya upofu hupata mwanga kutoka kwetu. Maimamu (viongozi halisi wa kiroho) daima watakuwa ni kutoka miongoni mwa kizazi

[401] Semi hii ni namba 21 kati ya semi zake "semi zake za hikima zilizochaguliwa," uk. 155, *Nahjul Balaghah*. Sayyid al- Radhi ameitolea ufafanuzi wenye maana sana, na hivyo hivyo Sheikh Muhammad Abduh. Wote unastahiki mazingatio ya mwanchuoni mwenye hamu ya uandishi.

[402] Kama ilivyoelezwa katika Jz.2, uk. 36 wa Nahajul-Balaghah katika Semi ya 140.

cha Hashim katika kabila ya Kuraishi. Wasiokuwa Bani Hashim hawafai wala kustahiki kuwa Maimam (wa jumla). Hakuna serikali itakayoweza kufanya kazi vizuri bila ya Imam kutoka miongoni mwa Bani Hashim." Katika maelezo mengine[403] alisema: "Wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipofariki umma ulirejea ulikotoka. Mapazia yalishuka machoni mwao. Walifanya ushirikiano na marafiki na wasaidizi wao. Walianzisha kiungo na wale ambao walikuwa hawana uhusiano nao. Waliwatelekeza wale ambao waliamriwa kuwapenda. Waliuondoa muundo wa Ukhalifa mahali pake pa msingi wa asili na wakajenga jengo jipya mahali pasipo sahihi. Wao ndio chanzo cha madhambi yote na maovu. Wao ni milango ya maumivu kwa kila mwenye kugonga mlango. Waliuingiza Umma katika vurugu na mkanganyiko na wakaufanya usahau matokeo. Wakifuata mwenendo wa kizazi cha Firauni. Wamekatizwa kabisa kutoka kwenye ulimwengu ujao na wanaendelea kubakia hivyo na wametengana kabisa na dini yao ambayo wanaendelea kuipinga."

Kwenye hotuba nyingine, ambayo aliitoa baada ya kupokea kiapo cha utii, ambayo ni moja kati ya khutba muhimu ndani ya *Nahjul-Balaghah*,[404] yeye alisema: "Msimlinganishe mtu yeyote miongni mwa watu wote wa Umma huu na kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.). Kwa wale ambao wao (kizazi cha Muhammad) wamekuwa wakarimu kwao kamwe hawawezi kuwa sawa nao. Wao ni jiwe la msingi la dini, nguzo za yakini; kupitia kwao waliopitukia mipaka watarejea, na kupitia kwao ambao wameachwa nyuma wataungana nao. Wana maadili na tabia bora ambazo kimsingi zinawapa ustahiki wa kutawala (juu ya Umma), na wadhamini wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ni warithi wake. Sasa haki imerudi kwa wenye haki na kuhamia kwenye sehemu yake sahihi." Na katika hotuba nyingine [405]ambayo kwayo anawashangaa wale ambao wanampinga: "Ni mshangao jinsi gani! Hakuna kinachonishangaza mno kuliko maoni ya kimakosa ya makundi haya, na tofauti kubwa baina ya hoja zao kuhusu dini yao. Hawafuati nyayo za Mtume (s.a.w.w.), wala mfano wa *wasii* wake…!"

Fatimah Zahra, (s.a.) alitoa malalamiko yenye hoja nzito. Mbili ya hotuba zake zilikuwa muhimu sana kiasi kwamba Ahlul-Bayt (a.s.) walizichukulia kama wajibu muhimu wa watoto wao kuzihifadhi hutuba hizi moyoni kama tu vile wanavyohifadhi Qur'ani Tukufu. Katika moja ya hotuba hizo, yeye anawashutumu wale ambao wamelihamisha jengo la Ukhalifa kutoka kwenye msingi wake wa asili na kulijenga sehemu isiyostahili. Alisema:

"Ole wao! Wamethubutu vipi? Wameuhamishia wapi Ukhalifa kutoka kwenye msingi wake wa utume na kitako cha nguzo ya utume, sehemu ya mashukio ya Roho Mwaminifu [*Ruuhul-Amiin* – Jibril], na kuuhamisha kutoka kwa mtu ambaye ni mjuzi zaidi katika mambo ya kidunia na halikadhalika ya kiroho? Kwa kweli hii ni hasara kubwa iliyodhihiri. Lakini kwa nini wanamchukia Abu al-Hasan, Ali (a.s.) kiasi hicho? Wallahi, wamekuwa na fitna kubwa dhidi yake kwa sababu ya kuchukia upanga wake, kuwakanyaga kwa nguvu zote makafiri chini ya miguu yake, na kuwapa adhabu kali na kuwauwa bila huruma katika kuinusuru dini ya Allah. Wallahi! Lau wote wangeshikamana katika kamba ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alimpa Ali mikononi mwake, na wakanyenyekea kwenye uongozi wake, basi angewaunganisha pamoja kwa usalama na kuandamana nao kwa wepesi kamili na faraja, bila yeye kupata mshtuko na angewaleta kwenye chemchemu yenye kutiririka maji angavu na safi ya mema kila upande, na angewarudisha wakiwa wameridhika kabisa na angebaki kuwa mtakia kheri wao katika faragha na hadharani, na wangerejea pamoja naye bila uchovu wa safari au kujihisi kiu kamwe baada ya hapo. Kwa hakika angewafungulia milango ya rehema ya mbinguni na ardhini kwa ajili yao. Allah atawaadhibu kwa ajili ya yale waliyoyatenda; hivyo, njooni msikilize! Sijaishi maisha ya faraja, anasa au ya fahari. Kwa hakika mnapenda na mna fahari na kile chenye kutoweka haraka. Mtakimbilia wapi

[403] Rejea mwisho wa uk. 48, Jz. 2 ya *Nahjul Balaghah* katika khutba ya 146.
[404] Utayakuta yamedondolewa mwanzoni mwa uk. 25; katika kuhitimisha khutba ya 2, Jz. 1, ya *Nahajul-Balaghah*,
[405] Rejea khutba ya 84, uk. 145, Jz. 1, ya *Nahjul Balaghah.*

kutafuta hifadhi? Nashangaa. Hakika kiongozi wao ni muovu na washiriki wake ni waovu. Na malipo ya wakandamizaji ni mabaya. Na Mwenyezi Mungu atavifunga vichwa vyao kwenye migongo yao na sehemu ya juu ya migongo yao italemaa, na Mwenyezi Mungu atawahuzunisha wale ambao wanadhani wanatenda mema. Tahadharini! Hakika ni madhalimu na wafarakanishaji bali hawalijui hilo. Ole wao! Je, anayeongoza kwenye njia ya haki ndiye mwenye kufaa kufuatwa au yule anayetegemea uongozi wa wengine? Mna matatizo gani ninyi? Mnahukumu vipi mambo?"[406]

Huu ni mfano wa hotuba juu ya suala hili kutoka kwa Ahlul-Bayt. Hii itakuwezesha kujua ni kwa uzito gani Ahlul-Bayt waliuhisi uporwaji wa Ukhalifa kutoka kwa Ali (a.s.) na kwa kiasi gani walilalamika dhidi ya hao waporaji. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

[406] Hii inanukuliwa na Abu Bakr ibn Ahmad ibn Abdul-Aziz al-Jawhari katika kitabu chake *Al-Saqifa* na *Fadak*, kutoka kwa Muhammad ibn Zakariyya, toka kwa Muhammad ibn Abdul-Rahman al-Muhallabi, toka kwa Abdullah ibn Hamad ibn Suleiman ambaye anamnukuu baba yake, Abdullah ibn al-Hasan aliyeisikia kutoka mama yake Fatima binti Husein aliyeihusisha na Zahrah (a.s), Vilevile imesimuliwa na Imamu Abul-Fadhil Ahmad bin Abu Tahir, ambaye alifariki mwaka 280 A.H., katika ukurasa wa 23 wa kitabu chake *Balaghatun-Nisa'* kupitia kwa Harun bin Muslim bin Sa'dan, kutoka kwa al-Hasan bin Alwan kutoka kwa Atiyyah al-Awfi aliyesimulia hotuba hii kutoka kwa Abdullah bin al-Hasan binal-Hasan kutoka kwa mama yake Fatima bint al-Husein, kutoka kwa bibi yake Zahra' (a.s). Wanachuoni wa Shi'ah wanasimulia khutba hii kutoka kwa Suwayd bin Ghuflah bin Awsajah al-Ju'fi kutoka kwa al-Zahra' (as). Tabrasi ameinukuu katika kitabu chake *Al-Ihtijaj*, na al-Majlis katika *Bihar al-Anwar,* na inasimuliawa na wasimuliaji wengi waaminifu.

# BARUA YA 105

## RABI'UL THANI 16, 1330 A.H.

**Maombi ya Hadithi Nyingine Kutoka kwa Wengineo.**

Ili kukamilisha mada hii nakuomba tafadhali ututolee malalamiko mengine yaliyofanywa kuhusiana na hili kutoka kwa watu wengine mbali na Imamu Ali (a.s.) na Zahra ((a.s.), na hivyo utakuwa umetusaidia sana. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 106

## RABI'UL THANI 18, 1330 A.H.

**I. Malalamiko ya Ibn Abbas,**

**II. Malalamiko ya Hasan na Husein,**

**III. Hoja Ya Sahaba Mashuhuri Shi'ah,**

**IV. Ya Shi'ah Maarufu Miongoni mwa Sahaba.**

**V. Dokezo za Haki ya Urithi wa Ali (a.s.) Katika Malalamiko.**

Ngoja nivute nadhari yako kwenye mazungumzo kati ya Ibn Abbas na Umar. Katika mazungumzo marefu kati yao, Umar alimuuliza: "Ewe Ibn Abbas! Je unajua kilichoufanya Umma kuwanyimeni Ukhalifa baada ya Muhammad (s.a.w.w.)?" Ibn Abbas kwa kuona asimjibu Umar, akamuambia: 'Kama mimi sijui Amir wa waumini [yaani, Umar] atakuwa anajua.'" Umar akasema: "Umma haukutaka kuona kwamba utume na ukhalifa vyote vibakie kwenye nyumba yenu tu; ili msije mkayadhuru maslahi ya taifa na kulikanyaga mpendavyo. Makureishi kwa hiyo walichagua kuutwaa Ukhalifa kwa ajili yao. Walifanya uamuzi mzuri na waliweza kufanikiwa kuupata."

Ibn Abbas akasema: "Ewe Amir wa waumini! Nina kitu cha kusema kama utaniruhusu na pia kuahidi kuzuia hasira zako?" Alijibu kwa kukubali: "Nakuruhusu na kukuahidi." Ibn Abbas akasema: "Ama kuhusu kauli yako, Ewe Amir wa waumini, kwamba Kureishi walijichagulia kwa ajili yao wenyewe na waliamua kwa usahihi na walifanikiwa kuupata, ningependa kusema kwamba lau Kureishi wangechagua kwa mujibu wa matakwa ya Allah, chaguo lao lingekuwa sahihi na lisingepingwa na kulaumiwa au kuonewa wivu na yeyote. Ama kuhusu kauli yako kwamba Makuraishi hawakutaka kuona utume na ukhalifa unabakia kwetu, nakukumbusha maneno ya Allah, Aza wa jallah, ambaye alielezea kaumu iliyochukia, alisema: **"Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao,'" (Qur'ani 47:9).** Hapo Umar akasema: "Ole wako ewe Ibn Abbas! kwani nimepokea taarifa kuhusu wewe ambazo nachukia kuamini isije hadhi yako machoni mwangu ikapungua." Ibn Abbas akamuuliza: 'Ni mambo gani, Ewe Amir wa waumini? Kama ni ya kweli kama uliyoarifiwa kwamba nimeyasema mimi, hakuna sababu ya kushusha hadhi yangu mbele yako, na kama sio ya kweli, niko tayari kujizuia na mambo hayo katika siku za baadae.' Kisha Umar akasema: 'Nimefahamishwa kwamba unasema kwamba wamekunyimeni ukhalifa kwa sababu ya wivu, dhulma na uonevu.' Ibn Abbas akasema: 'Ama kuhusu dhulma na uonevu, Ewe Amir wa waumini, basi hilo liko wazi kabisa kwa wote wale wenye elimu na hata wasio na elimu pia. Ama kuhusu wivu, basi Baba yetu Adam alionewa wivu, na hakuna la ajabu kama sisi ambao ni kizazi chake wakituonea wivu.' Umar akasema: "Haiwezekani, haiwezekani; Enyi kizazi cha Hashim! Wallahi wakati wote ninyi mmekuwa ni wenye wivu. Nyoyo zenu kamwe haziwezi kuondokana na wivu.' Ibn Abbas akasema: 'Subiri, Ewe Amir wa waumini! Fikiria upya hayo uliyoyasema. Usihusishe uchafu wa wivu kwenye nyoyo za wale ambao Allah amewaweka mbali na kila aina ya uchafu na akawatoharisha kwa utakaso kamili.'"[407]

[407] Tumeinukuu neno kwa neno kutoka kwenye *Al-Tarikh al-Kamil* ya Ibn Athir ambaye ameisimulia wakati akielezea wasifu na tabia ya Umar miongoni mwa matukio ya mwaka 23 A.H., ukurasa 24, Jz. 3, na vilevile imenukuliwa na Allamah Mutazili katika wasifu wa Umar, ukurasa 107, Jz. 3, ya *Sharh Nahjul Balaghah.*

Katika mazungumzo mengine, Umar alimuuliza Ibn Abbas: "Binamu yako umemuacha na hali gani?" Ibn Abbas alifikiri anaulizia kuhusu hali ya Abdullah ibn Ja'far; hivyo akasema: "Nimemuacha akiwa na marafiki wa rika lake." Akasema: "Sikumaanisha yeye; nilikuwa na maana ya mkuu na kiongozi wa ukoo wenu." Ibn Abbas akasema: "Nilipomuacha alikuwa anachota maji kutoka kisimani kwa ajili ya kunyweshea mimea huku akisoma Qur'ani." Umar akasema: "Ewe Abdullah nakusihi uniambie kwa ukweli kabisa, bila kuficha wala kuwa na shaka kama bado ana mawazo kwamba ukhalifa ulikuwa ni wake makhsusia." Akajibu kwa kukubali. Kisha Umar akauliza: "Je anadhani kwamba Mjumbe wa Allah alimteua maalum kama mrithi (khalifa) wake?" Ibn Abbas akajibu: "Ndio, kwa hakika; aidha nitakuambia mengine zaidi ya hayo. Wakati mmoja nilizungumzia madai yake mbele ya baba yangu ya kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimteua yeye kama khalifa au mrithi wake, na baba yangu alinithibitishia kwamba hiyo ilikuwa ni kweli." Umar akasema: "Mjumbe wa Allah alikuwa na desturi ya kuzungumza kuhusu Ali kwa sifa kubwa katika kumlinganisha na wengine.[408] Ndani ya khutba zake alikuwa akizungumza mambo kuhusu Ali ambayo hayakuweza kuthibitisha hoja (ya ukhalifa wake) na ambayo hayakuweza kutumika kama hoja halali (ya ukhalifa wake). Kwa kusema mambo kama hayo kuhusu Ali alijaribu kuupa mtihani umma kuhusu urithi wake;[409] na wakati alipokuwa mgonjwa [muda mfupi kabla ya kufariki] alitaka kuthibitisha uteuzi wa Ali kama mrithi (Khalifa) wake, lakini ilikuwa ni mimi niliyemzuia kufanya hivyo."[410]

Bado katika mazungumzo mengine kati yao, Umar alisema: "Ewe Ibn Abbas! Nafikiria dhulma imefanyika kwa mkuu wako Ali (a.s.) (kwa kunyimwa Ukhalifa)." Ibn Abbas akasema: "Ewe Amir wa waumini, basi tekeleza uadilifu na mumrudishie haki yake!" Lakini Umar aliondoa mkono wake mkononi mwa Ibn Abbas kwa hasira na huku akiunguruma, na haraka sana akapiga hatua mbele kisha akasimama, hivyo Ibn Abbas akamkimbilia. Umar akamwambia: "Ewe Ibn Abbas! Nadhani Umma ulimnyima haki ya ukhalifa kwa sababu ya umri wake mdogo." Ibn Abbas akamuambia kwa ukali: "Lakini Mwenyezi Mungu na Mjumbe Wake hawakumuona mwenye umri mdogo wakati alipoamriwa kuchukua Surat Bara'a [*Tawba*] kutoka kwa rafiki yako Abu Bakr kwenda kuisoma mbele ya makafiri na washirikina."

Aliposikia hili, aligeuza uso wake upande mwingine kutoka kwa Ibn Abbas na kuanza kutembea kwa haraka, Ibn Abbas akarejea kwenye sehemu yake."[411] Mazungumzo kuhusu maudhui hii, ni mara nyingi yamefanywa na Wino wa Umma huu, msemaji wa Bani Hashim, Abdullah ibn Abbas, ambaye ni binamu wa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Katika barua ya 26, umesoma malalamiko ya Ibn Abbas kuhusu jambo hili mbele ya kikundi cha wahaini kumi wenye hasira wakati yeye alipodondoa sifa kumi za kipekee za Ali (a.s.) katika hadithi ndefu na muhimu sana ambayo kwayo anamnukuu Mtume (s.a.w.w.) akiongea na wana wa Abul-Muttalib: "Nani miongoni mwenu atakuwa tayari kuwa walii na msaidizi wangu katika dunia hii na dunia ya Akhera?" Hakuna aliyejibu isipokuwa Ali (a.s.) ambaye alisema: "Nitakuwa msaidizi wako katika dunia hii na halikadhalika katika ile ya Akhera," ambapo Mtume (s.a.w.w.) akamuambia Ali (a.s.): "Ndio. Wewe utakuwa ndugu yangu katika dunia hii na ile ya Akhera….." na wakati Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alitoka kwenda kwenye vita vya Tabuk, na watu wengi wakakusanyika ili kufuatana naye, Ali (a.s.) alimuuliza: "Je, nifuatane na wewe?" Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akamkatalia ombi hilo; hivyo, Ali akaanza kulia. Ndipo hapo Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akamwambia: "Wewe huridhii

[408] Hii inarudi kwenye maneno yake: "Kuzungumza kwake katika namna ya kumsifia Ali kuliko wengine kulikuwa kama jiwe ambalo mtu analibeba ili kujua nguvu zake, na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kwa kuzidisha kwake kumsifia Ali alitaka kujua iwapo kama ummah utamkubali yeye kama Khalifa au la.

[409] Alimaanisha kwamba khutba ya Mjimbe wa Allah (saw) kwa ajili ya kumsifia Ali kwa maneno hayo, anaujaribu ummah kuona kama utamkubali kama mrithi wake.

[410] Hadithi hii ya Umar imenukuliwa na Imamu Abul-Fadhl ibn Abu Tahir katika kitabu chake *Tarikh Baghdad*, akionesha vyanzo vya kuaminika hadi kwa Ibn Abbas. Na Allamah Mu'tazili ameisimulia tena katika maelezo juu ya Umar ndani ya *Sharh Nahjul Balaghah*. Tafadhali rejea katika Jz. 3, uk. 97, wa kitabu hicho.

[411] Mazungumzo haya yamenukuliwa na waandishi wa vitabu vya wasifu katika maelezo yao juu ya Umar. Hapa tumeinukuu kutoka *Sharh Nahjul Balagha* ya Allamah Mu'tazili. Tafadhali rejea uk. 105 wa jalada la tatu.

kwamba kwangu wewe una cheo kama cha Harun kwa Musa, isipokuwa kwamba hakutakuwa na Mtume baada yangu? Kwa hakika haistahili kwangu mimi kwenda kwenye vita hivi bila kukuacha nyuma yangu [hapa mjini – Madina] kama khalifa wangu….." Na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) vilevile akamwambia: "Baada yangu wewe ndiye *walii* na Imam wa kila muumini….." Na akasema tena (s.a.w.w.): "Yeyote mwenye kuamini kwamba mimi ni *mawla* na kiongozi wake, Ali vilevile ni *mawla* na kiongozi wake….."

Wanaume wengi wa Bani Hashim mara kwa mara walitoa malalamiko kama hayo hayo. Wakati mmoja Hasan bin Ali (a.s.) alikuja kwa Abu Bakr ambaye alikuwa amekaa juu ya mimbari ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na akamuambia: "Shuka kwenye kiti cha baba yangu." Katika tukio jingine, inasemekana kwamba Husein bin Ali (a.s.) alisema maneno kama hayo kumuambia Umar ambaye alikuwa amekaa juu ya mimbari hiyo ashuke kwenye kiti cha baba yake.[412]

Vitabu vya wanachuoni wa Kishia vina malalamiko mengi kuhusu suala hili kutoka kwa Bani Hashim na wafuasi wao miongoni mwa sahaba na *tabi'in.* Anayetaka kupata uthibitisho anapaswa kuangalia vitabu vyao. Hapa yatosha kudondoa kitabu *al-Ihtijaaj* cha Imamu Tabrisi ambacho kwacho ananukuu malalamiko yaliyotolewa na Khalid bin Sa'id ibn al-As ul-Am'wiy,[413] Salman al-Farsi, Abu Dharr al-Ghifari, Ammar bin Yasir, al-Miqdadi, Buraydah al-Aslami, Abul-Hytham ibn al-Tiihan, Sahl na Uthman mtoto wa Hanif, Khuzaymah bin al-Thabit ash-Shahadatayn, Ubayy ibn Ka'b, Abu Ayyub al-Ansari, na wengine wengi miongoni mwa wale ambao wamefanya utafiti wa historia ya Ahlul-Bayt na wafuasi wao hawakuacha fursa yoyote iwaponyoke ya kutoa malalamiko kuhusiana na hili kwa kudondoa rejea za wazi au zenye kudokezea, kwa maneno mazito au kwa maneno laini, kwa maneno au maandishi, kwa insha au mashairi na tenzi, kwa jinsi mazingira yalivyowaruhusu. Ahlul-Bayt na wafuasi wao walirudia rudia malalamiko yao kwa watawala dhidi ya uporwaji wa haki ya Ali ya kumrithi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na mara nyingi walitaja uwasii kama hoja ya urithi wake kama wanavyolijua hilo watafiti. Wasalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

---

412 Ibn Hajar amenukuu matukio yote katika *Maqsad* ya tano wakati akifafanua juu ya aya inayoamrisha mapenzi kwa jamaa wa Mtume (Qur'ani, 42:23), ambayo ni kifungu cha 14 katika *Sawa'iq* Sura ya 11, uk. 160. Al-Dar Qutni amenukuu. tukio la al-Hasan na Abu Bakr, na Ibn Sa'd amenukuu tukio la al-Husein na Umar katika wasifu wa huyu wa mwisho katika *Tabaqat.*

413 Khalid bin Sa'id ibn Al'As alikuwa miongoni mwa wale ambao waliokuwa hawakubaliani na ukhalifa wa Abu Bakr. Hakuchukua kiapo cha utii kwake kwa muda wa miezi mitatu, kama ilivyoelezwa na kundi la Masunni waaminifu kama vile Ibn Sa'd katika maelezo juu ya Khalid katika *Tabaqat,* uk. 70, Jz. 4, akiongeza kwamba wakati Abu Bakr alipotoa jeshi kwenda Syria, alimteua Khalid kuwa jemedari mkuu na akaenda nyumbani kwake mwenyewe binafsi pamoja na bendera kwa ajili yake. Umar alipolitambua hilo akamuambia Abu Bakr: "Wakati unajua maoni yake kuhusu ukhalifa bado unatoa ujemedari wa jeshi kwake?" Alimshinikiza Abu Bakr kumbadilisha Khalid na mtu mwingine. Abu Bakr akamtuma Aba Urwah al-Dawsii ambaye amwambia: "Khalifa wa Mtume wa Allah (s.a.w.w.) anakuambia urudishe bendera yetu." Alifanya hivyo huku akisema: "Kuteuliwa kwangu hakukunifurahisha wala kuniengua kwenu hakunihuzunishi." Aliposikia kauli hiyo, Abu Bakr alimfuata na kumuomba radhi, na kwa upole alimuomba asimjulishe Umar kuhusu ujio huo, iwe ni siri. Waandishi wote ambao walitaja tukio hili la kampeni ya Syria halikadhalika walitaja tukio hili kwa urefu au kifupi, kwani ni moja kati ya matukio maarufu sana.

# BARUA YA 107

## RABI'UL THANI 19, 1330 A.H.

**Ni Wakati gani Walitaja Haki ya Uwasii wa Ali?**

Ni lini walitaja kuteuliwa kwa Ali kama '*Wasii*' wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na lini walilalamika dhidi uporwaji wa haki yake ya ukhalifa? Hatujui tukio lolote ambamo uwasii wake umetajwa isipokuwa mara moja mbele ya mama wa waumini [Aisha] ambaye aliukataa katakata, kama tulivyoeleza kabla. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 108

## RABI'UL THANI 22, 1330 A.H.

**Kuthibitisha Hoja ya Uwasii.**

Bali Amirul Muminin (a.s.) aliutaja wakati alipokuwa anahutubia juu ya mimbari, na tumenukuu baadhi ya mazungumzo yake katika Barua ya 104. Zaidi ya hayo, waandishi wa hadithi wote ambao wameandika "Hadithi ya Nyumba (ya Abu Talib) katika siku ya 'Kuonya ndugu wa karibu' ambamo kwa uwazi kabisa ulitangazwa uteuzi wa Ali kuwa '*Wasii*' (mtekeleza wosia na mrithi) wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wameisimulia hadithi hii hadi kufika kwa Ali (a.s.) mwenyewe. (Hii ina maana kwamba Ali alithibitisha madai yake mbele ya wanahadithi hao). Sisi vilevile tumeinukuu hadithi hii katika Barua ya 20. Na humo mna maandiko ya wazi yenye kuelezea kuhusu uwasii na ukhalifa wake. Imamu Abu Muhammad Hasan (a.s.), mjukuu wa Mtume (s.a.w.w.), na bwana wa vijana wa Peponi, alitoa khutba ya kusisimua wakati baba yake Amirul Muminin (a.s.) alipouawa ambamo alisema: "Mimi ni kizazi cha Mtume (s.a.w.w.) na mtoto wa '*Wasii*' wake," kama ilivyonukuliwa na al-Hakim kwenye ukurasa wa 172, Jz. 3, ya kitabu chake *Sahih Mustdrak.* Imamu Ja'far as-Sadiq (a.s.), kama kwenye ukurasa wa 254, Jz. 3, ya *Sharh Nahjul Balagha*, mwishoni mwa ufafanuzi wa khutba ya *Qasi'a*, alisema: "Hata kabla ya Ujumbe [wa Uislamu] kutangazwa hadharani, Ali (as) wakati akiwa anafuatana na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), alikuwa akiona mwanga na kusikia sauti [za malaika]." Vilevile anamnukuu Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Lau kama nisingekuwa mimi ni wa mwisho katika safu ya mitume, wewe Ali ungekuwa mshirika wangu katika utume. Hata hivyo, ingawa wewe si mtume, kwa uhakika wewe ni *Wasii* wa Nabii na mrithi wake."

Neno '*Wasii*' limetumika kuhusu Ali (a.s.) kwa maana ya mtekelezaji wosia na khalifa miongoni mwa Maimamu wote wa Ahlul-Bayt na wafuasi wao kuanzia wakati wa Masahaba mpaka sasa. Salman al-Farsi ananukuliwa akisema kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Hakika *Wasii* wangu, msiri wangu, na mtu ambaye ni mbora nitakayemuacha nyuma yangu na ambaye atatekeleza wosia wangu na kutimiza ahadi zangu na kulipa madeni yangu, (yaani atakayetekeleza wajibat zangu zote) ni Ali ibn Abu Talib." Abu Ayyub al-Ansari anasimulia hadithi ambayo kwayo anasema kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akimuambia Fatimah (a.s.): "Je, hujafahamu kwamba Allah Aza wa Jallah, alitupa jicho juu ya wakazi wa ardhini na akamchagua baba yako kuwa Mjumbe Wake, kisha akatupa jicho la pili na akamchagua mume wako, kisha akanifunulia nikuozeshe kwake na kumfanya Wasii wangu?" Buraydah amesimulia hadithi ambayo kwayo anasema kwamba alimsikia Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) akisema: "Kwa kila Mtume kuna Wasii na mrithi, na wasii na mrithi wangu ni Ali ibn Abi Talib," na hadithi hii ya Burayda na mbili zilizotangulia za Abu Ayyub Ansari na Salman Farsi tayari zimekwisha nukuliwa hapo juu katika Barua ya 68.

Wakati wowote Jabir ibn Yazid al-Ju'fi anaposimulia hadithi kutoka kwa Imamu al-Baqir (a.s.), alikuwa akipachika ile hadithi yenye maneno "*Wasii* wa *mawasii* amenisimulia hadithi…nk." kama ilivyoelezwa katika maelezo ya Jabir katika kitabu, Al-*Mizanul-I'tidal* cha al-Dhahabi. Umm al-Khayr bint al-Harish al-Bariqiya alitoa khutba fasaha kule Sufin akiwahimiza watu wa Kufa kuyapiga majeshi ya Mu'awiyah ambayo kwayo alisema: "Fanyeni haraka, Allah awe na huruma nanyi, kuja kumsaidia Imamu mwadilifu, *wasii* mwaminifu wa Mtukufu Mtume, mtekeleza ahadi na mtetezi mkuu wa haki….."[414]

[414] Hotuba yake yote ilikuwa katika mtiririko huu huu kama ilivyonukuliwa na Imamu Abul-Fadhi Ahmad ibn Abu Tahir al-Baghdadi kwenye ukurasa wa 41 wa kitabu chake *Balaghat al-Nisa*, akielezea chanzo chake kuwa ni Shu'bi.

Hawa ndio baadhi ya wahenga wetu walioanzisha utaratibu wa kumtaja Ali (a.s.) kama *Wasii* katika khutba zao na simulizi za hadith, na yeyote atakayetafiti hotuba na mazungumzo yao ataona kwamba walikuwa na desturi ya kutumia jina la *wasii* kwa Amirul Muminin (a.s.) kwa uhuru kwa namna ambavyo majina yanavyotumika kwa vitu vingine, yaani kama jina jingine binafsi na wala sio jina kisifa (*epithet*). Unaweza ukakadiria ueneaji wa desturi hii kutokana na ukweli kwamba mkusanyaji wa kamusi *Taj al-Arus* wakati akielezea neno *wasii* kwenye ukurasa wa 392, Jz. 10, anasema: "*Wasii* kama *Ghanii*, ni lakabu (jina la heshima) pekee ya Ali (a.s.)!"

Ama katika ushairi, neno Wasii limetumika mara nyingi sana juu ya Ali, kiasi kwamba haiwezekani kuidondoa mifano yote hapa kwa sababu ya wingi wake, lakini tunanukuu baadhi ambacho kitakidhi madhumuni ya kuimarisha hoja yetu. Abdullah bin Abbas ibn Abdul-Muttalib alimuelezea kwa ifuatavyo:

"Yeye pekee, miongoni wa Ahlul-Bayt ndiye *Wasii* wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Kama mpiganaji katika medani ya vita akitoa changamoto ya kutaka kupambana na mpinzani, yeye ndiye Shujaa jasiri wa kuijibu changamoto hiyo."

Al-Mughira bin al-Harith bin Abdul-Muttalib, katika moja ya beti zake ambazo kwazo anawahimiza watu wa Iraq kushambulia majeshi ya Mu'awiyah kule Sufin anasema:

"Huyu ni *Wasii* wa Mjumbe wa Allah na kiongozi wenu, na mkwewe Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na Kitabu cha Mwenyezi Mungu kimeeleza hayo."

Abdullah ibn Abu Sufyan bin al-Harith ibn Abdul-Muttalib anasema:

Miongoni mwetu ni Ali (a.s.), aliyekuwa shujaa wa Khaibar na vita vya Badr, wakati wapiganaji wote waliporudi nyuma; ambaye ndiye *Wasii* wa Mtume mteuliwa (s.a.w.w.) na binamu yake, Hivyo nani awezaye kuwa sawa naye? kushindana kwa heshima na hadhi?

Abdul-Haytham ibn al-Tiihan, mmoja wa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) Badr, ambaye alipigana vita vya Badr alisoma beti kadhaa wakati wa Vita vya Ngamia. Mojawapo ya beti zake ilisema:

*"Wasii* wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ndiye Imamu na kiongozi wetu. Pazia limefunuliwa na siri sasa zimefichuliwa."

Khuzaymah bin Thabit ash-Shahadatain, ambaye amepigana vita vya Badr, katika moja ya mashairi yake wakati wa Vita vya Ngamia anasema:

"Ewe *wasii* wa Mtume! Vita vimewatingisha maadui,

Na kwa ghasia wanawake wameingia katika uwanja wa vita."

Katika beti zake nyingine mbili, Allah awe radhi naye, alisema:

"Ewe Aisha! Ondosha uadui wako kwa Ali na jizuie na kumdhania makosa ambayo yuko mbali nayo kabisa na ambayo ni matokeo tu ya fikra zako tu. Yeye peke yake miongoni mwa Ahlul-Bayt ndiye *Wasii* wa Mtume wa Allah (s.a.w.w.), na wewe mwenyewe umeshuhudia heshima maalum ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa nayo juu yake."

Abdullah ibn Badiil bin Warqa al-Khuza'i shujaa miongoni mwa sahaba, ambaye aliuawa shahidi kule Sufin pamoja na ndugu yake Abdur-Rahman, alisema yafuatayo katika tukio la Vita vya Ngamia:

"Enyi watu wangu! Msiba mkubwa ulioje aliouleta Shetan!

Wanapigana vita dhidi ya *wasii* wa Mtume na mapambano yamekuwa ni muhimu."

Miongoni mwa beti zilizosomwa na Amirul Muminin mwenyewe akiwa Sufin ina maana kwamba:

"Kama mtu angemfikishia Ahmad taarifa kwamba hakika *wasii* wako analinganishwa na mnyonge wa kizazi chenye upungufu, yeye (s.a.w.w.) kwa hakika asingefurahi na angechukia."

Jariir bin Abdullah al-Bajali, sahaba wa Mtume (s.a.w.w.), alituma beti kadhaa kwa Shurhabil bin al-Samit, ambazo kwazo akizungumza juu ya Ali (a.s.) yeye anasema:

Miongoni mwa Ahlul-Bayt, yeye ndiye *Wasii* wa Mtume wa Rahman,

Askari mpanda farasi mwenye nguvu zifahamikazo amlindaye.

Umar ibn Haritha al-Ansari, katika shairi la kumsifia Muhammad mtoto wa Amirul Muminin, maarufu kwa jina la Ibn al-Hanafiyya, alisema:

"Kwa jina la Mtume (s.a.w.w.) ameitwa, na kwa sura anashabihiana na *Wasii*, na, Rangi ya bendera yake ni nyekundu iliyoiva."

Wakati watu walipokuwa wanakula kiapo cha utii kwa Ali (a.s.) baada ya kifo cha Uthman, Abdur-Rahman ibn Ja'iil alisoma beti mbili zenye maana:

Naapa kwa uhai wangu! Mmechukua kiapo cha utii kwa mtu ambaye ndiye mlinzi bora wa dini, anayejulikana sana kwa uadilifu wake, na ambaye rehma za Aza wa Jallah ziko juu yake;

Mwema, asiye na dhambi, Ali, *Wasii* wa Muhammad Mustafa na binamu yake, wa kwanza kutekeleza swala za wajibu, na mtu mwenye msaada mkubwa kwenye dini na uchaji na heshima."

Mtu mmoja wa kabila la Bani Azd alisoma beti zifuatazo wakati wa Vita vya Ngamia:

Huyu ni Ali; ndiye *Wasii*, Mtume katika Siku ya wokovu alimchukua kama ndugu yake na akamtangaza kuwa ni kiongozi na Imam (wa waumini wote) baada yake. Wenye busara walizingatia na kutia akilini, Mabazazi walisahau na kuiweka nyuma.

Wakati wa Vita vya Ngamia, kijana mmoja kutoka Bani Zabbah, ambaye alikuwa anapigana upande wa Aisha, alitoka nje ya safu zao na kusema:

Sisi Bani Zabbah ni maadui dhahiri wa Ali, yule yule Ali ajulikanaye siku zote kama *Wasii* (wa Mtukufu Mtume),

Na aliyekuwa Jemadari mkuu wa jeshi wakati wa uhai wa Mtume, Mimi sio kipofu juu ya sifa na heshima za Ali. Bali nimekuja tu kutangaza kifo cha Ibn Affan mcha-Mungu.

Sa'id bin Qais al-Hamadani, akipigana upande wa Ali (a.s.), alisema katika siku ya Jamal:

"Ni moto mkali kiasi gani wa mapambano ambao umewashwa! Mipini ya mikuki ya wapiganaji imevunjika.

Mfahamishe Wasii kwamba Bani Qahtan sasa wamefurika kwenye medani ya vita na wanamuomba awaite kuja kumsaidia, wale Bani Hamadani na watoto na ndugu zao."

Za'id bin Labid al-Ansari, mmoja wa maswahaba wa Ali, alitunga beti hizi wakati wa Vita vya Ngamia:

"Unawaonaje Ansari wanaopigana katika mapambano haya makali? Sisi ni watu kamwe hatuogopi kufa;

Katika uaminifu wetu kwa *Wasii* huyu, tunashambulia kwa ari, hatuogopi hasira ama uadui wa yeyote yule. Sisi Ansari ni wapiganaji makini, na sio wa kuchezewa (yaani tunaujua ukweli na tunashikamana

nao), Yeye ni Ali mwana wa Abdul-Muttalib. Leo hii tunamsaidia dhidi ya waongo. Yeyote aliyemuasi ametenda kosa kubwa."

Katika siku hiyo hiyo, Hajar bin Ad al-Kindi alisema:

"Ee Mola Wetu! Mhifadhi Ali kwa ajili yetu, tuhifadhie mtu aliyebarikiwa na mwenye kung'ara.

"Ambaye ni mwaminifu, mwana tawhiid na mchamungu, asiye na mawazo ya kipumbavu au aliyepotoka. Yeye ni kiongozi, Imam aliyebarikiwa na aliyeongozwa na Mwenyezi Mungu. Ewe Mola Wangu! Muokoe yeye na (kupitia kwake) muokoe Mtume.

"Yeye ndiye kipenzi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye alimchagua yeye kuwa Wasii wake baada yake."

Umar ibn Ahjiyah alitunga shairi akisifia khutba ya Hasan, aliyoitoa baada ya ile ya Ibn Zubayr, wakati wa Vita vya Ngamia akisema:

"Ewe Hasan mwema! Ewe taswira ya baba yako! Umesimama miongoni mwetu na ukatoa hotuba nzuri mno.

"Ulisimama ukatoa khutba ya kujibu ile hotuba iliyotolewa na mwenye kufedheheka kuhusu baba yako, ambayo alimuudhi Allah.

"Ibn Zubayr alishikwa na kigugumizi katika hotuba yake isiyokamilika. Alilegeza hatamu za farasi wake ili aondoke zake kwani alikuwa na shaka na mwenye kuaibika.

"Allah hakumtaka yeye kunyanyuka kufikia upeo wa mwana wa *wasii* na mtu mwenye kuheshimika zaidi (Ali).

"Wewe bila shaka yoyote, wewe ndiye uliyeteuliwa na Nabii mwenyewe, na akakutangaza kuwa mwema sana na Wasii naye akakutangaza kuwa mwadilifu katika hali yake bora kabisa.

Zajri ibn Qays al-Ju'fi vilevile alisema katika siku ya Vita vya Ngamia:

"Nitaendelea kuwauweni mpaka mtakapoukubali Uimam wa Ali, ambaye baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ndiye mtu bora miongoni mwa Quraishi wote, ambaye Mwenyezi Mungu amempamba kwa sifa na ubora na akamwita 'Wasii.'"

Na mnamo siku ya Sufin, yeye alisema:

"Mola amrehemu Ahmad, Mtume mwenye Mamlaka, Ambaye kupitia kwake aliikamilisha neema Yake kwetu.

"Rehema ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya Mtume mwenye mamlaka (s.a.w.w.) na baada yake, juu ya Khalifa wetu wa sasa, ambaye ndiye mahali pa kimbilio letu. Ninamaanisha Ali (a.s.), *Wasii* wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye walio dhidi yake ni wale waliopotoka miongoni mwa watu wa Umma huu."

Na Al-Ash'ath ibn Qays al-Kindi alisema:

"Mjumbe ametujia kwetu, mjumbe wa Imamu wetu. Katika kuwasili kwake, wimbi la furaha na shauku lilitanda kwa kila Mwislamu.

"Ni mjumbe wa *Wasii*, yule *wasii* wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye ni wa mwanzo na mwenye sifa kuu mno miongoni mwa waumini wote."

Na vilevile beti zifuatazo ni za kwake yeye:

"Mjumbe ametujia, mjumbe kutoka kwa Wasii, ambaye ni Ali (a.s.),

Ambaye ndiye mwenye kutambulika zaidi kati ya Bani Hashim,

“Na ni Wasii na mkwe wa Mtume (s.a.w.w.), waziri wake hakika,

Mbora wa viumbe na mbora wa walimwengu. (baada ya Mtume).”

Al-Nu’man ibn al-Ajlan al-Zarqi al-Ansari alisema yafuatayo wakati akipigana katika Vita vya Sufin:

“Kwa nini faraka yote hii wakati *Wasii* ndiye Imamu wetu,? Sivyo! Mkanganyiko huu na fadhaa, ni kutokana na utata na kugawanyika.

“Hivyo, muacheni mkosaji na mpotofu Mu’awiyah na fuateni Dini ya *Wasii*, ili mpate mwisho mwema.”

Abdur Rahman bin Dhuayb al-Aslami katika vita vya Sufin alimtishia Mu’awiyah juu ya shambulio kali kutoka kwa jeshi la Iraq akisema:

W*asii* wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na wapanda farasi hawa mpaka akurudusheni kutoka kwenye mzingile wa shaka na upotofu kwenye njia iliyonyooka.[415]

Abdullah bin Abu Sufyan bin al-Harith bin Abdul-Muttalib amesema:

“Mwenye mamlaka na mtawala baada ya Muhammad ni Ali ambaye nyakati zote amemlinda, alimsaidia na kuandamana naye, Yeye kwa hakika ndiye *Wasii* wa Mjumbe. Yeye na Mtume wa Mwenyezi Mungu ni matawi mawili yanayotoka kwenye mzizi mmoja. Yeye ndiye wa kwanza kuswali na Mtukufu Mtume na mwenye upole.”

Khuzaymah bin Thabit ash-Shahadatain anasema:

“Yeye peke yake miongoni mwa Ahlul-Bayt (a.s.) ndiye *wasii* wa Mjumbe na kiongozi wa askari wake wa farasi katika medani ya vita tangu mwanzoni kabisa.

“Pamoja na Bibi Khadija, yeye ni wa kwanza kuswali, hakuna aliyemtangulia, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa baraka.”

Zafar bin Hudhayfah al-Asdi anasema:

Mzungukeni Ali enyi watu na msaidieni. Kwani yeye ni *wasii* na wa kwanza kati ya Waislamu wa mwanzoni kuikubali dini.[416]

Abul-Aswad al-Duali amesema:

“Nampenda Muhammad Mustafa kwa mapenzi ya dhati na Abbas, Hamza, na yule ambaye ni *Wasii.”*

[415] Ubeti huu, na beti zote na nyingine zilizotangulia, zimenukuliwa kutoka vitabu vya wasifu na historia, hususan zile zinazungumzia Vita vya Ngamia na Siffin. zimenukuliwa na mwanchuoni mtafiti Ibn Hadid katika ukurasa wa 47 hadi ukurasa 50, Jz. 1, ya kitabu chake *Sharh Nahjul Balagha*, chapa ya Misri. Alizinakili beti hizi wakati anaelezea khutba ya Amirul Muminin (a.s.) kuhusu utukufu wa dhuria wa Muhammad (a.s.), ambamo alisema yafuatayo: “Wa oni mfano wa sifa zote za msingi kwa mtawala, na kwao wosia wa Mtume umehifadhiwa,” baada ya kunakili beti zote hizi na mistari ya kusisimua, Allamah Mu’tazili anaongezea: “Beti zenye neno hili *‘Wasii’* ni nyingi sana, lakini tumetaja hapa baadhi tu, hususan beti zile zinazosomwa kwenye Vita vya Ngamia (kama ilivyosimuliwa kwenye kitabu cha Jamal cha Abi Makhnaf) na Siffin kama ilivyosimuliwa kwenye kitabu cha Siffin cha Nasar bin Mudhahim. Mbali na hizi, rejea tulizoacha ni nyingi mno na zisizo na idadi, vinginevyo tungejaza kurasa nyingi zenye kuchosha.”

[416] Imamu al-Iskafi amesimulia katika kitabu chake *Naqd al-Uthmaniyya*, mashairi ya Zafra, na mashairi yaliyotangulia yaliyotungwa na Khuzaymah bin Thabit, na mashairi mawili yaliyotungwa Abdullah bin Abu Sufyan yaliyotangulia haya, yote na yanawasilishwa na Ibn Abul-Hadid mwishoni mwa ufafanuzi wake juu ya khutba ya *qasi’a* katika ukurasa 258 na kurasa zinazofuatia, Jz. 3, ya *Sharh Nahjul Balagha*, chapa ya Misr

Al-Nu'man bin Ajlan mshairi wa Ansar na mmoja wa viongozi wao, alitunga beti[417] hizi zilizoelekezwa kwa Ibn al-Aas anasema:

Mnamdharau Ali ambaye peke yake, kama mnavyojua, au mnavyoweza kuja kulijua hili, ndiye mwenye kufaa zaidi kuteuliwa kama Khalifa.

Kwani yeye, kwa msaada wa Allah, anawaita watu kwenye upande wa haki

Na anawakataza kutenda maovu, maasi na ukaidi.

Yeye ndiye *Wasii* wa Mtume Mteule (s.a.w.w.) na binamu yake,

Muuaji wa askari wa farasi wa ukafiri na upotofu kwenye njia ya haki.

Al-Fadhl bin al-Abbas katika shairi moja[418] amesema:

"Ifahamike kwamba, baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mbora wa watu kwa mujibu wa watu wenye elimu na uelewa ni *"Wasii"* wa Mtume Mteuliwa (s.a.w.w.).

Na ni wa kwanza kutekeleza ibada ya swala, na ni tawi litokanalo na mzizi mmoja pamoja na Mjumbe Allah, Wa kwanza kule Badr kushusha kombora la kifo kwa wale ambao walikuwa wamepotoka."

Hasan ibn Thabit alisoma beti hizi kama msemeji kwa niaba ya Ansar wote ambazo kwazo anamsifu Ali (a.s.). Zilinukuliwa na Zubayr ibn Bakkar katika kitabu chake *Muwaffaqiyyat*, na kunakiliwa na Abul-Hadid katika ukurasa wa 15, Jz. 2, ya kitabu chake *Sharh Nahjul Balagha*:

"Wewe umeyalinda maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) sisi tukiwepo, kwa uaminifu ulitekeleza majukumu aliyokupangia; kwani nani mwingine awezaye kudai kuwa na uhusiano wa karibu zaidi na kufungamana naye kwa mahaba zaidi kuliko wewe?

Wewe siye ndugu yake? Katika mwogozo wa kweli, na *Wasii* wake? Je, sio wewe mwenye elimu bora ya Kitabu cha Allah na Hadithi za Nabii aliyehifadhiwa (s.a.w.w.) kuliko wao?

Mmoja wa washairi alimsifu Hasan (as) kwa kusema:[419]

"Ewe mstahiki heshima wa watu wote! Ewe mtoto wa *wasii!*

Wewe ni mjukuu wa Mtume (s.a.w.w.), na mtoto wa Ali."

Umm Sinan bint wa Khayth'amah bin Kharsha'ah al-Madhhajia katika moja ya mashairi yake yanayomsifia Ali (as) na lililosomwa mbele yake anasema: [420]

"Baada ya Muhammad wewe ulikuwa ndiye Khalifa wetu. Alikuteuwa wewe kama wasii wake muaminifu, na ulitekeleza maelekezo yake yote na ukatekeleza majukumu yake yote."

---

417 al-Zubayr bin Bakar amelinukuu shairi hili katika kitabu chake Muwaffaqiyyadi. Linawasilishwa na mwanachuni wa Mu'tazili katika ukurasa wa 13, Jz. 3, ya kitabu chake Sharh Nahjul Balaghah, lakini Ibn Abd al-Birr ambaye amenukuu shairi hili akielezea wasifu wa al-Nu'man katika kitabu chake Isti'ab, ameuacha ubeti wenye neno 'Wasii' kwa mujibu wa desturi yake maarufu.

418 Ibn al-Athir amezinukuu beti hizi katika maelezo juu ya Uthman, katika ukurasa 74, Jz. 3, ya kitabu chake *Al-Tarikh al-Kamil.* Katika moja ya mashairi yanayofuatia, Fadhl anamwita Ali kama "Mbora wa watu wote," baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

419 Mshairi alizungumza na Hasan ibn Ali (as), kama ilivyonukuliwa na Sheikh Muhammad Ali Hashiishu al-Hanafi al-Saydawi katika tanbihi ya ukurasa 65 wa kitabu chake *Athar Dhawar al-Siwar*, katika maelezo juu ya Ghanima bint Amir na Mu'awiyyah. Shairi hilo lilisomwa mbele ya Mu'awiyyah wakati alipokuwa akizungumza na Hasan.

420 Kama inavyosimuliwa na Imamu Abu Fadhl Ahmad ibn Tahir al-Baghdadi katika maelezo ya Umm Sinan katika ukurasa 67 wa *Balaghat al-Nisa*. Sheikh Muhammad Ali Hashiishu al-Hanafi al-Saydawi vilevile amenukuu mashairi hayo ya Umm Sinan mwishoni mwa ukurasa wa 78 wa kitabu chake Athar *Thawar al-Siwar*.

Haya ni kiasi tu cha mashairi ya wakati uleule wa Amirul Muminin (a.s.) yaliyoweza kunukuliwa kwa haraka haraka. Ukosefu wa nafasi hauturuhusu kuongeza chochote katika orodha hii. Kama tukiyakusanya mashairi yote aliyosomewa Imam Ali (a.s.) au yanayomtaja kama Wasii wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), na ambayo yametungwa baada ya siku zake yeye, hiyo ni mengi sana kiasi cha kuweza kuenea kwenye kitabu kikubwa. Aidha, jaribio kama hilo sio tu litaishia katika kutuchosha bali pia kutusababisha kutoka nje ya mada ya mjadala. Katika kuunga mkono maelezo yetu kwa hiyo, tunanukuu yale mashairi yaliyotungwa baada ya siku za uhai wa Amirul-Mu'minin Ali (a.s.).

Katika shairi lake maarufu, al-Kumait bin Ziyad naye vilevile katika shairi lake amekisifia kizazi cha Hashim:

"Yeye ndiye *Wasii* aliyesaidia kulinda lile paa linaloanguka (la nyumba ya Ummaah), akaliweka sawa na kulisimamisha upya.[421]

Yeye ni sahili, mtukufu na wema, aliyeidhinishwa kufuta au kuimarisha agizo au amri,

Ndiye *Wasii*, na *Walii*, [422] na askari wa farasi shujaa, hana fujo wala sio mvivu.

Yeye ni '*Wasii'* ni *wasii* mwenye dhamira na busara, jitu la mraba kwa maadui zake katika uwanja wa mapambano (na katika medali ya mabishano)."

Kathir bin Abdur-Rahman bin al-Aswad bin Aamir al-Khuza'i, mashuhuri kwa jina la Kathir Azzat, alisema:

"(Ali) Ndiye *Wasii* wa Mtume Mteuliwa na binamu yake.

Mkombozi wa watumwa na mlipaji wa madeni."

Abu Tammam al-Ta'i, katika moja ya mashairi yake anasema:[423]

"Kabla ya hapa mlisababisha huzuni isiyoelezeka na mateso makubwa kwa *'Wasii'* wake;

Mlisababisha matatizo zaidi na mkamuandalia mabalaa mapya juu yake.

Na kuhusu cheo chake alichofadhiliwa, yeye ni ndugu mkwe wake Mtume (s.a.w.w.).

Hapajawahi kuwa na ndugu au mkwe mwenye mahaba na kujitoa muhanga kama yeye.

---

421 Mwanachuoni Sheikh Muhammad al-Rafi'i ameandika tafsiri juu ya mashairi yaliyotungwa na al-Kumait katika kusifia kizazi cha Hashim. Katika maoni yake juu shairi hili anaandika: "Wasii inamaanisha Ali, Allah ameubariki uso wake, ambaye anaitwa *Wasii* kwa sababu Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alimteua kama mtekelezaji wa wosia wake na mrithi wake pia." Katika kuunga mkono hili, yeye ananukuu Hadithi ya Ibn Buraydah ambaye anasimulia kutoka baba yake hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akisema: "Kwa kila Mtume kuna *wasii*, na huyu Ali ndiye *wasii* na mrithi wangu." Al-Tirmidhi, ambaye amesimulia ile hadithi ya Mtume (s.a.w.w.): "Kwa yeyote ambaye anaamini kwamba mimi ni bwana (*mawla*) na kiongozi wake, huyu Ali ni bwana (*mawla*) na kiongozi wake." Al-Bukhari anamnukuu Ibn Sa'd akisema kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) alipokuwa anakwenda kwenye vita vya Tabuk alimteua Ali (a.s.) kuwa khalifa wake hapo Madina, wakati Ali (a.s.) alipomuuliza: "Hivi unaniacha na watoto na wanawake?" Yeye (s.a.w.w.) akasema: "Je, huridhiki kwamba cheo chako kwangu ni kama cheo cha Harun kwa Musa, isipokuwa hakutakuwa na mtume baada yangu?" Rafi'i pia ananukuu shairi la Ibn Qays al-Raqiyyat lenye maana:

"Miongoni mwetu ni Ahmad Mtume, mthibitishaji wa Utume wake. Miongoni mwetu ni mchaji, mwenye hikma; Na Ali na Ja'far mwenye mbawa mbili; ni *wasii*, na mashahidi."

Rafi'I anaendelea kwamba, ilikuwa ni kawaida kumtaja Ali kama '*Wasii*' na kama mfano, ananukuu shairi la mshairi maarufu Kathiir Azzat ambalo tumeliandika hapa.

422 Muhammad Mahmud al-Rafi'i, mfasiri, anaelezea maana maneno ya neno '*Walii*' kama Makamu na khalifa baada ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.).

423 Shairi ambalo mwanzo wake ni: "*Adhabiatun* …..

Alikuwa ndio chanzo cha nguvu za mgongo wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama Haruun alivyokuwa chanzo cha nguvu za mgongo wa Musa (amani juu yao wote)."

**Da'bil ibn Ali al-Khuza'i katika ubeti ufutao katika kumsifu Bwana wa Mashahidi [Imamu Husein (as):**

"Enyi watu! Wakati umegeuka kiasi gani hivi!

Kichwa cha mtoto wa bint wa Muhammad na *wasii* wake,

Ee, enyi watu! Kimenyanyuliwa juu ya mkuki, na watu wote kuona…!"

Abu Tayyib al-Mutanabbi, wakati alipokemewa kuacha kuwasifia Ahlul-Bayt, wakati anapotunga tenzi au mashairi ya kumsifia kila muungwana na kila wa hali ya chini, alijitolea udhuru mwenyewe kupitia utenzi kama ilivyoandikwa kwenye diwani yake, alisema:

"Ilikuwa ni kwa makusudi hasa na sio kwa kupitiwa kwamba nilikwepa kutunga chochote katika kumsifia 'Wasii' kwani yeye ni nuru iliyonyanyuka juu kabisa na mionzi yake imeenea juu ya ulimwengu wote. Kitu kinapopata kilele kisicho cha kawaida, huwa kinajithibitisha chenyewe na kupata kujulikana moja kwa moja kwa wote. Ni kazi bure kuusifia mwanga wa jua (ile miale angavu inayotangaza kuchomoza kwake).

Vilevile alitunga beti zifuatazo katika kumsifia Abul Qasim Tahir bin Husein bin Tahir al-Alawi, na kama ilivyoandikwa vilevile kwenye diwani yake:

"Ni mtoto wa Mjumbe wa Allah na mwana wa Wasii wake, naye ni kama wao.

Nimeleta kufanana kwao, si kwa kubahatisha bali baada ya uzoefu wa muda mrefu."

Beti kama hizi ni nyingi, zisizohesabika zenye kutumia neno Wasii kwa ajili ya Imam Ali (s.a.). Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 109

## RABI'UL THANI 23, 1330 A.H.

Katika Barua yetu ya 19, tulionesha kwamba baadhi ya wenye taasubi ya kidini (ukumbatiaji wa kupindukia) wanasema kwamba ni makosa kunasibisha chimbuko la madhehebu yako, katika mizizi na matawi yake ya dini, hadi kwa Maimamu wa Ahlul-Bayt, na wanaeneza propaganda ya fitina kwamba madhehebu yenu haikubaliani na dini inayofuatwa na Maimam hao, si katika misingi ya imani wala taratibu za kisharia. Binafsi nilikusudia kukuuliza kuhusu suala hili pia. Sasa huu ndio wakati wa swali hili, ondoa shaka yao. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 110

## RABI'UL THANI 29, 1330 A.H.

**I. Imani ya Shi'ah ni kwa Msingi wa Mafunzo ya Maimamu wa Ahlul-Bayt,**

**II. Shi'ah Walikuwa wa Mwanzo Katika Shughuli za Uandishi na Waliandika na Kukusanya Vitabu Wakati wa Kipindi cha Masahaba,**

**III. Walikuwepo Waandishi Wasio na Idadi Wakati wa *Tabi'in,* na Wafuasi wao.**

I. Wale wote waliojaaliwa hikima na busara wanajua kwamba tangu awali hadi sasa Shi'ah Ithna'ashari wamekuwa wakiwafuata Maimam miongoni mwa Ahlul-Bayt katika misingi na matawi ya imani (yaani katika itikadi na vitendo). Wao wana maoni yale yale katika misingi na matawi na katika hukumu na rai zinazohusiana na Qur'ani na hadithi za Mtume (s.a.w.w.) za Maimamu wa kizazi kitoharifu katika kila suala linalohusika kwao au kwenye matawi yote ya sayansi ya teolojia. Hawategemei katika kuelewa kwao sayansi hiyo isipokuwa juu ya kizazi hicho, na hawafanyi rejea kwa yeyote isipokuwa wao. Wanamuabudu Allah Aza wa Jallah, na kuomba ukuruba, yaani radhi Zake Yeye Asiye na mapungufu, kwa imani ya Maimamu wa Ahlul-Bayt, bila kuona upotofu wowote humo, wala hawaoni mbadala wowote mzuri zaidi, na hawako tayari kuihama sera ya wahenga wao wema tangu wakati wa Amirul Mu'minin, Hasan, Husein na Maimumu tisa kutoka kizazi cha Husein (amani juu yao wote), mpaka wakati wetu huu. Miongoni mwa masahaba na wanafunzi wa Maimam walikuwepo Mashia wa kutegemewa wengi, idadi yao kubwa ni wale waliohifadhi hadithi tukufu za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Maimam na kundi kubwa la wale wanaojulikana kwa uchaji, kujizuia, na usahihi. Wale ambao walijifunza kaida na misingi ya dini au waliosikia hadithi na kupata elimu kutoka kwa Maimam kwa uaminifu kabisa, walisimulia yote haya kwa vijana wao ambao nao walikuja baadaye kuwasimulia wadogo zao. Desturi hii imeendelea kwa *tawatur,* kwa kizazi hadi kizazi, mpaka mafundisho hayo ya Maimam yakatufikia sisi yakiwa wazi kama jua la mchana, bila mawingu yoyote yenye kuizuia.[424]

Hivyo, sisi Shi'ah leo hii tuna itikadi ileile kuhusu mizizi na matawi ya imani kama zile za Maimamu kutoka kizazi cha Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Wahenga wetu wamekusanya maelezo ya mafundisho yao hata yale madogo kabisa, wakayahifadhi akilini mwao kwa uaminifu na kuyapitisha neno kwa neno hadi vizazi vilivyowafuata. Tumejifunza maelezo haya kutoka kwa baba zetu waliosikia kutoka kwa baba zao na kuendelea kwa vizazi vyote, katika zama za Imam Hasan Askari na Ali Naqi, Imam Taqi al-Jawaad na Ali Ridha, Imam Musa Kadhim na Ja'far as-Sadiq, Imam Muhammad al-Baqir na Zaynul-Abidiin, Imam Hasan na Imam Husein, wajukuu wa Mtume (s.a.w.w.), amani iwe juu yao wote, na mwishowe Amirul Muminin (a.s.). Leo hii hatuwezi kukisia hata kwa juu juu idadi ya wahenga wetu wa Kishia ambao walipata fursa ya kukaa pamoja na Maimamu wa Ahlul-Bayt (as), wakisikiliza maamrisho ya dini kutoka kwao, wakijifundisha matawi ya ilmu zinazohusiana na Uislamu.

Haiwezekani kufanya uchunguzi wa kutosha kuhusu wao na kuhesabu idadi yao. Lakini unaweza kupata wazo la juu juu kuhusu ukubwa wa idadi yao kutoka kwenye vitabu vya maana vilivyotolewa na wanachuoni wao mashuhuri wa Shi'ah na wafuasi wa Maimam. Waandishi na wakusanyaji hao wa Shi'ah walizama kwenye bahari ya ilmu ya moja kwa moja kutoka kwao, Wakahifadhi walichokisikia kwenye vinywa vyao na walichokipokea kutoka kwenye hotuba zao za moja kwa moja. Vitabu vyao ni ufupisho

[424] Angalizo: *Al-Huda*, Gazeti la Iraq, limenukuu barua hii na kuichapisha katika matoleo yake katika safu iliyosainiwa na mwandishi mnyeyekuvu.

makini na kamilifu wa elimu na taarifa za Maimam waliotoharishwa na hifadhi ya hazina ya hekima zao ambavyo vimeandikwa wakati wa maisha yao, na hivyo vimekuwa rejea kwa ajili ya Mashia kwa taarifa zote za kidini na ambavyo wanavichukulia kama marejeo kwenye mas'ala yote ya kidini. Kutokana na ukweli huu, ubora wa madhehebu ya Ahlul-Bayt ukadhihiri wenyewe dhidi ya madhehebu nyingine za Kiislamu.

Hatujui kama kuna mfuasi yeyote wa Maimamu wane wa Sunni, kwa mfano, ambaye ameandika au kukusanya kitabu juu ya dini kilichoelekezwa na wao wakati wa uhai wa Maimamu hao. Bali, watu bila shaka waliandika vitabu kwa wingi wakishughulika na dini yao, lakini ilikuwa ni baada ya Maimamu hao wane kuondoka duniani. Bado waliamua kwamba *taqlid* (kufuata Mujtahid) kuishie kwa Maimam hao wanne ambao peke yao tu ndio walichukuliwa kuwa ndio mamlaka ya juu kabisa katika kaida za sharia na kumfuata yeyote kati yao ilionekana ni muhimu kwa utekelezaji wa wajibu wa ibada na wokovu wake, hatimaye hakuna wa tano wa kushiriki kwenye fursa hii. Na katika wakati wa uhai wao, hawakuwa ni watu wa sifa mashuhuri, walikuwa hawafaidi sifa yoyote juu ya wengine wa tabaka lao; ndio maana hakuna mtu miongoni mwa rika lao (wanaolingana kielimu) aliyevutiwa katika kufanya juhudi yoyote kukusanya na kuandika maoni yao na hukumu zao katika mas'ala ya kidini, khutba na riwaya zao. Kinyume na juhudi ile kubwa iliyofanywa na Mashia katika kuandika maelezo ya Maimamu Ma'asum (a.s.), moja kwa moja kutoka kwao au kutoka vyanzo vya kuaminika.

Tangu mwanzo kabisa Shi'ah waliona sio sahihi kurejea katika masuala ya dini kwa mtu yeyote mwingine mbali na Maimamu hao waongofu, watukufu. Kwa sababu hii, wao walibaki katika kufungamana tu na Maimam wao na kupokea maagizo juu ya mas'ala ya kidini kutoka kwao tu. Hatimaye walihifadhi katika kumbukumbu zao au katika kuandika maelezo ya mdomo yote ya Maimam hao. Na hili walilifanya kwa ghera kubwa ya hali ya juu na juhudi ili kuzihifadhi riwaya za kisomi na kihekima za Maimam ambazo waliamini kuwa ndio elimu sahihi pekee mbele ya Allah swt. Vitabu vilivyoandikwa wakati wa uhai wa Imamu as-Sadiq (as) peke yake idadi yake ni mia nne vikishughulika na sharia ya dini, ambavyo viliandikwa na wafuasi wake mia nne ambavyo kwavyo waliandika katika wakati wa uhai wake fatwa zake juu ya mas'ala mbalimbali za kidini. Mbali na wafuasi mia nne, masahaba na wafuasi wengine wa as-Sadiq (as) wameandika vitabu vingi, mara nyingi, kama utakavyosikia kwa urefu hivi punde. Insha-Allah.

Amma kuhusu Maimamu wanne wa Sunni, hakuna yeyote aliyewaheshimu wakati wa uhai wao kama ambavyo Maimamu wa Ahlul Bayt (a.s.) walivyoheshimiwa na Shi'ah wakati wa uhai wao kutokana na elimu yao, hekima na uchamungu wao. Sivyo; wao walikuja kuheshimiwa sana baada tu ya kufariki kwao, kama ilivyoelezwa kwa uwazi na Ibn Khaldin al-Maghrabia katika Sura ya *fiqh* (sheria za matendo ya dini) aliyoitoa katika utangulizi wake mashuhuri wa kitabu chake, na ni ukweli unaokubaliwa na wanachuoni wengine wengi mashuhuri. Licha ya yote haya, hatuna shaka kwamba itikadi za Maimam hawa zilikuwa ni zile zile kama zinavyohubiriwa leo hii na wafuasi wao na ambazo zimetekelezwa mwote katika vizazi vilivyofuatana na ambazo zimeandikwa katika vitabu vya wafuasi wao ambao walizijua kwa undani vizuri nadharia za kidini zilizopendekezwa na Maimam wao, kama vile ambavyo Mashia walivyojua vizuri itikadi na kanuni za ibada za Maimamu wao watukufu miongoni mwa Ahlul-Bayt, na ambazo kwazo humuabudu Mwenyezi Mungu kwa usahihi, na kutafuta ukuruba na radhi Kwake pekee swt.

Wanachuoni watafiti wanatambua vizuri kabisa ule ukweli kwamba Mashia walikuwa mbele ya Waislam wengine kwa mbali kabisa katika kuandika matawi ya ilmu. Katika siku za masahaba, hakuna mtu yeyote isipokuwa Ali (a.s.) na wale waliojaaliwa na ilmu miongoni mwa Mashia waliojali kushughulika kuandika kumbukumbu za elimu. Sababu ya hili pengine yaweza kuwa kwamba kulikuwa na maoni mbali mbali

miongoni mwa masahaba kuhusu umuhimu wa kipaumbele cha uandikaji wa ilmu. Kwa mujibu wa Allamah Ibn Hajar al-Asqalaini katika utangulizi wake kitabu *Fath al- Bari,* anaandika kwamba Umar bin Khattab na idadi kadhaa ya masahaba wengine walikuwa wanapingana na wazo la kuweka elimu katika maandishi wakihofia kwamba huenda hadithi zikachanganyika na Kitabu cha Allah, na hatimaye ikawa ni ghasia. Lakini Ali (a.s.), na mwanawe Hasan al-Mujtaba (a.s), na kikundi cha masahaba miongoni mwa wafuasi wake walichukulia kwamba sio tu inaruhusiwa, bali ni kwenye manufaa sana kuiweka elimu katika maandishi. Tofauti hii ya maoni iliendelea katika kipindi chote cha kizazi cha awali. Ilikuwa ni katika wakati wa mwishoni mwa Tabiin ambapo walikubaliana kwa pamoja kuiweka elimu katika kumbukumbu ya maandishi, na Ibn Jariih akakusanya kitabu chake *Al-Athar* (kumbukumbu) kwa msaada wa Mujahid na Ata wakiwa mjini Makka, ambacho Imam Al-Ghazali kwa makosa anadhani ndio kitabu cha kwanza kuandikwa na Mwislamu. Ukweli wa suala hili ni kwamba ni kitabu cha kwanza kilichoandikwa na Mwislamu asiyekuwa Shia. Baada ya hicho Ibn Jariir Mu'ammar bin Rashid, wa San'a, Yemen, aliandika cha kwake, kisha *Muwata* cha Malik kikaandikwa, wa tatu katika waandishi wasiokuwa Shi'ah. Kwa mujibu wa utangulizi wa *Fath al-Bari* al-Rabii bin Sabih alikuwa wa kwanza kukusanya taarifa na kwamba aliishi katika wakati wa mwishoni wa *tabi'in* yaani katika kizazi cha pili. Vyovyote iwavyo, kama wa kwanza kuandika kitabu miongoni mwa wasiokuwa Shi'ah alikuwa ni Ibn Jariir au Rabii makubaliano ya wote pamoja ni kwamba Masunni hawakuandika kitabu hata kimoja wakati wa Masahaba, yaani wakati wa karne ya kwanza ya Kiislamu.

Ama kuhusu Ali na Mashia wake, hawa tangu mwanzo kabisa walianza juhudi kubwa za kunakili elimi kwa maandishi na mkusanyo wa kwanza wa Amirul Muminin Ali (a.s.) ulikuwa ni Kitabu cha Allah, Aza wa Jallah. Akiwa ameshakamilisha ibada zote za mazishi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Ali (a.s.) aliamua kuchukua kazi ya kukusanya Qur'ani kabla ya kushughulika na jambo jingine lolote. Kwa hiyo, aliikusanya na kuipanga katika mpangilio wa mahali na wakati wa kushuka kwake. Alionesha maana zake za makhususia kutoka kwenye jumla, za dhahiri na zenye kufichika, zenye kufanana kutoka kwenye za kiistiari, zenye ufutaji na zenye kufutwa, msisitizo muhimu na zenye umuhimu wa kawaida, maamrisho ya dini na maagizo ya kimaadili. Akionesha mazingira na sababu za kushuka kwa aya kadhaa zenye maana ya dhahiri. Pia alielezea zile aya ambazo kwa sababu moja au nyingine zilikuwa ni ngumu kueleweka. Ilikuwa ni kwa sababu ya sura hizi maalum za Qur'ani iliyokusanywa na Imam Ali (a.s.) ambapo Ibn Sirin alikuwa mara kwa mara akisema: "Kama tungeweza kuipata Qur'ani aliyokusanya Imam Ali (a.s.), basi tungeona humo ilmu nyingi." Hii inadondolewa na Ibn Hajar katika kitabu chake Al-*Sawaiq al-Muhriqa*, na waandishi wengine wengi maarufu. Masahaba mbalimbali walichukua uzito wa kukusanya Qur'ani Tukufu, lakini hawakuweza kuikusanya katika mpangilio wa kushuka kwake, wala mazingira na sababu ya kushuka kwake, ambazo zinaipamba ile Qur'ani iliyokusanywa na Imam Ali (a.s.). Hivyo Qur'ani iliyokusanywa na Ali ikiwa ni zaidi kuliko ile ya kukusanya tu, kwani ilikuwa na sherehe na ufafanuzi pia.

Wakati akiwa amemaliza kukifanyia kazi Kitabu cha Allah, aliandika kitabu ambacho alikitoa wakfu kwa Bibi wa Mabibi wa ulimwengu. Kilikuja kujilikana kwa watoto wake watoharifu tu kama *"Mus'haf Fatima,"* ambacho kinajumuisha semi za kweli (ambazo hazina ubishani), vipande vya hikima, na ushauri, maadili, hadithi muhimu na maelezo ya matukio na mambo ya kipekee. Alikiandika kwa kumpatia maliwazo Bibi Fatimah (s.a.) kwa ajili ya huzuni yake baada ya kuondokewa na baba yake Mtume adhimu (s.a.w.w.), Bwana wa Mitume wote. Baada ya hicho aliandika kitabu kinachoshughulika na fidia ya damu ambacho alikiita *Al-Sahifa.* Kinatajwa na Ibn Sa'd mwishoni mwa kitabu chake kinachoitwa *Al-Jami* kikitoa sifa ya uandishi kwa Amirul Muminin. Wote Bukhari na Muslim wamerejea katika kitabu hiki na kuchukua idadi kadhaa ya hadithi kutoka humo na kuzinakili kwenye *Sahih* zao. Miongoni mwa

simulizi zao ni kile ambacho wamenukuu kutoka kwa al-A'mash kutoka kwa Ibrahim al-Taymii ambaye anamnukuu baba yake. A'mash anasema kwamba, Ali (a.s.), siku moja alisema: "Mbali na Kitabu cha Allah, Qur'ani, hatuna kitabu kingine cha kusoma isipokuwa hiki *Sahifa*." Kisha akakitoa kitabu hicho ambacho ndani yake mna masuala yanayohusiana na vidonda na meno ya ngamia. Vilevile miongoni mwa yaliyomo ni maelezo yanayosomeka hivi: 'Madina ni sehemu takatifu (kutoka Ayr mpaka Thawr); yeyote mwenye kuunajisi, au kumhifadhi mwenye kuunajisi, atapata laana ya Allah, malaika, na watu.'"

Haya ni maneno ya Bukhari katika Mlango wa "Dhambi za wanaowakataa *Mawalii* wao," katika *Kitabul Faradh*, uk. 111, Jz. 4, wa *Sahih* yake, na inatajwa katika Mlango wa "Ubora wa Madina," katibu cha Hijja katika ukurasa wa 523, Jz. 1, ya *Sahih Muslim*. Imamu Ahmad bin Hanbal amerejea mara kwa mara kwenye *Sahifa* hii katika kitabu chake cha *Musnad*. Ananukuu hadithi ya Ali (a.s.) katika ukurasa wa 100, Jz. 1, ya *Musnad,* kutoka kwa Tariq bin Shihab ambaye anasema: "Nimemshuhudia Ali (a.s.) akiwaambia watu kutoka juu ya mimbari: 'Kwa jina la Allah! Hatuna cha kuwasomea mbali na Kitabu cha Allah Aza wa Jallah na hii *Sahifa*,' ambayo alikuwa ameichomeka kwenye upanga wake, 'nimejifunza yaliyomo humu kutoka kwa Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.).'"

Akimnukuu Abdul-Malik, al-Saffar anasimulia: "Abu Ja'far (Imam Muhammad Baqir) aliomba aletewe kitabu cha Ali, na mtoto wake Ja'far alileta kitabu hicho kikubwa kwa baba yake. Kilikuwa kimetengenezwa katika umbo la paja la mwanadamu. Miongoni mwa yaliyomo humo ni maneno: 'Kama mwanamume anakufa, mke wake hatarithi chochote katika vitu vyake visivyohamishika.' Abu Ja'far akasema: 'Kwa jina la Allah huu ni mwandiko wa Ali (a.s.) na imla ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.)!'" Kikundi cha Mashia ambao walikuwa rika moja na Imamu Ali (a.s.) walifuata nyayo za Amirul Muminin (a.s.) na wakaandika idadi ya vitabu wakati wa uhai wake. Miongoni mwa waandishi hao walikuwa: Salman al-Faris na Abu Dharr al-Ghifari, kama ilivyoelezwa na Allamah Ibn Shahr Ashub ambaye alisema: "Muislamu wa kwanza kuandika kitabu ni Ali bin Abu Talib (a.s.) kisha Salman al-Farsi kisha Abu Dharr – radhi za Mwenyezi Mungu juu yao."

Miongoni mwa Shi'ah hao ni Abu Rafi, mtumwa aliyeachwa huru na Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.), na aliyekuwa mweka hazina (*Baytul mal)* wakati wa utawala wa Amirul Muminin (a.s.). Alikuwa miongoni mwa wafuasi wake wakuu wenye uwezo ambao walitambua cheo na ubora wake. Aliandika kitabu kinachoshughulika na amri za dini, hadithi Tukufu za Bwana Mtume (s.a.w.w.) na hukumu za kisheria zilizotegemea moja kwa moja kwenye hadithi zilizosimuliwa na Ali. Kitabu hicho kilifaidi hadhi ya juu sana miongoni mwa wahenga wetu ambao walikitumia kama chanzo cha nukuu na hadithi. Miongoni mwao ni Ali bin Abu Rafi'i ambaye kwa mujibu wa wasifu wake katika *Isaba* ya Ibn Hajar Asqalani*,* yeye alizaliwa wakati wa uhai wa Mtume (s.a.w.w.) ambaye alimpa jina la Ali. Aliandika kitabu juu ya sayansi ya theolojia na *fiqh* kwa mujibu wa mafundisho ya Ahlul-Bayt (a.s.) ambao walikuwa wakikipenda na kukiheshimu mno kitabu hicho na waliwaambia Mashia wao warejee kwenye kitabu hicho na kukifuata kivitendo. Musa bin Abdullah bin Hasan anasema: "Mtu mmoja alimuuliza baba yangu kuhusu *tashahud*. Baba akaniambia nikalete kitabu kilichoandikwa na Abu Rafi, alikichukua akatusomea majibu kutoka humo." Kwa mujibu wa mkusanyaji wa *Rawdhat al-Jannat* kitabu hicho kilikuwa kitabu cha kwanza kinachoshughulika na theolojia na *fiqh* ya Mashia, lakini yeye, Allah amhurumie, kwa hakika alikosea.

Miongoni mwao ni Ubaydullah bin Abu Rafi, aliyekuwa mwandishi wa Ali (a.s.) na mmoja wa wafuasi wake wakuu. Alisikia hadithi kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) na akazisimulia hadithi hizo kwake. Ni yeye aliyesimulia ile hadithi Tukufu kuhusu Ja'far: "Muonekano na mwenendo wako ni sawa sawa na mimi." Hii imenukuliwa na wasimuliaji wa hadithi kutoka kwake. Ahmad bin Hanbal ameiandika katika kitabu chake '*Musnad*' na Ibn Hajar ameinakili katika Jz. 1 ya kitabu chake *Isaba* chini ya kichwa cha habari: "*Ubaydullah bin Aslam*," kwani Aslam lilikuwa ni jina binafsi la Abi Rafi, baba yake Ubaydullah. Huyu

Ubaydullah vilevile aliandika kitabu ambamo humo alitaja na kutoa maelezo juu ya masahaba wa Ali (a.s.) ambao walipigana katika Vita vya Sufin upande wake, ambamo kutoka humo Ibn Hajar amechukua nukuu na vipande vya habari kwa wingi sana katika kitabu chake *Isaba*; [425] ambacho unaweza kukirejea.

Vilevile miongoni mwao ni Rabi'ah bin Samiiy ambaye alikusanya kitabu kinachoshughulika na Zaka juu ya mifugo kutoka kwenye hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambayo imesimuliwa na Ali (a.s.). Katika hao kulikuwa pia na Abdullah bin al-Hurr al-Farisi ambaye alikusanya kitabu cha hadithi, "*Lama*," ambamo amekusanya hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zenye kumeremeta zote kama zilivyosimuliwa kutoka kwa Ali (a.s.). Na miongoni mwao ni Asbagh bin Nabatah, mfuasi na mwanafunzi wa Imam Ali (a.s.) ambaye alidumu kuwa mtiifu kwake (a.s.) mpaka kufariki kwake. Ni yeye ambaye amenukuu barua ya mkataba wa uteuzi wa Imamu kwenda kwa Malik al-Ashtar na wosia wake kwa mwanawe Muhammad. Zote zimeandikwa na jamaa zetu katika Sahih zao moja kwa moja kutoka kwa Asbagh bin Nabatah.

Alikuwepo Salim bin Qays al-Hilali, sahaba wa Ali (a.s.), ambaye ananukuu hadithi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama zilivyochukuliwa kutoka kwa Imam Ali na Salman al-Farsiy. Aliandika kitabu kinachoshughulika na Uimamu ambacho kimetajwa na Imamu Muhammad bin Ibrahim al-Nu'mani katika kitaba chake *Al-Ghayba*, akisema:

> "Shi'ah wote waliopata elimu kutoka kwa Maimamu au kupokea hadithi kutoka kwao wanakubaliana na ukweli kwamba kitabu kilichoandikwa na Salim bin Qays al-Hilali ni moja ya vitabu vikubwa na vya mwanzoni kabisa juu ya *usuul* (misingi ya dini) ambacho kutoka humo wanachuoni na wasimuliaji wa hadithi kutoka kwa Ahlul-Bayt wamenukuu, na ni moja ya chanzo kikubwa ambacho kwacho Mashia hukirejea na juu yake hukitegemea kwa mwongozo."

Kwa habari yoyote zaidi juu ya waandishi na wakusanyaji wa vitabu wa kizazi cha kwanza (yaani cha masahaba) unaweza kurejea kwenye vitabu vyao na orodha ya majina yao na maelezo binafsi juu yao kama yalivyoandikwa na waandishi wa Shi'ah wa baadaye.

Ama kuhusu waandishi na wakusanyaji wa Shi'ah miongoni mwa wahenga wetu wa kizazi cha pili, yaani, cha *tabi'in*, walikuwa ni wengi mno kuweza kuwataja hapa. Kwa orodha kamili ya waandishi hao, orodha ya vitabu vyao na vyanzo vyao vya habari na maelezo yao kwa urefu, tafadhali rejea kwenye orodha zao zilizokusanywa na wanachuoni wetu.[426]

Katika kipindi hiki cha Tabiin, nuru (ya elimu) ya Ahlul-Bayt (a.s.) iling'ara, ambapo ilikuwa mwanzoni ilizuiwa na mawingu ya ukandamizaji na ukatili wa madhalimu. Lakini ule msiba mkubwa wa Karbala uliwafichua wazi maadui wa kizazi cha Mtume (s.a.w.w.), na kuwashusha na kuwadhalilisha mbele ya macho ya wenye busara ambao waligeuzia nadhari zao kwenye janga lililowaangukia Ahlul-Bayt (a.s.) juu ya kumpoteza Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) kwa kifo chake. Hii iliwapa shauku ya kuchunguza mambo na kuweza kujua sababu za mateso na shida hizo za Ahlul-Bayt. Hawakupata shida katika kugundua sababu ya msingi na mbegu hiyo ya mateso na dhiki kubwa. Wale Waislam wanaojiheshimu walishawishika kulinda heshima na kuitetea hadhi ya Ahlul-Bayt (a.s.) na kuchukua kisasi kwa maadui zao, kwa sababu ni tabia ya mwanadamu kuwahurumia na kuwasaidia wenye kuonewa na kuwachukia waneovu. Hivyo msiba huu mkubwa wa Karbala, ambao uliwafungua macho Waislamu, uliwafanya watambue haki yao ya kuzaliwa, ukatingisha ulegevu wao na wakatokomeza utii wao usio na msingi kwa viongozi wao madhalimu, wakaingia katika zama mpya katika historia ya Waislam, ambao sasa wakamiminika hima kumzunguka Imamu Ali ibn Husein Zainul-Abidin (a.s), kwa utii na ufuasi kwake. Wakawa wanarejea na kutegemea kwake katika maelekezo kuhusiana na mizizi (*usuul*) na matendo ya imani na masuala yote

[425] Maelezo juu ya Jubayr bin al-Habab bin al-Mundhir al-Ansar katika Juz. 1, ya *Al-Isabah.*

[426] Kama vile faharisi ya Najashi, Sheikh Abu Ali *'Muntahal Maqal'* na '*Minhajul Maqal'* cha Mirza Muhammad, na vitabu vingi vingine vinavyoshughulika na tawi hili la elimu.

ya dini kutoka kwenye Kitabu na Sunnah. Baada ya kifo chake wakawa wameshikamana na mtoto wake Imamu (Muhammad) Abu Ja'far al-Baqir (a.s.). Kulikuwa na mamia ya maelfu ya wanafunzi na wafuasi Shi'ah wa Maimamu wote hawa, yaani Zainul-Abidin na al-Baqir (a.s.). Idadi yao hasa ni vigumu sana kuithibitisha. Miongoni mwao wamo takriban wanachuoni maarufu elfu nne ambao majina na maelezo yao kwa ufupi yamehifadhiwa katika vitabu vya wasifu na vitabu vyao ni elfu kumi au zaidi. Wasimuliaji wetu waliofuatia, wametegemea na kunukuu hadithi kutoka kwao. Baadhi ya wanachuoni mashuhuri hao ambao waliishi maisha marefu zaidi walipata bahati nzuri ya kukaa na Imamu as-Sadiq (a.s.) pia na kupata manufaa zaidi. Walikuwa wameshika nafasi za juu kabisa katika elimu na matumizi yake miongoni mwa waandishi wa zama zao.

Miongoni mwao alikuwa Abu Sa'id Aban bin Taghlib ibn Rabah al-Jarir aliyekuwa msomaji maarufu wa Qur'ani (kwa kughani), msimuliaji wa Hadithi, mfasiri wa Qur'ani, mwanafasihi na mtaalamu wa lugha ambaye alikuwa mmoja kati ya wanachuoni wanaoaminika aliyepata fursa ya kukaa na Maimamu watatu ambao kutoka kwao alipata ujuzi mkubwa sana na idadi kubwa sana ya hadithi ambavyo aliwafundisha watu wengine. Itoshe tu kwako ukweli kwamba alisimulia kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) peke yake hadithi elfu thelathini,[427] ambazo aliziandika na kuzisimulia kwa wengine, kama ilivyoandikwa na al-Mirza Muhammad katika maelezo yake juu ya Aban katika kitabu chake *Muntahal-Maqaal* akinukuu vyanzo sahihi vya taarifa zake hadi kwa Aban bin Taghlib ambaye amepokea kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) mwenyewe. Maimam wote watatu walionyesha heshima kubwa juu yake. Imamu al-Baqir (a.s.) alisema kuhusu yeye wakati walipokuwa wote katika mji wa mtukufu Mtume wa Madina: "Chukua nafasi yako msikitini na toa hukumu (*fatwa*) zako kwa watu kwani napenda kuona miongoni mwa Mashia wangu watu kama wewe." Imamu as-Sadiq (as) alimuambia: "Jadiliana na watu wa Madina (katika mambo ya dini), kwani napenda kuona watu kama wewe miongoni mwa wasimuliaji na wafuasi wetu." Wakati wowote anapokuja Madina watu walimjia kwa idadi kubwa na kumuandalia sehemu ya kukaa mahali palepale ambapo Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akikaa. Imamu as-Sadiq (a.s.) alimuambia Salim bin Abu Habbah: "Mtembelee Aban bin Taghlib, kwani yeye amejifunza idadi kubwa ya hadith kutoka kwangu, na unaweza na wewe pia ukisimulie kutoka kwangu chochote atakachokusimulia." Yeye (a.s.) akamuambia Aban bin Uthman: "Aban bin Taghlib amepokea kutoka kwangu hadithi elfu thelathini, hivyo unaweza kuzisimulia kutoka kwake." Wakati wowote Aban bin Taghlib alipomtembelea Imamu as-Sadiq (a.s.), Imamu humkumbatia na kumpa mkono na huamuru apewe mto wa kuegemea, na kumjali kikamilifu. Wakati taarifa za kifo cha Aban zilipoletwa kwake, yeye (a.s.) alisema: "Naapa kwa Jina la Allah! kifo cha Aban kimeumiza sana sana moyo wangu." Alifariki mwaka wa 141 A.H.

Aban amesimulia kutoka kwa Anas bin Malik, al-A'mash, Muhammad bin al-Munkadir, Sammak bin Harb, Ibrahim al-Nakha'i, Fadhiil bin Umar na al-Hakim. Ametegemewa na Muslim na wakusanyaji wengine wa *Sihah* nne za hadithi, wote wamezichukua hadithi zake kama tulivyoeleza katika Barua ya 16. Japo Bukhari hakunakili kutoka kwa Aban katika kitabu chake, hilo halidhuru kitu na si la kushangaza, kwani kila mtu anajua kwamba (Bukhari) alikuwa na mwenendo wake binafsi dhidi ya Maimamu wa Ahlul-Bayt (as) kama vile al-Sadiq, al-Kadhim, al-Ridha, al-Jawad, al-Taqi na al-Hasan al-Askari al-Zaki (a.s.). Bukhari hakuepuka tu kunukuu hadithi kutoka kwa Maimam hawa, hasha, bali pia alijizuia kuandika na kusimulia hadithi yoyote iliyosimuliwa na mjukuu mkubwa wa Mtume (s.a.w.w.), Bwana wa vijana wa Peponi, Hasan bin Ali (a.s.)! Kwa upande mwingine, alitegemea juu ya kunakili riwaya kama zilivyosimuliwa na watu kama Marwan bin Hakam, Umran bin Hattan, Ikramah al-Barbari na watu kama hawa. **"Hakika sisi sote ni wa Allah na Kwake ndio marejeo yetu."**

[427] Imedokezwa hivyo na mabwana wengi wa Simulizi kama vile Sheikh al-Baha'i katika kitabu chake *Wajiiza,* na wanachuoni wa Kiislam wengine mashuhuri wameisimulia hii.

Aban ameandika vitabu vya kadhaa vya maana sana. Kimojawapo ni Tafsri *Gharib al-Qur'ani*, ya aya za kipekee za kuvutia mno ambazo zimeelezwa na kuthibitishwa zaidi na nukuu nyingi za beti za mashairi ya Kiarabu. Baadaye Abdur-Rahman bin Muhammad al-Azadi al-Kufi alikusanya yaliyomo kwenye kitabu cha Aban, cha Muhammad bin as-Sayib ul Kalabi na cha Rauq Atiyya bin al-Harith na kuyachapisha katika kitabu kimoja akisisitiza mitazamo ya waandishi hawa watatu katika yale ambayo wanahitalifiana miongoni mwao wenyewe, na halikadhalika katika yale wanayokubaliana. Waandishi wetu walitegemea na kunukuu mara kwa mara kutoka katika vitabu hivi, mara kitabu cha Aban huja kikiwa peke yake, na mara huwa katika mkusanyo wa Abdur-Rahman. Miongoni mwa vitabu vingine vya Aban ni "Al-Fadhail," "Sifiin" na kitabu juu ya itikadi za msingi za Uislam ambacho Shi'ah wanakichukulia kama marejeo ya kuaminika juu ya amri za kidini. Kwa taarifa zaidi kuhusu vitabu vingine vya Aban tafadhali rejea vitabu vya wasifu.

Miongoni mwao ni Abu Hamza al-Thamali, Thaabit bin Dinar. Alikuwa miongoni mwa wanachuoni wa kutegemewa na waaminifu na mwenye heshima miongoni mwa wahenga wetu. Alipata elimu yake kutoka kwa Maimamu watatu: Imamu Zainul-Abidin (a.s.), Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) na Imam as-Sadiq (a.s.). Alikuwa mfuasi mtiifu na wa karibu nao, na akapata heshima kwao. Imam as-Sadiq alimsifia akisema: "Katika zama zake, Abu Hamza ni kama alivyokuwa Salman Farsiy wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mwenyewe." Na Imam Ridhaa (a.s.) amemsifu akisema: "Abu Hamza ni Luqman wa zama zake mwenyewe." Ameandika kitabu cha Tafsir ya Qur'ani. Imamu al-Tabris amemnukuu kwa uhuru na mara nyingi tu katika tafsri yake iitwayo *Mujma'al Bayan fi Tafsir al-Qur'ani*, [428]

Vilevile miongoni mwa vitabu vyake vingine ni "*Kitab un Nawadir*," kingine "*Kitab uz-Zuhdi*" na "*Risalat ul Huquuq*."[429]

Vitabu hivi viko juu ya msingi wa mafundisho ya Imamu Zainul-Abidin Ali bin Husein (a.s.). Kutoka kwake amesimulia maombi yake mwenyewe yaliyosomwa mwanzoni mwa mapambazuko ya asubuhi ambayo hung'ara kwa weupe kuliko jua na mwezi. Vilevile alisimulia hadithi Tukufu kama zilivyosimuliwa na Anas bin Malik na al-Sha'bi. Na yeye ananukuliwa na Waki'i, Abu Na'iim na Shi'ah na Sunni wa rika lao ambao pia wamenukuu kutoka kwake, kama tulivyoeleza katika wasifu wake katika Barua ya 16.

Kuna waandishi wengine wengi maarufu wa Shi'ah wa umri mdogo ambao hawakumuona Imamu Zaynul-Abidin lakini walipata heshima ya kuhudhuria vikao vya Maimam Muhammad al-Baqir na Ja'far as-Sadiq, amani iwe juu yao wote.

Miongoni mwao ni Abdul-Qasim Bariid bin Mu'awiyah al-Ajali, Abu Basiir Layth bin Muraad al-Bakhtari al-Muradi, Abul Hasan Zararah bin Aayun, Abu Ja'far Muhammad bin Muslim bin Rabah al-Kufi al-Ta'ifi al-Thaqafi na mbali na hao, kulikuwa na bendera nyingine nyingi za mwongozo na minara ambayo inaangaza katika giza katika zama zao. Kutoa maelezo zaidi juu yao au kuwataja wote kwenye nafasi hii ndogo hapa haiwezekani. Ama kuhusu hawa waandishi wanne waliotajwa hapo juu, kwa hakika walikuwa maarufu sana kiasi cha kupata hadhi kubwa maalum miongoni mwa wengine wa rika au zama zao. Wakati fulani Imamu alipowataja alisema: "Sijaona mtu ambaye ameliweka jina letu hai kama Zararah, Abu Basiir Layth, Muhammad bin Muslim na Bariid; bila wao hakuna mtu ambaye

[428] Rejea kwenye kitabu cha *Mujma ul-Bayan fi Tafsir Qur'ani* cha al-Tabris katika sehemu inayoshughulika na tafsir ya aya: **"Sema: Kwa haya siombi malipo yoyote kwenu isipokuwa mapenzi kwa ndugu (kizazi Changu)…(Qur'ani 42:23),** na utamuona amenukuu kutoka tafsir ya Abu Hamzah mwenyewe.

[429] Wanachuoni wetu wamenukuu kutoka kwenye vitabu vyote vya Abu Hamzah wakitaja vyanzo hadi kwake. Kwa maelezo zaidi angalia kwenye vitabu vya wasifu. Mwanachuoni wetu mheshimika Sayyid Sadr ad-Din al-Musawi aliandaa na kuchapisha toleo fupi la *Risat al-Huquuq* ili kutengeneza mwanzo bibliografia ya Kiislam. Lengo lake juu ya toleo hilo fupi lilikuwa ni kuwawezesha Waislamu kupata manufaa makubwa zaidi kutokana na kitabu hicho.

angefaidika kiasi hicho na elimu na mwongozo wetu.” Kisha akaongeza: “Hawa ni walinzi wa imani ambao ni waaminifu wa baba yangu kuhusu kulinda yale ambayo Allah ameamuru kama halali na pia yale ya haramu, Na wako mbele ya wengine katika kutufikia sisi katika maisha ya Akhera.” Wakati mmoja yeye (a.s.) alisoma aya hii:

وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ

**“Na wabashirie wanyenyekevu (ambao wanaomba kwa ajili ya kuipata Pepo Yetu) (Qur’ani 22:34).”** Na alifuatishia kisomo chake hicho kwa kuwataja watu hawa wanne, huku akiongezea katika maelezo marefu akiwasifia: “Baba yangu aliwaaminisha katika kutekeleza masuala ambayo Mwenyezi Mungu ameyahalalisha na aliyoharamisha. Walikuwa walinzi wa elimu ya baba yangu; walikuwa wafuasi wakweli wa baba yangu na leo wana nafasi ileile kwangu mimi; ni wasiri wangu na nyota angavu za muongozo wa Mashia wetu wakiwa hai au wakiwa wamekufa. Kupitia kwao Allah ataweka wazi kila uzushi (*bid’a*) na ubadilishaji katika imani na dini kutokana na uwongo wa wazushi na tafsiri za wenye kuvuka mipaka, na watawapinga na kuwaondoa hawa, na watabatilisha uelewa mbaya na tafsiri potofu (za Qur’ani na Sunnah) za wazushi, yaani za waliopotoka katika njia ya haki.”

Kuna hadithi nyingi nyingine mashuhuri za Imam zinazozungumzia elimu yao pana, moyo mkunjufu, ukarimu na uaminifu kama wafuasi. Kwa kweli katika muhtasari huu hatuwezi kutoa maelezo yao yote kutokana na ufinyu wa nafasi. Lakini licha ya sifa na ubora wote huu walishutumiwa na maadui wa Ahlul-Bayt (a.s.) kwa kila shutuma ya uongo dhahiri iwezekanayo, kama tulivyoeleza katika kitabu chetu “*Mukhtasar al-Kalam fi Mu’allifi al-Shi’ah min Sadr al-Islam.*” Hakuna kiwango chochote cha shutuma kitakachoshusha hadhi yao hiyo ya hali ya juu na umuhimu wao mkubwa mbele ya macho ya Allah Aza wa Jallah, Mjumbe Wake na Waumini. Wale ambao wanamuonea kijicho Mtume (s.a.w.w.) hawakuweza kuwadhuru chochote au kuvunja au kubadilisha hukumu zao za kidini. Bali, badala yake imekuwa ni chanzo cha kunyanyua tu hali ya juu ya hadhi zao, na uenezi na umaarufu wa dini yao miongoni mwa wale ambao wamejaaliwa hekima.

Wakati wa uhai wa Imam as-Sadiq (a.s.) elimu ilipata mendeleo makubwa kuliko ilivyokuwa kabla ya hapo. Mashi’ah wa baba zake (a.s.) walikimbilia kwake kutoka kila upande, mbali na karibu, na Imam aliwapokea kwa ukarimu mkubwa na kuwafanyia wema, na alifanya kila juhudi kuwaelimisha. Alifanya juhudi pia kwa kiasi alivyoweza katika kuwashehenisha siri za ilmu, mambo ya hekima na uhalisia wa mambo na matukio, kama ilivyoelezwa na Abul-Fatah al-Shahristani katika kitabu chake *Al-Milal wal Nihal*. Wakati akizungumza kuhusu Imamu as-Sadiq (a.s.) yeye anasema: [430]

> “Ni mtu aliyekuwa na ilmu kubwa ya dini na hikma nyingi mno. Alitelekeza kikamilifu kabisa dunia na kuzipa nyongo anasa zake na aliye jiepusha kabisa na maslahi binafsi.”[431]

Vilevile ameendelea kuandika kuhusu yeye: “Alikaa Madina kwa muda mrefu kiasi akiwasaidia Mashi’ah watiifu na kuwanufaisha wafuasi wake kwa kuwafundisha wingi wa siri za ilmu. Kisha alikwenda Iraq na akakaa huko kwa muda mrefu. Kamwe hakulalamika dhidi ya uongozi na watawala wala hakuwa na uchu wa mamlaka wala hakuingia kwenye mzozo wa Ukhalifa na mtu yeyote yule.” Anaongeza kusema: “Pwani haina bashasha na yeyote yule azamaye katika bahari ya ilmu na umaizi. Na yeyote apandaye kwenye kilele cha elimu fulani na ukweli kamwe haogopi kuanguka, kashfa au kuonekana kama dhaifu.” Mpaka mwisho wa maelezo yake.

[430] Tafadhali rejea kwenye maelezo juu ya Imam Muhammad al-Baqir na Ja’far as-Sadiq (amani juu yao) chini ya kichwa “Madhehebu ya Shi’ah” katika kitabu chake “*Al-Milal wan-Nihal*.”

[431] Alifanya hivyo alipotaja *Baqiriyya* na *Ja’fariyya* miongoni mwa madhehebu ya Shi’a katika kitabu chake *Al-Milal wal-Nihal*.

"Na ukweli unatamkwa na watu wote waadilifu na wakaidi." Idadi kubwa ya wafuasi na wanafunzi wa Imamu as-Sadiq (a.s.) walikuwa mbele katika elimu juu ya wanachuoni wengine wa zama zao. Walikuwa viongozi wa njia ya haki, taa katika giza, bahari ya elimu na nyota za mwongozo. Miongoni mwa wale ambao majina yao na wasifu wao umeelezwa katika vitabu vya wasifu na orodha za vyanzo ni watu elfu nne kutoka Iraq, Hijaz, Uajemi na Syria. Wote hawa wameandika vitabu ambavyo ni mashuhuri sana miongoni mwa Shi'ah. Miongoni mwao ni vitabu mia nne vya misingi ya imani tu ambavyo ni kazi ya waandishi mbalimbali mia nne kama ilivyokwisha kuelezwa. Vyote vikiwa vimeandikwa wakati wa Imam as-Sadiq (a.s.) na kulingana na fatwa (hukumu) zake za kidini. Baada ya Imam, Shi'ah walitegemea vitabu hivi kwa ajili ya taarifa juu ya nadharia na vitendo vya dini yao, kiasi kwamba kundi la wanachuoni mashuhuri wa Shi'ah wakavifanyia mukhtasari na maelezo mafupi katika vitabu maalumu ili kusaidia ufahamu wao kwa wenye kutafuta taarifa kuhusu nadharia na vitendo vya madhehebu ya Shi'ah na kuvifanya viweze kusomwa zaidi. Vilivyo bora miongoni mwa mkusanyo huo ni vitabu vine ambavyo ni vyanzo vikubwa kwa Mashi'ah juu ya mizizi na matawi ya imani na itikadi yao. Wamekuwa wakivirejea tangu zama za Imam as-Sadiq hadi leo hii, navyo ni hivi: *Al-Kafi, Al-Tahdhib, Al-Istibsar* na *Man la yahdhurul Faqih*. Vyote vimesimuliwa kwa mfululizo wa moja kwa moja, na usahihi wa yaliyomo haujatiliwa mashaka. *Al-Kafi* ni cha zamani, kina hadithi 16,199 ambazo zinazidi kile kiasi ambacho sasa kipo katika jumla ya sahih Sitta – *al-Sahih Sitta* za Sunni, kama alivyokiri al-Shahid katika kitabu chake *Al-Dhikrii* na wanachuoni wengine kadhaa mashuhuri.

Hisham bin al-Hakam mmoja wa wafuasi na mwanafunzi wa Imam as-Sadiq (a.s.) na al-Kadhim (a.s.), aliandika vitabu vingi, tisini na tisa kati ya hivi vikiwa ndio muhimu zaidi kuliko vinginevyo na ambavyo wanachuoni wetu na waandishi wanavitumia kama vitabu vya rejea na kuvichukulia kama vyanzo muhimu. Maelezo ya vitabu hivi yamo katika kitabu changu "*Mukhtasar al-Kalam fi Muallifi al-Shi'ah min Sadri al-Islam.*" Vyote ni vitabu vya kuvutia, kung'ara katika ubayana wa maandiko yao na kung'ara kwa hoja zao zenye uwazi mkubwa na mwanga. Vinashughulika na maeneo mbalimbali kama – mizizi ya dini na matawi, kaida za dini pamoja na *tawhid* na filosofia ya mantiki; vitabu hivyo hupinga na kukanusha imani ya washirikina, waasi wa dini, wanaviumbe, wana-majaliwa na kadara na ukafiri kwa ujumla, na pia wale ambao wanakuza au kupiga chuku imani juu Ali (as) na Ahlul-Bayt (a.s.) (kama vile kusema Ali ni Mtume au mungu nk.). Vilevile huwakanusha na kuwapinga Makhawarij na Manasib, (waliompiga vita kule Sufin, vita vya Ngamia na Nahrawan) wale ambao wanakataa kwamba Mtume hakuacha wosia kuhusiana na urithi wa Ali (a.s.), na waliompiga vita Ali na Ahlul-Bayt (amani juu yao wote), na wale ambao walikubali Ali kutanguliwa kama Khalifa na wengine kuliko yeye, na kupinga ile imani kwamba inaruhusiwa kupewa kipaumbele wasiofadhiliwa juu ya wenye kufadhiliwa n.k.

Hisham alikuwa miongoni mwa wajuzi wa ilmu zaidi wa karne ya pili Hijiria. Alikuwa ni bingwa katika elimu ya kuwezesha thibitisho za kisayansi za imani za kitheolojia, falsafa ya utukufu wa kimungu na matawi mengine ya elimu ya kisayansi na mapokezi ya kuhusu dini. Alikuwa mashuhuri katika *fiqh* na hadith, akiwa anampita kila mtu wa wakati wake katika tafsir na sayansi nyingine zote na sanaa. Alikuwa ni yeye ambaye alijadili dhana ya Uimamu kwa mafanikio mno na hivyo kuitangaza dini yake. Alipokea kutoka kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) na Imamu al-Kadhim (a.s.), ambao walimheshimu na kumsifu sana. Hii inaashiria cheo chake na hadhi yake katika elimu, uchamungu na huduma zake katika dini. Kabla ya kukutana na Imamu as-Sadiq (a.s.) alikuwa katika madhehebu ya *Jahamiah*. Mafundisho na mwongozo wa Imam vilisahihisha na kuzidisha elimu yake na kuimarisha umaizi wake na alijiunga kwenye kundi la Imam al-Kadhim (a.s.) na akawapita wafuasi na wanafunzi wa Imam na kuwa mashuhuri mno. Wale ambao walikuwa na wivu na uadui dhidi ya Ahlul-Bayt, waliojitahidi wakati wote kutaka kuizima nuru ya Allah, wakamshutumu kuwa na imani kwamba Mungu ana umbo la kimwili, na shutuma nyingine mbaya mno. Bali sisi tuna uzoefu mwingi sana kuhusu maoni yake juu ya dini kuliko mtu mwingine yoyote,

na katika kumbukumbu zetu tuna maelezo yake na kauli zake. Ameandika vitabu vingi katika kutetea madhehebu yetu kama ilivyoelezwa hapo juu; hivyo, haiwezekani kwamba tusitambue maoni ya kidini ya mmoja miongoni mwa wahenga na watangulizi wetu wema, ambapo wakosoaji wake ambao wako mbali na madhehebu na itikadi yake, na ambao hawajapitia vitabu vyake waweze kuwa na ujuzi zaidi juu yake yeye. Zile khutba za Hisham ambazo Shahristani amezinukuu katika kitabu chake *Al-Milal wal-Nihal* hazidhibitishi kwamba aliamini katika dhana kwamba Mungu alikuwa na umbo la kimwili. Ngoja ninukuu hapa kwa ajili yako aliyoyasema:

> "Hisham bin al-Hakam alikuwa na elimu ya *Usulud-Din* kwa kina sana. Madai yake aliyoorodhesha dhidi ya madhehebu ya Mu'tazila yasipotee machoni. Kwani mtu huwa nyuma ya yale anayoyalazimisha kwa mpinzani, na huwa mbali na yale anayoyadhihirisha. Yeye alikuwa yuko mbali na yale ambayo wapinzani wake wanamshutumu nayo, na mfano ambao aliutumia katika mahojiano na Allaf haukuwakilisha imani yake ya kidini kama inavyoweza kuonekana mwanzoni. Alimwambia Allaf: 'Unadai kwamba Muumba anajua kila kitu kupitia elimu Yake, na ilmu Yake ni ya asili; hivyo, na kwamba ilmu Yake haitofautiani na Dhati Yake, ambayo ina maana kwamba elimu Yake ni tofauti na elimu ya wanachuoni wengine [viumbe Wake]. Kwa nini basi vivyo hivyo husemi kwamba mwili Wake ni tofauti na miili yote ya viumbe Wake?'"

Hata kama ikichukuliwa kwamba kauli hii imenukuliwa kwa usahihi kutoka kwenye kitabu cha Hisham, haileti maana kwamba yeye aliamini Mwenyezi Mungu kuwa ana mwili. Sio kwamba kila anachosema mtu anayehoji kuhusu kitu fulani au kutoa hoja pinzani katika mjadala ni lazima kiwakilishe imani halisi au maoni ya mtoa hoja huyo. Kwani yamkini kwamba madhumuni yake ilikuwa ni kujaribu imani ya Allaf na elimu yake na sio zaidi ya hilo, kwani Shahristani mwenyewe amekiri kwamba mtu huyo (Hisham) yuko mbali na wapinzani wake wanavyomshutumu na mfano alioutumia haukuwakilisha imani yake kama wenyewe unavyoonyesha. Hata kama tutafikiria mfano huo kuwa kiashirio cha imani ya Hisham kuwa Mungu ana mwili, basi inawezekana ilikuwa ni imani yake kabla ya kukutana kwake na Imamu as-Sadiq (a.s.) kwani tumekwisha eleza kwamba kabla ya hapo, yeye alikuwa katika madhehebu ya *Jahamahi*. Alipopata elimu sahihi na mwanga kupitia mwongozo wa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.), akawa mmoja wa wanafunzi maarufu wa Maimamu (a.s.). Hakuna yeyote miongoni mwa wahenga wetu ambaye ameona uthibitisho wowote wa kile ambacho wapinzani wake wanamhusisha nacho, kama vile tu ambavyo hatuwezi kuona, licha ya juhudi zetu bora na utafiti wa kuaminika, kitu chochote cha kutilia shaka kwa Zararah bin Aayun, Muhammad bin Muslim, Mu'min al-Taq na wengine kama wao, kama maadui zao wanavyowasingizia. Madai na shutuma hizi dhidi yao hazina msingi wowote zaidi ya kuwa ni matokeo ya dhulma na chuki, kula njama na shutuma za uwongo; "**Wala usidhani kuwa Mwenyezi Munguameghafilika na wanayofanya madhalimu…..." (14:42).**

Shahristani amemshutumu Hisham kuhusu imani yake kwa Ali (a.s.) kama Mungu. Haya ni masihara ambayo hata mama aliyefiwa na mwanawe hivi punde anaweza kuangua kicheko juu yake. Hisham alikuwa anaheshimika sana kiasi cha kutoweza kujiingiza kwenye upuuzi na ushirikina huo kama maadui zake wanavyomsingizia. Hisham ametangaza *Tawhid* ya Allah kwa sauti kubwa kabisa kwa kumweka huru mbali kabisa na mabadiliko au umbile au kushushwa kwenye mwili, na mbali kabisa na kile ambacho mjinga anachokisema kuhusu Yeye. Na ndivyo yalivyo maelezo yake kuhusu Uimamu na urithi wa Ali, kwani anatangaza bayana kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ni bora kumshinda Ali (a.s.), na anadhihirisha wazi kwamba Ali (a.s.) alikuwa ni mmoja wa wafuasi tu wa Mtume (s.a.w.w.), mrithi na Khalifa wake (s.a.w.w.), na kwamba ni miongoni mwa watumishi wa Allah ambao walionewa na kutenzwa nguvu na ikashindikana kulinda haki zao, wakalazimishwa kusalimu amri mbele ya maadui zao, wakihofia na kuwaogopa maadui zao, wakiwa hawana wasaidizi wala wa kuwaunga mkono. Je haishangazi kwamba

Shahristani ambaye alikiri kwamba “Hisham bin al-Hakam alikuwa na elimu ya *Usulud-Din* kwa kina sana. Madai yake aliyoorodhesha dhidi ya madhehebu ya Mu’tazila yasipotee machoni. Kwani mtu huwa nyuma ya yale anayoyalazimisha kwa mpinzani, na huwa mbali na yale anayoyadhihirisha. Yeye alikuwa yuko mbali na yale ambayo wapinzani wake wanamshutumu nayo, na mfano ambao aliutumia katika mahojiano na Allaf haukuwakilisha imani yake ya kidini kama inavyoweza kuonekana mwanzoni. Alimwambia Allaf: ‘Unadai kwamba Muumba anajua kila kitu kupitia elimu Yake, na ilmu Yake ni ya asili; hivyo, na kwamba ilmu Yake haitofautiani na Dhati Yake, ambayo ina maana kwamba elimu Yake ni tofauti na elimu ya wanachuoni wengine [viumbe Wake]. Kwa nini basi vivyo hivyo husemi kwamba mwili Wake ni tofauti na miili yote ya viumbe Wake?” Kisha anatoa shutuma na kumhusisha na imani ya kwamba Ali (a.s.) ni Mungu?! Je hili sio jambo la wazi la kujichanganya mwenyewe binafsi? Je, ni sahihi kumhusisha mtu kama Hisham, licha ya ilmu yake kubwa na michango yake (kwa Umma), na upuuzi kama huu? Hakika sio sahihi. Lakini watu hawa burudani yao ni kutangaza shutuma potofu na madai yasiyo na msingi dhidi ya Ahlul-Bayt (a.s.) na wafuasi wao. “Hakuna nguvu wala uwezo isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.”

Uandishi na ukusanyaji wa vitabu ulistawi wakati wa Imamu al-Kadhim, al-Jawad, al-Hadi, al-Hasan al-Zaki al-Askari (amani juu yao wote) na kupata maendeleo makubwa. Wale ambao walikuwa wamesikia hadithi kutoka kwa Maimam au wanafunzi wao walikuwa wameenea kwenye miji mikubwa na midogo ya mbali na karibu. Wakapanua mikono ya nguo zao na wakatoka na kufanya juhudi kubwa kuiweka wazi na kuieneza elimu. Waliingia kwenye bahari za sanaa na sayansi, wakapiga mbizi kwenye siri zao, wakaorodhesha na kutatua matatizo yake na wakagundua mambo na kweli nyingi. Walifanya kila walichoweza katika kunakili elimu na kukusanya na kuhifadhi mambo na taarifa zilizotawanyika.

Al-Muhaqqiq (Mwenyezi Mungu ainyanyue hadhi yake Peponi), katika kitabu chake *Al-Mua’tabar*, anasema: “Miongoni mwa wafuasi wa al-Jawad (a.s.) walikuwepo watumishi na wanachuoni wenye maarifa mengi kama al-Husein bin Sa’id na kaka yake al-Hasan, na pia Ahmad bin Muhammad bin Abu Nasr al-Bizanti, Ahmad bin Muhammad Khalid al-Barqi, Shaadhan, Abul-Fadhl al-Ami, Ayyub bin Nuh, Ahmad bin Muhammad bin Isa na wengine ambao orodha yao ni ndefu kabisa… Wasomi hata katika zama zake yeye Muhaqiq walinukuu kutoka kwenye vitabu vyao kama marejeo ambayo ni ushahidi tosha wa ilmu yao kubwa.”

Kuhusiana na hili, ngoja nionyeshe kwamba al-Barqi peke yake aliandika na kutunga vitabu zaidi ya mia moja, na Al-Bizanti ameandika kitabu chake mashuhuri kiitwacho *Jami al-Bazanti*, na ambapo al-Husein bin Sa’id alikuwa mwandishi na mtunzi wa vitabu thelethini. Haiwezekani katika Barua hii kuorodhesha vitabu vyote ambavyo vimeandikwa na kutungwa na wanafunzi wa Maimamu sita ambao wanatokana na kizazi cha Imamu as-Sadiq (a.s.). Lakini nakuomba ufanye mazingatio katika vitabu vya bibiliografia (orodha ya vitabu) ambamo utakuta mpangilio mfupi na maelezo mafupi ya maisha ya Muhammad bin Sinaan, Ali bin Mahzyar, al-Hasan bin Mahbuub, al-Hasan bin Muhammad bin Sama’ah, Safwan bin Yahya, Ali bin Yaqtiin, Ali bin Fadhal, Abdul Rahman bin Najran, al-Fadhil bin Shaadhan (ambaye ameandika vitabu mia mbili), Muhammad bin Mas’ud al-Ayyashi (ambaye ameandika zaidi ya vitabu mia mbili), Muhammad bin Umayr, Ahmad bin Muhammad bin Isa (ambaye amewanukuu masahaba mia moja wa Imamu as-Sadiq – a.s.), Muhammad bin Ali bin Mahbuub, Talha bin Talha bin Zayd, Ammar bin Musa al-Sabati, Ali bin al-Nu’man, al-Husein bin Abdullah, Ahmad bin Abdullah bin Mahran ambaye anajulikana zaidi kwa jina la Ibn Khanat, Sadqa bin al-Munthir al-Qummi, Ubaydullah bin Ali al-Halabi ambaye alileta kitabu chake kwa Imamu as-Sadiq (a.s.) ili kihaririwe na kukithibitisha, ambacho yeye Imamu (as) alikifurahia na akasema: “Je, umeona kitabu kama hiki kilichotolewa na hilo kundi jingine?!” Abu Umar at-Tabiib, Abdullah bin Sa’id ambaye alileta kitabu chake kwa Imamu Abul-

Hasan al-Ridhaa (a.s.) kwa madhumuni yaleyale ya kuhaririwa, na Yunuus bin Abdur-Rahman ambaye alileta kitabu chake kwa Imamu Abu Muhammad al-Hasan al-Zaki al-Askari (a.s.).

Yeyote ambaye atafanya utafiti kwenye maisha na wasifu wa wahenga wema wa Shi'ah wa kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.) na kufuatilia majina ya wafuasi wote na wanafunzi wa Maimamu tisa kutoka kizazi cha Husein, atagundua kazi zao (vitabu) zote zilizotungwa wakati wa Maimamu wao na atajua ni maelfu mangapi ya wale waliosoma vitabu hivyo na kusimulia yaliyomo humo kwa wengine, na wakasikia na kunukuu hadithi za kizazi cha Muhammad katika kila tawi na mzizi wa dini na kaida zake. Kisha akitafakari juu ya ukweli kwamba elimu iliyopatikana kutoka kwa Ahlul-Bayt ilipitishwa kutoka kizazi hadi kizazi, kutoka kundi moja hadi jingine na kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kama ilivyowasilishwa kuanzia wakati wa Maimamu tisa maasum (a.s.) mpaka wakati wetu huu, basi atashawishika kufikia hitimisho lisilopingika kwamba dini ya Maimamu hawa wakati wote imekuwa ikiendelea na ni *mutawatir*, na ataondokana na shaka yoyote ambayo anaweza kuipata kuhusu ukweli wa kwamba ibada zetu kwa Allah Aza wa Jallah na imani yetu Kwake imetokana na watu ya Nyumba ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.). Hakuna atakayetilia shaka ukweli huu isipokuwa adui mwenye kiburi na chuki au mpumbavu na mjinga. Sifa na shukurani zote zimuendee Allah Ambaye ametuongoza kwenye hili, kwani bila mwongozo Wake, tusingeigundua Njia iliyonyooka. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 111

## JAMADI AL-ULA 1, 1330 A.H.

### KUSADIKISHA

Nashuhudia kwamba ninyi mnaamini katika kanuni za misingi ya imani ileile, na mnafanya ibada zilezile kama walivyofanya Maimamu kutoka kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Umefafanua suala hili na kuliweka wazi kabisa na kufichua lolote lile lililokuwa limejificha ndani yake. Mtu yoyote mwenye akili timamu hawezi kuwa na shaka juu ya hili, na kusababisha shaka yoyote au vurugu ni sawa na kuwapotosha watu wengine kwa makusudi kabisa. Umelifanya jambo hili kwa uwazi kabisa hivyo kuniwezesha mimi kulipitia vizuri. Imenivutia na kunifurahisha sana. Manukato mazuri ambayo nimeyavuta kutoka humo yamenichangamsha sana na harufu yake imenivuta kwa hali ya juu kabisa. Kabla ya ukweli kunishukia kupitia kwako wewe nilikuwa ninachanganyikiwa kuhusu imani yenu, kwa sababu ya yale niliyokuwa nikisikia miongoni mwa shutuma kutoka kwa madhalimu na waenezaji wa kashfa kuhusu dini yenu. Mwenyezi Mungu kwa huruma yake alipotukutanisha, nimekufuatilia mpaka nikafika chini ya bendera ya mwongozo na fanusi [taa] katika giza, na tulipoachana na wewe nilikuwa niliyestawi na kufanikiwa. Neema kubwa ilioje ambayo Allah amenijaalia kupitia kwako. Ni mafanikio makubwa yaliyoje yaliyoongezeka juu yangu kupitia kwako! Shukurani zote ni kwa Allah, Mola wa walimwengu. Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

# BARUA YA 112

## JAMADI AL-ULA 2, 1330 A.H.

### SHUKURANI

Nashuhudia kwamba una elimu pana na pia uwezo wa kwenda mbali zaidi katika upeo wa elimu. Umeonyesha utambuzi mkubwa. Umewapita wengine na unang'ara kuliko "Kimondo" (*meteor*). Ulipiga mbizi kwenye mjadala huu, ukapenya kwa kina kabisa katika kuchunguza ukweli kwa uangalifu, ukaupima kwa ufasaha na usahihi kabisa. Ulichunguza mielekeo yote na ukaidi wote pia. Ulijitolea muda wako na ukafikiria kujadiliana. Uliyapindua juu chini mas'ala yote ili kuweza kutambua siri zake, na kuzama chini kabisa ili kugundua uhalisia na mambo ya msingi, bila ya kuyumbishwa na chuki binafsi, wala kushawishiwa na masilahi binafsi. Hivyo, subira yako haikuchoka, wala rai yako kutawaliwa. Umezama kwa kina katika utafiti kwa upole ambao ni wa kuridhisha zaidi, na kwa kifua kipana kuliko dunia, ukiwa makini katika uhakiki, bila ya kujali maoni ya ndugu au jamaa, mpaka ukweli ukadhihiri wenyewe na haki ikawa bayana, kila mwenye macho kauona; hivyo, shukurani zote ni za Allah kwa kutupa sisi dini Yake, na kwa kutuwafikisha kupita katika Njia Yake aliyotuamrisha. Na sala na salam ziwe juu ya Muhammad na kizazi cha Muhammad.

Wassalam.

**Wako Mwaminifu, Sh.**

### ANGALIZO

Uandishi wa kitabu hiki umefikia tamati kwa msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na huduma Yake muafaka, kwa kalamu ya mwandishi wake, Abdul Husayn Sharafud-Diin al-Musawi al-Aamilil (Mwenyezi Mungu amhurumie na amsamehe makosa yake kwa ukarimu. Yeye ni Mwingi wa rehema).

Sifa zote anastahiki Mwenyezi Mungu kwamba tanbihi katika maandishi ya kitabu hiki zimekamilika. Maelezo yake yanafanya ujaziaji bora wa mapungufu ya kile kitabu cha asili. Maelezo haya yana manufaa sana na ya msingi muhimu kwa ajili ya kuelewa kwa mazingatio mazuri kabisa mafhumu ya maandiko hayo. Uchapishaji wa toleo hili lenye ufafanuzi ulikamilika katika mwezi Mtukufu wa Rajab 1355A.H. kwa kalamu ya watumishi wanyenyekevu kabisa wa dini na imani ya Kiislam na watiifu wa Madhehebu ya Maimam watokanao miongoni mwa Ahlul-Bayt (a.s.), naye ni Abdul Husayn bin Sharif Yusuf, bin Sharif Jawad, bin Sharif Isma'il, bin Sharif Muhammad, bin Sharif Ibrahim, maarufu kwa jina la ukoo kama Sharafud Diin bin Sharif Zaynul Aabidiin bin Ali Nuurud-Diin, bin Nuurud-Diin Ali bin al-Husayn al-Muusawi al-Aamili (Mwenyezi Mungu awahurumie na awarehemu). Sifa na Utukufu wote ni stahiki ya Mwenyezi Mungu ambaye ni wa Mwanzo na wa Mwisho! Na rehema na amani ya Mwenyezi Mungu iwashukie Muhammad na kizazi chake Muhammad!

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A. S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A. S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashariyyah
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera

31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a. S)
38. Adhana
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mtume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mtume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mtume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi

64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Huduma ya Afya katika Uislamu

97. Sunan an-Nabii
98. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
99. Shahiid Mfiadini
100. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
101. Ujumbe - Sehemu ya Pili
102. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
103. Ujumbe - Sehemu ya Nne
104. Kumswalia Nabii (s.a.w.w.)
105. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
106. Hadithi ya Thaqalain
107. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
108. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
109. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
110. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
111. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
112. Safari ya kuifuata Nuru
113. Fatima al-Zahra
114. Myahudi wa Kimataifa
115. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
116. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
117. Muhadhara wa Maulamaa
118. Mwanadamu na Mustakabali wake
119. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
120. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
121. Khairul Bariyyah
122. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
123. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
124. Yafaayo kijamii
125. Tabaruku
126. Taqiyya
127. Vikao vya furaha
128. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
129. Visa vya wachamungu

130. Falsafa ya Dini
131. Kuhuzunika na Kuomboleza - Azadari
132. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
133. Kuonekana kwa Allah
134. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
135. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
136. Ushia ndani ya Usunni
137. Maswali na Majibu
138. Mafunzo ya hukmu za ibada
139. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
140. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
141. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
142. Abu Huraira
143. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
144. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
145. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
146. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
147. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
148. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
149. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a. S)
150. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
151. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
152. Uislamu Safi
153. Majlisi za Imam Husein Majumbani
154. Uislam wa Shia
155. Amali za Makka
156. Amali za Madina
157. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
158. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
159. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
160. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
161. Umoja wa Kiislamu na Furaha
162. Mas'ala ya Kifiqhi

163. Jifunze kusoma Qur'ani
164. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
165. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
166. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
167. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
168. Uadilifu katika Uislamu
169. Mahdi katika Sunna
170. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
171. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
172. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
173. Vijana na Matarajio ya Baadaye
174. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
175. Ushia – Hoja na Majibu
176. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
177. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a. S.)
178. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
179. Takwa
180. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
181. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a. S.)
182. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
183. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
184. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
185. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
186. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a. S.)
187. Uongozi wa kidini – Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

# MUHTASARI